

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**BUNGE LA KUMI NA MOJA**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tano – Tarehe 1 Februari, 2016**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017, umetusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha hatua za maandalizi ya mpango wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Watendaji

wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius Beda Likwelile Kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu pamoja na maandalizi ya hotuba na kuandaa vitabu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017, ninayoyawasilisha leo katika Bunge lako Tukufu yatatumika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yamezingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020 - 2025, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka Kumi na Tano, Taarifa ya Awali ya Maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja yenye msisitizo wa ujenzi wa uchumi wa viwanda; na ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, pia yamezingatia malengo ya maendeleo endelevu ya mwaka 2020 - 2030, Mpango kazi wa kuharakisha maendeleo ya viwanda Afrika 2008; Sera ya Viwanda ya Afrika Mashariki pamoja na mkakati wa utekelezaji wake; Mwelekeo wa Viwanda wa SADC 2013 - 2018 na Mkakati wa Maendeleo wa Viwanda ya SADC 2015 - 2063.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo ya kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, utalii na maeneo mengine muhimu katika ukuaji wa uchumi yapo katika ukurasa wa tisa hadi wa 12 wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango. Aidha, ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango, umeelezwa katika ukurasa wa 13.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabili na changamoto hizo, zimeelezwa katika ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 15 wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kwa kifupi maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2016/2017. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 utakuwa na vipaumbele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, maeneo ya vipaumbele kwanza itakuwa ni viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake inapatikana nchini na hususan kilimo, mifugo, uvuvi, madini na rasilimali nyingine; pia viwanda vya kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi nchini kama vile nguo, viatu na mafuta ya kupikia; na viwanda vinavyotumia teknolojia ya kati na kuwaajiri watu wengi.

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ya kielelezo ili kuchochea ukuaji wa uchumi, baadhi ya miradi hiyo itakuwa ni pamoja na ifuatayo:-

Kwanza, ni uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji, yaani *Special Economic Zones* ya Bagamoyo, Mtwara, Kigoma na Kurasini; pili, ni mji wa kilimo Mkulazi; tatu, kiwanda cha chuma cha Liganga na Makao ya Mawe Mchuchuma; nne, ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*; tano, kujenga msingi wa viwanda vya kuzalisha mitambo, nyenzo na malighafi za uzalishaji; sita, ni kuimarisha huduma za usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa yetu makuu (victoria, Tanganyika na Nyasa) ikiwa ni pamoja na ununuzi wa meli mpya na kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege mpya.

Saba, ni kuanza maandalizi yatakayoweza mradi wa ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi ya kimiminika kwa Kiingereza ni *liquefied natural gas LNG Plant* kule Lindi; na nane, ni kusomesha vijana wengi hususan katika fani zinazohitajika zaidi za mafuta na gesi, uhandisi, kemikali, tiba na afya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maeneo wezeshi kwa maendeleo ya viwanda katika mwaka 2016/2017 maeneo wezeshi kwa maendeleo ya viwanda ni pamoja na miundombinu ya nishati, reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari na maji kwa ajili ya mahitaji ya viwanda, lakini pia mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

Aidha, itajumuisha kilimo kwa kuwa ni nguzo ya msingi katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula na malighafi za uzalishaji viwandani. Katika eneo hili msisitizo utawekwa katika miradi iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/2012 mpaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaweka msisitizo mkubwa katika kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu.

Maeneo mahususi yanayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na kuhakikisha usalama wa chakula, afya ikiwemo kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa dawa kwa wananchi, kuimarisha elimu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya msingi bila malipo, kuimarisha utawala bora, kuimarisha ubora wa elimu kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa Walimu walio kazini, kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, kuandaa mfumo endelevu wa ugharamiaji na kuimarisha mifumo ya ithibati na udhibiti, usimamizi na upatikanaji wa maji safi na huduma za maji taka, nishati ya uhakika, upatikanaji

wa ajira, hifadhi ya jamii, usawa wa jinsia na watu wenye ulemavu, utawala bora, mipango miji na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 yamebainisha maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na utalii, Misituta na wanyamapori, madini, hali ya hewa, ushirikiano wa kikanda na Kimataifa na utawala bora.

Katika eneo hili msisitizo utawekwa katika kukamilisha miradi ambayo utekelezaji wake ulianza katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ugharamiaji wa Mpango; Sekta binafsi itakuwa mtekelezaji mkuu wa Mpango huu. Serikali itakuwa na wajibu wa kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi ichangie kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka wa 2016/2017, Serikali inakusudia kutenga kiasi cha Shilingi trilioni 6.18 ili kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zitakuwa ni Shilingi trilioni 4.8 sawa na asilimia 77.8 ya bajeti ya fedha ya maendeleo.

Vile vile Serikali itawekeza mitaji katika Benki ya Uwekezaji wa Rasilimali (TIB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo TADB ili kuvutia fedha za mikopo ya masharti nafuu kutoka taasisi za fedha za ndani na nje kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu ufuatiliaji, tathmini na utaoji taarifa zinapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 19 na 20. Aidha, maelezo kuhusu vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na hatua za kukabiliana navyo yapo katika ukurasa wa 21 na 22 wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kwa muhtasari Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017, unawaelekeza wadau maeneo ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mipango na bajeti. Aidha, Mwongozo unaonyesha mwenendo wa viashiria muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikijumuisha mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mipango na miradi mikubwa ya Kitaifa, malengo na maeneo ya kipaumbele katika kipindi cha muda wa kati, ukomo wa bajeti 2016/2017 na mfumo wa utoaji taarifa.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo tena utekelezaji wa bajeti kwa nusu mwaka 2015/2016. Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi trilioni 22.49. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2015 mapato yote ya Serikali yalikuwa jumla ya Shilingi trilioni 10.23 ikiwa ni sawa na asilimia 88.8 ya makadirio ya nusu mwaka. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2015 Serikali imetoa mgao wa matumizi wenye thamani ya Shilingi bilioni 10,312 sawa na asilimia 89 ya lengo la Shilingi bilioni 11,531 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichotolewa Shilingi bilioni 8,181.5 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 2,130.9 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio, changamoto pamoja na hatua za kukabiliana na changamoto hizo zimeelezwa katika ukurasa wa 10 na wa 12 wa hotuba ya kuwasilisha Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/2017. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015; mafanikio, changamoto pamoja na hatua za kukabiliana na changamoto hizo, yameelezwa katika ukurasa wa sita na wa tisa wa hotuba ya kuwasilisha Mwongozo wa Kuandaa Mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu katika kuandaa mwongozo na Mpango wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017; kwanza ni shabaha za uchumi jumla; Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021, moja itakuwa ni pato halisi la Taifa kukua kwa 7% mwaka 2015, 7.2% mwaka 2016 na kuendelea kuongezeka hadi wastani wa 8% katika kipindi cha muda wa kati kwa kutumia takwimu zilizorekebisha za mwaka wa kizio cha 2007.

Pili, ni kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia sita *june* 2016 na kubaki kati ya 5% na 8% katika kipindi cha muda wa kati.

Tatu, mapato ya ndani ukijumlisha na mapato ya Halmashauri, kufikia 14.8% ya pato la Taifa mwaka 2016/2017 asilimia 15.1 mwaka 2017/2018 na asilimia 16.3 mwaka 2019/2020. Mapato ya Kodi kufikia asilimia 13.2 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017, asilimia 13.5 ya pato la Taifa 2017/2018 na kufikia 14.4 ya pato la Taifa ifikapo mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Spika, misingi ya mpango wa bajeti itakua ni pamoja na amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na nchi jirani kwamba vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa; pili, viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile pato la Taifa, biashara ya nje, ujazo wa fedha, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika. Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia lakini pia bei za mafuta katika Soko la Dunia zitaendelea kuwa nzuri. La mwisho ni hali nzuri ya hewa nzuri na katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kwa ufupi mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Kwa kuzingatia Sera za Uchumi pamoja na misingi na Sera za bajeti kwa mwaka 2016/2017, sura ya bajeti inaonyesha kuwa, jumla ya Shilingi trilioni 22.99 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuishwa na mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuongeza kufikia Shilingi trilioni 15.80 sawa na 68.7% ya mahitaji yote ikilinganishwa na 62.2% mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla Shilingi bilioni 14,106.6 sawa na ongezeko la 14.1% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2015/2016. Aidha, mapato yasiyo ya kodi na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni Shilingi bilioni 1,110.2 na Shilingi bilioni 584.4 kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inategemea kukopa kiasi cha Shilingi bilioni 1,782.3 kutoka vyanzo vya nje, vyenye masharti ya kibiashara. Aidha, mikopo ya ndani inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 3,300.5 zikijumuisha Shilingi bilioni 2,766.1 kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva.

Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 2,107.4 ikiwa ni misaada na mikopo sawa na 9.3% pungufu ya makadirio ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 Serikali inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 14.139 kutoka kwenye vyanzo vya kodi sawa na asilimia 13.2 ya pato la Taifa. Hii ni sawa na ongezeko la 15% ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 12.30 katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya ndani hadi sasa ni pamoja na vifuatavyo:-

Kwanza, kodi za ndani za moja kwa moja (*direct taxes*). Chanzo hiki kinajumuisha Kodi ya Mapato ya Watumishi (*Pay As You Earn*), Kodi ya Mapato ya Watu Binafsi; Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (*Business and Skills Development Levy*), Kodi ya Makampuni, Kodi ya Zuiio, pamoja na kodi nyinginezo ikiwa ni pamoja na kodi kutokana na michezo ya kubahatisha. Jumla ya mapato kutoka eneo hili ni Shilingi bilioni 5,298.7.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kodi za ndani zisizo za moja kwa moja (*indirect taxes*). Chanzo hiki kinajumuisha kodi za ushuru wa bidhaa za ndani kama vile vinywaji mbalimbali, sigara na muda wa matumizi kwa simu za viganjani, kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa bidhaa na huduma za ndani. Jumla ya mapato katika eneo hili ni Shilingi bilioni 3,920.9.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kodi zitokanazo na biashara za Kimataifa, *International Trade Taxes*. Chanzo hiki kinajumuisha kodi ya ushuru wa forodha, kodi mbalimbali zinazotowwa kwenye bidhaa za mafuta, *Petroleum Fee* ambayo inakwenda kwenye Mfuko wetu wa REA, kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa pamoja na ushuru wa Mifuko ya Maendeleo ya Reli na maji. Katika eneo hili, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 5,812.9.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2016/2017 Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi trilioni 22.99 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 16.80 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumlisha Shilingi trilioni 6.65 kwa ajili ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi trilioni 6.18 ambapo kiasi cha Shilingi trilioni 4.8 ni fedha za ndani sawa na asilimia 77.8 ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya fedha za bajeti ya maendeleo zitatumika kugharamia miradi ya huduma za jamii na kiasi kidogo kitatumika kama mtaji wa kuwekeza kwenye miradi inayoweza kutupatia mapato, ambapo wakopeshaji wataongeza mtaji huo na kusimamia utekelezaji wa mradi husika. Aidha, utaratibu wa PPP utatumika kuipunguzia Serikali gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017, umeainisha mambo muhimu yanayotakiwa kuzingatwa na Maafisa Masuuli kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kutekeleza sheria ya bajeti. Utekelezaji wa sheria ya bajeti namba 11 ya 2015 ulianza Julai, Mosi 2015. Hivyo Maafisa Masuuli wanaagizwa kuzingatia sheria hii na kanuni zake za mwaka 2015 katika maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti za mafungu yao. Aidha, sheria hii inaelekeza Maafisa Masuuli kuunda Kamati za Bajeti na kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya maandalizi ya mpango na bajeti katika fungu husika.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Bajeti yameainishwa katika kifungu cha 17(3) cha kanuni za bajeti za mwaka 2015. Kamati za Bajeti zinawajibika kutimiza majukumu yao pamoja na kuzingatia nyaraka za Msajili wa Hazina na nyaraka nyingine. Eneo la pili, ni ukusanyaji wa mapato. Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:-

(1) Mapato yote yatakusanywa na Wizara Fedha na Mipango. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali, Wakala, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, isipokuwa yale yanayokusanywa kwa

mujibu wa sheria ya fedha ya Mamlaka ya Serikali Na. 9 ya mwaka 82 inayoruhusu mamlaka hizo kukusanya mapato kwenye maeneo yao na kuyatumia, watatakiwa kuwasilisha mapato yote yatakayokusanywa yawasilishwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti za mafungu zitakazoidhinishwa;

(2) Pili, Utaratibu wa *retention* uliokuwa ukitumika awali umefutwa. Hivyo, mapato yote yatakusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kila fungu litapewa fedha kulingana na bajeti yake;

(3) Majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa makundi. Zoezi hili lifanyiwe katika Majiji, Manispaa, Halmashauri za Miji, Makao Makuu ya Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Miji midogo kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo ukikamilishwa;

(4) Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato;

(5) Kuboresha mazingira ya urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi;

(6) Kusimamia ipasanyo upatikaji wa matumizi sahihi wa mashine za *ki-electronic*;

(7) Kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya;

(8) Kuhakikisha Taasisi zote za Umma zinatumia mifumo ya *ki-electronic* katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(9) Kuingia mikataba na wazabuni, wakandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za *ki-electronic*; na

(10) Kupitia upya viwango vya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na viwango vya soko katika kutoa huduma za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa matumizi na hatua za kupunguza gharama, kwanza, Maafisa Masuuli wataelekezwa kufanya yafuatayo:-

(1) Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na Mikutano ya Bodi, Mafunzo na Semina inatumia Kumbi za Serikali na Taasisi za Umma. (*Makofi*)

(2) Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile bima, usafirishaji wa barua mizigo na vifurushi, matangazo na usafiri. *(Makofi)*

(3) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Mashirika hayo ni pamoja na TANESCO, TAZARA, TRL, ATCL, RAHCO, TEMESA, Wakala wa Vipimo, Bodi ya Mazao Mchanganyiko. *(Makofi)*

(4) Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. *(Makofi)*

(5) Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa watumishi wanaostahili na waliopo katika vituo vya kazi. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya sensa ya Watumishi wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili. *(Makofi)*

(6) Kuendelea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja *(in bulk)* kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji ili kupata nafuu ya bei, hivyo matumizi ya Wakala hayaruhusiwi.

(7) Kuendelea na ununuzi wa pamoja wa magari kupitia GPSA baada ya Maafisa Masuuli kupata vibali vya ununuzi kutoka kwa Waziri Mkuu.

(8) Kupunguza gharama katika maeneo mbalimbali ikiwemo matengenezo ya magari, mafuta ya magari, sherehe, matamasha na safari za nje ya nchi.

(9) Kuimarisha ufutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika ngazi zote.

(10) Kudhibiti matumizi ya taasisi za Serikali yasiyo na tija na kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji ili kuchukua hatua stahiki kwa maendeleo ya nchi.

(11) Kusimamia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuhakikisha kwamba mianya yote ya fedha za umma inayotokana na usimamizi hafifu inazibwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kulipa na kuzuia ongezeko la madeni ya Serikali, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kifungu Na. 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya 2015 na Waraka wa Hazina Na. 4 wa tarehe 31 Desemba, 2014 kwa kufanya yafuatayo:-

(1) Kulipa madeni yale tu yaliyohakikiwa na kuingizwa kwenye hesabu za Serikali;

(2) Kuwasilisha kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali taarifa ya madeni yaliyokaguliwa na Mkaguzi wa Ndani wa Fungu na kuidhinishwa na Afisa Masuuli wa Fungu husika;

(3) Kuzingatia maagizo na maelekezo mbalimbali yaliyokwisha kutolewa na Serikali siku za nyuma kuhusu ununuzi wa bidhaa na huduma, mfano ununuzi wa samani, kuhamisha watumishi, ununuzi wa magari, ulipaji na uzuiaji wa malimbikizo ya madeni;

(4) Ni kutumia *LPO* zinazotoka kwenye mfumo wa *IFMS* katika kupata huduma; na

(5) Kudhibiti uingiaji wa mikataba miradi inayotekelezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa kuzingatia Kifungu Na. 52 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha. Serikali itahakikisha kuwa inaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuelekeza matumizi kwenye maeneo yenye tija kwa manufaa ya Watanzania wote. Ni matumaini yangu kuwa wadau wote wanohusika katika uandaaji na utekelezaji wa mwongozo huu watazingatia maelekezo yaliyopo ili kuhakikisha malengo na matarajio ya mpango na bajeti ya mwaka 2016/2017 yanatimia.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 vinapatikana katika tovuti za Wizara ya Fedha, yaani [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz) na [www.mipango.go.tz](http://www.mipango.go.tz).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017 pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi ipasavyo wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu!

### **KAMATI YA MIPANGO**

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MHE. HAWA A. GHASIA (MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016, naomba kuchukua fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge la Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 yanatoa mwanga wa jinsi Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017 utakavyokuwa katika kuimarisha uchumi wa viwanda na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mapendekezo ya Mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vya kuendeleza viwanda ambavyo vitaimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi, miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kupaa na maeneo yatakayolenga kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Aidha, Mwongozo wa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vitakavyotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa 2015, inaonesha kwamba uchumi wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea, unatarajiwa kukua kwa kiwango cha 4% mwaka 2015 na 4.5% mwaka 2016. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa asilimia 6.9 kwa mwaka 2015 na unatarajiwa kukua kwa 7% mwaka 2016. Hata hivyo hali hii ya ukuaji wa uchumi hapa nchini bado haujaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa umasikini wa kipato kwa wananchi hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato halisi la Tanzania lilikua kwa wastani wa 7% mwaka 2014 na 7.1% mwaka 2015. Aidha, pato la Taifa kwa mwaka 2014 lilikua kwa Shilingi trilioni 79.442 kwa bei ya mwaka husika na idadi ya watu ilikadiriwa

kuwa watu milioni 46. Hivyo pato la wastani kwa kila mtu lilikuwa Sh. 1,724,416/= sawa na Dola za Kimarekani 1,038.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2015, pato la Taifa lilikadiriwa kufikiwa Shilingi trilioni 89 na pato la mwananchi kwa mwaka huo, lilikadiriwa kuwa Sh. 1,828,022/= sawa na Dola za Kimarekani 1,043. Pamoja na jitihada za kuongeza pato la kila mwananchi, bado tuko mbali katika kufikia lengo la Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo imelenga kufikia Dola za Kimarekani 3,000. Mfumuko wa bei uliongezeka kutoka 4% mwezi Januari, 2015 hadi 6.4% mwazi Julai, 2015 na kuendelea kuongezeka hadi 6.8% mwezi Desemba, 2015. Kwa mujibu wa taarifa za Serikali, inaonesha mfumuko wa bei umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa bei ya vyakula.

Hali hii inaonesha kwamba kuna tatizo la mgawanyo wa Chakula nchini, kwani katika kipindi cha mwaka 2014/2015 nchi yetu ilikuwa na kiwango cha utoshelezi wa chakula kwa asilimia 125. Hivyo ni dhahiri kwamba kuna tatizo la mgawanyo wa chakula ambalo yawezekana inasababishwa na tatizo la miundombinu. Endapo kungekuwa na miundombinu thabiti ya utawanyaji wa chakula, tatizo hili la mfumuko wa bei lingeweza kupungua kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ilishuka kwa kiasi cha Shilingi 1,731.31 Januari, 2015 hadi Shilingi 2,149.1 Oktoba, 2015. Pamoja na sababu zilizotolewa na Serikali, Kamati inaamini kwamba kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuingiza bidhaa na huduma nyingi zaidi kutoka nje kuliko kiasi cha huduma na bidhaa tunazouza nje ya nchi, hali inayopelekea nakisi kila mwaka.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaongeza kiwango cha akiba ya fedha za kigeni zinazoweza kugharamia mahitaji na huduma kutoka nje kufikia angalau miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa limeongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 18,643.8 mwezi Oktoba, 2014 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 19,221.4 mwezi Oktoba, 2015. Kamati inaishauri Serikali kwamba ihakikishe inatumia mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo tu. Aidha, Serikali ianze kuwa na utaratibu wa kushirikisha Bunge kabla ya kwenda kuchukua mikopo ili kupata maoni na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi trilioni 22.49 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2015. Mapato yote ya Serikali yalikuwa jumla ya Shilingi trilioni 10.23, hii ikiwa ni sawa na 88.8% ya makadirio ya nusu mwaka. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2015, Serikali imetoa mgao wa matumizi yenye thamani ya Shilingi trilioni 10.31, sawa na 89% ya lengo la Shilingi trilioni 11.53 katika kipindi hicho.

Kati ya kiasi hicho kilichotolewa, Shilingi trilioni 8.18 kilikuwa ni matumizi ya kawaida na Shilingi trilioni 2.13 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikuwasilisha utekelezaji wa nusu mwaka ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo ya Mwaka 2015/2016 kwa vipaumbele vya kisékta. Hata hivyo, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015 yameainishwa vizuri katika taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imepitia na kufanya uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2016/2017 na kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Mwaka 2016/2017 hauna budi kuoanisha vipaumbele vilivyoshindwa kutekelezwa ipasavyo katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2015/2016, pamoja na kulinganisha na yale yatakayokuwemo kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. Lengo ni kuona na kujiuliza, tumetoka wapi? Tumefika wapi? Tufanye nini ili Mpango unaokusudiwa utuelekeze kutekeleza malengo ya dira ya 2025. Aidha, Mpango huu pamoja na Mkukuta tu, ujikite katika kutoa majibu ya changamoto zilizopo katika kuondoa umasikini wa kipato.

Kamati inashauri Bunge kuangalia mapendekezo ya Mpango huu katika sura ya Kitaifa na kutathmini mahitaji ya rasilimali yanayohitajika katika kutekeleza Mpango huu. Bunge lisimamie uzingatiaji wa vipaumbele tutakavyokubaliana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/2017 hadi 2020/2021 hapo baadaye ili viguse maeneo machache ambayo yataibua fursa za kiuchumi za nchi yetu na kupunguza umasikini kupitia maendeleo ya viwanda. Aidha, ni vyema Sheria ya Bajeti ikatekelezwa kikamilifu katika kusimamia mipango ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha vyanzo mbalimbali vya kugharamia Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2016/2017 ambavyo kwa jumla vitatoa Shilingi bilioni 6,182.2. Changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini ni mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha katika Mpango uliopita, pamoja na kuwa Serikali iliainisha vyanzo vya fedha katika kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo ile ya Kitaifa ya kimkakati, hata hivyo bado fedha hizo hazikupatikana kwa wakati uliopangwa au kutokufika kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, Serikali ijipange vyema kuhakikisha kwamba inasimamia ipasavyo mapato ya ndani, mikopo na fedha za mifuko maalum pamoja na sekta binafsi ili kuhakikisha kwamba inapata kiasi hicho cha fedha cha kugharamia mpango husika. Aidha, Kamati inaona kuwa ni vyema sasa Serikali ikaanza kuona namna ya kupata mapato kutoka katika Sekta ya Gesi kupitia Sera ya Uanzishaji ya Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi ambao utatumika kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka miradi mikubwa ya kielelezo kama moja ya kipaumbele kikuu katika mpango unaotegemewa kutekelezwa. Kamati inaona kwamba kama Serikali itafanikiwa kutekeleza miradi hii hasa ile ya maeneo maalum ya uwekezaji ya Bagamoyo, Mtwara, Kigoma, Kituo cha Biashara na huduma Kurasini, Mji mpya wa Kilimo Mkulazi, ujenzi wa Kiwanda cha Chuma Liganga na ujenzi wa Reli ya Kati, basi Serikali itakuwa imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kukuza uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendeleo kuhamasisha uwekezaji, ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya EPZ na SEZ na kutoa fidia kwa wakati ili kuruhusu utekelezaji wa miradi husika kwa wakati. Miradi hii ya EPZ na SEZ iliyopo na ile ambayo ile tunategemea kuwa itakuwa imekamilika ni mwanzo wa msingi mzuri wa mwendelezo wa ujenzi wa viwanda na hivyo kupiga hatua kwa upande wa ajira, soko la malighafi nchini, kuvutia wawekezaji na biashara na hivyo kuiingizia nchi mapato ya kigeni hatimaye kukuza uchumi wetu na kuelekea hadhi ya nchi ya kipato cha kati. Aidha, Serikali iweke mazingira wezeshi ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kupitia Sera ya Manunuzi ili kutowakatisha tamaa wawekezaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia kuwa mapendekezo ya mpango yawe ni Dira ya kuagiza na kujenga nidhamu kwa vyombo vikuu vya kupanga, kufuatilia, kutathmini na kutekeleza mipango ya nchi. Mantiki ya maelezo yaliyotolewa ni kuisitiza kuwa Mapendekezo ya Mpango ya Mwaka 2016/2017 pamoja na kuelezea misingi na shabaha ya utayarishaji, ni lazima vilevile uoneshe mpango unaotarajiwa kujibu changamoto na vikwazo vya kimfumo vilivyojitokeza katika uendeshaji na kusimamia uchumi katika Mpango uliopita wa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo haya ni pamoja na kujenga nidhamu, pia sisitizo makini baina ya wawekezaji, watekelezaji na watendaji katika ngazi zote za Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona changamoto katika taratibu za usimamizi na ushirikiano wa vyombo vinavyosimamia mipango ya maendeleo kwenye ngazi mbalimbali za utawala na hivyo kusababisha kurudia upungufu na makosa yaliyojitokeza awali kwenye mipango husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikiandaa *programs* za kisékta ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja na melengo ya dira ya maendeleo ya Taifa ikiwa ni pamoja na kutumia fedha nje ya Bajeti. Mapendekezo ya Mpango wa 2016/2017 hayana budi kurekebisha upungufu huu ili kutimiza malengo tuliyojiwekea kwenye mipango husika. Aidha, ni vyema Serikali ikawa na utaratibu wa maalum wa kupanga bajeti ya ukutekeleza wa vipaumbele vikubwa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ni kuweka mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya ukuaji wa viwanda kupitia sera na mikakati madhubuti ikiwa ni pamoja na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi. Kamati inaelewa kuwa Sekta ya Viwanda haiwezi kupiga hatua bila kuweka mazingira mazuri ya kuiendeleza.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inafanyia kazi eneo la kupunguza gharama za uzalishaji; kwa mfano, upatikanaji wa umeme wa kutosha, kupunguza urasimu pamoja na kusimamia vizuri Sera ya Kodi na Fedha ili kuwezesha kuleta matokeo tarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa pamoja na mipango mingine tuliyopanga kwenye Sekta ya Viwanda, ni muhimu Mpango huu wa Mwaka Mmoja ukajielekeza katika kuhusisha mikakati mbalimbali ya Sekta ya Viwanda Vidogo, kuongeza thamani ya bidhaa zetu pamoja na kuongeza mauzo nje. Aidha, ni muhimu Mpango huu ukajielekeza pia katika kufikiria namna ya mchakato wa ujenzi wa viwanda vipya, kufufua na kukarabati viwanda ambavyo havifanyi vizuri na vile vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mpango huu uhusishe mkakati unganishi wa mpango kabambe wa Sekta ya Viwanda ambao unaibua mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha kuendelezwa viwanda vya kukuza mauzo nje, ikiwa ni pamoja na kulenga kufanya usindikaji wa mwanzo kwenye maeneo mbalimbali ya mikoani na mwambao wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kuwa, nchi nyingi duniani zimepiga hatua za kiuchumi katika viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ikiwa ni pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu Serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa za kukuza uchumi wetu na ushindani wa kikanda na Kimataifa kupitia sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhaulisha sheria zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji pamoja na ubia nchini. Kuhaulishwa kwa sheria hizi kutahamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika utekelezaji wa Mpango huu kwasababu taratibu za uwekezaji na ubia katika sekta mbalimbali zitakuwa chini ya mwamvuli mmoja. Aidha, kupitia sheria hizi, Sekta ya Umma kushirikiana na sekta binafsi, zitapata fursa za kujenga, kuendesha na kuwekeza katika miradi muhimu ambayo itasaidia kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na kuwezesha wananchi kupata ajira na kuongeza kipato kupitia miradi hiyo ya uwekezaji na ubia.

Pamoja na mapendekezo tuliyotoa hapo juu kwa ujumla, Serikali ijielekeze katika kutoa majibu ya haraka kwenye kutatua changamoto za uhaba wa umeme na maji, ushindani usio wa haki, miundombinu duni, uhaba wa mitaji, upatikanaji wa masoko, ukosefu wa wataalam na teknolojia duni na utatuzi wa sheria zinazokinzana katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi trilioni 22.99 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Mapato ya ndani ikijumlisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa Shilingi trilioni 15.8. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni Shilingi trilioni 14.1, mapato yasiyokuwa ya kodi ni Shilingi Trilioni 11.1 na Shilingi Bilioni 584.4 ni mapato ya Halmashauri.

Serikali inategemea kupata kiasi cha Shilingi Trilioni 2.1 ikiwa ni misaada na mikopo kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka wa Maendeleo 2016/2017. Vilevile Serikali inatarajia kukopa kiasi cha Shilingi trilioni 1.78 kama mikopo wa nje yenye masharti ya kibiashara ili kupunguza nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali katika mwaka wa 2016/2017 yanategemewa kuwa Shilingi trilioni 22.99 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi trilioni 16.8 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumlishwa Shilingi trilioni 6.65 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi trilioni 6.18 ambapo kiasi cha Shilingi trilioni 4.18 ni fedha za ndani na Shilingi trilioni 1.37 fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia mwongozo wa bajeti kwa mwaka 2016/2017. Kwa kiasi kikubwa inaipongeza Serikali katika maboresho ya mfumo wa maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato, shabaha za uchumi jumla na misingi iliyowekwa kwa ajili ya bajeti. Hata hivyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao katika mwongozo huo wa bajeti:-

Katika mfumo wa ukadiriaji wa majengo kwa mkupuo, Kamati inashauri kwamba Serikali iangalie pia hali ya uchumi wa eneo husika, thamani ya ardhi kwa maeneo husika na thamani ya jengo lenyewe. Kamati pia inaona kwamba ni wakati muafaka kwa Serikali kutekeleza mkakati wa kurasimisha rasilimali na biashara Tanzania na mpango wa kuboresha mazingira biashara Tanzania.

Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikiria kupima na kuainisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa hati miliki. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba ni vyema tahadhari ikachukuliwa ili kuepusha migogoro ya kimkataba na uwekezaji katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kufuata utaratibu wa *retention* ambao unakusudiwa na Serikali, Kamati inaunga mkono kusudio hilo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia sheria zilizoruhusu utaratibu wa *retention* kwa kila taasisi ili kuepuka mgongano wa kisheria unaoweza kudhoofisha utekelezaji wa majukumu ya msingi wa taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mashirika ya Serikali kujiendesha kibishara; moja ya sababu ya kutokufanikiwa kwa mashirika mengi ni ya umma ni madeni ambayo mashirika hayo yalikuwa yanaidai Serikali kutokulipwa kwa wakati. Kwa hiyo, Kamati inakubaliana na uamuzi huo. Hata hivyo ni muhimu Serikali ikalipa madeni na ikawezesha vya kutosha na kuwekewa malengo ya utekelezaji wa majukumu katika mashirika haya ili yaweze kufanya kazi na kuzalisha faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali katika suala la kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile Bima, usafirishaji wa barua, mizigo, vifurushi, matangazo na usafiri. Hata hivyo, Serikali iweke utaratibu wa kulipa huduma hizi kwa wakati ili kuepuka madeni mapya ya Serikali kwa Taasisi husika kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili lengo hili liweze kufanikiwa, ni vyema Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 ikafanyiwa marekebisho kurahisisha suala hili. Aidha, sasa ni wakati muafaka wa kupata huduma muhimu ya Mashirika ya Umma kama *TBC, TCCL, ATCL, TRL, TEMESA, TBA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutenga kiasi cha asilimia 35 ya makusanyo yote ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo uliowasilishwa na Serikali, haujaweza kubainisha utaratibu wa madeni ya wazabuni na wakandarasi ambayo wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokubainisha madeni hayo kwenye mwongozo wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017, hakutaleta picha halisi ya utekelezaji wa Bajeti ijayo hasa katika uhakika wa kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na kulipa madeni ya nyuma. Kamati inaitaka Serikali kuweka wazi madeni ya Wakandarasi na Wazabuni kabla ya kuanza mwaka wa fedha ujao.

Kamati ingependa kupata ufafanuzi kuhusu kushuka kwa gharama ya Mafuta mazito kwenye Soko la Dunia ukilinganisha na bei ya umeme unaozalishwa na mitambo inayotumia mafuta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyingine tena kwa kunipa fursa ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu na pia napenda kumshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao ambao wameipatia Kamati yetu pamoja na Wataalamuwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii pia kwa umakini wao mkubwa katika kujadili na kutoa mapendekezo. Naomba niwataje kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe ni Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbaraka Kitwana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umalize bila kuwataja Wajumbe wa Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA (MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Katibu wa Bunge, Dkt. Kashiillah kwa kuweza kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tulipaswa kusikiliza kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani lakini muda wetu hautoshi kwa sababu wanahitaji nusu saa. Kwa sababu hiyo, kwa mujibu wa kanuni ya 28 tutarudia kwenye Bunge, lakini tutaliahirisha kabla ya muda. Kwa hiyo, Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Kwa mujibu wa kanuni ya 28, kwa sababu tunasitisha Bunge kabla ya muda, kanuni inanitaka niwahoji Wabunge kama mnakubali hoja hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge litarejea saa 10.00 jioni.

*(Saa 6.45 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, leo ni siku yangu ya kwanza kukaa katika Kiti hiki nyeti, naomba nichukue fursa hii ya kipekee kwa heshima na taadhima kabisa kuwashukuruni nyote Waheshimiwa Wabunge kwa kura zenu mlizonipa na kupita bila kupingwa.

Waheshimiwa Wabunge, kubwa la msingi, tuko hapa kwa ajili ya maslahi ya Taifa. Naomba ushirikiano wenu na tufanye kazi kwa ajili ya wananchi na kwa heshima ya Bunge kwa kuzingatia Kanuni tulizonazo.

Basi naomba ushirikiano wenu mkubwa na baada ya kusema haya, nawashukuru tena. Katibu!

## **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Karibu.

**MHE. DAVID E. SILINDE (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5)(a), Toleo la Mwaka 2016 ya Kanuni zako za Bunge, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi kuhusu

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali, pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, kama ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kanuni husika imetenguliwa kutokana na muafaka uliofikiwa humu Bungeni, baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa hoja, inaonesha upungufu wa Kanuni uliopingana na Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 94 ilitakiwa kutenguliwa katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Oktoba – Novemba, kama Kanuni zinavyotaka, lakini Serikali imefanya kosa la kutengua Kanuni baada ya kuwasilisha Mwelekeo wa Mpango wa Miaka Mitano.

Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa makini wakati wa uwasilishaji wa hoja zake Bungeni, kwani inaonesha kuwa kuna ombwe kubwa la uelewa wa Kanuni na Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, Kambi Rasmi ya Upinzani inawasilisha maoni yake kama ilivyohitajika kwa manufaa ya Watanzania, tofauti na Watanzania wanavyoaminishwa kuwa Upinzani kazi yetu ni kukwamisha Mapendekezo ya Mpango bila sababu za msingi. Wakati Serikali imekiri na Watanzania wameshuhudia udhaifu mkubwa unaotokana na ukiukwaji wa Katiba na Kanuni za Bunge, kama ambavyo tuliapa kuzilinda, kuzitetea na kuzihifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya makosa makubwa ambayo Bunge la Kumi liliyafanya, ilikuwa ni kushindwa ama kuacha kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Kwanza wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, yaani 2011/2012 mpaka 2015/2016. Kwa sababu ya kosa hilo Mpango huo wa Kwanza haukutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema uwepo wa demokrasia ya haki ni pale tunapokubaliana kuwa kuna kushinda na kushindwa katika uchaguzi; na wananchi wana haki ya kuongozwa na wale ambao wamewachagua kupitia demokrasia ya sanduku la kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yanayoendelea kwa upande wa pili wa Muungano, yaani Zanzibar ni ushahidi ulio wazi kuwa demokrasia ya haki ambayo ni kichocheo cha maendeleo kwa nchi, bado kwa nchi yetu ni kitendawili.

Pia, haki ya wananchi kutoa na kupata habari kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 18 (b) na (c) ni suala ambalo Bunge kama Taasisi linatakiwa kuhakikisha haki hii ya Kikatiba inalindwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshuhudia kuwa siku za karibuni Bunge limeingia katika taharuki kwa Askari Polisi ambao hawakuvalia nguo rasmi za kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge, wakiingia na kufanya fujo. Hii ni kudhalilisha Bunge katika sura za Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wote ambao ni Wabunge wapya na hawafahamu haki za *minority* katika Bunge ni kuwa na haki ya kuzuia hoja ili kufikiwa kwa maamuzi yenye muafaka wa pamoja kwa hoja za Serikali. Jambo hili kwa mila na tamaduni za Kibunge halitafsiriki kama ni fujo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele (b), Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano lliyopita, yaani 2011 mpaka 2015, hali ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopita unaonesha kwamba ukuaji wa uchumi umekua kwa wastani wa 6.7%. Hata hivyo, sekta zinazoonekana kukua zaidi ni pamoja na Sekta za Madini, Elimu, gesi, Ujenzi, Uzalishaji, Mauzo ya Nje, Bidhaa za Viwandani, Huduma za Fedha pamoja na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zinazotajwa kukua ni sekta ambazo kwa ujumla wake hazina mahusiano ya moja kwa moja na uzalishaji wa ajira na/au kupunguza umasikini kwa wananchi wetu. Ndiyo maana kasi ya umasikini wa kipato inaendelea kuongezeka zaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji wa mpango ni kuwa pato la Taifa limekua kutoka wastani wa Sh. 770,000.3 kwa mwaka, kutoka mwaka 2010 hadi kufikia wastani wa pato la Sh. 1,724,415.6 kwa mwaka 2014. Hii maana yake ni kwamba, kwa mwezi wastani wa pato la mwananchi ni Shilingi 143,701.25. Ukigawanya kwa siku ni sawa na kipato cha Shilingi 4,970.04.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili na wananchi kwa ujumla kama Sh. 4,900/= kwa siku zinatoshia kuhudumia familia kwa siku nzima.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuacha kujitapa kwamba uchumi umeongezeka, wakati kipato cha mwananchi wa kawaida hakitoshelezi mahitaji na ugumu wa maisha unaendelea kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipendekezwa katika Mpango uliopita kwamba Serikali itenge 35% ya mapato yake ya ndani ili kugharamia Bajeti ya Maendeleo, lakini kwa miaka yote mitano Serikali haijawahi kufikia kiwango hicho, jambo ambalo limeiacha miradi mingi kutokukamilika kutokana na kutegemea fedha za Wahisani ambazo haziji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana namna ambavyo mpango ama mapendekezo yatakavyogharamiwa na kuonesha bayana vyanzo thabiti vya mapato ya kugharamikia Mpango na siyo kuweka ahadi za Wahisani ambazo hazina uhakika wa 100% kama vyanzo vya mapato vya kugharamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Mwaka 2011 - 2015 unasema, Sekta ya Elimu peke yake ilikuwa inahitaji Walimu 900,000 wenye ujuzi, ikilinganishwa na Walimu 238,000 waliopo sasa. Katika Sekta ya Afya idadi ya wataalam walikuwa wanahitajika 110,000 waliopo sasa; italazimika kuongezeka mara nne hadi kufikia wataalam 476,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inalenga kufikia mwaka 2015 kuwa na Wanasayansi 26,000; Wasanifu na Wahandisi 88,000; Wanasayansi wa Afya 22,000; Tabibu wa meno na mifugo 64,000; Wataalam wa masuala ya kiuchumi 30,000; wataalam wa Uhasibu na Usimamizi wa Fedha 63,000; Walimu 320,000, wataalam wa ngazi za Umeneja 130,000 ili kufikia malengo hayo ya Wataalam ifikapo mwaka 2015/2016. Tuna swali la kujjuliza: Je, tumefikia malengo hayo mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa iliyotolewa mwezi Juni, inaonesha kuwa wanafunzi katika vyuo vyote vya VETA nchini kote walikuwa 164,000 tu. Wanafunzi katika Vyuo Vikuu vyote nchini walikuwa 204,175 na Wahitimu mwaka 2015 walikuwa takriban 30,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango uliweka malengo mahususi katika Sekta ya Elimu ikiwemo kujengwa kwa *Campus* ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Muhimbili na utekelezaji wake mpaka sasa bado haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi tano za Elimu ya Juu kukarabatiwa na kuwa na wafanyakazi wenye utaalam wa VETA 635,000. utekelezaji mpaka sasa, watu wenye ujuzi wapo 200,000 tu. Taarifa za ukarabati wa Taasisi za Elimu ya Juu bado haijulikani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Nishati Mpango uliwekwa kuzalisha *Megawatt* 2780 za umeme kwa kipindi cha miaka mitano. Maana yake ni kwamba kila mwaka ilitakiwa kuzalisha *Megawatts* 556 ili kufikia lengo lililowekwa na Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, imeongezeka kwa *Megawatts* 346.24 katika uzalishaji wa umeme nchini. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tuliongeza uzalishaji wa *Megawatt* 69.248 hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwendo huu, ili kufikia lengo la kuzalisha *Megawatts* 2,780 tunahitaji miaka 40 ili kuweza kufikia lengo la Mpango ambalo linaweza kutimia ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili, ni kwa nini haikutekeleza lengo la Mpango wa Maendeleo wa kuzalisha *Megawatts* 2,780 katika kipindi cha miaka mitano ambayo inakwenda kwisha juni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba aliyekuwa Waziri wa Nishati katika Serikali iliyopita, ambaye ndiye aliyetekeleza huo Mpango, ndiye Waziri wa sasa wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili, Waziri wa Nishati wa sasa atakuwa na muujiza gani wenye nguvu wa kumwezesha kutekeleza Mpango huu, ikiwa alishindwa kutekeleza Mpango uliopita? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa barabara na usafirishaji, Mpango uliopita ulikuwa umeweka lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 5,204 kwa kipindi cha miaka mitano. Hii ina maana yake ni kwamba, kila mwaka zilitakiwa zijengwe kilometa 1,040.8 za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Utekelezaji ya Mpango uliopita inaonesha kwamba zimejengwa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2,775, sawa na 53% kwa kipindi cha miaka mitano, ikiwa ni pamoja na ukarabati wa barabara hizo. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tulijenga na kukarabati kilometa 555 tu kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili, itatekeleza vipi ujenzi wa barabara zilizosalia katika Mpango uliopita? Au Mpango huu mpya utakuwa unatekeleza viporo vilivyoachwa na Mpango uliopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi inapenda kuwakumbusha Watanzania kwamba, aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wa wakati wa utekelezaji wa Mpango uliopita, ndiye Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

ambapo alitekeleza Mpango kwa 53% tu katika Sekta ya Barabara. Je, Waziri wa Ujenzi wa sasa atakuwa na muujiza gani kutekeleza Mpango mpya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Usafiri wa Anga, hakuna jambo la maana la kiutendaji ambalo limefanyika, kwani Serikali inajaribu kuonesha ongezeko la abiria na kusema limekuwa likitokana na ujio wa Shirika la *Fast Jet* nchini pamoja na kufunguliwa kwa Kiwanja cha Ndege cha Songwe na ukarabati wa viwanja vingine vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Serikali haisemi na haijaliweka wazi ni kuwa, wameshindwa kufufua Shirika letu la Ndege kwa kununua ndege. Jambo lingine ambalo halielezwi, ni wazi kuwa kuongezeka kwa abiria ama abiria wameongezeka na hasa kutokana na ongezeko la wataalii kutokana na ukweli kuwa ni baada ya nchi ya Kenya kuingia na kupambana na wapiganaji wa Al-shabab kule Somalia na mashambulizi kuendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango uliopita uliweka lengo la kukuza Sekta ya Kilimo ili iwe inakua kwa 6% kwa mwaka. Hata hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huo sekta hii ilikuwa kwa wastani wa 3.4% tu kwa mwaka kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kwa kipindi cha utekelezaji wa Mpango, inaelezwa kuwa kiliongezeka kutoka hekta 345,000 hadi kufikia hekta 461,000 na hakikuweza kufikia lengo la hekta 1,000,000. Aidha, kwa mwendo huu wa kukuza Sekta ya Umwagiliaji, kukua kwa hekta 23,127 kwa mwaka, maana yake ni kuwa ili kufikia hekta 1,000,000 tunahitaji miaka 43 ili tuweze kufikia lengo hilo tulilojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ambacho kilitegemea kuchangia 12.9% kwenye pato la Taifa kiliishia kuchangia 7% tu. Aidha, katika utekelezaji wa mpango, mazao ambayo yanaonekana kuongezeka katika uzalishaji ni pamoja na mpunga, mahindi na miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umeshindwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo tangu uhuru yalikuwa ndiyo mhimili mkubwa katika kulipatia Taifa fedha za kigeni; mazao kama korosho, mkonge, kahawa, pamba, chai na tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi, inakipeleka wapi kilimo cha nchi hii ambacho imekuwa ikikiundia kaulimbiu mbalimbali; badala ya kukipeleka kilimo mbele inakipeleka nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya deni la Taifa ni ya kutisha sana na tunakoelekea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na wenye jukumu la kuisimamia Serikali ambao ni Bunge, basi nchi inaweza kufilisika kama ilivyotokea kwa nchi ya Ugiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa limekua na kufikia kiasi cha Dola za Kimarekani 19,141,000. Hii ni sawa na Shilingi trilioni 41.5 kwa *exchange rate* ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni hili limeongezeka mara dufu mwaka 2015 baada ya Serikali kukopa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 3.8467 au Shilingi trilioni 8.3 kwa *exchange rate* ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni mwa mwezi Juni, 2010 jumla ya deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani bilioni 9.9 kulingana na viwango vya kubadilisha fedha katika mwezi huo wa Juni. Kiasi hicho kilikuwa sawa na Shilingi trilioni 13.6, miaka mitano deni limefikia trilioni 41.5. Ni lazima kama Bunge, tushtuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ya kujiuliza, fedha zilizokopwa kuanzia mwaka 2010 mpaka 2015 zilifanya miradi ipi ya maendeleo? Mikopo hii ina riba kiasi gani? Tumeweka nini kama dhamana, ili kupatiwa mikopo hii? Au ile minong'ono mitaani kuwa vitalu vya gesi ndiyo dhamana, ni sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo mkubwa wa mwaka 2010 ambao ni sawa na 5.6% ya deni lote ulitumika kufanyia jambo gani? Fedha hizi zimetumika kugharamikia miradi gani? Au ndiyo EPA ya Uchaguzi wa Mwaka 2015? Maana kila utawala unapokuwa unaondoka ama kuingia utawala mpya, tangu Mfumo wa Vyama Vingi hapa nchini pamekuwepo na utaratibu wa EPA za Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 kulikuwa na EPA ya IPTL, Mheshimiwa Mwinyi kwenda kwa Mheshimiwa Mkapa; Mwaka 2005 kulikuwa na EPA ya BOT, Mheshimiwa Mkapa kwenda kwa Mheshimiwa Kikwete; Mwaka 2015 EPA ya deni la Taifa, Mheshimiwa Kikwete kwenda Mheshimiwa Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya maswali haya yatapatikana tu kama itafanyika *Special Audit* ya deni la Taifa. Mkopo huu ni hatari zaidi kama hautalipwa kwa wakati, kwani riba itaongezeka maradufu na kuifanya nchi ifilisike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya

Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) ya deni la Taifa na kuleta taarifa ya ukaguzi huo Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokulipa deni unalodaiwa ni ghali. Katika miaka ya 1980 Tanzania ilikopa Dola za Kimarekani milioni 49 kutoka Brazil ili kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha Morogoro na Dodoma. Deni hilo halikulipwa mpaka ilipofika mwaka 2010, deni liliongezeka maradufu hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 240. Bahati njema kwa Tanzania ni kwamba, baada ya mazungumzo ya muda mrefu, Viongozi wa Brazil walikubali kulifuta deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mikopo ya fedha isipolipwa kwa wadai kwa makubaliano yanavyosemwa, inasemekana kwamba baada ya mwongo mmoja fedha hizo zitafikia kiasi ambacho itakuwa vigumu sana kwa Tanzania kuzilipa.

Mathalan, iwapo mkopo utatozwa riba ya 5% kwa mwaka zinazopaswa kulipwa kila mwezi na mkopo huo usilipwe katika kipindi cha miaka kumi kiasi hicho kitakuwa kimeongezeka kwa 65% na deni likaongezeka maradufu katika kipindi cha miaka 15. Kutokulipa deni unalodaiwa ni ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi muda mrefu unavyopita bila kutimiza wajibu wa malipo, ndivyo riba inavyozidi kukua. Deni ambalo Serikali ya Tanzania ilikuwa inadaiwa na Brazil ni mfano dhahiri unaoonesha jinsi gani hali inavyoweza kuwa mbaya. Hatari inajitokeza zaidi katika mikopo ya kigeni inayotolewa kwa masharti ya kibiashara ambayo kwa kawaida haina muda wa unafuu (*Grace Period*) na kufanya malipo na kutoza viwango vikubwa vya riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi mwingine ni iwapo Tanzania itamudu kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati. Kwa sasa inashindwa kulipa madeni yake yote na kuendelea kukopa kibiashara, jambo ambalo linaweza kuiingiza nchi katika hali ngumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uwasilishaji wa Mpango wa Mpango wa Maendeleo wa Awamu ya Kwanza katika Bunge lako Tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, Serikali imekuwa na mipango mingi na vipaumbele vingi ambavyo mwisho wake italetta changamoto katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia kwa Waziri aliyekuwa anahusika na Mipango ya Serikali, Mheshimiwa Stephen Wassira, alibeza hoja hiyo ya Kambi ya Upinzani kuwa, ilikuwa haina msingi wowote katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano kwa Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitokana na Msingi kuwa tayari kulikuwa na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA). Katika hali ya kushangaza baadaye, Serikali hiyo hiyo kabla ya miaka mitano ya mwanzo kumalizika, yaani mwaka 2013 ikaja na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo (*framework*) ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 katika ukurasa wake, inaonesha kuwa Serikali mwezi Mei mwaka 2015 iliamua kuunganisha MKUKUTA wa Mpango wa Maendeleo kwa sababu mipango hiyo ilikuwa inafanana na pia ilikuwa na udhaifu katika uratibu, tathimini na namna ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani wakati huu ilikuwa sahihi na ndiyo maana Serikali ilikaa kimya ikachukua na kutekeleza kwa vitendo hoja hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kuheshimu na kutekeleza hoja mbalimbali zinazotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwelekeo wa Mpango unaowasilishwa unakosa vipaumbele kama ambavyo inaonekana katika nyaraka ya Mwelekeo, ukurasa wa tatu, ambao unasomeka kama ifuatavyo; *“Developing criteria on identifying Areas for prioritization and sequence of particular industries and sub-sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo huu ulitakiwa uwe na vipaumbele ili iwe rahisi kwa Waheshimiwa Wabunge, kujadili na kutoa maoni yao ili kuiwezesha Serikali kuwa na vipaumbele vinavyotekelezeka. Mwelekeo wa Mpango unaonesha maendeleo ya viwanda nchini pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinagusa masuala yote ya maendeleo ya viwanda toka nchi ilipopata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa nchi yetu haitapiga hatua kimaendeleo bila kuwa na maendeleo ya viwanda. Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo unaonesha kuwa Sera ya Maeneo maalum ya Uwekezaji (SME) na (IPZ) hayana mikakati ya kusimamia utekelezaji wake yaani ukurasa wa 19 wa mwelekeo wa Mpango. Aidha, tathimini ya tija ya maeneo maalum ya uwekezaji hayawezi kukidhi malengo ya uanzishwaji wake. Ikumbukwe kuwa maeneo haya ya uwekezaji yamechochea migogoro ya ardhi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwasilisha tena marekebisho ya Sheria ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji ili kutatua changamoto ambazo zinayakumba maeneo hayo ikijulikana kuwa na

sera pekee haitakuwa na nguvu ya utekelezaji, kwa kuwa Sera haina nguvu ya utekelezaji wa kisheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasimu ya mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2016/2017, ni mwelekeo na siyo Mpango wa Maendeleo. Kwa hiyo, kwa sababu Bunge linajadili Mpango na siyo Mwelekeo tu wa Mpango, kama ambavyo tulisema hapo awali Bunge lako Tukufu limetengua Kanuni ya 94 kwa hoja ya muda tu, badala ya kujadili Mpango uliopaswa kuwasilishwa mwezi Oktoba, Novemba ujadiliwe sasa, lakini dhana nzima ya matakwa ya Katiba ya Ibara ya 63(3)(c) ya kujadili Mpango iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kambi ya Upinzani inaona kuwa sababu kubwa inayosababisha Mpango wa Maendeleo ya Taifa uliopita kushindwa kutekelezeka ipasavyo na hivyo kutokufikia malengo yake ni kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa mamlaka kwa Bunge kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa kama katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kupitisha Mpango huo ama maelekezo hayo bila kutungia sheria hautatekelezeka kama Mipango iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mukstadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inalitaka Bunge iliagize Serikali kuleta mara moja kwa hatua ya dharura Muswada wa Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango mpya utakaokuja mwezi Juni wa Taifa wa Maendeleo kabla Bunge lako halijauidhinisha. Kinyume na hapo ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Silinde tunakushukuru sana. Naona umetumia muda wako vizuri kabla ya wakati, mzoefu, al-maarufu.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshapokea maoni yote kutoka kwa Wizara ya Fedha, Waziri, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na mbele yangu sasa tunaanza kuchangia.

Jumla hapa nina majina 57 kwa leo na ningeomba niwataje wengine wajijue kabisa anapoanza yule mchangiaji wa kwanza ni nani anafuatia. Kwa

kuanzia, naomba nimwalike Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulilie, yeye ataanza. Kila mchangiaji nampatia dakika kumi kwa mujibu wa Kanuni tulizokubaliana, lakini Mheshimiwa Mwanne Mchemba jiandae, baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Zacharia Issaay na mwisho pia kabla sijaendelea Mheshimiwa Pauline Gekul jiandae. Mheshimiwa Faustine Ndugulilie, karibu!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishaji mzuri pamoja na heka heka ambazo tumezipata mwanzoni mwa wiki, lakini Wahenga wanasema kawia ufike. Naomba nijielekeze moja kwa moja katika Hotuba na mapendekezo ya Serikali kuhusiana na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja, pamoja na vipaumbele vyote ambavyo tumeviweka, ningependa kuona Serikali inaweka kipaumbele katika ujenzi wa reli ya kati. Naungana na Wabunge wote wa mikoa yote ambao wamekuwa wanaliongelea suala la reli ya kati. Tukitaka kupaisha uchumi wetu, tukitaka kuimarisha uchumi wetu bila ya kuwa na reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* naamini kabisa tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Serikali itakapokuja kufanya hitimisho tunataka kauli iliyokuwa thabiti na wala isiyopinda kuhusiana na nini mikakati yetu ya kujenga reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, tumeliongea sana, tuliliongelea katika Bunge la Kumi, sasa umefika muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tungependa kusikia na kuona Mpango wa Serikali katika kuimarisha Bandari ya Dar es Saalam, tuipanue, kuna kazi kubwa ambayo mmeweza kuifanya na nimpongeze sama Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya ya maboresho katika bandari. Bado tunahitaji kupunguza muda wa utoaji mizigo pale na kuongeza ufanisi na ikiwezekana bandari yetu iwe inafanya kazi saa 24. Hii iendane sambamba na upanuzi wa Bandari ya Mtwara, ni bandari ambayo inakuja kwa kasi, tukiweza kuwekeza katika Bandari ya Mtwara, hakika kabisa tutakuwa tumepiga hatua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nichangie, ni ushirikishwaji wa sekta binafsi. Nchi yetu ina sera nzuri sana ya ushirikishaji wa sekta Binafsi (*Private Public Partnership*) na tuna sheria ambayo inaendana na hiyo sera ambayo tunayo. Katika upande wa utekelezaji tumekuwa na

changamoto kubwa sana, sasa nadhani umefika muda muafaka, miradi yote hii, mipango yetu yote hii, hatuwezi tukaifanya kwa hela ya Serikali, tuishirikishe sekta binafsi katika baadhi ya hii miradi ili sasa Serikali ijikite katika ile mipango mingine mahususi, haya mambo mengine tuweke mazingira mazuri ya uwezesaji ili sekta binafsi iweze nayo kufanya kazi na tuwape *support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja ambayo imekuwa ipo ni kwamba Serikali imekuwa na *bureaucracy* kubwa sana na tumekuwa tunawa-*frustrate* sana wawekezaji ambao wanataka kuja kushirikiana na sisi Serikali. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itengeneze mazingira mazuri ili kwa wawekezaji binafsi tuweze kuwashirikisha kwa kupitia mpango wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuligusia ni eneo la barabara hususani katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tumekuwa tunaliongelea sana jambo hili, Dar es Salaam sasa hivi kwa mtu kutoka maeneo anayoishi kuweza kufika mjini si chini ya masaa mawili na masaa mawili tena wanayatumia kutoka katika maafisi kwenda majumbani. Tumekuwa tunaongelea masuala ya barabara ya mzunguko (*ring roads*). Niiombe sana Serikali ifike sasa wakati tuwekeze na tuwe na dhamira ya dhati kuwekeza katika barabara za mzunguko katika Mkoa wa Dar es Salaam, tuondokane na hii adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kufanya *investment* kubwa kwa wakati mmoja, tunaweza tukawa tumeondokana na hili. Tuna miradi mingi ambayo tumeweza kuifanya, tuna Mradi *DMDP*, lakini tuje na mradi mahususi ambao utaondoa kero ya usafiri katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tunashukuru kwa kuona kwamba zile *flyovers* zimeanza kujengwa, lakini niongelee kwa upande wa mimi kama Mbunge wa Kigamboni, tumejenga daraja, linakamilika mwezi Machi, lakini tuna changamoto ya *approach roads* kwa upande wa Kigamboni lakini vilevile kwa upande wa Kurasini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili daraja halitakuwa na manufaa iwapo zile *approach roads* kuanzia Bendera Tatu mpaka Kamata hazitajengwa. Niiombe sana Serikali, tumefanya *investment* kubwa sana ya *over two hundred billion* pale katika Daraja la Kigamboni lakini tuhahitaji zile *approach roads* ili sasa lile daraja liweze kutumika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuligusia ni upande wa maji. Inasikitisha kuona kwamba nchi yetu ni asilimia ndogo sana ya wananchi ambao wana huduma ya maji. Ni jambo ambalo nalo tumekuwa tunaliongelea kwa muda mrefu sana, tumeweka mikakati na nakumbuka katika Bunge la mwaka jana au mwaka juzi tuliweka mikakati mahususi na tukatenga bajeti, kwamba, Serikali itumie fedha hii katika kuhakikisha kwamba huduma ya

maji tunaisambaza. Naungana mkono na Wabunge wengine ambao wana mtazamo tuwe na Agency kama REA kwa ajili ya maji vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, hii itasaidia sana na tu-specify vyanzo vya mapato ambavyo vitakwenda pale kuhakikisha kwamba kama tulivyokuwa na Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Umeme Vijijini, basi tuwe na chanzo cha fedha kwa ajili ya maji vijijini, itatusaidia sana kuweza kupiga hatua katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena katika eneo hilo la maji, tuna mradi wa maji ya chini kule Kimbiji, Kigamboni, mradi ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, unachimba visima 20,000. Niwaombe sana, mradi ule unasuasua mno na ni mradi muhimu sana kwa sisi wakazi wa Kigamboni ambao hatuko katika mfumo wa maji salama kwa DAWASA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mradi ule uharakishwe na usambazaji uweze kufanyika na wanufaika wa kwanza wawe wananchi wa Kigamboni. Hatutakubali maji yale yakaondoka Kigamboni bila wananchi wa Kigamboni kuwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka kugusia katika sekta ya afya, tuna changamoto kubwa sana. *Burden of disease* inazidi kuongezeka, tuna magonjwa ya kuambukizwa na sasa hivi tunaanza kuona magonjwa yasiyoambukizwa, *none communicable diseases*. Idadi ya wananchi wa Tanzania inaongezeka kwa kasi kubwa sana, sijui kama wachumi wetu na sisi mnakaa mnaliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunaongeza Watanzania takribani milioni moja, Watanzania hawa wanahitaji huduma za jamii, bajeti ya afya inashuka kila mwaka, sasa hivi tuko kwenye *eight to nine percent*. Kuna umuhimu sasa wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na vyanzo mbadala vya kuendesha sekta ya afya na mimi ni muumini mkubwa sana wa *universal coverage*, wananchi wote tuwaingize katika mfumo wa bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala la UKIMWI linatufedhesha sana. Asilimia 90 ya fedha za kuendesha mradi wa UKIMWI nchini zinatoka kwa wafadhili na sasa hivi tuko katika hali ngumu kidogo, wafadhili wametuingia tuweke *Matching Funds* ambayo sisi hatujaweka. Mwaka jana tumepitisha Sheria ya *Aids Trust Fund*, ni hatua nzuri, lakini niombe sana twende mbali zaidi ku-specify, kwa sababu mwaka jana tuliweka kwamba tuwe na *three hundred billion* Serikali haiku-commit hiyo fedha. Kwa hiyo, niombe sasa twende mbali, tu-identify vyanzo na tuweze kuwa na fedha za kuendesha Mfuko wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana na naipongeza Serikali kwa uwasilishaji mzuri. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache kuhusu mapendekezo ya Mpango kwa kazi tuliyokuwa nayo mbele yetu ya Kitaifa ya maendeleo.

Awali ya yote nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru wapiga kura wangu walionichagua baada ya kunipa likizo kwa miaka mitano tena. Kwa hiyo, nawashukuru mama zangu wameweza kunipa nafasi mbili nikiwa kama Mwenyekiti wao wa Mkoa, lakini si hilo tu wakanipa na nafasi ya Ubunge, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa taarifa na Mapendekezo ya Mpango aliotuletea. Wakati nasoma nimeona amegusa sekta zote na hizi sekta kubwa ambalo tunamwomba ni utekelezaji, hilo ndilo kubwa, lakini Mpango, Maelekezo, itakavyokuwa, lakini kitabu hiki kinakidhi maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja bila kupoteza muda kwenye upande wa viwanda. Viwanda hapa nchini amezungumzia kwenye ukurasa wa 24, viwanda twende kwa kufuata jiografia. Viwanda vingi vimefungwa, maeneo mengine hayana viwanda kabisa na sehemu nyingine viwanda vilikufa. Kwa mfano Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi, tunalima tumbaku, lakini mpaka sasa kiwanda kiko Morogoro. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika Mpango huu iangalie ni jinsi gani ya kuweka kiwanda cha uchakataji katika Mkoa wa Tabora ile ni *center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu kulikuwa na Kiwanda cha Nyuzi, kiwanda hiki kilikuwa kinachakata nyuzi kama nyuzi, nyuzi hizo ni za pamba. Wazalishaji wa pamba wakuu ilikuwa ni Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kigoma, lakini pamba hizi zinasafirishwa badala ya kuzalisha kwenye Kiwanda cha Nyuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali katika Mpango unaoletwa iangalie ni jinsi gani ya kuweka kiwanda kizito kama kile katika eneo hilo, kwa sababu lazima tutafute *center*, jiografia yetu inasemaje. Si hilo tu, kuna viwanda ambavyo vimefungwa na vinatarajiwa kufungwa kutokana na mafuta yanayokuja, kwa mfano, kutoka nje au viwanda ambavyo vinazalisha nchini kukosa malighafi. Pia kuna viwanda ambavyo mpaka hivi sasa, kwa mfano, Viwanda vya Mafuta, vingi vinategemea kufungwa kwa sababu mafuta yanaletwa kutoka nchi za nje. Hawa wanalipa kodi kubwa, lakini viwanda vinapofungwa ni athari kubwa kwa nchi yetu kwa sababu ajira inakuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla, watusaidie kuhakikisha kwamba wanalinda viwanda vyetu vya nchini ili kuweza kupata ajira ya kutosha. Pia kutoa elimu kwa vijana wetu ili waingie katika soko la ushindani. Kwa hiyo, tunaomba wenye viwanda pia waweze kutoa mafunzo kwa wale wafanyakazi wao ili tuweze kwenda nao pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma kulikuwa na viwanda vya *SIDO*. *SIDO* ni mkombozi mkubwa wa viwanda vidogo vidogo, hiyo nayo isisahaulike, *SIDO* ni mkombozi, akinamama wengi, vijana wengi wamejitokeza kupata mafunzo kwenye viwanda vidogo vidogo vya *SIDO*. Hata hivyo, si hilo tu, niombe Serikali yangu ni sikivu, haina wasiwasi, tena haya tunayoyazungumza asiwe na wasiwasi mtu yeyote kwamba hayatachukuliwa, yatachukuliwa na yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoathiri viwanda vya ndani na tusipoviwezesha viwanda vya ndani nchi yetu tunaikoshesha mapato, kwa sababu asilimia kubwa ya mapato inategemea sana viwanda. Kwa hiyo, kubwa ambalo ningeishauri Serikali, walinganishe, waoanishe, sera ya viwanda na sera ya biashara. Hivi vitu viwili vinakinzana na kama vinakinzana vinatuathiri sana. Nimwombe Waziri wa Viwanda aliangalie hilo, ashirikiane pia na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tena kwenye suala la reli, limezungumziwa kwenye ukurasa wa 53, lakini halikukaziwa, limewekwa juu, juu. Niombe kwa niaba ya wenzangu na wenyewe watachangia, tusilete mzaha kwenye suala la reli ya kati. Reli ya kati itatutenga sana. Hatuwezi tukaidharau kwanza kwa mambo mawili, wapiga kura wetu na wananchi wetu wa Tanzania wanategemea sana reli ya kati, wanategemea sana TAZARA, lakini si hilo, ubebaji wa mizigo barabara zote zinaharibika kwa sababu ya magari mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoweza kuimarisha reli, ingawa wamesema latiri 80 kwa kipande, kwa mfano, wamesema kati ya Igalula, Tabora, Lolangulu, jamani tuizungumzie yote ili ifike Kigoma, ifike Mpanda, ifike Mwanza ili wabebe mizigo yote, hata hao nchi za nje wanategemea reli hii iwaunganishe kutoka Dar es Salaam kwenda huko. Unaposema kwamba nyingine ianzie huku kwa kweli niombe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Bado dakika zangu.

**MWENYEKITI:** Kengele hiyo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati... Bado ni ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Ya pili? Hapana Mwenyekiti ni ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisibishane na wewe naunga mkono hoja, lakini ni ya kwanza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimemtaja Mheshimiwa Zacharia Issaay, hayupo basi Mheshimiwa Pauline Gekul, naye hajafika?

**WABUNGE FULANI:** Yupu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, karibu!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini nilikuandikia ki-note, naomba nichangie kesho asubuhi.

**MWENYEKITI:** Ruksa ahsante. Mheshimiwa Jesca Kishoa, yupo? Karibu!

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote, nikishukuru Chama changu kwa yote, lakini pia nimshukuru mume wangu David Kafulila ambaye pamoja na mimi kuwa mama ametambua ninayo nafasi ya kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye mjadala. Tunajadili Mpango, lakini niseme kwamba mipango siyo tatizo katika Taifa, Taifa hili hatuna umaskini wa mipango, ila tuna tatizo la utekelezaji wa mipango. Tumeshakuwa na mipango mingi, ukiangalia kuanzia mwaka 1981 mpaka 1986 tumekuwa na Mpango mwingine kuanzia mwaka 1987 mpaka mwaka 2002, huu ulikuwa ni Mpango wa kumi na miaka mitano ambao ulikuwa umelenga kwamba mpaka kufikia mwaka 2002 Tanzania iwe nchi ambayo itakuwa ina mfumo wa ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukaja kuwa na Mpango mwingine wa miaka 25 kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2025 ambao lengo lake lilikuwa ikifika mwaka 2025, Tanzania iwe ni nchi yenye uchumi wa kati na mipango mingine mingi iliyofuata. Hata hivyo, hii mipango haitekelezeki na haitekelezeki kwa sababu kubwa mbili. Sababu ya kwanza, ni mfumo mbovu tulionao katika Taifa hili na sababu ya pili ni ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi zote ambazo tumeshafatana nazo katika masuala ya maendeleo kuanzia mwaka 1963; Malaysia, Singapore, Korea Kusini, nchi zote hizi mpaka hivi sasa zimeshakuwa wahisani wetu na zimekuwa wahisani wetu kwa sababu mipango yetu inashindwa kutekelezeka. Nimetangulia kwa kusema kwamba sababu kubwa ni mfumo mbovu, lakini pia na ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mbovu kwa maana gani? Kwa sababu ya muda nitazungumzia kwenye suala la elimu kwenye suala la mfumo mbovu. Leo hii tunazungumzia elimu bure, ni suala ambalo naamini kabisa kwamba Watanzania na wazazi wote wa nchi hii wamelifurahia, lakini tunazungumzia elimu bure wakati huo huo kuna changamoto nyingi. Nilimsikia Mheshimiwa Waziri anasema hivi bado zimebaki changamoto ndogo ndogo pamoja na elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi changamoto ndogo ndogo zina uhusiano mkubwa na *performance* ya wanafunzi. Niseme hivi ni bora mngihakikisha mnaondoa hizi changamoto, halafu mkasema elimu bure. Mfano, mwaka 2015, Taasisi ya Haki Elimu ilitoa ripoti ikasema hivi; katika Taifa letu kuna upungufu wa madawati 1,170,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu ya haraka haraka kama kwenye dawati moja wanakaa wanafunzi watatu watatu, inamaanisha Taifa letu kuna wanafunzi milioni tatu na ushee wanakalia mawe, kwenye nchi ambayo ni ya tano kwa idadi ya misitu Afrika nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwanafunzi anakaa kwenye mawe, mwalimu anakuja darasani kufundisha somo la historia, anaandika zama za kale za mawe, anajuliza hizi ni za kale au ni za sasa? Ningeomba kwanza waelekeze kwenda kutatuta changamoto zilizopo kwenye mashule, halafu wakaja wakatuambia elimu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala la utawala bora, muundo wa suala la utawala bora kwa ujumla. Mfano mzuri ni hapa Zanzibar wala siyo mbali, unapuzungumzia Zanzibar leo hii ni aibu, hivi karibuni nilimsika Donald Champ, mgombea wa *Republican* Marekani, anasema Afrika wanahitaji miaka 100 kuendelea kutawaliwa kwa sababu hawajajitambua. Mpaka anafikia hatua ya kusema hivyo ni kwa sababu ya mambo kama yanayoendelea Zanzibar, tunadhaliisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, mnaweza mkasema kwamba labda kwa sababu mpo madarakani, lakini ni hivi Marekani wamesema uchaguzi wa Zanzibar ulikuwa *fair and free*, Ulaya wakasema uchaguzi wa Zanzibar ulikuwa *fair and free*, mtasema aaa! Hao ni wa mbali, SADC hapa Kusini kwetu

wamesema uchaguzi wamesema ulikuwa *fair and free*, AU wamesema ulikuwa *fair and free*. Tatizo ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 nikiwa na miaka mitatu, mlianzisha kitu kinaitwa *multipartism* mkimaanisha mfumo wa vyama vingi ambao mlilibaliana kwamba kila baada ya miaka mitano kutakuwa kuna utaratibu vyama vinagombea mbalimbali kinachochukua nafasi kinashika dola. Sasa niseme tu kwamba, kinachoendelea Zanzibar ni suala la kukosa ustaarabu tu na siyo vinginevyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Rais Mafuguli aweke mkono wake Zanzibar. Nasema hivi kwa sababu gani? Hata awe mzuri kiasi gani Zanzibar akiharibu hawatamwelewa, kuna msemu unasema hivi: “*You cannot stand for something you don't know and likewise it doesn't matter how much you know about something, if you cannot stand up on it.* Kinachoendelea Zanzibar kama Magufuli hataingia, maana yake ni kwamba Wazanzibari hawatamwelewa, maana ingekuwa Kilimanjaro angeingilia halafu ninyi mnahubiri kwamba hii ni nchi moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Magufuli, suala la Zanzibar alitazame kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ufisadi unaturudisha nyuma sana, namwomba Mheshimiwa Magufuli, kwa sababu ninaposema ufisadi namaanisha ni miongoni mwa sababu inayopelekea hii mipango tunayojadili hapa isitekelezeke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi unaoendelea sasa Mheshimiwa Magufuli anatakiwa auone na auangalie kwa ukamilifu kwa sababu huu ni muda sasa amemaliza kutumbua vipetele, atumbue majibu makubwa mengine anakaa nayo mezani. Imefika wakati ni lazima tuseme, kwa sababu kinachoendelea katika Taifa hili tukikaa kimya, tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka jana, kuna ripoti ililetwa hapa, tulieni siyo *ESCROW*, kuna mjadala ulikuja hapa ukiachana na *ESCROW*, lilikuwa ni suala la mabehewa. Mwaka jana Taifa letu limeingia hasara ya bilioni 238, hizi zilikuwa ni fedha za wananchi ambao zilikwenda kununua mabehewa, matokeo yake, mabehewa yalikuwa *fake*. Haya siyo maneno yangu, hii ni ripoti *PPRA* ambayo ilileta ripoti kwenye Kamati ambayo nipo mimi. Mabehewa yanaonekana kwanza ni *fake*, lakini cha ajabu hata kampuni iliyopewa tenda ni kampuni ambayo haikufanyiwa *due diligence* kwa maana ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa limeingia hasara ya bilioni 238 kwa sababu ya mtu tu kuwa mzembe kuwajibika, halafu leo jipu linahamishwa mkono wa kushoto, linapelekwa mkono wa kulia. Mheshimiwa Magufuli alitumbue na jipu hili liko humu ndani, tunaye Mheshimiwa Mwakyembe, leta ripoti hapa, ripoti kuhusiana na masuala ya mabehewa, mlikataa kuileta hapa kwa nini mnaficha, kama ni safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwakyembe umeaminiwa na Serikali na Magufuli lete ripoti hapa, tusijisahaulishe haya mambo tunayakumbuka tuliona hata tukiwa nje. Tunaomba tutendeeni haki wananchi wa Tanzania kwa sababu Bunge liliazimia ripoti iletwe Bungeni, naomba ripoti iletwe hapa Bungeni na tuweze kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca Kishoa. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Nsanzugwanko, naomba Mheshimiwa Mwalimu wangu Riziki Shahari ajiandae, Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Oscar Mukasa wajandae pia. Mheshimiwa Nsanzugwanko, karibu!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mapendekezo ya Mpango, nikisoma pamoja na mwongozo wake wa kuandaa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema katika Bunge hili kwamba katika utamaduni wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, Muswada kuwasilishwa mezani au na Waziri wa Serikali au na Mbunge na Muswada huu au hoja hii ikatolewa ni jambo la kawaida sana, ni jambo ambalo ni la kawaida kabisa na wala hakuna kitu ambacho ni cha ajabu. Nataka tuweke rekodi hizo kwa sababu yaliyotokea katika siku mbili ilionekana kama ni kitu kikubwa, lakini kumbe ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitajikita katika mambo makubwa matatu, nitajielekeza katika miradi ya Kitaifa ya kimkakati. Bila shaka huwezi kuzungumzia kukuza uchumi kama huwezi ukazungumzia miradi ya kimkakati. Miradi ya kimkakati tafsiri yake ni kwamba ni miradi ambayo ikitekelezwa itausukuma uchumi ule uweze kuzalisha mambo mengi zaidi na uweze kuzalisha fedha ziweze kutekeleza mambo mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika miradi ya kimkakati, kabla sijaendelea na jambo hilo naomba ukurasa wa tisa wa Mpango, tufanye marekebisho kidogo. Katika yale maeneo yanayolima kahawa, nimeona yametajwa pale katika ukurasa wa tisa, wamesema katika Wilaya za Moshi, Mbinga, Bukoba, Mbozi na Tarime, kana kwamba ndiyo zinalima kahawa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweke rekodi sawasawa, kwa takwimu za *Tanzania Coffee Board*, Mkoa ambao unatoa kahawa ya arabika bora katika nchi za Afrika Mashariki ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, naomba katika mpango ule katika ile miche ya kahawa, ijumuishie pia Wilaya ya Kigoma na Wilaya ya Kasulu ambako tunalima arabika ya kiwango cha juu kabisa na zaidi ya hapo hata *TaCRI* wana kitalu kikubwa sana cha kuzalisha miche zaidi ya 1,000,000 pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya kimkakati, niungane na wasemaji waliopita kuzungumzia suala la reli ya kati. Naona kuna *confusion* kidogo hapa, hivi tukisema reli ya kati maana yake nini? Reli ya kati maana yake ni kutoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma na unakuja *branch* ya Tabora kwenda Mwanza ndiyo reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa Mpango huu, reli ya kati ni pamoja na mchepuko kutoka Isaka pale Kahama kwenda Keza, Keza iko kwenye mpaka wetu na Rwanda na pia mchepuko wa kutoka Uvinza kwenda Msongati ya Burundi na pia mchepuko wa Kaliua, Mpanda kwenda Kalema bandarini na mchepuko wa Dodoma kwenda Singida, hiyo ndiyo reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka tuwe na uchumi wa viwanda, kama kweli tunataka nchi yetu ibadilike ingie katika uchumi wa kati, lazima tujenge reli. Sasa shida inakuwa pesa tunapata wapi, gharama ni kubwa kwa awamu kwanza tunahitaji takriba dola bilioni 7.6. Hii siyo fedha nyingi, nchi hii ni kubwa, tunakwenda kukopa, tuna marafiki wetu wa maendeleo, kuna Wachina na Wajapani wanatuamini na sisi tunawaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwamba hatuna fedha za kujenga reli, hatutaki kuisikia katika Bunge hili. Tunataka Serikali ije na mkakati mahsusi, mkakati wa msingi kabisa wa kwenda kukopa fedha hizi kwa Serikali ya Watu wa China, kwa Serikali ya Wajapani tujenge reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, bila ya kuwa na reli, tunacheza ngoma. Haiwezekani mizigo yote, makontena yote, mafuta yote yapite kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, ni nchi yetu pekee ambayo mizigo mizito inapita kwenye barabara. Matokeo yake

barabara hizi zinaharibika sana, inajengwa barabara ya kukaa miaka 30, uhai wake unakuwa ni miaka mitatu, minne, barabara inakuwa imeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, Waziri wa Fedha usipokuja na mkakati wa kujenga reli ya kati ikiwa na michepuko niliyoitaja, Isaka, Keza kwenda kubeba mzigo wa *nickel*, Uvinza - Msongati kwenda kwa ndugu zetu wa Burundi kuchukua mzigo wa Congo; mchepuko wa Kaliua, Mpanda - Kalema kwenda bandari ya Momba katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo kuchukua mzigo wa Lumbumbashi.

Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, utakapokuja na Mpango huo bila hiyo reli ya kati hatuwezi kuelewana katika Bunge na nitaomba Waheshimiwa Wabunge tusimame kidete kumwambia arejeshe Mpango huo mpaka atuwekee reli ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani miaka zaidi ya ishirini tunazungumza reli ya kati, lakini haijengwi, haiwezekani? Wenzetu Kenya wameanza kujenga Mombasa kwenda Kigali, kwa nini sisi hatujengi, kwa nini hatuanzi, utasikia tumekarabati kilomita 176 za latiri 80, hatutaki kusikia lugha hiyo na nchi yetu si maskini, ina rasilimali za kutosha, tunaweza tukazikopea kujenga reli ya kati na michepuko niliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati maana yake hizo reli zinakwenda kwenye mali, ukichepuka Isaka kwenda Keza, unakwenda kwenye *nickel* nyingi sana, tani milioni kwa mamilioni. Bandari ya Uvinza kwenda Msongati hiyo inapita Kasulu hiyo, Shunga - Kasulu, kwenda Burundi - Msongati maana yake ni madini ya *nickel* yaliyopo Burundi na mzigo ulioko Congo ya Mashariki. Isitoshe bila kujenga reli ya kati kwa *standard gauge*, tutaua bandari ya Dar es Salaam, bandari ya Dar es Salaam kwa miaka michache ijayo itakuwa haina mzigo, tutaua bandari ya Mwanza, tutaua bandari ya Kigoma na tutaua bandari ya Kalema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana, Waziri wa Fedha, bila kuja na mkakati mahususi wa reli hii, kwa tafsiri hiyo, tutashawishiana Wabunge wote tukuombe urudi tena mpaka uje na hoja mahususi ya kujenga reli ya kati. Bila reli ya kati hakuna uchumi wa viwanda, bila reli ya kati hakuna nchi kwenda kwenye pato la kati, kwa nini tuendeleo kujiharibia wenyewe, wakati tunaweza tukatenda haya na yakafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie ni maeneo wezeshi kwa maendeleo ya viwanda. Soma kwenye Mpango hapa, tumezungumzia juu ya nishati, reli na barabara. Nimefurahi kusikia kwamba washirika wetu wa Maendeleo wametupatia fedha kwa ajili ya kujenga gridi ya Taifa kutoka Geita sasa kuja Nyakanazi, Kwilingi na Kakonko, Mkoa wa Kigoma. Ningefikiri kupitia

kwa Washirika wetu wa Maendeleo hao hao, tungeendeleza hiyo *grid* sasa, ile *western grid*, ile *corridor* kutoka Kakonko iende Kibondo, Kasulu, Kigoma na Katavi. Hatimaye iweze kuja ku-*link* na Tabora, tuweze kuwa na umeme wa kutosha kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la msingi sana na la kisera na liko kwenye Ilani yetu ni barabara ya Kigoma – Kidahwe - Nyakanazi. Hii barabara ni barabara ya kihistoria, imesemwa kwa miaka zaidi ya 20 sasa na bahati nzuri mkandarasi yuko *site* pale. Yule mkandarasi nimepata habari, alikuwa ananiambia Waziri wa Uchukuzi hapa kwamba wamempa fedha kidogo ili aendelee. Sasa tunaomba barabara hiyo ni barabara ya kimkakati kwa sababu inatuunganisha na mikoa mitano ya nchi hii; inatuunganisha Kigoma - Kagera, Kigoma - Mwanza, Kigoma - Geita, na Kigoma - Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barabara ni muhimu sana. Tunamwomba Waziri wa Fedha, aje na mkakati sasa wa kuimalizia barabara hiyo. Na huyo mkandarasi ambaye yuko *site*, basi tunamwomba aendelee ili barabara hiyo ikamilike. Si hiyo tu, sisi tunaotoka Kigoma, hiyo barabara ndiyo siasa za Kigoma na tunasema barabara ya Nyakanazi kipindi hiki, ndio wakati wake na niseme tu kwamba tutaomba sana barabara hii ijengwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nswanzigwanko ahsante. Nilikuwa nimemwita Mwalimu Riziki Shahari na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae!

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI.** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze nami kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hiki alichotujalia ambacho hatukukipata kwa ujanja wetu, bali matakwa yake. Pia nikishukuru chama changu kwa kuniamini na kunifanya na mimi kuwa miongoni mwa wawakilishi wake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pale ambapo aliishia au *point* ambayo aliisema Mheshimiwa Jesca kuhusu suala la utawala bora, lakini naongeza pale kwamba huu Mpango wote umejiegemeza kwenye hali ya utulivu na amani. Sasa hili ni jambo ambalo tumekuwa tukiliimba sana Watanzania. Wataalam wa masuala ya amani wanatuambia *negative peace* siyo *peace* ya kujivunia. Kwamba kusema nchi haina vita, halafu mkajidai kwamba mna amani, nchi hii haina amani ya kuweza kuhimili mipango kama hii. Hiyo inawezekana imechangia kushindwa kwa hiyo mipango ambayo tulikuwa nayo huko nyuma ambalo si tatizo kuwa na mipango Tanzania bali ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukawa na mipango kama huna utawala bora. Suala la Zanzibar tumelisema humu, nalisema na tutaendelea kulisema, si

sahihi Serikali ya Muungano kukaa kimya wakati inaona hali ya usalama Zanzibar inazidi kudidimia. Tunarushiwa taarifa kila siku, watu sijui wanaitwa mazombi, kule nyuma mnakumbuka kulikuwa na kitu kinaitwa *janjaweed*, wana-*terrorize* watu katika mitaa ya Zanzibar, Serikali ya Muungano imekaa kimya, tunaimba tuna amani, hatuna amani kwenye nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora hauendi, labda mtueleze Serikali Kuu, kwa nini hatuna Meyya Jiji la Dar es Salaam mpaka leo? Kwa nini mnashindwa kuthamini mapenzi na mapendekezo na maamuzi ya wananchi? Hilo ni kwamba nasema mpango wote huu umejiweka mahali sipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala maalum machache ambayo pia ningependa kuyazungumzia. Suala la miundombinu kwa mfano, kumetajwa humu bandari na niliwahi kusema hapa wakati ule wa semina, kwamba tunajivunia vipi sisi bandari zetu au tunazitumia vipi sisi bandari zetu kuonesha kwamba kweli, tunanufaika na eneo letu au kuwepo kwetu kijiografia. Nchi ambayo ina pwani ndefu tu, lakini pia tumezungukwa na majirani wengi ambao ni *land locked countries*. Sasa hii *economic diplomacy* yetu inakwenda wapi ikiwa tunashindwa kutumia fursa hata hizi ambazo tunazo kihistoria. Nchi zinazotuzunguka tuna historia nazo ndefu za mahusiano, lakini tumeshindwa kutumia nafasi yetu hii ya kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu pia wakati mwingine naona kwa mfano, kwenye mwelekeo; kama kunazungumziwa au kunatajwa *variables* mchanganyiko. Kwenye eneo la anga wakasema katika mambo yaliyofanyika ni kujenga uwanja wa ndege wa Mafia. Sasa ule uwanja wa ndege wa Mafia ni kwa ajili ya watu wa Mafia au wale watalii wanaokwenda kule na ni ndege gani hizo hizi za *tropical* sijui za watu 12, 13 hizo. Ndiyo kweli tunaeleza kama ni *success story!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mafia wanaendelea kudhalilika na usafiri, usafiri wa maji ni mbovu kabisa, wala hatujui kwa nini Serikali bado inaendelea kuangalia hali kama ile. Ndege siyo ile inayozungumziwa hapa na kiwanja cha Mafia kile siyo kwa manufaa ya watu wa Mafia. Kwa taarifa yenu tulishaahidiwa uwanja wa Kimataifa wa ndege na wala hatujauona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukusanyaji wa mapato. Ukiangalia sioni jipya, mpaka wanazungumzia sasa kuhakikisha, kuorodhesha ile, kwamba majengo yote, sasa haya mambo mbona ni yale yale tu, hakuna jipya kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *specifically* pia nataka kuzungumzia hili suala la kuondoa utaratibu wa *retention*. Jamani tunataka kuua na hizi Taasisi. Sasa Serikali hii ya Awamu ya Tano ni mabingwa wa kushtukiza, sasa nawaomba

wazee wa kushtukiza, msishtukize kwenye *retention*. Taasisi hizi zilipokuwa zina-*retain some money*, angalau zilikuwa zinajiendesha jamani, OC haiendi kwenye taasisi hizi miezi mitatu, minne mpaka mitano. Sasa mnatarajia ziende vipi hizi Taasisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kuna mwalimu alirudisha watoto wa *boarding* nyumbani, akasema hana chakula, wakamjia juu hapa, ndiyo hali halisi. Hizi taasisi za umma, kikiwemo Chuo cha Diplomasia, mimi nimetoka kule na tulikuwa tuna hali ngumu, OC haziji halafu mnaondoa na *retention*, naomba mkae makini kabisa, msije mkaziua na hizi taasisi, mkazikoshesha uwezo wa kufanya kazi na kutimiza majukumu yao ambayo mmewapa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya. Orodha hii hapa inasema lakini sioni wapi wamezungumza *specifically* kuweka wafanyakazi wenye sifa vile inavyopaswa. Huwezi tu ukazungumzia kwamba nitahakikisha dawa zinapatikana. Hivi mnajua kuna zahanati ambako wale watoa dawa hawana sifa za kutoa dawa na siyo tu kwamba anatoa dawa yeye ndiye anamwona mgonjwa halafu yeye ndiye anasema wewe mgonjwa ukapimwe nini, halafu yeye anainuka anakwenda kumpima mgonjwa na kisha anasoma kile kipimo alichopima mwenyewe, halafu anakuja kuandika dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala si dawa tu, hizi dawa nyingi kwenye zahanati zetu huko kwingine, ni sumu kwa sababu zinatolewa na watu ambao si wenye sifa. Zahanati kadhaa Mafia zinahudumiwa na wahudumu wa afya, sio hata matabibu au wauguji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jamani tuwe makini, kwa sababu huu mpango wenyewe wote unasema pamoja na yote lakini unataka maendeleo ya watu. Maendeleo ya watu gani hayo ambao wale tulioko pembezoni, Mkoa wa Pwani pembezoni, sasa Mafia pembezoni mwa pembezoni. Haitufikii mipango kama hii, haionyeshi kwamba humu kweli yale masuala mahususi yanayotajwa au yanayogusa au yanayoathiri maisha ya wale maskini zaidi au walio pembezoni zaidi yanabebwa katika mipango kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie labda la mwisho, nizungumzie suala ambalo niliacha kulitaja pale kwenye miundombinu, kwamba tunaposoma watu wa Mafia kwamba kinatafutwa kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo, wakati sisi hatuna meli ya kututoa Mafia kutuleta Dar es Salaam, tunaona tunazidi kunyanyasika katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yenu tu niwaambie kwamba kuna gati kule limejengwa la mabilioni na limekamilika toka mwaka 2013 lakini mpaka leo hii wananchi wa Mafia hawana usafiri wa kuaminika wa meli na humu sioni ile *investment* yote ile imetajwa itashughulikiwa vipi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana mwanafunzi wangu mwema wa Chuo cha Diplomasia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwalimu Shahari. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Ruth Molell, wajiandae Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Prosper Mbena, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Ester Bulaya. Mheshimiwa Ruth Mollel, karibu! Yupo? Yes!

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada iliyoko mezani hapo na nimshukuru Mungu kuweza kuwepo mjengoni mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia review ya mwaka 2014/2015, vilevile ya mwaka huu wa sasa ambao tunauzungumzia. Kimsingi, tumekuwa na malengo mengi ambayo hayapimiki na nina maana gani ninaposema hayapimiki? Unakuta kwa mfano, mapitio ya mwaka jana tumesema tuta-*train* walimu 460, lakini hatuambiwi katika ule mwaka ni wangapi wamekuwa *trained*. Kwa hiyo, tunashindwa kujua sasa, hawa waliokuwa *trained* ni wangapi na mmeshindwa wapi kwa wale ambao hatukufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata ukipitia huu Mpango wa sasa hivi ambao Mheshimiwa Waziri ameuleta, bado tatizo liko pale pale, anazungumzia kusomesha vijana wengi kwa mkupuo katika fani mbalimbali, lakini hasemi anafundisha vijana wangapi, wa fani zipi na kwa mchanganuo upi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba katika Mpango utakaoletwa yale malengo yawe bayana, yaweze kupimika kusudi tuweze kuisimamia Serikali kwa jinsi ambavyo inatenda kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mpango umezungumzia suala la viwanda, tunataka Tanzania iwe nchi ya uchumi wa viwanda, lakini suala la rasilimali watu halijajitokeza bayana. Kwa sababu kama ni viwanda tutahitaji fani mbalimbali za kuweza kusukuma hili gurudumu la viwanda, lakini Serikali haijaleta mchanganuo wa fani zipi ambazo tutazihitaji kwa ajili ya huu uchumi wa viwanda.

Kwa hiyo, ni ushauri wangu Serikali ikachambue, ikaangalie kwa miaka kumi ijayo tunahitaji *human capital* gani, katika maeneo gani kusudi kila mwaka mpango wa mwaka unapoletwa hapa muweze kuainisha kwamba, mwaka huu Serikali itafanya hiki, mwaka wa kesho Serikali itafanya hiki, kusudi Bunge liweze kufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mpango huu ambao Mheshimiwa Waziri ameuwasilisha, kwa maoni yangu mimi kama Mbunge wa Chadema,

vipaumbele ni vingi, wala havitatekelezeka. Kwa mfano, katika ukurasa wa 25, Ardhi na Makazi. Tumesema upimaji na utoaji hati miliki, naomba muangalie hivyo vipaumbele vya Ardhi, Nyumba na Makazi; hivi kwa mwaka huu hatuwezi kuvifanya, haviwezi kufanyika wala havipimiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunataka Serikali ije na mchanganuo. Kwa mfano, anasema watapima majiji na vijiji na miji mikubwa. Sasa Serikali ituambie katika majiji, miji na vijiji ni vingapi? Ni mji mmoja, ni miji miwili, ni vijiji kumi kusudi itakapokuja taarifa ya utekelezaji tujue kama kazi hiyo imefanyika au haijafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia kuhusu rasilimali watu. Kama kweli tunataka kupata rasilimali watu ambayo itasaidia, Serikali katika kujenga uchumi huu, basi rasilimali watu hii iangaliwe tangu mwanzo. Waziri wa Elimu aangalie *laboratories* ngapi zinajengwa kwenye mashule, maana ndiko tunakochimbua wataalam ambao baadaye watakuja kusukuma huu uchumi wa kati ambao tunauzungumzia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala la kilimo. Serikali imesema kilimo ni uti wa mgongo, ni kweli, lakini je, Serikali inafanya nini kweli kusimamia kilimo? Kwa sababu lazima tukubali, kilimo nchi hii bado ni *subsistence farming*. Kwa hiyo, wakulima wanatakiwa kuangaliwa kwa jicho la karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali haijazungumzia kuhusu *Extension Officers*. *Extension Officers* wanahitajika wengi na ingependeza kama Serikali ingekuwa kuangalia *ratio* ya *Extension Officer* na wakulima, kama tunavyofanya *ratio* ya madaktari na wagonjwa, nesi na wagonjwa, kwa hiyo na *Extension Officers* ifanywe hivyo hivyo, kusudi muweze kufanikiwa katika kuinua kilimo ambacho pia kinatoa ajira kwa watu wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri kwa Serikali; Wizara ya Kilimo, SUA na Vyu vya Kilimo na mkulima wafanye kazi kwa pamoja (*tripartite*). Watu wa ugani wawezeshwe kwa vifaa, wawezeshwe kwa pikipiki, waweze kwenda kutembelea wakulima na wawe na mafaili kama ya wagonjwa hospitali. Nchi nyingine ndivyo wanavyofanya, unakuta Afisa Ugani anawajua wakulima wake kwa jina na ana *file* analokwenda kuangalia wakulima wake na kujua matatizo yao. Naishauri Serikali ichukue mapendekezo hayo ili iweze kwenda kuyafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la viwanda tunavyo viwanda vingi na vingi vimekufaa. Serikali inahitajika kuangalia viwanda katika maeneo mbalimbali, kwa mfano, Tanga kuna matunda mengi sana, kiwepo kiwanda pale Tanga cha ku-process matunda. Mahali kama Shinyanga kuna nyama

nyingi, ng'ombe wengi sana, kuna pamba nyingi sana, viwepo viwanda vya ku-process vitu hivi ili itoe ajira na kukuza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini juu ya hayo namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukamilisha uchaguzi. Nawashukuru wapiga kura wa Biharamulo na Watanzania kwa ujumla kwa kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nina maneno machache ya utangulizi. Siku moja nilikuwa kwenye benki moja ambayo sitaitaja jina, nikakumbana pale kwenye meza ya huduma kwa wateja na mzee mmoja ambaye alikuwa na malalamiko yanayofanana na ya kwangu. Yeye anasema ameweka kadi kwenye ATM, karatasi ikatoka kwamba pesa zimetoka, lakini pesa hazikutoka, nami nilikuwa na tatizo kama hilo. Alipowaeleza wale wahudumu, wakaja kama watano wanaeleza namna ambavyo mfumo wa *computer* unafanya *transaction* na maelezo mengi ya kitaalam. Yule mzee akawaambia vijana sikilizeni, mimi kama mteja wa benki yenu nina kazi mbili tu, nina kazi ya kuweka pesa na kutoa pesa. Hiyo habari ya mchakato unakwendaje, *transaction system* kazungumzeni huko halafu mje na pesa. Kwa nini nasema hivyo? Watanzania hawa ambao wanalitazama Bunge hili nao wana kazi tatu...

**MBUNGE FULANI:** Hawasikii hao!

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Vyovyote, watafahamu na watasikia, kuna namna watasikia. Wana kazi ya kufanya kazi, wana kazi ya kulipa kodi na wana kazi ya kudai huduma kwenye sekta mbalimbali basi, hawana kazi nyingine. Kazi hizi za kwamba kanuni iko hivi na nini ni muhimu, lakini mwisho wa siku wao wanataka matokeo.

Leo Mheshimiwa Zitto Kabwe, sijui kama yupo, huwa namheshimu sana, lakini leo amenishangaza. Amefanya...

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge alikuwa akimwingilia Mzungumzaji)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Sikiliza wewe, ni zamu yangu kuongea. Sikiliza, tulia, usinipotezee muda. Tunatambua kwamba...

*(Hapa kuna Mbunge alikuwa akimwambia mchangiaji aketi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Nikae, anasemaje?

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge alikuwa akimwingilia Mzungumzaji)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Wewe tulia, mimi ni mhuni zaidi yako, tulia.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, samahani. Tunapongea ndani ya Bunge Tukufu, kwanza kabisa naomba u-address kiti, hilo ni la kwanza, lakini naomba tuheshimu na tutumie lugha za Kibunge. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge alikuwa akimwingilia mzungumzaji)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Tulia wewee! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana rafiki yangu Zitto ni Mbunge makini. Nakwambia wewe Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Zitto, ni Mbunge makini na ninyi mnafahamu; lakini leo na siku chache zilizopita nimeshangaa kidogo na namwomba asiendeleo kunishangaza.

**MBUNGE FULANI:** Upo kwenye Mpango hapo.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Kwamba Ijumaa Bunge lilipoahirishwa nimefanya hesabu ya haraka haraka, nakubaliana kabisa kwamba kazi ya wapinzani ni kuisimamia Serikali na hawakuja hapa kuishangilia, hilo linafahamika kabisa. Hata hivyo, kazi hiyo lazima ifanyike kwa namna ambayo ina maslahi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ijumaa lilipoahirishwa Bunge, kwa hesabu ya haraka haraka, kwa kutofanya kazi kuanzia saa tano ile mpaka muda uliopaswa kufanywa zimepotea kama milioni thelathini na tatu. Zimepotea kwa sababu mmoja wa Wabunge alitaka kuonesha namna anavyoweza kusoma Kanuni. Ungeweza kuonesha unavyosoma Kanuni, lakini ukawaacha Watanzania salama kwa kutotumia hela yao vibaya. Watanzania wanatarajia matokeo, lakini Wabunge wenzangu wa CCM na mimi nakuja kwenu. Tuna kazi ya kuisimamia Serikali, nje ya Bunge kwenye vikao vyetu na tuna kazi ya kuisimamia Serikali hapa ndani. Kilichotokea Ijumaa na yaliyotaka kutokea leo ni dalili kwamba kazi yetu Wabunge wa CCM hatujaifanya kwa kikamilifu. Huo ndio utangulizi kwa Wabunge wa CCM na Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Watanzania wanatarajia matokeo, hawali Kanuni, hawali Sheria. Nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuchangia Mpango wa Maendeleo, napenda kuwa na kipaumbele kimoja ambacho ni mtambuka. Kipengele ambacho ni mtambuka, kwangu ni namna gani jitihada zetu za kukuza uchumi zinaendana na maendeleo ya uchumi. Ni namna gani chochote tulichokiandika kwenye mipango hii kinakwenda kugusa maisha ya mwananchi wa kawaida. Tukijenga reli, tukazungumzia barabara, tukazungumza yote hayo, kama hayagusi maisha ya mwananchi wa kawaida, Watanzania hawatuelewa, tutakuwa tunaimba wimbo wa kila siku ambao hauna tija kwao, wakati wao kazi yao ni kuona maisha yao yanabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano, ukurasa wa 27 wa hiki kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo unazungumzia namna ya kufunganisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Wanaonesha dalili hizo kwamba wanataka kusema hivyo, lakini ukienda kwenye maandishi kwa ndani, kwenye maudhui yenyewe, maeneo mengi huoni namna ambavyo Mpango huu unakwenda kugusa maisha ya mtu wa chini kabisa, nitatoa mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, tumezungumza barabara, lakini utaona hapa tunazungumza barabara kubwa tu; za Mikoa, barabara za Wilaya, lakini ndugu zangu nikumbushe kitu kimoja. Barabara kubwa ya lami ina maana, lakini kama kule kijijini anakoishi mwanandhi, ndani Kijiji cha Kalenge, Kijiji cha Kitwazi hakufikiki hata kwa baiskeli, hata kwa pikipiki, maana ya barabara kubwa inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetarajia tuone namna gani sasa tunaweza kuweka mipango ya kushuka chini. Wakati tunajenga barabara kuu zinazotuunganisha na mikoa umefika wakati sasa hata barabara zile zinazotoka (*feeder roads*) zinazokuja kukutana na barabara hizo ionekane wazi kabisa kwenye mpango kwamba sasa mwelekeo wetu ni kwenda kugusa mawasiliano ya barabara kwa mwananchi aliye kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu, ukiangalia kwenye elimu hapa kwenye utekelezaji na kwenye vipaumbele, utaona tunaongelea maabara, madarasa, lakini mwalimu tunasahau kwamba ndiye mfanyakazi wa umma wa nchi hii ambaye anafahamika anapofanya kazi, lakini hafahamiki anaishi wapi. Hatuzungumzii nyumba za walimu, hatuweki mkakati nyumba za walimu miaka nenda rudi, tunazungumza mambo ya maabara. Ni mazuri, lakini ukipita kwa mwalimu utakuwa umegusa mengine yote kwa upana na kwa namna ya kwenda kubadilisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara, nimeshangaa sana kwamba pamoja na kwamba nimezungumzia habari ya *feeder roads*, nashangaa sana kuona kwamba siioni barabara ya kutoka Bwanga kwenda Kalebezo, barabara

inayounganisha Mkoa wa Geita na Mkoa wa Kagera na nchi jirani ya Rwanda; barabara ambayo inakwenda kwenye Wilaya mama ya Rais anayeongoza nchi hii. Alikuwa mgombea wa Ubunge mara mbili pale Biharamulo, lakini Mikoa hii ya Geita na Kagera kama haitaunganishwa na nchi jirani kwa kiwango kinachostahili tunaua biashara pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, unaona pale kwenye utekelezaji wanaongelea tu hospitali za rufaa, ni vizuri kabisa. Hata hivyo, hospitali za rufaa bila kuweka nguvu kwenye zahanati na vituo vya afya hatutagusa maisha ya watu. Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili ya Dar es Salaam au ya Bugando ni muhimu iwepo lakini haina maana kama mtu hawezi hata kupata mahali pa kupata huduma ya kwanza ili aambiwe nenda rufaa. Ni lazima mpango huu ujikite kwenye zahanati na vituo vya afya kwamba sasa tunakwenda kuwagusa ili wakishindwa kutibiwa pale ndipo waende kwenye hospitali kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wangu ni kwamba, mipango yote tunayoiweka tuwe na kipaumbele mtambuka ambacho kinasema chochote tunachokifanya lazima kionekane wazi kwamba kinakwenda kugusa maisha ya mtu wa chini, vinginevyo maana yake inapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nawaombea kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wa CCM tuisimamie Serikali, lakini na Wabunge wa Upinzani tuibane Serikali kwa namna ambayo inaleta tija kwa wananchi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mukasa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Prosper Mbena na Mheshimiwa Mwita Waitara ujiandae!

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliompongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake yote ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa uwasilishaji mzuri wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijachangia, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo langu la Morogoro Kusini kwa imani kubwa waliyonionesha kwangu na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kura nyingi sana, nawashukuru sana. Ninachoomba tushirikiane kwa pamoja tuondoe umaskini ambao kwa kweli uko mwingi sana katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yaliyoletwa mbele yetu na Waziri wa Fedha ni mazuri na kwa kweli tunahitaji tumsaidie kuboresha ili aje na Mpango utakaokuwa mzuri zaidi kwa nia ya kuondoa umaskini katika nchi yetu. Kwa sababu hiyo, yangu zaidi ni ushauri katika maeneo machache ambayo nimeona yakiboreshwa pengine tutakuja na Mpango mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni eneo zima na falsafa nzima ya uchumi wa viwanda. Napata picha kwamba mapendekezo haya yameogopa kuja na mpango mkubwa zaidi ya mapendekezo haya yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza kuwa na uchumi wa viwanda nilitegemea nione mapendekezo mazito zaidi ya viwanda vitakavyotukwamua ili uchumi huu sasa kweli uitwe uchumi wa viwanda, lakini humu ndani sikuona sana. Nimeona viwanda vinavyozungumzwa ni vile vilivyobinafsishwa, vichache ambavyo havionekani moja kwa moja kama kweli tumedhamiri sasa kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Pia nimeona hata teknolojia inayozungumzwa humu inazungumzwa teknolojia nafuu na ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tukitaka tujifananishe na wanyonge wenzetu wale, tutabakia hapa hapa. Yupo Mheshimiwa Mbunge mmoja ameeleza kwamba kuna wakati tulifanana na nchi kama za Malaysia, leo hii wenzetu wametuacha sana, wao sasa wanakuwa wafadhili. Ni lazima tutoke hapa tulipo na sisi tuzungumze kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nashauri, kwa nini kwa mfano Serikali isichukue *model* kama ya China. China ya sasa hivi walifanya uwekezaji mkubwa sana miaka ya 1990. Wali-*phase out* viwanda vyao vile vilivyokuwepo wakati ule. Viwanda vyao vingi havikuwa na *efficiency* kubwa katika uzalishaji, wakavi-*phase out*. Wakachukua *technology* kutoka nchi za Magharibi na wakaingia kila sekta wakafanya uwekezaji mkubwa sana. Hivyo ndivyo viwanda vinavyozalisha sasa hivi ambavyo vinaifanya China iwe hii tunayoijua leo. Nashauri na sisi tufanye hivyo, tusiogope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye maamuzi ya uhakika kabisa ya makusudi, yatakayotuwezesha tutoke hapa. Tutafute teknolojia, tutafute mashine ili tuwe na viwanda ambavyo ni vya kisasa, tuwekeze humo. *Returns* zitakuja baada ya miaka 10, 20, lakini tukienda kiunyongeunyonge kama tunavyoonekana kwenye mapendekezo haya, tutaendelea ndugu zangu kuwa bado tuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie upande wa miundombinu iliyoelezwa. Miundombinu ni muhimu sana katika nia nzima ya kutaka kutoka kwenye umaskini lakini pia kujenga uchumi wa viwanda. Kama walivyosema wenzangu, miundombinu ya barabara, mathalani bado hajijagusa sehemu

nyingi ya kuwatoa hawa maskini ambao ndio tunawazungumzia sasa hivi. Kwenye Jimbo langu ni tatizo kubwa sana pamoja na kwamba ni *potential areas* za kuleta uzalishaji sana hasa kwenye mambo ya kilimo. Yapo maeneo ya Kongwa yanalima sana, Waheshimiwa Wabunge wengi mna mashamba yenu kule, lakini njia mbaya sana, barabara hakuna, hizi ni sehemu za uzalishaji, unaziachaje bila miundombinu ya namna hiyo, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia viwanda vitakavyokwenda kwenye eneo kama hilo la kilimo kutumia malighafi ya mazao kuweza kusindika na kuondoa tatizo la ajira kwa vijana wetu wengi. Hivyo, nashauri, barabara hizi ziende kwenye sehemu za vijiji, walipo watu, kwenye sehemu za uzalishaji, huko ndiko tuweke misisitizo. Nazungumzia maeneo ya kwangu kule, kama Kisaki, Mvaha na Uponda, hizo ni sehemu ambazo ni *potential* lakini hazina barabara pia na Bwira Juu, Bwira Chini, kote huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuzungumzie suala la umeme. Umeme wamejitahidi sana, lazima tuwapongeze. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Muhongo, lakini tunayo maporomoko madogo madogo. Kwangu kule yapo maporomoko ya maji ya Mlulu katika Mto wa Kibana, Kijiji cha Lugeni. Ni *potential* kutoa *megawatt* nadhani moja, ambayo ni *lilowatts* 1000. Tukiweza kujenga uwezo wetu kwa vijiji vya namna hiyo vyenye maporomoko, tukawekeza kule, tutawasaidia sana hata wakazi wa kule, hata watu wa vijijini kule. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali iangalie miradi kama hiyo pia iipe umuhimu mkubwa kuliko kuendelea kutegemea umeme ghali ambao tunatumia kwa ajili ya hawa wanaotumia mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie pia tatizo kubwa la ng'ombe. Ng'ombe tunawahitaji na viwanda tunavihitaji, lakini niishauri Serikali, moja ya njia ya kuondoa tatizo hili la migogoro ya wafugaji na wakulima kwa sasa hivi ni kuwekeza katika viwanda, hata kama vidogovidogo, kwenye maeneo hayo yenye matatizo ili wafugaji wasikae sana na ng'ombe zao na kukosa malisho. Nitafurahi sana kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo utakapofika wakati wake akaja kutueleza mkakati ambao unatekelezeka wa kuondoa tatizo hilo *once and for all*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie suala la viwanda vidogo vidogo, kwa sababu uchumi wa viwanda, nazungumzia uchumi wa viwanda kwa nia ya kuondoa umaskini kote. Tunahitaji kuwa na viwanda vidogo vidogo kwa kila Jimbo. Hii itasaidia ku-*address* tatizo la ajira kwenye Majimbo yetu na kwangu kule tayari nimeshatenga maeneo manne kwa ajili ya kuanzisha viwanda hivyo. Nitashukuru sana kumsikia Waziri wa Viwanda, muda utakapofika, atatusaidiaje kushawishi na kuweka viwanda vidogo vidogo katika maeneo ya kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbeni. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Mwitwa Waitara. Mheshimiwa Waitara, karibu! Mheshimiwa Bulaya jiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba nimshukuru sana Mungu, ameniwezesha kupitia wananchi wa Jimbo la Ukonga kuingia kwenye jengo hili na naomba nitoe mchango wangu. Naomba Waheshimiwa Mawaziri wanisikilize vizuri kwa sababu Wabunge hawa wa CCM hawatawasaidia sana kwenye utendaji wa kazi, kwa hiyo, ni muhimu sana. Wanasifia yote, halafu wanalalamika mwanzo mwisho, kwa hiyo mimi utaratibu huo siupendi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kaulimbiu ya Serikali hii ni Hapa Kazi Tu maana yake inaonesha hawa watu walikuwa wazembe muda wote tangu mwaka 1961. Wazembe tu ndio maana nasema wamezinduka sasa, eti hapa kazi. Kwa hiyo, mnapokuwa mnapendekeza kauli hizi ni muhimu mkachunguza kama zina mwitikio chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali inatumbua majipu, maana yake kuna wagonjwa wengi na ugonjwa huu umesababishwa na wenyewe CCM. Halafu Serikali ya CCM waoga sana. Ndio maana kuna polisi huku, wamezunguka jengo la Bunge, wanajaza askari humu ndani watu waogope kutoa hoja, maana yake ni waoga kweli kweli. Wangekuwa sio waoga wangetulia tushughulikiane kwa hoja na kwa vyovyote itakavyokuwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine waongo, Serikali hii inawaambia watu utawala bora, tena utawala wa kisheria, lakini ukiangalia kauli hii na yote yametajwa kwenye mapendekezo, mmetaja, nilikuwa nasoma hapa.

**MBUNGE FULANI:** Nenda kwenye hoja.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mmesema utawala bora, mimi naenda kwenye hoja. Hamjasoma vizuri, utawala bora. Naamini kikwazo cha maendeleo ya Tanzania ni CCM wenyewe.

Kwa hiyo, tukipanga mipango tukajadiliana, siku CCM ikitoka madarakani, nchi hii itapata maendeleo makubwa sana. Kwa hiyo, nawaambia Watanzania wajipange kuiondoa CCM madarakani ili wapate maendeleo kwa sababu shida ni CCM, mipango hakuna shida, rasilimali zipo, wataalam wapo, ardhi ipo, kila kitu kipo, shida ni hao wenyewe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yangu mawili ya msingi. Moja ni elimu. Nashangaa sana Waziri, kaka yangu Simbachawene wakati anachangia, akawa anakataa tuiseme elimu ya bure haipo. Jambo la kawaida kabisa, kwamba unalipa ada ya shilingi 20,000/= kwa shule za kutwa na shilingi 70,000/= shule za *boarding*, gharama zingine wazazi wanaingia halafu unasema eti elimu hii ni ya bure, lugha ya kawaida ya Kiswahili tu. Wekeni lugha hii ili msiwachanganye wananchi, elimu ni ya kuchangia, Watanzania wajue na wajue majukumu yao, wafanye kazi ya kusomesha watoto wao, kwamba Serikali ilichofanya imepunguza gharama, *very simple* ili watu waelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mnapowaambia watu elimu ni bure, akienda pale anadaiwa mahindi, apeleke maharage, halafu michango mbalimbali, wanaambiwa walipie mlinzi, semeni ili jambo lieleweke vizuri, kwani siyo dhambi. Hapa hakuna elimu ya bure, ni elimu ya kuchangia na Watanzania wajue. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sana hili jambo likawekwa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hizi shule, kwa mfano, nina madai hapa ya waraka uliotolewa ili wale walimu, wanasema Waraka kwa Watumishi wa Serikali Namba 3 wa mwaka 2014 kuhusu mishahara na posho ya madaraka kwa viongozi wa elimu. Hawa ni wakuu wa shule za sekondari na msingi na vyuo. Maana yake mpaka leo hawa watu wanadai, wametengewa tu shilingi 250,000/-, kwa hiyo maana yake hawa hawawezi kuwa na moyo wa kuendeleza elimu vizuri kama wenyewe wana madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Mkuu wa Chuo analalamika, Mwalimu Mkuu analalamika, na wazazi wanalalamika, wanafunzi wanalalamika, kwa hiyo mkitaka mambo yaende sawa, nilimsikia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amesema, yeye hataenda kwenye mpango wa tatu wa *REA*, mpaka makandokando ya mpango wa kwanza...

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii kauli ikifanyika itasaidia sana. Miradi yote ambayo Wabunge wanataja hapa, barabara ambazo zilipangwa, kama ile ya kutoka Kitunda kwenda Msongora, tangu wakati Mheshimiwa Magufuli akiwa Waziri awamu ya kwanza, awamu ya pili mpaka leo Rais, ni wimbo. Mvua ikinyesha watu hawawezi kwenda mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hivyo katika miradi mbalimbali ya maji kule Chanika, Msongora, Kidole, Mgeule, ikakamilika, maana yake watu wale ukizungumza habari ya maendeleo na uchumi wa kati watakuelewa. Kwa hiyo, mambo haya ni muhimu sana mkayakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya msingi sana ambayo mambo haya hamjayafanyia kazi na nimwombe Mheshimiwa Waziri anisaidie. Kwa mfano, kwenye upande wa elimu, Mawaziri, kila mtu anaibuka na jambo lake katika nchi hii. Tuliwahi kuwa na Mungai akaja hapa na *unified science*, mimi bahati nzuri ni mwalimu wa hesabu na kemia, akachanganya masomo watoto wakaogopa sana masomo ya sayansi, kwa hiyo watu wakarudi nyuma sana, Waziri akawa na mamlaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda hapa, akawepo Kawambwa, akaibuka na GPA na nampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako amefuta ile, namuunga mkono, turudi kwenye *division*. Kwenye Sheria za Baraza la Mitihani, kifungu namba 20, kinasema, *The Minister may give the Council directions of a general or specific character and the Council shall give effect to every direction*. Kumbe hiki kifungu ndiyo kifungu ambacho Waziri anaibuka asubuhi, anaenda anatoa maelekezo Baraza la Mitihani, wanaambiwa sasa hivi ni GPA, ni *Division*, hiki kifungu kiondolewe. Hata kama Waziri ana mamlaka ashauriane na wataalam wenzake, ili mambo haya yasiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake mnawayumbisha Watanzania, watoto hawa mnawayumbisha, mara *division*, yaani mnachofanya nyie ni kwamba kuna golikipa yupo mlangoni pale, anachofanya ameshindwa kiutaalam, kimpira, anaamua aongeze tu ukubwa wa goli, ili ionekane kwamba wamefunga. Hiyo maana yake ni *failure*, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wa elimu hapa, hatuna vile vitu vya kitaalam kwa mfano *Teachers' Profession Board*, haipo, *Quality Assurance Board*, haipo. Kama ambavyo kuna Wanasheria wana Chama cha Wanasheria, Walimu wana chama ambacho kinaelekea kuwa chama cha kisiasa siku hizi. Sasa hawa watu lazima wawezeshwe ili waweze kusimamia, lakini ni muhimu sana mkaangalia mambo ya maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unaleta mpango wa kipato cha kati unazungumza habari ya viwanda, halafu shuleni hata matundu ya choo hamna, hivi kweli hayo ni maendeleo? Yaani uzungumze upate mainjina wakaendeshe viwanda, matundu ya choo tu ni shida. Yaani madawati ni shida, mnazungumza vitu vikubwa, vidogo tu vimeshindikana hapa. Wewe unazungumza habari hii wakati hata choo hakipo shuleni. Sasa hivi watoto wameandikishwa katika shule hizi, kuna shule ina watoto 617, ina madarasa mawili ya darasa la kwanza. Sasa huu uchumi wa kati nataka nione miujiza, hapa kazi tu na jipu, tuone mambo yatakavyokuwa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho, utawala bora. Zamani niliwahi kumuunga mkono Mheshimiwa Nape, wakati nilipokuwa kule chama cha

zamani, lakini nikagundua Mheshimiwa Nchimbi aliwahi kufuta kanuni ili Nape asigombe Uenyekiti, naona alikuwa sahihi.

Huyu jamaa amekuja hapa, anaondoa hoja, unawaambia watu utawala bora, wana haki ya kupata taarifa kwa mujibu wa Ibara ya 18, Waziri anakaa chumbani, tumelalamika jana yake, kesho yake amekuja hapa akatuambia kuna utafiti wa Uingereza, yaani unawezaje Waziri kujifunza kuzuia taarifa, usijifunze demokrasia ya Uingereza, miundombinu na vitu vingine vikubwa, wewe ukajifunza kuzuia taarifa tu. Unatuambia, kuna utawala bora hapa? Yaani, unazuia Watanzania wasijue tunazungumza kitu gani humu kwenye hili Bunge. Halafu Waziri Mkuu na Mawaziri, wengine ni wataalam na wasomi, wanaunga mkono na kupiga makofi. Ndiyo maana nikawaambia Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge wa CCM hawawezi kuwasaidia sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo kwa kweli ni muhimu mkayatafakari upya. Haiwezekani mkazuia taarifa ya kile kinachoendelea, unatuambia suala la muda wa kazi, sasa, hivi asubuhi na jioni, upi ni muda wa kazi mzuri? Kwa hiyo, asubuhi mnaonesha, jioni mnazima. Yaani jioni saa tisa na nusu, ndiyo muda sasa umekwisha, halafu asubuhi mnaonesha. Unarekodi masaa saba, halafu mna-*edit* mnatoa kwa saa moja, mnatoa mnayotaka wenyewe muone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar itakuwa hoja yangu ya mwisho. Mimi najua na CCM wanajua kwamba Zanzibar uchaguzi ulikwenda vizuri na Maadlim Seif alishinda. Huo ndio ukweli, hata kama hamtaki. Dunia inajua, Afrika inajua, Tanzania inajua, CCM mnajua na Taifa hili mnajua na Mwenyekiti unajua. Uchaguzi wa Zanzibar ulikwisha. Kwa hiyo, mnachofanya ni magumashi na sisi kama watoto wa Tanzania hii hatuwezi kuunga mkono mambo haya. Nchi hii ni ya demokrasia kila mtu ana haki ya kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukienda kwenye uchaguzi watu wakapiga kura, hakuna malalamiko, aliyeshinda apewe haki yake, ndiyo mpango mzuri wa maendeleo utakavyokwenda. Twende kwa amani kwa kuheshimiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, sijaunga mkono hoja mpaka kwanza Mpango wa Maendeleo uje, ndio nitaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru baba zangu, mama zangu wa Jimbo la Bunda Mjini kwa unyenyekevu mkubwa, bila kujali umri wangu, bila kujali jinsia yangu, mkasema ng'wana Bulaya ndiye chaguo sahihi la Jimbo la Bunda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindi wangu umetoa fundisho kwa wale wote wenye kiburi cha kukaa madarakani muda mrefu. Pia ushindi wangu umetoa fundisho, wananchi wataangalia *product* bora inayopelekwa na chama husika na si ukubwa wa chama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitoe pongezi kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Wale ma-*senior* kama mimi asilimia 30 tuliorudi, mnajua kwamba *issue* si Mipango, *issue* ni utekelezaji wa Mipango. *Issue* si Serikali ya awamu hii, ni utekelezaji wa Serikali husika. *Issue* si Ilani ya 2015, ni utekelezaji wa Ilani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia tena mapinduzi ya viwanda. *This time don't talk too much*, fanyeni kazi. Rais wa Awamu ya Nne alipokuwa akizindua Bunge, alisema mapinduzi ya viwanda, kwenye Ilani ya mwaka 2010 ukurasa 171, imezungumzia mapinduzi ya viwanda. Hatuhitaji tena mzungumzie, tunahitaji mtende. Tunataka mtende! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kwetu sisi tu, Taifa hili linatuangalia, tutembe kwenye maneno yetu. Wenzetu wanachukua Mipango yetu wanaenda ku-*implement* kwenye nchi zao. *Please*, wapeni Watanzania wanachokitara. Tuache kusema, tutende. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wote waliozungumzia reli ya kati na naungana na hoja ya kuhakikisha tuna viwanda, tuvifufue vya zamani, tuwe navyo. Ni jambo la msingi sana, lakini leo hii tunazungumzia mapinduzi ya viwanda. Tumemaliza ujenzi wa VETA kila Wilaya? Mambo haya yanakwenda sambamba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ma-*graduate* wenye *masters*, wenye *degree* wale ni ma-*supervisor*. Tunahitaji kuandaa *product* nyingine ya *certificate*, ya diploma tuipeleke kwenye viwanda. Tunatakiwa tuwe na VETA, VETA na mapinduzi ya viwanda yanaenda sambamba. China ilifanikiwa kwa mtindo huo. *Please* tuwe na VETA, tuwe na viwanda, tunatoa watu huku kwenye VETA tunaingiza viwandani tunatatua tatizo la ajira kwa vijana. Tupange kwa makini, tutekeleze kwa makini kwa maslahi ya vijana wa sasa na wajao, *please* mkaangalie tena. Tusiseme tu VETA kwenye kila Wilaya ziko wapi tumezungumza miaka mitano iliyopita, *this time* mara ya mwisho tuongeele mapinduzi ya viwanda Watanzania waone viwanda si maneno, *do not talk too much*, tendeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakapoamua kwenda kuwekeza kwenye viwanda, kuna mmoja alisema angalieni na jioografia, sisi kwetu kule Kanda ya Ziwa hatuhitaji katani kule ni pamba, ng'ombe na uvuvi. Hiyo niliyosema ya

VETA mwenye *degree* ataenda kusimamia samaki wanasindikwa vizuri yeye hataenda kusindika. Mwenye *degree*, mwenye *masters* hataenda kutengeneza viatu atasimamia viatu vimetengenezwa vizuri, ni ushauri chukueni ufanyieni kazi. Hamtaimba tena 2020 hapa, fanyeni kazi siyo maneno, *it is not about slogan* ni utendaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlikuwa hapa na Maisha bora kwa Kila Mtanzania yako wapi? Leo hapa kazi iko wapi? Siyo maneno ni vitendo. Siyo tu wingi kwa kuandika kwenye Ilani mmeziandika sana tendeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumezungumzia kuhusiana na Shirika letu la Ndege jamani kuwa na Shirika la Ndege ni ufahari tukiwa kwenye nchi za wenzetu. Tunapishana tu na ndege za Kenya, Rwanda, sisi tunasema tu tutafufua, tutafufua lini? Nchi ndogo kama Malawi wana ndege. Baba wa Taifa aliacha ndege tunahitaji ndege. Mnaenda Dubai mnapishana na ndege za Kenya, Rwanda na kadhalika tunahitaji ndege. Kuwa na ndege jamani unachangia pia kwenye sekta ya utalii, watu mnaosafiri mnajua. Ukishuka pale Kenya wazungu wote wanaishia Kenya halafu wanakuja Kilimanjaro, tungekuwa na ndege wangeshukia Dar es Salaam fedha zile wanazoziacha Kenya wangukuja kuacha kwenye nchi yetu lakini ndege moja, sijui mtumba kila siku tunazungumzia ndege, ndege ziko wapi? Kwa nia njema tutende ili tulitendee haki Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapozungumzia sekta ya utalii watu wanajua utalii ni tembo tu, siyo tembo, wenzetu kule wametengeneza visiwa, sisi *mashallah* Mungu ametupa hatuhitaji kuvitengeneza, tunavitumia kwa aina gani vile visiwa? Tunaboresha maeneo yetu mengine ya utalii, tuna Mbuga pale ya Saa Nane, ukienda kule unaona Mwanza nzima jinsi ilivyo nzuri lakini cha kushangaa hata hoteli kule hatuna. Tungetengeneza huu Ukanda wa Kaskazini na Kanda ya Ziwa ungekuwa sekta ya utalii. Mtu anatoka Ngorongoro, anaenda Serengeti, anaenda Saa Nane anaenda kwenye visiwa vyetu ambavyo Mungu ametujalia. Wenzetu nchi nyingine wanatengeneza visiwa na maeneo ya utalii lakini sisi tunayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ashakum si matusi wengine wanasema visiwa vyetu wanaenda kujificha wake za watu na wanaume za watu. Visiwa vyetu tunatakiwa tuvitumie kwenye utalii ndugu zangu. Tunayaongea haya kwa uchungu mkubwa, Mungu ametupa mali hatuzitumii. Haya ni mambo ya msingi tumeyasema na Mwenyekiti wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Utalii. Watu wanakuja wanayalalamikia haya, mambo kama hayo lazima tuyaweke katika mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie deni la Taifa, nakubaliana kabisa hakuna nchi isiyokopa. Kukopa ni jambo lingine, kwenda kuwekeza katika kile

ambacho wamekikopea pia ni jambo lingine. Leo hii tunadaiwa *US Dollar* milioni 19. Nimesema kukopa siyo shida, je, tunazitumiaje hizo fedha tunazokopa? Tunakopa tunaenda kuwekeza kwenye eneo gani? Fedha zetu za ndani tunaweza kuwekeza katika maeneo ya huduma za kijamii hizi fedha tunazokopa twende ku-*invest* katika maeneo ambayo yatazalisha na tutaweza kulipa deni kwa mujibu wa mikataba tuliyoingia na kuondokana na mlundikano wa riba kama ambavyo upo humu kwenye ripoti. Hilo ni jambo la msingi sana. Tatizo hata katika hii Mifuko yetu ya Hifadhi ya humu ndani ambayo tunaikopa na hatulipi, tunaenda kuwekeza sehemu ambazo hatuzalishi. Hilo ni jambo la msingi ukikopa nenda kawekeze eneo ambalo litakuwezesha kulipa deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtende, msiendelee kuongea, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nichukue nafasi hii kwanza kutamka rasmi naunga mkono mapendekezo ya Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchangiaji wangu utajikita katika suala zima la viwanda, lakini pia nitazungumzia masuala ya Zanzibar kama wengine walivyozungumza japo tunaandaa Mpango Kazi. Napenda utambue kwamba kitambulisho changu cha Uanzibar ni Na.010242768 ambacho ni halali na kitambulisho changu cha Tanzania ni Na.196650102-12114-0001-17. Nimeona nijitambulisho nafasi hiyo ya Uanzibari kwa sababu kuna watu Zanzibar wanaijua kwa ramani lakini wanaisema kama vile wanakaa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zanzibar tuliiachia Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar ambayo imetoa maelekezo na mpambano ni tarehe 20 Machi, 2016. Huwezi ukakaa unasema wewe unaendeleza demokrasia, unaijua na unataka haki itendeke wakati unawaaambia wananchi wako wasiende kupiga kura. Demokrasia ya kweli inachagua viongozi wanaowataka wao siyo kwa kiongozi mmoja kutamka watu wangu msipige kura, hiyo demokrasia ya wapi? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia Zanzibar ni shwari na salama atakaye aje. Zanzibar ingekuwa siyo shwari Wabunge tusingekuwa hapa. Wabunge wote tungekuwa tumeshaenda Zanzibar kwa ajili ya hekaheka ya Zanzibar lakini Wabunge kutoka Zanzibar tuko hapa hii inaashiria jinsi gani Zanzibar iko shwari. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa)*

*wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kukumbusha, humu ndani hakuna Amiri Jeshi Mkuu anayeweza kutangaza hali ya hatari. Nakumbuka tarehe 29 Oktoba, 1978, Nduli Iddi Amini alivyoingia Tanzania, Amiri Jeshi Mkuu ndiye alitangaza kwamba tuna hali ya hatari nchi yetu iko kwenye vita. Sasa humu ndani ni nani aliyekuwa Amiri Jeshi Mkuu anayetangaza Zanzibar si shwari? *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa siku zijazo, kwa kuwa Wabunge tunatoka kwenye kampeni tukija hapa labda kidogo akili zina-change itabidi tupimwe kwanza akili ndiyo tuingie Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu mpaka sasa hivi wanaongea wanafikiri wako kwenye kampeni, wamesahau kwamba kampeni zimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Mpango na kama nilivyosema nauunga mkono. Tunavyo viwanda ambavyo vinahitaji kufufuliwa, naomba viwanda vile vifufuliwe vikiwepo vya korosho na vya nguo. Sambamba na hilo naunga mkono pia utaratibu wa kujenga viwanda vipya, naomba vijengwe katika maeneo husika ambapo malighafi inapatikana. Isije ikawa kama tulivyofanya Kiwanda cha Almasi kinajengwa Iringa wakati almasi haipatikani Iringa. Naomba tuangalie kipaumbele cha namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo naomba vijana wetu wawezeshwe katika kupata elimu ya utaalumu huo ili tusije tukajaza wataalamu kutoka nje na vijana wetu wakakosa ajira. Katika ajira hizo, naomba vijana waangaliwe zaidi siyo kwamba hatutaki uzoefu wa wazee, tunaomba ule uzoefu uende pamoja na uzoefu muda ukifika wastaafu ili vijana wapate nafasi. Kumekuwa na tabia baadhi ya wazee ambao wako kwenye nafasi wanapoanzisha mradi wanaanza kubadilisha majina, anakuwa *Project Manager* inapokuja kuanza kazi wanatengeneza CV zinazolingana na wao walivyo ili vijana wasipate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba hali hii ibadilike vijana wapewe ajira na *experience* wataipata wakiwa kazini, wanayo nafasi ya kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba wafanyakazi walipwe mishahara mizuri ili kuondoa migogoro kwenye viwanda hivyo. Kwa sababu kama kutakuwa na migogoro viwanda vitafungwa vitashindwa kuzalishwa na majipu yatazidi kuonekana. Katika hili nikukumbushe majipu mengi makubwa huwa yanatoa na alama ya sehemu gani ukamue ili kiini kiweze kutoka. Upande wa pili unaong'ang'ania CCM tuna majipu kule kuna matambazi, yale majipu makubwa ambayo hayaoneshi mdomo uko wapi? Mimi nikuhakikishie majipu ya namna ile lazima yatumbuliwe na mikasi. Majipu makubwa makubwa kama yale ambayo yanaitwa matambazi mengi yako upande wa pili japo hawataki kuyasema. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napenda kuongelea kuhusu sekta binafsi. Naomba sekta binafsi zipewe ushirikiano wa kutosha kwa kuondoa urasimu na ukiritimba ili waweze kufanyiwa maamuzi ya haraka ili vijana wetu wapate ajira na tupate maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, naomba niseme naunga mkono wale wote waliochangia kuhusu kuboresha miundombinu ya umeme, bandari, barabara, maji, reli na mawasiliano ili tuweze kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nasisitiza, Zanzibar ni shwari atakaye na aje. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwepo jioni hii kuchangia mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wanaliwale kwa kuniamini na niko tayari kuwatumikia. Vilevile napenda kuwapongeza wapiga kura Wanaliwale kwa kuiweka CCM kuwa Chama cha Upinzani Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wangu nitaulekeza katika maeneo yafuatayo. Kwanza kabisa, msingi wa Mpango. Msingi wa Mpango tumeambiwa ni amani, utulivu lakini nataka nitoe angalizo hapa ni lazima tutofautishe uvumilivu wa watu wachache na amani. Nataka nitumie neno ukondoo, ukondoo wa Wazanzibar tusiuchukulie kama ni kigezo cha amani. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba ukondoo huu tusitegemee kwamba utakuwa ni wa kudumu. Kama tunakusudia huu Mpango utuletee matunda tunayokusudia ni lazima tuhakikishe kweli tunapambana kuhusu suala la amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu tumeambiwa kuna kuimarisha elimu, mimi nitajielekeza kwa upande wa elimu. Hatuwezi kuimarisha elimu tukiwasahau walimu. Walimu wetu maisha yao ni duni sana. Hapa nataka niongelee jambo moja. Walimu wanapewa kazi nyingi sana, mimi naomba tufike mahali hawa walimu tuwapunguzie kazi. Nitoe mfano walimu hawa ndiyo wasimamizi wa uchaguzi nchi hii inapofika kwenye uchaguzi na madhara wanayoyapata ni pale ambapo Chama cha Mapinduzi hakijapita, huyu mwalimu aliyesimamia, aidha ni Mratibu au Mwalimu Mkuu ajira yake iko hatarini. Natoa mfano huu katika Jimbo langu la Liwale leo hii wako walimu ambao waathirika kwa matukio haya. Sasa hatuwezi kuboresha elimu iwapo walimu hawana utulivu, walimu wanaidai Serikali, naomba tuliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye sekta ya afya. Tusitarajie mpango huu unaweza ukafanikiwa iwapo watu wetu hatujawajenga kiafya. Kwa upande huu wa afya nafikiri siasa imekuwa nyingi kuliko utekelezaji. Kama ambavyo watangulizi walivyosema nchi yetu watu ni wapangaji wazuri sana na mimi nasema huu Mpango tukiamua kuuza kwa nchi yoyote wakiutekeleza miaka mitano ijayo watakuwa mbali sana, lakini kwa Watanzania Mpango huu hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nchi yetu imekuwa na mipango mingi sana na kitu kikubwa sana nachokiona mimi ni kwamba nchi yetu inaongozwa na mawazo ya watu wachache. Leo hii tukibadilisha Waziri hapa Wizara hiyo itabadilika kwa kila kitu, hatuna *common goal* kwamba nchi inataka kwenda wapi, hilo ndiyo tatizo letu. Leo hii tukibadilisha Rais anakuja na mambo mengine. Mheshimiwa Mkapa alikuja na *Mtwara Corridor* baada ya Mkapa kuondoka *Mtwara corridor* ikafa. Mheshimiwa Kikwete alikuja na maisha bora na yenyewe sijui kama itaendelea. Pia alikuja na Bandari ya Bagamoyo na sijui kama kwa utawala huu kama hiyo bandari bado ipo.

**MBUNGE FULANI:** Wamesema haipo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Sasa kwa mtindo huu hatuendi kwamba kila Waziri, kila Rais atakayekuja na la kwake hatuna *common goal* kama Taifa. Hili limeshatuletea matatizo sana, nitoe mfano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki tulipozungumzia habari za reli tulilalamika hapa, sisi tulikuwa walalamishi wakubwa sana, watu wa Uganda na Rwanda walipoamua kuondoka kujiunga kutengeneza reli tukaanza kulalamika, mnalalamika nini? Mnachelewa wenyewe halafu mnategemea wao wawasubiri hatufiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwa upande wa reli, sidhani kama kweli tuna dhamira nzuri kuhusu hiyo reli ya kati. Hivi unampaje mtu kusimamia reli ya kati ana malori ya usafirishaji zaidi ya 5000, hayo malori ayapeleke wapi? Ana malori ya usafirishaji 5000 halafu mnamwambia asimamie reli ijengwe halafu yeye malori apaleke wapi akafugie kuku? Tuache utani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye Bunge hili kama Waziri wa Miundombinu alisema Sera ya Taifa letu ni kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami. Nisikitike kusema sisi Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Liwale inaitwa Wilaya ya pembezoni, kwa mawazo yangu nikajua Wilaya ya pembezoni maana yake ni Wilaya inayopakana na nchi nyingine, lakini ndani ya Tanzania kuna Wilaya za pembezoni. Sisi Liwale tunapakana na Mkoa wa Morogoro, Ruvuma niambieni kama kuna barabara inayotoka Morogoro kuelekea Liwale, hakuna. Hatuongelei barabara za lami tunaongelea hata barabara za changarawe, kutoka Liwale kwenda Tunduru hakuna barabara. Wilaya ya Liwale leo iko pembezoni inapakana na nchi gani? Halafu mnasema tunaweza kwenda sambamba na huu mkakati, huu mkakati nasema kwamba hauwezi kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye upande wa amani, tumewapa kazi Polisi kwamba wao ndiyo walinzi wa amani, lakini nipende kusikitika kwamba hao polisi tunaowategemea wanaishi kwenye viota na mtaani. Hivi wewe polisi unakaa mtaani mwanangu anauza gongo utamkamata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale imekuwa Wilaya mwaka 1975 mpaka leo hawana Kituo cha Polisi. Kituo cha Polisi cha kwanza kilikuwa kwenye gofu la mkoloni, NBC walipojenga nyumba yao wakahamia huko, ile nyumba ilikuwa ni ya mtu binafsi leo hii inamwaga maji kila mahali, mafaili yanafunikwa na maturubai halafu polisi hao hao ndiyo tunategemea walinde amani, hapo tunacheza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nijielekeze kwa upande wa sekta ya viwanda. Sekta ya viwanda hasa kwa sekta binafsi huku ndiyo tumekwama kabisa. Kama tumefika mahali tunawaacha vijana wetu wahangaike na hawa matajiri wakubwa, eti ndiyo wa-*bargain* mishahara. Mimi

nasikitika jambo moja, sielewi imekuwaje. Zamani nilisikia wale ma-TX walikuwa na vibali vya kuishi miaka miwili leo hii tuna ma-TX kwenye viwanda vya watu binafsi mpaka wafagizi na madereva, sijui Uhamiaji wanafanya kazi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mpaka naingia hapa Bungeni nina miaka 30 kwenye sekta ya watu binafsi, nimetembea zaidi ya viwanda sita, usiniulize kwa nini nimebadilisha viwanda vyote hivyo, ni kwa sababu nilikuwa sitaki kunyanyaswa. Haiwezekani leo hii tuna ma-TX, mtu ana cheti cha uinjini ni dereva, ana cheti cha uinjini anasimamia upakizi wa mizigo kiwandani, hii nchi imeoza, ni kama vile haina mwenyewe. Ndiyo maana nikasema kama ni kutunga sheria sisi tunaongoza kwa kutunga sheria nzuri sana na kama kwa mipango sisi tunaongoza lakini utekelezaji zero. Kama walivyotangulia kusema wenzangu, Waheshimiwa Mawaziri mliopewa dhamana nafuu msikilize Wabunge wa Vyama vya Upinzani wanasema nini, lakini mkiwasikiliza wa huko mtapotea na kama majipu ninyi mtakuwa wa kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze upande wa kilimo. Kilimo ndugu zangu hakiendeshwi na ngojera hizi za kilimo kwanza wala kilimo uti wa mngogo, tuna matatizo ya masoko. Nikupe mfano Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Liwale, sisi tunalima korosho, ufuta, mbaazi lakini wakulima wetu sasa hivi bado wanahangaika. Mwaka juzi mbaazi ilipanda bei watu wakajikita huko, mwaka huu korosho zimepanda bei, ufuta umeshuka. Kwa hiyo, watu bado wanahangaika yaani wanalima kwa kubahatisha kwamba ukilima ufuta ikikuangukia bahati umepanda bei ndiyo unanufaika, ukivuna korosho mwaka huu imepanda bei ndiyo umenufaika. Hizi ngonjera za Kilimo Kwanza bila kutafuta masoko ya mazao yetu hatutakwenda huo mkakati ni wa kufeli. Mimi sijaona kwenye mpango huu wapi kumeelezwa suala kuimarisha masoko. Ntoa angalizo hatuwezi kuimarisha kilimo kwa ngojera ya kilimo kwanza wala kilimo uti wa mngogo ni lazima tufanyekazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye huu Mpango uliowasilishwa na Waziri wetu wa Fedha. Kwanza nauunga mkono kwa asilimia moa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hapa nilipofika. Maandiko yameandikwa kwamba Mwenyezi Mungu humpa amtakaye na kumnyima amtakaye. Kwa hiyo, nashukuru kwamba wenzetu ambao wanapiga kelele sana Mwenyezi Mungu aliamua tu kwamba hawa hawafai kwa sasa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kwa kuiba.

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru wananchi wangu wa Tabora kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Tabora Mjini. Pia hawa ndugu zetu wanapoongelea suala la Hapa Kazi Tu, nashindwa kuelewa sijui hawaoni au hata hawasikii kwa sababu unapoongelea kauli mbiu ambayo wewe unaona kwa vitendo inafanyika, mimi nashangaa kama hawaoni hata kama kuna mabadiliko hata ya ukusanyaji kodi tu nayo hawaoni. Kama tunakwenda kwa kauli, mnaelewa kuna viongozi ambao walisemwa kwenye Bunge hili hili, wakatukanwa sana, lakini leo wakaja na kauli mbiu ya siku 100 nyumba za nyasi hamna wakati kwao kuna nyasi nyingi tu lakini leo wanakumbatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mimi nianze kuchangia kwa suala la reli. Sisi ambao tuko Kanda ya Ziwa, suala la reli kwetu ni muhimu sana na siyo tu Kanda wa Ziwa lakini kwa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Reli ya kati kwa jinsi ilivyo sasa kuanzia Dar es Salaam kuja Tabora lakini kutoka Tabora kwenda Mwanza, kwenda Kigoma na Mpanda ni chakavu sana na ndiyo maana mara kwa mara reli hii imekuwa na matatizo ya kukatika vipande vipande. Kwa hiyo, lile suala la *standard gauge*, naiomba Serikali iipe kipaumbele reli hii kwa sababu inasaidia vitu vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la viwanda, kwa mfano Tabora tulikuwa na Kiwanda cha Nyuzi nimeshawahi kuzungumza hapa ambacho sasa kimekufa kwa sababu ya mwekezaji ambaye hakuwa mkweli. Sasa Mheshimiwa Waziri mhusika nadhani nilizungumza niliongee kwa ufupi kidogo, kile kiwanda yule aliyebinafsishiwa sasa amegeuza *godown* lakini pia kakifunga. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Viwanda, Tabora tunahitaji sana viwanda kwa sababu *raw materials* zipo, tunahitaji pia Kiwanda cha Tumbaku kwani inalimwa zaidi Tabora kuliko mkoa mwingine wowote, hakuna sababu ya Kiwanda cha Tumbaku kuwa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wanatabora tunaomba katika kuweka vipaumbele mkikumbuke Kiwanda cha Tumbaku Tabora kwa sababu ndiko zao linakolimwa zaidi. Kwa sasa tuna vile viwezeshi vingi vya kufanya hata ile tumbaku yenyewe ifikiwe kiurahisi. Barabara hii inayokatisha Manyoni maeneo ya Chaya imebaki kama kilomita 82 kufika Tabora Mjini. Kama barabara ile itakuwa imekamilika basi Tabora mtakapokuwa mmetuwezesha Kiwanda cha Tumbaku mtakuwa mmetusaidia. Siyo suala tu la kama wameisaidia Tabora, lakini na uchumi kwa sababu hata wale ambao wanasafirisha tumbaku ile kuitoa Tabora kuipeleka Morogoro ni gharama kubwa lakini pia gharama zile zinafanya wakulima wa tumbaku wanaumia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora wamekuwa waaminifu sana wote mnafahamu, imekuwa ni ngome ya Chama cha Mapinduzi hata kama wapinzani wanajaribu kubeza lakini ile imekuwa ngome ya Chama cha Mapinduzi. Mkoa wetu wa Tabora watu huwa hawasemi sana wanaenda kwa vitendo. Kwa kuwa hawasemi sana naomba tusiwachukulie upole wao kwa kuwacheleweshea vitu ambavyo vinaonekena kwa macho. Nadhani mnaelewa Tabora ukiwaudhi kidogo unakaa miaka mitano unatoka nje ya ulingo. Tabora katika miaka thelathini hajjawahi kumrudisha Mbunge zaidi ya miaka mitano na hizi ni hasira zao. Pamoja na hayo bado hawachagui mpinzani, watamtoa wa CCM wataweka wa CCM kwa maana ya kwamba bado wanaimani na Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

**MBUNBGE FULANI:** Sakaya je?

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tabora pia tunarina asali kwa kiwango kikubwa. Naomba tunapoweka mipango hii tuweze kukumbuka hata kuwa na kiwanda kidogo cha kusindika asali Tabora. Si hilo tu, Tabora pamoja na Shinyanga na mikoa inayofuata wafugaji ni wengi sana, ngozi inayopatikana kule, viwanda kama *leather goods* lakini pia viwanda vya kusindika nyama vinahitajika kule. Maana ili uwe na viwanda pia ni vizuri kama kile kiwanda kiwe ni kiwanda ambacho kina faida kwa uchumi wa Tanzania na siyo siasa zaidi. Kitu cha kujiuliza *raw materials* zinapatikana maeneo yale, Tabora zinapatikana. Kwa hiyo, naomba mtukumbuke kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine ambalo linahusiana na reli hiyohiyo ya kati kutoka Isaka kwenda mpaka Keza na kutoka eneo la Uvinza kwenda Msongati hii ni reli mpya. Reli hii tunaihitaji kwa ajili ya uchumi, tunaihitaji kwa ajili ya kupata maendeleo katika maeneo hayo ambayo kwa kweli ni ngome ya Chama cha Mapinduzi kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie reli upande wa hapa Morogoro hasa maeneo haya ya Godegode. Kila mara imekuwa pale ndiyo pana matatizo makubwa, tatizo ni nini kama Malagarasi imeshajengwa? Kama Malagarasi daraja limeweza kufanya kazi nina imani Serikali hata pale Godegode inawezekana. Hata hiyo *standard gauge* tutakayoitengeneza kwa mujibu wa mpango huu basi isije ikawa tena kufika Godegode yakawa yaleyale. Naomba Waziri anayehusika na hilo aweze kulitilia maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nizungumzie...

#### **TAARIFA**

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya taarifa Mheshimiwa Mtulia.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah.

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa mazungumzaji kwa kutumia Kanuni ya 64(1) (a) amezungumza maneno ambayo siyo sahihi na katika Bunge hili Tukufu Mbunge yeyote hatakiwi ama hapaswi kuzungumza uongo. Mzungumzaji aliyekaa ametoa taarifa za uongo ya kwamba Tabora hakuna Mbunge wa Chama cha Upinzani isipokuwa ni CCM tu wakati humu ndani tuna Mbunge wa Chama cha Wananchi (CUF) kutoka Tabora. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Huko siyo Tabora ni Kaliua.

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliweke sawa hili labda pengine unajua Kiswahili kina matatizo yake. Mimi ni Mbunge wa Tabora Mjini na hawa wanaongelea sijui Kaliua mimi sijaongelea Kaliua. Nimezungumzia miaka 30 ambayo inahusiana na mjini na huu ni ukweli.

**MBUNGE FULANI:** Ulisema Tabora.

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Narudia Tabora Mjini haijawahi kutokea katika miaka 30 Mbunge akarudi mara mbili. Naomba nieleweke sijaongelea Kaliua kwa hiyo sikusema uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde zile dakika zangu ambazo imeingia hoja ambayo nayo haikuwa ya kweli. Tunapongelea hii reli, reli ina matatizo mengine ambayo Serikali bado nadhani haijaka sawa. Ni vizuri kukumbuka suala la wafanyakazi wa reli, reli hii imekuwa ikihujumiwa mara nyingi sana. Kile kipindi cha *transition* wakati reli imechukuliwa na wale wawekezaji wa India, wafanyakazi wale walipokuwa wanarudi kujiendesha wenyewe waliahidiwa kulipwa mafao yao ambayo yatakuwa tofauti na mkataba wa mwazo ambayo mpaka leo hayajalipwa kwa wafanyakazi wale. Wafanyakazi wengi wa reli kwa muda mrefu wamekuwa katika kipindi cha malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweze kufikiria kulipa wale wafanyakazi haki zao stahiki ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na waweze kuipenda kazi yao. Kwa sababu mengine yanatoka inakuwa ni hujuma tu kwa sababu mtu hajaridhika na kitu anachokipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli kuna matatizo wafanyakazi hawajalipwa haki zao ambazo ziliahidiwa na Serikali kwamba akishatoka yule mwekezaji wa

Kihindi basi kuna maslahi ambayo watalipwa ambayo wanayapigania mpaka sasa. Nina imani wale wafanyakazi watakapokuwa wamelipwa zile staili ambazo waliahidiwa basi ufanisi katika Shirika letu la Reli la Tanzania utakuwa umeboreka na utakuwa wa kupendzesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja Mpango huu kama ulivyowasilishwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ili na mimi niweze kutoa yangu machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kuniwezesha kuwa mmoja wenu katika Bunge hili. Aidha, nawapongeza Wabunge wenzangu ambao wamefanikiwa kuingia katika Bunge hili. Nakupongeza wewe kwa nafasi hiyo, nampongeza pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzio, nawatakia kila la kheri katika kazi hiyo na najua mnaimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi sikupata nafasi ya kuzungumza wakati wa kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba kidogo nichukue nafasi hii na mimi kumpongeza Mheshimwia Rais, kwanza kwa ushindi mnono alioupata lakini pia kwa hotuba nzuri sana aliyoitoa ambayo imegusa nyoyo zetu sisi na wananchi karibu wote. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ameonyesha uwezo mkubwa na ameonyesha ukweli wake. Kwenye kampeni alikuwa akisema nipeni nifanye kazi, msema kweli mpenzi wa Mungu na kweli tunamuona anatenda yale ambayo alisema angefanya. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye Mpango, napenda nimfahamisha kijana wangu ambaye alizungumza hapo awali, nadhani ni Mbunge wa Liwale, ni kijana madogo kwa hiyo anahitaji kusaidiwa. Amenigusa alivyoanza kuzungumzia *Mtwara Corridor*, misamiati, kaulimbiu zinazotolewa, Mheshimiwa Rais Mkapa amekuja na *Mtwara Corridor* ipo wapi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amekuja na maisha bora yapo wapi. Mheshimiwa Mbunge pengine kwa ajili ya umri wako, leo unazungumzia *Mtwara Corridor*! Sasa hivi wenyewe wa *Mtwara* wanasema *Mtwara* kuchele. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Muongo.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** *Mtwara Corridor* isingewezekana bila ya kuwa na miundombinu na moja ni barabara. Wakati Mheshimiwa Mkapa akizungumzia *Mtwara Corridor* hata barabara ilikuwa hakuna, daraja lile la Mkapa lilikuwa halipo na limepewa jina sahihi kabisa, limejengwa katika ku-*facilitate Mtwara Corridor*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ukienda Mtwara siku nyingine unaweza ukalala mwezi mzima daraja la Mkapa hujafika kule. Leo Mheshimiwa Mbunge najua kwa umri wako pengine wakati ule hujawahi hata kusafiri, lakini mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kazi nzuri imefanywa na *Mtwara Corridor*, ule mradi wote wa gesi umeanzia huko kwa Mkapa. Maendeleo ni mchakato, maendeleo hayaji siku moja. Mchakato ule ndiyo sasa unaonekana kule Mtwara, viwanda vinajengwa na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, inauma sana ukimsikia mtu anasema maisha bora kwa Mtanzania ilikuwa inapitapita tu, kweli tulikuwa hivi, hata Bunge halikuwa kubwa kama hili. Sekondari za Kata mara hii mmezisahau, vituo vya afya, zahanati kila kona, nchi hii imefunguliwa kwa kuwa na mtandao wa barabara, kama siyo maisha bora kwa kila mwananchi ni nini hiyo? Isitoshe angalieni *UDOM* hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

**MBUNGE FULANI:** Hamjalipa.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wake *university* ngapi zimeongezeka hapa nchini? Ndiko tunakoenda kuchukua maisha bora kwa kila Mtanzania ndugu zangu. Pamoja na simu zilizokuwa mifukoni kwa kila mwananchi yale yote ni matokeo mazuri ya maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye vipaumbele. Kwanza nampongeza sana Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri aliyoifanya na wameweka vipaumbele vizuri. Nataka nimkumbushe kwamba Mheshimiwa Rais alipokuwa akisoma hotuba yake alisema tutakamilisha miradi ya mwanzo na kuanzisha mipya. Hivyo basi, ni bora tukakumbuka miradi mikubwa ambayo ilikuwepo kabla ya Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni suala zito sana duniani, huko tunakokwenda ukiangalia mabadiliko ya tabianchi, wataalam wanasema vita ya tatu itatokea kutokana na kugombea maji.

Kwa hiyo, miradi mikubwa ya maji ambayo napenda kuikumbusha, napenda wakumbuke kwamba zaidi ya miaka kumi iliyopita kuna mradi mkubwa wa maji wa Kipera, tuliambiwa kule Kibada kuna bahari ya maji kule chini, mradi ule upo wapi? Tunakazania Mradi wa Mto Ruvu lakini kuna bwawa la Kidunda silioni! Bwawa la Kidunda ni lazima lijengwe, vinginevyo tunaachia maji yanaenda baharini, bahari haina shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa ya Ziwa Viktoria kupeleka maji Lamadi, Magu na Tabora. Hebu tuhakikishe miradi hii ya maji na mengine

inakamilika. Maji ni suala linalomhusu mwanamke na watoto, mwanamke anaamka asubuhi sana kutafuta maji, watoto wengine hawaendi shule ili waende kutafuta maji. Kwa hiyo, sisi wanawake linatugusa sana suala hili la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni la elimu. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuja na utaratibu wa elimu bure. Ndugu zangu kama nilivyosema maendeleo ni mchakato, elimu bure tulianza kwanza kujenga shule nyingi sasa wengi wataweza kusoma kwa elimu bure. Tatizo langu tunahitaji kuwa na elimu bora (*quality education*). Hiyo *quality education* isianzie sekondari tunahitaji elimu ya awali iweze kujenga msingi bora kwa watoto waweze kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi ilivyo sasa hivi mtu anamaliza *university* hajiamini, lakini ameanza toka kule kwenye msingi kujifunza kwa uoga. Kwa hiyo, naomba sana kwenye elimu tuwasaidie walimu kwa kuwaendeleza zaidi, tupate walimu bora ili watoto waweze kupata elimu bora zaidi na hasa elimu ya awali. Mimi naamini sana akitoka na elimu nzuri kwenye elimu ya awali hawatapata tabu huko watakapokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Geita Vijijini kwa kuniamini kwa kura nyingi, hawanioni lakini mmo mtapeleka taarifa, kwa kuniamini na kunipa Jimbo la Geita Vijijini pamoja na mikwara mingi iliyokuwepo kule maana *helicopter* ziliteremka zaidi ya mara nne. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kuzungumzia kidogo tu suala la Zanzibar. Ninyi ndugu zetu wa Upinzani acheni kuwachanganya watu, ngoma imetangazwa subirini mkashinde. Watu wanaojiamini hawaji hapa kutafuta sifa za kupiga kelele. Hata leo hii mkitengua uteuzi wangu tukarudia uchaguzi nawapiga bao kwa sababu ninapendwa. Kama mmeshinda kwa halali acheni kuja kuchukua sifa humu ndani za kuwadanganya watu mlishinda, mlishinda vipi, kama mlishinda mbona mko nje? Ujumbe umefika. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Mpango wa Maendeleo kama tunavyoendelea kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo mengi, hapa tunajadili Mpango na sisi Wabunge wapya tunasema Mpango huu ni mzuri isipokuwa tuusimamie. Hatutaki kuzungumzia Mpango iliyopita tunazungumzia Mpango tulionao. Huu Mpango ni mzuri na sisi wenyewe tutakabana kuukamilisha na kuusimamia. Wala tusianze kupotosha kwa kusema mambo ya miaka iliyopita sisi ni wapya tuzungumze haya tunayoanza nayo na kasi ya Mheshimiwa Rais aliyepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la reli. Upande wa reli naomba tuondoe hii sintofahamu. Sisi watu tunaotumia reli tunaomba kwanza kabla hatujajenga reli ya kwenda kuungana na Rwanda tuimarisha reli zetu ambazo zipo. Tusianze kuongeza mambo ya kutengeneza uhusiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati kwetu huku kumeoza, tuimarisha kwanza ya kwetu, ya kwenda Mwanza, Mpanda, Kigoma baada ya hapo sasa ndiyo tufikirie kutafuta mahusiano na nchi zingine za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naona humu halizungumzwi kabisa, sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa, ukienda Mwanza leo barabara zinazokatisha *airpot* kwenda Igombe zilishafungwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa kiwanja cha ndege. Kwa kweli ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza umekuwa unasuasua kwa miaka mingi. Humu ndani sijaona kabisa wapi pamesema tutaujenga uwanja wa Mwanza uwe uwanja wa kimataifa na mkizingatia Mwanza ni mji mkubwa nadhani ukiondoa Dar es Salaam sasa Mwanza ndiyo inafuata. Pia Mwanza tuko kilomita 92 tu kwenda Serengeti lakini hatuna uwanja watalii wanatua Arusha wanatembezwa kilometa 300 mpaka 400 na zaidi, kwa nini tusiimarisha uwanja wetu wa Mwanza ili na Mwanza nayo ikawa na utalii, tukajaribu ku-*balance* na wenzetu wa Kanda ya Kaskazini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye Mpango huu tuzungumze kuhusu uwanja wa ndege wa Mwanza, ni tegemeo kubwa. Leo hii ukienda Mwanza watu wana hoteli hakuna wateja wa kulala. Sisi Wasukuma ni washamba tukiona ghorofa tunakimbia hatulali humo. Tulijenga ghorofa kwa ajili ya wageni, wageni wanaishia Arusha tu. Niombe sana Mpango huu tuachane na porojo tumalizie Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza. Eneo tunalo na nguvu kazi na kila kitu kiko Mwanza, naomba sana hilo tulizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia suala la wachimbaji wadogo. Sikuona mahali kabisa linatajwa humu, sikuona! Kwa vile nilishazungumza na Profesa Muhongo nikamwambia Bunge lililopita ulipata figisu figisu ukaondoka, ukaingia kama mwanaume kwenda kugombea Jimbo, umerudi sasa na kasi ya Jimbo, porojo porojo tena hakuna. Kwa hiyo, sisi watu tunaotoka kwenye maeneo ya wachimbaji wadogowadogo tunahitaji kuwa na maeneo yetu ya kudumu, tena uwanyang'anye Wazungu wala usihangaikie kututafutia mapya. Kwa sababu sheria inasema kila baada ya miaka mitano unawanyang'anya

kiasi fulani unaturudishia, upeleke wataalam wako watafute maeneo yenye dhahabu za kina kifupi utukabidhi sisi wachimbaji wadogowadogo tuweze kuchimba na kupata dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la kilimo na viwanda. Ukianza Musoma mpaka Bukoba sisi tunazungukwa na Ziwa, ni neema pekee ambayo tumepewa na Mungu. Watu wa Kanda ya Ziwa wala hatuhitaji elimu kubwa ya kutusaidia katika suala la ajira. Tulikuwa na viwanda vingi lakini vimekufa vyote. Sasa ni jinsi gani Serikali inakaa upya na watu wenye viwanda kule Kanda ya Ziwa waweze kuweka mpango mzuri ili viwanda vyote vile vinavyozunguka kwenye kanda ile viweze kufunguliwa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wana nia sana ya kuwekeza katika viwanda vya samaki na viwanda vingine. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu vijiji vya Kagu, Nyewilimilwa, Bugurula tunaweza kuweka viwanda hata vya unga wa muhogo lakini hakuna barabara, umeme na maji hatuwezi kuweka viwanda kama hivi viambatanishi havijafuatana pamoja. Kwa hiyo, niwaombe wahusika waweze kuzingatia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda kwa Kanda ya Ziwa tunalihitaji, hatuhitaji maelezo marefu. Nataka niwaambie watu wote wa Kanda ya Ziwa tutaungana kwa sababu tunataka kuwa na viwanda vyetu. Humu hakuna itikadi, watu wanahama vyama lakini tunachotaka ni viwanda, sitaki kusema ni nani mnaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie suala la kilimo, sisi tunatoka sehemu za wakulima. Ukizunguka kule kwetu kote wimbo mkubwa ni kilimo cha pamba ambacho hakieleweki na hakuna mtu ataweza kukisimamia hata rafiki yangu Mwigulu hutaweza. Hii ni kwa sababu biashara ile imezungukwa na matapeli na Serikali inaona na tumeshindwa kabisa kuwadhifiti watu hawa.

Sasa mimi nilikuwa napendekeza na nikizungumza humu watu wananicheka, yako mazao ambayo hayahitaji kupigiwa debe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliuliza swali, niulize tena kwa sababu tuko kwenye Bunge la pamoja kwamba ni utafiti gani uliwahi kufanyika na waliofanya ni madaktari gani mpaka tukafika mahali tukapitisha mirungi kuwa dawa za kulevyaya? Nasema kila siku, ukienda Nairobi mirungi inasindikizwa na SMG za Jeshi la Kenya. Kuna ndege mbili Boeing zinateremka kwa wiki mara mbili kupeleka mirungi nchi za Ulaya. Sisi ukienda Tarime, Morogoro, Bunda kuna mirungi mingi, kwa nini tusirudie kufanya utafiti upya ili hii mirungi ikarudi kuwa zao la biashara ambalo halina utapeli, ni biashara inayoenda moja kwa moja? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia twende sambamba na bangi msinicheke, hata bangi mimi sina hakika kama inafaa kuzuiwa. Watafiti wetu waliofanya utafiti kuhusu madhara ya bangi hebu wafanye na utafiti wa madhara ya viroba. Tufanye utafiti kiroba na bangi ni kipi kinachowaumiza vijana wetu huko mitaani? Mimi naamini huko Usukamani mtu akila bangi analima heka mbili kwa siku. Sasa kwa nini tusiiboreshe tukaangalia madhara yake tukaiweka kuwa zao la biashara? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani wako wengi tu wanaotumia bangi tunaweza kutoa mifano na wala hawana shida na ndiyo vigogo kwenye hili Bunge. Sasa kama ninyi wenyewe watunga sheria mnatumia, message imeenda. (Kicheko/Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la maji, tunatoka kwenye Ziwa lakini hatuna maji. Tunaamini hii kauli mbiu ya Mama Samia kwamba baada ya miaka mitano akinamama hawatahangaika na suala la maji itatekelezwa. Tuusimamie vizuri Mpango huu ili uweze kwenda sambamba na kauli ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu wa Upinzani, tunapofika humu sisi wageni tunawashangaa. Tulipokuwa kule nje nilikuwa nikiwaona watu fulani sitaki kuwataja nahemkwa kusikiliza, lakini ukikaa humu ndani naona kama watu mnacheza maigizo. Mtu anasimama hapa anasema watu kondoo, wanaoitwa kondoo wenyewe wanashangilia, tunawafundisha nini watu wanaoangalia Bunge?

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, samahani Taarifa, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kuhusu bangi au?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri unaoburudisha anaotoa mchangiaji Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, napenda kuumpa taarifa kwa sababu ameuliza kuhusu utafiti kwamba bangi ama mihadarati ya aina ya mirungi ina madhara gani kwa binadamu. Kitaalam

napenda kumwambia bangi pamoja na mirungi inasababisha kitu kinaitwa *alosto* maana yake ni kwamba ukitumia kwa muda mrefu ile *addiction* ikazidi kwa muda mrefu unaweza ukaugua ugonjwa wa akili unaojulikana kama *cannabis-Induced psychosis*. Kwa maana hiyo, bangi ina madhara kwa afya ya binadamu na siyo vyema sisi kama viongozi tukatafuta namna yoyote ile ya kuchangia ili kuhalalisha kwa sababu za kiuchumi.

**MBUNGE FULANI:** Mwambie aache kuvuta bangi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea lakini nataka pia nimwambie afanye uchunguzi na viroba navyo pengine vina madhara zaidi ya mirungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bangi, sigara na bia...

**MWENYEKITI:** Una dakika mbili zimebaki malizia.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hizo nazitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana unaona hata upande wa pili kuhusu huu mwongozo wa Mheshimiwa Kigwangalla hawauungi mkono. Naomba tuendeleo kufanya uchunguzi wa kina. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia pia suala la elimu bure. Ndugu zangu wa Upinzani tumwogope Mungu, pengine ninyi hamtoki huko na wala hamjapokea taarifa kutoka kwenye shule zenu, hebu fanyeni ziara kwa kukashifu hili neno la elimu bure. Kaka yangu mmoja alikuwa anaomba Mwongozo hukumpa, hebu nenda kule Usukumani ukazungumze hayo mambo watakushangaa.

**MBUNGE FULANI:** Watakupiga.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure ndiyo sera yetu na hata Wabunge wengine wa CHADEMA na Madiwani wanaunga mkono, kwa nini tusibadilike, huu ni mwanzo. Kama ameahidi Mheshimiwa Rais elimu bure miezi mitatu au siku mia moja utamaliza matatizo yote? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ndugu zangu wa Upinzani wajazie nyama, zungumzia upungufu unaouona katika suala hili ili Serikali iyachukue

ikafanye marekebisho tukirudi Bunge lijalo tunamsifu Rais kwa mpango wa elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, *happy new year* Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie fursa hii kuwashukuru Wanambeya kwa kunirudisha tena mjengoni kwa kipindi cha pili na kunifanya niwe Mbunge niliyechaguliwa kwa kura nyingi kuliko wote humu ndani, *the most voted MP* kwenye *election* ya 2015. Kama Waziri Mkuu anatokana na Wabunge waliochaguliwa wangeangalia kura nyingi *may be* mimi ndiye ningekuwa Waziri Mkuu humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kitu kimoja, tunapanga Mpango wa Maendeleo humu ndani au tunajadili Mipango ya Maendeleo lakini wale wanayoipokea hii Mipango ya Maendeleo sidhani hata kama tayari wako *cemented* katika mazingira yao. Sina uhakika hata kama tayari mmeshapewa *instrument* ya kazi na Rais. Rais anapochagua Baraza la Mawaziri anawapa *instrument* ambayo ndiyo kama *job description*. Sasa nina wasiwasi kama hawa walishapewa na matokeo yake ndiyo maana wanaenda hovyoo vyo tu kwa kufuata mizuka ya Rais. Rais akitumbua majibu huku wao wanatafuta kule kwenda kutumbua, kinachotakiwa siyo kutumbua majibu twende tutumbue mpaka viini. *(Kicheko/Makofi)*

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbilinyi, Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 68 pamoja na Kanuni ya 64, mambo yasiyoruhusiwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa msemaji aliyekuwa anaongea kwanza ametumia maneno ya kuudhi lakini ametumia maneno ya dhihaka kwa kutaja jina la Rais kwa dhihaka. Kanuni ya 64(d) inasema hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haya ni maneno kweli yanayostahili heshima ya Rais kusema kwamba anaongozwa kwa mzuka? Mzuka ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri utusaidie kutupa mwongozo wako kama maneno hayo na Kanuni ile ya 64(d) yanaweza kweli kubeba maudhui ya kulitumia jina la Mheshimiwa Rais katika mazingira tuliyonayo hapa. Kwa nini asiyaondoe maneno haya halafu achange tu hotuba yake kwa staha na watu wote waweze kumwelewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph, kwa heshima kabisa mdogo wangu naomba ufute maneno hayo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapambana na changamoto ya *generation gap*, ndiyo inayomkuta Mheshimiwa Waziri. Mizuka ni neno la Kiswahili lina maana ya hamasa yaani ile amshaamsha kwamba Rais anaamshaamsha na wao kwa sababu hawajapewa *job description* wanaiga, huyu yuko buchani anaangalia nyama, huyu anafunga mageti, huyu naye sijui anafanya nini, hiki ndiyo kitu wanachokifanya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaozomeazomea niwaonye, wengi wenu waliokuwa wanazomea hawajarudi hapa. Waliorudi ni wajanja kama Dkt. Mwinyi wako kimya tu. Wanaozomeazomea wengi hawajarudi, hamtaonja *term* ya pili, siyo mchezo, hiyo nawaambia wazi kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye mchango...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbilinyi, Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko pale pale kwenye Kanuni ile ile na naendelea kuisitiza, Mheshimiwa Rais wetu haongozi kwa mzuka, kwa hamasa, anaongoza kwa taratibu, Katiba na sheria, haongozi kwa mzuka au eti kwa hamasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ana Ilani, Katiba, sheria, na taratibu anazozitumia kuongoza. Kwa hiyo, huu uongozi wa kufuata *generation* eti Rais anaongoza kwa mzuka, kwa hamasa, haiwezi kukubalika. Haya ni maneno ambayo yanaudhi na yanataka kudhalilisha jina la Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hiyo ifutwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge Mbilinyi!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia imeanza kujitokeza kutaka kufanya kama Rais sijui au huyu Rais wa Awamu ya Tano *untouchable*, haguswi kwa kauli wala nini, lazima tutasema. Sijasema Rais anaongoza kwa mizuka, nimesema hawa ambao hawajapewa *job description* ndiyo wanafuata mizuka ya Rais, wanafuata vigelegele, ninyi mnafuata vigelegele. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba unipe nafasi niendeleo kuchangia.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Utapokea Miongozo baadaye, naomba unipe nafasi ya kuchangia. *President* Magufuli siyo *untouchable* ni mhimili mwingine na hili Bunge litajadili bila kumkashifu na bila kumtukana pale atakapokosea, kwamba anapotumbua majipu aende mpaka kwenye viini, anafukuza watu kazi, watu hawapewi nafasi ya kujitetea, halafu tunaongea humu mnataka kusema vitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata maendeleo bila demokrasia...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, naomba unyamaze kimya kwanza. Hii hoja imetolewa na Waziri wa Nchi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, uendeleo.

**MBUNGE FULANI:** Aendeleo nini?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaongozwa na Kanuni, kama Mheshimiwa Mbilinyi hataki kufuta usemi wake na Kanuni zinaeleza wazi kama Mbunge anaamrisha hataki kufuta usemi wake, kwa nini usitumie mamlaka yako kwa Kanuni ya 5 ili uweze kufanya maamuzi sahihi? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Unakifundisha kiti, eeh!

**MBUNGE FULANI:** Kwani mzuka maana yake nini?

**MWENYEKITI:** Samahani, samahani, naomba tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi, naomba ufute kauli yako.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoomba unatarajia kupata au kukosa. Katika hili nimekataa kufuta kauli kwa sababu anachokisema nimesema sicho nilichosema. Nenda kwenye *Hansard* utaona maneno niliyoyaongea kwa ufasaha wake kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo umeamua nyuma, usubiri uende kwenye *Hansard* utaangalia, kama yakiwa maneno aliyosema Mheshimiwa Mama Waziri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi naomba utulie.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Ambaye yupo kwenye tatizo la *generation gap* basi ningefuta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi naomba utulie.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Naomba na muda wangu ulindwe lakini.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa sababu umekataa kufuta kauli, nasema tutakwenda kwenye *Hansard* kuangalia kimezungumzwa nini ili hatua ziweze kuchukuliwa. Tunaendelea, malizia dakika zako chache.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo dakika chache, ni dakika nyingi tu kwa sababu mmenikata wakati nikiwa kwenye dakika moja au moja na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kujadili maendeleo bila demokrasia, bila ya utulivu wa kisiasa kwenye nchi. Rais anasema yeye ni Rais wa vyama vyote, alisema kwenye kampeni mpaka juzi yuko Arusha, naona anaongea na watu, anasema yeye ni Rais wa vyama vyote, lakini Waziri Mkuu wake yule pale anatukataza Wapinzani tusifanye mikutano ya vyama vyetu vya siasa. Demokrasia iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kujadili maendeleo bila demokrasia, bila uhuru wa vyombo vya habari, wanafungia magazeti kiholela tu, wanakuja wanazuia wananchi wasiangalie Bunge kwenye *TBC* ambayo ni Televisheni ya Taifa halafu anakuja Nape anataka kufananisha sisi na Sri Lanka. Hivi toka lini sisi tumewahi kufanya mambo yanayoshabihiana na Sri Lanka? Kwa nini usiige Marekani ambako kuna *TV* inayoonesha *Senate* saa ishirini na nne inayoitwa *C-Span*, iko maalum kwa ajili hiyo, halafu unakwenda kuchagua *Weakest link*, unaenda Sri Lanka, unaenda Australia, ambako hatushabihiani wala hatushirikiani katika mambo yoyote. Ukifananisha na tunavyoshirikiana na

Marekani na tunaweza kuwaiga vitu vizuri kama hivyo wana *channel* inayoitwa C-Span ambayo inaonesha Bunge la Marekani masaa yote ndugu zangu.

Ndugu zangu katika suala la *drugs* hatuwezi kujadili maendeleo wakati nguvu kazi inazidi kuharibika. Sasa mimi najiuliza nguvu kazi inazidi kuharibika kwa dawa za kulevya, mmekomaa na ganja (*bangi*) kama alivyosema yule Mheshimiwa aliyepita, lakini mimi naomba....

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Again? I can't even speak eeh?*

### TAARIFA

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), si kweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amepiga marufuku vyama vya siasa visifanye shughuli zao za siasa na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliifafanua vizuri hiyo hoja siku ya Alhamisi alipoulizwa swali na Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutoa taarifa hiyo.

**MWENYEKITI:** Umeipokea taarifa Mheshimiwa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikataa, Waziri Mkuu anatakiwa afute kauli yake kabisa na aseme vyama viko huru siyo kupindapinda, kwamba niliongea kama Mbunge, sijui niliongea kama nini, aseme kwamba ni ruksa kwa watu kufanya shughuli zao za kisiasa kama kawaida. Hicho ndicho anachotakiwa asema. Ingekuwa ni uongo angekanusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajaribu kusema, mnazungumzia dawa za kulevya, Rais Kikwete alimkabidhi Rais Magufuli ripoti ya kazi yake ya miaka kumi yenye kurasa 54. Miaka ya nyuma huko Kikwete alisema anayo majina, je, yale majina kwenye hii ripoti ya kurasa 54 hayakuwepo? Kama hayakuwepo kwenye hii ripoti ya kurasa 54 kulikuwa na nini basi labda wananchi tungeambiwa kwa faida ili tujue nchi inakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye mipango ya maendeleo Kimataifa, safari za nje siyo tatizo. Kuna gharama nzuri na gharama mbaya. Gharama

mbaya ni pale kama vile Kikwete alikuwa anaenda sijui anapokelewa sijui na Mkuu wa Shule, Mkuu wa Chuo, sijui anapokelewa na Meya, sijui anapokelewa na Mkuu wa Taasisi gani, lakini ni lazima ili tuende sambamba na dunia, sisi siyo kisiwa, lazima Rais Magufuli aende UN, lazima aende AU kwenye vikao vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna Mkutano Davos wa Kimataifa, dunia yote iko kule inazungumzia uchumi, wewe umekaa huku, unasemaje Mipango ya Maendeleo. Kwa hiyo, kuna gharama mbaya na gharama nzuri. Gharama nzuri unakwenda Davos, unakutana kule na dunia, kina Putin na akina nani, mnajadili dunia inavyokwenda masuala ya uchumi, unatangaza na visima vyetu vya gesi kule kwa *deal* nzuri na vitu vingine kama hivyo ndugu zangu.

Kwa hiyo, gharama nzuri ni pamoja na kwenda Davos, kwenda UN, lakini pia kuangalia *delegation* iwe ndogo siyo kwenda na *delegation* ya watu 60, watu 70. Kwa hiyo, *President Magufuli he has to go abroad* akajifunze. *Take a jet brother, he have to take a jet* akajifunze dunia inafanya vipi, Marais wanafanya vipi, watu wapo Davos huko akina Putin, akina nani, yeye amekaa hapa. Apunguze *delegation* tu, aende na watu kama kumi na tano, 10 inatoshia, aache kwenda na watu 60, 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu mnasema mnaboresha wakati wafanyakazi bado wananyanyaswa, wanafukuzwa hovyoy. Hapa leo niko Bungeni, tayari huko Mbeya Cement kwangu, kuna wafanyakazi wanapunguzwa. Mtu kafanya kazi miaka nane, anakuja kupewa 180,000/= ndiyo kiinua mgongo huko. Mnaboresha vipi masuala ya wafanyakazi. Umeme, naona hata kazi kuchangia hivi vitu *in details* kwa sababu miaka mitano nimechangia na mpaka leo bado tuko vilevile, ndiyo maana unaamua kutupia tu kama hivi. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme, Profesa Muhongo, nimeangalia ukurasa wa 41 kwenye mpango wa umeme, nishati. Sijaona mpango wa umeme kutumia chanzo cha joto ardhi (*geothermal*), ambao dunia nzima inajua ndiyo umeme rahisi, kule Italy kuna kituo cha *geothermal* toka mwaka 1911 mpaka leo kinafanya kazi, wanabadilisha tu nyembe zile kwa sababu chanzo ni cha uhakika na cha maana zaidi. Katika hili, Serikali hii imeanzisha Kampuni, kuna meneja, kuna *management* wako kule Mbeya wamekaa hela hamuwapi wanahitaji dola milioni 25 kutuletea umeme huu nafuu, lakini ninyi mnakaa mme-*mention* hapa kila kitu mambo ya *geothermal* (joto ardhi) hamna, maana yake nini? Mtakwenda kesho mtawatembelea ofisini, mtasema hawafanyi kazi, mtawafukuza kazi, mnasema mmetumbua majipu wakati hela ya kufanyia kazi hamjawapa ndugu zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitoe angalizo kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nakufahamu siyo sana kwa kukufuatilia weledi wako, wewe ni *technocrat*, siyo mwanasiasa, usifuate hawa wanasiasa wanazomeazomea, tunaamini kwamba ukitulia, ukatumia nafasi yako kama *technocrat* ukacha *cheap politics, populism*, unaweza ukaisaidia nchi pengine na sisi tutaku-support ili twende vizuri. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii fursa ya kutoa mchango wangu. Nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wa Nkenge kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kunirejesha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia, kupongeza hotuba aliyotoa Mheshimiwa Rais alipozindua Bunge hili. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa taarifa aliyowasilisha leo hii hapa Bungeni ambayo imezingatia pia maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa 16, alibainisha kwamba matarajio yake ifikapo mwaka 2020 angalau viwanda viweze kutoa ajira 40% ya ajira zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa sasa na taarifa za Mheshimiwa Waziri alizowasilisha, inaonesha kwamba kwa mwaka 2014 viwanda vimetoa ajira kwa asilimia 3.1. Sasa lengo letu ni kuhakikisha sasa viwanda vitoe ajira ifikapo mwaka 2020 kwa 40%. Sasa kutoka asilimia 3.1 kwenda 40% kuna kazi kubwa ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo, nitabainisha masuala muhimu ambayo yakizingatiwa tutaweza kufikia 40% ya ajira kutolewa na viwanda. Jambo la kwanza, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amebainisha kwamba, kwa vyovyote vile itakavyowezezana lazima tutekeleze utekelezaji wa miradi mikubwa ya kielelezo au wanasema *flat projects*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimepitia ile orodha ya ile miradi, nikagundua kuna mradi mkubwa umesahaulika kwa bahati mbaya na mradi wenyewe ni ujenzi wa *Kajunguti International Airport*. Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye kampeni, jambo mojawapo aliloahidi wana Misenyi, alisema akiingia Ikulu, fedha zote atakazozikuta atazileta Misenyi kulipa fidia kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Kajunguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwakumbusha wasaidizi wake, wahakikishe katika Mipango ijayo, wahakikishe wanazingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, lakini pia *Kajunguti International Airport* ni muhimu siyo tu kwa Misenyi, lakini pia kwa Taifa. Tunazungumza kuanzisha masoko ya kimkakati kwa sababu uwanja huo wa Kajunguti, siyo tu tutajenga uwanja wa Kimataifa lakini utaendana na ujenzi wa viwanda, utaendana na kuendeleza maeneo

maalum (*Special Economic Zones*), utaendana na kuweza kuzalisha bidhaa mbalimbali zilizo karibu na Soko la Afrika Mashariki ukizingatia ukweli kwamba tunapakana na Rwanda, Burundi na Uganda, lakini pia tunaweza kuuza maeneo mengine. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia, tunaposema kwamba tunahitaji kuwa na uchumi wa viwanda, hatuwezi kusahau kilimo. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyowasilisha leo hii hapa, nimesoma yote, lakini sioni maneno ya kilimo kwanza yakijitokeza, nikafikiri labda tumeanza kusahau sahu kilimo kwanza. Nitoe ushauri, kilimo kwanza ni jambo la muhimu, hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda bila kuwa na kilimo kinachozalisha kwa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimesoma hotuba hii, mara tatu, mara nne, sikuona maneno *Big Results Now* yakijitokeza. Nikaanza kufikiri kwamba labda sasa *Big Results Now* siyo msisitizo tena, lakini nikumbushe kwamba *Big Results Now* ni muhimu, zile sekta sita ni muhimu, zisipozingatiwa kwenye mipango yetu tutafika sehemu tuisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwamba unapozungumza kwamba unataka uwe na uchumi wa viwanda lakini unapenda vilevile kuhakikisha una kilimo kinachozalisha kwa ziada, lazima tuhakikishe migogoro ya wafugaji na wakulima inakoma. Jimboni kwangu kuna mgogoro mkubwa wa Kakunyu. Mgogoro huu umechukua zaidi ya miaka 15. Sasa kuwa na mgogoro ambao haumaliziiki. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alishatoa maelekezo mgogoro huu uishe na Mheshimiwa Magufuli ametoa maelekezo mgogoro huu uishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi pia washirikiane kuhakikisha wanamaliza mgogoro huu kabla sijaanza kuchukua hatua nyingine ambazo nitaona zinafaa kama mwakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niseme naunga mkono hoja. (*Makofi*)

(*Bunge lilirudia*)

**MWENYEKITI:** Naomba niahirishe kikao hiki cha Bunge hadi kesho Jumanne tarehe 2, Februari 2016, saa tatu asubuhi.

(*Saa 7.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Februari 2016, Saa Tatu Asubuhi*)

**Kikao cha Sita – Tarehe 2 Februari, 2016**

**HOJA ZA SERIKALI**

**KAMATI YA MIPANGO**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na tuna orodha hapa ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Zacharia Issaay, yupo?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Nipo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sawa, dakika kumi!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia, pamoja na Mpango huu tunaoadili wa Bajeti, nami nitoe mchango wangu kwa sehemu ambayo naiona katika Mpango huu. Kwanza napenda kuishauri Serikali katika ukusanyaji wa kodi. Ifike mahali sasa tukusanye kodi kwenye viwanda, tukusanye kodi kwenye makampuni makubwa, bandarini na tuwe na lengo kubwa la kukusanya kodi kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya Mpango huu wa Bajeti wa mwaka huu unakabiliwa na changamoto kubwa huko mbele. Kwa hivyo, tusipokusanya kwa kiwango kikubwa mapato ya Serikali, Mpango huu unaweza kuwa mzuri sana kama ulivyowasilishwa kwetu sisi, lakini hatimaye usiwe na matumaini na mafanikio mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango huu ninaoutoa katika kukusanya mapato ulenge zaidi yale makundi makubwa ya walipakodi kuliko wale wananchi wa ngazi za chini na wafanyabiashara wa ngazi za chini. Ifike mahali sasa tujijengee dhana ya udhibiti wa mapato ya Serikali na jinsi ambavyo wananchi wana hamu kubwa ya kupata huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kutokana na muda, ni eneo la elimu bure. Nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mheshimiwa Rais kwa kutoa elimu bure. Naomba nishauri mambo machache.

Katika eneo hili sasa Serikali ije na mpango wake wa kuajiri nafasi zile za wazi katika Serikali ikiwemo zile za wale vijana wanaofanya vibarua katika shule hizi za sekondari ili gharama ipungue kwa mwananchi, lakini pia namna ya kupunguza zile gharama zilizobaki. Hadi sasa bado kuna michango mikubwa katika eneo hili la elimu ya sekondari na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweze kuona ni namna gani inajaza nafasi za wahudumu, wapishi, walinzi na pia nafasi za kupunguza gharama zile zinazotokana na mwananchi ili wanafunzi wengi wapate elimu hii na kwa nafasi yao wapate kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo linalohitaji kuboreshwa zaidi. Katika mchango wangu naomba kuishauri Serikali.

Kwanza ichukue nafasi kubwa ya kuweza kuanzisha Vyuo vya VETA, lakini pia Vyuo vya Ufundi Stadi vilivyopo katika Wilaya na kwenye Majimbo yetu, vibadilishwe kuwa Vyuo vya VETA haraka ili vijana wetu wengi wapate hatua ya kuwa na nafasi ambayo vijana wanapata ujuzi na ufundi stadi na kuweza kuajiriwa na hatimaye kumudu changamoto zitakazotukabili katika uanzishaji wa viwanda.

Eneo la viwanda, naomba basi niishauri Serikali, eneo hili la viwanda, tuweze kufanya utafiti kama Serikali, tuone kiwanda gani katika kanda ipi, rasilimali gani inahitajika na ipo katika eneo hilo ili kupunguza gharama na viwanda hivyo viweze kuwa na tija na kwa hivyo tunapofanya hivyo tunapunguza gharama kubwa ya uendeshaji wa Serikali katika kuanzisha viwanda na kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, nitoe angalizo pia katika eneo hili, ni eneo ambalo linatupa kazi kubwa kwenye madeni ya Serikali. Jimboni kwangu, nichuke nafsi hii kukuomba sana. Serikali ina madeni makubwa sana, isifumbie macho. Madeni ya maji, madeni ya maabara, madeni mengine mengi ya barabara, lakini wakati huu Mpango umewasilishwa kwetu ni mpango mzuri, tutashindwa kutekeleza kule mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali, wakati wa sasa hadi kufikia bajeti, ikusanye orodha kubwa na takwimu kubwa ya madeni ya Serikali ya miradi iliyoanzishwa. Kama Jimbo ninalotoka, madeni ni zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia. Fedha zinazodaiwa na wakandarasi kwa ajili ya malipo yao, wale waliokamilisha kazi na wale ambao wamefikia hatua mbalimbali, ni zaidi ya shilingi milioni 700, lakini hata kama tumekuwa na Mpango mzuri mbele ya safari tutakuja kuhitilafiana na hatutakuwa na tija katika hii mipango mizuri kama hatutaweza kuona ni kwa namna gani madeni

ya maji, barabara, maabara zilizoanzishwa na wananchi kwa kiasi kikubwa sana na sasa hata umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo ninalotoka mimi, umeme umekwenda kwa vijiji takriban tisa au kumi, huku Waziri anatupa matumaini makubwa sana. Naomba kama itawezekana maeneo haya ambayo tayari Serikali imekuwa na madeni makubwa, yawekwe kwenye Mpango huu wa sasa ili yaweze kutatuliwa na wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ni jambo jema kama tutakuwa tunakamilisha miradi na inatoa huduma. Miradi ya aina hii iko mingi, kwa mfano, tulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais katika barabara ya Magara inayounganisha Mji wa Mbulu na Mji wa Arusha na Mji wa Babati kwa maana ya Makao Makuu ya Mkoa, Babati na Makao Makuu ya Mkoa wa Arusha. Kilometa 13 za ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imewekwa kilometa moja na nusu hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Magara katika barabara hiyo, ambayo imepoteza maisha ya Watanzania wa Wilaya ya Mbulu na Wilaya ya Babati Vijijini, haikuwekwa hadi leo, kutoka ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ahadi ya Mheshimiwa Mkapa na leo ahadi ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli na ni kilometa hiyo yenye mazingira magumu na hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapanga mipango, ikifahamu kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais ni moja ya utatuzi wa kero za wananchi. Pale ambapo Rais anafanya ziara, anapokutana na changamoto ya kero zao anawaahidi. Kufanyike utaratibu wa kuratibu ahadi za Mheshimiwa Rais. Iwekwe kwenye Mipango ya Serikali, ili Serikali kila wakati na kila mwaka katika bajeti yake, iweze kutatua. Barabara hii ya Magara, ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi, nashangaa kama tena leo, tunatafuta fedha za usanifu kwa ajili ya Mlima Magara na Daraja la Magara, wakati Serikali imetumia pesa nyingi kufanya usanifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, ahadi nyingi za Rais ziwekwe katika bajeti hizi na Mlima Magara usipowekwa kwenye bajeti ya mwaka huu, natoa angalizo kwamba sitakuwa tayari kupitisha Mpango wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kuzungumzia eneo la kero ya akinamama, wauza matunda, mbogamboga, ndizi, waendesha bodaboda, kodi hizi ziondolewe, ni kero. Haya ni makundi madogo, hayana uwezo wowote na hali hii inawasababishia mazingira magumu ya kufanya kazi zao. Naomba nitoe mchango huu kwa kuishauri Serikali itazame

kwa jicho la huruma makundi haya ambayo tayari ni makundi ya jamii. Yanafanya shughuli hizi, wana mapato madogo, hawa watazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe angalizo kwa jinsi tunavyopoteza muda wetu katika ukumbi huu. Mara nyingi tumekuwa wa kuzomeana, mara nyingi tumekuwa wa mipasho, mara nyingi kiti chako kimeshindwa kulinda kikao na kwa mara nyingi tunashindwa kupata nafasi ya kutoa michango yetu. Tunaminywa katika dakika hizi mnazotupa kwa sababu ya mipasho, mizozo na migongano ya kisiasa yasiyo na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, miaka mitano ni kama mshale wa saa na Rais alisema tupunguze mipasho, mizozo na vijembe. Sasa Bunge hili, takriban muda wote tuliotumia ndani ya ukumbi huu, tumetumia muda mwingi vibaya na kwa hivyo hasara hii ni kubwa kwa Bunge, ni kubwa kwa Serikali, tunagharamikiwa kwa kodi za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uongozi wa Bunge, kutoka kwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti, watusimamie ipasavyo kwa kulingana na kanuni zetu humu ndani. Ili haki itendeke kwa kila mmoja wetu kukosolewa, kurekebisha na kuadhibiwa ikibidi. Kwa sababu tusipofanya hivyo, tutafanya makosa makubwa na mbele ya safari tutaleta uvunjifu wa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imefika mahali, unafika mlangoni unaambiwa uvue mkanda. Hii ilikuwa jeshini, ilikuwa magerezani, sio huku. Huku ni eneo la heshima, tunatakiwa tujiheshimu na wale wenzetu wanaotuhudumia watuheshimu na hata kiti chako kiti kwa jinsi ambavyo tunafanyiwa, sio vizuri na sio itifaki ya Bunge. Naomba nafasi hii itumike vizuri, tusikejeliane na yeyote yule ambaye hataki kuheshimu kwa kweli tunakoseana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay muda wako umekwisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nafasi hii ni ndogo sana na ni ya hasara kwetu sisi na tunaminywa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mapendekezo yangu kuhusu Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Nina

maeneo machache sana ambayo naomba yafanyiwe *improvement* katika Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza linahusiana na ujenzi wa uwezo wa watu kwa ajili ya kuwaandaa kwenye uchumi wa viwanda. Katika ukurasa wa 25 wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2016/2017, kifungu cha 3.2.2; miradi mikubwa ya kielelezo, Serikali imezungumzia kusomesha vijana wengi kwa mkupuo katika fani za mafuta na gesi, wahandisi kemikali, viwanda vya kioo na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba, hatuwezi tu kuwa na watu ambao wamesomeshwa katika ngazi ya Vyuo Vikuu na hatuna watu ambao wako kwenye ngazi za chini. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba, tuongeze katika vipaumbele vya miradi mikubwa ya kielelezo (*flagship projects*) uwepo kwa VETA na Vyuo vya Ufundi vya Kati, kwa maana ya *Technical Colleges*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mafundi wa kuwasaidia Wahandisi na bila kuwa na VETA za kutosha nchini, hatutakuwa na mafundi wa ngazi za chini na bila kuwa na *Technical Schools* za kutosha nchini, hatutakuwa na mafundi mchundo wa katikati, ambapo kila Mhandisi mmoja, anahitaji zaidi ya mafundi mchundo 25 ili kuwezesha kazi kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba, kwa sasa hivi, kuna *low-hanging fruits*. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba kuanzia sasa, kila Kambi ya JKT, iwe ni Chuo cha VETA, iwe *designated* kuwa chuo cha VETA na wale vijana ambao wanakwenda JKT kwa hiari, wale wa miaka miwili wale, watoke na ujuzi badala ya kuwafundisha tu masuala ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, wapate mafunzo ya kuweza kwenda mtaani na kuweza kufanya kazi, itatusaidia kupunguza tatizo la ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, naomba tupate *support* Kigoma kule kuanzisha Chuo cha Ufundi wa Kati. Pendekezo langu ni kwamba angalau kila mkoa uwe na *Technical School* moja, maana yake sasa hivi vyuo ambavyo vipo, kama *Dar Tech*. imekuwa *Dar es Salaam Institute of Technology*, Mbeya *Technology* sasa hivi imekuwa ni Chuo Kikuu, vimegeuzwa kuwa Vyuo Vikuu. Kuna haja ya kurejea kila mkoa kuwa na *Technical School* moja na kila Wilaya iwe na VETA kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya na kwa kuanzia tuanze na Kambi za JKT kuweza kuwa VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili ni suala la reli. Tunahitaji kupata tafsiri ya reli ya kati na baadhi ya Wabunge wamezungumza jana hapa na naomba niongezee nguvu tu, kwamba tunapaswa kuwa makini sana kwenye siasa za kikanda. Tusikubali maslahi ya nchi zingine yafunike maslahi ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuanze kwanza kuhakikisha mtandao wa reli ambao utaisaidia nchi yetu ndiyo ambao unakwenda sawasawa. Juzi nilisikia kwamba, tuna tatizo la fedha. Mwaka jana Bunge lilipitisha Sheria ya *Railways Development Levy*, kodi ya maendeleo ya reli ambayo kila mzigo unaoingia nchini, unatozwa asilimia 1.5 kama niko sahihi; naweza nikarekebisha, kwa ajili ya reli. Kwa hiyo, ina maana kwamba tunacho chanzo cha uhakika cha fedha, tunachokihitaji ni kuhakikisha kwamba chanzo hiki kinatumika kwa madhumuni yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba tupate tafsiri ya reli ya kati na kwetu sisi, reli ya kati ni inayotoka Dar es Salaam mpaka Tabora, mpaka Uvinza kwenda Msongati Burundi, kutoka Kaliua kwenda Mpanda mpaka Kalema kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Kalema na kutoka Isaka kwenda Keza, Ngara kwa ajili ya madini ya *nickel* ambayo yamegundulika kule Ngara ili yaweze kusafirishwa kupelekwa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba jambo hili liweze kutazamwa, ni muhimu sana na ni *priority*. Naungana na wote walioongea jana kuhusiana na reli, ya kwamba bila reli na tafsiri hii, hakuna kitakachoendelea katika mfumo mzima wa bajeti ambao unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulipendekeza ni ukurasa wa 29, usafiri wa anga. Namba tatu pale ununuzi wa ndege mpya mbili za Shirika la Ndege la Tanzania. Watu wamezungumzia sana hili, lakini kuna haja, Serikali haiwezi kuwa kila wakati inanunua ndege za *ATCL*, lazima kulifanyia marekebisha Shirika na tunajua na tumewahi kuzungumza huko nyuma, Mheshimiwa Mwakyembe atakuwa anakumbuka maana yake alianza kidogo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wanafaidika na kuwepo kwa Shirika la Ndege. Hawa ni Taasisi zinazohusu utalii, lazima tuzihusishe hizi taasisi ziweze kuhakikisha kwamba zinashiriki katika kuwepo na *national carrier*. Hapa nazungumzia Ngorongoro, *TANAPA*, hawa kutokana na wingi wa watalii wanaoingia nchini wao wanapata mapato. Turuhusu mashirika haya yawe na hisa ndani ya *ATCL* ili kuweza kupata fedha shirika liweze kujiendesha kibiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo siyo kama tunalianza upya, lilishaanza Mheshimiwa Mwakyembe anakumbuka, kuna maelekezo yalitoka, ni kiasi cha Waziri Ndugu Mbarawa kukaa na Msajili wa Hazina, wakubaliane utaratibu ambao unapaswa kuwa ili mashirika yenye ukwasi yaweze kusaidia mashirika ambayo bado yako chini ili tuweze kwenda mbele katika nchi yetu, kwa sababu hatuwezi kuwa tunapanga bajeti ya kununua ndege kila siku. Hizi mbili sawa zitanunuliwa, lakini kuna haja kubwa sana ya kuweza kuangalia huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, maana yake kengele imegonga ambalo ningependa nilichangie ni ukurasa wa 30. Ukurasa wa 30 huduma za fedha namba nne, Serikali inasema inataka kuanzisha Mfuko wa Mzunguko (*Revolving Fund*). Wakati wa kampeni tulisikia, kulikuwa kuna ahadi ya shilingi milioni 50 kila kijiji, naamini kila kijiji na mtaa na leo asubuhi Profesa Muhongo ametupa takwimu ya idadi ya vijiji nchini, 15,209 ndiyo vilivyoko nchini. Ukichukua 50,000,000 *times* idadi ya vijiji unapata zaidi ya shilingi bilioni 750 kwa mwaka ndiyo itakayokuwa ya 50,000,000 ya kila kijiji.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwakumbushe, tulikuwa na mabilioni ya JK, mnakumbuka namna ambavyo yalitumika vibaya, kwa sababu hapakuwa na mfumo mzuri wa namna gani fedha hizi zitatumika. Naomba nishauri, moja ya kipaumbele ambacho Waziri wa Fedha jana amezungumza hapa ni Hifadhi ya Jamii. Naomba niwashauri kwamba, tutumie fedha hizi kama *incentive* ya watu kuwekeza kwa ajili ya *social security*, kwa kufanyaje? Tuweke *incentive* kwamba, raia wetu mmoja akichangia shilingi 20,000/= kuingia kwenye Mfuko wowote ule wa Hifadhi ya Jamii, Serikali imwekee shilingi 10,000/= zinakuwa ni shilingi 30,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idadi ya fedha ambazo zitapatikana, mwanzoni nilikuwa napiga hesabu ya vijiji elfu kumi na mbili, maana yake ni kwamba ndani ya mwaka mmoja, tutakuwa na *one point eight trillion* ambayo iko kwenye *saving* ya *social security* ambayo Serikali mnaweza mkaitumia kwa miradi yoyote mikubwa mnayoitaka. Kwa sababu *social security liability* yake ni *long term*, kwa hiyo mnao uwezo wa kujenga madaraja, mnao uwezo wa kujenga *irrigation schemes* kwa sababu mtu akiingia kwenye mfumo wa *social security now* anakuja kupata yale mafao ya muda mrefu baada ya miaka 15, baada ya miaka 20. Kwa hiyo, naomba jambo hili liangaliwe na nitaliandika vizuri, tuweze kuona ni namna gani ya kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweke mawazo yangu katika hoja ambayo iko mbele yetu. Awali ya

yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa afya njema ili tuendeleo kutekeleza wajibu wetu ambao Watanzania wametukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Jambo la kwanza ambalo Serikali imeona na naomba ninukuu na hili jambo limenishtusha. Ukurasa wa 22 katika kitabu cha Hotuba ya Waziri, anasema kwamba; "Mapato yote yatakusanywa na Wizara ya Fedha, mapato ambayo yanatoka katika Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa watatakiwa kuwasilisha mapato yote yatakayokusanywa yawasilishwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti za mafungu zitakazoidhinishwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni kubwa sana, picha ninayopata hapa Halmashauri zetu zitakufa. Amesema mapato yote na kimsingi ukiangalia tunakwenda kuuwa Serikali za Mitaa. Leo tutakusanya mapato ushuru wa stendi, wa wafanyabiashara, chochote ambacho Halmashauri zetu wanakusanya tuweke kwenye Mfuko wa Serikali. Tukumbuke historia ya ugatuaji madaraka katika Serikali zetu (*decentralization*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1982 Baba wa Taifa alijuta tulivyofuta mfumo mzima wa Serikali za Mitaa; barabara hazikwenda, hospitali zilikuwa mbaya na mwaka 1980 wanakumbuka wale waliosoma historia, kwamba ilifikia hatua hata *outbreak* ya *cholera* ilishindikana kuzuiwa huko chini kwa sababu kila kitu kilifanywa na *central government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi kule ambako Muasisi wa Taifa hili aliona kulikuwa na tatizo na alijutia na akasema hili jambo halitojirudia tena. Serikali hizi za Mitaa wamepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria zetu za mwaka 1982. Wana mamlaka ya kuajiri, mamlaka ya kukusanya mapato na kuyatumia kwa kiasi fulani, lakini wana mamlaka pia ya kutunga sheria mbalimbali ambazo zinasaidia katika kukusanya ushuru huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapotaka pesa zote katika nchi hii tukusanye *at central level*, halafu tutengeneze bajeti zetu huku chini, tupeleke Serikali Kuu wao ndiyo waanze kutupimia, athari yake ni nini? Athari yake tutaua morali ya wale wanaokusanya hizo kodi ndogo ndogo huko chini, kwa sababu maendeleo hayataonekana; kutakuwa na ubaguzi wa kupeleka fedha hizo katika Halmashauri hizo, japo watu wengine wanakusanya, lakini pia hapatakuwa na maendeleo huko chini kwa sababu fedha haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe wakweli; ukiangalia bajeti ya Serikali kwa muda mrefu, fedha za *own source* katika Halmashauri zetu ndiyo zinasaidia miradi ya maendeleo mbalimbali, miradi midogo midogo. Hizo fedha ndiyo

zinasaia kuchonga barabara zetu, lakini angalia fedha zinazotoka Hazina haziendi kwenye Halmashauri zetu kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kwenye bajeti ya mwaka jana, mwaka juzi, hata katika hivi vitabu, inaonyesha fedha za wafadhili ndiyo zinakuja kuliko fedha zinazotoka Hazina. Nitoe mfano, katika Halmashauri yangu ya Mji wa Babati, 11% tu ya fedha za Hazina ndiyo zimeingia na ni miaka yote fedha zinazotoka Serikali Kuu haziingii. Kwa kubariki kila kifanyike *at central level*, huku chini watu wakusanye tu halafu watu wachache wapange, tupeleke sehemu fulani, tusipeleke sehemu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo nakuhakikishia tunaua Halmashauri zetu, hakuna maendeleo yatafanyika, mtafanya mambo yenu makubwa makubwa katika *central level*, lakini yale yanayohusu maslahi ya wananchi wa hali ya chini na maendeleo yao nakuhakikishia tunarudi kwenye historia ya mwaka 1980 ya jinsi ambavyo *decentralization*, Baba wa Taifa Mwalimu aliona kwamba ni jambo muhimu sana kwa sababu *central level* hawawezi kufanya wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imebariki kwamba hizo sheria ziangaliwe, maana yake Sheria inayotajwa ni mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa, kwamba sasa tunachukua uhuru wa Serikali za Mitaa kukusanya kodi zao na kuzifanyia matumizi, Serikali Kuu ndiyo inafanya. Naomba Bunge hili tusithubutu kufanya hivyo, bali tusaidie Serikali za Mitaa kubainisha vyanzo ambavyo hawakusanyi, tuviimarisha na Sheria hizo ziimarishwe badala ya Serikali kuu kuchukua madaraka yote. Sasa tunakusanya kila kitu *at central level*, hatuwezi tukapitisha kitu kama hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa *retention premium* ya ardhi 30%, hizo fedha huwa hazirudi. Tunauza viwanja huko, tunapeleka makusanyo yote ardhi, Wizara ya Ardhi hawapelekewi hizo pesa na Wizara ya Ardhi wao wakipata chochote na wanajitahidi chochote wanachopata kutoka Hazina wao wanapeleka 30% katika hizo Halmashauri, lakini Serikali Kuu, Hazina hawapeleki hizo fedha hata hiyo tu *premium* ya ardhi hawapeleki. Iweje leo tuwapelekee eti fedha zozote tunazokusanya kwenye Halmashauri zetu, tupeleke kwenye Serikali Kuu. Tunaua Halmashauri zetu na maana yake tunaua suala zima la Serikali hizi mbili Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, wanataka sasa kila kitu wafanye wao. Hiki kitu Bunge hili tusifanye vinginevyo maendeleo yatakwama katika Halmashauri zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *service levy*. Wamezungumza hapa ushuru wa huduma na vitu kama hivyo. Kwa muda mrefu tumeishauri Serikali, suala la mitandao ya simu ni chanzo kimojawapo katika Halmashauri zetu. Leo mitandao hii wamiliki wa makampuni haya ya simu ushuru wa huduma

wanaolipa haueleweki kwa sababu Halmashauri imefikia hatua wanakusanya sijui ushuru wa nguzo, sijui *service levy*, hiyo asilimia *zero point three* Wizara ya TAMISEMI mwaka jana na Wizara ya Mawasiliano walikaa chini wakasema watashauriana na wakaandikiana barua kwamba wakusanye katika *central level*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pata picha mpaka leo hawajawahi kukaa, hawajawahi kupeleka kwenye hizo Halmashauri kwamba ni kiasi gani wanastahili kupitia kwa makampuni haya ya simu, hata hilo kama tulishindwa, tunathubutuje leo, eti kwenda kuchukua hata vile vyanzo ambavyo kidogo tunajitahidi Halmashauri zetu zinakusanya, lakini sisi *at central level* kitu ambacho Wizara mbili walitakiwa wakae *wa-reconcile* wapi ambapo haya makampuni hayalipi, halafu zile asilimia zigawanywe zipelekwe kwenye Halmashauri zetu *equally* hawapeleki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaua Halmashauri zetu tunasema tunafanya sisi, wakati ya *premium* ya ardhi mmeshindwa, hii *service levy* mmeshindwa, halafu Serikali Kuu, hivi kweli hiki kiburi kinatoka wapi cha kusema kwamba, sasa ninyi mnakusanya, halafu mtugawie sisi tuwaletee tu bajeti. Hili ni jambo kubwa sana na ninaona kama hatujalipitia na hatujalielewa vizuri, lakini kama tukipitisha jambo hili ambalo linapendekezwa katika ukurasa wa 22, tumeua Serikali zetu za Mitaa *totally*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize sana kuhusu hili tusilipitiche na tuliangalie kwa upya, lakini suala zima la kurasimisha biashara zetu ni kwa nini sijaona Mpango unaoonesha vijana wetu ambao wanafanya biashara ndogo ndogo waweze kuboreshewa maeneo yao. Kwa muda mrefu hata kwenye Hotuba ya Rais alizungumzia suala zima la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara kwa vijana wetu, Wamachinga. Hawa wakipangwa pesa zikatengwa, zikajengwa *shopping malls* ambazo zitasaidia vijana wetu tukawapanga, watalipa ushuru katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea leo, hawa wafanyabiashara wanaokuwa taratibu, hawajawahi kupangwa kokote, hawajawahi kutengewa maeneo, lakini kingekuwa ni chanzo kizuri ambacho tukakaa tukawaangalia jinsi gani Serikali za Mitaa wakapanga maeneo kwa ajili ya hawa vijana, wakafanya biashara wakalipa ushuru mbalimbali na tozo mbalimbali, itasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali. Kwa hiyo, nishauri kwamba inawezekana Serikali inawaza mambo makubwa, bandari, sijui ndege, sijui vitu gani wakati kuna watu ambao wakipangwa tu wanaweza wakasaidia kuleta marejesho katika Mfuko wetu na katika Halmashauri zetu ili tuone ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukafanya maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaweza vikaajiri hawa vijana, limezungumziwa lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Nachingwea kwa imani kubwa ambayo wameionyesha kwangu ili niweze kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda naomba nijielekeze katika kuchangia Mpango huu, kwanza, kwa kuwapongeza watu wa Wizara wakisaidiwa au wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo wamewasilisha Mpango huu ambao umekuwa na mwelekeo wa kutaka kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kabla ya yote, nomba niunge mkono wale ambao wametangulia kusema kwamba hatuwezi kutekeleza Mpango huu kama hatuwezi kujielekeza katika kufanya makusanyo mazuri katika kodi, lakini pia katika kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo vitatuwezesha kutimiza malengo ambayo tumejiwekea. Mengi yameshasemwa lakini Mipango mingi imeshapangwa kwa kipindi cha nyuma ambacho sisi tumekuwa nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ubunifu wa ukusanyaji wa mapato yetu. Nimeupitia Mpango huu vizuri sana, yako maeneo ambayo nafikiri wenzetu wa Wizara wakisaidiana na wadau mbalimbali wanatakiwa kuendelea sasa kujifunza kutoka katika maeneo mbalimbali ili tuweze kukusanya kodi kwa uhakika tuweze kutimiza malengo ya Mpango wetu. Pia Mheshimiwa Waziri nikuombe tuendeleo kutumia wataalam wetu mbalimbali hata walio nje ya Wizara ili waweze nao pia kutoa mawazo ambayo yatasaidia katika kukamilisha Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo ningependa nijielekeze kama ambavyo malengo ya Mpango wetu yanavyozungumza. Kuna eneo la viwanda na Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza katika kuimarisha viwanda. Kwa sisi ambao tumetoka Mikoa ya Kusini kwa maana ya Lindi na Mtwara, tumekuwa ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya biashara; tuna korosho, tuna ufuta na sasa hivi tuna mbaazi. Hatuwezi kujadili kujenga uchumi mkubwa wa

nchi yetu kama hatuwezi kujadili namna ya kuwaimarisha na kuwaendeleza wananchi katika ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wilaya ya Nachingwea inavyo viwanda vikubwa viwili ambavyo vimebinafsishwa. Tuna Kiwanda cha Korosho pale Nachingwea na tuna kiwanda cha kukamua mafuta, vyote wamepewa wawekezaji na viwanda hivi vimeshindwa kuendelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri, tunamwomba Rais wetu katika ari hii aliyoanza nayo, hivi viwanda nafikiri kuna kila sababu ya kwenda kuviangalia na tuweze kuvirudisha ili viweze kwanza kutoa ajira kwa wananchi wanaozunguka maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuweze kuimarisha upatikanaji wa huduma ili tuweze kuandaa mazao yetu wenyewe katika maeneo haya ya kuanzia ngazi za chini. kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunapojadili viwanda viko viwanda ambavyo tayari hatuhitaji kufanya kazi kubwa ili tuweze kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia, ni suala zima la miundombinu, Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara kwa kutoa hizi malighafi ambazo nimezizungumza ambazo tunahitaji kujenga viwanda bado tumekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano na hasa katika eneo la barabara. Leo tunajadili Mkoa kama wa Lindi bado hatujafikia hatua ya kuweza kuunganisha kupata mawasiliano ya uhakika. Bado tuna tatizo la barabara sasa hatuwezi kufikiria kufanya mambo makubwa wakati bado wananchi wetu wanaendelea kupata shida ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo toka nimepata akili mpaka leo bado zinazungumzwa na bado hazijafanyiwa kazi. Tuna barabara ya Nanganga - Nachingwea, tuna barabara ya Masasi – Nachingwea, bado tunahitaji barabara hizi zijengwe kwa kiwango cha lami. Pia tunahitaji tujengewe barabara ya kutoka Nachingwea kwenda Liwale na haya ndiyo maeneo ambayo yanazalisha kwa sehemu kubwa mazao ya biashara ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji pia barabara ya kutoka Nachingwea - Ruangwa na barabara zile zinazounganisha Mkoa wa Lindi pamoja na Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Ruvuma. Haya yote ni maeneo ya kiuchumi ambayo kwenye Mpango huu lazima tujielekeze kwenye bajeti yetu tuone maeneo haya yanapata huduma muhimu ili tuweze kufikia malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa pia kuchangia, ambalo pia nimepitia katika huu Mpango ni eneo la nishati na madini. Tunayo changamoto, naomba niungane na wenzangu kumpongeza Waziri ambaye anashughulika na eneo hili Profesa Muhongo, iko kazi kubwa

naomba nikiri kwamba imefanyika na inaendelea kufanyika, lakini bado tunazo changamoto ambazo tungependa kushauri Serikali yetu iongeze jitihada. Leo maeneo mengi ya vijiji vyetu yanapata umeme, lakini tungependa speed iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Muhongo, wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ndiyo sasa hivi wanatoa gesi ambayo tunaitumia Tanzania nzima. Ni vizuri sasa mipango hii ambayo tunakwenda kuipanga, tuanze kunufaika watu wa maeneo haya ili wananchi wetu waweze kujikwamua na kupata uchumi ambao tunaukusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulisemea ni katika upande wa madini. Mkoa wa Lindi na Mtwara bado ziko fursa nyingine ambazo ningependa kuishauri Serikali ijielekeze kufanya utafiti. Sasa hivi Wilaya kwa mfano ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi sehemu kubwa ina madini. Madini ambayo bado hayajatumika, madini ambayo bado Serikali haijatangulia kwamba yanaweza yakakuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo madini maeneo ya Nditi, Kilimarondo na Marambo, haya ni maeneo ambayo nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima, aelekeza wataalam wake waje tutawapa ushirikiano ili waweze kufanya utafiti wa kutosha tuweze kupata madini mengi zaidi ambayo yatalisaidia Taifa letu na pia yatasaidia wananchi wanaozunguka maeneo haya, kwa maana ya kuwapatia ajira na kukuza kipato cha Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni eneo la elimu. Nimepitia vizuri huu Mpango, naomba niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Naomba nimpogeze kwa upekee kabisa Rais wetu mpendwa aliyepita Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Iko kazi kubwa ameifanya ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inatakiwa kuiendeleza. Leo hii nimezunguka ndani ya Jimbo langu Kata zote 32, changamoto kubwa ambayo tunakutana nayo ni ukosefu na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliona hili Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alianzisha kwa makusudi jitihada za ujenzi wa maabara. Maabara hizi sasa hivi zimesimama, hazina msukumo; nilifikiri lengo lake lilikuwa ni zuri. Sasa kupitia Mpango huu naomba kwenye bajeti tunayokwenda kuipitisha, maabara hizi sasa tuzitoe mikononi mwa wananchi kwa sababu wamechangia nguvu zao kwa sehemu kubwa, badala yake Serikali ichukue kwa maana iliahidi itatoa vifaa, itamalizia majengo haya ambayo tayari tumeshayajenga ili tuweze kuzungusha tupate Walimu ambao watakwenda kufundisha kwenye shule zetu na tutapata wasomi wazuri wa masomo ya sayansi ambayo watasaidia katika

kada nyingi ambazo tumekuwa na tatizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili niliona ni pendekezo ambalo nalo pia ningependa kulizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la afya. Bado kwenye Mpango hatujaeleza ni namna gani Serikali imejipanga kusaidia kuona namna gani tunajenga vyuo vingi zaidi ili tupate wataalam. Leo hii hospitali zetu, zahanati zetu zina matatizo makubwa ya wataalam. Hii tutaipatia majibu kwa kutengeneza mkakati wa kusomesha wasomi wengi zaidi ambao watakwenda kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, ni eneo hili la uchumi kwa maana ya Mawaziri wetu ambao wamechaguliwa na Mheshimiwa Rais wetu, msaidieni Rais wetu, Rais wetu ameanza vizuri anafanya kazi nzuri. Naomba niwasihi Mawaziri wetu fanyeni kazi, sisi tuko nyuma yenu, tunaahidi kuwapa ushirikiano, lengo letu ni kuwakwamua Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe katika eneo la kilimo, naomba nitoe pongezi pia kwa Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. Ipo changamoto ambayo nimeiona, ambayo ningependa kuishauri Serikali yangu. Kuna eneo la umwagiliaji, utengenezaji wa miundombinu, pesa nyingi inatengwa kwenda huko, lakini miradi mingi inahujumiwa huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watu wa Kanda, kaka yangu Mwigulu yupo hapa ndani, namwomba afuatilie hili eneo. Pesa nyingi inapotea, miradi mingi ya umwagiliaji haifanyi kazi, nenda Nachingwea, upo mradi mkubwa pale Matekwe ambao ungeweza kunufaisha Watanzania, pesa yote imepotea, hakuna mradi uliokamilika. Nimewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, miradi mingi ya umwagiliaji ni hewa, pesa ukienda inasimamiwa na watu wa Kanda. Naomba Mheshimiwa Waziri fuatilia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la pembejeo, nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Pembejeo, pesa nyingi ya pembejeo Mheshimiwa Waziri inapotea katika eneo hili. Malengo ya Serikali ni mazuri, lakini pesa hii hakuna mtu wa kumwamini sasa hivi. Naomba Serikali kupitia Wizara Fedha, kupitia Wizara ya Kilimo ifuatilie kwa karibu eneo hili. Tulete mapendekezo mazuri yatakayosaidia ili wananchi wetu kweli wanufaike kwa kupata pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba nishukuru, lakini pia naomba niunge mkono hoja juu ya Mapendekezo ya Mpango huu ambao lengo lake ni kuwasaidia Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa

kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na wananchi wa nchi hii na pia Baraza la Mawaziri na viongozi wengine wote ambao wamepewa dhamana ya kuiongoza nchi hii, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niupongeze Uongozi wa Bunge, nikitambua kabisa kwamba kazi kubwa tuliyonayo ya Bunge hili ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Kama kazi yetu ni kuisimamia Serikali na kuishauri, maana yake kama mambo yatakuwa hayaendi vizuri, basi Bunge hili haliwezi kukwepa wajibu kwamba hatujafanya kazi yetu vizuri ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuruni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba sasa tumepata viongozi wazuri wanaoweza kuikokota na kuisukuma nchi yetu ikafika kuwa nchi ya kipato cha kati. Kwa muda mrefu tulikuwa tunatafuta viongozi, tulikuwa tunatafuta Rais ambaye ana maono ya mbali, sasa Mungu ametupa uwezo, tumebahatika tumepata Rais mwenye maono ya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni tajiri sana kwa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba, ambayo imejaa karibu kila kona. Tuna madini ya kila namna, tuna misitu, tuna mlima mrefu kuliko milima yote katika Afrika na wa pili duniani kwa urefu, tuna mbuga nyingi za wanyama, mito, maziwa, bahari na zaidi ya hapo tuna watu zaidi ya milioni 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *competitive advantage* ambayo tunayo. Kwa maana hiyo, tuna vitu vingi vinavyoweza kuiwezesha nchi yetu kuendelea na kufika kuwa nchi ya kipato cha kati. Sasa tatizo kwa muda mrefu limekuwa ni nini? Tatizo kubwa ni tatizo la uongozi na hili ndio limekuwa likitusumbua sana. Sasa wakati huu tumepata viongozi, nadhani tutaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta Mpango huu na kueleza dira na kuonekana mambo ambayo tunaweza kuyafanya. Mpango huu umezingatia dira ya Taifa na pia umezingatia Hotuba ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba nichangie katika eneo la kilimo. Katika Mpango huu kilimo bado hakijapewa nafasi nzuri sana na hakijapewa mkazo kama ambavyo kingekuwa kimepewa. Sisi kule Wanavwawa ni wakulima, wananchi wa Vwawa wanalima sana, tunalima kahawa kwa wingi, mahindi, tunalima mazao mengi na tunaamini kabisa kama

Serikali itatuwekea misingi mizuri, ikatupatia pembejeo kwa wakati, tuna uwezo wa kuzalisha chakula kwa kingi ambacho kinaweza kikatumika sehemu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe wazo kwamba tuiseme mazao ya biashara, sasa kila zao ni zao la biashara, hata mahindi ni zao la biashara, hata maharage ni zao la biashara. Kwa hiyo, mazao yote yanayoweza kulimwa yapewe uzito unaostahili ili tuweze kuzalisha chakula kingi, tuweze kuzalisha kwa ajili ya kuuza sehemu zinginezo. Kwa hiyo, kilimo ni muhimu sana tukakipa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, ambayo ningependa nichangie, tumezungumzia viwanda, kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itakuwa ni Serikali ya viwanda. Hata hivyo, viwanda ambavyo tumesema, nimesoma kwenye huu Mpango hatujaainisha, tunataka viwanda vingapi na viwe wapi? Hilo hatujalisema, lakini pia tulikuwa na viwanda vingi sana ambavyo vilijengwa katika nchi hii, nini kilitokea viwanda hivyo vyote vikafa? Tulikuwa na mikakati mingi ambayo tuliweka juu ya viwanda, tumejifunza nini katika mipango yote tuliyokuwa nayo katika kujenga viwanda vilivyopita? Sasa haya yanatakiwa yawe ni msingi mzuri wa kutuwezesha kuweka mikakati mizuri ya kuweza kujenga viwanda tunavyovihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ili tuweze kwenda sambamba kufika kwenye hiyo nchi ya viwanda, tunahitaji viwezesha, vitu vitakavyotuwezesha kufika huko, tunahitaji umeme, barabara na vitu vingine vingi. Sasa naomba nichangie kwenye suala la umeme; umeme wa REA umesambazwa nchi nzima katika vijiji vingi sana. Katika Jimbo langu kule watu wengi wamepata, lakini vijiji vingi bado havina umeme. Kuna Vijiji kama Nanyara, Nswiga, Irabii umeme unapita juu kwa miaka mingi, unawaruka wananchi unakwenda wapi, wananchi wale wanahitaji wapate ule umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kwamba umeme ni muhimu sana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameona kule kuna joto ardhi, kule kuna chanzo kizuri sana cha kuweza kuzalisha umeme. Naomba mkazo uwepo katika kuanzisha na kutumia nishati hii inayotokana na joto ardhi ambayo inaweza ikatusaidia sana kutukwamua katika suala hili la umeme ambalo ni muhimu sana katika kuipeleka nchi kuwa nchi ya kipato cha kati.

Suala lingine ambalo ningependa kuchangia, ili tuweze kuwa nchi ya kipato cha kati, tunahitaji wataalam wetu, tunahitaji watu wawe na ujuzi wa kuweza kufanya kazi na kuweza kutekeleza majukumu yetu. Sasa hivi vyuo vyetu tulivyonavyo na mfumo wa elimu tulionao, hauwaandai vijana kuweza kupata ujuzi unaohitajika sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunayo kazi kubwa ambayo napenda nishauri, Wizara ya Elimu tutafakari kwa undani mitaala tuliyonayo inatuandaa, inawaandaa vijana wetu kwenda kuwa nchi ya kipato cha kati? Sasa hivi mkazo utatiliwa kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu. Naomba nishauri, lazima tuwe na vyuo vingi vinavyotoa elimu ya kati *tertiary institutions* ambazo zitatoa wataalam watakaoweza kushiriki kufanya kazi katika viwanda tunavyovihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye upande wa elimu, ningependa mitaala ile wakati inaandaliwa, iandaliwe vizuri, iwe ni *demand driven rather than supply driven*, halafu wapatiwe sehemu za kwenda kufanya *field* ili waweze kuiva na kukomaa hilo litatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba nishauri mambo mengine yafuatayo:-

Kwanza, ili tuweze kufika na kutekeleza mpango huu ambao ni mzuri, nashauri, lazima tuweke nguvu sana katika ukusanyaji wa mapato, bila kukusanya mapato huu Mpango utakuwa hautekelezeki. Sasa hivi lazima tuweke mkakati wa kutosha wa kuhakikisha kwamba nchi inajitegemea kimapato kuliko kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tubadilike kifikra ili watu watambue kwamba wajibu wa maendeleo ya nchi hii ni sisi wenyewe ndiyo tutakaoleta maendeleo, ni wananchi wa nchi hii ndiyo watakaoleta maendeleo na si mtu mwingine.

La tatu, naomba kushauri, tumekuwa tukiimba kila wakati kwamba huko vijijini wananchi wanahitaji huduma za fedha, bila kupeleka huduma za fedha, bila kuanzisha hizi *micro-institutions* za kuweza kuwa-*support* wakulima, ku-*support* watu mbalimbali huko vijijini, ku-*support* vikundi mbalimbali, hatuwezi kuleta maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri tuimarisha huduma za fedha mpaka vijijini ili wananchi wetu waweze kupata mikopo mbalimbali na kugharamia vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni vipaumbele, tunahitaji tuwe na vipaumbele vichache, ambavyo vitagharamiwa na Serikali. Viwanda naamini vitagharamiwa vitakuwa vinaendeshwa na watu binafsi siyo Serikali tena. Sitegemei kuona Serikali inaweka mkono mkubwa wa kuendesha viwanda wakati uwezo wetu ni mdogo, labda viwanda vile ambavyo ni *strategic*, lakini viwanda vitaendeshwa na *private sector*. Katika maeneo ya elimu, kilimo, uvuvi

na ufugaji, afya na maji, miundombinu, barabara, viwanja vya ndege, umeme; hivyo Serikali lazima iwekeze vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nishauri tumezungumzia sana kwamba tunahitaji viongozi ili waweze kuisukuma nchi hii. Hata hivyo, katika nchi hii hatuna utaratibu wa kuandaa viongozi, wala wa kuwafundisha, wala kuwaelekeza namna ya kutekeleza majukumu yao.

Sasa umefika wakati tuwe na mfumo mzuri wa kutambua viongozi wazuri na kuwaendeleza na kutambua vipaji vyao ili wakabidhiwe kufuatana na uwezo walionao. Hilo litatusaidia kuwa na viongozi wanaoweza kujenga, wazalendo wenye uwezo wa kuleta maendeleo ya kweli katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana na pia naomba Serikali izingatie mawazo yetu. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuleta haya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017. Wamejitahidi sana kuweza kuoanisha na nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango na timu yake kwa kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu Mpango naomba nichangie maeneo machache kwa sababu ya muda. Jambo la kwanza ambalo ningependa nishauri, ili tuweze kuwa na maendeleo katika huu mwaka mmoja, tuendeleo kupunguza urasimu uliopo katika maeneo mbalimbali, ambayo ndiyo yanaongeza kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo imeshaanza kufanyika bandarini, TRA na kwenye border zetu kama Tunduma, Kyela, Namanga kote huko tuendeleo kufanyia kazi. Pia Mamlaka husika kama ya mazingira na yenyewe pia iendeleo kuangalia muda ambao wana-process vibali mpaka mtu anapata kuweza kufanya shughuli ambayo ameiomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie eneo lingine ambalo ni suala zima la uchumi. Ili uchumi uweze kukua kuna vigezo mbalimbali, lakini kuna michango ambayo inachangia kukua kwa uchumi na vipato vyetu. Tumeangalia kipato kimekuwa mpaka kimefikia shilingi 1,700,000/=, ni hatua nzuri ya kuonesha kwamba uchumi umekuwa, lakini kuna sekta hambazo hazikufanya vizuri katika kipindi kilichopita na hasa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kufikia 3.4%, na lengo lilikuwa ni 6% na upande wa kilimo ndio eneo ambalo limeajiri zaidi ya watu 70%. Sasa tunaomba kwenye huu Mpango wa mwaka mmoja 2016/2017 na katika bajeti, Serikali iangalie matatizo yaliyojiri, tukafikia 3.4%, badala ya 6% na iweze

kurekebisha na hasa ni katika fursa mbalimbali na pembejeo ambazo wakulima hawapati ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika Mpango huu tumezungumzia kuboresha fursa upande wa viwanda, lakini hatujagusa upande wa viwanda vidogo vidogo. Sehemu kubwa ambayo naiona bado elimu ya ujasiriamali kwa watu wetu haijafika ipasavyo na wafanyakazi wa Halmashauri hasa Maafisa Biashara, wanatakiwa waifanye kazi hiyo ili watu wetu wajue na wapate hizo fursa za kufungua biashara ndogo ndogo na hizi ziendane kutokana na maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, katika kuongeza mapato, ni Taasisi za Serikali, zamani tuliona Jeshi la Magereza likiwa ni mojawapo likijishughulisha na uzalishaji, mazao ya biashara na mazao ya chakula. Hata hivyo, sehemu nyingi sana sasa hivi za Magereza hayazalishi, sasa tatizo liko wapi? Liangaliwe na wenyewe waingie katika kuchangia kwenye pato, tunawagharamia sana Magereza lakini uingizaji ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mapato na kukuza uchumi na swali leo limeulizwa na Mheshimiwa Risala ni utalii, mbuga ya Katavi, Ruaha, Udzungwa, Mikumi ni sehemu ambazo haziangaliwi na kupewa kipaumbele. Matatizo ambayo yameoneshwa tunaomba Serikali kupitia Wizara zake, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa pamoja ziangalie kwenye bajeti hii ya mwaka 2016/2017, kuboresha miundombinu ambayo inakwenda kwenye hizi mbuga ili tuweze kuongeza kipato, pamoja na kuzitangaza. Kwa hiyo, tunaingia gharama lakini Serikali itaingiza fedha kwa kupitia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine napenda niizungumzie tena, ni kuhusu mashirika ya umma. Tumekuwa na mashirika ya umma ambayo yanaendelea kuitia hasara Serikali, hayajiendeshi kibiashara. Namuunga mkono Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Zitto, suala la *Air Tanzania* liangaliwe, *retrenchment* ifanyike, watu waingie kwenye mikataba ya ajira mipya, wapunguzwe wafanyakazi na tuweze kwenda kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na yote tunayozungumza hapa, lazima turejee kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tuone kitu gani ambacho kimeandikwa na tuangalie utekelezaji. Katika ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeahidi kutengeneza reli katika kiwango cha Kimataifa, *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, katika haya mapendekezo gharama za upembuzi yakinifu, reli mpya kuanzia Mpanda kwenda Kalema na kukarabati kuanzia Kaliua mpaka Mpanda, iingie na iwemo

na reli ya kuanzia Uvinza kwenda Burundi na yenyewe iingie iwemo katika upembuzi yakinifu kwa mwaka huu 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu tayari nchi ya Burundi ina uhitaji wa haraka na wenzetu wa Kongo na wenyewe kwa habari ambazo sina hakika wameshaanza kutengeneza reli ya kuja Ziwa Tanganyika ili mizigo ipitie Kalema. Sasa sisi kwa upande watu tuanze kazi haraka iwezekanavyo na tunamwomba Mheshimiwa Waziri iingie katika bajeti hii, huu upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ripoti ya miaka mitano iliyopita ya maendeleo, tulisema tutajenga reli kilometa 2,707. Mwaka huu wa mwisho tulisema tutajenga kilometa 197, lakini tumeweza kujenga kilometa 150. Tuangalie ni wapi tulikwama, tatizo ni fedha au tatizo ni utawala? Tunaomba reli yetu ya kati iwekewe kipaumbele, iweze kutengenezwa katika kiwango cha Kimataifa na ili tuweze kuingiza mapato kutokana na mizigo ya ndani pamoja na mizigo ya nchi jirani. Hilo nalo iingie katika huu mwaka 2016/2017 na lionyeshwe kwa kutajwa kilometa zitakazotengenezwa na maeneo wapi mpaka wapi na isiwe tu nadharia inayotaja idadi bila kujua na maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kwenye suala zima la elimu. Tumeelezwa kwamba kutokana na mafunzo ya kiujumla kusomesha watu, lakini kuna Kanda nyingine hakuna Vyuo Vikuu. Tanzania ukanda wa Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa ukanda ule pia hakuna Vyuo Vikuu. Sasa katika kugawa rasilimali kijografia na yenyewe tuangalie tuweze kupata Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niongezee katika suala zima la miundombinu. Tumeeleza fursa Tanzania ni nyingi na lazima kuwe na viwezeshi, kiwezeshi kimojawapo pia ni kuboresha miundombinu ili wawekezaji waweze kufika. Hata hivyo, katika sehemu nyingi barabara hatuna na hasa Mkoa wa Katavi. Tuna fursa nyingi, tuna madini, gesi, mafuta, lakini barabara hakuna. Barabara ya kuunganisha kutoka Uvinza kuja Mpanda tunaomba ianze na iingie kwenye bajeti hii na pia tuweze kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii na naunga mkono na naomba yote niliyopendekeza yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyenijalia kunipatia afya njema inayoniwezesha kuchangia katika hoja iliyokuwepo mezani. Napenda kukishukuru Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kuniona kuwa nina uwezo wa kulitumikia Taifa hili na kunipa nafasi ya Ubunge wa Viti Maalum na sasa hivi nipo katika Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumshukuru Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad kwa juhudi zake anazozifanya, Mwenyezi Mungu atamjalia na atampa haki yake iliyokuwepo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunipa afya njema na leo nitajaribu kuchangia katika hoja iliyokuwa mezani hasa katika upande wa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuliingia katika uwekezaji kwa nguvu zote tukitegemea uwekezaji utatupa faraja kubwa na kuinua kipato cha nchi yetu. Tunazungumzia kipato cha 7.3%, lakini hiki ni kipato cha watu waliokuwa na uwezo wa hali ya juu. Ukienda kuangalia uhalisia huko vijijini watu ni maskini wa kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Tanzania tutaweza kukusanya mapato ya trilioni 14, hii ni pesa ndogo sana. Hizi pesa kuna wafanyabiashara sasa hivi wanazo, wameingia katika soko la dunia na kuonekana wao ni matajiri wakubwa, wana uwezo wa kuwa na trilioni 26, Serikali tukiwa na trilioni 14 kwa maana moja tumezongwa, tumekamatwa na wafanyabiashara wao ndio wataitawala nchi, hii Serikali itakuwa haina uwezo wa kuweza kujitambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia katika uwekezaji, tumeingia katika uwekezaji lakini tulisema tulikuwa na malengo, *goals, strategic, commitment, transparent, implementation, monitoring and evaluation, corruption*, tumekwama wapi? Tafiti zote hizi zilifanywa na tukasema sasa hivi Tanzania uchumi wetu utakuwa mkubwa mpaka nchi nyingine kama Rwanda uchumi wao unakuwa kwa kasi sisi tupo nyuma pamoja na kuwa na *resources* zote ambazo tunazo. Tunataka tuseme kwamba tumekwama kwanza hatupo katika usimamizi uliokuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *corruption* imesimama kwa hali ya juu, baadhi ya viongozi wanaosaini mikataba wanaangalia matumbo yao, siyo kuangalia nchi inafanya nini. Usimamizi na ufuatiliaji wa miradi, Sekta ya Uwekezaji imeingia katika kila sekta kwa mfano, ukienda katika madini kuna uwekezaji bado hatujafanya vizuri; ukienda katika kilimo kuna uwekezaji, bado hatujafanya vizuri; ukienda katika viwanda na biashara kuna uwekezaji, bado hatujafanya vizuri; tumekwama wapi? Tusilizungumzie pato la asilimia 7, hakuna kitu hapo ni uchumi mdogo sana kwa Mtanzania na Watanzania tunakua, tunahitaji maendeleo, watoto wapate elimu na sisi wenyewe tuwe na maisha bora, lakini maisha bora kama hatujaweza kuangalia usimamizi huu tuliokuwa nao, tutakuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala la utalii, utalii unaingiza kipato cha nje (*in forex*), lakini leo utalii unaingiza asilimia 22.7, mianya ni mikubwa katika uwekezaji. Wawekezaji ambao wapo ndani ya utalii, ndani ya mbuga zetu hawataki kuchangia hata *concession fee*. Tunajiuliza usimamizi uko wapi? Kama wale watu wanapata nafasi yote, TANAPA inajenga barabara, Ngorongoro inajenga barabara na mazingira yote ya kuwapelekea maendeleo wale watu, lakini hakuna pesa wanazotoa. Matokeo yake tumekwama katika usimamizi, tungepata mapato makubwa kama tungekuwa tunasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Selous ambayo ni mbuga kubwa ya kwanza duniani, lakini haina kipato. Wawekezaji kule ni ujangili kwa kwenda mbele na hata hao watu wanaokamatwa, leo tunaona watu wanakamatwa na meno ya tembo 30,000, lakini hatujapata taarifa yoyote humu ndani ya Bunge. Mtu anakamatwa na pembe 30,000 ina maana ameua tembo 15,000 amefanywa nini, usimamizi upo wapi, mapato ya Taifa yapo wapi, tunaiacha nchi inaangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na wanyamapori na misitu hakuna mapato yatakayopatikana ndani ya utalii. Utalii watu wanakuja kuangalia mazingira yetu tuliyokuwa nayo, iwe wanyama, na misitu yetu. Leo misitu inakatwa kama hatumo humu ndani, kuna Mtendaji wa Kijiji, kuna DC, kuna Mkuu wa Mkoa na watendaji wengine wanafanya nini kuhakikisha misitu inaimarishwa? Tembo atajificha wapi, faru atajificha wapi na simba atajificha wapi misitu yote inaangamia, mkaa kwa kwenda mbele, njia za panya zinaachwa, lakini viongozi wanahusika. Tunataka Serikali itupe tamko je, hali hii ya kuhakikisha utalii unakufa itaisha lini? Tunaona katika TV sasa hivi mpaka kobe, kasa wanatoka wanakwenda nje, sura pana wamekuja kuleta fujo ndani ya nchi hii, lakini tunawafanya nini sura pana? Hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika viwanda, wamechukua viwanda vyote wawekezaji vikiwemo Viwanda vya Korosho, Viwanda vya Mafuta, Viwanda vya Ngozi, lakini sijasikia viwanda vile kwa miaka 20 vikifanya kazi na Serikali ipo humu ndani, Mawaziri wapo humu ndani, watendaji wapo wanasimamia nini. Nenda Nachingwea kile kiwanda, ni ghala la kuweka mbao na majangili kuweka mapembe ndani ya vile viwanda, nani anafuatilia hivyo vitu? Nenda viwanda vya Mtama vya Korosho havifanyi kazi, Mtwara havifanyi kazi, Mbagala havifanyi kazi, halafu tunasema tunataka tupate uchumi endelevu, tutaupataje huo uchumi kama hakuna usimamizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe makini katika kusimamia, tufuatilie, tuachane na *corruption*. *Corruption* imekuwa ni donda ndugu ndani ya nchi hii. Hatujitambui, tumeachia uchumi tunaosema tuna uchumi, lakini uchumi huu ni kwa wageni, siyo Mtanzania halisia, nenda vijijini hakuna uchumi huo tunaozungumza hapa. Tusidanganye watu, tujipange katika uchumi ambao

utamgusa mwananchi kijijini, siyo uchumi unawagusa watu waliopo Dar es Salaam na maghorofa. Maghorofa yale siyo ya Watanzania yale maghorofa ni ya wawekezaji ambao wanakwepa ushuru, wanakwepa kulipa kodi halafu tunajumuisha kuonekana Tanzania kuna uchumi wakati hakuna uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kuzungumzia suala la ajira na uwekezaji. Kwa vile hatusimamii humu ndani tumewahi kuuliza kwa Waziri, leo tunaona Wachina wanauza karanga Kariakoo, katika majumba ma-godown Wahindi wamejaa mle, wanatoka India kuja kufanya kazi za vibarua, je, Mtanzania atapata wapi ajira? Hakuna ajira kwa Watanzania, Watanzania hawana ajira, ina maana uchumi wa Tanzania unahamishwa kupelekwa kwa wageni. Tumejipanga kwa hilo, tunajiuliza maswali kama hayo kwa kujua, je, kama sisi Watanzania wazalendo tunajiangalia vipi. Tumeuhamisha uchumi tunaupeleka kwa wageni, lakini tumekaa hapa tunasema tunapanga mipango mipango, kila baada ya miaka mitano mipango, tunarudi nyuma katika enzi ya ujima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika upande wa kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo, lakini jiulize kila mwaka Tanzania kuna njaa. Hivi kweli kilimo kwanza kimemsaidia Mtanzania? Hakijamsaidia Mtanzania. Leo unampelekea Mtanzania kilo tano za mahindi, ana watoto, wajukuu, familia kubwa je, kilo tano alizopelekewa zitamsaidia nini Mtanzania yule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mahali unajiuliza, mvua kama hivi sasa hivi ya kutosha ipo Serikali imetoa juhudi gani kuwapelekea wananchi pembejeo, Serikali imetumia juhudi gani kuwapelekea wananchi mbegu iwe za mahindi, ufuta au karanga, hakuna, lakini utasikia mwakani tunaomba msaada wa chakula. Hii inatokana na sababu kwamba, hamjazisimamia sekta ya kilimo, mnawafanya wananchi wanahangaika na hata pale anapoweza kulima, akapata mazao yake, hakuna soko kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima ni kundi ambalo wamekuwa watu wa kutangatanga wakitafuta soko; inapofika wakati wa mazao, wanakuja wababaishaji kuja kuchukua mazao yao kwa bei ya kutupa. Mazao yale wanayapeleka nchi za kigeni kuwa kama *raw material*, nchi haifaidiki hata na mazao yetu. Tanzania hata mchele tunapeleka nje, tunaletewa michele mibovu, Tanzania tunatoa mbegu za alizeti, lakini tunaletewa mafuta mabovu kutoka Ulaya kwa nini. Ndiyo maana sasa hivi Tanzania tuna kasi kubwa ya kansa, tunakula mafuta mabovu, lakini je, viwanda vyetu vinafanya nini, tulikuwa na viwanda vya kusindika mbegu na kupata mafuta Mwanza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lulida muda wako umekwisha.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye Mpango uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kuendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kaliua kuendelea kuniamini kuwa mtumishi wao na kunipa tena fursa ya kuweza kuwepo ndani ya chombo hiki cha uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hiki nimekipenda sana kwa kuwa kina Mipango mizuri kweli kweli, tena sana. Nina imani kabisa kama itakwenda kutekelezwa vizuri nchi yetu itapiga hatua kubwa sana. Wasiwasi wangu ni wale wanaokwenda kutekeleza, juzi nilichangia kwa ufupi, tuna shida kubwa ya watendaji wa nchi yetu. Tumekuwa na *gap* kubwa, watu hawafanyi kazi kwa kuwajibika, hii Mipango yote haiendi kufanywa na *robot*, inakwenda kutekelezwa na watu kwa kutumia *brain* zao, mikono yao na akili Mungu alizowapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye kitabu, kwenye mradi mmojawapo mkubwa ni kusomesha vijana wengi kwa mkupuo katika fani mbalimbali. Sijaona Mpango gani wa kwenda kubadili *mindset* za watendaji wa nchi hii na vijana wetu wakasome, wakielewa wanakwenda kusoma kwa ajili ya kwenda kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida kubwa kama Serikali haitaangalia hili, Mipango yote hii iliyopo huku haina watekelezaji. Kwa hiyo, shida kubwa namna gani kwenye mipango yao ya kawaida ya Serikali lazima waliopo kazini, wanaoingia, waliopo mashuleni wakajengewe uwezo namna gani ya kujituma, namna gani ya kuwajibika, namna gani ya kujipima na kwenda kutekeleza miradi ya Kitaifa ambayo ipo kwenye mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze suala kubwa tulilionalo ni suala la maji, tena niseme kwa uchungu mkubwa. Nchi yetu ina shida kubwa sana ya tatizo la maji na ni tatizo ambalo linawatesa watu, nina maumivu makubwa na zaidi kabisa kwa kina mama na watoto. Kina mama wengi wanakosa hata fursa za kuhudumia familia kwa sababu ya maji, lakini watoto wengi na hasa wa kike wanakwenda kufuata maji wanakosa hata muda wa vipindi kwenye madarasa wanachelewa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa miradi ya maji, nimesoma mingi huku, ninavyosikia Serikali inasema kwamba tutaendelea na utaratibu wa maji

vijijini, ndiyo hadithi miaka yote. Nimekaa ndani ya Bunge hili miaka 10 tunaambiwa miradi ya maji, miradi ya *World Bank*, kwenye Wilaya yangu ya Kaliua, kati ya vijiji vyote vijiji vitatu tu vilipatikana na maji na yale maji hayakusambazwa popote, yameishia pale pale. Kwa hiyo, unavyosema kwamba tutaendelea na utaratibu wa kumaliza au kutekeleza Miradi ya Maji ya Vijiji 10 ya *World Bank almost 70% ili-fail*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba lazima tunapokwenda kuangalia miradi ya maji tuone kweli inafanikiwa. Nimeangalia kwenye Mpango hapa, Mkoa wetu wa Tabora tulipata faraja baada ya kuambiwa kwamba kuna mpango wa kutoa maji Ziwa Victoria kuleta Wilaya zote za Mkoa wa Tabora, kuanzia Nzega kwenda Igunga kwenda Bukene mpaka Sikonge, Tabora Mjini mpaka Urambo, Kaliua haikuwepo. Nimeangalia hapa tena haipo kwenye Mpango wa mwaka huu, haipo kabisa, kwamba ule Mpango umeishia wapi? Ni miaka mitatu uchambuzi yakinifu unafanyika, miaka mitatu upembuzi unafanyika, miaka mitatu utafiti unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais hapa alisema ule uchambuzi na upembuzi yakinifu utakuwa haupo tena kwenye Serikali hii, mbona huu upembuzi unaendelea miaka mingi. Naomba sana kwenye mpango wa mwaka huu mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kuleta Mkoa wa Tabora na Wilaya zake utimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya yangu ya Kaliua Mpango wa Victoria haupo na mpango uliokuwepo kwenye Wilaya ya Urambo kuanzia mwaka 2013 ni kutoa maji kutoka Ziwa Ugala. Ni jambo la kusikitisha juzi nimesikia Mheshimiwa Waziri anasema hapa, mchakato bado unaendelea 2014 zilitengwa milioni 450 kufanya uchambuzi yakinifu na upembuzi, leo ni mwaka wa tatu bado uchambuzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Serikali ikaja na mpango wa kwenda kutoa maji Malagarasi, bado tunaambiwa uchambuzi yakinifu unaendelea. Naiomba Serikali, kwenye Mpango huu uwepo mradi wa maji katika Wilaya ya Kaliua wa kuondoa machungu na mateso kwa akinamama wa Kaliua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuendelea kushuka kwa shilingi ya Tanzania. Nilikuwa nazungumza, nitaendelea kuzungumza, ndiyo wajibu wangu kama mwakilishi. Tumekosa udhibiti wa shilingi yetu ya Tanzania kabisa kwa miaka yote na nimekuwa namlaumu hata Benno, Gavana Mkuu, ameshindwa kusimamia, kusimama kwa shilingi ya Tanzania. Ni Tanzania pekee, dola inatumika kununua vitu madukani, ni nchi gani utakayokwenda ukatumia *Tanzania shillings* kununua vitu madukani kwao. Tanzania tunatumia fedha ya nje kununua vitu, kutoa huduma kwenye maduka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni Tanzania pekee kuna utifiri wa *bureau de change* kila kona unakuta viduka vya kubadilisha fedha. Leo ukienda Kariakoo watu wana dola mikononi, mikononi tena Wamachinga watu wadogo, wanashika dola wanauza nchi gani hii! Kuendelea kushuka kwa shilingi ya Tanzania kumeendelea kushusha uchumi wetu, hili hatulifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi nyingine kubadilisha fedha unaingia gharama kubwa unateseka kweli na wana *centers* Tanzania tunaongea hapa halifanyiwi kazi. Kwenye Mpango wa mwaka huu tunataka tujue mpango wa kudhibiti matumizi ya dola ndani ya nchi yetu, mpango wa kudhibiti maduka holela ya fedha hapa nchini na mpango wa kuimarisha fedha yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusafirishi chochote Tanzania, sisi ndiyo tumekuwa masoko ya wenzetu, tunauza kila kitu, ni masoko tu, masuala mengine hayajaleta viwanda vikubwa vya ajabu. Hivi kweli, tunahitaji kiwanda cha aina gani kutengeneza pamba *stick*, tunaagiza kutoka nje. Tunahitaji kiwanda cha aina gani kutengeneza *toothpick* ya kuchokonolea meno, tunaagiza kutoka nje, tunahitaji kiwanda gani kule kuleta ndani ya nchi yetu vibiriti, vitu vingine ni vidogo vinatutia aibu, ni Taifa kubwa, lakini hebu aibu hii iondoke. Vile vitu ambavyo tuna uwezo navyo ndani ya nchi yetu tusiagize, tumezidi kuwa masoko ya wenzetu, tunatoa ajira kwa wenzetu, sisi tunaendelea kunyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kusikia kwenye hotuba hapa, kwamba, kuna viwanda kuendana na jioografia ya nchi yetu. Tuna bahati kweli Watanzania, maeneo mengi *almost* karibu kila kanda ina vitu ambavyo Mungu ameweka. Mkoa wa Tabora tuna misitu, tunasafirisha mbaao, kuna magogo, jambo la ajabu vijana wanadhurura, hawana ajira, lakini mbaao zinapelekwa China zinakwenda kutengeneza *furniture* tunarudishiwa makapi, tunanunua. Tunaomba kwenye Mpango wa mwaka huu kuwepo kiwanda kikubwa Mkoa wa Tabora cha kutumia rasilimali ya mbaao na magogo ya Tabora, badala ya kusafirisha yaende nje, vijana wapate ajira, lakini pia tuweze kuzalisha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema hapa Bungeni, itahakikisha samani zote za ofisi zinanunuliwa ndani ya nchi. Huu ni mwaka wa nne, Serikali wameshindwa wanaagiza, leo ukienda ofisi zote za Serikali ni samani za Kichina, wakati tunao vijana, tunazo mbaao, tunayo magogo, miti ya thamani, mininga, mikongo mnapeleka China, tunaletewa makapi, tunanunua vitu ambavyo ni *very low quality, this is shame!* Naomba sana Serikali kwenye Mpango ihakikishe sasa ile mipango ya miaka mitatu, minne iliyopita hakuna kutoa kitu nje, tuwezeshe vijana wetu, tuwezeshe Magereza, tuwezeshe Jeshi ili tununue vifaa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kilimo. Hili ni muhimu kwa hiyo, lazima tuligusie, lazima tuwe na kilimo cha uhakika, lakini pia lazima tuhakikishe kilimo chetu kinaendana na hali halisi. Leo kilimo chetu kimekuwa cha jembe la mkono kwa asilimia kubwa. Lakini pia utaratibu unaotumika kupata pembejeo sio mzuri, ni wizi unafanyika, Serikali kila mpango unaokuja nao hautekelezeki. Sasa tunaomba, tunapokwenda kwenye uchumi wa viwanda uende sambamba na uchumi na kilimo chenye tija. Umwagiliaji, pembejeo, *mechanization*, wawezeshaji wale watumishi wawe wa kutosha lakini pia wawe na ujuzi wa kutosha kuweza kutoa elimu kwa ajili ya kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni suala la elimu. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais ameamua kutoa elimu bure kwa Watanzania, ni jambo jema. Naomba suala la elimu bure liendane na miundombinu ya watoto, ukiwapa leo watoto elimu bure, wengi wanakaa chini, kwangu Kaliua kule watoto wanasomea chini ya mti. Mtoto anasomea chini ya gogo, kwanza hajui kama kuna elimu bure kwa sababu ananyeshewa na mvua, anapigwa na jua, lakini pia tuhakikishe watoto wetu wanakaa kwenye madawati yote. Kwa hiyo, naomba kwenye Mpango huu, mwaka huu Serikali ihakikishe ndani ya mwaka mmoja, watoto wote wa Tanzania vijijini na mijini wanakaa madarasani, lakini pia wanakaa kwenye madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, angalau kila mtoto atajua kwamba Serikali yake inamjali, atathamini sana elimu ambayo anapewa, lakini pia itamjengea uwezo. Leo tumekuwa tunapata kwenye taarifa zetu kwamba mtoto anamaliza shule hajui kusoma wala kuandika. Kwa sisi ambao tunatoka vijijini hushangai, kama mtoto anakaa chini ya mti, mvua inamnyeshea miaka miwili, mitatu, hajui kusoma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya muda wako tayari.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Monduli kwa kuniamini na kunituma kuwa mwakilishi wao katika jengo hili lakini pia nimshukuru Mungu kwa kuendelea kutupa afya njema hadi muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ulioko mbele yetu kwa mtazamo wa kimaandishi ni mpango mzuri sana, kama ambavyo wamesema wengine, nchi yetu tunalo tatizo la kutekeleza Mipango, lakini mmekuja na kaulimbiu hapa kazi tu, tunataka tuwapime katika hili. Kumekuwa na *excuses* nyingi na ni Tanzania pekee duniani nchi inayofanya *trial and error* kwa miaka 54 ya uhuru kutafuta msimamo wa uchumi wa nchi na elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza tulikuja na Kilimo Kwanza, tukaja na *BRN* imekwama, leo tumekuja na nyingine ya viwanda ambao umekuwa ni wimbo wa Taifa kila wakati, kila wakati tunabadilisha. Amekuja Waziri hapa wa Elimu amebadilisha elimu yetu mara nyingi, tunamshukuru Profesa Ndalichako amesema yeye anarudisha ile *division* na ni kweli ali-sign vyeti vyetu.

Katika hili lazima tuwe na misingi inayodhibiti elimu, haiwezekani kila Waziri anayekuja anaamua yeye aina ya elimu tunayotaka, lazima kuwe na mjadala unaoshirikisha wadau hasa Walimu na wenye *professional* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aina gani ya elimu ya watoto wetu tunahitaji! Leo tunataka tuagize wageni kutoka nje kwa sababu ya gesi na tunajua tuna rasilimali hii ya gesi, lakini hatujafanya *investment* ya kuwasomesha vijana wetu kuanzia ngazi ya chini kuhusu rasilimali tuliyonayo. Ni ajabu kwenye nchi tuna gesi ya kutosha, tuna madini ya kutosha, lakini hatuna wataalam wa kutosha kwa sababu hatuwajengei msingi wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaendelea kufundisha kwamba binadamu aliwahi kuwa sokwe, ndiyo masomo tunayofundisha watoto wetu, watategemewaje! Kwa hiyo haiwezekani tukawa na nchi ya namna hiyo kwamba mpaka leo hatujui aina ya elimu tunayotaka kuwapa Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kama walivyosema wenzetu katika suala la elimu tunawashukuru, kwa hii kaulimbiu ya elimu bure. Wengine wamezungumza sana habari ya miundombinu, lakini nashukuru na niseme niipongeze Serikali kwa kuleta fedha ya chakula yote kwa wakati katika Jimbo la Monduli katika shule zote za sekondari kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri Mheshimiwa Simbachawene, nilimpigia simu na nikawashukuru sana. Hili ni jambo jema sana, lakini walimu wetu hawana mahali kwa kulala na mnafahamu maeneo ya vijijini. Tatizo la mipango ya nchi yetu, wataalam wengi wanafikiri nchi yetu ni Dar es Salaam, nchi hii siyo Dar es Salaam peke yake. Mnapanga mipango kwa kuangalia pale Dar es Salaam siyo kweli! Yako maeneo ya nchi hii mnatakiwa mfike muangalie namna ya kujenga rasilimali za Taifa zinufaishe Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema mnafanya tafiti lakini kwenye Majimbo ya Wabunge hao wote hata wengine wanaowashangilia wanaotoka CCM hamjafika kwenye Majimbo yao. Sasa hizi *term of reference*, hizi *sampling* mnazozichukua mnachukulia Dar es Salaam, mnachukulia wapi! Nchi yetu ni kubwa lazima mfike muone maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza uchumi wa kati, lakini uchumi huu hau-*reflect* maisha ya kawaida ya Mtanzania na hau-*reflect* kwa sababu hatu-*invest* katika miradi midogo inayosaidia Watanzania wenzetu.

Leo mnazungumza viwanda vikubwa, lakini hamzungumzi habari ya mifugo ambayo kwato ni rasilimali, nyama ni rasilimali, ni malighafi ya kubadilisha, ngozi, maziwa, lakini sehemu kubwa ya wafugaji wa nchi hii, eneo kubwa ni la wafugaji pamoja na kwamba mnatufukuza kila mahali, lakini hamzungumzi habari ya kubadilisha mifugo kuwa kama zao la biashara, bali mnaangalia kama wanyama waharibifu tu, kila siku kuwahamisha, kila siku kuwafukuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipotazama sekta ya mifugo kwa mtazamo wa kuona kama zao la biashara kama mazao mengine, hatutaweza kuwaendeleza wafugaji wetu. Hatutaweza kwa sababu lazima kama tunatafuta masoko kwa ajili ya mifugo, ni lazima wananchi wetu watapunguza mifugo wenyewe kwa sababu wanajua kuna masoko ya kwenda kuuza mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze katika suala lingine la wanyamapori. Ni kweli nchi yetu ina wanyama wa kutosha, lakini kama hatuzungumzi namna ambayo wananchi wataona hawa wanyama ni faida kwao, hatuwezi kuwa na wanyamapori na wataendelea kufanyiwa ujangili kadri iwezekanavyo kwa sababu hatujali wananchi wanaozunguka maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi anatakiwa aone wanyama wale ni muhimu, pale ambapo mazao yake yameharibiwa na wanyama basi fidia inayolingana na madhara yaliyofanyika, ifanyike kwa wananchi, yule mwananchi atamlinda yule mnyama. Ikiwa yule mnyama atakuwa ni sehemu ya kuharibu rasilimali zake, akija mtu wa kuua, anasema mwache aue tu, ananipunguzia kero ya kuharibu mazao. Kwa hiyo, tutazame kwamba wananchi wanaozunguka maeneo yale waone faida ya kuwa na wale wanyama, watawalinda wala hatutahitaji kupeleka bunduki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili anazungumza habari ya wanyama Monduli, maeneo mengi Simanjiro, hakuna magari ya kulinda wale wanyama. Hivi unafanyaje doria kama huna magari, huna silaha, huna wataalam. Huu ni mchezo na ndiyo maana wanyama wataendelea

kuuawa. Unapiga simu watu watoke Ngorongoro waje kufanya doria Mto wa Mbu pale baada ya wanyama kuuawa, baada ya masaa sita, huyo jangili anayekusubiri masaa sita ametoka wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tunataka kulinda wanyama wetu ambao ni chanzo cha mapato ya nchi yetu, ni lazima tufanye *investment* ya kutosha, tuwe na magari ya kutosha katika kudhibiti ujangili, maana wananchi wetu wanatoa ushirikiano lakini unapiga simu, wale watu wa *game controller* wanakuja baada ya masaa manne, baada ya masaa matano kwa sababu ya tatizo la gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko gari moja Monduli pale la Mimitu, linaangalia Longido, Kiteto, Simanjiro na maeneo mengine ya Tarangire, gari moja la misitu tena bovu. Hatuwezi kulinda wanyama wetu kwa sura hiyo, lazima kama tunadhiti ujangili tuhakikishe tunapata vifaa vya kudhibiti suala la ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la afya. Hatuwezi kuwa na Taifa linalozalisha rasilimali kama afya zao zina mgogoro. Katika maeneo mengi tatizo hili la afya ni kubwa sana kwenye nchi yetu, tunajenga majengo lakini hakuna dawa, tunajenga majengo lakini hakuna watumishi. Hivi Taifa gani, ni nguvukazi gani itakayofanya kazi ya kuzalisha kama hawana afya nzuri? Kila siku tunazungumza habari ya upungufu wa dawa, lakini ni *story* ya kila siku Serikali kusema tunaendelea, tunaendelea kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa kweli katika zahanati hizi lazima tuboreshe afya za watu wetu ili waweze kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Vinginevyo hatutaweza kuwa na maendeleo katika uchumi, katika viwanda, kama jamii yetu inayoshiriki nguvukazi haina afya bora ya kufanya kazi hizo ambazo zinapaswa kufanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho, ni suala la kukuza uchumi na kukusanya mapato ya Serikali. Tunavyozungumza habari ya kukusanya mapato lazima tudhibiti pia mapato hayo yatumike kwa njia inayostahili kufanyika. Tumeshuhudia, Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda akavumbua makontena ambayo tunaambiwa yameibiwa karibu 2000 sijui na mia ngapi, lakini *business as usual*, *story* hiyo imekwisha, hatusikii wale wenye makontena wamekamatwa na wamefunguliwa kesi za uhujumu uchumi kwa kiwango gani! Kwa hiyo, tulikuwa tunafanya *show* ya kwenye TV. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana imezungumzwa hapa habari ya mabehewa hewa, unawashughulikia wataalam, lakini yule Waziri aliyekuwa anahusika katika kudhibiti suala hilo umemwacha. Hatuwezi kuwa na nchi ya *double standard*, unawaonea hawa, unawaonea huruma hawa, haiwezekani! Kama Mawaziri wamehusika, lazima Bunge lisimamie Serikali, Mawaziri

waliokuwa wanasimamia Wizara wakati uhujumu unafanyika, washughulikiwe na ndiyo maana *reports* zote zinazohusu uhujumu wa uchumi haziletwi kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekuwa na *story* ya tokomeza imefichwa; mmetengeneza Tume ya Majaji, imefichwa; mmekuwa na ile inayoshughulikia Migogoro ya Wakulima na Wafugaji, imefichwa; mmetengeza Tume nyingi za kuangalia hiyo ya bandari na wizi huo, umefichwa kwa nini? Ni kwa sababu wenyewe mnahusika na hivyo hamuwezi kujifunua kwa sababu ya utaratibu huo. Kama tunataka tujenge nchi yetu kila mtu atendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwafukuza tu Wakurugenzi, tukawaacha wanasiasa wanaoingilia kazi za kitaalam wao wakiwa salama. Ndiyo maana hawaogopi kwa sababu wanaagiza maagizo kwa mdomo, wataalam wanachukuliwa hatua, yeye anabaki salama. Tuanze na hao tuliowapa dhamana ya kusimamia Wizara hizo wakati uharibifu unatokea wao walikuwa wapi! Kama hatuchukui hatua hiyo tutakuwa tunacheza ngoma ambayo haina mwisho wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Maana nimekaa muda mrefu naona wanaongea mara mbili, mara tatu mimi nakosa nafasi, lakini nashukuru kwa kupata hiyo nafasi.

Kwanza, niwapongeze wananchi wa Kiteto kwa kunichagua, wale wananchi wamenipa kura nyingi, wameniamini. Wananchi wa Kiteto nawashukuru sana na naendelea kuwaomba na naahidi kwamba nitawatumikia kama ambavyo wameniamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia upande wa kilimo kwa sababu kwanza ni bwana shamba, ni mkulima, ni mfugaji, nina uzoefu kwenye kilimo zaidi ya miaka 25. Kilimo cha nchi hii kimeshindikana, lakini nadhani kuna mahali ambapo yawezekana tumejichanganya, hebu tufikirie ni wapi tumekosea. Nchi hii sasa hivi tuna- *import* zaidi ya asilimia 60 ya mbegu za mahindi na mbegu za aina nyingine. Tunapolalamika, tumejiuliza kwamba sasahivi tumejiuliza habari ya pembejeo, lakini hata huyo msambazaji wa pembejeo atapata wapi hizo pembejeo. Nchi nzima hakuna mbegu asilimia 60, tunayo ardhi ya kutosha, tunao wataalamu, tunazo benki kwa nini watu wetu hawawezi ku-*invest* kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali haijachukua jukumu la kuwabinafsishia watu maeneo wakaweza kuendesha kilimo cha kuzalisha mbegu kiasi kwamba mbegu zikatosha na usumbufu ukapungua kwa wakulima

wetu. Kuna Kanda ya Ziwa ukiangalia Kigoma, ukaangalia Kagera, ukaangalia ile kanda ya Kibondo nzima, mvua zinatoshwa, tungeweza kutenga maeneo, ule ukanda wote tukaweza kuzalisha mbegu, zikaweza kusaidia nchi yetu kwa maana ya kilimo, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Benki ya Kilimo imeanzishwa, ukiangalia mtaji wa Benki ya Kilimo, ukikopesha watu utakopesha watu ambao hawazidi 10, 20 hii benki na jinsi ambavyo tunawakulima na asilimia kubwa ya watu wetu ni wakulima na wafugaji hebu niambie kwa mtaji huu tunakwenda wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamisheni pesa zilizoko kwenye ile Benki ya TIB, zipelekwe kwenye Benki ya Kilimo, kopeni pesa ingiza kwenye ule Mfuko, ruhusu wananchi wetu wakakope waweze kufanya kazi. Hata tutakapokwenda kutoza kodi, kuna kitu cha maana cha kutoza kwa sababu watu watakuwa wamezalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki nyingi za kibiashara zimeweza kukopesha wakulima na wakulima wengi wamefeli kwa sababu ya riba kuwa juu. Hata hivyo, jambo kubwa na shida kubwa hapa inaonekana ni kwa sababu hizi benki, Benki Kuu imekuwa inakopa, inaweka *government guarantee* na bado hazilipi zile benki na zile benki kwa sababu zinaogopa kufilisika haziwezi kushusha *interest*, mkulima na mfugaji wataponea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Benki Kuu haiwezi ku-*guarantee*, iki-*guarantee* hailipi zile benki, hicho kilimo kitaenda wapi, watapunguza riba waende wapi na wanapesa za watu! Naomba kushauri, Benki ya Kilimo iimarishwe, mitaji ihamie huko, watu wakakope huko, wakachape kazi. Ukimaliza unawaandikisha VAT na TIN halafu wanalipa kodi kwa raha zao, wanaendelea kutambaa kwenye nchi yao kwa neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto tunazalisha mahindi kwa maana ya kulisha *central zone including* Dar es Salaam, Morogoro, Arusha na Manyara. Awamu iliyopita, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alizungumza suala la kutujengea lami kutoka NARCO kwenda Kiteto ili mazao yaweze kutoka kwa salama. Mpaka leo hii barabara tumeimba, tumeomba, nimemwambia Ndugai, Ndugai amelia Bungeni, imeshindikana barabara, hebu niambieni hii barabara inajengwa lini niende kuwaambia wananchi. Maana Magari yanaanguka sasa hivi madaraja yemekwisha, magari yameanguka, chakula cha msaada kimeshindwa kwenda, watu watakufa njaa, barabara imekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa mniambie leo, mimi sijui cha kuwaambia. Maana wananchi watakuja wenyewe hapa hapa maana Kiteto ni karibu hapo, wakiamua saa nne wako hapa, sasa mniambie niwaambie nini, hii

barabara kwa nini haijengwi na sisi tunalisha watu? 90 percent ya mazao yanayokuja NFRA hapa yanatoka Kiteto, lakini Kiteto imegeuka vumbi, sisi hatuna *benefit* yoyote kwa sababu hata wananchi wetu hizi barabara wamezikosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu amani; Kiteto ni Darfur ndogo. Bunge lililopita wame-*debate*, mapigano ya wakulima na wafugaji watu wamekwisha. Nataka kuiuliza Serikali iniambie leo tunafanya nini ili kuhakikisha kwamba amani inatengemaa Kiteto, wakulima na wafugaji waweze kubaki salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel hebu tulia kidogo. Tafadhali usiite Kiteto ni Darfur ndogo, wote tunajua nini kinaendelea Darfur, tafuta mfano mwingine tafadhali.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Haya nimefuta, lakini si zilipigwa na wewe unajua? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ukishafuta usiendeleo tena na maneno mengine, futa uendeleo kutoa hoja yako.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Haya nimefuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto watu wameumizana, lakini katika mambo ambayo yamesababisha ile Kiteto watu waumizane ni pamoja na viongozi, watendaji wa Serikali kushindwa kufanya kazi. Katikati ya mgogoro wa wakulima na wafugaji kuna watu wana-*benefits* ndani ya haya. Wanashindwa kufanya kazi za sehemu zao ili amani iweze kupatikana na kusema ukweli na kuusimamia. Hapa watendaji wa Serikali tuamini, tuseme waliteleza na walishindwa Serikali kuchukua hatua kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu NGOs. Kiteto kuna NGOs zinapenyeza penyeza zinakuja, wanazungumza, mara tunataka hifadhi ya nyuki, mara *pingos*, mara nini, kila siku wamo, wanazunguka, wanaita makundi machache, wanafanya vikao, wanalipana posho. Mmoja akiulizwa Mbunge wenu yuko wapi, wanasema, Mbunge tumechelewa kumpa taarifa kwa sababu ilikuwa ni haraka haraka. Mipango na haya mambo yanayopangwa ndani ya ile Wilaya, ndiyo matokeo ya kumaliza watu yanayoendelea sasa hivi. Niombe Serikali iliangalie hili, Serikali ifungue macho ione lakini ichukue hatua za haraka na za makusudi kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wanasiasa. Siasa zinazochezwa Kiteto zimekuwa ni za kihuni, sasa hivi tuko salama. Sasa niombe Serikali inisaidie, wale wanasiasa uchwara wanaokuja kutembeza siasa pale, tupige siasa wakati wa

siasa, lakini wakati wa kazi, tuchape kazi badala ya kugombanisha wakulima na wafugaji. Wewe ukitafula siasa, njoo wakati wa siasa tupige, tukimaliza tuhimize amani, tuhakikishe kwamba watu wote wana uwezo wa kufanya kazi, mkulima aende shambani, mfugaji aende shambani. Niombe Serikali inisaidie kupima ardhi ya Kiteto vizuri, iipime yote, mkulima ajue anaishia wapi na mfugaji ajue anaishia wapi, mwisho wa siku sisi tujenge amani na Serikali isimame katikati kutekeleza hilo, huu muda wenyewe ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie afya, hospitali ya Kiteto, tumeomba pesa, tumeahidiwa, tumeambiwa, sasa tumechoka. Tunaomba jamani ile hospitali ikarabatiwe maana sasa hospitali itakuwa chanzo cha magonjwa ya mlipuko pale. Wodi ya wanaume iliyoko pale imechanganya na wale wagonjwa wa *TB (Tuberculosis)*, wote wanachanganyika humo humo, sasa wale watu wataponea wapi? Aliyejeruhiwa ameanguka na pikipiki humo humo, aliye kwenye dozi ya *TB* yumo humo humo. Sasa tutajengewa lini hii wodi za wanaume zitenganishe hawa watu ili wananchi wasiweze kuambukizana magonjwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali inisaidie na Waziri wa afya, hakikisheni kwamba mnaweza kunitatulia huu mgogoro na ile hospitali ikarabatiwe maana sasa imefika mahali tunafanya *repair* tunazibaziba wenyewe, tunakwenda huko tunakarabati mahali, tunasogezasogeza ili lile jengo lisije likaangukia wagonjwa halafu tukaongeza wengine tena wadini, tukaongezea yale magonjwa wanayoumwa, halafu tunaongezea mengine tena ya jengo kuwaangukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine tulilionalo Kiteto ni la maji. Kata za Dongo, Songambe, tumechimba visima, ile nchi ni kame. Hebu Serikali iangalie mfumo mpya wa kutusaidia, ile nchi ni kame, wamechimba visima havifiki. Visima vilivyochimbwa vikipatikana maji havifungwi mapampu ili watu waweze kupata maji. Niombe Serikali iweze kuliona hili kwamba kama inawezekana, tuchimbiwe mabwawa ya kutosha, watu watatumia maji na mifugo itatumia maji hayo hayo ili angalau tuweze kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ndani ya Mji wa Kibaya; ule mji Rais ametuahidi visima kumi, ametuahidi pesa, vile visima vimeshindikana. Sasa ule Mji wa Kibaya mnataka watu waende wapi, imeshindikana, watu hawapati maji na tumeahidiwa maji muda mrefu sana. Naomba Serikali iweze kuliona hili ule Mji wa Kibaya uweze kuokolewa maana watu wameongezeka, maji hatuna, tuna visima viwili, maji hayatoshi, watu wanabeba ndoo, akinamama wameota vipara. Na mimi niliwaahidi akinamama nikiwa Mbunge mtaota nywele mwanzo mwisho. Naomba Serikali ichukue jukumu la kuhakikisha kwamba hawa akinamama wanaota nywele kichwani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Sasa atafuata Mheshimiwa Jamal Kassim Ali.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia, nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni kwa kunichagua kuja kuwa mwakilishi wao katika Bunge letu hili Tukufu. Ni imani yangu ya kwamba tutashirikiana pamoja katika kuleta maendeleo ndani ya Jimbo letu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, niwapongeze Watanzania kwa kuendelea na kuwa na imani na Chama cha Mapinduzi na kukipa fursa kuongoza nchi yetu kwa kipindi kingine. Naamini hivyo hivyo kwa Wazanzibari wenzangu wataendelea kukipa fursa chama chetu kuongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wachangiaji waliotanguliwa kumpongeza Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania; Waziri Mkuu na timu yote ya Serikalini kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameanza kuifanya kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Nimpongeze Dkt. Mpango na timu yake yote kwa kuwasilisha Mpango mzuri kabisa ambao umekwenda kujibu au kutafsiri ile dhana ya Rais wetu ya kusema anataka kuipeleka nchi yetu kuwa nchi ya viwanda. Niwapongeze sana Wizara kwa kuandaa mpango wetu huu mzuri na kuwasilisha vizuri katika Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo nitayagusia, eneo la kwanza, ni eneo la kodi. Nimpongeze Rais, Waziri Mkuu na Waziri mwenyewe kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweka mikakati kuona namna gani tunaendelea kukuza makusanyo yetu ili tuweze kumudu mahitaji yetu ya maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejionea ongezeko kubwa kabisa la ukusanyaji wa kodi ambalo taasisi yetu ya TRA kwa kipindi hiki cha miezi miwili ambayo imefikia. Niwapongeze sana na juhudi hizo waziendeleze ili kukuza makusanyo, kwa sababu tunaamini kabisa makusanyo hayo ndiyo yatafanya Mpango wetu utimie na yale maendeleo ambayo tunakusudia kuwapeleka wananchi yafikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la kodi, kwa kipindi kirefu kabisa, kumekuwa na masikitiko au malalamiko yanayohusu masuala ya bidhaa na vitu ambavyo vinatoka Tanzania Zanzibar kuja Tanzania Bara. Mfumo wetu wa kodi

uliokuwepo hivi sasa kwa bidhaa hizi zinazotoka Tanzania Zanzibar kuja Tanzania Bara kunakuwa na tozo la kodi ambalo linaitwa *difference*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati tunajiuliza, iweje tufikie hapo? Tuna Taasisi moja ya kodi ambayo ni *TRA*, Taasisi hii na Zanzibar ipo, inatumia sheria moja na mwongozo huo huo mmoja, wa Kamishna huyo huyo mmoja wa Forodha. Tumekwenda kutengeneza mfumo ambao umetengeneza urasimu, manung'uniko na baadhi ya wakati hata ukokotoaji wa kodi hizi hauko wazi, wananchi wetu hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ana *television* yake tu akifika pale Bandarini Dar es salaam anaambiwa alipie kodi hajui alipie kodi vipi na ile *TV* ameinunua Zanzibar. Kwa hiyo, mambo kama haya, *are very peanut*, lakini huko mtaani tunakwenda kutengeneza bomu ambalo wananchi wetu wanalinung'unikia lakini Serikali yetu inachukua muda mrefu kabisa kulipatia majawabu mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi najiuliza, *TV* ili itozwe kodi ya forodha maana yake lazima mkadiria kodi aijue *CIF* yake, aliijuaje? Kwa hiyo, hizi kodi hazina base yoyote, tumekuwa tunatengeneza fursa ya maafisa wetu kujiamulia tu haya mambo na kwa asilimia kubwa yametengeneza urasimu na mifumo ya rushwa. Kwa hiyo, nimwombe kabisa Mheshimiwa Waziri, hili jambo linawezekana, halihitaji mshauri mwelekezi, yeye mwenyewe anatosha kulielekeza, kulifuta, hao wananchi basi wa-enjoy fursa ya Muungano wetu, Wabara waende Zanzibar na bidhaa zao bila tabu, Wazanzibari wakija bara, waje bila taabu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nitalizungumzia, eneo la viwanda. Tumeona kabisa Mheshimiwa Rais, toka alivyokuwa katika kampeni zake na alivyozindua Baraza lake la Mawaziri alikuwa anazungumza sana kuhusu suala la viwanda. Lengo lake ni kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Nampongeza na namuunga mkono katika hilo na naamini kabisa, viwanda ambavyo tutavianzisha ndiyo vitakwenda kujibu matatizo ambayo nchi yetu inayakabili kwa sasa, viwanda hivi hivi ndiyo vitaenda matatizo ya ajira kwa vijana wetu, viwanda hivi hivi ndiyo vitaenda kujibu matatizo ya masoko kwa wakulima wetu, wafugaji na wavuvi. Viwanda hivi hivi ndiyo vitakwenda kujibu tatizo letu...

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu. Mpango huu ni mzuri, hivyo nina mambo machache sana.

La kwanza, ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha Kimataifa cha *standard gauge*. Namwomba Mheshimiwa Waziri aseme ni ujenzi wa reli ya

kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora mpaka Mwanza, kutoka Tabora mpaka Kigoma, kutoka Kaliua mpaka Mpanda mpaka Kalema, kutoka Uvinza kwenda Msongati na kutoka Isaka kwenda Keza. Haya mambo ya kutosema ndiyo baadaye tunabaki hatuna hata pa kumuuliza. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri aje kwenye Mpango atakapouleta maana haya ni mapendekezo, aseme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la *retention scheme*. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana usiingie kwenye historia ya kuua taasisi za nchi hii. Viwanda vya nchi hii vilikufa miaka ile kwa sababu kila fedha inakusanywa inapelekwa Hazina, wanaomba kuagiza *raw material* mpaka fedha zitoke Hazina, *by the time* wanapewa pesa ndiyo viwanda vikaanza kufa. Leo mnakuja mnataka kuua Halmashauri, mnataka kuua Taasisi za Serikali! Naomba Wabunge mnikubalie tupinge habari ya kuondoa *retention*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema, leo mnasema fedha zote ziende *Central Bank*. Nataka nimuulize Waziri wa Fedha, fedha zinazokusanywa na *Pension Funds*, wasipoziwekeza *Pension Funds* hazifi hizi? *Pension Funds* zinakusanya fedha mnapeleka Hazina, watazalishaje, watalipaje *pension*? Leo mnasema *retention scheme* za kwenye *airport* zote ziende Hazina, kitakachotokea mtawafukuza watendaji, kwa sababu ndege zitashindwa kutua, mtakuwa hamjapeleka OC kwa sababu hela mmekusanya, mmepeleka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zinakusanya fedha za *own source*, mnasema peleka Hazina, hizi Halmashauri zitakufa, mnasema leo *own source* zote za TANAPA, za nani ziende Hazina. Kitakachotokea, Mbuga za nchi hii zitaanza kufa mbuga moja baada ya nyingine. Mnataka Bunge hili tuingie kwenye historia ya kuua mbuga za nchi hii? Halafu kama hoja ni kuweka hela Hazina hawajaanza leo. Hebu tukumbushane ilikuwaje miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati BOT imeungua, ndiyo wakati hela ziliondoka Hazina, zikapelekwa NBC, alivyokuja Gavana yule Rashid akasema sasa sizitaki hizi fedha. Urasimu ulikuwa ni mkubwa sana. Nasema kama ni fedha za Serikali za Bajeti weka Hazina hakuna atakayekupinga, lakini fedha zinazozalishwa huku, mkisema zote ziende Hazina, mtaua taasisi moja baada ya nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu, hatuwezi kuwa na *contradiction*, mnasema *D by D, D by D* gani sasa? *Unless* mniambie kwamba sasa hatuzitambui Halmashauri zote. Kwenye Vyuo vya Maendeleo, kwenye shule za sekondari watoto wanalipa pesa wanunue chakula, mnasema peleka pesa zote peleka Hazina, muda wa kununua chakula utakuwa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mheshimiwa Waziri, nchi hii inaongozwa kwa sheria. Ziko taasisi zimeletwa kwa sheria, mnatakaje kuleta mambo kwa *decree*, mnaamua tu bila kufuata sheria? Ningeomba Waziri wa Fedha, tulettee sheria zote zilizoanzisha taasisi hizi ambazo kwenye sheria kuna mambo ya *retention*, tuangalie ili tubadilishe sheria za nchi. Haiwezekani mnakaa na *TR* mnaandika barua, fedha zote zitapelekwa Hazina kesho Jumatatu. Hii ni nini? Mnapewa sekunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mashirika kufungua akaunti lazima muwaite *Board Meeting* leo ninyi mnawapa siku nne, wawe wamepeleka fedha *BOT*. Kuna haraka kweli? Nasema na nawaomba sana Wabunge, hili la *Retenteion* tulipinge, tunalipinga kwa sababu *We have a cause*, tunataka kuzuia watu kuua mashirika ya nchi hii na ni kwa sababu watu wa Hazina hamtaki kufikiri. *Chenge one*, imewapa vitu vya kukusanya mapato, hakuna hata kimoja mmekiandika humu. Bahari kuu iko wapi, kila siku mnatuambia habari ya bahari kuu, tutakwenda kufanya utaratibu, mpaka lini huo utaratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya pale *Treasury* watu hawataki kufikiri. Angalia vyanzo vya mapato ni vilevile toka nimeingia Bungeni havijawahi kubadilika. Naomba sana niseme tulikubaliana wakati tunaanzisha *VAT* kwamba *VAT* itapungua na ningeomba twende 16 wanavyokwenda Wakenya ili tuweze kushindana na Kenya, lakini tumekaa *rigid*, matokeo yake tunapambana. Nasema viwango vya kodi visiposhushwa hatuwezi kupata *compliance*, viwango vya kodi vya nchi hii vinatuma watu kukwepa kodi kwa sababu viwango ni vikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TRA* najua wametembea duniani kote kuangalia viwango vya kodi, wakienda duniani kuangalia viwango vya kodi wanaangalia nini? Ukienda Mauritius kodi ziko chini na wanakusanya zaidi yetu, wako mpaka *fifteen percent* hadi *cooperate tax* na wanakusanya zaidi, sisi tumekalia kupandisha *rate* na mnajua kwa nini tunapandisha *rate*, ni kwa sababu hatutaki kufikiri kutafuta *tax base* zingine. Tumeji-zero in kwenye *tax base* ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, suala la reli kwetu sisi ni kufa na kupona. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, *Walvis Bay* wanajenga reli kwenda Congo, Nakara wanajenga reli kwenda Zambia, Wakenya wanakwenda Kigali. Reli zote zikiisha Tanzania hatuna cha kwetu. Haiwezekani Mungu ametuumba Tanzania imewekwa hapa *geographically* Mungu ana sababu na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungukwa na nchi nane, lakini hatutaki kutumia hizo *opportunity*, tatizo ni nini? Halafu mtatuambia kujenga reli, tukope

maana Waziri wa Fedha juzi anasema, hatuwezi kujenga reli hii ni fedha nyingi, nani kasema, fedha nyingi nani anazitoa, fedha ziko duniani tukazitafute....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, muda wako umekwisha.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha kikao cha Bunge mpaka saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile ni mara yangu ya kwanza, napenda kwanza nimshukuru kabisa Mwenyezi Mungu, muweza wa yote, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa imani yenu kwangu mimi. Naomba sana ushirikiano wenu mzuri hasa katika kuheshimu na kutii Kanuni zetu za Kudumu za Bunge. Ni matumaini yangu kwamba nitapata ushirikiano mzuri kutoka kwenu. Katibu!

## **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaanza na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kutoka CHADEMA.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichukue nafasi hii kwanza kabisa niwashukuru wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo la Serengeti, Mbunge wa kwanza wa CHADEMA tangu Serengeti iwe Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache nahitaji kuchangia kwenye Mpango. Jambo la kwanza ni kuhusu mapato ya Serikali. Nimekuwa Diwani tangu mwaka 2010 katika vipindi vilivyopita ambapo Mpango wa kwanza ulianza, kwa kweli hali ya makusanyo ya mapato ilikuwa ni hafifu sana. Tangu niwe Diwani nimewahi kuona fedha za maendeleo kwa miaka miwili tu na hata hiyo miaka miwili fedha za maendeleo zinazokuja ni 20% au 22%. Sasa

kwa namna hii haya malengo ambayo tumejiwekea hayawezi kufikiwa hata siku moja. Kama hatuwezi kukusanya kiasi cha fedha zinazotosha kwa ajili ya maendeleo yetu ni ngumu sana, tutaendelea kudanganyana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu elimu. Kwanza niwashukuru sana wazazi wa nchi hii kwa moyo wao mkubwa wa kujitoa kujenga shule na madarasa mbalimbali. Natambua Serikali ya CCM inajinasibu kwamba wao wamejenga shule kila kona lakini ukweli wajenzi wa madarasa, wanunuzi wa madawati ni wazazi. Kwa hiyo, nawashukuru sana wazazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya mambo yafuatayo bado hatuta-improve chochote kwenye elimu, mimi kitaaluma ni Mwalimu. Ukiangalia shule za binafsi zinafanya vizuri sana kuliko shule za Serikali, tatizo ni nini? Walimu walewale wanaotoka Serikalini wakienda kule *private* wanafanya vizuri kwa nini wakiwa Serikalini wanafanya vibaya? Nilichogundua ni kwamba hakuna *motivation* kwa Walimu wa Serikali. Mwalimu mshahara uleule anaoupokea ndio huohuo afanyie mambo yote, haiwezekani! Lazima ifikie sehemu Serikali iwatazame Walimu, iwa-motivate walimu mkiwaacha hivi wanakuwa *demoralized* hawawezi kufanya kazi kwa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Serikali imesahau elimu ya chekechea. Huwezi uka-base kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba bila kuangalia elimu ya awali. Elimu ya awali tumeiacha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *issue* ya maabara, wazazi wetu wamejitahidi wamejenga maabara kila shule lakini sasa vifaa vya maabara hamna. Siamini kama Serikali hii miaka mitano itaisha ikiwa imepeleka vifaa kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Serengeti ni Jimbo ambalo sehemu kubwa ya Hifadhi ya Serengeti ipo. Serengeti ni mbuga ambayo inaongoza kwa kuwa na watalii wengi kuliko mbuga zote za wanyama zilizopo katika nchi hii. Hata hivyo, ukija katika Wilaya ya Serengeti, siongelei *Serengeti National Park*, naongelea wanapoishi binadamu, Mheshimiwa Maghembe nakumbuka mwaka jana umekuja pale, maji ya kutumia ni shida. Kilichosababisha nikawapiga CCM kwa muda mrefu maji hakuna. Tangu 2009 limejengwa Bwawa la Manchila mpaka leo hakuna chujio, hakuna usambazaji wa maji. Kwa hiyo, maji yale yako kwenye Bwawa la Manchila lakini namna ya kuyachukua yale maji kutoka pale kuyasambaza hakuna. Ingawa *feasibility study* ilishafanyika tangu mwaka 2009 mpaka leo *implementation* hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeupitia Mpango huu kwenye ukurasa wa 14, nilitegemea kuona Bwawa la Manchila lakini sijaona. Sijui huu Mpango ume-base kwenye nini. Ukiangalia kwenye huu Mpango ukurasa ule wa 14 kuhusu

maji naona wame-base Dar es Salaam sijafahamu miji mingine itakuwaje. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango unapokuja ku-*wind up* tuambie kwamba mji mingine kwenye Mpango kwa nini haikuingizwa? Nimeona mme-base zaidi Dar es Salaam, je, miji mingine ambayo iko nje ya Dar es Salaam mnafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni barabara, kwenye ukurasa wa 10 - 12 wa Mpango, nilikuwa najaribu kuangalia barabara za mikoa, karibia mikoa yote nchi nzima imeunganishwa kwa miundombinu ya barabara isipokuwa Mkoa wa Mara. Sasa nikasema ngoja niangalie Mkoa wangu wa Mara kama umeunganishwa na Mkoa wa Arusha. Mwalimu Nyerere kabla hajaondoka madarakani ali-*propose* ujenzi wa barabara ya Musoma – Butiama – Isenye - Nata - Mugumu - Tabora B na kadhalika lakini mpaka leo zimepita awamu nne barabara ile haijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi sijawa Mbunge nilikuwa natazama Bunge nasikia kwamba zimetengwa *billions of money* kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile, lakini hata mita moja ya lami haijawahi kujengwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango unapokuja ku-*wind up* kwenye huu Mpango, hebu tuambie watu wa Mkoa wa Mara barabara ya kutuunganisha na Mkoa wa Arusha itanza kujengwa lini na itakamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri tufahamu kwamba Mkoa wa Mara na hususan Wilaya ya Serengeti kitega uchumi kikubwa tulichonacho ni *Serengeti National Park* na *Game Reserve* zilizopo lakini watalii ili waje Serengeti ni lazima tuwe na miundombinu mizuri ya barabara. Kwa mfano, barabara ya kuanzia Tarime - Mugumu, barabara ya Musoma - Sirori Simba - Magange - Ring'wani - Mugumu, ni vizuri zikawekwa lami ili watalii wanapokuja basi waweze ku-*enjoy* sasa hivi ni za vumbi hata hazieleweki. Haiwezekani mji wa Mugumu ukakua kwa haraka. Ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais wakati anafanya kampeni mwaka jana Serengeti hakuja kwa sababu ya tatizo la barabara. Barabara za Serengeti ni mbovu kuliko zote nchi nzima. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mipango unapokuja ku-*wind up* hebu tuambie watu wa Serengeti ni lini barabara ya Musoma – Makutano –Butiama - Nata, Isenye - Tabora B - Claims na Loliondo itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kilimo. Serengeti kwa sasa chochote tunacholima tunatengenezea tembo. Ukilima mahindi, mihogo, jua unasaidia tembo kushiba. Tukakubaliana wananchi wa Serengeti tulime tumbaku lakini tumbaku tunayoilima haina soko. Sasa tukimbilie wapi watu wa Serengeti? Nye CCM mmepewa nafasi na wananchi wa nchi hii kwamba muiongoze nchi hii, lakini nawaambia kama msiposimamia rasilimali za nchi hii fursa zikaenda kila eneo mwaka 2020 mtapigwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe jana umetupokea na kwa kweli wananchi wangu wa Serengeti wamekushukuru sana. Naomba utusaidie wananchi wa Serengeti, tumesaidia tembo kutoka 3000 – 7000, sasa hivi tembo wanatutesa, hebu tusaidie basi hata gari moja. Serengeti nzima unapokuja hatuna gari hata moja ambalo mmetupa ninyi Wizara, gari moja tulilondalo alitupa mwekezaji, *Grumeti Game Reserve* ambalo kwa sasa limechakaa haliwezi kufukuza tembo hebu tusaidieni magari kwa ajili ya kufukuzia tembo. Namshukuru Mungu kwamba tumepata zile ndege (*drones*) najua zitasaidia lakini haziwezi kusaidia kama hawana magari. Tusaidiane magari ili tuweze kufukuzana na hawa tembo. Sisi watu wa Serengeti tumeamua ku-*conserve* mazingira ya *SENAPA* na tumeamua tushirikiane na watu wa *Serengeti National Park* hebu basi na nyie tuoneni majirani wenu kwamba tunaumia na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni kuhusu madeni ya Walimu. Nimekuwa Mwalimu Serikalini, nimekuwa Mwalimu *private*, Walimu wana shida kubwa sana. Sijaona kwenye Mpango kama kuna sehemu yoyote ambayo mmekusudia kuwalipa Walimu. Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* utuambie ni lini mtalipa madeni ya Walimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijaanza kuchangia, naomba nitoe shukranl zangu mbele ya Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufika hapa. Pia napenda kushukuru chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (*CHADEMA*) kwa kunifikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Mpango huu kuna mambo mawili au matatu ambayo nahitaji kuchangia. Jambo la kwanza ni kuhusiana na uvuvi haramu pamoja na uwindaji haramu ambao unaendelea katika nchi yetu. Sasa katika Mpango huu ambao nimeupitia sijaona kama kuna mkakati wa kuweza kuzuia hao majangili ambao wanaendelea kuua watu wetu na kuiba wanyama. Pia kuna wawindaji ambao wanapewa vibali halali, ningepomba Serikali sasa kupitia huu Mpango iweke mkakati wa kuhakikisha kwamba pamoja na kupewa vibali lakini ijulikane ndani ya hizo *National Park* wanafanya shughuli gani. Nikitoa mfano kwenye Mkoa wangu wa Katavi kuna Wapakistan zaidi ya 40 ndani ya lile pori, lakini ukiulizia ni shughuli gani wanafanya siyo za kiuwekezaji. Nimewahi kutembelea pale, unakuta wengi wao ni madereva lakini wengine wanapika, ndiyo wanaohudumia kwenye hoteli pale ndani. Kama Serikali tuangalie hawa wawindaji ambao wana vibali kabisa vya kuwinda katika mbuga zetu wanafanya shughuli gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mbuga pia kuna viwanja vya ndege, sasa hatuwezi kuelewa hawa wawindaji wanasafirisha vitu gani. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tusiendeleo kulalamika kwamba ndovu wanaibiwa inabidi kuchukua hatua. Nitoe masikitiko yangu kwa rubani ambaye alitunguliwa na hawa majangili katika mbuga ya Meatu. Kama Serikali au TANAPA wameshindwa kuweka usalama kwa hawa mapolisi ambao wanalinda wanyama wetu pamoja na mbuga zetu basi ni bora tukajua ni jinsi gani tunawalinda hawa wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mchango wangu wa pili unajikita katika viwanda. Mapinduzi ya viwanda yanatakiwa yaendane na uzalishaji wa umeme yaani huwezi ukazungumzia viwanda bila kueleza unaongezaje nguvu ya umeme katika viwanda vyetu. Mpaka sasa Tanzania tunazalisha umeme *megawatts* 1,247 lakini Mpango Mkakati wa Miaka Mitano uliopita Serikali iliweka mpango wa kuongeza uzalishaji wa umeme wa *megawatts* zaidi ya 2,780 lakini hatukufikia malengo. Tunapozungumzia mapinduzi ya viwanda basi tihakikishe kwamba nguvu kubwa tutaongeza kwenye uzalishaji wa umeme kwa sababu hatuwezi tukazungumzia viwanda bila umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme hatuzungumzii kwenye viwanda tu pia tunauzungumzia kwenye matumizi ya kawaida ya wananchi wetu nikitoa mfano wa Mkoa wangu wa Katavi. Mkoa wa Katavi mpaka sasa tunatumia umeme wa *generator* hata kama tuna viwanda vidogo vidogo kwenye mkoa wetu basi hatuwezi kuzalisha *product* ya aina yoyote kwa sababu umeme siyo wa uhakika. Kuna kipindi inafikia wiki nzima wananchi wa Mpanda au Mkoa wa Katavi wanakosa umeme. Kwa hiyo, mapendekezo yangu katika suala la umeme Serikali iangalie sasa ni jinsi gani tunakwenda kuweka mikakati mizuri katika kuweka nguvu ya kuzalisha umeme hasa kwenye kipimo cha *megawatts*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu unajikita zaidi kwenye afya. Kama Serikali tunahitaji kufikia malengo, maana nimesoma Mpango huu una mipango mizuri kabisa ambayo inatakiwa tuifikie kwa ajili ya ku-*achieve* hizo *goals* ambazo mmeziweka. Kitu ambacho nakiona kinafeli zaidi katika Mipango yote ni kwamba tuna mipango mizuri lakini lazima kuwe na *implementation* na *monitoring* lakini Serikali inawekeza fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali tatizo hakuna ufuatiliaji. Kwa hiyo, naomba Serikali hata kama mnajikita kwenye sekta binafsi, sekta za afya, pamoja na elimu, inapopangiwa bajeti fulani basi *implementation* iongezwe kwa kiwango kikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo la afya, Mkoa wangu wa Katavi ni *almost* kama miaka saba iliyopita mpaka leo tumepata Manispa Serikali ilitoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa na kuna eneo kubwa

karibuni heka mia tatu lilishanunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo lakini mpaka sasa hakuna dalili yoyote ambayo inaonesha hospitali itajengwa lini. Pia wale wananchi ambao walikuwa wanakaa kwenye eneo ambalo Serikali ililininua mpaka sasa wengi wao hawajalipwa. Naomba Serikali katika mpango wenu mhakikishe ujenzi wa hospitali katika mikoa au manispaa mbalimbali unafanyika lakini pia bajeti yake ipangwe na kuonyeshwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nilitaka kuzungumzia kuhusiana na ukusanyaji wa mapato. Tunapozungumzia ukusanyaji wa mapato kama Serikali ya CCM miaka yote tunalalamika lakini mchawi ni nani? Kuna watu ambao hawalipi kodi lakini Serikali imekaa kimya, miradi inashindwa kutekelezwa, tuna mipango mizuri lakini kodi tunapata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lililopita 2010, kulikuwa kuna kashfa ya sukari, kuna watu ambao walihusika na kutoa vibali vya Serikali na wengine wakaenda kununua sukari nchini Brazil kuleta Tanzania. Hasara tuliyopata kwenye kashfa ile ya sukari ni zaidi ya shilingi bilioni 300. Wengi wao wengine tunawafahamu kwa majina akiwepo Mheshimiwa Mohamed Dewji. Kwa hiyo, naomba kabisa ile ripoti ya Kamati ya Bunge iletwe hawa watu washughulikiwe na walipe kodi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa kama hizi zinapotea kumbe tungeweza kufanya maendeleo kutokana na kodi hiyo. Kuna watu tunawaachia wanarandaranda na wanatumia pesa za wananchi. Kwa hiyo, naomba Serikali tuwe *strict* kuangalia ni mianya gani inayosababisha tunapoteza pato la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaposema tunahitaji kuwekeza katika elimu basi tuwakumbuke Walimu wetu kwa kuwalipa mishahara yao lakini pia tutengeneze mazingira mazuri katika shule zetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mchinga, Mkoa wa Lindi, kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kueleza huzuni kubwa niliyonayo kwamba Diwani wa Kata ya Kimwani, Jimbo la Muleba Kusini kupitia Chama cha Wananchi CUF jana ameua akiwa nyumbani kwake kwa kukatwakatwa mapanga. Tunashukuru Jeshi la Polisi tayari limekwishamkamata mgombea wa CCM ambaye alishindwa na tunaamini haki itatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza mipango ya kwenda kutatua changamoto za wananchi, lakini wenzetu mliopo madarakani hamkubali kushindwa. *This is very shameful to our country. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naanza kuchangia mapendekezo haya, niyakumbuke maneno ya Profesa mmoja Mchumi wa Uingereza lakini kwa bahati mbaya anafundisha mpira. Wiki iliyopita timu yake ilicheza na timu nyingine na kwa bahati timu yake ndiyo nilikuwa naishabikia. Baada ya matokeo timu yake ikawa imefungwa, anahojiwa na Waandishi wa Habari anasema, *we had good attitude and fantastic spirit despite the result. Anasema attitude ni nzuri, spirit ni fantastic lakini matokeo ni mabovu, wamefungwa. Ndiyo hili ninaloliona siku zote Tanzania tunapanga mipango mizuri, mipango ambayo inapoletwa ndani ya Bunge inapata sifa kubwa kwamba ni mipango mizuri na inatoa dalili ya matumaini kwa Tanzania lakini matokeo siku zote yamekuwa ni mabovu.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuishauri Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, asije mwisho wa siku akalalamika kama alivyolalamika kocha wangu mimi kwamba *good attitude and fantastic spirit despite the result* na ili yasimkute haya aangalie anumia mfumo gani kuwapata Watendaji Serikalini na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumesikia ametumbua majipu kwa Mabalizi. Hatuwezi kustaajabu kuona Mabalizi wetu wanafanya kazi chini ya kiwango, wanachukuliwa makada wa CCM walioangushwa kwenye Ubunge, wananchi wamewakataa, ndiyo wanakwenda kuwa Mabalizi, utatumbua tu. Napenda Mheshimiwa Magufuli asije akashindwa, aangalie mfumo wake wa kuwapata wasaidizi na watendaji wake ili mipango mizuri hii tunayoipanga iweze kuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Lindi, tuna changamoto kubwa Lindi ya misitu yetu kuvamiwa, sijui niwaite majangili wa misitu au niwaite watu gani. Mkoa wa Lindi ulikuwa ni miongoni mwa mikoa yenye hifadhi kubwa ya misitu, Hifadhi ya Selous iko kule lakini tuna hifadhi kubwa ya misitu ambayo wananchi na Serikali kwa nia nzuri kabisa tuliambia kui-*conserve* kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sisi Mkoa wetu wa Lindi unapatikana katika hali ya kitropiki ambapo mvua zetu tunategemea misitu na bahari. Waziri wa Muungano anayeshughulikia misitu naomba asikilize hili, kuna uvunaji wa kupita kiwango wa misitu ambao unawahusisha vigogo wa Serikali. Ndiyo maana mimi kama Mbunge na Wabunge wenzangu tumekuwa tukilalamika, tumekuwa tukiwaeleza Wakuu wa Wilaya, tumekuwa tukimueleza Mkurugenzi, kila siku misitu iliyohifadhiwa na Serikali inaisha na ukikamata mbao unakuta zimegongwa, tunapata shida. Hatuwezi kutengeneza mipango ya

maendeleo wakati rasilimali na maliasili hii tunaiacha ipotee hivihivi tu. Hawa watu hawalipi kodi na hata wakilipa kodi wanafanya *over harvesting* (wanavuna zaidi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ulichukue hilo, *very serious*. Tuna shida misitu Lindi inaisha, inapotea, mmeleta ng'ombe wengi wasiokuwa na idadi lakini hiyo ni nafuu, tumeweza kuwa-*accommodate*, hatuna migogoro ya wafugaji na wakulima, shida yetu kuna majangili wa kukata misitu hovyoy. Kuna msitu mkubwa wa hifadhi katika Jimbo la Mchinga, Msitu wa Nkangala unavunwa, Mkurugenzi anajua, Mkuu wa Wilaya anajua, Mkuu wa Mkoa anajua, naomba mchukue tahadhari katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uvuvi, mimi nashangaa kwelikweli. Jimbo la Mchinga ama Mkoa wa Lindi umepakana na Bahari ya Hindi, inafikia wakati samaki wanazeeke na kufa wakaja tu kuokotwa ufukweni hivi, maana yake kwamba ile bahari watu hawajavua na wavuvi hawajawezeshwa. Staajabu yenyewe kubwa iliyopo maeneo yote ambayo bahari imepitia ndiyo kuna watu maskini kwelikweli. Bahari badala ya kuwa ni faraja au kitega uchumi muhimu imegeuka kuwa laana kwani walio karibu na bahari wote ni maskini. *This is very shameful.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wenzetu wanatumia bahari tu uchumi wao umekuwa mkubwa sisi watu tuliokuwa karibu na bahari ndiyo maskini. Kwa bahati mbaya mnapopanga hii mipango, pangueni na namna ya kuwasaidia wavuvi, msipowasaidia ndiyo wanatumia zana haramu za uvuvi. Watu wanapiga mabomu, wanatumia makokoro na kadhalika, hatuwasaidii, tunabakia kulalamika tu kwamba achene uvuvi haramu, hawataacha kwa sababau hawana *alternative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri suala hili mlichukue, wakati mnakwenda kutengeneza huo mpango ambao mtau-*submit* tena, wekeni nguvu kwenye sualala uvuvi. Nilishukuru kweli, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 23 aliweka msisitizo kwa suala la uvuvi, alisema kwamba viwanda, uvuvi na kilimo ni ajenda yake. Naomba tuone kwa vitendo wakati mtakapo-*submit* Mpango wa Miaka Mitano au wa mwaka mmoja, tuone mmewekeza nguvu kubwa katika suala la uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, suala la viwanda, Mkoa wa Lindi na Mtwara imejaliwa. Imekuwa nyuma kimaisha kwa muda mrefu, uchumi wetu umekuwa wa chini sana lakini Mwenyezi Mungu ametuletea neema ya gesi ambayo ni utajiri na ni umeme pia. Tunashukuru Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo pamoja na REA wamejitahidi vijiji vingi hivi sasa vinapata umeme Lindi na Mtwara. Mie nashukuru Jimboni kwangu zaidi ya 80 % ya vijiji vimepata miradi ya REA. Naomba tu Mheshimiwa Muhongo unimalizie vile vijiji kumi na tano

vilivyobakia ili Jimbo zima liwe linawaka umeme. Haitakuwa upendeleo maana umeme unatoka kwetu, gesi ipo kwetu, tukiwa na umeme namna hii ni jambo la kheri na ndiyo wananchi watapunguza kelele ya gesi ibaki na mambo kama hayo. Tumelalamika, watu wakapigwa, tukaelimishwa tukaelewa, bomba limejengwa, sasa hivi tunalilinda, tuwekeeni umeme katika kila kijiji ili tuone sasa kumbe manufaa ya gesi ni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili liendane na viwanda. Tuna rasilimali nyingi, tuna maliasili nyingi, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo anajua, kuna madini mengi yako Lindi. Jimbo la Mchinga kuna madini mengi ya kutengeneza cement na vitu vingine ninyi wenyewe mnajua. Wasaidieni wachimbaji wadogowadogo waweze kupata mitaji ili wao waweze kuchimba. Tusiwaachie hao watu wanaanzisha viwanda, yeye ndio ameanzisha kiwanda, yeye ndio awe ana-transport minerals, tusifanye hivyo tutashindwa kutoa fursa kwa wananchi maskini hawa. Naomba nishauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ili mipango yetu yote iende vizuri tunahitaji tuwe na amani. Tunahitaji tuwe na amani ya kweli siyo amani inayozungumzwazungumzwa tu. Tunalalamika kuhusu suala la Zanzibar, Bukoba watu wanauana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kuwapa pole wananchi wangu Ulanga kwa janga la ajali ya kivuko. Ajali hii ya Ulanga siyo ya kwanza, nashangaa Ulanga sijui tumeikosea nini Serikali hii. Daraja mwaka wa tatu haliishi, miradi yote mikubwa inakuja inakwisha, ile ya Kigamboni imekwisha, mradi wa mabasi yaendayo kasi umekwisha, daraja la Ulanga haliishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wakandarasi waliopewa mradi ule kila mwaka wanaomba kuongezewa muda. Nashangaa wakati wanaomba kujenga lile daraja walikuwa hawajui kama kuna kipindi cha masika? Kwa mfano, sasa hivi hawapo, ujenzi hauendelei. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha alisimamie suala hili kwa sababu sasa hivi mafuta hayaendi Ulanga, bidhaa haziendi Ulanga, vile viboti vidogo walivyoweka kwa ajili ya kuwavusha watu mvua zikinyesha haviwezi kufanya kazi. Mimi mwenyewe shahidi juzi nilivyoenda nimenusurika kifo. Tumefika katikati ya mto boti limezimika. Kwa hiyo,

ili kuwanusuru wananchi wa Ulanga naomba tuwasaidie kile kivuko kisitumike tena, daraja liishe wananchi wanufaike na daraja lao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili, naomba nimpongeze Rais Magufuli na uongozi wote uliochaguliwa. Nampongeza Mheshimiwa Magufuli kwa utendaji wake, nawashangaa ndugu zangu Wapinzani wanasema kuwa Mheshimiwa Magufuli anatekeleza Ilani yao, sasa kama anatekeleza Ilani yenu mbona mnalalamika. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea Bungeni, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya familia, kwa ofisi za Bunge kwa namna walivyoshughulikia ugonjwa wa mama yetu mpendwa Celina Kombani, walivyoshughulikia shughuli yote ya msiba. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa mama yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa jinsi walivyolichukulia suala lile na kuchukua nafasi ya mzazi. Naomba waendeleo kutuchukulia hivyo hivyo kama watoto wao, hatuna cha kuwalipa bali tunawaomba maisha marefu yenye afya na mafanikio makubwa. Pia siwezi kusahau uongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa namna walivyotusaidia katika msiba ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Rais mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa uongozi wake mahiri wa miaka kumi kwa kutunza amani na utulivu. Pia napenda kuipongeza Serikali ya CCM kwa kusimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa demokrasia ya hali ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kusoma kwake hotuba kwa umahiri. Ila nilikuwa napenda kumwambia kuwa katika *level* ya Ubunge kuna vitu vya *ku-present* mbele za watu siyo kila anachoandikiwa asome. Akili za kuambiwa uchanganye na za kwako. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda *ku-declare interest* nimeoa mchaga, Mheshimiwa Mbowe ni mkwe wangu, sasa mkwe kuonyesha udhaifu mbele ya mkwe wake ni aibu. Tunapozungumzia Upinzani Bungeni tunamzungumzia Mheshimiwa Mbowe. Sasa naomba nimpe taarifa kuwa mkwe wake nipo humu Bungeni, hatakiwi kuonyesha udhaifu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mpango wa kuimarisha umeme vijijini, naomba niwape taarifa, kipindi cha masika Ulanga umeme haupatikani. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Muhongo umeme umefika Ulanga lakini zile

fito walizoweka za kupeleka umeme kipindi cha masika zote huwa zinavunjika kwa hiyo hatupati umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mto Kilombero pale unatuletea mafuriko kila mara. Naomba ufanyike mradi kama ulioko Mto Ruvu. Badala ya mto ule kutuletea mafuriko tutumie yale maji kwa kuyanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau upande wa viwanda, Ulanga kuna Kiwanda cha Pamba lakini hakijaingizwa katika mpango huo wa kufufuliwa. Nimeona sehemu zingine tu lakini Ulanga imesahaulika. Bila kusahau Morogoro, Morogoro ndiyo ulikuwa mkoa ambao unaongoza kwa kuwa na viwanda vingi lakini sasa hivi yamebaki magofu, sijaona mpango wa kufufua viwanda vya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi na kwa sababu ndiyo naanza haya yanawatoshia. *(Kicheko)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema aliyonijalia. Nawashukuru wanawake wa Dodoma kwa kunipenda tena na kunichagua kuwa Mbunge lakini pia Chama changu cha Mapinduzi. Nawapongeza sana Watanzania kwa uamuzi wa dhati walioufanya kwa kuichagua tena CCM kuitawala nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Goodluck amenifurahisha, nampongeza sana. Tunachofanya leo ni kuisaidia Serikali. Wameleta mwelekeo wa Mpango na tunatakiwa tujadili na kuwapa mawazo mapya ni wapi wanaweza wakapata mapato zaidi ili matumizi yaendane na mapato. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo kazi kubwa tuliyonayo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma taarifa ya Serikali na nimeona jinsi sekta ambayo Watanzania ni wengi ilivyochangia kwa kiasi kidogo sana, 4% ya pato la Taifa, ni sekta ya kilimo, uvuvi na misitu. Najuliza kwa nini sekta ya kilimo na ufugaji ichangie kidogo? Tanzania kila kona kuna ugomvi wa wakulima na wafugaji ina maana tuna mifugo mingi ambayo haileti faida ndani ya nchi, haichangii kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa. Ndiyo maana mifugo, kilimo, misitu, uvuvi imechangia 4% tu. Lazima tutafute ni wapi tulipokosea mpaka sekta hii isichangie pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Kuna mazao yanayotokana na mifugo mfano maziwa, ngozi, nyama na kuna mifugo mingi sana ndani ya Tanzania. Nadhani Serikali itafute sasa namna ya kushughulikia matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho siyo kupima ardhi ni kuwasaidia wafugaji kupunguza mifugo. Nilikwenda Mkoa wa Arusha kipindi fulani tukaambiwa, tena alisema mfugaji mwenyewe yeye ana ng'ombe 10,000. Kama mtu mmoja ana ng'ombe 10,000 na hana jinsi ya kupunguza mifugo yake lazima ugomvi wa wakulima na wafugaji utaendelea lakini hatuwezi kuona faida ya kuwa na mifugo mingi. Vilevile hatuwezi kuona faida ya wavuvi wakati maziwa tunayo yamezunguka nchi yetu; tuna Ziwa Tanganyika, Ziwa Viktoria lakini tuna bahari. Nadhani Serikali iangalie namna ya kutumia sekta hii kuzalisha kwa wingi. Tupate viwanda vya nyama, viwanda vya maziwa, viwanda vya kusindika samaki, viwanda vya matunda, tutaona ugomvi wa wafugaji na wakulima hautakuwepo tena. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumemuudhi Mwenyezi Mungu, siku hizi mvua hainyeshi inavyotakiwa. Kwa hiyo, tukiendelea na kilimo cha kutegemea mvua hatutafika mbali. Ndiyo maana mvua isiponyesha vizuri baada ya muda mfupi wananchi wetu wana njaa. Kwa hiyo, lazima tutafute namna ya wakulima wetu kuwa na ukulima endelevu. Bila hivyo, kila mwaka tutakuwa tunalia hatuna chakula, sekta ya kilimo haijachangia kwa kiasi kikubwa lakini hatuna mipango mizuri kwa wakulima na kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fukwe nzuri sana kuanzia Mtwara hadi Tanga, tunaweza kuzalisha kupitia fukwe zetu. Siyo lazima Serikali ifanye, tunaweza tukaingia ubia na watu binafsi. *National Housing* ni mfano mzuri, wana ubia na makampuni na watu binafsi na tunaona *National Housing* inavyofanya kazi kubwa katika nchi hii. Kwa nini tusiungane na sekta binafsi katika kuhakikisha kwamba nchi yetu tunapata mapato ya kutosha kwa ajili ya huduma za jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna madeni mengi. Wakandarasi waliotengeneza barabara wanatudai, wanaopeleka vyakula katika shule, inawezekana Mheshimiwa Magufuli amelipa hilo deni, lakini kipindi cha nyuma tulikuwa tunadaiwa na Walimu walikuwa wanadai kwa sababu hatuna mapato ya kutosha. Pia matumizi yetu, hata ukiangalia taarifa ya Waziri, ni makubwa kuliko mapato tuliyonayo, kwa nini matumizi yetu yasiendane na mapato? Hata kama nakisi inakuwepo, isiwepo nakisi kubwa kama iliyopo kwenye ripoti ya Serikali. Tusipoangalia namna tunavyotumia na namna tunavyopata mapato kwa kweli tutabaki kila siku miradi yetu ya maendeleo haikamiliki tukitegemea fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaolima Nyanda za Juu Kusini wanalima vizuri lakini masoko pia bado shida. Mwaka jana walipiga kelele sana mahindi yanaoza Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. Lazima tutafute masoko ya uhakika kwa wakulima wetu. Tanga kuna matunda mengi lakini hawana soko, hakuna

kiwanda. Bado kuna haja ya kuwa na uhakika wa masoko ya wakulima wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeangalia pia Kitabu cha Wizara, suala la utalii sikuliona vizuri. Kwa sababu utalii unachangia kwa asilimia kubwa katika pato la nchi yetu lakini sikuona mikakati iliyowekwa na Serikali kwa ajili ya kutangaza utalii wa ndani na wa nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze pia kuhusu *retention* kwa mashirika haya yanayoshughulika na mambo ya utalii; ukiondoa *retention* kwamba fedha zote ziende Hazina, TANAPA itakufa, Ngorongoro itakufa. Kwa hiyo, niombe kabisa suala la *retention* liangaliwe kwa mashirika ambayo aidha hayafanyi vizuri, lakini mashirika kama TANAPA, Ngorongoro, ambayo *retention* inawasaidia pia kutengeneza miundombinu kwa ajili ya watalii naomba *retention* yao wasinyang'anywe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nirudi kwangu Dodoma ambako wanawake wanapata tabu ya kubeba ndoo na kuamka alfajiri kwa ajili ya kutafuta maji. Suala la maji Wilaya ya Bahi tumeongea tumechoka. Tuliomba shilingi milioni 500 mwaka jana mpaka bajeti imemaliza muda wake mpaka tukaanza bajeti nyingine hatujawahi kuona hayo maji. Bahi maji ni ya chumvi mno hayafai kwa matumizi ya binadamu. Niiombe Serikali, wanapoangalia namna ya wananchi au miji ile midogo iliyoanza hivi karibuni kupata maji suala la Bahi lisiwekwe pembeni. Shida ya maji Kondo ni ya muda mrefu, tumeshalizingumza mpaka tumechoka. Suala la maji Wilaya ya Chemba wameshindwa hata kujenga Wilaya, hakuna maji pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Waziri wa Maji atakumbuka tumepiga kelele sana kuhusu suala la kilimo cha umwagiliaji na tuliambiwa bwawa kubwa sana linachimbwa pale Farkwa na bwawa lile lingesaidia wakulima wa mpunga wa Bahi, wakulima wa Chamwino, wakulima wa Chemba na baadhi ya wakulima wa Kondo lakini mpaka navyozungumza hilo bwawa utaratibu wa kujengwa sijauona. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ni kengele ya pili, lakini taarifa hii haina mpango wa Serikali kuhamia Dodoma.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia

afya njema sote kuwa hapa. Pia, shukrani za kipekee niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa namna ambavyo wameniamini na wakanichagua kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa mara ya kwanza Jimbo la Rufiji tumeweza kuandika historia kwa sababu katika nchi hii toka tumepata uhuru na toka mfumo wa vyama vingi ulipoanza haijawahi kutokea Rufiji kwa Mheshimiwa Rais kupitia Chama cha Mapinduzi kupata kura nyingi. Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi wote wa Jimbo la Rufiji. Pongezi pia nikupe wewe Mwenyekiti, naamini kwa uzoefu na uwezo ulionao wa kisheria utatusaidia na utaliongoza Bunge hili vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa Mpango huu wa Maendeleo kama ulivyowasilishwa, binafsi nina masikitiko makubwa sana kwa sababu sielewi sisi wananchi wa Jimbo la Rufiji tuna matatizo gani katika nchi hii kwa sababu katika Mipango yote ya Maendeleo Rufiji tumeachwa mbali kabisa. Labda nilikumbushe Bunge lako kwamba Rufiji tumechangia asilimia kubwa ya upatikanaji wa uhuru wa nchi hii, tukizungumzia Pwani lakini na Rufiji kwa ujumla. Pia Rufiji inabaki kuwa ni miongoni mwa Wilaya pekee ambazo tumeshawahi kuendesha Vikao vya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi lakini sasa ukiangalia Mipango mingi ya Maendeleo imetuweka mbali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza suala zima la kilimo kama lilivyozungumzwa katika ukurasa wa 17, napata tabu kabisa kwa sababu Mpango huu wa Maendeleo hauzungumzii kabisa ni namna gani Rufiji itarudi katika ramani ya kilimo. Sote tunafahamu kwamba Rufiji miaka ya themanini ndiyo Wilaya pekee ambayo ilikuwa na uwezo wa kulisha nchi hii. Tunalo Bonde la Mto Rufiji, bonde hili ni zuri sana na tunaiomba Wizara pamoja na Kamati zinazohusika basi kufikiria ni namna gani wataweza kuliendeleza bonde hili. Pia tunafahamu kuna baadhi ya miradi kwa mfano ule mradi wa RUBADA ambao ulikuja pale Rufiji, naamini kabisa mradi huu ni mradi ambao watu wameutengeneza kwa ajili ya kujipatia pesa na hauna faida yoyote kwa Wanarufiji. Kwa hiyo, naomba kwanza Serikali ikae chini na kufikiria ni namna gani wataweza kupitia kumbukumbu zote walizonazo ili kuangalia ufisadi mkubwa ambao umeshawahi kufanywa katika mradi huu wa RUBADA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Rufiji tunayo ardhi nzuri na ardhi kubwa isiyokuwa na tatizo lolote la migogoro ya ardhi, tunaiomba Serikali sasa kufikiria mpango wa kuanzishwa Chuo cha Kilimo Rufiji ili sasa kiweze kusaidia suala zima la kilimo kwa sababu tunayo ardhi nzuri sana. Pia mchakato wa uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao, naishauri Serikali uanzie Rufiji kwa sababu tunayo ardhi nzuri yenye rutuba na tunalo bonde zuri. Niseme tu katika nchi hii hakuna ardhi iliyo nzuri kama ya Jimbo letu la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika suala zima la viwanda, kumbukumbu zangu zinanionesha kwamba Mheshimiwa Rais pamoja na Makamu wake tarehe 9 Septemba, Makamu wa Rais alituahidi mchakato wa ujenzi wa viwanda Rufiji. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa hivi viwanda ambavyo vitajengwa kuanzia Rufiji kwa sababu kila aina ya kilimo sisi tunacho na tunaishauri Serikali sasa mchakato huu uanze haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye tatizo la maji. Ukurasa wa 46 wa Mapendekezo ya Mpango huu wa Maendeleo umezungumzia suala la maji. Sisi wananchi wa Jimbo la Rufiji pamoja na Majimbo ambayo tunakaribiana, nazungumzia Kisarawe, Mkuranga, Kibiti pamoja na Rufiji yenyewe, tuna shida kubwa sana ya maji. Labda niseme katika Jimbo langu ya Rufiji ni 5% au 6% tu ya wananchi ndiyo wanaopata maji safi na salama. Katika eneo dogo la Tarafa ya Ikwiriri ambayo ndiyo walikuwa wakipata maji safi mota imeharibika huu ni mwezi wa tatu. Mchakato wa tathmini ya utengenezwaji wa mota upo katika Wizara hii ya Maji, huu ni mwezi wa tatu hatujui Katibu Mkuu wa Wizara hii anafanya mchakato gani ili kuweza kuharakisha mota hii kuweza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoweza kuona maeneo mengine, Ziwa Viktoria wana uwezo wa kutoa maji sehemu moja na kupeleka sehemu nyingine katika Mikoa mbalimbali na sisi tunaishauri Serikali sasa Mpango huu wa Maendeleo kufikiria mchakato wa kuboresha huduma ya maji kwa kutoa maji katika Mto wetu wa Rufiji na kusambaza katika Wilaya zetu zote ambazo zinazunguka katika Jimbo la Rufiji, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo, kwa mfano kule Ngarambe kuna tatizo kubwa sana la maji. Akinamama pamoja na watoto wanawajibika kuamka alfajiri kwenda kuchota maji na wengine hawarudi majumbani, wanachukuliwa na tembo, wanauwawa na maeneo mengine wanachukuliwa na mamba! Kwa hiyo, shida ya maji katika Jimbo la Rufiji ni kubwa sana. Tunaomba Mpango huu wa Maendeleo kulifikiria suala hili la maji kwa kuliboresha vizuri kwa kutumia Mto wetu wa Rufiji katika kuliweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika suala zima la afya, mimi nina masikitiko tena makubwa. Niseme tu kwamba tunayo Hospitali yetu ya Wilaya pale iliyojengwa mwaka 60 lakini toka mwaka 60 hakuna ukarabati wowote ambao umeshawahi kufanywa. Mimi mwenyewe nilishaanza mapambano kuweza kuhakikisha kwamba tunapata wawekezaji kutusaidia. Sasa tunaiomba Serikali kuharakisha huu Mpango wa PPP ili wawekezaji wa kutoka Uturuki waweze kutusaidia kujenga hospitali ya kisasa kabisa ambayo itakuwa na *European Standard* yenye mashine zote za kisasa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kuharakisha Mpango huu wa PPP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukija suala zima la elimu, niharakishe kidogo kwa sababu ya muda, niseme tu kwamba sisi wananchi wa Jimbo la Rufiji tuko nyuma sana kwenye suala zima la elimu, hata Serikali imetuacha yaani tumekuwa kama watoto wa kambo, hatujui sisi tuna matatizo gani? Suala la elimu ni shida kubwa hasa ukizingatia Rufiji ni kubwa kuliko hata Mkoa wa Kilimanjaro lakini tuna shule moja tu ya sekondari ya kidato cha tano na cha sita kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa. Tunaiomba Serikali kufikiria mchakato wa kuboresha elimu katika Jimbo letu la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo, kwa mfano kule Mtanange na maeneo mengine watoto hawasomi kabisa kutokana na umbali wa shule za msingi ambapo mtoto inabidi asafiri umbali wa zaidi ya saa tano, saa sita kwenda kufuata shule. Hali hii imewafanya wazazi wengi kushindwa kuwapeleka watoto wao shule. Kwa hiyo, naona kabisa kwamba mchakato huu wa elimu bure sisi wa Rufiji tutaachwa kando kabisa kwa sababu wazazi watahindwa kuwapeleka watoto wao shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija suala zima la mchakato wa benki, mimi niseme Rufiji ni Wilaya ya sita wakati wa mkoloni na ni Wilaya ya 21 wakati tunapata uhuru lakini utashangaa Wilaya hii ya Rufiji kwa namna ambavyo Serikali imeamua kuiacha hatuna hata benki kabisa. Tunawajibika kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa 120, kwa wale wananchi wanaotoka kule maeneo ya Mwaseni na Mloka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishauri Serikali huu mchakato wa uanzishwaji wa Benki za Ardhi, kama ulivyoainishwa katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 35, tunaiomba Serikali sasa kufikiria benki hizi waanze kujenga katika Jimbo letu la Rufiji kwa sababu tunayo ardhi ya kutosha, hatuna migogoro ya ardhi, ardhi ni bure kabisa tunawakaribisha lakini tunaiomba Serikali pia kuona namna gani ya kuwekeza kwenye suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika suala zima la miundombinu, nina masikitiko haya mengine kwamba Rufiji japokuwa ni Wilaya ya zamani lakini tunabaki kuwa ni Wilaya pekee ambayo hatuna hata nusu kilometa ya lami. Kama tulivyoona Mapendekezo haya, hakuna hata sehemu moja ambayo inazungumzia Rufiji tutasaidiwa vipi kuboresha miundombinu yetu. Mama yetu Makamu wa Rais pamoja na Rais mwenyewe alituahidi kwamba tutajengewa lami barabara ya kutoka Nyamwage - Utete, ili iweze kusaidia kupunguza vifo vya akina mama ambao inabidi wakimbie Utete kwa ajili ya kwenda kujifungua. Pia barabara ya kutoka Ikwiriri – Mwaseni - Mloka yenye kilometa 90, tunaiomba Serikali kuharakisha mchakato wa ujenzi wa barabara hii na barabara nyingine kutoka Mwaseni - Mloka - Kisaki pamoja na kutoka Mwaseni - Mloka - Kisarawe.

Barabara hizi iwapo zitajengwa zitasaidia kufungua biashara na wananchi wa Jimbo langu la Rufiji wataweza kufanikiwa katika mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaishauri Serikali na tunaiomba iharakishe mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Utumishi pale Ikwiriri. Tulishatoa ardhi kubwa lakini mpaka leo hii Wizara husika haijachukua hatua zozote za mchakato wa ujenzi wa Chuo hiki cha Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaishauri Serikali kuachana kabisa na mchakato huu wa mambo ya *retention*. Suala hili litatuletea shida kubwa na tunaiomba Serikali kuepokana nalo, kuacha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishauri Serikali kuanzisha *community centre*. *Community centre* hizi zitaweza kusaidia wananchi wetu kwa maeneo mbalimbali ya vijiji ili waweze kujifunza mambo mbalimbali kwa ajili ya kunyanyua uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naomba maombi yangu haya yote kama nilivyozungumza yaweze kuchukuliwa na kufanyiwa kazi. Vinginevyo kama Serikali haitachukua basi sitaunga mkono kabisa mapendekezo mwezi Machi yatakapoletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru Mungu kwa sababu ya kutuwezesha sisi sote kushinda uchaguzi mwaka jana na kuingia kwenye Bunge hili. Kipekee kabisa nipongeze Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Vyombo vyao kwa kusimamia uchaguzi huo vizuri. Kwa kufanya hivyo, wameniwesha mimi na mdogo wangu Mchungaji Msigwa, kuingia kwenye Bunge hili. Ahsante sana Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo katika Mpango uliowasilishwa. Kwanza, natambua kabisa kwamba yako maeneo mengi ambayo Mpango umejielekeza na hasa upande wa barabara na reli. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, naomba nisisitize tu kwamba sisi Watanzania tunaamini kwamba uboreshaji wa Reli ya Kati ile tunayoijua yaani ya kwenda Kigoma – Mwanza baada ya pacha ya Tabora ndiyo tunayoisema na matawi yake ya kwenda Mpanda. Mikoa kumi na tano itanufaika na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwa ufupi, Tanzania ilivyo na hasa Wilaya ya Makete na Mkoa wa Njombe, ni Mkoa ambao ni tegemeo kubwa sana kwa sababu ya uchumi wa Tanzania na hasa uzalishaji wa mazao ya chakula. Naomba sana barabara inayotoka Njombe - Mbeya kupitia Makete ipewe kipaumbele kwa sababu hata Ilani ya CCM imeiweka barabara hii ni barabara ya kwanza. Umuhimu wa barabara hii si tu kwa sababu Norman Sigalla King anatoka Makete ni barabara muhimu kwa maana ya uchumi wa Tanzania kwa sababu Hifadhi ya Kitulo ndiyo hifadhi pekee ya maua Afrika. Hifadhi hii ili iboreshwe ni lazima miundombinu ya barabara za lami iwe bayana na hii itasaidia kukuza utalii ndani ya hifadhi hii na si tu kukuza utalii lakini pia kuboresha uchumi wa Wilaya ya Makete. Kwa sababu Wilaya ya Makete pamoja na uchumi wa mazao ya chakula pia ndiyo Wilaya ambayo inaongoza baada ya Mafinga kwa mazao ya mbao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni jambo la muhimu sana, niishukuru Serikali ya CCM kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuboresha elimu. Wilaya ya Makete pale tuna Chuo cha VETA, bahati mbaya sana yako madarasa lakini hakuna mabweni. Wilaya ya Makete kwa jiografia yake haiwezekani wanafunzi wa kutoka Tarafa za Matamba, Ikuo, Lupalilo, Ukwama, Bulongwa kwenda kusoma kwenye chuo kilichoko Iwawa-Makete. Ni muhimu sana Serikali ijenge mabweni ili kunufaisha wananchi wa Tarafa zote ikiwemo Taarifa ya Magoma. Hili nimeliwasilisha kwa Waziri mhusika, naomba sana kwenye Mpango wetu wa Maendeleo tufasili kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu pia naomba nisisitize jambo moja. Mtihani tulionao sasa ukisikiliza hotuba ni kana kwamba muhimu kwa Watanzania ni kupata shahada ya kwanza, ya pili ama ya tatu. Mtihani tulionao sasa ni aina ya elimu tunayowapa watoto na watu wetu. Sote tunajua nguvu ya uchumi wa Tanzania ni kilimo, asilimia 77 ya watu wetu wanategemea kilimo. Hata hivyo elimu yetu kuanzia darasa la kwanza mpaka chuo kikuu hakuna mahali ambapo mwanafunzi anakutana na kilimo. Ni hatari sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamarekani na nchi zilizoendelea nguvu yao ni kwenye teknolojia ndiyo maana mtoto wa Kimarekani wa miaka nane au kumi anacheza na komputa, ana-feed data na analipwa. Kwao Wazungu wanasema hiyo siyo *child labour* lakini Mwafrika, Mtanzania akibeba jembe akiwa na miaka kumi na mbili, kumi na tatu tunamfundisha kilimo ambacho ndiyo nguvu yetu tunasema *child labour*. Tunaingia kwenye ugonjwa huu, matokeo yake tutakuwa na wanafunzi wanao-graduate kwenye level ya digrii ya kwanza, ya pili na ya tatu lakini hawana mahali pa kutumia elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, baada miaka ile mitatu ya kujua kusoma na kuandika kwa watoto wetu ni muhimu sana watoto hawa wajifundishe ABC ya kilimo, siongelei kilimo nadharia, kilimo vitendo. Mtu

anatoka Kanda ya Ziwa basi ajue akifika darasa la saba ni jinsi gani ya kutumia mbolea kulima pamba, kama anatoka Nyanda za Juu Kusini kwa mfano ajue kwa nini tunatumia *DAP* na kwa nini tunatumia *urea*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dozi hiyo ya *course* inaongezewa uzito anapomaliza kidato cha Nne ili tuwe na Watanzania ambao wakihitimu kidato cha nne hawana haja ya kutafuta shahada maana elimu waliyonayo inatosha kujitegemea. Nafikiri hili Wizara ya Elimu iliangalie kwa namna ya kipekee sana maana vinginevyo tutajuta kwa sababu tutakuwa na watu wengi walio-*graduate*, lakini hawana mahali pa kutumia elimu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusisitiza umuhimu wa Bwawa la Lumakali. Kaka yangu Mheshimiwa Profesa Muhongo yuko hapa. Mto wa Lumakali ambao uko Bulongwa, Wilaya ya Makete, ni kati ya mito michache katika Tanzania ambayo haipungui maji kwa miaka 40 sasa ya utafiti. *Document* ambayo ni *official* ya *TANESCO* inaonyesha kwamba umeme unaotakiwa kuzalishwa kwa kutumia mto ule ni *megawatts 640* hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali itekeleze mradi wa Lumakali kwa sababu utasaidia sana kutoa ajira kwa wananchi wa Makete, Mbeya na Njombe kwa sababu ni bwawa kubwa lakini pili utasaidia sana kuongeza umeme wetu. Mheshimiwa kaka yangu Profesa Muhongo chondechonde, naomba sana Mto Lumakali upewe nafasi yake ya kipekee kabisa ili Wilaya ya Makete ipate kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe hotuba yangu kwa kuongelea umuhimu wa kuunganisha barabara ya kutoka Ludewa - Mlangali. Niipongeze Serikali kwa sababu ya kufungua barabara hiyo lakini ni vizuri ifunguliwe kwa kiwango cha lami kutoka Mlangali - Lupila kutokea Ikonda - Makete, kutoka Chimala - Matamba - Kitulo - Mbeya, kutoka Mbeya - Ishonje - Makete - Njombe na kutoka Makete - Bulongwa - Iniho - Ipelele - Isonje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mungu akubariki na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia Mpango ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa suala zima la upunguzaji wa umaskini. Katika jamii watu ambao ni maskini kuliko wote ni watu wenye ulemavu kwa sababu ulemavu unasababisha umaskini na umaskini unasababisha ulemavu. Pia niseme kwamba hapa Tanzania *statistics* tunazotumia katika kuelezea idadi ya watu wenye ulemavu katika nchi hii zina

upungufu mkubwa. *Tanzania Bureau of Standard* wanasema asilimia nne, tano au milioni mbili ndiyo watu wanaoishi na ulemavu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa sensa hakuna ushirikishi katika kuhakikisha kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yanajumuishwa katika sensa. Kuna ulemavu wa aina nyingi mwingine unaonekana kama mimi nilivyo sioni, naonekana kama sioni, lakini kuna ulemavu ambao hauonekani (*hidden disability*) kama viziwi au watu wa *pyschosocial*, watu wa *down syndrome*, *dyslexia*, huwezi kuona. Kwa hiyo, wanapofanya zile sensa wanasahau kujumlisha aina nyingi sana za ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mipango yetu katika Wizara zote tufuate ile *statistic* iliyotolewa na *WHO* pamoja na *World Bank* kwenye *Disability World Report* ya 2011 inayosema kwamba katika kila nchi asilimia 15 ni watu wenye ulemavu. Sasa basi sisi Tanzania ambao tuko milioni 46 mpaka 50 tukitumia hiyo *statistic* ya *World Report* ina maana kwamba watu wenye ulemavu nchi hii ni kati ya milioni 6.2 mpaka milioni 7.0, hii si idadi ndogo. Naomba Mipango inapopangwa itumie hiyo ripoti mpaka hapo itakapofanyika sensa nyingine ya kuonyesha jinsi *data* ya watu wenye ulemavu itakavyokuwa *captured* katika sensa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ulemavu unasababisha umaskini na umaskini unasababisha ulemavu, unakuta watu wenye ulemavu wako katika hali mbaya. Nataka kusema kwamba hii bajeti inayokuja izingatie kuweka bajeti kwa ajili ya maendeleo ya watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, mtu asiyeona akitaka kwenda hospitali inabidi aende na msindikizaji au kiziwi inabidi aende na mkalimani na unapokwenda na msindikizaji ina maana kwamba unalipa nauli yako na ya msindikizaji wako na kiziwi inabidi alipe nauli yake na ya mkalimani wake. Ina maana kwamba *spending* ya mtu mwenye ulemavu ni mara mbili kuliko ya mtu asiyekuwa na ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo basi naomba familia zile zenye watu wenye ulemavu ambao ni *severely disability*, kuna familia ambazo zina watoto wenye ulemavu ambao hawawezi kutembea, hawawezi kuongea, hawawezi chochote na anahitaji uangalizi masaa 24 siku saba. Hizi familia ni nyingi, nimeshaanza kufanya *data collection*, wafikiriwe kupewa *cash* ya kuwawezesha kuishi. Kwa mfano, hawa akinamama ambao wanatunza watoto ambao ni *severely disabled* hawana nafasi kabisa ya kufanya kitu chochote kile cha kuwasaidia kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaposema itafikiria *pension* kwa wazee, ifikirie pia *pension* kwa wale *members of family* ambao hawana

nafasi hata kidogo ya kutafuta kibarua ili aweze kuishi. Mtu anakuwa na mtoto mwenye ulemavu kuanzia asubuhi mpaka jioni na siku zote hana nafasi ya kutafuta chakula. Kwa hiyo, nao wapewe hiyo *pension* angalau hata Sh.30,000 kwa mwezi kwa maana ya Sh.1000 kwa siku ili waweze kununua chakula cha kuishi kwa sababu hawana nafasi kabisa ya kushughulika na shughuli za kujiongezea kipato. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *cash transfer* wenzetu wengine wameshaanza ku-*effect*, nchi kama Malawi na Kenya. Nafikiri sisi siyo maskini kuliko Malawi lakini wanafikiria pamoja na wazee na wale *severely disabled people* wapewe hiyo *cash transfer* ili waweze kuishi. Utakuta wengi ambao wanaachwa na hawa watoto ambao ni *severely disabled* ni akinamama kwa sababu baada ya mama kupata mtoto mlemavu au mtoto aliyelemaa, waume zao huwakimbia na kuwaacha akinamama wakihangaika na hao watoto. Naomba Serikali ifikirie kuwapa jinsi kuishi hizi familia ambazo zina walemavu ambao ni *severely*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nilioutoa, kuna wafanyakazi ambao wana ulemavu matumizi yao yako juu, Serikali inaonaje kuanza kuwapunguzia ile *tax* ya *Pay As You Earn (PAYE)* kwa sababu hizo nilizoieleza. Mtu mwenye ulemavu anatumia zaidi kuliko mtu asiye mlemavu. Kwa hiyo, Serikali imsaidie yule anayefanya kazi kwa kumpunguzia kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, wenzetu wa Kenya Serikali yao ilishaona hili miaka mitano iliyopita, sasa hivi mwenye ulemavu yeyote pale Kenya anayelipwa mshahara wa kuanzia Sh.1-150,0000 ya Kenya ina maana Sh.3,000,000 ya Tanzania, inapozidi Sh.151,000 ile Sh.1 ndiyo wanaanza kuitoa kodi lakini ile Sh.150,000 wanamuachia kwa sababu wanajua matumizi ya mtu mwenye ulemavu ni makubwa. Naomba Serikali hii ifikirie katika jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika suala la elimu, kweli elimu imetolewa bure mpaka kidato cha Nne. Nategemea watoto wenye ulemavu pamoja na kwamba watasoma bure lakini vifaa vyao ambavyo vingi havipatikani hapa Tanzania vinaagizwa, vitabu vyao vinachapishwa katika maandishi ambayo wanaweza kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ina mtambo wa kuchapisha vitabu vya wasioona lakini huu mtambo kwa miaka mingi umefanya kazi chini ya kiwango chake. Hauna vifaa, hauna fedha za kununua makaratasi, matokeo yake ni kwamba watoto wasioona ambao wanahitaji *braille* na wale wa uoni hafifu ambao wanahitaji *large print* hawana vitabu vya kiada katika shule mbalimbali hapa nchini. Serikali kupitia Wizara ya Elimu ifikirie kukiboresha

kile kiwanda cha kuchapisha vitabu vya wasioona na wale wenye uoni hafifu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala lingine la uchukuzi. Kama Waheshimiwa Wabunge wengi mnavyojua usafiri wa bodaboda unasababisha vifo na ajali nyingi na vina-*create* ulemavu kwa watu wengi sana hapa nchini. Baada ya miaka mingi mtakuta Watanzania wamelemaa kwa ajili ya hizi bodaboda. Nashauri Serikali iweke *measures* za kusimamia hawa waendesha bodaboda, aidha wawapatie *training* au watafute njia nyingine ili kupunguza watu wanaolemaa migongo, wamekatika miguu kutokana na hizi ajali nyingi zinazosababishwa na bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi tena katika suala la viwanda, tunasema kwamba kuna mkakati wa kufufua viwanda. Naomba Serikali ikumbuke kwamba watu wenye ulemavu pia wanahitaji ajira, hivyo viwanda viwe *accessible* ili waweze kuajiriwa kama wanavyoajiriwa Watanzania wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilisikitika kwa vile nilinyoosha mkono niulize swali la nyongeza sikuipata nafasi. Waziri alipokuwa anazungumzia Morogoro akasema kuna asilimia tano ya fedha za TASAF kwa ajili ya wanawake, asilimia tano kwa ajili ya vijana, kwa nini hakuna asilimia tano kwa ajili ya watu wenye ulemavu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kusema kwamba Tanzania iliridhia ule Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa 2006 na pia ikaja na Sheria Na.9 ya 2010 kuhusu Watu Wenye Ulemavu. Naomba sasa *implementation* ya hizi sheria ifanyike kwa sababu hakuna maana ya kusaini na *ku-ratify and then* hakuna *implementation*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuomba Serikali isaini ule Mkataba wa Kimataifa kuhusu *copyright* kwamba watu wenye matatizo ya kusoma maandishi ya kawaida wakiwepo wasioona, wenye uoni hafifu, wenye *dyslexia*, wenye *down syndrome*, wale *publishers* wa-*publish* kazi zao kwa maandishi ambayo ni *accessible* ili watu wenye ulemavu waweze kusoma vitabu. Naomba Serikali isaini na kuridhia ule Mkataba ili na sisi watu wenye ulemavu wa kutoweza kusoma maandishi ya kawaida tufaidike na *treaty* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa. Vilevile niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Siha kwa kuniamini kwamba naweza nikawawakilisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni kwa Mwanri.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Jafo anamjua Mwanri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwa kusema kwamba kama kweli tunataka kuitoa Tanzania kutoka sehemu moja kwenda nyingine ni lazima tuwe na tafakuri ya juu sana katika kuamua ni namna gani tunatumia rasilimali za nchi yetu. Hata hivyo, nimshukuru Rais John Pombe Magufuli kwa sababu kwa muda mrefu watu wamekuwa wakisema kwenye jengo hili kwamba kuna ufisadi, kuna ubadhirifu wa rasilimali za nchi, yeye amekuwa shahidi namba moja, twendeni tukapambane na huo ufisadi. Amekuwa shahidi yetu kwamba yaliyokuwa yanasemwa kwa miaka yote ni kweli kabisa. Sasa wote kwa umoja wetu bila kujali vyama vyetu twendeni tujikoki silaha zetu tukapambane kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia ardhi kwa Wilaya ya Siha. Wilaya ya Siha ina eneo kubwa la ardhi ambayo haitumiki inaitwa ardhi ya Serikali ni zaidi ya heka 32,000, zipo tu na hakuna matumizi yoyote. Vilevile ardhi ambayo haiendelezwi vizuri inayosemekana Ushirika wameishika ni zaidi ya heka 14,000 na ardhi ambayo inasemekana wawekezaji wamemiliki ni zaidi ya heka 39,000. Ukijumlisha heka zote unakuta kuna heka 120,000 na zaidi. Unakuja kugundua ardhi hiyo kwa heka ni zaidi ya wananchi wa Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi na Mawaziri wengine wahusika nimewaeleza na wamenisaidia, wamenisikiliza vizuri. Niseme karibuni Wilaya ya Siha, karibuni Mkoa wa Kilimanjaro kwa sababu ni mkoa mdogo sana na matumizi yake ya ardhi yanatakiwa yaangaliwe kwa jicho tofauti na kwingine ambako kuna mapori makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niombe, tuna shamba ambalo lina ukubwa wa heka 3,429 linaitwa shamba la Gararagua. Ni shamba ambalo linasemekana linamilikiwa na *KNCU*. Shamba lina miundombinu ya maji ndani yake ambayo ndiyo *backup* ya maji ndani ya Wilaya ya Siha na kwenye Halmashauri lakini shamba hili anauziwa mwekezaji ambaye anakuja kulima maparachichi na mwingine kufuga kufuga kuku. Tuna uzoefu na huo uwekezaji wa maparachichi, nimeuliza ndani ya Wilaya ya Siha unaiingizia Halmashauri

shilingi ngapi hamna chochote zaidi ya maparachichi yaliyoharibika kulipiwa ushuru wa geti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu anataka kuongezewa eneo lingine ukipiga bei kwa kila heka yeye anaenda kuchukua kwa Sh.2,000,000 kwa heka moja. Ni heka moja yenye maji ndani yake thamani yake ni kubwa mno. Tutafute tafakari ya juu ya namna gani tutatumia hiyo ardhi kwa maslahi ya Taifa letu. Kwa sababu tukimjenga mwananchi wa chini ili aweze kuzalisha vizuri, alipe kodi na akapata ardhi nzuri ndivyo ambavyo tutaweza tukasema tunaweza kutekeleza bajeti tuliyonayo kwa sababu hatutegemei hela kutoka Serikali Kuu, tunategemea hela kutoka kodi wanazolipa wananchi wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionye tu kuhusu shamba hili, mwekezaji ambaye alipewa na *KNCU* kwa muda wote wa miaka mingi toka nikiwa mtoto akichangisha Sh.50,000 kwa kila mwananchi kukodisha kulima mazao. *KNCU* wanasema wanataka kuuza hili shamba kwa sababu wana deni la Sh.4,000,000,000 wanalodaiwa na *CRDB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wetu kama Wilaya na Mkoa kabla ya kusema unauza shamba hili, tujulize aliyechukua Sh.4,000,000,000 kutoka Halmashauri kwa nini alishindwa kurejsha? Kama ni jipu litumbuliwe kabla ya kwenda kusema unaenda kurudisha hela za *CRDB*. *KNCU* inajulikana kwamba imekuwa kidonda ndugu kwa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kuua zao la kahawa na kufanya mambo mengine ambayo wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro hawaridhika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuonyesha kuna tatizo hapa, nimetembelea mashamba zaidi ya 23 niliyoyazungumzia lakini nilipofika katika hili shamba la Gararagua mwekezaji aliyeko pale aliagiza walinzi wake wanizuie nisiingie kwenye shamba. Nilipoingia alienda Polisi kusema nimemwingilia shambani kwake. Cha kusikitisha amepiga simu toka Dar es Salaam, Polisi na Serikali ya Wilaya ya Siha ikawa inakimbiakimbia inanitafuta mimi, nikajjuliza kazi ya Mbunge ni nini? Sisi tumechukua silaha zetu tunakwenda kutumbua majipu watu wachache ambao wanahisi majipu yao tunaenda kuyatumbua wanaamsha Serikali yetu inapingana na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa kwenye Wilaya au Mikoa yetu kuna shida moja mnapokuja ziara. Nashauri muanzishe utaratibu mzuri kama aliouanzisha Mheshimiwa Mwigulu kwamba kabla ya kwenda eneo fulani anaonana na watu wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la la elimu. Nielezee kitu cha tofauti, imesemekana elimu ni kitu ambacho tunaenda kukiangalia kwa jicho lingine. Nimshukuru Mheshimiwa Ndalichako, naamini unaweza ukaenda

ukafanya hilo lakini tuangalie pamoja na kwamba tutaboresha shule, tutaboresha kila kitu lakini tuna eneo ambalo tunatakiwa tuliwekeze nalo ni eneo la mtoto na uwezo wa akili wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni tuwekeze katika lishe ya watoto wetu ili tunapowapeleka shule basi ukuaji wa ubongo uwe umekua vizuri ili aweze kupata kile kinachotakiwa. Kwa sababu wenzetu wametuzidi kiteknolojia siyo kwa sababu tu wana rasilimali nyingi au wana vitu vingi ni kwa sababu wana watu wenye uwezo wa kufikiri zaidi ya kufikiri katika ubongo (*thinking beyond the brain*). Tunatakiwa na sisi tuanze kujenga watu wenye uwezo huo ili tuweze kuwekeza kwenye teknolojia. Kama hatujawekeza vizuri kwenye ubongo wa mtoto kwa maana ya ukuaji pamoja na elimu nzuri hata kama tutajenga vyuo vikuu vizuri namna gani hatutakuwa na ubongo wa kuweza kuelewa teknolojia ambayo tunaitaka tuitengeneze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala kilimo. Wilaya ya Siha ni Wilaya mojawapo iliyozunguka Mlima Kilimanjaro lakini utalii huo haufaidishi Wilaya ya Siha na vilevile tunahitaji tuboreshe miundombinu iliyozunguka Wilaya hiyo. Ukiangalia barabara ambayo inapitia ile *Kisimiri Corridor* kwenda *Londrosi Gate* imechimbika sana na Rais ameahidi kuishughulikia na nasikia kwamba tayari *procurement* imeshafanyika kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami imebaki kusainiwa mkataba. Naomba hilo suala liharakishwe kwa sababu magari yamekuwa yakianguka katika barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuboreshe eneo la kilimo, wananchi wamekuwa wakizalisha mazao mengi lakini wakati wa mavuno mipaka yetu imekuwa ikufungwa. Nina zao moja katika Jimbo la Siha ambalo wananchi wako tayari kulima hata mashimo wanyeshee nalo ni zao la nyanya. Cha kushangaza wanapovuna mahindi mengi wanakosa pa kuuza. Naomba ikiwezekana wananchi wakivuna waruhusiwe kuuza popote wanapoweza kuuza ili kuhamasisha mazao ya chakula kuzalishwa na hata wananchi wawe tayari kuchimba mashimo watafute maji ili wanyeshee na tutaweza kuzalisha chakula kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Siha wamekuwa wakizalisha zao la kahawa. Naomba Waziri wa Kilimo tusaidiane...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na afya na kutuwezesha kukusanyika katika Bunge hili la Kumi na Moja la Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili la Kumi na Moja, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunipa fursa nyingine ya kuwaongoza kama Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo. Niwaahidi tu kwamba nitawatumikia kwa juhudi zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa hoja hii ambayo imewasilishwa ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa mwaka 2016/2017. Niipongeze Serikali kwa kutoa kipaumbele kwa ujenzi wa viwanda kama mkakati maalum wa kuendeleza ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa nchi yetu. Huu ni mkakati sahihi ambao unajipanga moja kwa moja kupiga vita umaskini katika nchi yetu na mkakati ambao utawezesha kuzalisha ajira nyingi na kuwaondoshea kadhia vijana wetu wa kiume na wa kike ambao wanahitimu katika vyuo vyetu mbalimbali na shule mbalimbali, wanaingia katika soko la ajira na kukosa ajira. Niwapongeze kwa hilo, huu ni mkakati sahihi ambao tukienda kwa kasi hii kwa miaka mitano bila shaka nchi yetu itakuwa katika hali nyingine kabisa na kujenga maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa viwanda huu utatumia malighafi za ndani za kilimo, mifugo, misitu na uvuvi lakini viwanda pia vitazalisha bidhaa kadha wa kadha ambazo tunazihitaji kwa ajili ya matumizi ya wananchi wetu. Pia zitazalisha ajira kama nilivyosema hapo awali lakini pia viwanda hivi vitawezesha kulipa ushuru na kodi mbalimbali ambazo ni fedha nyingi zitakazowezesha Serikali yetu kuwa na mapato makubwa zaidi na kuiwezesha Serikali kuweza kumudu huduma za jamii katika nchi yetu. Sina namna bali kuunga mkono na kupongeza juhudi hii katika Mpango huu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali yangu kupitia Wizara ya Fedha na Mpango kwamba wakati tunaweka mkazo huu wa ujenzi wa viwanda, tufahamu kwamba viwanda hivi hivi vinajengwa ardhini. Kwa hiyo, jambo muhimu sana katika Mpango huu ni kuhakikisha kwamba Serikali inamiliki ardhi ili iweze kujenga viwanda hivi. Maeneo yote yale ambayo tunahitaji kujenga viwanda katika mwaka huu unaofuata wa fedha Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba ardhi ile imemilikiwa na Serikali ili mkakati mzima wa ujenzi wa viwanda usije ukaingia katika matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu Bagamoyo tuna mpango maalum wa uwekezaji ama SEZ ambao unajumuisha ujenzi wa viwanda na Bandari ya Mbegani. Katika eneo hili, Serikali tayari imeshatambua eneo la ujenzi wa viwanda hivyo au eneo la uwekezaji. Mwaka 2008 uthamini wa ardhi umefanywa na jumla ya shilingi bilioni 60 zinahitajika kulipwa fidia, lakini hivi sasa mwaka 2016 katika shilingi bilioni 60 zile bado wananchi wanadai shilingi bilioni 47 kwa maana asilimia kubwa ya wananchi bado hawajalipwa fidia. Huu ni mwaka tisa wananchi hawajalipwa fidia lakini mwaka wa tisa pia tumepoteza fursa kadhaa za uwekezaji wa viwanda kwa vile wawekezaji hawatoweza kuweka viwanda ardhi haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka tisa ambayo tumepoteza ushuru na kodi mbalimbali lakini miaka tisa pia ambayo tulipoteza fursa za ajira mbalimbali kama viwanda vingekuwa vimejengwa. Kwa hiyo, naomba niikumbushe Serikali yangu katika mkakati huu na Mpango huu wa maendeleo kuweka mkazo wa kumaliza ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Bagamoyo ambao wamekuwa tayari kutoa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na ujenzi wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo wezeshi la ujenzi wa viwanda ni ujenzi wa bandari. Nashukuru Serikali katika Mpango huu wa Maendeleo ukurasa wa 28 umeonyesha kwamba Serikali itajipanga kujenga bandari mpya ya Mwambani Tanga na Mbegani Bagamoyo. Hii ni fursa kubwa ya kiuchumi, bandari ni fursa pekee za kiuchumi ambazo mataifa mengine yametumia vizuri kama Singapore na nchi zingine na kuwawezesha kujenga uchumi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamasishe Serikali yangu kwamba katika Mpango huu tusichukue muda mrefu na hasa pale ambapo mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo umeshasainiwa kati ya nchi yetu na nchi rafiki ya China na Oman. Wenzetu hawa hawatapenda kupoteza muda. Kwa hiyo, tujipange vizuri sana katika mwaka wa fedha unaofuata kuhakikisha kwamba maandalizi ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo yanakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba viwanda hivi na bandari hizi zinajengwa katika ardhi, wananchi katika Jimbo langu la Bagamoyo eneo ambalo litajengwa bandari, wananchi wa Pande na Mlingotini wako tayari hivi kuhama ili kupisha ujenzi wa bandari hiyo. Haikuwa rahisi sana wao kukubali lakini kwa sababu ya maendeleo ya Taifa letu wamekubali wahame kwa ajili ya kupisha ujenzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari eneo limetengwa shamba la Kidagoni ambalo awali lilikuwa shamba la NAFCO lakini sasa lina mwekezaji binafsi. EPZ tayari imelianisha shamba hilo kwa ajili ya kuingizwa kwenye mradi wa uwekezaji. Tatizo ni kwamba ardhi hiyo inalazimika iweze kulipiwa fidia ili

wananchi hawa waondoke katika maeneo ya ujenzi wa bandari wakabidhiwe eneo lingine na wao wako tayari kuhama hata leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kilio chao kikubwa ni kwamba wana ndugu zao, jamaa na marafiki ambao wanaondoka duniani, hawapendi kuwazika pale Pande na Mlingotini kwa vile ardhi hii sasa hivi itachukuliwa kwa ajili ya bandari lakini hawana namna ya kwenda Kidagoni kabla Serikali haijalipa fidia ya Kidagoni ili wakabidhiwe eneo hilo. Naiomba Serikali yangu Tukufu ijitahidi haraka na kuweka msisitizo wa kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja mapema iwezekanavyo shamba lile liwe limelipiwa fidia na wananchi wa Pande na Mlingotini waweze kuhamia katika eneo hilo na ujenzi wa bandari usiweze kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la uwezeshaji kwa uchumi wa viwanda ni nishati. Nimefurahi kwamba katika Mpango huu wa Maendeleo, nishati imeainishwa vizuri na msisitizo mkubwa umewekwa katika usambazaji wa nishati katika nchi yetu kuwezesha viwanda na wananchi kuweza kubadili hali ya maisha yao kupitia nishati na hasa nishati ya kutumia gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho napenda kuikumbusha Serikali katika ukurasa ule wa 25 umeonyesha kwamba kutakuwa na mkakati wa kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam, nilichokishangaa Mkoa wa Pwani haukutajwa na Mkoa wa Pwani kuna ugunduzi wa gesi mpya Mkuranga na Bagamoyo. Gesi hii imegunduliwa na uchumi wa gesi ni uchumi mkubwa utatuwezesha kuongeza rasilimali, kuongeza fedha katika Serikali yetu na kutuwezesha sisi kuweza kupiga hatua kubwa za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali injumuisha katika Mpango huu mradi wa uendelezaji wa gesi Bagamoyo, Mkuranga na maeneo mengine ya Pwani lakini pia uelimishaji wa wananchi katika Mkoa wetu wa Pwani ili waweze kushiriki vizuri katika uchumi wa gesi katika nchi yetu. Tuepukane na fujo ambazo tulizipata huko awali ambazo zilitokana pia na wananchi kutokuwa na elimu. Tuhakikishe kwamba Mpango huu unajumuisha maendeleo ya gesi katika maeneo yetu Bagamoyo, Mkuranga na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani ili tuweze kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia naomba nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kujiunga katika Bunge hili na nimshukuru zaidi Mwenyezi Mungu kwa sababu amerahisisha safari yangu ya kutoka kwenye Utumishi wa Umma na kuingia kwenye Ubunge kwa sababu nilipita bila kupingwa, kwa hiyo Ubunge wangu ulianza tangu tarehe 21 Agosti, 2015 wale wenzetu wa upande mwingine hawakurudisha *form*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii sasa, kumpongeza Waziri wa Mipango Dkt. Philip Mpango, na Watumishi wenzake, ambao wametuletea mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ambao wote tunauona unafaa, unatoa matumaini mapya na ni kweli Tanzania yenye viwanda inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu, utajikita kwenye maeneo ya vipaumbele. Eneo la kwanza ni lile la kutangaza Mtwara kuwa eneo la uwekezaji, naomba niishauri Serikali, unapozungumzia Uchumi wa Gesi, huwezi kutofautisha Mtwara na Lindi. Kwa hiyo, naomba vilevile Lindi uangaliwe uwezekano na yenyewe kuwekwa kama eneo maalum la uwekezaji, kwa sababu unapozungumzia uchumi wa gesi na mafuta unazungumzia Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikizungumzia Mtwara ambapo kumetangazwa eneo la uwekezaji kuna changamoto nyingi sana ambazo naomba tupeleke rasilimali za kutosha ili eneo hili litumike ipasavyo. Kwanza kuna ujenzi wa bandari, fedha za kutosha zipelekwe kwa ajili ya upanuzi wa bandari yetu ya Mtwara.

Pili, kama walivyosema wachangiaji waliyopita kuna suala la uwanja wetu wa Ndege wa Mtwara ukabarati umefanyika miaka ya nyuma sana, uwanja huo sasa hivi wa Mtwara hauna taa na hivyo Ndege haziwezi kutua au kuruka usiku, sasa eneo gani la uwekezaji ambao unaweka masharti kwamba Mwekezaji afike mchana tu usiku hawezi kuingia, kwa hiyo turekebishe kasoro hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna ujenzi wa reli ya Mtwara Bamba bay na mchepuko wake ule wa kwenda Liganga na Mchuchuma. Reli hii imesemwa tangu siku nyingi sasa muda umefika tutekeleze, kwa hiyo naomba Serikali yetu sikivu ya awamu ya tano ihakikishe kwamba inatenga fedha za kutosha ili Mradi huu sasa uanze. Ni aibu kwa sababu Mwekezaji wa Kiwanda cha Dangote analeta sasa malighafi ya mkaa toka nchi za nje wakati tuna mkaa wa kutosha toka Mchuchuma ni vizuri reli hii ijengwe ikamilike ili Dangote aanze kutumia rasilimali za humu humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la hospitali ya Rufaa ya Kanda ya kusini. Wawekezaji watapenda kujihakikisha masuala ya uhakika wa afya zao. Kwa hiyo, naomba ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Kanda yetu ya Kusini nashukuru ujenzi umeishaanza na kama alivyojibu Naibu Waziri wakati ule wakati anajibu swali la nyongeza alisema kwamba jengo la wagonjwa wa nje linakaribia kukamilika, tunaomba fedha za kutosha zitengwe ili hospitali hiyo Rufaa ikamilike mapema ili isiwe kikwazo kwa Wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ili Mji wetu wa Mtwara uweze kuwa kivutio cha Wawekezaji tunaomba barabara ambazo zinaunganisha Wilaya za Mkoa wa Mtwara nazo zijengwe kwa hadhi ya lami, kuna barabara maalum barabara ya uchumi, barabara ya korosho, Mtwara, Nanyamba, Tandahimba, Newala Masasi. Barabara hii inasafirisha asilimia themanini (80%) ya korosho ya Tanzania. Kwa hiyo Barabara hii ni muhimu na lazima zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utajikita kwenye zao la korosho. Hapa nitazungumzia changamoto zilizopo kwenye Mifuko yetu miwili kwanza kuna Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho, Mfuko huu unapewa fedha nyingi sana, takribani bilioni 30 kwa mwaka, lakini matumizi ya fedha hizi hayana matokeo yaliyokusudiwa kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba tathmini ifanywe, uchunguzi ufanywe na kama kuna kasoro ambazo ziko wazi, basi hatua za mara moja na za makusudi zichukuliwe ili fedha nyingi ambazo zinapekekwa huku, zionekane katika upatikanaji wa pembejeo, pembejeo zipatikane za kutosha, kwa wakati na za bei nafuu na sivyo ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu kwamba eneo la uchunguzi ukifika Mtwara ni pamoja na Mfuko huu, umeniambia kwamba una ziara karibuni ya kuja Mtwara. Tembelea Mfuko huu, upate maelezo ya kutosha kwa Wataalamu, kwa *Management*, lakini hata na wanufaika, Wakulima na wale wauzaji wa pembejeo za korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu Bodi ya Korosho, ukisoma ile Sheria ambayo imeanzisha Bodi ya Korosho wana majukumu mengi sana, lakini ile Bodi ya Korosho ufanyakazi wake bado hauna matokeo makubwa tunayotarajia kwa Mkoa wetu wa Mtwara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwigulu Waziri wa Kilimo hebu fuatilia kwa ukaribu, utendaji wa Bodi hii na ikiwezekana marekebisha makubwa yafanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka nizungumzie suala la umeme vijijini. Mtwara ndiko kwenye Kiwanda cha Uchakataji wa Gesi Madimba na kile Kiwanda cha Msimbati. Hata hivyo, umeme vijijini bado haujawanufaisha vizuri wakazi wa Mkoa huo, kwa hiyo, naomba idadi ya Vijiji iongezwe na sioni kwa nini Serikali isitangaze kwamba tuwe na *universal coverage* kwa Mkoa wa

Mtwara kwamba vijiji vyote vya Mkoa wa Mtwara vipitiwe na mradi huu wa umeme vijijini, kwa sababu wao ndiyo wazalishaji wa ile gesi ambayo ipo Madimba na kule Msimbati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Jimbo langu la Nanyamba nina Vijiji 87, lakini vijiji ambavyo sasa hivi kuna umeme wa uhakika ni vijiji vitatu tu, sasa hapo Wananchi hawatuelewi. Gesi ipo kama kilometa 30 kutoka Nanyamba lakini Vijiji vitatu tu vyenye umeme hatueleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho niende kwenye uboreshaji wa sekta ya Elimu. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa jitihada ambazo inafanya ya kutoa elimu bure. Kwa kweli manufaa yake yanaonekana kwa wananchi wale ambao wanabeza ni kawaida yao kubeza, lakini mwananchi wa kawaida anajua kabisa nini ya maana ya Elimu bure, lakini ningepomba sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano sasa hivi tujikite kwenye *process teaching and learning process* tusijikite kwenye *output mambo ya division, GPA* hayamsaidii mtoto anapotoka shuleni, tujikite maarifa na ujuzi anaoupata mtoto akiwa darasani.

Tuhakikishe vitabu vinapatikana vya kutosha, Walimu wanalipwa vizuri ili wawe na *moral* ya kufanya kazi, vilevile Walimu hawa wanajengewa nyumba za kutosha, lakini pia zana za kufundishia zinapatikana za kutosha na maabara zinakamilika na kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kuna Kitengo cha Udhubiti wa Ubora wa Elimu, Wakaguzi wa shule. Hiki kitengo hakifanyi kazi yake ipasavyo, vilevile hawapewi rasilimali za kutosha, kule nyuma kulikuwa na mawazo kwamba kitengo hiki nacho kipelekwe TAMISEMI. Kukawa na mawazo kwamba hawawezi kumkagua Mkurugenzi, lakini sikubaliani na hoja hiyo, kwa sababu kwenye Halmashauri kuna Mkaguzi wa ndani bado anamkagua Mkurugenzi na anapeleka ripoti kwake. Kwa hiyo, naomba ili kitengo hiki kiwe fanisi basi wathibiti wa ubora wa shule nao wapelekwe TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami kwa moyo mkunjufu kabisa japokuwa najua hawanioni, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kawe, kwa kunipa heshima kubwa, najua kuna watu walifikiria lile Jimbo nimeazimwa miaka mitano, sasa hii nguvu ya kuingia mara ya pili kwa tofauti ya kura 17,000 nadhani imetuma somo huko, mjue kwamba watoto wa

kitaa wamenisoma vizuri na uzuri upande wa huko wengi ni wananchi wangu, kwa hiyo mtanivumilia kwa kipindi hiki cha miaka mitano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane kabisa na Mheshimiwa Peter Serukamba alivyozungumza asubuhi, baada ya Kamati ya Bajeti kuundwa, Chenge one na Chenge two, ilitoa mapendekezo ya kina baada ya Kamati kujadili, baada ya Bunge kujadili, na Kamati kwenda ku-compile, ilitoa mapendekezo ya kina ya vyanzo mbadala vya kodi vya Serikali. Leo tunakuja hapa, yaani ni kama vile akitoka Rais huyu, akiingia Rais mwingine, ni kama vile imetoka mbingu, imekuja dunia, hakuna connectivity.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna Wabunge ma-junior hapa, tuko asilimia thelathini (30%) tumerudi ma-senior, lakini nawaambieni hii miaka mitano lugha ninayoizungumza leo mtakuja kuizungumza 2019. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mmechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Zanzibar wamewakataa mnataka kulazimisha, ndiyo maana Tanganyika waliwakataa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikawabeba beba tu kindakindaki na ninyi mnajua. Nashukuru Mpango ametusaidia, katueleza yaani jinsi Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilivyo-fail kwenye huu, alivyo review miaka mitano, anatuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli mlipanga kukarabati, Reli ya Kati, kilometa 2,700, mmeweza 150 hivi hamuoni aibu? Halafu mtu anakuja hapa anasifia tu vyanzo tulishawapa Kambi ya Upinzani iliwapa miaka mitano iliyopita, kila mwaka tunawapa. Kamati ya Bajeti iliwapa mnakuja mnaumiza vichwa vya watu hapa for nothing.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mabehewa ya Mwakyembe, 274 tunaambiwa na yenyewe feki, yaani hayo yenyewe ndiyo yamenunuliwa basi na yenyewe Mheshimiwa Sitta katuambia siyo sisi, akaunda Kamati yake pale Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara Mzee Magufuli mwenyewe...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Upi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende tena kule kwenye ile Kanuni ya 63 ili nimweleze, maana ni lazima nijieleze Kanuni ya 63(3), nataka nimweleze mwanafunzi wangu na Mbunge wangu wa Kawe, hapa tuko Bungeni hamna ubabe ngoja nikueleze ukweli uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nikimwambia Halima niletee behewa ambalo halifanyi kazi atashindwa kulileta au kunionesha, wewe ni msomi wa sheria, kwenye mkataba wowote kuna kipengeke kinaitwa *defects liability period*. Kipindi ambacho ndiyo nina dakika tatu soma Kanuni, Mheshimiwa Kubenea siyo magazeti haya! nina dakika tatu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema hicho kipindi...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, samahani Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakyembe alitakiwa asimame, asome Kanuni, aseme nimevunja Kanuni gani, anitake mimi ama nijibu, ama nisijibu, ama wewe utoe Mwongozo, kisha wewe kama utataka yeye..

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye kikao, ama tu ni vurugu kama Kariakoo sokoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nani mimi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakyembe endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Anaendelea kufanya nini sasa.

**MWENYEKITI:** Aendelee kusoma utaratibu wake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Anatoa utaratibu, anafanya nini?

**MWENYEKITI:** Ndiyo anaendeleo na utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sasa ndiyo aseme sasa, asome Kanuni aseme nini...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halima unaogopa nini, ubabe wa nini kaufanye nje, sikiliza, Kanuni ya 63..

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Soma Kanuni wewe simamia.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63(3) inajieleza.

**MWENYEKITI:** Naomba usome Mheshimiwa Mwakyembe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VINANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Kanuni ya 68. Naomba Mwongozo wako, Bunge hili linaongozwa kwa Kanuni, akishapewa mtu mmoja nafasi ya kuzungumza, mtu mwingine anatakiwa asubiri atulie mpaka mtu mmoja anayemaliza amalize kuzungumza. Naomba Mwongozo wako, hivi ni kwa nini kiti, vurugu watu wanavunja Kanuni tu, halafu wanaachwa tu, hakuna hatua yoyote, kwa nini hatufuati utaratibu?

**MWENYEKITI:** Jamani Waheshimiwa Wabunge, tunaendesha Bunge hili kwa mujibu wa taratibu na Kanuni zetu na Sheria, tunaomba mtu anapotoa taarifa mwingine akae, ndiyo Kanuni inavyosema, naomba Mheshimiwa Mwakyembe usimame na kutoa taarifa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, unataka nisome hiyo Kanuni? Hapana sisikilizi midomo mingine huku.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nisome Kanuni?

**MWENYEKITI:** Soma ndiyo.

**WAZIRI WA KATIBA NASHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63(3) inasema: Mbunge mwingine yeyote, anaweza kusimama mahali pake na kutamka kuhusu utaratibu, kama nilivyofanya na baada ya kuruhusiwa na Spika au Mwenyekiti kama hivyo, na kudai kwamba Mbunge aliyekuwa nasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisemea Bungeni.

Fasili ya (4) inaendelea kusema, Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa Fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuridhisha Bunge, ndiyo ninachokifanya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msomi huyu anasema, kuna mabehewa 274 *fake, it is a lie*, nikimwambia kesho atuthibitishie hawezi, kwa sababu mabehewa yote 274 yanafanya kazi. Yanafanya kazi kwa sababu yalipoletwa ni mimi mwenyewe, niliyesema kuna mabehewa ambayo siyo mazuri, nikaunda uchunguzi, lakini tuliunda uchunguzi ni kwa sababu tulikuwa na haki chini ya Mkataba, inaitwa *defects liability period* ilikuwa bado ndani ya mwaka mmoja, wakaja wale waliotuzia mabehewa kuyatengeneza upya, sasa haya mabovu yako wapi, kama siyo porojo tu za hawa watu ambao hawana hoja ya msingi?

Vile vile suala hili, juzi tumelitolea mwongozo kwako kwenye kiti, tatu lithibitishwe suala hilo, Halima hana hoja anaanza kuleta porojo upya hapa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakyembe ahsante kwa taarifa, tunaomba Mheshimiwa Halima Mdee uendelee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Walikwambia wewe ni jipu? Sikiliza, mimi nimesema hivi, kwa mujibu wa Mheshimiwa Samuel Sitta alivyoenda Wizara ya Uchukuzi aliyasema hayo maneno. Sasa hayo mambo mengine wakamalizane wao wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, alikuwa Mheshimiwa Magufuli. Walijipanga kujenga na kukarabati 5,204, wameweza kukarabari 2,700, na ni kati ya Mawaziri ambao walikuwa wanakuja na vitabu vikubwa sana na mikwara mingi, lakini kumbe hata nusu ya lengo haijatumia, Chama cha Mapinduzi.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Vipi tena.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(d) kwamba Mbunge yeyote hatotumia jina la Rais, kwa dhihaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

Mbunge anayeendelea kujenga hoja yake, anajaribu kutumia jina la Rais, kutaka kulieleza Bunge ama kulishawishi kwa namna yoyote ile, jambo ambalo haliruhusiwi Kikanuni, naomba atoe mchango wake kwa namna nyingine yoyote lakini siyo kulihusisha jina la Rais na ujengaji wake wa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba Halima uendelee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Halafu hii biashara ya kufanya Rais hashikiki, wala hakamatiki wakati sisi jukumu letu ni kuisimamia Serikali ikome. Mimi hapa nimerejea...

**MWENYEKITI:** Naomba utumie lugha ya staha Bungeni kwa mujibu wa taratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi hii biashara ya kufanya Rais ni mtu ambaye hashikiki, hagusiki, hatajwi, hazungumzwi iishe kwa sababu jukumu la Bunge ni kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea niliyoitoa hapa ni mafanikio ya ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba ukae, Mheshimiwa Waziri azungumze.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hivi nyie mbona mnajikomba sana kwa *President*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu! Tunachokifanya ni matakwa ya kikanuni. Haya maneno wala siyo kwamba tunasimama hapa tunasema bila utaratibu, kanuni ya 64 imeorodhesha mambo ambayo hayaruhusiwi Bungeni. Ukiyasoma mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, kipo kifungu cha (d) na vipo vifungu vingine ambavyo havitakiwi humu ndani kutaja jina la Mheshimiwa Rais kwa dhihaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwenye Kanuni ya 64...

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti taarifa 68(8), taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Jamani naomba heshima ya Bunge itunzwe, mmoja mmoja azungumze. Mheshimiwa Waziri wa Nchi endelea mara moja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa 68 (8).

**MWENYEKITI:** Jamani hakuna taarifa juu ya taarifa, taarifa moja moja kwa mujibu wa utaratibu. Subiri atoe taarifa na wewe utatoa yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niisome Kanuni ya 64(d) katika mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Mbunge hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote lile kwa namna fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti (e) inasema hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yoyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kutatolewa hoja mahsus kuhusu jambo husika. Sasa sisi hatuyatoi haya kichwani tunafuata Kanuni na kukuomba wewe mwongozo. Wewe ndiyo mwongozo utatujibu kama jambo hilo linatakiwa ama halitakiwi.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mwenyekiti naomba nitoe taarifa kwa Kanuni ya 68 (8). Mbunge anachotaka Halima asifanye...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mwenyekiti taarifa yangu ni kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Heche aendelee kwanza.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kitabu anachotumia Halima kuzungumza ni review ya kazi ambayo imefanyika wakati Magufuli akiwa Waziri, lazima tumtaje. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Kuhusu utaratibu Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Utaratibu wa mwisho jamani.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu John Heche ajifunze Kanuni. Kwa sababu huwezi kutumia Kanuni ya taarifa wakati hakuna Mbunge anayesema. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (8). Jifunze Kanuni usibishe.

Kwa hiyo, kwa matumizi bora ya Kanuni zetu ni vema ukawa unawauliza Wabunge anapotaka kuongea anataka kuongea kuhusu Kanuni ipi, anasimama kwa Kanuni ipi. La sivyo, tutafanyiwa vurugu na mijadala itashindikana hapa kwa sababu watu hawajui Kanuni.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jamani naomba basi kwa maslahi ya Taifa letu tuache majadiliano haya, naomba Mheshimiwa Halima Mdee aendelee.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Wasipotoshe hapo, ameomba Kanuni wakati bado Jenista anaongea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Narejea

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee naomba uheshimu Kanuni na katika mazungumzo.

**MHE HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Miaka Mitano iliyopita, wakati Mheshimiwa Magufuli ambae sasa ni Rais, alipokuwa Waziri wa Miundombinu hatimae Ujenzi na kila kitu, barabara zilizotakiwa kukarabatiwa na kujengwa ni kilomita 5,204 lakini sasa hivi tunaambiwa zilizokarabatiwa ni 2,775 kilometa. Kidumu Chama cha Mapinduzi! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kuna watu hapa wanazungumza utafikiria hii Serikali ni mpya, kumbe ninyi tokea mwaka 1961 mmepata dhamana kuanzia TANU mpaka CCM, watu tunaumiza *brain* tunatoa mawazo hamfanyi kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo: Tukija kwenye sekta ya kilimo kimekua kwa asilimia 3.4 tuliokuja Bungeni miaka 10 iliyopita, kilimo kilikuwa kimekua kipindi kile kwa asilimia minne, tena malengo ya Serikali ilikuwa ni asilimia 10. Serikali ilivyoona inabanwa ikashusha mpaka asilimia sita. Leo tunaambiwa kilimo kimekua kwa asilimia 3.4 maana yake kwanza mmeshuka chini. Ie asilimia sita imekuja hapa chini mmeshindwa kui-*balance*, halafu mnasema eti mapinduzi ya kilimo! Hapa kazi tu! Yaani, kilimo cha umwagiliaji, wakati mkoloni anaondoka, tuna hekta za umwagiliaji 400,000, ninyi hapa mmetushusha mpaka 345,000 halafu mmnatuambia mmeongeza asilimia 46, wakati mnajua miaka mitano iliyopita tulikuwa tuna hekta 350,000. Yaani mnacheza na mahesabu, *figure* iliyokuwepo mnaongeza 5000 halafu mnajumlisha mnasema ni mafanikio. *It is a shame!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sijui 64 baada ya uhuru, asilimia 10 ya wananchi wana hati za kawaida na hati za kimila, hivi migogoro ya ardhi itaacha kuwepo? Miaka 64 sijui 54 baada ya uhuru, asilimia 20 ya ardhi yetu ndiyo ipo kwenye mipango, hivi mgogoro wa wakulima na wafugaji itaacha kuwepo? halafu inakuja Serikali hapa inaleta mpango, ime-*adress* vipi hivi vitu ambavyo ni *critical*, hakuna! Eti! mnaenda mnabomoabomoa Dar es Salaam, hivi tungekuwa na utaratibu wa kuwapa Watanzania maskini viwanja kwa gharama nafuu, kuna mtu anataka kwenda kujenga mtoni? Kuna mtu anataka kujenga mabondeni? Viwanja vya Serikali huna milioni sita, huna milioni saba hununui kiwanja, tena milioni 10, milioni 20 hununui kiwanja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, vipaumbele, miaka mitano iliyopita tulikuwa tuna miundombinu, tulikuwa tuna kilimo, tulikuwa tuna viwanda, tulikuwa tuna *human development*, tulikuwa tuna tourism, miaka mitano baadae majamaa yamegeuka, viwanda, kufungamanisha maendeleo ya watu, miradi mikubwa ya kielelezo, ujenzi wa maeneo wezeshi, yaani kilimo wameweka pembeni, kinaajiri asilimia 70 ya Watanzania, inachangia asilimia 30 ya pato la taifa, asilimia 40 ya fedha za nje umeweka pembeni, halafu

unatuambia eti hivi vitu tulivyoviacha viporo vitajumuishwa, vinajumuishwaje kama havipo kwenye kipaumbele? Tutatengaje bajeti kama haipo kwenye kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Mother* tulia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Taarifa Mheshimiwa

**MHE HALIMA J. MDEE:** Umesimama au umekaa maana mimi sikuoni (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee naomba uongee naona hayupo tayari na taarifa (*Makofi*)

**MHE HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Kamati ambayo imesema hivi ni muhimu kama kweli tunataka kuwasaidia Watanzania. Kama tunataka kuwasaidia Watanzania lazima tuingize kilimo kama kipaumbele cha msingi. Kamati ya Bajeti imesema na tukiingiza kilimo tutenge bajeti, mwaka jana tulikuwa tunasema hapa kwamba haiwezekani kitabu cha maendeleo cha Wizara ya Kilimo, fedha za maendeleo kwenye vocha ya kilimo imetengewa bilioni 40 wakati Jakaya Mrisho Kikwete ametengewa bilioni 50 kusafiri nje. Kwa hiyo, kama we *mean business* tuwekeze kwenye kilimo, tutapunguza Watanzania hao maskini kuwa wategemezi kwa Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti dakika ngapi huyu anatumia?

**MWENYEKITI:** Bado nusu dakika

**MHE, HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima miundombinu irejeshwe sababu kama tunataka viwanda, hivi viwanda bila uzalishaji kuna viwanda au kuna matope? Kwa hiyo lazima....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MH. DKT. RAFAEL M. CHENGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, na mimi niungane na wenzangu wote ambao tumeingia kwenye uchaguzi huu baada ya kuwa tumeshashinda kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Tanzania ya leo imempata Rais ambaye Watanzania wote wanamuhitaji

na lazima tuwe na mahali pa kuendelea. Serikali si kwamba inakatika ni mwendelezo. Mheshimiwa Kikwete alifanya kazi kubwa sana kwa Watanzania na Mheshimiwa Magufuli amekuja kuendeleza pale Kikwete alipoishia na kuongeza zaidi kasi. Ni rahisi kuwa msemaji mzuri wa kupinga kila kitu, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge sisi ni watu wazima tufike mahali tuwe *more objective* katika mazungumzo yetu. Watanzania wanatuangalia kutupima kwa jinsi tunavyoongea na uwakilishi wetu humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia Mpango, tunazungumzia Mpango wetu wa Taifa. Bunge hili ningefurahi sana tukijikita kuzungumza tutoke hapa twende wapi, hivi vijembe na hadithi hazisaidii kwa sasa hivi, bali Watanzania tusema sasa tunataka tu-*achieve* kitu gani, yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ya kuongea, jambo la kwanza naomba ni-*acknowledge* kwamba tumeanza Awamu ya Tano ikiwa na deni la shilingi trilioni 1.8, ukiangalia siyo hela ndogo ni hela kubwa sana. Watanzania lazima tufunge mikanda na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekuja na kauli mbiu ya kwamba hapa ni kazi tu. Maana yake ni nini? Kila mmoja awajibike kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Waziri Mpango kama ilivyo jina lake Mpango ameleta mpango mzuri sana, ninaomba Watanzania tuu-*support*. Mpango huu utakuwa mzuri tu ikiwa tutakubaliana sisi kama Bunge twende na Mpango huu kipamoja na siyo tumegawanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia makusanyo ya kodi tumeona kwa kipindi kifupi baada ya kudhibiti mianya ya kodi yamepanda sana. Sasa hivi *the tax and revenue effect* ni asilimia 12 ya GDP. Kitu ambacho bado ni chini inapaswa iongezeka. Itaongezeka tu kama tutaweza kuweka miundombinu ya kuongeza uchumi wetu.

Hapa naomba niungane na wasemaji wote, huwezi ukazungumzia uchumi bila kuwa na miundombinu ya uchumi. Lazima swala la miundombinu ya barabara na reli iwekewe kipaumbele kikubwa sana. Reli ya Kati, reli ya TAZARA lazima iwekewe kipaumbele kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaposema viwanda, kweli tunataka nchi ya viwanda lazima tuweke miundombinu ambayo itawezesha viwanda hivi viweze kweli kufanya kazi yake kikamilifu. Ukiangalia leo hii hata kwenye viwanda vya nguo malighafi inayotoka nje au inakuwa rahisi zaidi kuliko mali inayozalishwa hapa nchini.

Kwa hiyo, lazima upande wa nishati tuboreshe nishati ipatikane kwa bei ya ambayo itawezesha uzalishaji wetu uweze kupambana na bidhaa za kutoka nje. Mheshimiwa Muhongo amethibitisha, ni Waziri ambaye amejitoa mhanga, kazi yake ni sahihi na naomba tumuunge mkono jitihada zake hizi (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda mbali na suala zima alilosema Mheshimiwa Mdee suala la kilimo, lazima kilimo vilevile tukipe kipaumbele, hapa siyo kusema ushabiki kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wanashughulika na kilimo, kilimo hiki kiweze kuwapatia Watanzania ajira na kuongeza pato la Taifa. Bila kufanya hivyo hatutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia juzi hapa kwamba Msajili wa Hazina ameamua fedha yote kwenye taasisi za Serikali wafungue akaunti Benki Kuu. Ni uamuzi sahihi na nauunga mkono, kwa sababu leo hii kama Serikali iweze kujua kwamba hizi *public enterprises* zote zinazalisha kiasi gani na mwenye mali ambayo ni sisi Watanzania tujue kinachozalishwa na kinatumikaje. Bila kujua vile inakuwa ni tatizo na ofisi ya Msajili kwa sasa naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tumuunge mkono sana Msajili aliyepo sasa hivi Ndugu Mafuru, kwa sababu huko nyuma ofisi ya Msajili haikuwa inafanya kazi inavyotakiwa hata haikujua haya Mashirika yanafanya nini yanazalisha nini wanaleta kiasi gani Serikalini, lakini kwa muundo huu mpya itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna benki hapa zitalalamika lakini Mheshimiwa Mwenyekiti niseme hivi, hela ya serikali ambayo ipo kwenye mabanki ni trilioni 1.1, katika hela hiyo bilioni 335 iko kwenye *current account*, haizai faida yoyote ile hawa jamaa wanatumia kuzalisha wenyewe, matokeo yake hata riba zinakuwa ziko juu. Sasa tuweke uwiano sawa ili benki zi-*compete* vizuri kwamba hakuna pesa ya bure. (*Makofi*)

Serikali hii ina hela hela zake kwenye *current account* na inakopa tena kwa riba kubwa zaidi, sielewi ni uchumi wa aina gani huu na sijui wanapokuwa wanafanya wanafikiria kitu gani. wewe hela za kwako uende kukopa tena kwa riba ya juu unafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hili niunge mkono kabisa kwamba Serikali kupitia Msajili wa Hazina waandae utaratibu ambao hautaleta matatizo ili pesa inayozalishwa ichangie kwenye bajeti ya Serikali, ichangie kwenye mapato ya Serikali na kuondoa ufujivu wa fedha ya Serikali. Kuna mashirika hapa walikuwa wanajigawia fedha wanavyotaka wenyewe, Bodi ikiamua imeamua. Tuachane na utaratibu huo, sasa hapa ni kazi tu. Dada yangu Halima Mdee hapa ni kazi tu, lazima pesa ipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge tunalalamika pengine baadhi ya vitu vyetu havijakaa sawa, ndiyo Serikali haina pesa itatoa wapi na sisi

tuhangaike kutoa mchango utaokasaidia Serikali iweze kukusanya mapato ya kutosha na iweze kutoa huduma kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna benki hapa Tanzania 54, lakini mabenki tisa tu ndiyo yamekuwa yakichezea hela ya Serikali mengine hapana! Sidhani kama kutakuwa na ulalamishi wowote ule kwa nini walalamike, isipokuwa tuongeze mapato ya Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia; huko Busega, asubuhi nilisema hapa, kuna tatizo kubwa na hili siyo la Busega peke yake, ni maeneo yote ambayo yanapakana na hifadhi za Taifa. Naiomba Serikali kupitia Wizara husika na kuwashirikisha Mawaziri wanaohusika na wadau wote, tuwe na mkakati wa pamoja. Tunahitaji tulinde hifadhi zetu za Taifa, tu-promote utalii, lakini wakati huo huo tujali maisha ya wananchi na mifugo yao ili kuweza kujenga usalama na mahusiano ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa agizo la Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alilolitoa hapa, limefanya kazi. Mifugo ile nimeambiwa bado kuna hapa na hapa lakini baadhi ya mingine imeanza kuachiwa. Naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie tena ili vijana wako wa *Game Reserves* waheshimu wakulima na wafugaji walio kandokando ya hifadhi hizi. Kwa maana hiyo, tusiwe na uhasama ambao hauna tija yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Waziri Mkuu. Waziri Mkuu ameanza kazi vizuri, endelea kuchapa kazi, Serikali yako na wanachama wote, Watanzania wote, pamoja na Rais watawaunga mkono, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, siyo tu katika Bunge hili la Kumi na Moja, lakini katika Bunge kwa ujumla wake. Nipende kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu kwa uzima na afya zetu wote humu ndani maana uzima na zetu zinatoka kwake. Pia nipende kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini na niwahakikishie kwamba, nitakuwa mtumishi wao bila kujali itikadi zao, nitawatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa sikupata fursa kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais nipende pia kumshukuru na kumpongeza na pia kuwapongeza Mawaziri na Serikali kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wameanza kazi kwa kasi inayotia moyo wananchi. Nafahamu kutakuwepo na kukatishwa tamaa kwingi lakini niwatie moyo, tusonge mbele, katika lolote jema unalolifanya mtu lazima hapakosekani mtu wa kukukatisha tamaa. Sisi tuchape kazi tuwatumikie Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi na mimi nijikite katika suala zima la Mapendekezo ya Mpango. Kwanza kabisa nikubaliane na nimuunge mkono Profesa Muhongo kwa sababu bila nishati ya umeme hata hii ndoto ya viwanda hatutaweza kuifanikisha. Pia nimuombe Profesa, kwa ujuzi na utaalim wake twende mbele zaidi kwa sababu kwa kuwa na gesi haitoshi tu kuwa na umeme, kama ulivyokuwa umesema *megawatt* 10,000 kwa malengo, sawa itatusaidia, lakini hebu kwa kutumia utaalim wako na wataalam mbalimbali wa masuala ya jiolojia tu-*extend* namna gani tutanufaika na gesi. Kwa mfano, kitaalam gesi ni kitu ambacho kinahitajika sana duniani. Tunaweza kusafirisha gesi siyo kwa kujenga bomba lakini kwa kufanya *liquidfaction* na tuka-*export* gesi kwa nchi jiraji kama vile China na India ambazo kutokana na *geographical location* yetu tunaweza kusafirisha gesi kwa kutumia meli kubwa.

Kwa hiyo, nikuombe Profesa kwa utaalim wako tu-*extend* ili kusudi gesi hii, tunapokwenda katika uchumi wa kati tuweze kunufaika zaidi kama ambavyo nchi kama Russia zinavyoweza kunufaika na gesi, siyo kwa kutumia tu katika kuzalisha ndani lakini pia kwa kuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pilli, nipende kuzungumzia sekta ya utalii. Hata katika taarifa ya utekelezaji wa Mpango ambao umepita Sekta ya Utalii imethibitika kwamba ilikua kwa kasi na mchango wake katika pato la taifa ulikuwa ni mkubwa sana. Niombe tu, katika mpango kwa kuwa hii ni sekta ambayo ilionesha wazi imekua kwa kasi hebu tuendeleo kuipa nguvu. Pia tutanue wigo wake. Tunaweza kutanua sekta ya utalii kwa kuitangaza kupitia michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi jirani wanatangaza sana utalii kupitia michezo hasa mchezo wa riadha. Hebu tujaribu pia kuona namna gani tunaweza kuwekeza. Nafahamu *geographically*, kama ambavyo nchi jirani kuna wanariadha wanatoka maeneo fulani fulani, na sisi pia tuna maeneo hayo ambayo tungeweza kutengeneza wanariadha wa kutosha ambao wangetumika siyo tu kwa kuongeza kipato lakini pia kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona Mheshimiwa Massay juzi alikuwepo kwenye riadha pale kutoka huko Hanang Mbulu. Tunaweza kutengeneza wanariadha wazuri ikawa siyo tu *source of income* kwa nchi lakini kwa kuitangaza nchi. Kupitia michezo tumeona tumeona mchezaji Mbwana Samata pamoja na kuwa baadhi ya vyombo vya habari vilipotosha na kuonyesha kama anatoka DRC au anatoka Botswana na kadhalika, lakini ni sehemu ambayo inatosha kabisa kutangaza utalii na hivyo kukuza utalii na mwishowe kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nizungumzie suala la miundombinu. Ni kweli kabisa naona Waheshimiwa Wabunge wengi wakisimama wanazungumza kuhusu reli ya kati ni vizuri, lakini pia tusisahau reli ya TAZARA. Sisi watu tunaotoka Nyanda za Juu Kusini tunalima vizuri mazao ya nafaka. Reli hii ingeweza kutosha kabisa kusafirisha siyo tu mazao ya chakula kama mpunga na mahindi, lakini hata mazao mengine ya biashara na hasa zao la mbaao kutoka huko Nyanda za Juu Kusini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala zima la miundombinu, nashauri Mpango pia ujaribu kuelekeza au kutazama miundombinu kuelekea maeneo ambayo tayari ni ya uzalishaji. Kwa mfano, sisi katika Wilaya ya Mufindi barabara ya kutoka kiwanda cha Mgololo unakutana na *semi-trailers* kila siku, ni uchumi mkubwa kama tutaijenga barabara hii kwa kiwango cha lami maana yake ni kwamba tuta- *stimulate* uchumi wa watu wa maeneo ya jirani na mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wakisimama, na hata mpango unaeleza ambavyo sekta binafsi ni *engine* ya ukuaji wa uchumi. Pia, hebu tujaribu kujiuliza hii sekta binafsi inafanya kazi na nani? Nakubaliana nanyi kwamba ni *engine* ya uchumi; lakini *engine* ambayo huweki *oil* kwa wakati, *engine* ambayo huweki maji kwa wakati bila shaka ita-*nock*. Sasa maji na *oil* ni nani? Maji na *oil* ni Watumishi wa Umma wa nchi hii. Mimi ni-*declare interest* nilikuwa Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mpango pia ujielekeze kwa Watumishi wa Umma, uwatazame katika maslahi yao, kuanzia mishahara yao, wakati wanapokwenda likizo; utakuta kwamba mwaka huu watapewa nauli mwaka mwingine hapewi nauli, lakini pia hata nauli ya kwenda kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwa Dar es salaam kuna Wizara zina gari za kuwapeleka wafanyakazi kazini na kuwarudisha, lakini kuna maeneo mengine mfanyakazi kwa mfano anatoka Kongowe anafanya kazi katikati ya mji, je, tunategemea mfanyakazi huyu atakuwa na moyo wa kuchapa kazi ipasavyo wakati maslahi yake uki-*compare* na hao wa *private sector* yako chini kwa kiwango cha kupindukia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nishauri; katika mpango hebu tutazame pia Watumishi wa Umma kwa sababu kama tunasema *private sector* ni *engine*, basi wao tuwachukulie kama vile ni *oil*. Ndiyo maana katika ofisi za umma *survival* ya watu wengi ni kusubiri safari za kikazi kwa sababu ule mshahara hautoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema kwamba, kama ambavyo Profesa Muhongo amesema watahakikisha

wanamalizia vipoto vya REA awamu ya kwanza na ya pili. Nashauri kabla ya kutekeleza Mpango unaokuja hebu tukamilishe viporo, kama kuna viporo vya zahanati, kama kuna viporo vya miradi mbalimbali tuvikamilishe, hiyo itatupa nafasi ya kuweza kusonga mbele na kutekeleza ipasavyo mpango unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kusema, katika kumaliza viporo hivyo niombe hasa katika sekta ya afya. Hebu tuangalie maeneno kulingana na *population* na namna ambavyo tunahudumia. Naomba kuunga mkono mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa naongea kwa mara ya kwanza katika Bunge hili, nichukue fursa hii kumshukuru Mungu na mimi kuwepo hapa. Zaidi niwashukuru wananchi wa Moshi Vijijini kwa maamuzi waliyofanya ambayo yameweza kunifanya nikawa mwakilishi wao, Mungu aendelee kuwaimarisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kabla sijaenda kwenye mchango niweke *record* sawasawa. Wakati ule tukiwa tunafanya semina hapa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema wakati akijaribu kutuaminisha kwamba yeye ni Mwanasheria wa kila kitu. Mwanasheria Mkuu wa Mihimili yote, alisema yuko mtu mmoja alilishtaki Bunge katika Mahakama ya haki ya Afrika Mashariki na yeye akaenda kulitetea Bunge kule kama Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye niliyeishtaki lakini sikulishtaki Bunge. Niliishtaki Serikali ya Jamhuri ya Tanzania na nilimshtaki Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kesi yangu ni *reference* Na. 7 ambayo ni Anthony Calist Komu *versus Attorney General of United Republic of Tanzania*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi hiyo nilishinda, Mwanasheria Mkuu amekata rufaa na nina uhakika nitamshinda tena ili wanilipe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye kazi hii ambayo iko mbele yetu. Kama mwenzangu aliyenitangulia alivyosema, kama unataka kukamua ng'ombe ni lazima umlishe vizuri, vinginevyo utakamua damu. Ukienda kwenye haya Mapendekezo ya Mpango, idadi ya watu na pato la kila mtu. Mapendekezo haya yanasema, nchi hii itakwenda kwenye kipato cha kati, na itakwenda kwenye kipato cha kati kwa sababu hapa wamefanya makadirio. Wanasema kipato cha Mtanzania kinakua na sasa hivi kimefikia dola za Kimarekani 1,043, maana yake Shilingi 1,724,716 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya hesabu utaona kwamba kila Mtanzania anapaswa awe anapata kipato cha Shilingi 1,043,000 na pesa

kidogo. Sasa nauliza, hivi kweli ni Watanzania wangapi wana kipato hicho siku ya leo? Kima cha chini cha mshahara kwenye viwanda vyetu, viwanda vya Wahindi, Wachina ni Sh. 100,000 na hilo huwezi kulichukua kama ni pato ambalo mtu anakwenda nalo nyumbani kwa sababu bado hujatoa gharama za kumuwezesha yeye kwenda kutekeleza wajibu huo unaompa kwa Sh. 100,000. Maana yake ni lazima alipe nauli, ale mchana halafu ndipo sasa apate kitu fulani. *Ma-house girls* mmewahi kusema chapa Bungeni kwamba wanapaswa kulipwa Shilingi 80,000 kwa mwezi. *Ma-bar maid* ambao ni wengi sana katika nchi hii. Sasa hizi takwimu zinatuu-*mislead* na hapa ndiko tunakokwenda kukamua ng'ombe ambaye hatumlishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye viwanda vingi, ukienda kwenye mashamba, sisi tuna mashamba yale ambayo yalikuwa *nationalized* kule Moshi vijijini, watu hawaajiriwi, watu wanakuwa vibarua kwa miaka mitatu, minne, mitano. Akifika ule muda wa kuambiwa ajiriwe anapewa likizo isiyokuwa na malipo au anakuwa *terminated* halafu anaomba tena akianza anaanza upya tena. Sasa kwa utaratibu huo ni lazima tuangalie sana mipango yetu na hizi takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni. Niko hapo hapo kwa Mtanzania. Tukitaka kwenye uchumi huu wa kipato cha kati ni lazima tuwe na sekta binafsi ambayo ina nguvu. Leo haya madeni yanayozungumzwa na bahati mbaya yanayowahusu watu wa ndani, sekta binafsi ambayo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa sana Rais Magufuli, Rais wetu wa Awamu ya Tano; Wakandarasi wanadai madeni makubwa sana. Sasa, ukiangalia katika Mpango huu wote hakuna mahali ambapo inaonesha kwamba Serikali imejipanga kulipa haya madeni hasa ya watu wa ndani (Wazawa). Sasa hii sekta binafsi ambayo ndiyo yenye mchango mkubwa sana katika huu Mpango, kwa sababu ukisoma huu Mpango utaona kwamba mapato ambayo ni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika ule mwelekeo uliyoletwa hapa au hata ukifanya mapitio ya Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano, utaona kwamba ni wastani wa trilioni 8.9 ndizo ambazo zinapaswa kutumika kila mwaka. Lakini katika hizo trilioni 8.9, 2.9 ndizo ambazo ni mapato yetu ambayo naweza kusema Serikali ina uwezo nayo. Trilioni sita zinapaswa kutoka kwenye Sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna mkakati wa makusudi, wa kuhakikisha sekta binafsi inalindwa, inalipwa ili kutoa huduma na inalipwa kwa wakati, hatuoni kama tunaanza kuzika huu mpango kabla haujaanza. Kwa hiyo, naishauri sana Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ukienda kwenye Sekta ya Elimu utaona kwamba kuna mambo mazuri yanayozungumzwa, tuna madarasa

fulani tunajenga, tuna hiki tunajenga, lakini siamini kama kuna *review* ya yale ambayo yalikuwafanyika, kwa sababu kungekuwepo na *review*, toka nimekuwa Mbunge nime tembea karibu Kata zote za Jimbo langu, hakuna Kata hata moja ambayo nimekwenda nikaacha kukuta kuna madarasa ambayo hayafai, yameshakuwa *condemned*, hakuna vyoo, unakuta shule ina watoto 370 haina choo. Shule ina watoto 188 haina choo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwe inafanya na kile kitengo cha ukaguzi kwenye mashule wapo tu, hawana fedha, hawafanyi ukaguzi. Kwa hiyo hakuna ripoti za hali halisi ilivyo kwenye *field*. Hivyo hivyo kwenye sekta ya maji, hapa wanasema maji ni asilimia kadhaa, lakini ukienda kwenye *reality*, unakuta kwamba hakuna hayo wanayoyazungumza. Kule kwangu wanasema Kata ya Uru Kusini ina maji, Kata ya Uru Kaskazini ina maji. (Makofi)

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nichukue fursa hii adhimu kabisa kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkuranga katika Mkoa wa Pwani, naomba niwahakikishie ya kwamba kazi yao walionituma ya kuwawakilisha nitaifanya kwa weledi, uaminifu, juhudi na maarifa yangu yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi, nami kwa kuwa sikupata fursa ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa hapa katika Bunge lako hili Tukufu, naomba nichukue fursa hii pia kusema kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais ilimaliza kazi yote, nami binafsi baada ya pale nilifanya ziara katika Jimbo langu la Mkuranga kwa ajili ya kutoa shukrani na Wanamkuranga wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Wanasema Mheshimiwa Rais aendeleo na kazi yake na imani yetu ya kuiona Tanzania ikielekea katika uchumi wa kati ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendeleo katika hoja hii inayohusu Mpango wa Maendeleo ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa Bungeni. Kwanza kabisa ningenda kugusa katika eneo la viwanda. Mkakati wa Serikali yetu ni mzuri, na mimi binafsi nauunga mkono kwa asilimia 100. Hata hivyo, yapo mambo ambayo ningefikiri kwamba hatuna budi kujielekeza kuona ni namna gani tunajipanga nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la viwanda, pale Mkuranga, neema ya viwanda imeshaanza kuonekana. Tunavyo viwanda vingi sana sasa ambavyo vinajengwa kila kukicha. Sababu yake kubwa ni pamoja na kwamba Dar es Salaam imeshajaa na sasa inapumulia katika Wilaya ya Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwetu imekuwa ni faraja kubwa sana na tungeomba jambo hili liendeleo na hata Serikali iendeleo kutusaidia kuhamasisha kuhakikisha kwamba wawekezaji wa viwanda mbalimbali wanaendelea kumiminika pale katika Jimbo letu hili la Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango mkakati wa maendeleo uliopita, wakati tunaujadili utekelezaji wake, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema neno, kwamba katika mambo yaliyotufanya tushindwe katika uwekezaji wa viwanda hapo nyuma ni pamoja na fidia za ardhi. Fidia ya ardhi ipo kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya mwaka 1999, lakini ninalo jambo ambalo nilikuwa nikilifikiri sana na nilikuwa nafikiri kwamba wataalam walichukue wakalijadili, waone ni namna gani tunaweza tukaboresha kitu cha namna hii. Hizi fidia za ardhi zimekuwa zikifanywa kila mara, lakini kama fidia ya ardhi inayohusu biashara, hasa ya viwanda na sisi tunataka uchumi wa viwanda kuelekea uchumi wa kati umilikiwe na Watanzania wenyewe, nafikiri tuanze kubadilisha mtazamo wetu. *(Makofi)*

Watanzania wamekuwa wakipewa fidia, si jambo baya, ni haki ya kisheria, lakini wakishapewa ile fidia, wanaelekea wapi. Tumeona watu wakipewa fidia Dar es Salaam, kule Kibada, Kigamboni watu wanalipwa fidia vizuri sana tu wanakwenda na sisi pale Mkuranga tutalipwa fidia, lakini baada ya hapo tunasogezwa, tunaondoka. Sasa tutasogea mpaka tutafika Rufiji, tukitoka Rufiji tutakwenda mahali pegine, ardhi ile tumepoteza na uchumi ule hatutaendelea kuumiliki. *(Makofi)*

Wazo langu nililokuwa nafikiri ni kwamba, ni lazima itafutwe mbinu nzuri zaidi ya kuwafanya Watanzania hawa wawe ni sehemu ya umiliki wa vile viwanda, wao mchango wao uwe ni ile ardhi yao. Tuliweke jambo hili vizuri badala ya kuja kuwapa fidia ya 1,500,000. Anaondoka Mtanzania yule wa pale Mkuranga, ameacha kiwanda kimetengenezwa pale, ile haitamsaidia. Kama ungetengenezwa mpango madhubuti na mzuri, maana yake ni kwamba eneo lake linakuwa ni mchango katika kiwanda kile atakula yeye, watoto wake, wajukuu wake na mpaka vitukuu vyake! Nadhani hii itakuwa ni namna bora zaidi ya kuwafanya Watanzania wamiliki uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo la viwanda, nimewahi kuzungumza kwamba pale sisi tunavyo viwanda vingi lakini viwanda hivi lipo tatizo la ajira, ajira zile zinazotolewa tunasema kwamba sio *decent*. Hazina staha! Vijana wetu wako wengi kweli wanapata vibarua mule ndani, ajira zile ndani ya saa kumi na mbili hawapumziki hata kidogo. Baada ya hapo analipwa 4,500, lakini ni ajira hatarishi kwelikweli. Naomba jambo hili wakati tunaendelea kuomba hivi viwanda tuliangalie vizuri ili tujiandae nalo lisije likatuletea matatizo hapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa maji ambao umesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba maji ni uhai na Mbunge mwenzangu wa Rufiji amesema vizuri sana hapa mchana huu wa leo juu ya suala la maji. Kutoka Rufiji, Mto Rufiji mpaka Mkuranga, hazizidi kilometa 100. Maji kule yamekuwa ni mengi mno yanaleta hata mafuriko! Tusaidieni tuondokane na tatizo la maji na liwe ni historia. Yatoeni maji kutoka Mto Rufiji, yafike Mkuranga, yapite Kibiti, Ikwiriri, Bungu na maeneo mengine ya Wilaya zetu hizi. Mkifanya hivi mtakuwa mmetusaidia sana. *(Makofi)*

Vilevile upo mkakati wa maji mkubwa pale katika Kijiji cha Kisemvule, ninggeomba maji ya pale Mpera yasiondoke kwenda Dar es Salaam mpaka kwanza na sisi watu wa Mkuranga tuwe na faida nayo maji yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaendelea kuangalia namna ya kuboresha uchumi wetu, naomba nizungumzie miundombinu. Wilaya ya Mkuranga kama tulivyosema, Jimbo letu hili lipo kabisa kimkakati kwamba ni sehemu ya kupumulia katika Jiji la Dar es Salaam. Ombi langu hapa ni kuhakikisha kwamba pesa katika Mfuko wa Barabara ziongezeke. Ziongezeke ili tuweze kutengeneza miundombinu yetu. Sisi pale tuna uchumi mzuri, lakini uchumi ule umekwama kwa sababu miundombinu ya barabara katika Jimbo hilo ni mibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu wa Rufiji alisema kwamba Rufiji katika umri wake wote toka iwe Wilaya hata nusu kilometa ya lami hakuna, sisi hata robo kilometa ya lami haipo katika Wilaya yetu ya Mkuranga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wataallah* aliyenijalia uzima na afya njema hadi nikichangia mapendekezo ya mpango mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti nami nisiwe mwizi wa fadhila, niwapongeze kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Mtambile kwa kunichagua kwa kura nyingi kwa kipindi cha Nne mfululizo, toka mwaka wa 2000. Miongoni mwa Wabunge *senior* mimi ni *senior*, nikimuona Mheshimiwa Bahati Ali Abeid pale na Mheshimiwa Faida Bakar kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kwenye ukurasa wa 34 kwenye Mpango huu ambao unashughulikia zaidi kuhusu utawala bora na naomba ninukuu kwenye (vi), inasema, kuimarisha mfumo kujitathmini kiutawala bora (APRM) yaani *African Peer Review Mechanism*. Utawala bora ni

jambo pana, jambo kubwa. Hakuna utawala bora kama Katiba inavunjwa katika nchi hii, hakuna utawala bora kama sheria hazifuatwi katika nchi hii, hakuna utawala bora kama haki za binadamu hazilindwi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanayotokea Zanzibar ni kitu gani, ni utawala bora au bora utawala! Inasikitisha! Inaumiza! Inasononesha sana. Leo hii tunaimba kila wakati tukisema kwamba tunataka amani na utulivu, lakini amani na utulivu wa midomoni. Inakuwaje leo kuna watu wanatembea kwa magari wakiwa na silaha za moto, tena wakiwa wamebeba misumeno, wanapita wanapiga watu, wanavunja vibanda, na Polisi wapo. Hee! jamani. (Makofi)

Mwaka jana tulipitisha Sheria hapa ya *The Firearms and Ammunition*, nani wamiliki wa silaha. Leo niulize jamani, inakuaje watu wanaachwa, wanapita wamevaa ma-socks maninja, kama *Janjaweed*, wakiwa na silaha za moto, wanakatakata vibanda vya watu, wanapiga watu, na Jamhuri ya Muungano ipo! Tabia hii mbaya lini mtaacha Serikali, hawa si watu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama kwa kipindi kirefu, kwa muda wa miaka 10 sasa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Naombeni sana Polisi mnisikilize kwa makini na naombeni sana Idara ya Usalama wa Taifa mnisikilize kwa makini sana. Usalama wa nchi hii ni wetu sote! Haiwezekani, haiingii akilini kwamba upande mmoja wa Muungano mmeuacha watu wanafanya watakavyo. Hii ni aibu, ni tabia mbaya. Ni aibu kwa Taifa hili, ndani ya nchi na nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki! Hili halikubaliki! Ni aibu. Nadhani kama tatizo ni uchaguzi, uchaguzi halali wa huru na haki ulioangaliwa na Mataifa mbalimbali, uliokubalika na Mataifa mbalimbali, ulikuwa tarehe 25, Oktoba. Umeshapita, Rais halali wa Zanzibar ambaye kwamba hatua zote za uchaguzi kuanzia kupiga kura, kuhesabu kura, matokeo yalibandikwa katika mabanda yote na Mawakala wakapewa matokeo na mshindi alikuwa ni Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye alipata kura 207,847 sawa na asilimia 52.84. (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Muongo!

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Ukome na Dkt. Shein alipata kura 182,011 sawa na asilimia 46.28. Matokeo hayo yalibandikwa yote.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa ukae, taarifa

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba na sheria zinazotuongoza nchi hii ya Tanzania, matokeo ya Urais kwa Zanzibar hayajatangazwa rasmi namwomba mtoa hoja aondoe maneno aliyoyazungumza

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesimama kwa Kanuni gani, ataje kanuni! Haondoi maneno.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni taarifa

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Taarifa yake siipokei, naitupa. Tulia mgangwe maradhi si kifo!

**MBUNGE FULANI:** Kama hupokei na mimi sikai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba tusikilizane. Taarifa iliyotolewa kwamba habari unazotoa siyo sahihi kwa mujibu wa Tangazo la Serikali. Kwa hiyo, naomba ufute kauli yako mara moja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwe makini sana, tunaposema uchaguzi ulifanyika, matokeo ya Urais yalibandikwa katika mbao zote.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Haya, taarifa. Tuendeleo na taarifa mara moja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mtanipa taarifa ngapi!

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti, 63(3) ndiyo niliyosimamia. Mzungumzaji anayezungumza sasa hivi anasema uwongo. Kwa sababu kwa kuthibitisha Kanuni ya 63 (4), nathibitisha kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 104 ndiyo iliyosimamia uchaguzi wa Zanzibar na 119 Katiba ya Zanzibar Tume ya Uchaguzi ndiyo inayosimamia uchaguzi wa Zanzibar, Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, kifungu cha 42 (1-5) ni kwamba Tume peke yake ndiyo yenye mamlaka ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais. Sasa atuambie matokeo anayoyatangaza yeye yametokana na Tume ipi?(Makofi)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa! Mheshimiwa Mwenyekiti, haikutangaza Tume, katangaza Jecha peke yake.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini Mheshimiwa! Mheshimiwa ambaye alikuwa akitoa hoja, naomba uipokee hiyo taarifa na ufute kauli yako.

**WABUNGE FULANI:** Hafuti!

**MWENYEKITI:** Maneno ambayo umezungumza hayajatatamkwa rasmi na Serikali, kwa hiyo naomba ufute kauli yako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Kuna ushahidi wa fomu kutoka kisanduku kimoja baada ya kimoja, Unguja na Pemba, ndiyo maana...

**MWENYEKITI:** Naomba mheshimu Kiti!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa taarifa hizo, tuna uthibitisho wa kusema kura zilizopigwa Pemba, idadi ya wananchi wanaoishi Pemba siyo iliyopigiwa kura. *(Makofi)*

*(Hapa Baadhi ya Wabunge walizomea)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Huyo ni muongo, hatufuti hakuna Serikali Zanzibar, kuna majambazi.

**MBUNGE FULANI:** Hizo bangi!

**MWENYEKITI:** Jamani, naomba tusikilizane. Mheshimiwa hayo ambayo umezungumza unaweza kuthibitishia Bunge hili?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo

**MWENYEKITI:** Tunaomba uwasilishe uthibitisho wako, na ikiwa utashindwa, hatua za kisheria zitachukuliwa. Naomba uendelee umalizie. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawatambui Kanuni na Katiba hao.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea. Kwamba matokeo yote katika hatua zote za uchaguzi kuanzia kupiga kura, kuhesabu kura na baadaye majumuisho katika maeneo mbalimbali, Majimbo yote yalibandikwa kwenye kuta. Matokeo ya Rais wa

Zanzibar yote yamewekwa kwenye kuta, Mawakala wote walipewa ushahidi kamili, wapo. Wawakilishi wote walipewa vyeti vyao 27. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba urudi kwenye hoja iliyo mezani.

**MHE. MASOUD ABDALLAH. SALIM:** Utawala bora, Wawakilishi wa CUF 27.

**MWENYEKITI:** Suala la Zanzibar naomba lisizungumzwe kwenye ajenda hiyo kwa sababu halihusiani na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Naomba tuheshimiane na tuheshimu Kiti, Mheshimiwa kama una hoja ya kuchangia katika maeneo mengine suala hili limo ndani ya mikono ya Serikali, tunaomba uheshimu vinginevyo kama hujasikia itabidi nichukue hatua ya kukutoa nje tafadhalli sana.

*(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele)*

**MWENYEKITI:** Endelea na hoja nyingine, kama ni hiyo naomba ukae.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo niko katika APRM *(Africa Peer Review Mechanism)* Mpango wa kujitathmini wenyewe kwenye utawala bora suala la Katiba, suala la Sheria lazima hapa lizungumzwe. Kwa hiyo, Wawakilishi ishirini na sita walipewa vyeti vyao kama ilivyo kawaida. Naomba niendeleo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba nimruhusu Mwanasheria Mkuu

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii niwashauri Waheshimiwa Wabunge. Tumeshauri hapa mara nyingi na mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi Makamu wa Rais, Muungano amelifafanua vizuri suala hili. Suala la Uchaguzi wa Zanzibar kwanza linasimamiwa na Katiba ya Zanzibar. Katiba ya siyo moja ya masuala ya Muungano, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inazaliwa na hiyo Katiba, ikiwa kuna hoja zozote kuhusiana na utendaji wa Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ambayo ni Tume huru isiyoingiliwa katika maamuzi yake, suala hilo linapaswa lijadiliwe ndani ya vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linaloingilia mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ina Katiba yake ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar suala hili linasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Sisi tumeshauri hapa kwamba

ikiwa kuna hoja yoyote ya msingi basi suala hili lishughulikiwe na Mahakama ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri! Naomba Waheshimiwa Wabunge tuliheshimu Bunge hili tusifanye Bunge hili kuwa uwanja wa siasa. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeshatangaza tarehe ya marejeo ya uchaguzi, wanaoamini kwamba wana uwezo wa kushinda kihalali waende wakashindane kwenye uwanja kule siku ya marudio ya uchaguzi. Kwa sababu Bunge hili halitachagua Rais wa Zanzibar na wala Bunge hili halichagul Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Matokeo ya uchaguzi wa Zanzibar yanajadiliwa na mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya endelea

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Muda wangu ulindwe, niko makini, naendelea kusimamia hoja yangu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowaonesha Watanzania, ninachowaeleza tena kwenye Bunge hili ni jinsi gani ya uonevu ukandamizaji wa demokrasia, tusiwe na malumbano tusiwe na jazba, naomba niseme kwamba, wakati huo Mwenyekiti wa Wilaya ya Chakechake ambaye ni Mbunge wa Chonga, Mohamed Juma Khatibu Mwachawa, masaa mawili kabla ya kufutwa kwa shughuli ile pale waliitwa Makao Makuu ya Polisi na wakaambiwa hivi, naomba mtulie, wafuasi wenu muwatulize kwa lolote litakalotokea! Sasa hoja kwa nini tusiseme kwamba kuna mkono ambao ulilazimisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleee nije kwenye mambo ya usafiri wa baharini.

**MBUNGE FULANI:** Hayo ndiyo muhimu.

**MWENYEKITI:** Endelea naomba utulivu tafadhali Bungeni.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mambo mengi katika hali ya kuwanusuru wananchi, sioni Mpango wa aina yeyote! Sioni mpango wa aina yeyote wa kununua meli kutoka Tanga kuja Pemba. Sasa Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mpango huu uko wapi? Mpango wa kunusuru maisha ya watu, sioni Mpango wowote katika kitabu chako wa kununua meli kutoka Dara es salaam kuelekea Mtwara, meli za uhakika! Sioni mpango wowote ambao utanunua boti za kisasa katika Bahari ya Hindi na kwenye maziwa, pale inapotokea ajali, watu kila siku wanakufa! Mpango uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo halikubaliki. Ni jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa na lazima lifanyiwe kazi, lakini kubwa kuliko yote Rais aliyepita alisema wizi, ubadhirifu na ufisadi hautavumiliwa. Marehemu Dokta Abdallah Omari Kigoda, Mungu amlaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kigoda alisema kwamba, umaskini uliopo katika Mikoa ya Kusini kwa mujibu wa Viwanda vile vya Korosho, viwanda ambavyo vimebinafishwa basi vitafanyiwa kazi, alituhidi kwamba, wale wote waliopewa viwanda na hawakuviendeleza atawaita, lakini sasa hadi leo hakuna aliyeitwa na kubwa zaidi tulikuwa tunauliza viwanda vile mmiliki wake ni nani?

*(Hapa Kengele Ililia)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kengele ya kwanza tulia! Viwanda vile wamiliki wake ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe viwanda vile imebainika na imedhihirika kwamba viwanda vile vimebinafishwa Tanzania ilikopa dola milioni ishirini kwenye miaka ya 1970 na 1980 kutoka Japani vikajengwa viwanda vya korosho kule Lindi na Mtwara badaye wamekwenda kupeana vigogo wa Serikali kama njugu, wakapeana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Dkt. Mpango na Msaidizi wako mniambie viwanda ambavyo hasa nataka kuvitaja ni nani waliomilikishwa? Kwanza naomba uniambie Mtwara Mjini, ambacho kinaitwa Taasisi ya Fursa kwa Wote nani mmiliki wake? Mheshimiwa Naibu, *Newala One* nani mmiliki wake, mtuambie hapa? Likombe nani mmiliki wake? Masasi nani mmiliki wake? Lindi Mjini nani mmiliki wake? Nachingwea nani mmiliki wake? Mtama nani mmiliki wake? Aibu tupu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema tunakopa mabilioni ya fedha, wananchi wanaendelea kuwa masikini! Watu wanauza korosho ghafi badala ya kuuza korosho safi, tatizo nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu mimi naona sasa kwamba ni vyema Serikali ikae makini kwamba kama iliahidi kwamba kuna wakati ambapo watu wale ambao wamepewa viwanda vile kwa bei ya kutupa viwanda vile haviendelezwi vimekuwa ni maghala virejeshwe. Huo ndiyo msingi, ili wananchi wale wapate faida iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hayo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, tunaendelea na demokrasia ya kweli, nakipongeza Chama changu cha Wananchi CUF, nampongeza Rais halali Maalim Seif Sharrif Hamad

wa Zanzibar na Baraza Kuu la Uongozi wa Taifa CUF kwa kutoingia katika uchaguzi,. Tunasema kwamba tuko makini, UKAWA tuko makini na Chama cha Wananchi CUF kiko makini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Rukwa kwa kuniwezesha kuwawakilisha Bungeni, Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa ushindi mkubwa alioupata na kuanza kazi mara moja ya utekelezaji wa ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa utakaokuwa dira ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kuchangia na kuishauri Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwamba, mpango huu ungetoa kipaumbele cha kwanza cha maji safi na salama hivyo kutokana na shida kubwa wanayoipata wanawake wa Mkoa wa Rukwa kufuatia maji kwa mwendo mrefu wakati huo shughuli za kilimo zinawasubiri, kulea watoto kunawasubiria, hata akinababa wanawasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Mkoa wa Rukwa wanapata shida sana ya maji, imepelekea kwamba na wananachi wengine wameamua kuchimba visima vya kienyeji ambavyo vimepelekea kuleta matatizo ya watoto kutumbukia kwenye visima hivyo na vijana wengine wawili kufariki kwa sababu ya kutumbukia kwenye hivyo visima.

Mheshimiwa Injiniya Stella Manyanya yupo hapa ni shahidi, naishukuru kwanza Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilileta mradi wa bilioni 30, lakini huo mradi hakuna maji mpaka sasa hivi. Naomba niishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi huo mradi uishe mara moja ili tatizo la maji liweze kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye suala la kilimo, ili kwenda kuwa Tanzania ya viwanda lazima wakulima waangalie sana katika kuwapatia zana za kilimo na pembejeo. Suala la pembejeo ni muhimu sana kwa sababu wakulima wanapata pembejeo na mbolea kwa kuchelewa. Ili tuweze kwenda na wakati kwa Tanzania ya Viwanda lazima wakulima wapate pembejeo kwa wakati na mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la uwezeshaji, kama ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyoeleza kwamba itawawezesha wanawake na

vijana kwa kutoa milioni hamsini kwa kila kijiji, Mpango huu ni mzuri naomba sasa Serikali itekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuingia tena kwa mara ya pili katika mjengo huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Kwela kwa kuniwezesha, kwa kuniamini kunirudisha tena ili niweze kuwatumikia na wananchi hao walisimama kidete sana japo kuwa kulikuwa na mizengwe mingi sana lakini wananchi waliweza kusimama na hatimaye kuniwezesha kurudi katika ukumbi huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Magufuli, kwa kasi hii aliyoianza ya kusimamia wananchi. Ni kasi ya hali ya juu na mimi nawapongeza wale ambao wanatambua kwamba kasi ile ndiyo iliyokuwa inahitajika katika nchi hii kwa sasa. Nawapongeza na Mawaziri wote ambao wametambua hivyo na wameanza na kasi hiyo, ninachowaomba Mawaziri wote mtambue kwamba mna watu wenu mpaka huko chini waimarisheni, wabadilisheni kifika ili waendane na kasi hii ya Mheshimiwa Magufuli. (Makofi)

Kwa sababu Mheshimiwa Magufuli hawezi kufanya kazi peke yake bila sisi wote kujibadili kufanana na yeye, atachoka lazima tumsaidie na kumsaidia ni kuweka mtandao wa kasi kuanzia ngazi ya juu mpaka kule chini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu katika kuchangia Mpango wa Maendeleo 2015/2016. Sisi tunatambua kwamba mpango huu wa maendeleo umelenga katika kukuza uchumi, katika kuhakikisha wananchi wanaondokana na umaskini, katika kukuza pato la Taifa. Hata hivyo, nataka nichangie kwa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sisi wote kwamba nchi yetu sehemu kubwa ya wananchi wanategemea kilimo na katika kilimo, nataka nizungumzie jambo moja, lazima tujiridhishe hivi Watanzania wote waliopo mijini na vijijini wote wana ardhi ya kutosha kuwaendeleza? Hilo ni la kwanza kujiuliza, na mimi nasema baadhi ya maeneo yanawezekana yanatosha lakini maeneo mengi bado ni tatizo. Ni tatizo kwa sababu tumeachia watu wachache wameatamia maeneo makubwa, Serikali inazungumza kila siku haichukui hatua. Sijaona ni kwa sababu gani Serikali inachelea kuchukua uamuzi wa haraka, hii haitaji hata kusubiri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara nyingi nimekuwa nikisimama hapa nikitetea wananchi wa Jimbo la Kwela kuhusu shamba la Malonje nimelizungumza kadha wa kadha hatimaye hata kwenye uchaguzi imeniletea mpambano mkubwa sana lakini Mwenyezi Mungu akisimama hakuna ubishi ndiyo maana niko leo hapa. Wananchi wa Jimbo la Kwela nitaendelea kuwatetea lazima shamba hilo lirudishwe mikononi mwa wananchi. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe Mwenyewe umefika mara ya mwisho ukasema mimi nitakuwa mtu wa mwisho kuzungumzia suala la ardhi hii ya shamba hili la Malonje naomba utimize ahadi yako wananchi wale warejeshewe lile shamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine katika upande wa ardhi na mimi nataka niishauri Serikali. Serikali ni kweli ilitenga Mapori ya Akiba. Unaposema mapori ya akiba lazima uende na pande zote mbili, mapori ya akiba aidha kwa wanyama lakini mapori ya akiba kwa binadamu, tusiende upande mmoja. Wakati mapori yale yametengwa baadhi ya wananchi walikuwa hawajaongezeka lakini sasa hivi watu wameongezeka. Unaita pori la akiba lakini wananchi wananyanyasika hawana kwa kulima, pori hilo halina mnyama hata mmoja hata ndege mmoja, Jamani huu ni ubinadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Pori la Uwanda Game Reserve. Linatesa wananchi isivyo kawaida na halina faida yoyote kwa Serikali na nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii nimeongea na wewe, nimekusimulia kwa kirefu sana na nikakuomba ufike, inawezekana maneno haya ninayozungumza usiyaamini, basi ufike ukaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakatiza mle kwenye lile pori la akiba, wananyang'anywa majembe, wananyang'anywa panga zao, wananyang'anywa fyekeo, pikipiki, wanapigwa wana nyanyasika, wakati pori lenyewe halina mnyama hata mmoja. Jamani tumefika wapi hapo? Haya mambo mengine ni ya kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uamini, maana mara nyingine mnachukulia sisi kama ni wanasiasa uende, namwomba Waziri wa Maliasili afike eneo lile. Hata hivyo, nikupongeze kwa sababu nilipokueleza ulitoa amri ya wananchi kurejeshewa vifaa vile walivyokuwa wamenyang'anywa, nakupongeza katika hilo na naomba uendeleo katika kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni umeme, tunatambua kabisa maendeleo hayawezi kuja bila umeme, lakini nitoe masikitiko kidogo katika Jimbo langu au Wilaya yangu ya Sumbawanga Vijinini, pamoja na Wilaya hii kuwa ya siku nyingi, pamoja na jitihada zote za Serikali, Jimbo langu halina umeme hata kijiji kimoja. Vijiji 114, Kata 27, watu zaidi ya 450,000, halina hata kijiji kimoja chenye umeme

**MBUNGE FULANI:** Pole! Upo Tanzania kweli!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Wakati mwingine Serikali inaweza ikatutambua sisi viongozi, tunaotokana na Chama cha Mapinduzi kama vile tunaipinga Serikali hapana, ni masikitiko ya kuona wananchi wanahangaika, hivi Serikali hii inaendeshwa kwa upendeleo?

**MBUNGE FULANI:** Anakusikia Muhongo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Muhongo ni mchapakazi na nimeongea na wewe ninataka kwa kweli wananchi hawa wapate umeme, awamu ya kwanza ulisema utatoka Sumbawanga- Laela, ni nguzo tu zimelala, awamu ya pili ni Ukanda wa Ziwa Rukwa, kwa hiyo naishauri Serikali iweze kuhimiza kwa haraka ili wananchi hawa waweze kupata umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni kupunguza ukubwa wa maeneo ya Utawala, nazungumzia Jimbo langu la Kwela ni Jimbo kubwa na lina watu zaidi ya 450,000 lina sifa zote za kugawanya na nilipozungumza hapa kwa mara ya mwisho na Waziri Mkuu Mstaafu ali-*support*, kwa sababu anafahamu. Hata Mheshimiwa Keissy juzi amezungumza, hata baadhi ya Wabunge ambao wamekwenda kule akina Paresso wanafahamu, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Aeshi wanafahamu, ni Jimbo kubwa kuliko, wakati mwingine unasema nitafanyaje kazi katika Jimbo hili, ni kubwa ukienda upande huu wengine wanakusahau.

**MBUNGE FULANI:** Eee kweli!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Naishauri Serikali na bahati nzuri uliyekuwa Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Manyanya uko hapa, naomba jambo hili tulivae wote, tuihabarishe Serikali inatuletea matatizo makubwa sana, Jimbo hili linatakiwa kugawanyika, kama tunatenda haki kwa sababu lina sifa zote. Yapo Majimbo yamegawanywa zaidi ya mara 3, hayana sifa zote. Lakini Jimbo langu limebaki pale pale.

**MBUNGE FULANI:** Mwambie na mapendekezo tumeleta.

**MBUNGE FULANI:** Hatari.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mapendekezo tumeleta yote ya kuomba Jimbo, kuomba Wilaya, kuomba Halmashauri, hakuna hatua hata moja ambayo imechukuliwa, sasa jamani na hawa wananchi mnawaweka katika

upande gani? Naishauri Serikali ijariibu kutenda haki kwa maeneo yote yenye matatizo kama haya, nimeona nilizungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miundombinu ya barabara, ninapozungumzia barabara nizungumzie barabara ya kutoka Kibaoni, kuja Kiliamatundu na kwa maana hiyo ukifika Kiliamatundu unatakiwa ukatishe uende Kamsamba, ukatokee Mloo. Ile barabara ina zaidi ya kilometa 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali kwa sababu katika ilani mmeiweka katika kipaumbele cha kuifanyia usanifu. Hata hivyo, naomba isiwe usanifu ile barabara inatakiwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ina uchumi mkubwa sana. Hizi kilometa 200 ninazosema karibuni kila baada ya kilometa tano kuna kijiji cha wananchi wenye uzalishaji, ukitengeneza barabara hii utakuwa umeufungua ukanda ule kiuchumi, utaongeza pato kwa wananchi, utaongeza pato kwa Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kushughulikia barabara ile kwa kiwango cha lami, ikiwa ni pamoja na kutengeneza daraja la mto Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa miaka mitatu tunaambiwa upembuzi yakinifu tumechoka na maneno hayo, tunataka waanze kujenga. Ukijenga daraja hilo umeshawaunganisha wananchi na Wilaya ya Momba wanaotokea Mloo, uchumi utaenda kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuchukua jambo hili katika masuala ya utekelezaji, kwa sababu linaumiza sana na ni ukanda wenye uchumi mkubwa sana, uzalishaji wa mpunga, ufuta, uvuvi. Sasa tunapozungumzia kutengeneza barabara si tuangalie na vigezo, vigezo ni kuongeza uchumi wa wananchi na Taifa zima kwa ujumla siyo unapeleka barabara huna hata matumaini ya kurejesha uchumi wenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umeongezeka nashukuru.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.(Makofi)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, kuchangia, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, ambaye ametupigania mpaka leo tupo hapa. Jambo la pili niwashukuru sana wananchi wa Tarime ambao kwa miaka mingi na miaka yote wameonesha imani kwangu walinichagua, kuwa Diwani wa Kata ya Tarime Mjini nikiwa Mwanafuzi wa Chuo Kikuu, lakini vilevile pamoja na mapambano makali yaliyokuwepo kwenye uchaguzi huu mpaka mauaji yaliyofanyika tarehe kumi mwezi wa Tisa, wananchi walisimama imara na wamenileta hapa na

nataka niwahakikishie nitawawakilisha na nitasimamia kero zao kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana usiku nilijitahidi sana kusoma na ku-google nchi mbalimbali kuhusiana na Uongozi, nikajaribu kuangalia mambo yaliyofanyika siku za hivi karibuni hapa Bungeni, ya Polisi kuingia ndani ya Bunge wakiwa wamevaa *Head gear*, bunduki, sijui mipini kujaribu kupiga Wabunge waliokuwa hawana silaha. Nikagundua kwamba hata Idd Amini, hata Adolf Hitler, hakuwahi kuingiza Polisi kwenye Bunge kujaribu kupiga watu wanaopinga. Kwa hiyo, hapo mtajaza wenyewe kwamba mna uongozi wa aina gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuongoza nchi hii kwa takwimu za uongo. Hapa Dkt. Mpango naomba unisikilize vizuri, nimesoma vitabu vya Mpango hivi, takwimu zilizoko hapa, ni takwimu feki, na kwa takwimu hizi hamuwezi kufanya kitu chochote hata muwe na nia njema. Kwa nini nasema hivyo, kwa mfano, maji vijijini kitabu hiki kinaonesha cha Mpango kwamba kuna maji Vijijini kwa asilimia 68.

**NAIBU WAZIRI (SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU- MHE. DKT. ABDLLAH S. POSSI):** Taarifa

**MHE. JOHN W. HECHE:** Nimejaribu kuangalia kwenye Jimbo langu peke yake...

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI (SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU- MHE. DKT. ABDLLAH S. POSSI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8), taarifa tu kuweka rekodi sahihi. Adolf Hitler wakati wa Utawala wa *Nazi Nationaal Socialistische* hakukua na Chama kingine chochote kinachompinga. Kwa hiyo, hakukuwa na mtu anayepinga mazungumzo yake. Kwa hiyo *is the question of history, you should have correct history*, tusidanganyane humu ndani.

**MWENYEKITI:** Haya tumepokea taarifa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu

**MHE. JOHN W. HECHE:** Dkt. Possi nakuheshimu sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Mwanasheria Mkuu amesimama naomba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nyingine kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, shughuli za Bunge zinaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni na Sheria ya Mamlaka na Haki na Kinga za Wabunge na Sheria zile pia zimeweka makosa ya

jinai, kwa hiyo Askari wanaweza kulazimika kuingia humu ndani, ili kutuliza ghasia na fujo.

Kwa hiyo, kuingia kwa Askari siku ile ndani humu ilikuwa ni halali kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka, Haki na Kinga za Wabunge na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili. Huo ndiyo Utawala Bora, Utawala Bora ni Utawala wa Sheria. Serikali isingeruhusu watu wakaanza kuuana humu ndani, kwa hiyo nimeona niitoe hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa hiyo taarifa Mwanasheria Mkuu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu, naamua kuwapuuza wote niendeleo tu. Nilikuwa nazungumzia kuhusu takwimu. Takwimu za maji kwa mfano vijijini wamesema maji yapo kwa asilimia 68, lakini nimeangalia Jimbo langu ni Jimbo la Vijijini tuna Kata 26, katika Kata 26 hizo asilimia 68 ya 26 ni Kata 17 ina maana kwa mujibu wenu kwenye Kata 17 kuna maji hivi sasa tunavyozungumza, kitu ambacho ni uwongo na hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mijini mmesema kuna maji asilimia 95, hii ni aibu ina maana kila watu 10 watu tisa wanapata maji, au kila watu 100, watu 95 wanapata maji, lakini pale Dar es Salaam ni kielelezo, kipindupindu kinawaumbua kila siku, kwamba hakuna maji na takwimu mnazoleta humu ni za uongo. Kwa hiyo, kama mnataka kulitoa Taifa hili hapa ni lazima tuwe na takwimu ambazo zinaeleza ukweli, na takwimu ambazo zitawasaidia kujenga kwenda mbele, lakini mkija na takwimu za uongo hapa mnajidanganya wenyewe na wananchi wanawaona.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, zetu ni mbovu...

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tunatoa taarifa za uongo, suala la upatikanaji wa maji, huwa hatupimi kwa namba ya Kata, huwa tunachukua idadi ya watu wanaopata maji katika eneo fulani *percentage* yake. Ukiingia mjini tunaangalia mji huu unawatu wangapi na ni wangapi wanapata maji katika umbali wa mita 400, ndivyo tunavyofanya takwimu zetu, sasa ukitaka kusema za kwako ulete zile ambazo ni sahihi, siyo kwa kubabaisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa taarifa endelea.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Nawashauri Mawaziri tulieni msikilize, kwa mujibu wa Sera ya Maji ya Taifa hili, maji ambayo mnahesabu kwamba watu wanapata wapate ndani ya mita 400 kutoka wanapokaa, sasa kwenye hivi vijiji mimi ninavyosema watu wanafuata maji mpaka kilometa moja, mbili, sasa unatoa taarifa gani hapa. Tulia usikilize tukueleze wananchi watapima kule anasema nani uongo kama maji yapo au kama hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, barabara zetu ni mbovu, kwa mfano barabara za Tarime. Kutoka Tarime kwenda Serengeti ambako kuna Mbuga kubwa ya wanyama. Inapita Nyamongo kwenye eneo la Mgodu wa Nyamongo, barabara ni mbovu, na mimi ninamwomba sana Waziri achukue hii hoja ya barabara hii iwemo kwenye Mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati; leo mnakuja hapa kuzungumza kuendeleza Taifa, wakati watu wanapikia kuni. Dar es Salaam peke yake, ambayo mkaa unakwenda pale magunia tani na tani, mngeweza kama kweli mnataka kuendeleza Taifa hili, kuliko kurukaruka hapa, mngechukua Dar es Salaam ile peke yake, mkazuia utumiaji wa mkaa na magogo na kila kitu mkapeleka gesi pale kwa bei rahisi watu wote watumie gesi pale Dar es Salaam, Arusha na Mwanza, tayari mngekuwa mmesaidia misitu ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnakuja humu mnaimba tu misitu tuta-conserve misitu, mazuia watu. Kama kule Jimboni kwangu naona eti Afisa Misitu anazuia watu wasitumie mkaa, nimemwambia wananchi watakuchapa wewe! Wapelekee kwanza gesi ndiyo uwazuie kutumia mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Serikali; nataka mtuambie hapa, hicho mnachojisifia kwamba mmekusanya mwezi wa 12 ni *arrears* au ni vyanzo vipya mmeleta na mmekusanya. Kwa sababu msije mkajisifu hapa tumekusanya tirioni 1.4 kumbe ni *arrears* za huko nyuma ambazo ni za watu ambao ni majipu na majipu wengine wako humu mnawajua wanatakiwa walipe na ni madeni. Sasa huko mbele mmetengeneza vyanzo gani, mmvionesha wapi kwenye Mpango huu, vyanzo vipya. Leo mnataka mchukue pesa kwenye Halmashauri na hili msithubutu Mheshimiwa Waziri, Halmashauri watu wakusanye pesa wao wenyewe, wakupelekee Benki Kuu, halafu wewe ndiyo urudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, tunaidai Serikali pesa za ardhi ambazo ni asilimia 30 miaka karibia sita zaidi ya milioni 500, tunapeleka pesa zetu wakati wa kurudi hazirudi. Leo ndiyo wamerudisha milioni 27, leo tena tuchukue pesa zetu za mapato ya ndani tuwapelekee na nyie mnajua, kama mnataka kuendeleza uchumi wa watu kule vijijini mabenki yaliyoko kule Wilayani ndiyo yanakopesha watu wanaofanya biashara ndogondogo na benki hizi zinategemea pesa kutoka kwenye Halmashauri, leo

mnataka mchukue pesa zitoke Halmashauri mabenki yakose pesa, yashindwe kukopesha watu wetu kule chini, biashara zife kule chini, halafu mnasema mnataka kuendeleza Watanzania au mnataka kuwa-*suffocate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekuja hapa mnasema viwanda, kila mtu anasimama hapa viwanda. Viwanda gani, viwanda vinategemea *foreign direct investment*, Wazungu hawa mnaoenda kuingia mabakuli wamesema wako *concerned* na mambo yaliyofanyika Zanzibar, hakuna amani, Zanzibar kule kuna Nkurunziza. (*Makofi*)

Mmechukua hamtaki kutoa nchi kwa mtu aliyeshinda, kwa maana hiyo Wazungu wanakwenda kuzuia hiyo misaada sijui mtapata wapi pesa za kuanzisha hivyo viwanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika naomba ukae.

**WABUNGE FULANI:** Bado!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mungu

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge dakika zako ni chache, kwa hiyo naomba uwe-*very brief*.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mungu kwa kupata muda, lakini mimi siyo wa kuzungumza dakika chache ila nitajitahidi maana mara nyingi huwa napiga hapa nusu saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Dkt. Mpango kwa kuleta taarifa nzuri. Nianze na suala la viwanda mimi nizungumzie kilimo cha biashara. Ni vema Serikali ikajikita kwenye kuanzisha viwanda vidogo ili wakulima hasa wa matunda, badala ya makampuni yanayotuzia *juice* kununua *juice* nje ya nchi, yanunue matunda yetu ya ndani. Tukifanya hivyo tutakuza na tutakuwa na kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme watu wamekuwa wakizungumza sana humu ndani ya Bunge, wanazungumza kuhusu Polisi kuingia humu ndani. Nataka leo nisimame kuwatetea Polisi kwa sababu wao hawawezi kuja humu. Polisi ukimwona mahali popote kaenda kama *Field Force*, ujue ameitwa na watu wa eneo hilo. Wabunge, tuache tabia ya kuwaita Polisi, ukifanya fujo unawaita Polisi, na Polisi wameshaingia Kanisani wakati wa mgogoro ule wa Dayosisi ya Pare, Polisi wameshaingia Msikitini wakati wa fujo, Polisi wameshaingia Bungeni baada ya Wabunge wa Upinzani kuanzisha fujo. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Waambie hao!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukimwona Polisi kaingia mahali ujue kaitwa, na kama ninyi ni wageni hamuelewi utaratibu wa humu ukianzisha fujo umeita Polisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna watu wamekuja hapa bado hawajapigwa semina, kwa hiyo ngoja leo niwaelimisha. Mmesema vizuri na mfano uliotolewa na Mheshimiwa Heche hapa mdogo wangu ambaye mimi nimemfundisha siasa, kwamba eti anataka kulinganisha Chama hiki na kina Hitler, lakini leo nawaambia Chama chochote cha Upinzani duniani kikishindwa kushinda uchaguzi katika vipindi vitatu, kinageuka kuwa chama cha kigaidi, ndiko wanakoelekea hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndipo wanapoeeleka, maana kinakuwa chama sugu, kinakuwa Chama cha Upinzani sugu, tulikubaliana wakati ule, kwamba ili kuthamini haki za binadamu walau kila chama kitakachoshinda basi kilete mtu mmoja walau mwenye ulemavu wa ngozi. Yupo wapi albino wao hawa? Wabaguzi hawa na inawezekana hata wakati ule wa mauaji wako inawezekana walikuwa wanahusika hawa, yuko wapi? CUF waliwahi kuleta hapa alikuwepo Mheshimiwa Barwany, CCM yule pale wa kwao yupo wapi hawa? *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze hapa, kwamba usiwaone wanazungumza hivi na nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana, nimpongeze sana Mzee Lowassa, Lowassa aligundua hawa wamemchafua sana akaamua kwenda kwao wamsafishe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Lowasa aligundua walimwita fisadi, walimwita fisadi papa, Edward Lowasa ana akili sana. Mchawi mpe mtoto amlee, akajua nakwenda kwao wanisafishe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mtanzania mwenye akili atakayewasikiliza tena hawa, hivi wewe unakaa na jirani yako mwanaume anakuja anakwambia mke wako malaya, mke wako mhuni unamuacha, asubuhi anamuoa utamwamini tena? Hawa hawaaminiki, hakuna kitu watakachokieleza wakaaminiwa duniani. Kwa sababu wana ndimi mbili kama za nyoka hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachokisema leo kesho watakibadilisha hawa, ndimi mbili za nyoka...

**MBUNGE FULANI:** Tena nyoka wa kijani.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mnawaona leo wanasema hiki, leo wanageuka hivi, nataka nichukue fursa hii kumpongeza Jecha, kwa utaratibu huu wa kila Mzanzibar kuwa Tume ya uchaguzi, Jecha alikuwa sahihi kufuta yale matokeo. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anajifanya Tume, wenyewe unaowaona hapa wameletwa baada ya Tume ya Uchaguzi kuwatangaza ila Mheshimiwa Seif wanamtangaza wao, hawa ni wanafiki wakubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, nakushukuru. Muda wako umekwisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Washa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niseme jana kuna mtu mmoja alisimama hapa akasema Serikali hii inaanzisha slogan mara Hapa Kazi tu...!

*(Hapa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Niachie hawa nawamudu mimi tu, hawa hamna kitu...

**MWENYEKITI:** Jamani muda umekwisha kwa mujibu wa Kanuni, Katibu!

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niahirishe Bunge kwa siku ya leo hadi kesho tarehe 3 Februari, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.45 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Februari, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*

## Kikao cha Saba – Tarehe 3 Februari, 2016

### KAMATI YA MIPANGO

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Tunaendelea na shughuli yetu ya leo ambapo Bunge linaketi kama Kamati ya Mipango kuendelea na hoja iliyo mbele ya Bunge.

Kwa orodha ya wachangiaji niliyonayo bado tuna shughuli pevu lakini tujitahidi. Tuanze na hawa watatu au watano wa mwanzo ili mjipange vizuri. Tutaanza na Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Conchester Rwamlaza. Karibu Mheshimiwa Soni, hayupo, basi Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia uzima. Vilevile niwashukuru wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini kwa kunirejesha tena kwenye nafasi hii. Nawaahidi nitawatumikia kwa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu wote wanaounga mkono hoja hii. Katika kuchangia, naomba nianze na kuiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika ukurasa wake wa 16, alijaribu kubainisha maeneo ambayo yakishughulikiwa yanaweza kuwa na mchango mkubwa sana katika kuinua uchumi wa nchi hii.

Vilevile alielezea namna ambavyo sekta mbalimbali zinavyochangia katika uchumi wa Taifa na kutoa ajira. Sekta hizo ni kilimo, uvuvi na ufugaji bila kusahau wachimbaji wadogowadogo. Tunafahamu kwamba kilimo kinachangia kuwapatia ajira Watanzania kwa zaidi ya asilimia 75. Vilevile kwenye GDP kilimo kina mchango wa zaidi ya asilimia 25 na kinasaidia kutuingizia fedha za kigeni kwa zaidi ya asilimia 30. Kwa hiyo, kwa wachumi na maafisa wetu wanaopanga mipango, hapa ndiyo mahali ambapo pangezingatiwa tungeweza kuubeba mzigo mkubwa na kuhakikisha kwamba tunaboresha uchumi wa nchi yetu ambao umezorota kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia napenda kuangalia katika suala zima la kilimo. Ninavyoona mimi kilimo hatukiendeshi vizuri licha ya sera nzuri ambazo tumeziweka kwenye kilimo za kuchangia pembejeo mbalimbali, lakini bado kumekuwa na uchakachujaji ambao umesababisha matarajio kutofikiwa.

Inaonekana hakuna anayesimamia kilimo kwa karibu. Nashukuru kupata Waziri wetu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, naomba ajielekeze kwenye kilimo. Ametueleza kwenye historia yake kwamba ametoka kijijini na amekuwa mtoto wa mkulima sasa adha zile alizozipata na aka-*fluke* kwa kubahatisha mpaka kufikia hapo alipo leo, ndiyo zimewabana Watanzania wengi. Akikaa vizuri kushughulikia kilimo, anaweza akawatoa watu wa aina yake wengi ambao wamekosa fursa kwa sababu kilimo hakishughulikiwi na watu wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie sekta hii, wakulima, wafugaji na wavuvi, hawapati *incentive* zinazotakiwa kutoka Serikalini. Ruzuku inayotengwa kwa wakulima haziwafikii wakulima, kuna watu wako katikati hapa wanachakachua na inaonekana ni kama tunawashindwa. Nawashangaa Wizara hii ambayo imesheheni wasomi mnashindwaje kutatua changamoto hizi ambazo zinatusumbua kila mwaka? Katika miaka kadhaa tunahangaika jinsi gani ruzuku itawafikia wakulima, mbolea zinachakachuliwa, fedha zinatengwa na tumeona takwimu hapa lakini hatuoni tija, ni jambo la kushangaa. Naomba tuielekeze Serikali yetu ihakikishe wakulima wanatazamwa kwa macho mawili na changamoto zinazowahusu zishughulikiwe vizuri kwa sababu zinabeba Watanzania wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima wamegawanyika, tunaposema wakulima wako wavuvi pia. Katika Jimbo langu vijiji zaidi ya 30 viko mwambao wa Ziwa Tanganyika. Hawa ndiyo wamesahaulika kabisa, hawajasaidiwa chochote, Serikali haijaonyesha juhudi kuwasaidia wavuvi. Wavuvi wanaishi tofauti na mazingira yao, mazingira yanaonyesha kuna utajiri mkubwa lakini maisha yao bado ni hafifu sana. Maeneo mengi ya wavuvi utakuta ni watu ambao wanatumikia watu wengine licha ya kwamba rasilimali zinazowazunguka zinaonyesha utajiri mkubwa lakini wameshindwa kwa sababu hawajasaidiwa inavyotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu isaidie kwa kuwapa vifaa vya kisasa vya uvuvi na ikiwezekana kuwapelekea vitu ambavyo vinaweza kuwa vichocheo vya uwekezaji na kichocheo kimojawapo ni umeme. Suala la umeme lingefanyiwa utaratibu tukapata umeme wa kutosheleza katika maeneo ya Ziwa Tanganyika maana yake tungeweza kuwavutia wawekezaji katika sekta hii. Ule ukibarua wanaofanya sasa hivi wa kupeleka samaki na dagaa nje ya nchi kwenda kuuza wangeweza kuwekeza hapahapa na tungeweza kuwa tumewasaidia vizuri kuliko ilivyo sasa. Naomba suala hilo liangaliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ambayo napenda kuchangia ni suala hili hili la umeme lakini nazungumzia kupatiwa umeme mkubwa zaidi kuliko uliopo sasa. Katika bajeti ya mwaka jana kulikuwa na utaratibu wa kusafirisha umeme kwenye Gridi ya Taifa kutoka Nyakanazi kuleta Kigoma, Mpanda na

Sumbawanga. Lengo kubwa lilikuwa ni kuunganisha Mikoa hii na umeme mkubwa zaidi kwa kujua kwamba ni mikoa ambayo kwa kweli ni tajiri na ina bahati nzuri ya kilimo na ingeweza kusaidia pia ku-attract wawekezaji ambao wangeweza kutusaidia.

Kwa hiyo, nia hii naomba iendelee, tusiachie maana katika mipango hii iliyowekwa sasa hivi sijaona kama kuna mwendelezo huu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione wazo hili linapewa kipaumbele na tunaenda nalo ili kuwasaidia wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la msingi na la mwisho ni barabara. Katika kuunganisha mikoa yetu, ipo miradi ya barabara inayosuasua. Barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda ni barabara ya muda mrefu na hatuwezi kuzungumzia masuala ya uchumi kuwasaidia wananchi kama hatuwezi kuboresha miundombinu hii kwa kasi inayotakiwa, sasa hivi ujenzi wake unasuasua sana. Nashauri Serikali kuongeza kasi katika ujenzi wa barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali isisahau barabara zinazoenda kwa wakulima. Katika Jimbo langu kuna barabara ambazo zinaelekea kwenye vijiji vya Katani na Myiula. Vijiji hivi vinazalisha kwa wingi lakini inafika wakati barabara zinajifunga. Kwa hiyo, juhudi ambayo wananchi walikuwa wamewekeza kwenye kilimo inakosa faida kwa sababu hawafikiwi na masoko na wala huduma muhimu kama za pembejeo kwa sababu barabara zimefunga. Kwa hiyo, muone uwezekano wa kuongeza fedha ili kushughulikia barabara zinazoenda kwenye maeneo ya uzalishaji kama maeneo ya Myiula, Chonga, Charatila ambayo katika Jimbo langu ni muhimu sana kwa uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu kulizungumzia ni suala la maji. Maji katika maeneo yetu yamekuwa ni tatizo na hapa tumekuwa tukizungumza juu ya miradi mbalimbali ya maji ikiwepo mradi wa King'ombe. Mradi wa King'ombe ulitengewa zaidi ya shilingi 500,000,000 kwa kijiji kimoja lakini mpaka fedha hizo zimekwisha kijiji hicho hakijapata maji. Jambo hili tumelizungumza kwenye Bunge lililopita, Mheshimiwa Keissy amezungumza sana hapa, hakuna anayesikia suala hili. Mpaka mwisho tunakuwa na wasiwasi pengine hawa watu tunaowaambia ni sehemu ya tatizo.

Naomba mliangalie suala hili. Ukienda King'ombe kama kiongozi na mdau wa kisiasa watakufukuza, hata wakati mwingine wanawafukuza watalaam kwa sababu wanaona fedha nyingi zimeingia lakini hazina tija, hawapati maji jambo ambalo ni hatari sana. Kuna wizi mkubwa umefanyika lakini hakuna mtu anayefuatilia jambo hili. Naiomba Serikali ijaribu kufuatilia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyerwa ambao wamenichagua kuwa Mbunge wao. Nachowaahidi wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa sitawaangusha. Nimejipanga vizuri na najua yanayoendelea kule Jimboni lakini mimi ndiye Mbunge wa Jimbo la Kyerwa hakuna mwingine. Hao wanaojipanga wanasema wanasubiri siku mbili, sijui miezi miwili hakuna lolote mimi ndiye Mbunge wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kupongeza hotuba ya Waziri na niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Rais ambapo aligusia maeneo mengi mazuri yanayomlenga Mtanzania halisi. Kwa kweli mimi nasema Mpango huu ni mzuri na nauunga mkono lakini kuna maeneo ambayo nataka nijikite. Maeneo ambayo nataka kujikita, niombe Serikali, Mpango huu umlenge mwananchi wa kawaida, twende kule chini. Tunaongelea kujenga viwanda lakini tunapoelekea kwenye kujenga viwanda vikubwa tusipoangalia huyu mwananchi wa chini ambaye hali yake ni mbaya hatutaweza kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunaenda kwenye uchumi wa kati lazima tuende huku chini, huyu mwananchi ambaye hali yake ni mbaya tunamuinuaje kwanza. Tuna vitu ambavyo lazima tviangalie, kwa mfano, mimi natoka maeneo ya wakulima. Kule kwetu Mkoa wa Kagera na Jimbo langu la Kyerwa tuna uwezo wa kulima kwa mwaka mpaka mara tatu lakini hawa watu wanapolima hawana pa kuuza mazao, hawana soko la uhakika. Lazima tuwawekee mazingira rafiki wanapolima wapate mahali pa kuuza mazao yao, ndipo tutaweza kumuinua mwananchi na ndipo tutaweza kusema tunaingia kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali na Wizara ya Kilimo, kwa mfano kule Kyerwa kuna masoko ya kimataifa yanajengwa pale Mkwenda na Mrongo mpakani na Uganda lakini masoko haya hayaendelei. Tulitegemea masoko haya yangekamilika mwananchi wa hali ya chini angeweza kuuza mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu miundombinu. Kwa kweli naomba niambie Serikali ni kama kuna maeneo ya Watanzania na mengine labda siyo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kule kwetu Kyerwa hakuna hata kilomita moja ya barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami, hali ni mbaya. Barabara inayotoka Murshaka - Nkwenda - Isingilo - Murongo ni mbaya sana haipitiki. Tulipotoka kwenye uchaguzi, nimefanya utafiti magari yote yanayopita kwenye barabara hii yote yamepasuka voo kila baada ya wiki moja ni kwenda kufanya service, hali ni mbaya.

Naiomba sana Serikali kama wanaweza kutusaidia watusaidie barabara hii inayotoka Murshaka mpaka mpakani na Uganda. Hii ndiyo barabara muhimu na tunayoitegemea. Watu wanaotoka Uganda - Murshaka - Kayanga - Bukoba hii ndiyo barabara tunayotumia. Niombe sana Serikali na niwaombe hao wataalam mnaowatumia, kuna barabara inayotoka Mgakolongo - Kigalama - Bugomola - Uganda, mmesema itajengwa kwa kiwango cha lami, niulize Serikali ni lini barabara hii itaanza kujengwa? Vilevile barabara hii ya Murshaka - Mulongo itaanza kujengwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati lazima tuangalie, wananchi wa Jimbo langu la Kyerwa hawana maji safi na salama, hatufiki hata asilimia 10. Nimuombe Waziri wa Maji na Serikali yangu, najua hii ni Serikali sikivu, wananchi wa Kyerwa tuangaliwe na sisi ni sehemu ya Watanzania, kile kidogo tunachokipata wote tufaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna suala la afya, Wilaya yangu ya Kyerwa ni mpya hatuna Hospitali ya Wilaya. Wilaya hii tuna vituo vya afya vinne tu ambavyo havina dawa na hata kwenye zahanati hakuna dawa. Haya mambo ameyazungumzia sana Mheshimiwa Rais, niombe sana Serikali tunapopeleka dawa ziwafikie wananchi. Naiomba sana Serikali katika hilo itufikirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niliongelee ni kuhusu hawa vijana wetu wa bodaboda. Serikali iliweka utaratibu wa kusajili pikipiki baadaye wamesema pikipiki hizi zitabadilishwa namba. Ninyi mwanzoni mmesema mmesajili kwa kutumia namba 'T' leo mnasema mnataka kutumia namba nyingine, gharama hizi zinabebwa na nani? Leo wananchi wanapigwa, wananyanyaswa wakasajili pikipiki upya lakini makosa haya yalifanywa na nani? Niombe sana Serikali tunapofanya makosa sisi kama gharama za kusajili pikipiki tukasajili sisi bila kuwabebesha mzigo hawa vijana wa bodaboda, hili siyo sawa. Lazima tuangalie hawa vijana wamejiajiri leo wako mitaani

wananyanyaswa, wanapigwa, wanaambiwa sajili mara ya pili hili siyo sawa. Niiombe Serikali ilianganalie suala hili na ilitolee ufafanuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ndugu zangu nataka kusema tumemaliza uchaguzi, kila chama kilipeleka Ilani kwa wananchi na chama walichoona ni bora ni Chama cha Mapinduzi. Hakuna chama kingine ambacho kimepewa kuongoza Tanzania ni Chama cha Mapinduzi. Sasa tusije hapa tukaleta mbwembwe, tukaanza kuitukana Serikali sisi ndiyo tunaotawala lazima muwe wapole. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ndugu zangu hapa kuna maagizo, tunataka tuonekane mbele ya Watanzania kuwa sisi tunajua kupanga, tunajua kuongea lakini Watanzania wana akili. Tumekuwa tukisikiliza hapa Bungeni mkisema vitu mbalimbali, uovu ulio ndani ya Chama cha Mapinduzi ni kweli ulikuwepo lakini Chama cha Mapinduzi kimeamua kufanya mageuzi. Hao mliokuwa mnawataja leo wako kwenu. Sasa hivi ninyi mna ujasiri wa kusimama mbele ya Watanzania kusema mafisadi?

**MBUNGE FULANI:** Hawana.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Huo ujasiri mmeutoa wapi maana mmewabeba ninyi, mliwasema wako kwetu leo wako kwenu. Kwa hiyo, msije hapa kwa mbwembwe Watanzania wana akili, wanajua kinachofanyika na wamepima wameona hamfai.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Habari ndiyo hiyo. (Kicheko/Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaambie, hawa Watanzania wana macho wanaona, wana masikio wanasikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha usiendeleo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana, hoja iliyo mbele yetu ni Mapendekezo ya Mpango unaokusudiwa kuletwa na Serikali. Naelewa fika mnapenda kujibishana hoja za kisisasa, ndiyo, lakini tusivuke mpaka. Mimi

napenda tuisaidie Serikali na nchi yetu katika kuboresha mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali ili tuweze kujenga misingi mizuri, ahsanteni. (Makofi)

Tunaendelea na Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa na kwa sababu umempa *alert*, ngoja tu tumwache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu mpaka tulipofikia leo ni mwaka wa 55 tangu tumepata Uhuru. Wakati tunapata Uhuru na mpaka Baba wa Taifa anatoka madarakani, nchi yetu ilikuwa na viwanda karibu 366 ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilivibinafsisha, ikaviua kabisa na tuna mifano thabiti. Kwa mfano, mpaka 1984 viwanda vya nguo vilikuwa 12 leo hakuna kiwanda cha nguo hata kimoja kinachozalisha. Tulikuwa na viwanda vya kubangua korosho 12 leo hakuna kiwanda hata kimoja kinachosimamiwa na Serikali kwenye kubangua korosho. Tulikuwa na viwanda vya sukari, mkonge, viwanda mbalimbali vilikuwa 366. Tulikuwa na Shirika la Ndege mwaka 1984 tulikuwa na ndege 12 au 11 leo Shirika letu la ATC halina ndege hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasema tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda ni wazo jema, lakini Mpango wa miaka mitano uliopita ndiyo ulitakiwa uondoe vikwazo vya kuelekea kwenye uchumi wa kati wa viwanda. Ukipitia kwenye Mpango wa miaka mitano uliopita, viwanda vinahitaji umeme, tuliwaambia na tulilieleza Taifa kwamba ndani ya kipindi cha miaka mitano lazima tuzalisha *megawatts* 2,780. Leo tuna *megawatts* 1,247 ambazo zimetoka mwaka 2010 - 2015 yaani tumepata ongezeko la *megawatts* 347 kwa miaka mitano. Bado hatujafikia lengo la miaka mitano hapo tunakwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda ambao upo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, unaona kabisa kwamba kikwazo hiki bado hatujaondokana nacho. Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka lengo la barabara zaidi ya kilomita 5,000 lakini mpaka sasa ni kilomita 2,773 sawa na asilimia 53 ndizo ambazo zimejengwa. Sasa unajjuliza kwamba huu uchumi wa viwanda ambao vikwazo vyake tulipaswa kuvitatua katika Mpango wa awali wa Miaka Mitano haujakamilika, je, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda wa namna gani? Hayo ndiyo maswali ambayo Serikali inapaswa kutujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaangalia tu *focus* ambayo Wizara imetuletea, inasema tuna matarajio mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 kuwa na bajeti ya shilingi trilioni 22.9 bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni shilingi trilioni 22.45 yaani tumeongeza shilingi bilioni 450 kutoka katika bajeti ya mwaka uliopita. Ukiangalia watu wa Kenya, jana na wenyewe walikuwa wanatoa Mpango wao wa Taifa, bajeti yao ni *Kenyan money trillion* 2.19 ambazo ni sawasawa na trilioni

44.5 za Kitanzania. Kenya wana bajeti ya trilioni 44.5 sisi Tanzania tuna bajeti ya trilioni 22 halafu unasema tunakwenda kwenye uchumi wa kati? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tukisema ni maagizo mtatulaumu lakini unaona kabisa haileti sense. Bajeti ya Maendeleo ya Kenya ni nusu, asilimia 47 ya bajeti ya Taifa, trilioni 20.195 ya Kenya ndiyo bajeti ya maendeleo sisi bajeti yetu ya maendeleo haifiki hata trilioni 10. Kila mwaka tukikaa ndani ya Bunge tunaishauri Serikali kwamba angalau bajeti ya maendeleo ifikie asilimia 35 ya bajeti husika ya nchi lakini hicho kiwango hatujawahi kufikia katika historia ya hili Taifa.

Sasa unajiuliza tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda ama tunapiga *propaganda* za kuwaambia Watanzania kwamba matarajio yetu ni haya, maana tumekuwa ni watu wa kubadilisha *slogan* ili kuwateka wananchi katika mambo ambayo tunashindwa kuyafikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa ni watu wa kuwashauri tu, tumekuwa ni watu wa kuwaambia lakini mmeshindwa kuyatekeleza haya. Sasa leo tunawauliza kwenye hizo trilioni 22 bajeti ya maendeleo ina-*reflect* viwanda? Unakuta hai-*reflect* viwanda ambavyo tunatarajia kuwekeza. Kwa hiyo, mwakani Waziri wa Fedha atakuja na visingizio hivi hivi kwamba bajeti ilikuwa ndogo ndiyo maana tumeshindwa kufikia malengo. Tunahitaji kujenga reli ya kati, tunahitaji kujenga viwanja vya ndege na kununua ndege, nchi yetu haijawahi kuwa katika vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iran juzi wametoka kwenye vikwazo wamekwenda Ufaransa kwenye Shirika la *Airbus* wameagiza *Boeing* 108, hawa watu walikuwa kwenye vikwazo sisi ambao tumekuwa kwenye amani kwa kipindi chote tunazungumza stori za namna ileile. Unajiuliza hivi Watanzania tunayoyasema ndiyo tunayoyatekeleza? Tunaulizana kila siku kwa nini tunashindwa kutekeleza masuala ya msingi ambayo kama Taifa tumekuwa tukiyahitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuzungumze...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Silinde naomba uketi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Haya.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimamia Kanuni ya 68(8) kutoa Taarifa kwa rafiki yangu Kamanda Mheshimiwa Silinde, anachangia vizuri lakini taarifa zake zinapotosha umma mpaka mimi mtu mwenye dhamana ya viwanda nashindwa kukaa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nayotaka kumpa Mheshimiwa Silinde, anatumia takwimu lakini anapotosha. Mheshimiwa Silinde ni mwanakamati mwenzangu wa Kamati ya Nishati, anajua kwamba lengo la *megawatts* 2,700 tulitumia nguvu nyingi kujenga bomba ambalo limepatikana lakini *capacity* ya umeme ya kuzalisha saa hizi ni *megawatts* 980, unataka tuzalishe 2,700 tukaziweke *store*, umeme hauwekwi *store*. (Makofi)

Mheshimiwa Silinde anapotosha kwa mambo anayoyajua, anajua kwamba kuna viwanda vya nguo vinazalisha, anasema hakuna kiwanda kinachozalisha. Mheshimiwa Silinde anajua kwamba tumetoka kwenye sera ya *government* kumiliki tumeiachia sekta binafsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa usichangie.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nayompa, Kamanda asipotoshe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde unaikubali taarifa hii?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is the fact* ipo kwenye taarifa ya Wizara ya Fedha, taarifa yenyewe imesema kwamba mpaka 2010 tumezalisha *megawatts* 900, kutoka 2010 - 2015 tumeongeza *megawatts* 347 tu. Kama Wabunge ndiyo jukumu letu kueleza Serikali. Kwa hiyo, hayo matarajio ambayo tulikuwa tumeyapanga tufikie 2,780 ifikapo 2015 ambayo bado hatujafikia. Kwa hiyo, *that is the fact* Mheshimiwa Waziri. Kwenye upande wa viwanda, *the same applies*, Taifa linaelewa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia, kama Taifa na Bunge nashauri katika bajeti ya mwaka 2016/2017, lazima tutunge sheria kwenye Sheria ya Bajeti tuingize *provision* ya kuhakikisha kwamba Serikali inaweka *at least 40 percent* ya bajeti ya nchi kuwa ya maendeleo, tuiwekee sheria. Hii asilimia 35 ambayo tumekuwa tukiizungumza haina sheria ndiyo maana utekelezaji wake haupatikani. Kwa hiyo, nalishauri Bunge na hata Wizara mnapotengeneza ile *Finance Bill*, moja ya *provision* ni kuhakikisha kwamba asilimia 40 ya fedha inayotokana na bajeti nzima inakwenda kwenye maendeleo na tunaitungia sheria ili utekelezaji wake upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine bandari tumeeleza, Bunge hapa lilitunga Sheria ya Mawasiliano (*Telecom Act*) ya 2009 na kuna Sheria ya Madini

ya 2010 ambayo zinaitaka Serikali kuhakikisha Makampuni ya Madini pamoja na Makampuni ya Simu yanajisajili kwenye Soko la Hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia Makampuni ya Simu yana mapato makubwa, angalia mzunguko wa Mpesa, angalia wateja ambao wako kule lakini angalia kodi wanayolipa kwenye Serikali! Makampuni ya Simu tangu 2009 mpaka leo miaka saba yameshindwa kujisajili. Kodi wanayopata Serikali siyo stahili kwa sababu tumewaambia kabisa mkiyasajili tutakuwa tunaona uendeshaji wao lakini Serikali miaka yote haifanyi. Sisi kama Wabunge jukumu letu ni kuwashauri na tumekuwa tukiwashauri lengo letu kuhakikisha Serikali inapata mapato sahihi na mkipata mapato maana yake haya yote tunayoyazungumza hatutayajadili tena kwa maana ya mdomo tutajadili utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokuwa tunawashauri wakati mwingine muwe mnapoekea siyo mnabisha tu. Uwezo wa kujenga hoja tunao na uwezo wa kusema Tanzania ni mkubwa kweli kweli, tatizo la Tanzania ni utekelezaji wa yale ambayo tumekubaliana ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri mnapokuja Mpango na mnajua kabisa haya mapendekezo ama mwongozo wa Mpango tunaoujadili leo ilitakiwa iwe ni *extract* kutoka kwenye Mpango wa Miaka Mitano kwa sababu hatuna ule Mpango wa jumla wa Miaka Kumi na Tano. Tunasema tuna *Strategic Plan* ya miaka kumi na tano lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache juu ya Mpango huu wa Serikali ambao umeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Silinde kusema kwamba tunayo maneno mengi na mipango mingi lakini utekelezaji ndio umekuwa tatizo kubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye gharama za uendeshaji wa miradi katika nchi yetu. Kwa muda karibu wa miaka miwili ndani ya Bunge hili tumekuwa tukiishauri Serikali kufanya marekebisho katika Sheria ya Manunuzi. Ukitazama tangu Naibu Waziri wa Fedha alipotusomea hapa mwelekeo lakini

katika vitabu vyote hivi ambavyo vimeletwa na Waziri malalamiko yao na maoni yao yamegusa namna ya kudhibiti manunuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya tatizo kubwa ni Serikali kushindwa kuleta sheria hii ili tuirekebishe. Tumelalamika sana, Wabunge wamepiga kelele kuhusu namna sheria inavyosababisha ukiritimba na kuifanya Serikali miradi yake kuwa ya bei kubwa, miradi mingi inashindwa kukamilika na inayokamilika inakuwa na gharama ambazo zimeifanya Serikali iwe na madeni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize ni lini sasa Serikali italeti marekebisha ya Sheria ya Manunuzi? Wakati mwingine nakuwa na wasiwasi kwamba mnashindwa kuleta sheria hii kwa sababu wako watu ndani ya Serikali ambao wananufaika na matumizi ya sheria hiyo. Mmeongelea suala la kudhibiti mtadhibitije kama sheria bado ni ileile. Kwa sababu sasa imekuwa ni kawaida ya Serikali manunuzi yake hayaendani na soko. Kalamu ambayo inauzwa kwa shilingi 200/= wao watainunua kwa shilingi 1000/=. Mradi wa Serikali ambao ungeweza kutekelezwa kwa shilingi 50,000,000/= unatekelezwa kwa shilingi 100,000,000/=. Naiomba Serikali ibadili sheria hii na ilele haraka sana ili tuweze kuifanyia marekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu elimu. Yako mambo mengi na Waziri wa Elimu ametuambia kwamba atakuja na mipango hasa ya upande wa ukaguzi, lakini mimi naomba niongelee kuhusu mgawanyo sawia wa walimu katika nchi yetu. Unaweza kukuta kuna shule ambazo zina walimu 30 na shule nyingine zina walimu wawili.

Naomba nitolee mfano katika Jimbo la Bukoba Vijijini katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Halmashauri hii katika Mkoa wetu imekuwa ya mwisho kielimu, lakini hata shule ambayo imekuwa ya mwisho kiwilaya na kielimu inatoka katika Halmashauri hii inaitwa Kamkole ipo katika Kata ya Rukoma, ina wanafunzi 215 ina walimu wawili tu. Mwaka jana Halmashauri ya Wilaya iliomba walimu 280, haikupata mwalimu hata mmoja. Mwaka huu tunakwenda kuomba walimu 300, tunaomba Wizara ifikirie namna ya kupeleka walimu katika Halmashauri hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka siku za nyuma yuko Mkuu wa Wilaya ambaye amewahi kupiga baadhi ya walimu viboko 20 lakini tatizo hakuna walimu katika Halmashauri hii, wanapoomba walimu hamuwapi, shule ina walimu wawili au watatu. Kama Waziri wa Afya alivyotuambia kwamba anakwenda kufanya sensa ya kuona kwamba madaktari wanakwenda sawia hata katika mikoa ya pembezoni, tunaomba walimu nao wagawiwe kwa usawa siyo shule moja inakuwa na walimu 300 na hasa shule za mijini. Pamoja na kwamba tunatetea wanawake lakini na wanaume nao wawe wanaomba uhamisho kufuata wake zao ili waende katika shule hizo isiwe kila siku sisi

wanawake ndiyo tunawafuata wanaume ifike mahali na ninyi mtufuate huko tuliko. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni yangu kuhusu hii *retention*. Kamati ya Bajeti imekubaliana na mapendekezo ya Serikali. Inawezekana Serikali ina jambo lililoliona labda kuna matumizi mabaya ya fedha hizo lakini naomba niwakumbushe. Mwaka 1972 wakati Serikali imefuta *Local Government* ikaleta utaratibu wa madaraka mikoani, baada ya miaka kumi Serikali ilishtuka kwamba imeondoa huduma kwa wananchi na ikarudisha *Local Government*. Hata hivyo, baada ya kurudisha *Local Government*, Serikali imekwenda kufuta vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vinasaidia halmashauri hizi kuweza kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita mimi nilikuwa kwenye Kamati ya TAMISEMI, katika kupitisha bajeti, Wakuu wa Mikoa wote wamelia jinsi Serikali inavyoshindwa kurudisha ruzuku ya vyanzo hivi. Ukipitia bajeti ya mwaka jana, karibu mikoa yote Serikali ilishindwa kupeleka fedha mpaka wengine walipata asilimia 28 – 30, hii imesababishwa na Serikali Kuu kubeba pesa zote. Mimi nina wasiwasi na naungana na wale wanaosema Serikali inakwenda kuuwa mashirika haya. Serikali kwanza ituambie imeona mpaka ikaondoa *retention*? Hata ndani ya Halmashauri, kwa mfano, Idara ya Ardhi, vyanzo vyote vya mapato vinakwenda Wizarani lakini Wizara ya Ardhi imeshindwa kurudisha pesa hizo na unakuta halmashauri zinashindwa kupima viwanja kwa sababu hawana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *retention* ina maana gani? Ina maana kwamba pesa yote itakusanywa Hazina na tujue hii Serikali ina wakora, kuna watu wengine ni wakora huko, wanaweza kutumia mwanya huu kuhakikisha kwamba hizi fedha hazirudishwi inavyotakiwa. Serikali itueleze, ina mpango upi sasa ambao utawezesha fedha hizi kutoka Makao Makuu Hazina kuzirudisha katika wilaya ikiwa ni pamoja na Halmashauri. Halmashauri zinalia na mmekwenda kuziua na zinakwenda kufa. Serikali ifikirie namna ya kurudisha baadhi ya vyanzo. Kama inashindwa kupeleka fedha za bajeti irudishe vyanzo vile ambavyo vilikuwa vinawezesha Halmashauri kuweza kupata mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya chama chetu cha CHADEMA ya 2010 tulikuwa tumepanga kurudisha Serikali za Majimbo, CCM ikapiga kelele na kusema ni ukabila siyo ukabila, hii nchi ni kubwa. Ndiyo maana watu wanaiba mpaka CAG atambue wizi umetokea mahali fulani inakuwa imepita miaka mitano. Nchi hii ni kubwa, inahitaji chombo kingine hapa katikati ambacho kitahakikisha wananchi wanapata huduma zao na kudhibiti mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya kwanza imeshalia, naomba niongelee juu ya utawala bora. Nitaongelea Wilaya ya Kyerwa, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum naruhusiwa kuongelea mkoa mzima. Utawala bora ni pamoja

na mambo ambayo mmeona yanafanyika katika uchaguzi. Mtu anashinda kiti chake lakini anatangazwa ambaye hakushinda. Wasimamizi wa Uchaguzi ni Wakurugenzi, Mkurugenzi anatangaza matokeo halafu anapitia dirishani. Tume na ninyi mnafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kuwaambia haya mambo yanaweza kuwa ni kung'ang'ania kupata madaraka sawa lakini mnalea kizazi ambacho hakiwezi kuvumilia mambo haya. Kizazi cha sasa hivi hakina siasa za mwaka 1947, tunao watoto na vijana wapya. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kumbe ni Mbunge wa dirisha.

**MHE. CHONCHESTA L. RWAMLAZA:** Msifikirie kung'ang'ania madaraka ni jambo jema. Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa CHADEMA ilipata Madiwani 13 wakati CCM ilipata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwaheri.

**MHE. CONCHESTA L. LWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbunge wa dirisha huyo. *(Makofi)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuzungumza lolote, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kuwa Mbunge ...

**MWENYEKITI:** Nataka tu Jimbo Mheshimiwa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mtwara Mjini.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa kunibariki kuwa Mbunge wao. Pili, naomba niwashukuru wananchi wangu wa Mtwara Mjini kwa kuniamini na nawaambia waendeleo kuniamini nitawawakilisha vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hoja, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mtwara Mjini kumetokea maafa, mvua imenyeshwa,

kuna mafuriko na jana nilitoa taarifa hii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba Waziri husika ashughulikie suala hili, kuna nyumba zaidi ya 500 zimeharibika. Nachukua fursa hii pia kuwapa pole wananchi wote walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo. Mpango huu umezungumzia suala zima la viwanda na Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hoja alisema kuna utaratibu wa kuhakikisha inatawanya viwanda kila eneo la nchi. Pia alisema kuna maeneo ni *special investment zone* kwa maana kwamba ni ukanda maalumu wa uwekezaji na akataja Mtwara, Bagamoyo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mtwara Mjini kuna Kiwanda cha Dangote. Kiwanda hiki kina wafanyakazi wengi lakini kwa masikitiko makubwa kabisa mle ndani kuna kampuni tatu za Wahindi na Wachina, kuna AYOK, UCC na CYNOMA. Naomba nimpe taarifa Waziri husika kwamba kampuni hizi zilizopo mle ndani zinanyanyasa wafanyakazi. Sijui ni utaratibu gani huu wa kwamba tunajenga viwanda badala ya kuwanufaisha Watanzania vinawanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine katika Kiwanda hiki cha Dangote, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inaondoa umaskini kwa wananchi wa maeneo husika. Kwa kiasi kikubwa kiwanda hiki kinaajiri watu lakini wenyeji wa Mtwara wengi hawapati nafasi. Mimi kama Mbunge nimejaribu kutembelea kiwanda hiki zaidi ya mara mbili kwenda kuzungumza na Maafisa Masuuli lakini kuna manyanyaso makubwa ya wafanyakazi mle ndani. Mishahara inatoka kiasi kikubwa lakini wale vibarua na wafanyakazi wanapewa pesa ndogo sana. Nimuombe Waziri husika atembelee Kiwanda cha Dangote - Mtwara kuona manyanyaso yanayofanywa na Wahindi pamoja na Wachina lakini manyanyaso yanayofanywa kwa wananchi wa Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini na maeneo ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala zima la bandari. Katika hoja hii limeelezwa suala zima la kuboresha bandari, lakini Bandari ya Mtwara imetajwa tu kwamba kuna mpango na mkakati wa kujenga magati. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini nimetembelea Bandari ile ya Mtwara. Pale kuna gati moja limechukuliwa na watu wa gesi wanaitwa BG, lakini ile gati kwa muda mrefu zile meli za BG hazipo. Sasa hivi tumebakiwa na gati mbili tu ambapo tunataka tusafirishe korosho lakini ile gati iko *empty* na wanasema kwamba pale meli nyingine yoyote hairuhusiwi kutia nanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika mpango huu wa kuendeleza bandari wahakikishe Bandari ya Mtwara ambayo ina kina kirefu Afrika Mashariki na Kati, wala haihitaji kutumia gharama kubwa kama ilivyo ujenzi wa Bandari mpya ya Bagamoyo, Wizara husika irekebishe Bandari ya Mtwara na ijenge yale magati manne. Sambamba na hilo ihakikishe inamwezesha yule mwekezaji

ambaye ameomba eneo, Mheshimiwa Aliko Dangote kuweza kumaliza mchakato wake ili tuweze kuongeza magati kwa ajili ya Bandari ile ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nazungumzie suala zima la miundombinu. Kule Mtwara tuna barabara inaitwa barabara ya Ulinzi, ni miaka mingi barabara hii haizungumziwi kabisa. Naomba Wizara husika ihakishe inashughulikia barabara ya kutoka Mtwara Mjini – Kitaya - Newala na maeneo mengine kwani ni barabara ya Ulinzi ambapo mwaka 1972, mashujaa wetu au wanajeshi wetu walikuwa wanaitumia barabara ile kulinda mipaka ya Tanzania Ukanda huu wa Kusini lakini imesahaulika kabisa. Kwa hiyo, naomba Mpango huu uhakikishe barabara hii ya Ulinzi inajengwa kwa kiwango cha lami, inapita Kitaya - Mahulunga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba barabara hii ambayo ni kitovu kikubwa cha uchumi wa korosho inayoanzia Mtwara Mjini kuelekea Majimbo yote ya Mkoa wa Mtwara kwa maana ya Mtwara Vijijini, Nanyamba, Newala, Tandahimba hadi Masasi iwekwe kwenye Mpango ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Mimi kabla sijazaliwa naisikia barabara hii inazungumziwa kila siku. Mheshimiwa Nandonde alishawahi kuzungumza kwa miaka mingi sana katika Bunge hili lakini mpaka leo bado barabara hii inasahaulika, kwa hiyo, tunaomba iwekwe kwenye Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la utalii. Pale Mtwara Mikindani kuna magofu ya kihistoria lakini Serikali imeyaacha na haina mkakati wowote wa kuhakikisha kwamba tunatangaza vivutio vile ili viweze kutoa ajira na kuingiza kipato kwa Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo yale ya Mikindani kuna vivutio kuliko hata maeneo mengine ya Tanzania, naomba Serikali ianze kuyatangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema mambo machache. Ilizungumzwa hapa kwamba amani na utulivu ndiyo chachu ya maendeleo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo chachu itakayowavutia wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania. Kila mmoja ni shahidi, hata Waheshimiwa wazee wetu wa Chama cha Mapinduzi wanafahamu kabisa tarehe 25 Oktoba, 2015 kule Zanzibar chama kilichoshinda ni Chama cha Wananchi - CUF lakini Tume ya Uchaguzi na yule aliyeshindwa hawakutaka kumtangaza aliyeshinda. Kwa hiyo, niombe tu mshindi wa Zanzibar atangazwe ili nchi yetu iendelee kuwa na amani na utulivu na ili wawekezaji waweze kuja kuwekeza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba usafirishaji wa reli ni muhimu sana. Kama ilivyokuwa kwenye reli ya kati na kule Kusini pia kuna reli,

lakini kwenye Mpango huu sijaona sehemu yoyote iliyoandikwa kwamba reli hii ya kutoka Mtwara – Liganga - Mchuchuma itajengwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafiri wa ndege, niungane na wenzangu kusema kwamba ATC ina ndege moja tu tena ni ya kukodi, tuna ubia na wale watu wa South Africa. Naomba ndege ziongezwe kwa sababu ni za Serikali lakini pili gharama yake ni nafuu sana. Nilienda kuulizia tiketi ya ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. (Makofi)

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mtemi wa Kabila la Wasukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu ya kushauri. Pengine nianze na hili la *retention* ambalo limezungumzwa na Mbunge aliyepita Mheshimiwa Rwamlaza. *Retention* kwa mapendekezo ya Serikali ni jambo zuri kwa sababu uzoefu unaonesha sisi ambao tumekuwa tukishughulika na mahesabu ya Serikali, ziko taasisi ambazo wanatumia fedha hizi vibaya. Kwa hiyo, Mpango huu wa Serikali ni mzuri, waendeleo nao, isipokuwa Halmashauri zote nchini pamoja na Mifuko ya Hifadhi za Jamii, hao wasiwekwe kwenye kundi la kupeleka fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, waendeleo kubaki na makusanyo. Bahati nzuri Mheshimiwa Rwamlaza tuko Kamati moja nadhani kule tutaendelea kushauriana vizuri ili Halmashauri zetu zisije zika-*suffocate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la kilimo. Iko mikoa ambayo kila mwaka inakumbwa na njaa na haipungui mikoa 12 lakini kwenye Mipango yetu hapa sijaona mipango mahsusini na ya makusudi ya kuhakikisha kwamba mikoa hii wanaiwekea miundombinu ya umwagiliaji. Mikoa mingi upande wa Kanda ya Ziwa tuna maji ya uhakika, tunahitaji miundombinu ya umwagiliaji, tumechoka kuletewa chakula kila mwaka. Labda tuambizane hapa kwamba mikoa ile ambayo inakuwa na njaa kila mwaka tumeitelekeza na kwamba tutaendelea na Kamati za Maafa ili tuwe tunaendelea kuwapeleka tani za chakula ilhali wao ndiyo wamebahatika kuwa na maji ya uhakika, wanaweza wakamwagilia na tukapata chakula tukajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pale Bunda tayari eneo la EPZ limetengwa zaidi ya hekari 1,350. Naishauri Serikali kwenye Mpango huu, hebu

sasa mikoa ile ya Kanda ya Ziwa kwa kuanza na maeneo hayo ya EPZ watuwekee miundombinu ya umwagiliaji ili tusiendeele kuombaomba chakula. Kila mmoja hapa anajua madhara ya njaa, watu wenye njaa hawatawaliki, watu wenye njaa hawatulii na watu wenye njaa hawawezi wakashiriki kwenye maendeleo ya huu Mpango tunaouweka hapa. Utashirikije kwenye maendeleo wakati una njaa? Wakati mwingine hatutulii humu ndani, hakuna amani na utulivu kwa sababu watu wana njaa za aina mbalimbali humu. Wengine wana njaa ya pesa, wengine wana njaa ya kushika madaraka, huwezi kutulia humu ndani, ni mifano ya njaa ukiwa na njaa huwezi kutulia. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la reli. Kwenye Mpango huu nishauri jambo moja na hii itakuwa ni hatari kwa Serikali. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 12 ameelekeza kujenga reli ya kutoka Dar es Salaam - Rwanda na kwa kwenye Mpango Serikali inasema itajenga reli ya kati kwa *standard gauge*. Sasa kitendo cha kunyamaza au cha kuwa na kigugumizi sijui kimetoka wapi cha kutotaja reli yetu ya kati ya kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na michepuko yake ya kwenda Kalema kwenda Msongati, michepuko ya kwenda Mwanza na baadaye twende Dutwa kule kwa ajili ya *nickel*. Serikali inaweza kutumia uchochoro huo na kwa sababu wanamshauri vibaya Mheshimiwa Rais, kama wameweza kutaja michepuko ya kutoka Mtwara kwenda Liganga na Mchuchuma, michepuko ya reli kutoka Tanga kwenda Arusha na Musoma na michepuko ya Minjingu na Engaruka kuna kigugumizi gani cha kutotaja reli ya kati kwamba ndiyo inayoenda kujengwa kwa *standard gauge*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango huu kuna eneo la kukarabati reli ya kati. Kwa hiyo, tunaweza kukuta ule mtandao wetu wa reli ya kati ukaishiwa kukarabatiwa halafu tusiwe na *standard gauge* matokeo yake wanampelekea Rais Kagame. Nani asiyejua Kagame anatamani Bandari ya Dar es Salaam? Nani asiyejua Kagame aliwahi kusema akipewa mwezi mmoja atakusanya fedha za Bandari ya Dar es Salaam kuendesha Rwanda kwa mwaka mzima? Nani asiyejua Kagame alianzisha UKAWA ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wakamtenga Rais wetu ili waweze kujenga reli ya Mombasa mpaka Rwanda na sasa wanavuka Naivasha. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye utalii. Tunahitaji kuinua pato la Taifa na ili tuliinue ni lazima tushughulike na ujangili ambao unatishia wanyamapori na ujangili unaotishia watalii kuja Tanzania.

Naomba Mheshimiwa Maghembe haya mambo ya kuandika humu kwamba tunataka kuboresha miundombinu, kununua zana za kupambana na majangili, mpaka sasa zana za kupambana na majangili unazo, tulikuwa na helkopta juzi majangili wameitungua, hizo ndizo zana za kupambana na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama majangili wameanza kutungua ndege ambazo ndizo zana za kupambana na majangili maana yake tukiendelea kukupa hizi zana za kupambana na majangili wataendelea kuzitungua. Idara yako ya Wanyamapori na Hifadhi yako ya Ngorongoro ndiko kwenye wafanyakazi wasiowaaminifu kwenye Idara ya Intelejensia ambao wanaazimisha silaha za kivita, wanawapa majangili halafu wanatungua ndege. Waheshimiwa Wabunge, hizi ndege zinaendelea kuanguka kwenye hifadhi hata ile ya Marehemu Filikunjombe ilianguka kwenye Hifadhi ya Selous. Kwa nini nisiamini kwamba inawezekana kwa sababu walikuwa kwenye Hifadhi ya Selous ambako ujangili wa tembo ni mkubwa, ni majangili hawa hawa walianguka ndege ya Mheshimiwa Filikunjombe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje ninyi katika kuajiri askari wa wanyamapori na kwenye Kikosi cha Intelejensia hamuwa-*vet*? Watu wengine wamefukuzwa polisi ndiyo hao mnawachukua, mnawachukua kwa sababu ya ubinamu, ujomba na mwingine ameshiriki kuanguka ndege ya Rubani Gower, maskini Mungu aiweke roho yake mahali pema. Mtu huyu ameajiriwa wakati alifukuzwa ni mhalifu, ni jambazi matokeo yake ameshiriki kwenye tukio hili. Mheshimiwa Maghembe unafanya kazi gani na yule Mhifadhi pale ambaye ndiye anashughulika na ajira za watu wa namna hii? Tutaendelea kuwa na majangili hata ukileta zana za kupambana nao kama wafanyakazi wa Idara yako hautawa-*vet* na kuwasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja. Mpango huu ni mzuri sana na katika uzuri wake ndiyo maana tunaomba kuendelea na mapendekezo haya ili Serikali ije na rasimu ikiwa inaonesha sasa Mpango huu unatekelezeka. Nakuhakikishia Mpango huu ukirudi jinsi ulivyo mkadharau mapendekezo ya Wabunge hautatekelezeka, zitabaki ni hadithi, zitabaki ni porojo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kutaja maeneo ambayo reli yetu inaenda kujengwa kwa *standard gauge* kwa kisingizio kwamba hamuwezi kutaja kila kitu, kama hamuwezi kutaja kila kitu mbona maeneo mengine mmetaja? Kama mtakuja hapa bila mwelekeo wa reli ya kati, nitakuwa mtu wa kwanza kusema kwamba rasimu hii hatuikubali, nitakuwa mtu wa kwanza kutokubaliana na bajeti ya kupitisha mpango ambao hauna dhamira nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule pembezoni Kanda ya Ziwa mfuko mmoja wa simenti shilingi 20,000 wakati Dar es Salaam ni shilingi 12,000, Watanzania hawa watajenga lini nyumba? Misumari, nondo, gharama za usafirishaji zinakuwa kubwa lakini tunaendelea kupiga chenga zaidi ya miaka 15. Hayo makelele yenu mliyonayo huko kwenye mambo ya *tender*, sisi hatutaki vurugu zenu huko, endeleeni kukaa vizuri, tunachotaka ni kujenga reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taarifa, reli hii Waheshimiwa Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Ahsante sana Mtemi wa Wasukuma. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nianze kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kunipa kura nyingi ili niwe mwakilishi wao. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitafanya kila linalowezekana niwawakilishe vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sikupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais basi na mimi nichukue nafasi kumpongeza sana, hotuba yake ilikuwa nzuri na kweli imetoa mwongozo na mwanga jinsi nchi yetu inavyoweza kwenda.

Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Mawaziri, niwaombe wawe na amani, wafanye kazi kwa bidii wawatumikie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijikita sasa kwenye Mpango, niseme mpango ni mzuri lakini nina mambo machache ya kusema. Watu wa Kanda ya Kati wanasema reli ya *standard gauge* lakini sisi wa Mkoa wa Njombe na Mbeya tuna reli tayari pale ya *standard gauge* ya TAZARA lakini malori bado yapo barabarani. Tukiacha hilo, kwenye Mpango tunasema kuna upembuzi yakunifu wa kujenga reli kutoka Mtwara - Mbamba Bay zaidi ya kilomita 800, sikatai, ni vizuri kwa maana ya kwamba ni kufungua mikoa iliyopo pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutoka Makambako - Liganga ni kilomita 200, hivi shida iko wapi? Hivi kipi ni rahisi, k ujenga reli kutoka Makambako - Liganga ambako chuma ndiko kipo au kuanza kufanya upembuzi wa kilomita 800 za reli mpya ya Mtwara – Mabamba Bay? Nashauri tufanye kile cha rahisi na pafupi chuma kitoke Liganga ili tufanye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe ndiyo unategemewa kuwa Mji Mkuu wa machimbo haya ya Kusini mwa Mkoa wa Njombe. Ndiyo mji utakaopokea wageni wengi, ndiyo mji ambao utatoa huduma lakini mji huu hauna maji. Kinachosikitisha zaidi katika Mji wa Njombe, mito miwili mikubwa imekatiza katikati ya mji. Niombe Serikali na nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Lwenge, ameshaniahidi tutaenda Njombe tukaone ni namna gani sasa Mji wa Njombe utapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote vya Jimbo la Njombe Kusini au Mjini havina maji. Wananchi walichanga fedha wakiahidiwa kwamba kutakuwa na mradi wa Benki ya Dunia kusaidia ujenzi wa mradi wa maji. Fedha zao zimekaa huko Serikalini lakini maji hakuna. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshaniahidi basi niamini hilo litaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la afya, tunakwenda kujenga uchumi wananchi hawana afya itasaidia nini? Pale Njombe sisi tuna hospitali ambayo mara inageuzwa Hospitali ya Mkoa, mara Hospitali ya Rufaa ya Mkoa lakini ukifika huwezi kujua kama umefika hospitali kwa jinsi ilivyochakaa. Utajiuliza hivi hapa ilitokea vita au kulitokea nini, lakini ukiingia ndani utaona watu wamelala, ni wodi. Hali ya hospitali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali ione nini tufanye katika hospitali ile. Hospitali ile imerithiwa kutoka kwenye Kampuni ya TANWAT ikakabidhiwa Serikali kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri zimekuwa zikiongezeka mpaka sasa ziko tano bado zinatumiya hospitali ile ile na sasa inakuwa Hospitali ya Mkoa bado ni ile ile, eneo lenyewe la hospitali halizidi heka mbili.

Kwa kuwa mkoa umeshapewa eneo katika kijiji cha Mkodechi kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Mkoa ambapo wameshafanya uthamini, wameshalipa fidia na wameshaweka mipaka, niombe Serikali itafute fedha tujenge hospitali hii. Tukijenga Hospitali ya Mkoa wa Njombe maana yake itasaidia sasa wananchi wa Njombe kwa maana ya mkoa pamoja na hao wawekezaji wanaokuja kwenye migodi hii kupata huduma ya afya na kuendelea na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Niipongeze sana Serikali kwa hatua iliyochukua, changamoto zipo sikatai. Ni muhimu unapoanza jambo upambane na changamoto ili kusudi ujipange vizuri zaidi. Naomba sana Serikali ijitahidi changamoto hizi iziangalie kwa haraka. Wengi wamesema hapa lipo tatizo la walimu, maslahi yao yaangaliwe vizuri, wana madai, wamekwenda likizo hawalipwi, wanapandishwa vyeo nyongeza zao hawapewi, niombe sana suala hili lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo kwangu naliona ni kubwa, tatizo la elimu kwa watoto wa kike. Tatizo hili ni la kitaalam kidogo na ni tatizo linalotokana na makuzi ya mtoto wa kike. Mtoto wa kike katika makuzi yake anafika mahali haudhurii shule kwa sababu ya kukosa zana za kujisitiri. *(Makofi)* Mheshimiwa Mwenyekiti, tena tuna bahati sana Waziri wa Elimu ni mama, Naibu Waziri wa Elimu ni mama, Makamu wa Rais ni mama na Waziri wa Afya ni mama, naomba tulione hili. Watoto hawa wa kike hawahitaji hata zaidi ya

shilingi 10,000 kwa mwaka ili wajisitiri. Hawawezi kuhudhuria shule kwa sababu hali zao siyo nzuri. Haudhuri shule kwa zaidi ya siku 30 ata-*perform* vipi vizuri, mbona haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona taasisi nyingi za kina mama hazizungumzii habari ya watoto wa kike tuwasitiri namna gani ili wahudhurie shule. Taasisi zote zinazunguka zunguka tu pembeni zinafanya vitu vingine visivyo vya msingi. Naomba sana suala hili liangaliwe, Serikali ione namna gani itafanya kusaidia watoto wa kike wahudhurie shule siku zote za masomo ili kusudi waweze kupata elimu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Nashukuru sana Profesa Muhongo amefika Jimboni kwangu na tumejaribu kuona vyanzo vya umeme na ameniahidi kwamba Jimbo langu litapata umeme. Tatizo ninaloliona kama nchi kwa suala la umeme ni nguzo. Sisi Njombe tunazalisha nguzo nyingi sana, Serikali ifike mahali ifanye maamuzi kwa kuwawezesha wafanyabiashara wa Njombe wawe na mitambo ya kusindika nguzo zile. Kwa sababu nguzo hizi na umeme tunaoenda kusambaza nchi nzima ni mwingi sana, tunahitaji nguzo nyingi sana na Njombe sisi tuna uwezo wa kutoa hizo nguzo zote zikapatikana, lakini nani awezeshe wale wananchi ili waweze kuwa na mitambo ya kusindika zile nguzo?

Kwa hiyo, Wizara ya Nishati na Madini kwa namna itakavyowezekana iwawezeshe wananchi wenye nia ya kufanya shughuli hiyo ya kusindika nguzo ili wazalishe nguzo nyingi zaidi. Tunaagiza nguzo South Africa, Zimbabwe na Kenya, tena ni hadithi ya kusikitisha unaambiwa nguzo zimetoka Njombe zimepelekwa Kenya zimenunuliwa na mkandarasi zinarudishwa Mara na wakati Njombe sisi nguzo pale zimebaki hazina mnunuzi. Kwa hiyo, niombe sana suala hili lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni elimu ya ufundi, hivi tujiulize... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie Mpango uliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sote hapa tumeamka salama na tunaendelea na shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika namna ya kipekee kabisa niwashukuru wapiga kura wa Mafia kwa kuniwezesha kuwa Mbunge kwa kura nyingi sana na leo nimesimama kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu nikichangia Mpango huu. Ninachotaka kuwaambia wananchi wa Mafia, imani huzaaa imani. Wamenipa imani na mimi nitawarejeshea imani. Ahadi yangu kwao, nitawapa utumishi uliotukuka uliopakwa na weledi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wenyewe watakuwa mashahidi, wameshaanza kuona baadhi ya ahadi ambazo niliziweka kwao zimeanza kutekelezeka. Wananchi wa vijiji vya Juwani na Chole wa visiwa vidogo ambavyo hawakuwa na maji kwa muda mrefu, maji yameshaanza kutoka kule. Wananchi wa visiwa vidogo vya Bwejuu na Jibondo maji wataanza kupata baada ya wiki mbili kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali makini na Serikali sikivu ya CCM kwa kuanza na sisi wananchi wa Mafia. Nimeongea na Waziri makini kabisa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi tukiomba watupatie meli ya MV Dar es Salaam ili kuondoa kero ya usafiri baina ya Kilindoni na Nyamisati. Kimsingi Waziri amekubaliana na hilo na naomba niwafahamisha watu wa Mafia kwamba Serikali imekubali kutuletea meli ya MV Dar es Salaam. Hivi sasa mchakato wa masuala ya kitaalam na ya kiutawala unaendelea na meli hiyo itakuwa Mafia ndani ya muda mfupi kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo vilevile kuipongeza Serikali, tuliomba gati na niliongea na Waziri, Mheshimiwa Mbarawa, bahati mbaya hayupo, lakini ndugu yangu Mheshimiwa Ngonyani upo nakuona hapo, tuliomba gati lifanyiwe maboresho kwa kuletewa tishari kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuwafahamisha wananchi wa Mafia na Bunge lako Tukufu kwamba tishari lile limefika Mafia juzi, taratibu za kuli-*position* kwenye gati lile zinaanza na usafiri baina ya Nyamisati na Kilindoni utaboreka zaidi.

Naomba ndugu yangu Mheshimiwa Ngonyani unifikishie salamu kwa Mheshimiwa Waziri, bado tuna matatizo upande wa pili wa Nyamisati, kule maboresho bado hayajafanyika. Tunatambua kwamba Mamlaka ya Bandari ilishatenga bajeti kwa ajili ya kufanya maboresho upande wa Nyamisati. Meli hii itakayokuja kama upande wa Nyamisati hakutafanyiwa maboresho itakuwa haina maana yoyote.

Kwa hiyo, nakuomba kwa namna ya kipekee ndugu yangu Mheshimiwa Ngonyani na nikimaliza kuchangia nitakuja hapo kwako nikuelezee *in details*. Maboresho ya Bandari ya Nyamisati ni muhimu sana katika kuhakikisha meli ile

ya MV Dar es Salaam inafanya kazi zake baina na Kilindoni na Nyamisati bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee pia nikushukuru ndugu yangu, mzee wangu Mheshimiwa Profesa Muhongo. Nilikuletea *concern* yetu watu wa Mafia kuhusiana na kusuasua kwa mradi wa REA. Ukachukua hatua na ninayo furaha kukufahamisha kwamba nimeongea na watu wa TANESCO na tumekubaliana kwamba mradi ule utakabidhiwa baada ya mwezi Machi, hivyo basi nakushukuru sana. Pia tulinong'ona mimi na wewe kuhusu suala la *submarine cable* kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni...

**MBUNGE FULANI:** Changia hoja.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Tulia wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *submarine* ndiyo *solution* ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau, naomba sana tuendelee kutumia lugha ya Kibunge.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nilikuomba Mheshimiwa Muhongo kwamba ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la umeme Mafia ni kuzamisha *submarine cable* kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni.

Kimsingi ukaniambia niendelee kukukumbusha. Mimi kwa kuwa wewe ni jirani yangu hapa kila nikifika asubuhi shikamoo yangu ya kwanza ni *submarine cables*...

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 60, elekeza maongezi yako kwa Mwenyekiti.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** *Submarine cable* itakuwa ndiyo salamu yangu ya kwanza ya asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nianze sasa kuchangia Mpango. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ashatu wameleta Mpango mzuri sana. Mimi naamini madaktari hawa wawili watatuvusha, tuwape ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye ugharamiaji *(financing)* wa Mpango huu. Mpango uliopita ulipata matatizo makubwa sana kutokana

na ukosefu wa fedha. Naamini kwa ari na kasi iliyoanza nayo Serikali ya Awamu ya Tano ambapo ukusanyaji wa mapato umekuwa mkubwa sana sambamba na kubana matumizi ya Serikali, *financing* ya Mpango huu wa sasa haitakuwa tafizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* yangu ipo kwenye sehemu ya pili ya *financing* ya Mpango huu ambayo ni sekta binafsi. Sekta binafsi wanakuja kuwekeza lazima sisi wenyewe tuweke mazingira wezeshi kama mlivyosema katika Mpango wenu, kwamba ili watu waje kuwekeza hapa lazima mazingira yawe mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, ninachotaka kusema ni kwamba tuwe waangalifu na hawa wawekezaji wanaokuja. Nitatolea mfano kule Mafia na Mzee wangu Mheshimiwa Lukuvi naomba unisikilize vizuri sana hapa, tuna Kisiwa kinaitwa Shungimbili. Mafia imezungukwa na visiwa vingi tu lakini kimoja kinaitwa Shungimbili. Kisiwa hiki cha Shungimbili kimebinafsishwa au sijui niseme kimeuzwa au sijui niseme kimekodishwa bila ya Serikali ya Wilaya kuwa na habari. Namuuliza Mkurugenzi anasema hana taarifa, namuuliza DC wangu anasema hana taarifa, naomba sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwishakwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Fedha.

Kwanza, niwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Lulindi ambapo katika uchaguzi uliopita nilishinda Ubunge kwa asilimia 87. Siri kubwa ya ushindi katika uwakilishi kwa wananchi ni kupunguza maneno na kufanya kazi na kuondoa kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua zote anazoanza katika kuhakikisha Taifa hili linaelekea kwenye uchumi wa kati, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapa pole sana wapiga kura wangu kwa maafu waliyopata kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika vijiji vya Matogoro kule Msanga, Mkangaula, Lupaso na

maeneo mengine ambayo sikuyataja, nawapa pole sana na nataka kuwahakikishia kwamba nipo pamoja nao katika mkasa huu uliowapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja katika hoja, nianze kuzungumzia kuhusu mapato. Kwanza, nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa jinsi ambavyo imejipanga kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato ya kutosha ili tuweze kwenda kuondoa kero za wananchi ambapo kwa muda mrefu wamekuwa wakisubiri huduma kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Wizara ya Fedha na watendaji, baadhi ya watendaji wengi hapa nchini wanashindwa kuwa wabunifu wa vyanzo ni kwa sababu wenyewe wanaendelea kupata riziki yao kwa maana ya mshahara na wanaendelea kupata pensheni baada ya kustaafu, wako tofauti kabisa na taasisi za binafsi ambapo wenzetu wamekuwa wabunifu sana. Mimi naomba sana tuhakikishe tunakuwa wabunifu na kupata vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho chanzo kikubwa sana cha mapato ambacho hatukitumii *cha property tax*. Mheshimiwa Mnyika atakubali kule Dar es Salaam tunazo nyumba nyingi sana kama zingeweza kulipa *property tax* vizuri na tukawaweka katika makundi mawili, wale ambao tunaweza kutathmini nyumba zao lakini wale ambao tunaweza kuwaweka katika kundi la ukadiriaji na tukakadiria katika kiwango ambacho mwananchi anaweza akalipa, ni chanzo kikubwa sana cha mapato. Naomba Wizara na Halmashauri ziweze kuona ni jinsi gani tunaweza tukakusanya mapato kutoka kwenye chanzo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuziwezesha halmashauri zetu kuweza kukusanya mapato ni jambo lingine. Kwa mfano, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Masasi, tarehe 23 Januari, 2013 nilipata janga kubwa sana la watu waliovamia Halmashauri na kuchoma magari 11 lakini pia kuchoma ofisi tano. Serikali ilituahidi kwamba halmashauri yetu ingeweza kupata fidia ya shilingi 1,337,000,000/= lakini tangu mwaka 2013 hadi sasa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Masasi imekuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa hiyo, hata viwango tunavyopangiwa kukusanya tunapata ugumu mkubwa sana. Namwomba Waziri wa Fedha, namuona Naibu yupo, hebu chukueni jambo hili ili kuhakikisha kwamba Halmashauri hii inapata fidia ili tuweze kununua magari, tuweze kutengeneza majengo yale ili ifanye kazi yake inavyostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala zima la barabara. Barabara ni jambo muhimu sana na sisi wote tunajua. Kwa mikoa ya Kusini sisi ni wazalishaji wakubwa wa zao la korosho na moja ya barabara ambayo ni ya

kiuchumi ni ile inayotoka Mtwara – Newala - Tandahimba - Masasi kupitia Lulindi. Barabara hii imeahidiwa na Mheshimiwa Rais na ipo kwenye Ilani na tayari kuna dalili za kuanza kujenga barabara hii.

Naiomba sana Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu kuhakikisha katika miaka mitano barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni barabara ya Ulinzi. Katika miaka mitano iliyopita tumezungumza sana juu ya barabara ya Ulinzi ambayo inapita kwenye zaidi ya Majimbo manne. Jimbo Mtwara Vijijini kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa Mheshimiwa Mkuchika, kwa Mheshimiwa Katani kule Tandahimbi, kwangu kwenye Jimbo la Lulindi na kwa Mheshimiwa Dua kule kwenye Jimbo la Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilikuwa na madhumuni makubwa mawili, kwanza ilikuwa ni barabara ya ulinzi. Wakati ule tunapigana na Mreno kule Msumbiji barabara hii ndiyo ilitumika vizuri sana kuhakikisha kwamba tunapambana naye. Pia tulianzisha vijiji vya ulinzi katika barabara yote hii lakini vijiji vile vyote havipati huduma ya barabara kwa sababu tuliomba iingizwe kwenye TANROADS lakini hadi sasa Wizara haijakubali. Namuomba sana Waziri anayeshughulika na Wizara hii ya Miundombinu tuhakikishe kwamba barabara ile tunaiweka TANROADS ili iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nilieleze ni suala zima la umeme. Nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Muhongo, tulikuwa wote kwenye Kamati ya Nishati na Madini, kwa kweli kazi yake kila mmoja wetu hapa tunakiri ni kazi iliyotukuka, hongera sana Mheshimiwa Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa ameeleza hapa kwamba wanatagemea kwenda Mtera kufanya tathmini ya REA I na REA II, yako mambo ambayo ningeomba mkayazungumzie. Kwanza, ni kwamba kwenye REA I na REA II idadi ya wananchi wanaotakiwa kupewa umeme kwa bei ya shilingi 27,000/= ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji. Kwa hiyo, jambo hili ni muhimu sana mkalizungumzie ili kuhakikisha kwamba idadi ile inaongezeka kulingana na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo limejitokeza ni kwamba wakati vijiji vinavyowekwa kwenye mradi wale wanaokwenda kufanya survey wanaacha vijiji vya katikati bila kuviingiza kwenye mpango, jambo ambalo linatusumbua sana wakati mpango ukiendelea. Ningeomba sana Profesa hili mkalishughulike kwa nguvu zenu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari kengele ya kwanza imeshagongwa, nichukue fursa hii kuzungumzia suala la viwanda. Kule Kusini

zao letu la korosho linahitaji kuongezewa *value* lakini itategemea na jinsi ambavyo tutaanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri mwenye dhamana afanye juhudi katika miaka mitano hii kuhakikisha kwamba viwanda vya korosho vinafufuliwa katika Mikoa ya Kusini ili korosho ipewe thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuokoa muda, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na ni mara yangu ya kwanza kuongea kutoka *back bench*. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutoa mchango wangu ndani ya Bunge hili na naahidi kushirikiana na wengi ili tuweze kutoa mchango wa Bunge kama unavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Wilaya na Jimbo la Hanang walionipa kura nyingi kurudi hapa Bungeni. Kulikuwa na changamoto na hujuma nyingi lakini hawakutetereka. Naomba waendeleo kusimama na msimamo huu wa kujenga Wilaya yetu. Wale wabinafsi wakae kule wenyewe na sisi tuendeleo kuliendeleza Jimbo letu la Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda sana kuwashukuru wananchi wa Hanang kwa kumpa Rais John Pombe Joseph Magufuli kura nyingi na CCM ikapita. Nashukuru sana na nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amedhihirisha kutoka CCM wananchi wa Tanzania wanaweza wakapata mabadiliko ya kweli na ya uhakika. Kwa sababu wengi walifikiri mabadiliko yanaletwa na vyama vya upinzani lakini Mheshimiwa Rais ameonesha kwamba mabadiliko yaliyo dhahiri na ya uhakika yataanzia kutokana na Mpango huu wa pili na wa kwanza wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye Mpango ambao uko mbele yetu. Msingi wa Mpango huu ni ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ujenzi wa uchumi wa viwanda utaleta maendeleo ya watu na si maendeleo ya vitu kama utaunganishwa na maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi, shughuli ambazo zinahusu Watanzania walio wengi. Mimi kama Mbunge wa Hanang nashukuru sana kwa sababu Wilaya yangu kwa kiasi kikubwa ni ya mifugo, ni ya ukulima na kutokana na Ziwa Basotu kuna wavuvi vilevile. Kwa hiyo, viwanda vikijielekeza kwenye kuendeleza tija ya kilimo maendeleo ya watu yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutambue kwamba kilimo kimekuwa ni shughuli ya watu wengi lakini na inaonesha kwamba maendeleo ya kilimo yanasuasua. Jambo moja ambalo ni dhahiri ni kwamba lazima tuunganishe

mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo jambo ambalo liliharibika wakati wa ukoloni lakini hatujawahi kulirudisha mpaka leo. Viwanda hivi vitasaidia kwa sababu kwanza kutokana na viwanda teknolojia inayotakiwa kwenye kilimo itapatikana, zana bora zinazotakiwa kwenye kilimo na mifugo zitapatikana pia. Badala ya kuuza mazao yetu nje bila ya kuongeza thamani viwanda hivi vitasaidia kuunganisha mnyororo ule. Kwa hiyo, naomba sana viwanda ambavyo tutavianzisha viwe na uhusiano wa karibu sana na kilimo, mifugo na uvuvi bila ya kusahau utekelezaji wa Liganga na Mchuchuma ambavyo ni viwanda mama vitakavyojenga viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni maendeleo na maji ni siasa. Ukiangalia katika kampeni ambazo tumezimaliza juzi wananchi wa Tanzania walio wengi walikuwa wanadai maji. Maji ni kazi ya akina mama ambapo wanaacha watoto nyumbani wanaanguka au wanaungua na moto kwa sababu ya kutafuta maji kwa umbali mrefu. Bila maji itakuwa ni vigumu sana viwanda kuendelezwa. Kwa hiyo, naomba sana, kabla sijafika kwenye maji, kuna misingi ambayo tunapaswa kuitekeleza katika Mpango huu. Kwa mujibu wa makubaliano hata ya kimataifa, sekta ya kilimo inapaswa kupewa si chini ya asilimia kumi ya bajeti kila mwaka ndipo ambapo tutaona maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango huu, mkiunganisha na maji, suala la kujenga mabwawa ya kumwagilia ambayo yatatoa maji kwa mifugo na kusaidia maji hata kwa wananchi litakuwa ni suala muhimu. Maji ni muhimu kwa ajili ya uhai lakini yatasaidia vilevile kuongeza tija kwenye kilimo. Kwa hiyo, naomba suala la mabwawa tulitilie mkazo katika Mpango huu na mimi narudia kusema tena kuhusu suala la Wilaya ya Hanang ya kuomba maji ya Mlima Hanang yakusanywe kwenye Bwawa la Gidahababieg ili watu waweze kupata maji ya uhakika, ili watu waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji na ili mifugo mingi ya Hanang nayo iweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka kwenye wilaya ya wafugaji, watu wanaohamahama. Naomba nikazie elimu kwani ndiyo itakayobadilisha *mindset* ya wafugaji wanaohamahama. Ili tuweze kuhakikisha watoto wa wafugaji wanapata elimu ya uhakika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na wale wote wanaohusika na TAMISEMI waone suala la mabweni na hosteli kwenye Wilaya za wafugaji linatiliwa mkazo kwa sababu hawataacha kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya kwanza imelia, naomba niseme kwamba jamani nzi anakwenda pale ambapo kuna mzoga haendi kwenye marashi. Kwa hiyo, tukitaka mambo ya polisi na FFU kutokuingia humu ndani, naomba Wabunge tuwe waungwana wakati tunatoa michango yetu. Humu ndani sisi ni Wabunge, sisi ndiyo dira ya wananchi, ni wawakilishi wa wananchi, tukileta fujo humu ndani, tunaashiria kwamba kule nje napo wafanye fujo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tuwe watulivu, tuwe waungwana, tuheshimiane humu ndani na tuliweke Taifa letu mbele ili tuongee mambo yanayohusu maendeleo ya watu wa Tanzania badala ya kuongelea mambo ambayo kila mmoja anataka ajiinue ili aonekane. Tukiwa waungwana, tukitumia muda wetu vizuri, wananchi wa Tanzania watatuona zaidi kuliko tunavyopiga kelele humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo, naomba niishie hapa na mimi nitasaidiana na Waziri wa Mipango kwa sababu nilikuwa naye kabla nikiwa Waziri wa Mipango ...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Katika kuleta mambo ambayo yatasaidia Mpango huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kushiriki Bunge hili kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda siyo rafiki sana, dakika kumi nazona chache, napenda kuanza kuzungumzia suala la utawala bora. Tunapozungumzia utawala bora tunamaanisha, usiwe utawala bora wa maandishi uwe wa vitendo. Tunapozungumzia vitendo, amezungumza mzungumzaji aliyepita sasa hivi, kazi yetu sisi siyo kupongeza Serikali, kazi yetu ni kuikosoa na kuisimamia Serikali. Hatuwezi kuogopa polisi pale ambapo tunaona kuzungumza ni haki yetu, hatuwezi kuogopa kupigwa pale tunapoona Serikali imekosea, tutaisimamia na tutaikosoa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utawala bora, nianze na suala la maslahi ya walimu. Walimu wa nchi hii ni watumishi kama watumishi wengine. Kama kweli utawala ni bora, kwa nini madai yao imekuwa ni wimbo wa nchi hii? Kila Mbunge anayesimama hapa akizungumzia Jimbo lake anazungumzia masuala ya walimu. Leo ukitazama hata kwenye vyuo, kwa sasa wanachuo wakikosa haki zao muhimu, wanaposimama kudai haki yao wengi wanafukuzwa vyuoni, je, huo ni utawala bora? Tukisimama hapa tukidai haki zetu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tuisaidie Serikali na nchi yetu kuboresha mapendekezo ya Mpango. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona yule alizungumza habari ya nzi?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniongoza kwa sababu najua ni kazi yako. Ninapozungumzia suala la utawala bora hatuzungumzi kwa sababu ya uoga na nidhamu ya uoga sisi wengine hatuna. Mnapozunguka mnatazama nchi zinazounda Umoja wa Afrika utawala bora wanafanyaje, lakini utawala bora wa Tanzania tunauzungumzia kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele mlivyoleta kwenye Mpango, Serikali makini haiwezi kuwa na vipaumbele vingi visivyokuwa na idadi. Inaonyesha ni jinsi gani mmeandika tu lakini utekelezaji ni sifuri. Nikianza na suala la kilimo. Natokea Mkoa wa Rukwa, tunalima sana mahindi na maharage. Leo hii wakulima wa Mkoa wa Rukwa wanajiona kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Pembejeo ni tatizo kwao lakini hata vile vichache wanavyopata kwa nguvu zao ili angalau kuzisaidia familia zao kuna ushuru usiokuwa na tija. Tunapozungumzia ushuru, huyo Mtanzania wa Rukwa ambaye ni mkulima, amekosa pembejeo, amejikongoja akalima kilimo chake tena kwa mkono lakini na kilekile kidogo Serikali inatoza ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini watakapoanza kuwathamini wakulima wa nchi hii hasa wa Mkoa wa Rukwa? Wamelima mahindi na mnajua walikosa soko, mmezungumzia hapa, lakini huyu mkulima wa Tanzania ili ajue kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inamthamini, inamthamini kwa lipi, kwenye pembejeo ni shida, kwenye masoko ni shida.

Naishauri Serikali, kama kweli tunaamini asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima, tutengeneze mazingira rafiki ya wakulima hawa. Isibaki stori za kwenye madaftari na vitabu yanabaki kwenye makabrasha, tunataka vitendo vifanyike. Kama kweli ni kazi tu mmemaanisha mfanye kazi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala la maji, nikiwa natazama Bunge kwa njia ya TV, Mheshimiwa Keissy imekuwa ni wimbo wake, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, iko Mkoa wa Rukwa. Watu wa Nkasi Kaskazini na wenyewe ni Watanzania kama Watanzania wengine, kwa nini kila siku iwe ni wimbo tu wa maji? Kwenye Mpango mnaoleta mtuambie ni mikakati gani mipya mliyokuja nayo ukiachana na nyimbo mnazoimba kila siku. Mikakati mipya iko wapi ambayo itatufanya sisi tuwaamini kama kweli mnakwenda kutenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi, imefikia mahali wamechoka na nyimbo hizi sasa wanataka utendaji. Ukitazama Bunge hili Wabunge wengi wanasimama wanazungumzia suala la maji, sawa, yawezekana tunazungumza na tunaleta kwa maandishi kama hivi, ni kitu gani kinawazuia sasa

mnapoandika mnashindwa kutenda? Kama kweli ni Serikali sikivu na siyo kinyume, tendeni sasa, muache kupiga *story*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu. Mkoa wa Rukwa umesahaulika kwa kila kitu. Watu wa Rukwa siyo Watanzania? Ukizungumzia Nkasi Kaskazini na Kusini barabara ni hadithi. Amezungumza hapa Mheshimiwa Mipata na anazungumza kila siku lakini sisi tunapozungumza hatuombi, tunaitaka Serikali ifanye kwa sababu ni wajibu wenu kufanya na msipofanya tunajua hamsikii na hamuelewi. Msifikiri Chama cha Mapinduzi kuendelea kuongoza ni kwamba mnapendwa sana, *no*, lazima mjitafakari. Pale mliposhinda kwa haki mjitafakari lakini mapito mliyoyapata katika kipindi hiki mnajua kwamba ni jinsi gani mmekosea *step*, lazima mjipange. Sasa kwenye Mpango mnaokuja nao tunahitaji mikakati madhubuti ambayo kweli inamaanisha kwenda kuwasaidia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la elimu. Suala la elimu haliwezi kufanikiwa kama mnakurupuka lazima mtafakari kabla ya kusema. Mnasema elimu bure, elimu bure itakujaje wakati walimu wenyewe madaai yao yako palepale? Sawa wanafunzi wamefika shuleni lakini sasa hivi wanafunzi idadi yao ni kubwa kuliko walimu. Hii elimu bure inakwenda sambamba na yale mnayoyasema au mnasema tu ili kutimiza wajibu? Mimi naamini hata hili mmeibuka tu kulisema, hamjajipanga. Ni mipango gani madhubuti ambayo mmetuonyesha hapa kama kweli mmekusudia kutoa elimu bure? Mimi nawashauri msiwe mnakurupuka, mjipange kwanza. Mkiona UKAWA wamekuja nayo wanazungumza msifikiri na nyie mnaweza mkafanya.

**MWENYEKITI:** Lakini walimu si lazima wawe wachache kuliko wanafunzi. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi yangu kuiambia Serikali pale walipokosea lazima wajirekebishe na wasikurupuke lazima wajipange. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa na maneno mengi kuliko kutenda na Watanzania wanaona. Haya wanayoyazungumza inaonyesha ni jinsi gani kweli wamekurupuka, hawajajipanga. Vipambebe ambavyo wanashindwa kuvitekeleza, vipambebe vingi, hakuna Serikali inayoendeshwa kwa staili hii. Lazima uwe na vipambebe unavyojua utatekeleza. Ni kipi ambacho mlilikleta kwenye Mpango uliopita na mmetekeleza kama mlivyokuwa mmepanga, hakuna! Imekuwa ni maneno ya kila siku ya kuandikwa yanashindwa kutekelezeka. Tunaitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi iachane na porojo, ifanye kazi. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Nami kwa vile nachangia kwa mara ya kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata hii fursa, nakishukuru chama changu cha CHADEMA kwa kuniamini na kunipa fursa na nawashukuru wananchi wa Jimbo la Segerea walionipigia kura zaidi ya 49,000. Kwa bahati mbaya sana, nikiwa nimejitoa katika Tume ya Uchaguzi na nimetimiza masharti yote lakini kwa yale yale tunayoyasema kukosa utawala bora, *within a deadline*, jina langu likarudi nikapigiwa kura zote. Nawashukuru kwa kutupa Madiwani 13 wa UKAWA na tukiwa tumeshinda kwa kura nyingi sana kwa wagombea wote wawili na nawaahidi nitawatumikia, gamba kwetu halina nafasi. (Makofi)

Ndugu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, kumradhi, mimi ni Mbunge mgeni kwa hiyo nitahitaji sana kujifunza. Nimepitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63(2) kinataja wajibu wa Mbunge kwamba ni kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla sijaja mahali hapa nilishangaa sana. Je, Wabunge wa CCM kweli huwa wanasoma Katiba? Nini wajibu wetu kama Wabunge? Sisi ni mhimili, kama ulivyo mhimili wa Serikali, kazi yetu ni kuishauri Serikali, kuwaambia tunataka wafanye moja, mbili...

**MWENYEKITI:** Mimi nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge, maana ukisema kwamba huna uhakika na Wabunge wa CCM kama wanasoma Katiba na wewe ni mgeni, sasa umepata uzoefu wapi? (Makofi)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimepata uzoefu kwa kuangalia kwenye *television* kwamba hatutimizi kazi yetu ya msingi ambayo ni kuishauri Serikali. Mimi ndiyo nachoenda kufanya, kuishauri Serikali. Sipo hapa kwa kazi ya kuisifia Serikali, sipo kwa kazi ya kumsifia Magufuli kwa sababu aliomba kura mpaka kwa kupiga *push-up*, kwa sababu alijua jukumu analoenda kufanya. (Makofi)

Tumekuwa na changamoto ya ardhi. Nimepitia Mpango na mnaonyesha takwimu zenu kwamba kwa nchi ya Tanzania, mmeweza kupima 10% tu ya ardhi ya Tanzania. Natokea katika Jiji la Dar es Salaam ambalo limekuwa na migogoro mikubwa ya ardhi. Wananchi zaidi ya kaya 16,000 zimewekewa alama ya "X" kwamba wanaishi kwenye mabonde, wanaenda kubomolewa majumba yao. Zaidi ya watu 99,000 watakuwa ni watu wasio na makazi. Changamoto ni kwamba Serikali ilikuwepo, watendaji walikuwepo, Waziri Lukuvi ambaye ni Waziri sasa alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alifanya nini wakati wote ambapo wananchi wameishi katika maeneo hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 1998 yalitengwa maeneo ya Tegeta ili wananchi waliokuwa wanaishi mabondeni wahamie hali kadhalika mwaka 2011 akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Wananchi wa Jimbo la Segerea, wananchi wa Ilala, wanataka viwanja vyao kwa sababu wanasema anahusika katika uporaji wa maeneo waliyopewa wananchi waliokuwa wanaishi mabondeni. Kama hiyo haitoshi, tuna changamoto ya migogoro ya ardhi kwa sababu Wizara ya Ardhi haijafanya kazi. Kuna migogoro ya wakulima na wafugaji kwa sababu asilimia kubwa ya maeneo hayajapimwa. Alivyochaguliwa au alivyoteuliwa juzi, pale katika Wizara ya Ardhi kulikuwa na *National Council of Professional Surveyors*, ni Bodi ya ma-surveyor, ameenda pale akaivunja. Pengine alifanya kitu cha msingi lakini tokea ameingia katika huo wadhifa amefanya nini baada ya kuvunja hiyo Bodi ambayo ilikuwa inashiriki katika kukagua na kudhibiti wanavyofanya kazi ma-surveyors? Tunaendelea kutengeneza migogoro juu ya migogoro. Tunafanya kazi kwa kutafuta sifa. Tumekuwa watu wa hapa kazi tu na tunafanyia kazi kwenye TV. Mawaziri wanashindana nani leo ataonekana kwenye *media*, hapa tuwashauri mfanye nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni ma-celebrity wazuri tu. Katika kitabu cha *Ideal State*, Plato aliainisha makundi ya aina tatu. Kuna *iron*, *silver* na *golden*. Kuna wengine walipaswa kuwa ma-celebrity leo ndiyo tumewapa Uwaziri na tunawapa dhamana kubwa ya kuongoza Serikali. Tunakosa cha kuwashauri kwa sababu kila mwaka mnakuja na mipango mizuri ambayo haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye suala la miundombinu hususan Jiji la Dar es Salaam. Mmejipanga kwamba mnataka viwanda lakini viwanda tunaviwekaje katika maeneo ambayo hayana barabara? Unasafirishaje hayo *material* pamoja na vilivyozalishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine? Ni changamoto ambazo ni za msingi. Segerea hatuna barabara kwani zote ni mbovu na hatuna barabara za mitaa zote ni mbovu. Serikali ipo miaka 54 ya Uhuru na mnataka tuwashauri, tuwashauri nini wakati mmekuwa mnasema kila siku mnashindwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lingine ambalo nitalizungumzia ni *gap* baina ya walikuwa nacho na wasiokuwa nacho. Inaonyesha, tangu mwaka 1992 tulikuwa na umaskini kwa asilimia 39 lakini mpaka mwaka 2007 mmeweza kupunguza kwa asilimia nne tu. Miaka 15 mmepunguza umaskini kwa asilimia nne tu na leo mnasema tuwashauri, tuwashauri nini? Tunachoweza kuwashauri, tokeni, mmeshindwa, tunaomba tuweze kuongoza nchi kwa sababu tunastahili. (Makofi/Kicheko)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabungewalikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazaliwa Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, nitawasemea. Nimeenda katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, nilichokikuta, Waziri wa Mambo ya Ndani aende kuona, kuna watu wamejitangazia nchi ndani ya nchi. Kuna watu wanajulikana kama Runyogote, Daniel na mwingine alikuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri, wametangaza nchi yao ndani ya nchi. Wana uwezo wa kuamrisha, wakaamrisha Askari wakaenda kukamata watu, wakakata migomba na wakapiga wananchi. Wanaweza kutangaza tunafunga barabara na wakafunga barabara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana, kwa saa hizi kuleta maombi ya kuchangia inakuwa vigumu kwelikweli *unless* kuna dharura ya dhati kweli. Naomba mtuelewe, inakuwa vigumu sana ku-*manage* orodha iliyo mbele yetu. Kwa hiyo, yale ambayo ni ya msingi tutajitahidi kwa kadri tutakavyoona na haya yaliyoletwa mbele yangu nitampatia katibu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni.

*(Saa 06.58 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*( Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia )*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa tutamsikia Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, halafu Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba ajiandae. Mheshimiwa Hamad hajafika! Mheshimiwa Bukwimba! Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba tafadhali endelea!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu. Nichukue nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa dhamana kubwa waliyonipa kuwawakilisha ndani ya Jimbo hili. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya na uhai wa kufika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nijielekeze katika suala la miradi mikubwa ile, hasa suala lile la miradi mkubwa wa *Village City* ambao uko Mkulazi unapatikana katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ndani ya Morogoro Vijijini katika Jimbo ninalotoka mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nijielekeze hapa kwa sababu huu siyo mradi wa kwanza kupewa ndani ya Jimbo hili lakini utekelezaji wake unachukua muda mrefu. Kwa mfano, tuna mradi wa bwawa la Kidunda mpaka sasa hivi unaenda una suasua. Hata hivyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kutupa mradi huu, lakini naomba nisisitize katika utekelezaji ufanyike haraka iwezekanavyo; hasa katika kuandaa miundombinu rafiki kwa ajili ya uwekezaji. Kwa mfano, sasa hivi Mkulazi vijiji vyake vyote vinne ambavyo ni Usungura, Chanyumbu, Mkulazi yenyewe na Kidunda vyote havina mawasiliano, vyote barabara haipitiki mwaka mzima, lakini pia hata maji yenyewe ndiyo hayo ya kubahatisha pia havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeiomba Serikali ingekuja na mpango kabla ya kuwekeza huo mradi mkubwa kuandaa hayo mazingira ili kuwavutia wawekezaji, hata wale watu wenye nia ya kuja kuwekeza ndani ya Morogoro vijijini, ndani ya Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki wawe na moyo kwamba mazingira yanaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu suala la viwanda, Morogoro ambayo ndiyo Mji wa mwanzo kabisa baada ya uhuru Serikali iliamua kabisa kuitenga mahsusi kwa ajili ya viwanda. Tunashukuru kwa hilo na kulikuwa na viwanda vingi tu ambavyo viikuwa vinasaidia ajira ndani ya Morogoro vijijini, Morogoro Mjini na Taifa kwa ujumla, lakini viwanda vile vingi havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kabla ya kuja na Mpango wa Pili wa viwanda wangekaa na hawa ambao waliobinafsishiwa ili kujua changamoto gani ambazo zimewakabili mpaka sasa haviwezi kuzalisha vile viwanda na kutoa ajira kwa Watanzania. Tulikuwa na viwanda vya *Moro Shoes*, Viwanda vya *Ngozi*, Viwanda vya *Mafuta*, Viwanda vya *Nguo* vyote hivyo vimekufa vimebaki vya *Tumbaku* na vile vya *Sukari*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwauliza wale wa wawekezaji wanatuambia jambo moja tu, wanasema kwamba viwanda tukizalisha hapa havilipi, kwa

hiyo, ndiyo maana rai yangu Serikali ni vizuri mkakaa na hawa mliowabinafsishia mkajua changamoto zao, hata kama mnataka tuvichukue tena lakini itatusaidia kubaini changamoto mapema ambazo zitatusaidia katika Mipango mipya kwa hapo kuanza kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu viwanda hivyo hivyo, suala la Viwanda vya Tumbaku kuwa Morogoro. Morogoro kwanza watu tuisahahu kwamba na sisi ni wazalishaji wa tumbaku, lakini pia unapoanzisha kiwanda mahali popote, wote humu Wabunge tungetamani kila Jimbo kuwe na kiwanda. Hata hivyo, kiwanda unaanzisha kwa kutugemea *cost benefit*, unatazama wapi nikiweke hiki kiwanda ambacho kitanilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya makampuni Morogoro ilijaliwa kwa Mwenyezi Mungu mwenyewe katika kuwa pale, kwa sababu ndiyo mikoa michache ambayo ilikuwa na rasilimali nzuri tangu wakati huo, lakini pia ndiyo sehemu iliyokuwa na maji ya uhakika, kulikuwa na umeme wa uhakika, lakini pia Morogoro ndiyo karibu na Dar es Salam ambako ndiyo kuna bandari kuu ya kusafirisha mazao. Kwa ushahidi huu ndiyo maana hata sasa hivi wafanyabiashara binafsi bado wanaitamani kuwekeza Morogoro kwa sababu ya jiografia na hali ya hewa iliyokuwepo Morogoro. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii Serikali muendeleo kutupa nafasi kubwa zaidi Morogoro kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda kwa sababu mazingira ni rafiki ambayo yanavutia na yana gharama nafuu sana ya uendeshaji. Nitoe mfano tu, hiyo tumbaku inazalishwa songea, Morogoro, Iringa na Tabora na mikoa mingine. Siyo rahisi kwa mwekezaji kuweka kila kiwanda katika kila mkoa ni kwa sababu inategemea na wingi wa *raw material*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nizungumzie kuhusu wajasiriamali. Mpango huu umekuja lakini umeweka nje wajasiriamali, kwa sababu tukizingatia hivi maendeleo ya viwanda ambao ndiyo Mpango wa muda wa Pili huu unakuja utategemea sana maendeleo ya kilimo. Hata hivyo, wajasiriamali wa nchi hii, hususani wanaojishughulisha katika mazao ya kilimo wamewekwa kando ya mfumo wa soko letu hapa Tanzania. Leo hii mfanyabiashara au kijana aliyemaliza elimu ya Chuo Kikuu au elimu ya sekondari ambaye anataka kujijaji mwenyewe hususani katika shughuli za kilimo hana fursa hiyo kwa mfumo wa soko uliokuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana aneyesifiwa mfanyabiashara mzuri ni yule anayefanya *importation*, akienda nje ya nchi akinunua mazao kitu chochote bidhaa amuuzie mkulima huyo anaruhusiwa na atapewa vigelegele, lakini yule ambaye anakwenda kununua mazao kwa mkulima afanye *exportation* ataambiwa mwizi, kibaraka, mnyonyaji, kibaraka wa Wahindi na majina yote ya ajabu ajabu atapewa huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali waje na Mpango mzuri jinsi ya kuliboresha soko letu ili sekta hii ya sehemu hii wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa waweze kushiriki kikamilifu katika ununuzi wa mazao ya biashara kutoka kwa wakulima moja kwa moja. Kwa sababu sasa hivi mfumo uliopo umewatenganisha kati ya mnunuzi na muuzaji. Leo hii mnunuzi hajui mzalishaji anahitaji nini na mzalishaji hajui mnunuzi anahitaji nini kwa viwango ambavyo wanavitaka. Matokeo yake baadaye biashara zetu zinakosa masoko baada ya uzalishaji na hatimaye wakulima wetu wanakuwa watu wa kuhangaika, leo wanazalisha zao hili, kesho zao lile, hakuna zao moja ambalo ana uhakika nalo la kumuinua kimaisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nizungumzie mgogoro wa wafugaji na wakulima. Sisi Morogoro kiasili ni wakulima lakini sasa hivi tumevamiwa kwa kiasi kikubwa na wafugaji wasiofuata sheria, taratibu hata na kanuni zile za kufuga. Baada ya kuchunguza muda mrefu nimeona wanahama kwa sababu wanakosa malisho maji huko wanakotoka. Niiombe Serikali ije na mpango mkakati wakuboresha miundombinu ya wafugaji huko wanakotoka na kuwapa elimu ya kufuga kisasa ili waendele kubaki huko ili janga ambalo mnatuletea Morogoro limeshakuwa kubwa linatuzidi uwezo wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa mfano jana tu, wakulima wangu kule Kata ya Tununguo na Vijiji vyake wamepigwa na wafugaji. Mfugaji anakuja anaingia ndani ya shamba anamwambia mkulima kwamba, mifugo ni muhimu kuliko chakula wanageuza mazao ya wakulima ndiyo chakula cha mifugo. Wanawatandika bakora hata wakienda sehemu yoyote hawasilizwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ije na Mpango mkakati wa kumaliza tatizo hili la wafugaji nchini, hasa kujenga miundombinu ya wafugaji sehemu za wafugaji na kupima ardhi yote ili tuweze kujua eneo la wafugaji lipi na wakulima? lakini hasa kuimarisha hiyo miundombinu ya kifugaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho haina maana kwa umuhimu, kuhusu suala hapo hapo suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo na najua maendeleo ya viwanda vinakuja baada ya maendeleo ya kilimo kuwa endelevu. Serikali kwenye Mpango wenu mmesema kabisa haijafanya vizuri kwenye kilimo, bila kuimarisha kilimo hata hivi viwanda tunavyotaka kuviweka vitakuja kukosa *raw material* baadaye italazimika tu-*import raw material* kwa ajili ya viwanda hivyo. Niishauri Serikali ije na Mpango Mkakati thabiti wa kuimarisha kilimo, kuongeza uzalishaji, kuwavutia masoko ili ku-*adress* matatizo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa mwaka 2016/2017. Kabla sijaanza kuchangia, kwa heshima kubwa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika katika Bunge hili, lakini pia nawashukuru Watanzania wote kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi kwa kishindo kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Masasi kwa kazi kubwa waliyofanya ya kampeni takribani miezi mitatu, minne hivi katika uchaguzi mdogo. Hawakukata tamaa walifanya kazi usiku na mchana hatimaye CCM imeshinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya kipekee, naomba nitumie fursa hii kuwaambia wananchi wa Masasi chaguo walilolifanya ni chaguo sahihi kukichagua Chama cha Mapinduzi, lakini kunichagua mimi mtoto wao ili niwapigania na tutatekeleza tuliyo waahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Serikali iendeleo kuweka nguvu kubwa katika kukusanya mapato. Iendeleo kuweka nguvu kubwa katika kuhakikisha kwamba wanakusanya kodi na kuwachukulia hatua wakwepa kodi wote pamoja na kuongeza juhudi zake za kupambana na ufisadi. Haya ni mambo ambayo tukiyafanya kwa nguvu kubwa tunaimani kwamba tunaweza tukasonga mbele kiuchumi.

Vile vile niwashukuru sana wale walioandaa mapendekezo haya na niseme tu mapendekezo haya yameakisi kwa kiasi kikubwa Hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini pia yameakisi kwa kiasi kikubwa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa mchango wangu katika sekta ya kilimo, kila mmoja wetu hapa anafahamu umuhimu wa sekta hii, namna ambavyo sekta hii ina uhusiano mkubwa sana na Sekta ya Viwanda. Hata hivyo, niseme tu Serikali ina mzigo mkubwa sana kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inasonga mbele na lazima tuelezane wazi kwamba hatuwezi kusonga mbele katika viwanda kama sekta ya kilimo haitapewa uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba niishauri Serikali lakini pia nimshauri Waziri mwenye dhamana kuwa ana kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba kilimo kinasonga mbele. Tunapozungumzia kilimo tunazungumzia sekta tofauti tofauti, lakini pia tunazungumzia suala la mazao ya

biashara. Kwa kweli hali ya manunuzi na mauzo ya mazao yetu ya biashara haijafikia kwenye kiwango cha kutembea kifua mbele. Nasema hivi nikiwa naakisi Jimbo langu la Masasi ambapo mchakato mzima wa ununuzi wa zao la korosho kama zao kuu la biashara umegubikwa na mambo mengi ambayo yanamkandamiza mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali ihakikishe kwamba kama tunataka kusonga mbele katika viwanda basi ni lazima kuhakikisha kwamba tunaondoa kero zote zinazomkandamiza mkulima wa zao la korosho. Zipo kero nyingi, kuna makato yasiyo na sababu za msingi, kuna sheria ambazo kimsingi zinapaswa zifanyiwe marekebisho ili kusudi korosho imnufaishe mkulima na iwe ni zao lenye tija. Pia mchakato mzima wa pembejeo na usambazaji wake nao umegubikwa na mambo ambayo kimsingi yanamkandamiza mkulima. Wapo wanaopata pembejeo ambao hawakustahili pembejeo. Namwomba Waziri mwenye dhamana aliangalie sana eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo deni kubwa kwa Watanzania na tusingependa kusikia tena Watanzania wakiendelea kulalamika kuhusu mazao yao ya biashara. Kero hizi namwomba Waziri mwenye dhamana na Serikali ihakikishe kwamba inaziondoa na tutaisaidia Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakiona kilimo chao kikiwa kina tija. Pamoja na mambo mengine wakati wote wakulima wetu wamekuwa hawana dhamana ya kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe nguvu kubwa kuhakikisha Benki ya Kilimo inawafikia wakulima, lakini tuhakikishe kwamba rasilimali zao zinarasimishwa ili waweze kupata mikopo, waweze kupata hati miliki na waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika Jimbo la Masasi tunacho Kiwanda cha Korosho, kiwanda hiki ni cha muda mrefu tungependa pia kiwanda hiki kiweze kufanya kazi ili wananchi waweze kubangua korosho zao na kuzisafirisha zikiwa zimebanguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengine ya msingi nitazungumzia kuhusu barabara, tunapozungumzia Kusini na mchango wake katika uchumi ni lazima tukumbuke kwamba wakulima wanaweza kurahisishiwa shughuli zao za kusafirisha mazao kama barabara zetu zinapitika. Tunalo tatizo kubwa tumeona katika mpango kuna kilomita kadhaa zilizotengwa kwa ajili ya barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa Serikali safari hii iangalie Mikoa ya Kusini ambayo imekuwa ikisahaulika sana kwa ujenzi wa barabara zetu. Zipo barabara zina umuhimu mkubwa kama waliotangulia kusema wenzangu kama vile barabara ya Ulinzi inayotokea Mtwara inakwenda Tandahimba na

Nanyamba - Newala inakuja kutokea Nanyumbu, hii ni barabara muhimu sana. Ipo barabara nyingine ya kutokea Mtwara unakwenda unatokea mpaka Jimbo la Lulindi unaingia Jimbo la Masasi hii ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya kipekee tunaiomba Serikali itutengenezee barabara ya Masasi kwenda Nachingwea, tunaomba Serikali itutengenezee barabara inayotoka Jimbo la Masasi inaelekea Jimbo la Ndanda na inakwenda kukutana na Jimbo la Nanyumbu kupitia katika Kata za Mwengemtapika Kata za Mlingula, Kata zote hizo mpaka tunafika katika hayo Majimbo mawili. Hizi ni barabara muhimu kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango mwingine kwa upande wa elimu, tunalo tatizo kubwa. Katika elimu tunazo changamoto lakini pia tunakila wajibu wa kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya. Sisi ambao tumeishi katika Ualimu takribani miaka 15, 16; tunajua namna ambavyo Wananchi wameguswa na suala la Serikali kufanya elimu bila malipo. Hili ni jambo la msingi sana na sote tunapasa kuipongeza Serikali kwa kazi yake kubwa iliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba Waziri mwenye dhamana pamoja na Serikali iangalie namna ambavyo tunataka kuboresha elimu isisahau elimu nje ya mfumo rasmi. Tunapotaka kuboresha elimu, tusifikirie tu kuboresha elimu kwa upande elimu iliyo rasmi, tuangalie pia elimu nje ya mfumo rasmi. Ningeiomba Serikali ifanyekazi pamoja na Wizara husika, kukaa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ione namna ambavyo inaweza, ikatoa mchango mkubwa katika kuelimisha watu nje ya mfumo ulio rasmi wa elimu. Ni lazima tukubali kwa sasa kwamba tunao Watanzania wengi wasiojua kusoma na kuandika, tunao Watanzania wengi wenye hitaji la elimu lakini wako nje ya mfumo rasmi wa elimu; hawa wanahitaji msaada mkubwa tusije tukawasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la maji, Mapendekezo ya Mpango yameonesha namna ambavyo Serikali inakwenda kulitatusa tatizo la maji. Niseme tu, niishukuru Serikali kwa namna ya kipekee kwa kujumuisha mradi mkubwa wa maji wa Mbwinji na kutaka kutengeneza mipango ya kuuendeleza kwa sababu mradi huu ni muhimu sana, kwa wananchi wa Jimbo la Masasi, lakini pia ni muhimu sana kwa Watanzania. Nawashukuru sana Serikali kwa kuweka mpango huu ili kusudi maji sasa yafike katika vijiji vyote vya Jimbo la Masasi, ambavyo havina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza kuhusu suala la barabara, lakini ni muhimu kuelewa kabisa, tunapoizungumza Mtwara na miundombinu yake lazima tuzungumzie pia uwanja wa ndege. Uwanja huu umekuwa ukiimbiwa mara nyingi kwamba unahitaji marekebisho ya kina, lakini marekebisho haya yamekuwa hayafanywi. Si jambo zuri mpaka leo tukiwa tunazungumzia uwanja

ambao ni uwanja wenye sifa za kuweza pengine kuwa wa Kimataifa, lakini hauna taa. Uwanja huu haujafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Tunaiomba Serikali yetu sikivu ifanye kazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa katika huduma zetu za afya, katika Jimbo la Masasi zipo zahanati saba tu. Tunajua Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba kila Kijiji, kila Kata kinakuwa na zahanati, lakini lengo hili halijafikiwa ipasavyo katika baadhi ya maeneo. Tunaiomba Serikali wakati inataka kupiga hatua mbele kuelekea katika uchumi wa kati unaotegemea viwanda, tuangalie pia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, kuniwezesha kusimama leo na kutoa mchango wangu katika mada iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongoea katika Bunge hili, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Malinyi, Jimbo hili siyo jipya tumebadilisha jina zamani lilikuwa linaitwa Ulanga Magharibi. Nawashukuru sana kwa kunirudisha kwa awamu ya pili najua wana imani kubwa kwangu na naomba niwaahidi kwamba, sitawaangusha, nitawatetea, tutafanya kazi pamoja kuleta maendeleo katika Jimbo na Wilaya yetu mpya ya Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Malinyi na Wilaya ya Ulanga. Mvua zinaendelea kunyesha, mvua hizi zimeleta madhara makubwa, zimeharibu miundombinu, zimeharibu na mashamba. Sasa hivi ninavyozungumza maeneo mengine hayafikiki kabisa, kutokana na uharibifu wa barabara uliosababishwa na hizo mvua. Kama mtakumbuka siku ya Jumanne, nimetumia Kivuko kile kilichozama Kivuko cha Kilombero, saa kumi na mbili jioni nimetoka Jimboni nimetumia kile Kivuko, lakini saa moja na nusu Kivuko kilekile kimezama na kimepoteza ndugu zetu pamoja na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali wamekuwa karibu sana na wananchi na wamekuwa wasikivu mara moja, siku ya pili asubuhi tulikuwa na Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Profesa Mbarawa, ameahidi na nawaomba tafadhali Serikali ahadi ambazo mmeziahidi naomba niwakumbushe maana muda unakwenda. Ahadi ya kwanza ya kurudisha haraka mawasiliano, Ulanga na Malinyi wako kwenye Kisiwa, kwa hiyo tumeahidiwa mawasiliano yatarudishwa, pamoja na ngalawa zilizoletwa, au boti zile za Wanajeshi hazitoshelezi. Tuliomba na tunaendea kuomba, warudishe kivuko kingine pale, maana bila kivuko pale jamani wale watu wanaishi katika maisha hatari na

wale watu wanaishi katika maisha magumu gharama za bidhaa zinazidi kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inayotishia nyingine stock za dawa zinakaribia kuisha mwishoni mwa wiki hii, hatujui baada ya wiki hii tutaishije kwa wale ambao watapata bahati mbaya ya kuugua. Pamoja na maombi hayo na kwa kuwa Serikali imeahidi, tunaomba ahadi ile itimizwe, umaliziaji wa ujenzi wa lile daraja la Kilombero. Serikali wameahidi kwamba kabla ya mwezi wa 12 mwaka huu daraja lile litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijikite mchango wangu katika mada iliyokuwa mezani kwetu na nitajikita katika maeneo matatu, mawili hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu ugharamiaji wa Mpango huu. Tumeshuhudia na taarifa ambayo tumeipokea bado miradi mingi kutegemea na Mpango wa mwaka jana, haikuweza kutimizwa. Changamoto kubwa hatuna fedha ya kutosha, wenzangu wameshauri, na mimi ninashauri ile ripoti ya Chenge one, ripoti ya Chenge two ifike muda sasa Serikali mtusikie, muanze kutekeleza hasa ninyi wataalam ripoti ile imechimba kwa kina zaidi na wataalam hao kwenye Kamati ile tunaendelea kuishauri mtekeleze angalau machache muone namna gani mnaweza mkaongeza pato la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutegemea na taarifa ya ripoti ya tafiti iliyofanywa na Dkt. Ngowi na wenzake wa Chuo Kikuu cha Mzumbe wakishirikiana na *Norwegian Church Aids* imebainika kuna upungufu mkubwa, watu hawalipi kodi. Wale wanaostahili kulipa kodi karibu milioni 15 nchi hii hawalipi kodi na asilimia ambayo imetoa ile ripoti ni asilimia 12 tu ndiyo wanaolipa kodi, maana yake nini asilimia 88 nchi hii tunakosa mapato. Kwa hiyo, kama Serikali wakija na mfumo mwingine na wigo wakiupanua zaidi, haya mambo tunayozungumza hapa, miradi inashindwa kukamilika itakuwa imefikia mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri Wizara hii ya Fedha na Mipango, hebu wasilianeni, muungane na watu wa *NIDA*, iwapo kama wenzetu wa *NIDA* watamaliza zoezi la Utambulisho wa Kitaifa, ni rahisi kuoanisha zile *nationa ID* na kumbukumbu za watu hao ambao wanakwepa siku zote kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, utahusu maeneo wezeshi kwa viwanda, na nitayabainisha maeneo kama matatu ama manne. Tunazungumzia viwanda ambavyo tunavyovilenga ni vile viwanda vitatumia malighafi ya kilimo, mifugo na uvuvi. Nikitoa mfano katika maeneo ambayo ninatoka maeneo ya Wilaya ya Malinyi, Kilombero na Maeneo ya Wilaya ya Ulanga. Maeneo haya yamebainishwa katika Mpango wa *SAGCOT* lakini

kwenye Mpango huu wa mwaka huu, hakuna chochote kinachozungumzia SAGCOT. Jamani mpango ule ni kuwawezesha wakulima kulima kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo cha biashara kitoe tija kuna mambo manne tu, kuna suala la nishati, miundombinu, maji na masoko. Suala la nishati Jimbo letu la Malinyi, ni vijiji 20 tu ndio vimeunganishwa na ule mradi wa REA kwa umeme. Kama vijiji vyote vingepata umeme hii ingekuwa na tija sana kwa wakulima kuongeza thamani ya mazao yao na upande wa pili kuongeza ajira kwa watu wanaojihusisha na kilimo, sasa niombe basi Serikali wamalizie ile miradi ya REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba ili kilimo kiwe na tija kuwe na barabara. Barabara zetu Wilaya ya Malinyi, Ulanga ni aibu, sasa hivi huwezi kufika maeneo mengine kwenye Wilaya ya Malinyi, kama ile Tarafa ya Ngoilanga ina watu 60,000 lakini leo hawafikiki kabisa sababu ya ubovu wa barabara. Mkandarasi yuko *site*, lakini amekimbia kwa sababu Serikali wenyewe wanajua, kwa hiyo naomba nisisitize katika mpango huu.

La kwanza, malizieni ile barabara ambayo tunaizungumzia, kuanzia Kidatu, Ifakara, Lupilo kwenda Mahenge, kutoka Lupilo kwenda Malinyi Kilosa kwa Mpepo, Londolumecha - Namtumbo. Barabara hii yenye kilometa 396 ni muhimu sana. Maana siku zote mnaendelea na mchakato. Hata kwenye taarifa hii mliyoandika watu wa mipango bado mmeweka barabara hii inaendelea na mchakato ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri, kwa sababu Mkandarasi yuko *site*, mumuongezee spidi amalizie huo mchakato wa upembuzi yakinifu. Baadaye tuzungumzie mwaka kesho tuanze kujenga hii barabara. Haitakuwa na tija tu peke yake kwa wakazi wa maeneo haya, barabara hii ni *shortcut* ya kutoka Mikoa ya Kusini kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie ya mwisho kuhusu Utawala Bora. Wilaya ya Malinyi ni mpya na Wilaya hii ipo pembezoni, tunaomba mtuwezeshe ujenzi wa majengo ya Wilaya hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako tayari umekwisha.

**MHE. DKT. HADJI HUSSEIN MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nami niungane na wengine kwa kuwa ni mara

yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa kuniadini na kunichagua kuwa Mbunge wao, kwa kura zaidi ya 87,000 dhidi ya yule ambaye upande wa pili wanamwita hajawahi kushindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika hoja yangu katika kuchangia Mpango wa Maendeleo, katika ukurasa wa 50(6)(a) ambayo ni Vihatarishi katika Mpango. Vihatarishi katika utekelezaji wa Mpango, vimeelezwa kwamba ni pamoja na kumekuwa na changamoto katika upatikanaji wa mikopo kwa wakati, na riba kubwa hivyo kuathiri uwezo wa nchi kukopa, kwa upande wa misaada kumekuwepo na masharti magumu na utayari wa washirika wa maendeleo kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa hapa kwamba vihatarishi vya Mpango ni pamoja na Washirika wa Maendeleo kukataa kutoa fedha kwa wakati. Washirika wa Maendeleo nchi ya Marekani, Taifa kubwa duniani, tayari limekataa kutoa fedha za MCC, na Umoja wa Ulaya uko njiani kuzuia misaada. Sababu wanasema kwamba kuna tatizo Zanzibar, uchaguzi wa Zanzibar umefanyika na kuna tatizo kubwa la msingi ambalo linapaswa kutatuliwa, sisi tuko hapa Bungeni tunajifungia ndani ya Bunge hili, tunajifanya hamnazo, tunaona kwamba Zanzibar hakuna tatizo tunashangilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasimama katika Bunge, wanajipa mamlaka wa kuwa Maamiri Jeshi Wakuu, na wanatangaza kwamba Zanzibar hakuna tatizo. lakini ukweli ni kwamba, uchaguzi wa Zanzibar utatuletea matatizo makubwa kama Taifa, tusipokuwa makini katika kutatua tatizo hili. Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hakuna namna yoyote ya Bunge hili kukwepa kuzungumza suala la Zanzibar. Uchaguzi wa Zanzibar ulifanyika tarehe 25 Oktoba na matokeo yote yakawa yameshakusanywa na yapo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar .

**MWENYEKITI:** Jina nani Mheshimiwa unayeomba Mwongozo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Naitwa Hafidh Ali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh Ali, mwongozo unaombwa mpaka mtu akimaliza kuongea. Mheshimiwa Kubenea endelea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba ulinde muda wangu. Iwapo matatizo haya Zanzibar hayatatatuliwa kwa umakini vinginevyo mpango huu mzima hautatekelezwa.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh nitakupa nafasi baadaye. Malizia Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa sababu Mbunge anayezungumza, anazungumza mambo yasiyo sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea naomba ukae. Mheshimiwa Hafidh unampa taarifa Mheshimiwa Kubenea?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Nampa taarifa Mheshimiwa Kubenea kupitia kwenye Kiti chako.

**MWENYEKITI:** Sawa endelea.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 68,(7)na (8) yake, Mjumbe wakati anazungumza anazungumzia suala la Zanzibar, suala la Zanzibar ni la utendaji moja kwa moja la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Hafidh, Mheshimiwa Halima Mdee naomba ukae tafadhali, utapewa nafasi na wewe, naomba ukae, utatumia Kanuni ambayo yeye akimaliza kuongea utapewa na wewe. Ili yeye amalize anachotaka kusema.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Hafidh naomba umalizie.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile Katiba ya Zanzibar. Hizi ni Katiba mbili tofauti na ndani ya Katiba hizi imesema wazi kwamba kutakuwa na Serikali mbili ndani ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Moja ni ile ya Zanzibar, moja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Katiba hizi zina mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiyo haitoshi ndani ya Katiba hizo zimesema kwamba kutakuwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, litakalokuwa linazungumzia na kushughulika mambo ya Muungano na kutakuwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambalo litakuwa linazungumzia sala zima la Baraza la Wawakilishi na Mwenendo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Anayezungumza sasa hivi, anayoyazungumza hayako katika mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuzungumzia mambo ya Zanzibar ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba azungumzie mambo yaliyokuwemo katika mada ambayo tunaizungumzia ya Maendeleo, suala la Zanzibar halina mamlaka ya kuzungumziwa ndani ya Bunge hili. La pili, mamlaka ambayo Bunge ilikuwa linaweza kuzungumza ni pale tulipokuwa tunazungumzia Hotuba ya Rais, kwa sababu aligusa kwamba atafanya kazi kwa matatizo ya Zanzibar. Lile limekwisha Hotuba ya Rais tumemaliza tunazungumzia Maendeleo, Maendeleo haikuguswa Zanzibar katika kitabu hiki. Kwa hiyo Mjumbe asizungumzie Zanzibar kwa sababu humu ndani Bunge halina mamlaka ya kuzungumzia Zanzibar. Mamlaka ya kuzungumzia Zanzibar yako katika Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tena unifahamu...

**MWENYEKITI:** Naomba ujitahidi umalize.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Namaliza. Marais wawili waliopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna Rais mkubwa, wala hakuna Rais ambaye yuko juu ya mwenziwe. Wote Marais hawa wanaendeshwa kwa mujibu wa Katiba za sehemu yao; ndani ya Jamhuri ya Muungano kutakuwa na Marais wawili. Mmoja wa Zanzibar mmoja wa Bara, Bunge halina mamlaka wala Katiba haijasema kwamba Bunge hili linaweza kuzungumzia mambo ya Zanzibar

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Huyu bwege kweli kweli huyu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea uendeleo.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba ulinde muda wangu, lakini nimepokea maelezo ya Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, nimemshangaa kwamba anataka tusizungumzie masuala ya Zanzibar, wakati yeye ametoka Zanzibar amekuja hapa kuiwakilisha Zanzibar. Yuko kwenye Bunge hili kwa sababu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Mpango wa Maendeleo na ninapozungumzia maendeleo, tunazungumzia maendeleo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar ikiwemo, Katiba hii imeitaja Zanzibar kuwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; asome vizuri. Matatizo ya Zanzibar ya uchaguzi yasipopatiwa ufumbuji wa kudumu tukakaa humu ndani tukajifanya hatujui kama Zanzibar kuna tatizo, Maaskofu wanahubiri katika Madhabahu, Mashehe wanasema katika Misikiti, wadau wa maendeleo wanatukanya, kwamba Zanzibar kuna matatizo sisi tunakaa hapa tunajidanganya. Nchi yetu tunaipeleka pabaya na Mpango huu wa Maendeleo hautafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea mwaka 1964 mpaka mwaka 1980 hakuna Mpango wowote wa Maendeleo uliofanikiwa kwa zaidi ya asilimia hamisini kwa sababu wadau wa maendeleo walikataa kutoa fedha. Fedha za maendeleo kutoka kwa nchi wahisani zilikuwa hazitoshi na huu mpango mzima unaokuja hapa unategemea fedha za wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa thelethini na moja wa kitabu hiki, kimeelezwa juu ya suala zima la utawala bora. Bunge hili ambalo Mpango unasema kuimarisha utawala bora, lilifanya kazi kubwa sana katika Bunge la Kumi, kulipitishwa maazimio hapa juu ya fedha za escrow, Tume zikaundwa, Majaji ambao walituhumiwa kuhusika na kashfa ya Escrow wakaundiwa Tume za uchunguzi, ilitangazwa. Mawaziri wanne wakajiuzuru katika Bunge hili, Wenyeviti wawili wa Kamati za Bunge wakajiuzuru. Serikali ikasema inaunda Tume lakini Tume ya majaji haikuundwa, Mawaziri waliojiuzuru mmoja Profesa Sospeter Muhongo amerudishwa katika Bunge hili akiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyeondolewa na Bunge leo anaongoza Bunge kama Mwenyekiti wa Bunge. Hii maana yake nini, maana yake suala zima la rushwa lililotajwa katika ukurasa wa 34 kwamba ni tatizo katika nchi yetu linaonekana halina tatizo kabisa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Nampa taarifa Mheshimiwa Saed Kubenea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy naomba ukae tafadhali.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nampa taarifa tu Mheshimiwa kidogo.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kanuni ya 68.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy nitakupa fursa wewe itafute hiyo Kanuni Mheshimiwa Kubenea endelea.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nipe taarifa tu, naomba taarifa tu. Nampa taarifa aelewe, nampa taarifa kidogo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nimpe taarifa tu.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae, Mheshimiwa Keissy nitakupa nafasi.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Naomba taarifa, Kanuni ya 68!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea endelea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa naeleza na bado nasisitiza kwamba suala la utawala bora ni jambo la muhimu sana katika Taifa letu. Hatuwezi kukaa hapa tukawa tunahubiri amani na utulivu wakati Taifa letu halina utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana mmoja wa wachangiaji katika Bunge hili alisema kwa sauti kubwa kwamba Chama ambacho kimegombea uongozi kwa vipindi vitatu mfululizo kikishindwa kitaingia kuwa chama cha ugaidi. Hata hivyo, namsamehe kwa sababu hasomi historia anaishia hapa hapa Tanzania. Ukienda India, Uingereza, Canada na Newzealand vyama vyote vikubwa vilivyoshindwa uchaguzi vimebaki kuwa imara, Chama kinachoshindwa uchaguzi lakini kinaendelea kuimarika kwa kushinda Majimbo mengi na kuchukua Halmashauri nyingi na kile ambacho kinashinda uchaguzi, lakini kinaendelea kuporomoka siku hadi siku kipi kinachoelekea kwenye ugaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka Chama kile ambacho kinashinda uchaguzi lakini kinaendelea kuporomoka siku hadi siku ndicho kinachoelekea katika ugaidi. Hayo yanaonesha ni jinsi gani Taifa letu leo usalama wa raia wetu ulivyokuwa mashakani. Mimi mwenyewe ni muhanga wa usalama wangu na nimetajwa katika Bunge hili la Kumi katika ripoti ya *richmond*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanauwawa, watu wamepigwa na Serikali iliyopo madarakani imeshindwa kulinda raia na mali zao. Waandishi wa Habari kina Mwangosi, Mwandishi wa Habari mwenzangu ameuwawa, Absalom Kibanda amepigwa, Dkt. Steven Ulimboka ametekwa na kutupwa katika Msitu wa Mabwepande, lakini Serikali imekaa kimya na inasema hawa

watu wasiojulikana. Serikali ni lazima ichukue hatua madhubuti kulinda usalama wa raia na mali zao ili kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wanazungumza sana mambo ya reli ya kati na mimi naomba nizungumze kuhusu reli ya Kati.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Katika Mpango huu kuna mkakati madhubuti.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Naitwa Nchambi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea *just a seconds*.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Naitwa Suleiman Masoud Nchambi

**MWENYEKITI:** Naomba usubiri kwanza nimekuona umesimama, lakini naomba tumuache Mheshimiwa Kubenea amalize.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akimaliza tutashindwa kutoa taarifa

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunilinda.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inaturuhusu, tunakuomba sana ufuate Kanuni...

**MWENYEKITI:** Naomba ukae nimesimama..

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Tunasimama kwa mujibu wa Kanuni...

**MWENYEKITI:** Naomba ukae nimesimama, naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge, hizi Kanuni zetu ni nzuri sana zinatusaidia kuendesha mijadala yetu ukiambiwa ukae haimaanishi hautapata fursa. Muda wako, nisikilizeni basi niwaeleze, hizi Kanuni ukikataliwa taarifa unaweza kusimama akishamaliza kuongea, muda wake umebaki ni sekunde chache, muache amalize omba kwa kutumia Kanuni nyingine, nitakupa fursa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nazungumza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae tafadhali, Mheshimiwa Kubenea malizia.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mpango mzima wa reli ulioletwa hapa na Serikali, wakati sisi tunaonya kwamba nchi wahisani zimekataa kutoa fedha na kwamba mipango hii ya maendeleo haiwezi kutekelezwa. Kuna Mpango umekuja hapa wa reli. Reli hii inahitaji dola bilioni saba, karibu shilingi trilioni kumi na tano. Serikali ya Tanzania ilikuwa inaomba fedha kutoka Serikali ya China. Naomba niwapeleke shule, Serikali ya China imekataa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga reli ya kati, mtafute fedha kutoka maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea muda wako umekwisha!

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuanah Wataala* kwa kunipa afya njema nikawa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitakuwa mchoyo wa fadhila na shukrani zangu za dhati kabisa kama nitashindwa kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Tandahimba ambao wamenichagua kwa asilimia 57 nikawa Mbunge wa kwanza Tanzania kutangazwa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Mapendekezo ya Mpango, ukienda ukurasa ule wa kumi yamezunguzwa sana mambo ya maji. Jambo la ajabu kwangu mie Tandahimba kunakozungumzwa maji ambapo kuna vyanzo vya maji vya kutosha, Serikali kama ingekuwa makini tusingeendelea kuimba wimbo wa maji leo hapa. Maana kwenye Jimbo langu sisi tupo mpakani mwa Msumbiji na Tanzania na tuna mpaka wa Tanzania na Msumbiji ni Mto Ruvuma. Jambo ambalo kama Serikali ingekuwa makini tusingekaa hapa watu wa Mtwara tukazungumza habari ya maji. Niiombe Serikali kupitia suala hili la bajeti, waone kabisa kuna kila sababu ya kuona Mkoa wa Mtwara hatuwezi kurudi tena tukazungumza suala la maji na maji yamejaa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu zangu wamezungumza suala la kuboresha kilimo. Tunapozungumza kuboresha suala la kilimo tunazungumza na suala la barabara pia. Tumezungumza 2014 ukitoa dhahabu ni korosho ambayo imeingiza Taifa bilioni 647.9. Ukitoka Mtwara kwenda Tandaimba, Newala, Nanyamba ambapo ndiyo wazalishaji wakubwa wa korosho hizi hawana lami kwa miaka 54 ya CCM bado mnasema mna mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara ya Fedha niombe Mawaziri wenye dhamana wawafikirie wakulima hawa wa korosho ambao wanaleta pato kubwa la Taifa lakini bado ukasafiri kwa masaa sita, saba kwenda sehemu yenye umbali wa kilometa 95 kama Jimboni kwangu Tandahimba kutoka Mtwara Mjini kwenda Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wamezungumza sana suala la bandari. Nimeona mipango ya kuandaa bandari mpya ya Mbegani sijui wapi huko, nyingine ya Tanga, lakini bandari yenye kina kirefu Tanzania na Afrika Mashariki ni bandari ya Mtwara. Umezungumzwa mpango wa kujenga magati manne, lakini kwenye ule mpango limezungumzwa gati moja tu lenye urefu wa mita 300, lakini halijaelezwani lini lile gati litajegwa. Niiombe Serikali watakapokuja na mpango sasa wawaambie wana Mtwara gati hilo la mita 300 litajengwa lini na litakwisha lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema Mtwara tuna fursa kubwa kama Serikali itakuwa inaona umuhimu huu. Leo unakwenda Uchina unakwenda nchi za Ulaya ukitafuta bandari, bandari ya Mtwara yenye kina kirefu haipo kwenye ramani. Sasa Serikali hii ya CCM bado mnajivuna, mnazungumza suala la viwanda na gesi tunayo Mtwara mtajengaje viwanda vya korosho Tandahimba ambapo umeme wenyewe haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo REA phase II iliyozungumziwa mpaka leo ukija sehemu zenye uzalishaji umeme bado haupo. Napata shida sana, tunapozungumza suala la viwanda wakati sehemu yenye umeme bado wananchi wake hawana umeme, lakini mnazungumza kupeleka viwanda, unapelekaje viwanda sehemu ambayo haina umeme? Sasa niombe muwe makini sana mnapoleta mipango hii, na mara zote CCM mmekuwa wazuri sana wa ku-plan, ni wazuri sana wa ku-plan, implementation ndiyo shida. Sasa ninaiomba Serikali ya CCM kama ina nia njema, yale mliyoyaweka kwenye mpango myatekeleze. Vinginevyo sisi tuna take off 2020, tunachukua nchi hii kabisa. Haya wala siyo masihara mimi kwangu kule nimeshawapiga, Madiwani nimeshachukua kila kitu nimezoa zoa pale. Tunajiandaa kuisafisha CCM 2020, Mtwara kama hamkuleta mambo mazuri kule, kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeele kuzungumza suala la umeme, ambalo nimekuja kuzungumza hapa, tulipata shida, sisi ndiyo tulipigana, tulipigwa tukakaa jela wakati tunaitetea gesi, lakini watu wa Mtwara hawakuwa na shida ya Serikali kutoa gesi Mtwara kwenda Dar es Salaam, watu wa Mtwara walikuwa wanatetea maslahi ya watu wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo bomba limekwenda Dar es Saalam kilometa 542, lakini Mkoa wa Mtwara kuna watu hawana umeme. Wakilalamika mnataka wasilalamike, wakilalamika mnawapiga, sasa Serikali imekuwa ni ya kupiga piga tu hovyoy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza suala la elimu hapa, wakati mnazungumza suala la elimu tumepongeza Mpango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Magufuli, suala la elimu bure, lakini vitu vya ajabu, kama Rais

amesema elimu bure iweje leo mtoto anakwenda hospitali kupima anaambiwa atoe pesa na ndiyo kauli ya Rais. Kama Rais amesema bure vyombo vyake vingine kama ni suala la kupima mwanafunzi aende apimwe bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *joining instruction* nayo ni shida wakienda Mahakamani wanatakiwa watoe pesa sasa hata kwa vitu vidogo hivi! Hata kwa vitu vidogo hivi! Hebu msaidieni Rais Magufuli huyu aonekane alichokisema kina maana ya bure kweli. Tusikae hapa kuzungumza bure watoto wanaenda hospitali tu wanaambia elfu tano ya vipimo, mwanafunzi anakwenda Mahakamani anaambiwa shilingi elfu tano ili aandikiwe sijui kitu gani sijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Serikali hii kama ina dhamira njema kama ilivyozungumza tuone haya mambo mnaweza kuyarekebisha, lakini mlizungumza vitu vizito, wenzangu wakazungumza suala la *airport* ya Mtwara. Ukisoma hotuba ya Rais kuna maeneo yanaonekana *airport* ya Mtwara, uwanja umekarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Waziri mwenye dhamana kama utapata fursa njoo Mtwara, ile *airport* tunayozungumza kwamba imekarabatiwa ndege ikitua ni balaa. Utafikiri unatua kwenye maporomoko, sijaona uwanja wa ndege wa namna hiyo wa ovyo. Mataa hakuna sasa akina Dangote watakuja asubuhi tukiwa na mambo ya dharura ya usiku inakuwaje! Ndiyo maana hata Mawaziri hamji Mtwara usiku kwa sababu hakuna *facility airport* pale, taa hakuna mmezibeba taa zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nione kama mna dhamira njema ya kuleta viwanda mnavyosema, kuboresha miundombinu mnavyosema. Hebu wafakirieni watu wa Mtwara kwa namna nyingine sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu limezungumzwa suala la elimu kwa maana ya VETA nataka niizungumzie VETA kidogo, kwa maana ya viwanda mnavyosema, viwanda na Vyuho Vikuu. Kwangu pale kuna kata moja ya Mahuta, kuna majengo pale yaliyoachwa na Umoja wa Wazazi Tanzania. Kuna majengo yanayotosha Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama una shida ya majengo ya VETA njoo tukukabidhi Mahuta pale ili watu wa Tandahimba wapate fursa ya kuwa na VETA ili iwasaidie watu wa Newala, Masasi, Nanyamba watapata fursa kwa sababu majengo tayari tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mchango wangu ulikuwa huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie kwenye Mpango uliowasilishwa na Serikali. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye kwa rehema

zake amenipa kibali niwe miongoni mwenu kuwatumikia Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu. Vile vile, nitumie fursa hii kuwashukuru sana ndugu zangu wa Mkinga kwa kunipa heshima kwa mara ya pili, kuwa Mbunge wao niweze kuwawakilisha katika Bunge letu ninawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaahidi kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kwa maarifa ya hali ya juu, na niimani yangu kwamba, kile tunachokikusudia tutakipata. Nitumie fursa hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameanza kushika hatamu za kuliongoza Taifa letu. Watanzania wana imani kubwa na uongozi wake, nimpe maneno ya kumu- encourage kwamba, tupo pamoja naye katika kuwatumikia Watanzania na Watanzania wanaamini kwamba, kasi ya mabadiliko waliokuja nayo itakuwa ni kasi ya ukweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie maneno, niazime maneno ya Rais wa 33 wa Marekani aliyekuwa akiitwa *Harry Truman* aliandika katika memo yake, *Years of Trial and Hope* katika ile volume ya pili anasema, "*Being a President is like riding a tiger, a man has to keep on riding or be swallowed.*"

Anaendelea kusema: "*A President either is constantly on top of events or if he hesitate events will soon be on top of him.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia Mheshimiwa Rais Watanzania wana imani naye, aendelee na mwendo huo aliouanza nao bila ku-hesitate, tunaiona Tanzania yenye mabadiliko na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nichangie mpango huu ulioko mbele yetu. Nimejaribu kuusoma mpango huu, lakini vilevile nikapata fursa ya kusoma *Household Survey Report*, lakini vile vile nikasoma report ile *Human Development Report* nikajaribu ku-combine maudhui tunayoyapata kutokana na taarifa zile. Maudhui ya taarifa zile yanatuambia kwamba tuna namba nzuri sana za mafanikio ya ukuaji wa uchumi. Namba zile zinatofautiana, ukisoma *household survey* na ile report nyingine zinatofautiana takwimu kidogo lakini *bottom line* ninachosema ni kwamba, hatujafanya vizuri sana katika maendeleo ya binadamu, maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi ni viongozi lazima tuwe wakweli kwamba, tuna changamoto kubwa mbele yetu ya ku-translate ukuaji wa uchumi ili uweze kuleta maendeleo ya watu. Ndiyo maana hapa naipongeza Serikali kwa kutuletea Mpango huu wa Pili ambao una vionjo vinavyoonyesha kwamba, tunakwenda sasa kwenye kuunganisha ukuaji wa uchumi lakini vilevile ku-translate ukuaji huo kwenye maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kujenga uchumi wa viwanda ambavyo vitazalisha ajira, viwanda ambavyo vitapelekea kupunguza umasikini, tunaelekea huko. Lakini lazima tujiambie kama viongozi, tuwe wakweli tujiambie kwamba mMango huu tuliouleta ambao tunaenda kuufanyia marekebisho ili baadaye uje upitishwe ndani ya Bunge hili, utekelezaji wa Mpango huo tutakaokuwa tumeuleta, ukiwa chini ya asilimia 70 tutakuwa tumeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha hatushindwi. Takwimu zinatambiaje, takwimu zinatambia tulilenga kuwa na maeneo ya kilimo cha umwagiliaji hekta 1000 tumetoka kutoka kwenye hekta 345 tumekwenda kwenye hekta 461. Lakini hekta tulizonazo zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika nchi yetu tuna hekta milioni 29.1, tulichofanikiwa ni asilimia 0.39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuje na mikakati ya kuhakikisha tunakwenda mbele. Nimeona hapo ujenzi wa viwanda, ujenzi wa bandari ya uvuvi ni jambo zuri, lakini ili tufanikiwe lazima tuunganishe jambo hili la ujenzi wa bandari ya uvuvi tuliunganishe na jambo la ufugaji wa samaki maana dunia ndiyo inapokwenda huko. Haiwezekani leo hii nusu ya samaki wanaoliwa duniani wanatokana na ufugaji wa samaki halafu sisi tusione umuhimu wa kufuga samaki, lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ile itakapojengwa lazima tujenge miundombinu ya ufugaji wa samaki, twende kisasa lazima tuwe na *aquaculture industrial zone*. Tuunganishe pale, bandari ya uvuvi, viwanda vya kuchakata samaki, viwanda vya kuchakata barafu na kadhalika na kadhalika na ufugaji wa samaki uwe pale pale. Katika maeneo yaliyotajwa katika kujenga bandari. Nilisema kipindi kilichopita ilianishwa bandari ya Dar es Salaam wote tunajua. Bandari ya Dar es Salaam hapafai kuna msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Moa kule Mkinga namshukuru Rais maana kila alipokuwa akisimama kutoa hotuba yake anasema ukanda wote wa bahari kutoka Moa kule Tanga mpaka Mtwara hakuna kiwanda cha samaki. Njooi pale Moa wekeni bandari ya uvuvi maana katika maeneo yaliyotajwa matatu Moa ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu lilitajwa Bagamoyo lakini Kamati iliyopita ilitushauri hapa ndani. Ikasema hivi tunaondoaje Chuo cha Mbegani, twende tukajenge bandari ya uvuvi, ni imani yangu Serikali imesikia njooi Moa tuweke mambo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanda lazima uzingatie vile vile kuweka mkazo kwenye kujenga.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muda wako umekwisha.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kwa ruksa yako, niwashukuru wapiga kura wote wa Mkoa wa Pwani wakiongozwa na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli pamoja na Baraza lake la Mawaziri. Mheshimiwa Rais wewe endelea na kuchapa kazi kama kaulimbiu yako ulioitoa ya “Hapa Kazi Tu” haya maneno ya humu ndani ni sawa na wimbi la baharini, Waswahili sisi kule baharini tunasema wimbi la nyuma halimsumbui wala halimkeri mvuvi, kwa hiyo ya nyuma yamepita sisi tusonge mbele, tuchape kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijikite kwenye mpango ambao tunao mbele yetu. Mpango huu unauzungumzia ujenzi wa uchumi. Nianze kwa kuipongeza Serikali kuwa na uamuzi wa kufanya elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari na chekechea yake lakini nitoe msisitizo tunaposema elimu bure tusaidie kutengeneza mazingira bora. Kwenye Mpango haikugusa maeneo ambayo yatamfanya Mwalimu, yatamsaidia Mwalimu kuweza kufanya kazi zake kwa amani zaidi ya hivi sasa anavyofanya. Majengo, Nyumba za Walimu, miundombinu na mambo mengine yale muhimu kwa ajili ya kuendeleza elimu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo itakayotusaidia kuinua uchumi wetu na hasa huo uchumi wa viwanda tunaouzungumzia. Kuna masomo ya sanaa na masomo ya sayansi, tunapozungumzia masomo ya sayansi ndipo tutakapopata wataalam wa viwanda, sasa hivi tujikite katika kujenga vyo vya VETA, kupeleka wanafunzi wengi, ili waweze kuajiriwa maeneo mbalimbali katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni vipi Mpango umemuangalia mwanamke katika kuinua uchumi wa viwanda, ni vipi mwanamke atashirikishwa, ni vipi umeme utaweza kusaidia kwenda kijijini ili mwanamke au gesi itakavyoweza kusaidia inayotoka Mtwara ifike mpaka kijijini ili mwanamke yule apungukiwe na mzigo wa kutafuta kuni, apungukiwe na mzigo wa kuhangaika na mambo mengine, aweze kwenda kushiriki katika kazi za kuinua uchumi katika, katika kuajiriwa kwenye viwanda, hata kuweza kuwa na

viwanda vyao wenyewe wanawake kama Serikali ilivyotuwezesha kuwa na Benki yetu ya Wanawake kuwa na Benki ya Kilimo. Hayo ndiyo mambo ninayoomba mimi, huu Mpango uangalie na uende ukarekebishe tuone hayo yatafanywaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kumkomboa mwanamke aweze kushiriki katika ujenzi wa uchumi, tuangalie na mazingira ya mtoto wa kike toka anasoma chekechea. Watu wamegusia suala la maji humu ndani, maji ni msingi unaoweza kuleta maendeleo katika nyanja zote, lakini maji hayo kama hayatofika kila mahali na kwa wakati, kuna udumazi wa maendeleo utakaotokea na kuwanyima wengine haki ya kuweza kwenda kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa maana kwamba tunahitaji uvunaji wa maji mashuleni, uwezo wa kuchimba visima kama *water table* iko chini sana basi itengenezwe miundombinu ya kuvuna maji ya mvua. Mahitaji ya maji ya mtoto wa kike au ya mwanamke ni makubwa zaidi ya wanaume, tunahitaji watoto wa kike wawekewe utaratibu, wanapewa pesa za kuwasaidia lakini wawekewe na utaratibu wa kupewa mataulo ya kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa wa Jimbo la Ludewa Mjini aliyeguswa na maendeleo na mahitaji makubwa ya mtoto wa kike. Nakushukuru sana na nakupongeza, wanawake wote tunasema tuko pamoja na wewe na tumekutaja leo kwenye vikao vyetu tutakushirikisha ili uone tutasaidiaje watoto wa kike katika kuleta maendeleo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali kutoa misaada. Mtoto wa kike anaweza asiende siku saba shule, yuko nyumbani, mama anahitaji maji zaidi ya baba, anahitaji ndoo tatu, nne kwa siku. Leo hii kama mama hapati maji ya kutosha hawezi kwenda kushiriki kwenye uchumi, kwa hiyo suala la maji ni suala la kuwekea msisitizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la gesi. Naipongeza Serikali kwa juhudi iliyofanya, gesi inatoka Mtwara imefika Dar es Salaam mpango haukueleza, katika Mkoa wetu wa Pwani inapoanzia Rufiji watu watanufaika vipi! Tunahitaji gesi ile ipate manufaa Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Mkuranga, Wilaya ya Kisarawe, Wilaya za Kibaha, Bagamoyo, ambako pia nako kuna uwezekano pamoja na Mkuranga kupata gesi tuone tutafaidika vipi, viwanda vingapi tumeandaliwa kuletewa, gesi imekuja, tunawaambia watu wasikate mkaa, watu wamezoea kukata mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam yote inalishwa mkaa unaotoka Pwani, sasa Mpango huu unaelezaje, gesi hii imeandaliwa vipi na Serikali ili wale wakataji wa mkaa waweze kunufaika na biashara yao wakaacha, misitu yetu ikarudi pale pale. Sasa hivi misitu imekuwa kama vipara, eeh unakwenda

unakuta pembeni kuna miti lakini ukienda katikati miti hakuna. Mama anahangaika kutafuta kuni asubuhi mpaka jioni. Watani zangu kule Usukumani miti yote imekwisha matokeo yake wanatumia mavi ya ng'ombe. Kwa hiyo, niwaombe, ufanywe utaratibu Serikali ihakikishe gesi na umeme inafika kwa watu wote ili kuleta maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wangu mniwie radhi nasema ukweli wa maisha. Niseme kwamba suala la maendeleo katika Wilaya ya Mkoa wa Pwani, naomba tuliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Rufiji. Rufiji watu wameanza ujasiriamali, wanachonga vitanda lakini ushuru wa kitanda ni laki moja na ishirini. Huyo muuzaji atanunua hicho kitanda kiasi gani? Ushuru wa mkaa umepanda asilimia moja na kumi na nne, huyo mwananchi anayekata miti na mbaao anafanya biashara ya kujisaidia ataendelea vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Nyamwage mpaka Utete na Utete ndiyo kuna hospitali ya Wilaya, tunatarajia watu watolewe Utete wapelekwe kwenye hospitali ya Wilaya Kibaha, barabara mbaya, Wilaya ile ni miongoni mwa Wilaya kongwe katika nchi hii, mpaka leo hii hatujaiona lami. Tunaomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika twende Mafia. Kuna barabara inaanza Kilindoni hadi Bweni haina lami, lakini pia Mafia kuna utalii, naomba Serikali kupitia Wizara ya Utalii, hebu ijaribu kuangalia ni vipi watainua wilaya ile na kuifanya wilaya ya kiutalii. Watalii wengi sana wanakwenda, tunashukuru, gati limejengwa tunangoja tishari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuu uwanja wa ndege umejengwa tunasubiri taa ziwekwe, watalii waingie asubuhi na jioni hali kadhalika na wananchi waingie asubuhi na jioni. Hata hivyo, bado tuna tatizo la hospitali zetu, Wilaya zetu za Mkoa wa Pwani, zimepakana na Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kwenye vituo vya afya na zahanati na hospitali za Wilaya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii. Pia niwashukuru wananchi wa Manyoni Mashariki kwa kura zao nyingi, kwa imani yao kubwa kwangu mimi mpaka kuniingiza katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema, nimepitia mapendekezo ya mpango huu, nimeyapitia vizuri sana, nikiitazama nchi yangu Tanzania, nikiwatazama Wabunge wenzangu humu ndani kama Wawakilishi wa wananchi. Mpango huu nimeuelewa vizuri, sijaona mahali pabovu. Ni sisi tu Wabunge kujazia nyama ili Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake, waende sasa kuuandaa vizuri kwa ajili ya kuja kuuwasilisha kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kabla hata ya Mpango huu kuanza naona gari limeshaanza kuondoka na ninahisi gari hili kasi yake itakuwa kubwa. Nikimtazama dereva aliyepo ndani, Dkt John Pombe Magufuli ni dereva mahiri ametia imani Watanzania, gari litakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, naomba niende moja kwa moja kwenye mjadala. Baada ya kuupitia mpango huu, kuna vitu na mimi kama Mbunge ambaye ni moja ya kazi zangu naomba sasa nijazie. Mpango huu ni mzuri, utatuvusha kama tutayazingatia yote hayo. Kila mmoja kama akitimiza wajibu wake Waziri kwa maana ya Serikali watimize wajibu wao kwa kutenda na sisi tutimize wajibu wetu katika kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna kipengele cha sheria, tukitazame kwa makini. Kuna sheria nyingi ambazo zinahitaji marekebisho, sheria zile ambazo zinagusa mpango huu. Sheria kwa maana ya sheria zile *Principle Legislations*, Sheria kubwa lakini pia sheria ndogo kwa maana *Subsidiary Legislations*, nikitazama naona nyingi zina upungufu. Hazitakwenda na kasi ambayo Mheshimiwa Rais na Serikali yake ambayo naiona ni kubwa ni lazima kama Wabunge tuzitazame sheria hizi. Kuna Kamati zimeundwa, kuna Kamati ya Sheria na Katiba. Naomba wakae chini watizame sheria zote zinazogusa mpango huu, tafadhali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria ya Manunuzi ya Umma namba Saba ya mwaka 2011, sheria hii imeijeruhi sana nchi yetu, sana tu. Naomba iangaliwe upya, Kamati hii ilete mapendekezo baadaye Waziri mhusika ailete, kama ni kurekebisha turekebishe, kama ni kufuta na kuandika nyingine ifutwe na tuandike nyingine, naomba tuiangalie ni sheria mbaya kabisa, sheria inayoruhusu kununua vifaa chakavu, sheria inayochukua mlolongo mrefu kwa muda kidogo tu. Kwa mfano, kujenga nyumba, jengo labda la ghorofa mbili, inachukua karibu miezi sita. Tunakwenda kwenye uwekezaji, tunakwenda kwenye kujenga viwanda, lazima sheria hizi ziwe rafiki, zichukue muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Mpango huu unatajwa kuinasua nchi kwenda kwenye kipato cha kati, bila kuja na sheria mahiri ya kuzuia na kupambana rushwa, tutakuwa tunatwanga maji na kuishia kulowa. Naomba sheria hii pia ibadilishwe, irekebishwe, hatuwezi

kuendelea kuvumilia baada ya jalada la uchunguzi kukamilika, liende kwa DPP, ofisi inayojitegemea, Mkurugenzi wa TAKUKURU hawezi kumfuatilia huyu, kuhimiza kwamba muda ni mfupi, inachukua muda mrefu, hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama Maalum imetajwa, sheria hii itakapoundwa maana yake Mahakama Maalum kwa ajili ya makosa ya rushwa tu lazima iundwe. Nazigusa Sheria ziko sheria nyingi, Sheria za Uwekezaji, milolongo mirefu na *regulations* zake zina milolongo mirefu sana zinafukuza wawekezaji, lazima tuweke mazingira rafiki kwa wawekezaji wetu.

Niguse maeneo wezeshi kidogo tu angalau. Upimaji wa ardhi; hatuwezi kuzungumzia viwanda bila kupima ardhi zetu, hatuwezi! Tutumie wataalam tupime ardhi zetu. Tuainishe maeneo, maeneo ya makazi, maeneo ya viwanda, maeneo ya biashara, lazima tutenganishe. Huu ndugu zangu ndiyo ustarabu wa mwanadamu, *planning*. Tutumie wataalam wetu tu-*plan*, tu-*plan* Miji yetu, tuiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mbeya, nilipita Kibaigwa hapa, kuna Mji mmoja unaitwa Tunduma, ka-*centre* kamoja kanakua kwa haraka sana. Ukiangalia nyumba zilivyomwagika kama takataka. Inaondoa ustaarabu wa mwanadamu. Tunao wataalam, tupime miji yetu. Msongamano wa Tunduma ule kama Mji ungekuwa umepimwa tusingekuwa na msongamano kama ule. Kibaigwa ule ni mji mmoja mzuri sana, lakini kama ungepimwa viruzi, ule mji ni ungekuwa ni mzuri sana. Tutumie wataalamu sasa wetu, kupima miji yetu. Pia kupima inasaidia kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri pia kwenye suala hili la mapato kwa maana ya kukusanya kodi. Hebu tuunganishe ukusanyaji wa kodi za majengo na ukusanyaji wa kodi za ardhi zilipwe katika eneo moja. Tutumie wataalam wetu wapo, *GIS* kwa maana *Geo Information System* nzuri kutambua maeneo na kuweza kukusanya kodi kwa urahisi kabisa. Tunayo *deed capital* kwenye majengo haya, kubwa mno kama tutatumia wataalam tutaweza ku-*realise* mapato makubwa sana ya kugharamia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo suala la utalii. Utalii pia ni chanzo kimoja kikubwa cha mapato yetu. Sisi Manyoni pale, Jimbo la Manyoni Mashariki tunalo eneo linaitwa Kilimatinde, eneo hili linavuma sana kwa umahiri kwa kumbukumbu nzuri ya mambo ya kale. Ukipita pale Manyoni kuna njia ya Watumwa ambao walipita karne ya 18. Tangu karne ya 18, pale alipokanyaga mtumwa mpaka leo hapaoti jani wala mti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Mtuka muda wako tayari.

**MHE. WIFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Unapozungumzia suala la reli ya kati, reli ya kati kwa Kagera haiishii Mwanza. Reli ya kati inaishia katika bandari ya Kemondo ambapo siku za nyuma wakati bado reli inafanya kazi vizuri reli ya kati, tulikuwa na meli ambayo ilikuwa inapakia mabehewa na kuna njia ya reli ambayo inaishia bandari ya Kemondo. Tunapozungumzia reli wananchi wa Kagera, Mheshimiwa Lugola amezungumzia kwa upande wake namna gani ambavyo bidhaa zinavyosafirishwa kwa njia ya barabara zinavyokuwa na bei kubwa zinapofika katika eneo lake. Sasa nazungumza kwake ni tisa, kumi ni Kagera, sisi ndiyo tuliopo pembezoni mwa nchi hii. *Cement* ni shilingi elfu ishirini na mbili kufikishwa pale Bukoba Mjini na bei hii naamini ni kwa sababu bidhaa ya *cement* na bidhaa nyinginezo zinasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwetu sisi kukosekana kwa reli ya kati kwa wananchi wa Kagera na hususani Bukoba mjini, ni kwamba mipango hii inayopangwa bila kuzingatia kuweka reli, wananchi wa Kagera mnataka waendeleo kuwa maskini. Na mimi niseme hivi, umaskini huu unakwenda mpaka kusababisha bei ya kahawa kushuka, kipindi cha nyuma kahawa ilikuwa inasafirishwa kwa reli, yale mabehewa yalikuwa yanayokwenda mpaka Bukoba kupeleka bidhaa pale Kemondo, yanarejesha bidhaa ya kahawa mpaka kwenye bandari zetu tayari kusafirishwa kwenda nchi za nje, kwenye masoko. Usafiri wa barabara wa kusafirisha kahawa umechangia pamoja na sababu nyingine umechangia kushusha bei ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe, tunapopanga mipango hii Waheshimiwa, tujitahidi kuangalia kina na kiini cha ni namna gani watu mipango mnayoipanga inashindwa kuwaondoa ndani ya umaskini. Niseme kwa wananchi wa Kagera na Bukoba *in particular*, tukumbushane hata ahadi zinazofanyika mziweke katika mipango na zitekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkapu katuahidi meli baada ya Mv. Bukoba kuzama; Mheshimiwa Kikwete katuahidi meli, Mheshimiwa Magufuli naye wakati akiomba kura ameahidi meli. Sasa huko mbele tunapokwenda leteni mipango kanyaboya, leteni mipango ambayo haioneshi ahadi zilizopita.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare naomba ukae. Taarifa Mheshimiwa Nchambi

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanaumwa! Kanuni yetu ni ile ile ya 68(8), Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akichangia hapa kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, unapotaja jina la Mbunge ni Mheshimiwa Mbunge, unapotaja jina la Spika ni Mheshimiwa Spika

na hata Rais ni Mheshimiwa Rais. Sasa anaposema Magufuli, kwanza anashusha hadhi ya cheo cha Urais. Anatakiwa kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, aseme Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli ameahidi hivi, Lazima aanze na Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba Mwongozo wako juu ya suala hilo, nilitaka nitoe taarifa hiyo, lakini nimwombe atake radhi juu ya kauli aliyotoa ya kutaja jina Rais bila ya kuanza na Mheshimiwa. Aombe radhi ni taratibu za kawaida tu hizi, ugeni ndiyo unawasumbua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nchambi, uliomba taarifa na hiyo taarifa umempa Mheshimiwa aliyekuwa anachangia, siyo mwongozo maana mwishoni umesema tena mwongozo. Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WIFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ili roho yake ipone pamoja na kwamba na yeye amemwita Magufuli basi Rais Magufuli, furahi basi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, nilikuwa nazungumzia suala la ahadi, tuliahidiwa meli, meli haijaja. Sasa katika uchunguzi wangu tatizo linalotupata katika mipango inayopangwa na Serikali, suala la kutoleta sheria inayopaswa kwenda sambamba na mipango inayoletwa. Matokeo yake hakuna nidhamu ya utekelezaji wa mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata ndani ya Bunge hili, kulikuwa na utaratibu wa kuunda Kamati ya *Governance Assurance Committee*, Kamati ya Ahadi za Serikali, hii Kamati naamini ingeweza kusaidia katika suala la kuishinikiza na kuisimamia Serikali kwa ahadi zinazotolewa Ndani ya Bunge hili. Matokeo yake hakuna Kamati hizi. Kwa hiyo, mipango inayopangwa na naamini hata hii mipango inayopangwa, kwa kuwa hatuna sheria, hatuna Kamati inayosimamia hii mipango, huenda hizi ahadi na mipango ikawa hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria hizi hazipo na mimi hapa ndiyo maana namuunga mkono Mheshimiwa Warioba katika Katiba ya Warioba ambayo ilikuwa inahitaji Mawaziri wasiwe Wabunge. Kwa sababu tatizo la nchi hii kutokana na kwamba hatusimamiwi na sheria, kila mmoja anayepata nafasi ya kuwa Rais, kuwa Waziri Mkuu, kuwa Waziri, wote wanaanza kukimbilia kuangalia kwao kunahitajika nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ajabu tukaanza kusikia hata mipango mingine zaidi ya Bagamoyo, zaidi ya viwanja vya ndege, zaidi ya kupeleka mabomba ni kwa sababu watu hawasimamiwi, watu mipango inapangwa kufuatana na nani yuko wapi na ana-influence gani na Hazina. *That is the*

*problem!* Kwa hiyo, niombe sambamba na mipango hii sheria itungwe lakini ile *Governance Assurance Committee* ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nipo Chuo Kikuu Walimu wangu akiwemo Profesa Baregu, Profesa Mutahaba, Marehemu Profesa Liviga waliwahi kuniambia na kunifundisha kwamba mahala ambapo hakuna *good governance* hakuna *true democracy*. Mipango yoyote haiwezi kuenda. Mheshimiwa Mpango naamini na wewe ni msomi unaamini kabisa, najua unaamini kwamba mipango yote unayoipanga kama itakuwa na sokomoko la kutuingiza tena katika mgogoro wa miaka yote mitano kuingia sakata lililokuwepo mwaka 2000 mpaka 2005 kule Zanzibar hakuna mipango itakayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme ndugu zangu sikio lililokufa halisikii dawa. Hawa CCM, kwanza niwashukuru wananchi wa Bukoba Manispaa, waliuthibitishia ulimwengu na Taifa hili na wakathibitishia wengine waliosema wana ushahidi ndani ya dunia hii na mbinguni kwamba Lwakatare ni gaidi. Malipo ya wananchi wa Bukoba waliyoyatoa ni kuhakikisha Lwakatare anashinda kwa kishindo na anakabidhiwa Halmashauri kuja Bungeni hapa. *(Makofi)*

Sasa niwaambie Makamanda hizi nyimbo, miongozo, taarifa mnaopigwa iwape nguvu ya kukanyaga mafuta ndani ya Bunge. Nilipokuwa likizo nje ya Bunge nilikuwa naona mlikuwa mnaanzia hapo mpaka hapa. Leo tumewasukuma, tumekwenda mpaka pale nawahakikishia Bunge linalokuja mtasogea hivi na wengine watapita njia hii. *(Makofi)*

Makamanda nilikuwa likizo nje ya Bunge, wananchi huko nje ya Bunge wanatuelewa. Wananchi nje ya Bunge sisi uwanja wetu wa kucheza na watu wanaotushangilia wako nje, hapa wacha washangiliane wenyewe kwa wenyewe. Nawahakikishia Makamanda msirudi nyuma. Mapigo mliyopiga akina Msigwa ndiyo yamezaa leo Halmashauri za kutosha, imezaa Wabunge wa kutosha na 2020 *Wallahi* na Mtume nawaambia tunachukua Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la Zanzibar CCM mumshukuru Maalim Seif. Maalim Seif uzuri wenyewe anapenda Ikulu lakina ni mtu mfaidhina, ni mtu anaswali swala tano ndiyo bahati yenu, angekuwa kama akina a.k.a Nkurunzina wallahi pangechimbika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja zilizoko mezani juu ya Mpango wa Miaka Mitano. Kwanza

namshukuru Mungu kuniwezesha kufika katika Bunge lako Tukufu. Pia nashukuru chama changu kuniona nafaa kuiwakilisha jamii. (Makofi)

Awali ya yote, napenda kuungana na wale wote ambao wamechangia hoja inayohusu Tanzania ya viwanda kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa kwamba Tanzania ya viwanda lazima iendane na afya ya wananchi, elimu, utawala bora, miundombinu, maji na ardhi. Nafahamu kabisa kwamba nia na madhumuni ya mpango huu ni kuleta ustawi wa jamii kwa wananchi wa Tanzania ndiyo maana Upinzani na Chama Tawala tunachangia kwa hoja nzito ili tuweze kuleta ustawi wa jamii kwa Watanzania wote. Lengo letu siyo malumbano, lengo letu ni kuhakikisha kwamba Watanzania ambao wanatumia pesa zao kwa ajili ya kutuweka hapa wanapata haki stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye mada halisi. Ningependa kuongelea afya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba hakuna ufanisi katika Tanzania ya viwanda bila wananchi kuwa na afya bora. Tukiangalia maeneo mengi ya Tanzania tunakuta kwamba huduma za afya ziko hafifu. Kwanza nakumbuka asubuhi ya leo kulikuwa na msemaji mmoja ambae alitoa haja yake kuhusu hali halisi ya afya ya Watanzania na mazingira wanayoishi. Waziri husika alijibu kwamba Serikali siyo sababu ya wananchi kupata matatizo ya afya, isipokuwa wananchi wenyewe ndiyo sababu ya kupata matatizo ya afya au magonjwa ya kipindupindu na magonjwa ya mlipuko. Mimi napenda niulize Serikali iliyoko madarakani kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa kwamba kuna sekta zinazoshughulikia afya na kama kuna tatizo la kipindupindu ina maana kwamba sekta inayohusika haijawajibika. Nataka nijielekeze kwa mfano, natoka Mkoa wa Pwani Wilaya ya Kibaha, ilitokea mlipuko wa kipindupindu na sababu kubwa ni kwamba, Wizara ya Maji kwa Pwani haina mamlaka isipokuwa tunatumia DAWASCO ambayo kwa Pwani hakuna miundombinu ya kutoa maji machafu. Ina maana utiririshaji wa maji machafu ni lazima kwa sababu DAWASCO haijawajibika na watu wa Pwani wanahitaji mamlaka yao ili waweze kuiwajibisha pale inapokuwa haiwezi kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, narudi kwa Waziri aliposema kwamba siyo wao wanaosababisha, yeye kama Waziri anafahamu kabisa ni nani ambaye hakuwajibika mpaka mlipuko wa magonjwa utokee. Kwa hiyo, hawezi kusema kwamba yeye siyo sababu. Napenda kumwambia kwamba yeye na Watendaji wenzake hawakuwajibika. Walitakiwa wawajibike ili ugonjwa wa

kipindupindu usitokee kwa sababu wapo ambao wako kwa ajili ya kazi hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kwenda kwenye sekta ya elimu, tunaangalia Tanzania ya viwanda ambayo inatakiwa iende na elimu. Ni kweli tumedahili watu wengi kwa ajili ya sekta mbalimbali, lakini tuangalie sheria zinazo-govern uanzishwaji wa viwanda. Tunafahamu kabisa uanzishwaji wa viwanda siyo ufufuaji wa viwanda pengine ni uanzishaji wa viwanda kwa mashirika yanayotoka nje, wawekezaji kutoka nje. Hautaondoa umaskini Watanzania kama waanzishaji wa viwanda wanakuja wa watu wao kutoka nje, kama sheria za nchi haziwezi kusimamia kuhakikisha kwamba rasilimali watu iliyopo hapa ambayo ni watoto wetu ambao wamesomeshwa kwa pesa za Watanzania wanaajiriwa katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba au niishauri Serikali kwamba, itakapoanzisha mpango huo ihakikishe kwamba inatunga sheria ambazo wawekezaji watakuwa nazo wakiangalia kwamba Tanzania ina watu ambao wanaweza kufanya kazi ambazo wanaleta watu wao kuja kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, kuna bomba sasa hivi linatoka Ruvu chini kupeleka maji Dar es Salaam. Nimeshuhudia kwa macho yangu, mpaka yule wa kufukua udongo, yule mtu wa kufanya kazi za *welding* ni Mhindi wakati tuna Watanzania tunawasomesha VETA hizo mnazosema zimeanzishwa wamekaa mitaani hawana kazi. Sasa unajiliza je, huu umaskini tunaouimba hapa utaondolewaje kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na hapo naomba niende kwenye kilimo, nimesoma, nimeangalia jinsi Waziri wa kilimo alivyojipanga, lakini naomba niongee machache juu ya hilo. Nimeona kilimo kina ufugaji, kina kilimo yenyewe, lakini nikiangalia kuna ufugaji, naomba ni-*declare interest* mimi ni mfugaji wa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mara nyingi sana kuku wakitoka Kenya wanajazwa pale Dar es Salaam kiasi kwamba wafugaji wa Tanzania tunashindwa, wajasiriamali wa Tanzania tunashindwa kuweza kufanya biashara. Sasa ningependa Wizara katika Mpango huu wa Tanzania ya viwanda basi wahakikishe kwamba Wizara husika inasimamia kidete hali hii ili Watanzania wajasiriamali waweze kufaidika na kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa upangaji wa bei, mkulima amelima kwa shida zote, Serikali inakuwa mpangaji wa bei. Serikali inapanga bei wakati mkulima amelima kwa gharama zake. Anapokosa mapato mkulima anashindwa kuendeleza kilimo. Kwa hiyo, umaskini hatuwezi kuondoa kama

Serikali haiwezi kusimamia kilimo ipasavyo, kutafuta masoko ambayo yana tija na kuhakikisha kwamba mkulima anapata faida ili kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu. Nimeangalia miundombinu nikaona kwamba kwa usafiri kwa mfano wa Dar es Salaam, msongamano wa Dar es Salaam nilivyouangalia, sisi sote tunafahamu kwamba *time ni factor ya production*, kama hatuwezi ku-*save time tuna-consume time* kwenye kutembea kwenye barabara masaa manne kutoka Kibaha mpaka ufike Dar es Salaam, masaa manne kutoka Mbagala mpaka city center ukafanye kazi, ina maana muda mwingi unapotea hapo katikati bila kutumika. Hii ina maana kwamba Tanzania ya viwanda watu watakuwa wanatembea kwenye magari masaa manne hawajafika kiwandani ina maana utekelezaji wake utakuwa mgumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuende kwenye miundombinu ya maji. Nimesoma na nimesikiliza lakini nimeshangaa kusikia kwamba asilimia 68 ya Watanzania wanapata maji. Jamani mimi natoka kijijini kwetu Makambako chini kule hawajawahi kuona maji ya bomba hata siku moja. Nimekuja huku Kisarawe Mkoa wa Pwani wanachota maji ya visima, hiyo asilimia 68 ambayo wamei-*calculate* wakapata hapa sijaweza kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kweli tuna nia ya dhati ya kuhakikisha wananchi wetu wanakuwa na afya bora, hebu Serikali ijipange kuhakikisha maji ya uhakika yanapatikana kwa ajili ya kuwapa afya bora Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye ardhi. Ni kweli kabisa ardhi ndiyo mpango mzima wa Tanzania ya viwanda ya Mheshimiwa Magufuli, lakini naomba nitoe ushauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha mchangiaji. Kabla Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe hajasimama, Mheshimiwa Mary Deo Muro umesema habari ya Mhindi kuwa anachimba mtaro. Waheshimiwa Wabunge tunao Wahindi ambao ni Watanzania. Kwa hiyo, naomba kauli za namna hiyo tuangalie namna ya kuzitoa isije ikaonekana Bunge linafanya ubaguzi. Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe!

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Mpango uliopo mezani. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunijaalia afya njema. Vile vile nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kukishukuru chama changu kwa kunifuata kuwa Mbunge wa

Viti Maalum ili niweze kuwatetea Watanzania. Niende moja kwa moja kwenye mchango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la Utawala Bora, tunaimba amani, amani, amani na utulivu, lakini niseme ukweli ni miaka 54, hakuna amani na utulivu Tanzania. Wanawake hatuna amani wala utulivu kwa sababu tunadhaliishwa, mfano kwenye Mkoa wangu wa Njombe... *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumsikilize.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mkoa wangu wa Njombe wanawake wengi wanabakwa, vilevile wafanyakazi wa kike wanaokwenda maofisini wanatakiwa kutoa rushwa za ngono. Hii ni wazi na ni dhahiri lakini sisi tumefumba macho tunasema amani. Hii ni amani kwa watu wachache, lakini kwa watu wengine hatuna amani au hawana amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna mambo mengi ambayo yanaendelea ya wanawake wajasiriamali. Wanawake wajasiriamali sasa hivi wanahangaishwa, wanakimbizwa huku na huku. Mfano, Mkoa wangu wa Njombe, wanawake wanatolewa barabarani kama vifurushi. Wanatolewa mizigo yao au bidhaa zao zinawekwa kwenye magari ya kutolea takataka, kwa kweli huu ni udhalilishwaji na huu ndiyo tunasema utawala bora, huu siyo utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomoa bomoa, wanaodhalilishwa sasa hivi, wanaopata matatizo ni wanawake na watoto kwa sababu mali zao ziko nje na baridi, wanahangaika na baridi na watoto. Ni kweli! Kwa hivi kwa kweli tunasema bado Serikali ya sasa ijipange, ndiyo mmetuletea Mpango lakini je, utatekelezwa? Utatekelezeka?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge utulivu tafadhali, tumsikilize.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi naiomba Wizara, Wizara husika inayohusika na wanawake na kwanza niomba Serikali, nasikitika sana kwa sababu imefuta Wizara moja inayohusika na Wanawake Jinsia na Watoto. Nasikitika kwa sababu ni chombo ambacho kingeendelea kuwatetea wanawake, Wameunganisha na Wizara kubwa, kwa nini wanatuonea wanawake? Kweli naiomba Serikali mtufikirie wanawake inatumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tena juu ya utawala bora tunaona kabisa malalamiko na kutoridhishwa baadhi ya watu kwa mfano watu wa Zanzibar, tunaona kuna kilio kikubwa sana lakini bado tunaimba utawala bora. Naomba hilo tulifikirie Serikali. Tuifikirie na tuone ni namna gani tunawasikiliza hao watu. Jamani Rais aliyetakiwa kutangazwa atangazwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; asilimia kubwa ya wakulima ni wanawake na wanawake ndiyo wanaoshinda mashambani wanabebeshwa mizigo wakiwa na watoto wao, lakini ni wanawake hao hao wanaonyanyasika na Serikali haiwaangalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo wanazopatiwa ni feki, mfano Mkoa wa Njombe, safari hii wamepata *ridom*, dawa ile ya kupuliza ya ukungu ili viazi visipate ukungu, wamepata *ridom* feki ambayo imesababishia watu hawa kukosa mazao yanayotakiwa kama kipindi kingine wanavyovuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni hasara kwa hawa akinamama ningesema, maana akina mama ndiyo Taifa kubwa, ndiyo wanaolima sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pembejeo; Pembejeo zingine ni gharama sana kwa mfano, mbolea ya kupandia, watu wengi wanashindwa kupandia mbolea, wanapanda bila mbolea matokeo yake wanakuwa na mashamba makubwa, wanalima bila utaalum mwisho wa siku wanavunia kwenye kiganja. Halafu bado tunasema kwamba tunataka mapinduzi ya viwanda, tunataka kuwa na viwanda ambavyo vinategemea tena kilimo, sasa kilimo cha aina hii ni kweli tutaweza kutoka hapa tulipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi; tunaomba wanawake kwenye huu Mpango, ioneshe wazi kwamba wanawake na wenyewe wanaweza kuwa wasemaji au waingie kwenye mpango na vilevile washirikishwe katika maamuzi ya ardhi. Pia wawe wamiliki wa ardhi. Kwa nini ardhi wamiliki akinababa peke yao na sisi akinamama tuna haki. Haki sawa kwa binadamu wote. Kwa hiyo, naomba huu Mpango tujaribu kuangalia namna gani tunawaingiza akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara; tena akinamama ndiyo waathirika wa miundombinu mibovu, kwa sababu akinamama ndiyo wanaobeba ujauzito kwa miezi tisa, wanatakiwa kwenda hospitalini kupimwa, lakini mwisho wa siku kwa sababu barabara ni mbovu wanajifungulia njiani. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wabheja sana. Awali ya yote nakushukuru. Vile vile nakupongeza kama walivyosema, akinamama nanyi mnataka haki sawa, lakini waliimba hawa waimbaji, hata

wakati wa kutembea, akinamama mbele, akinababa nyuma. Kwa hiyo, bado tunawaenzi. Akinamama wa Tanzania endeeleni kufarijika kwamba Serikali inayosimamiwa na Chama cha Mapinduzi...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika! Mwongozo!

**MBUNGE FULANI:** Endelea Nchambi, mbona unakaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliyesimama naomba ukae. Huwezi kutoa mwongozo wakati kuna Mbunge anayeongea. Ni lazima amalize ndiyo unaomba mwongozo. Mheshimiwa Nchambi, endelea. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, usiyashangae haya, ukienda kusoma Biblia Luka 6:38 utayakuta. *(Kicheko/Makofi)*

Maana kile ambacho wanakipanda hapa, ndicho ambacho wataktivuna. Niliwaambia shemeji zangu wa Kigoma, namshukuru sana Mheshimiwa Zitto, huwa anatumia *knowledge* yake kuleta mambo ambayo yana mashiko kwa Watanzania; lakini shemeji zangu wengine wote hawajarudi humu ndani. *(Makofi)*

Niliwaambia Luka 6:38, kile mnachokipanda humu ndani, ndicho mtakuja kukivuna 2015 Oktoba. Kwa hiyo, wamektivuna na hawa wengine, wala usiwe na mashaka, maana katika safari ya mamba na kenge na mijusi wamo, wala usitie mashaka juu ya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho ambacho kimetokea hapa kabla ya kuanza michango yangu kwa Mheshimiwa Lwakatare. Amemaliza dakika zake zote, hakusemea Manispaa ya Bukoba. Mimi ni Mbunge wa Jimbo Kishapu, nimetokana na watu shapu, Wilaya yangu ni Shapu, mimi mwenyewe ni shapu. Naleta mambo yangu humu kwa ushapu kwa ajili ya wananchi wa Jimbo...

**MBUNGE FULANI:** Shapu! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Shapu! *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wabunge wengine humu wanasimama wanapoteza muda wao wanaongelea mambo ambayo hayahusu. Mheshimiwa Lwakatare amesema sana, lakini hajatetea wananchi wake. *(Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niwaeleze ndugu zangu Wabunge kidogo, kazi ambayo huanza juu kwenda chini, ni kazi ya kuchimba kaburi peke yake. Kaburi huanza kuchimbwa juu kwenda chini.

Kazi nyingine zote huanzia chini kwenda juu. Kwa hiyo, hata sisi hapa, kama Bunge ambalo Watanzania hawawezi kuenea humu ndani, wametutuma Wawakilishi wachache, tuje tuwasemee kuhusu mambo yanayohusu jamii na Taifa letu. Kwa hiyo, kazi tutakayoifanya hapa, ni ile wanayosema Wazungu a *journey of thousand miles starts with a single step to a thousand steps*. Tunaanza na hatua moja, mbili mpaka tunafika 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaobeza, lakini Mungu ameleta Mitume wengi sana, hakuleta Mtume au Nabii mmoja. Lazima, *we still keep on learning through history*. Mungu hakuleta Mtume mmoja, alileta mitume wengi na alikuwa na makusudi maalum. Nasi hapa Mabunge yatapita mengi, Wabunge watakwenda wengi, kwa sababu kazi za kibinadamu zinaendelea siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, nataka niwaambie, maneno machache sana; mpango huu umeletwa humu Bungeni, kwa mujibu wa kanuni ya Kibunge ya kwetu ya 94; lakini yapo mambo yaliyosemwa hapa ni kwamba siyo sahihi jambo hili kuletwa kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe, ukisoma kitabu chetu cha Sheria za Bajeti, 2015, Kifungu cha 20 naomba ninukuu: "*The Minister responsible for planning commission shall prepare and lay before the National Assembly and the National Development Plan which shall be the basis for the preparation of the National Budget.*" Kifungu hiki kinapelekea maandalizi katika sheria yetu ya 2015 ya kitabu chetu cha bajeti Kifungu na 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuwekane sawa. Hapa hatukuja kutekeleza jambo, tumekuja kuandaa Mpango. Waheshimiwa Wabunge tusimamame hapa kwa Utaifa wetu, tusimame hapa kwa vitabu vyetu vya kikanuni, sheria na kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Hata dini, ninaposimama mimi Muislam nasoma the *Holy Quran* nina-refer; Wakristo wanasoma Biblia na kwa sisi wengine tunaamini Taurati na Injili. Hivi vitabu tuvipitie sana. Tuko kwa ajili ya Watanzania walio wengi nje, tuko kwa ajili ya Utaifa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu Na. 26, ni lazima tuliweke jambo hili sawa ili Watanzania walioko nje wasione tu tunawaburuza, tunakwenda hatua kwa hatua. Naomba ninukuu:

*"The National Assembly shall on or before 30th June each year and after debating the National Assembly, approve the Annually National Budget of the Government for the next financial year, by the way of open vote and call of the name of each Member of Parliament."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa mmoja baada ya mwingine katika Mpango. Hapa sisi tunatoa mapendekezo ya mpango. Nawaomba sana, wote tunatoka katika Majimbo hata wenzetu wa Viti Maalum, Majimbo yanaunganishwa, yanaletwa. Ni imani yangu, Chama changu, Chama cha CHADEMA na wengine, wanawaleta Viti Maalum pia ambao wanajua watasaidia wananchi wote na hasa akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nielekeze sasa michango yangu kwenye maeneo, kama ilivyo kawaida ya Mbunge *sharp*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote haiwezi kupiga hatua, ni lazima iwe na mipango ya kiuchumi, tena mipango na mikakati mathubuti. Katika maeneo ya mipango ambayo itatekeleza uchumi, maana suala lote hapa, wanasema Mheshimiwa Magufuli ameahidi wanafunzi bure; tunataka watu watibiwe bure, fedha zitatoka wapi?

Mheshimiwa Magufuli amekuwa mstari wa mbele kutaka kuibadilisha Tanzania hii iende katika uchumi wa kati. Mambo yafuatayo ningeomba sana Waheshiwa Wabunge tuyasemee sana. Jambo la kwanza ambalo Mungu ametujalia Watanzania ni rasilimali watu. Tuna rasilimali watu, tena Watanzania wenye nguvu na sifa ya kuchapa kazi.

Jambo la pili ambalo nikiukumbuka sana Mheshimiwa Muhongo alikuwa akipigwa madongo sana siku za nyuma; leo sote mashahidi, Wabunge tunapishana Ofisi za REA na maeneo mengine kuomba umeme na mambo mengine ambayo yatasaidia kututoa sisi katika uchumi wetu huu wa kimasikini kutupeleka katika uchumi wa kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ulinzi ni suala muhimu sana. Lazima mtu yeyote anapotaka kuwekeza awe ana uhakika, yuko salama, ana imani anapowekeza mambo yake yatakwenda vizuri. Ujenzi wa barabara zetu; wakulima wetu wanapolima wanasafirishaje? Katika gharama zipi? Ujenzi wa reli; eneo hili ni muhimu sana ndugu zangu naomba niwaambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako mimi nimekuwa dereva wa *bus*; kwanza nimekuwa mpiga debe *stand*, nimebeba abiria mgongoni, nimekuwa dereva wa *bus*, nimekuwa dereva wa malori; najua gharama za kusafirisha mizigo; na sasa ni mwekezaji, tena mfanyabiashara mzuri tu, wala sina matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuendelea katika nchi yetu, lazima tuwekeze katika miundombinu. Moja, reli itatusaidia sana. Lazima reli yetu iboreshwe katika level ya *standard gauge*, wananchi wetu wasafiri *on and off*.

Unaweza ukatoka Kigoma kwa shemeji zangu kule *amagambo bukebuke* wakaja Dar es Salaam, asubuhi akanunua bidhaa akarudi. Mambo ni meeza, sivyo shemeji zangu, Mheshimiwa Zitto! Mambo yamekwenda! Wale wa Mwanza unaweza ukatoka jioni Mwanza ukaenda Dar es Salaam na ukarudi kesho, bila kulala *guest*. Ie fedha itasaidia kusomesha watoto na kuanzisha ujenzi wa nyumba zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba katika mipango yetu, Waheshimiwa Wabunge tuungane, tuhakikishe tunapata reli ili kupunguza gharama za maisha ya Watanzania; lakini tusafirisha bidhaa zetu kwa urahisi. Atakayelima matunda leo; nenda *South Africa* ukaangalie reli walivyojenga; nenda Uingereza uone mambo yalivyokwenda. Mwalimu wangu hapa Mheshimiwa Ndassa, anajua. Mimi leo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa!

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, wabheja wabheja, naunga mkono hoja. Kwa pamoja naomba... *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo nami niweze kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ndiye anayeniwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kuwashukuru wananchi wa Kalambo, tulikubaliana kwamba nuru mpya ya Kalambo, kwa pamoja tunaweza; na hakika wamenirejesha kwa kishindo, nawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ulioletwa unaleta matumaini makubwa sana. Tanzania ya viwanda inawezekana. Viwanda vipi ambavyo tunaenda kuvijenga? Ni hakika Serikali lazima ijenge viwanda vya kimkakati lakini, ni wajibu wa sekta binafsi kushiriki katika viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotaka kujenga kiwanda maana yake ni lazima rasilimali fedha iwepo ya kutosha. Bila mtaji wa kutosha hakuna viwanda ambavyo tunaweza kujenga. Serikali ikijenga viwanda vya kimkakati, tukaiachia Sekta binafsi, wanaenda kutoa pesa wapi Hawawezi kwenda kukopa katika mabanki ya kibiashara, kwa sababu unapowekeza katika kiwanda hutarajii *return* ya haraka. Lazima ni mtaji mkubwa ambao *return* yake utaipata kidogo kidogo.?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, haiwezekani tuka-*plan* kwenda kushindwa. Tunapokuwa na Benki ambayo hatujaipa mtaji, kwa maana ya *TIB*, hakika ni kwamba tume-*plan* kwenda kushindwa. Tusikubali kufanya kosa hili, tuhakikishe tunaiwezesha Benki yetu ya *TIB* ili itoe fursa kwa wananchi kwenda kukopa kwa riba ambayo ni rahisi kulipika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashuhuda kwamba asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima na hasa ambao wako vijijini. Sitafarijika hata kidogo na wala sitaki kuamini kwamba Serikali imesahau mpango mzima wa *SAGCOT*. Tumesema lazima tuwekeze katika kilimo, ikaja mipango mizuri, naamini na hili litakuja; ni kwa sababu inawezekana bado wanakumbuka, ikija *detail report* itaainisha masuala yote ya kuhakikisha kwamba tunajitosheleza katika kilimo na tena kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, kwa utaratibu wake na Mpango waliokuja nao wa kuhakikisha kwamba tunaenda kubana matumizi, kutumia pale tu ambapo itaongeza tija. Ni jambo jema. Serikali imeagiza kwamba kuanzia sasa pesa zake zote ambazo Taasisi zimekuwa zikiweka katika Benki za kibiashara, zipelekwe Benki Kuu maana zote ni mali ya Derikali. Sina ubishi! Ubishi wangu unakuja pale ambapo kama utaratibu tutakaoenda kuufanya utasababisha mashirika yetu ambayo yashaanza kufanya vizuri, tukaya-*suffocate*. Haitapendeza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la *control*, naomba niikumbushe Serikali irejee Sheria ya Bajeti Kifungu cha 17, inaeleza kabisa kazi ya *Treasury Registrar* kwamba mashirika yote ambayo yako chini ya *TR* watapeleka bajeti zao kule, ataidhinisha na hata kama kuna suala la kwenda kuwekeza, ni lazima wawe wamepata idhini kutoka kwake. Hiyo ni *control* ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile ambavyo wananchi na Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tunapata wasiwasi, ni kwamba utaratibu wa kuhamisha pesa zote kupeleka Benki Kuu, inaweza kuziua Halmashauri zetu. Hakika pia inaweza ikaua mashirika yetu. Sisi ni mashahidi kwamba mwaka 2015 tulivyokuja hapa tulisema kwamba ni vizuri Taasisi zetu zikawezeshwa ikiwa ni pamoja na *TPDC* ili iweze kushiriki katika uchumi wa gesi na mafuta. Sasa kama utaratibu itakuwa hatuwezeshi wakawa na fungu la kutosha, wakaweza kuwekeza, hakika ushiriki wa Watanzania kwa kupitia shirika letu hautaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nyie ndugu zangu nyote ni mashahidi kwa jinsi ambavyo Shirika letu la Nyumba la Taifa lilivyokuwa na hali mbovu, leo hii limekuwa ni miongini mwa mashirika machache ambayo yanapigiwa mfano kwa namna ambavyo wanawekeza na naamini na Kalambo watakuja. Sasa zile taratibu kwa wale watu wanaofanya kazi vizuri tusianze kuwa-*frustrate*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesoma katika Mpango kuna suala zima la kununua ndege. Ni jambo jema sana, lakini haitapendeza tunaposema tunataka kufufua Shirika letu la Ndege, zinanunuliwa ndege mbili, lakini kwa utaratibu ambao utakuwa umewekwa kwa makusudi, wakashindwa hata kununua mafuta kwa sababu OC haijawafikia. Itakuwa hatutendi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala zima la Wakandarasi wa ndani. Wakandarasi wa ndani wamekuwa wakiidai Serikali kwa muda mrefu. Kutowalipa Wakandarasi tafsiri yake ni nini? Barabara zetu hazijengwi zikakamilika kwa kiwango kwa wakati unaotakiwa. Tafsiri yake ni kwamba, miradi mingi inajengwa kwa gharama kubwa, kwa sababu kwa kutowalipa, wanalazimika kuidai Serikali riba, lakini hali kadhalika wanashindwa kulipa kodi kwa sababu wao wanaidai Serikali na Serikali haijalipa. Nasi tunataka kuwe na mzunguko wa kutosha; walipwe na Serikali, walipe kodi, lakini pia waweze kutoa ajira kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee, Serikali ihakikishe kwamba miradi ile ya barabara ambayo imeshaanza, ikiwa ni pamoja na mradi wa barabara kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda; Mradi wa barabara kutoka Sumbawanga kwenda Kalambo *Port*, unakamilika kwa wakati ili tuhakikishe kwamba kasi ya Tanzania ya kwenda kuwa nchi ya kipato cha uchumi wa kati, inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tukubaliane, kupanga ni kuchagua. Haiwezekani tukatekeleza yote, ndiyo maana tukubaliane kwamba bila kujenga reli kwa *standard gauge*, hakika uchumi ambao tunataka upae na kufika uchumi wa kipato cha kati hatutaweza. Niwasihi ndugu zangu wote bila kujali unatoka eneo gani la Tanzania, tukubaliane mkakati wa kuhakikisha kwamba reli inajengwa. Bahati nzuri nyie ni mashahidi, kuna fungu ambalo lilitengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwekeza lazima utarajie kupata kule ulikowekeza. Tujiulize, kutokana na bomba la gesi, ni kiasi gani kinapatikana kama *return* kwa Serikali na hicho ambacho kinapatikana kipo kwenye mfuko upi? Kama siyo hapo tu, mkongo wa Taifa, pesa nyingi sana imewekwa, tunataka tujue, baada ya kuwekeza *return* yake iko wapi? Iko mfuko upi kwa manufa ya Watanzania? (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa jioni hii kuchangia. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kusimama ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wapigakura wa Mkoa wa Pwani kwa kukiwezesha Chama chetu kushinda Majimbo yote ya Mkoa wa Pwani, iliyopelekea kutuingiza Wabunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Awamu ya Tano pamoja na Baraza lake la Mawaziri. Naona ameanza kazi vizuri na anasema Serikali yake siyo Serikali iliyochoka; Serikali makini ambayo inakusanya trilioni 1.4; Serikali ambayo inatumbua majibu kadiri inavyoweza; Serikali ambayo imechaguliwa na watu takriban milioni nane; Serikali ambayo ndani ya Bunge hili ina 74% ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hiyo haijachoka na Chama hicho kinaaminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye Mwelekeo wa Mpango 2016/2017. Wakati najielekeza, naomba ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge hili, ukurasa wa 22 aliposema: "Tunataka tuwatue akina mama ndoo kichwani. Tunatambua umasikini hauwezi kuondoka nchini kama wananchi hawapati maji safi na salama."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mwelekeo wa Mpango 2016/2017 kwa kuwa umejielekeza kwenye miradi ya maji; Mradi wa Maji wa Ruvu Juu, Mradi wa Maji wa Ruvu Chini, Mradi wa Maji wa Chalinze, Mradi wa Maji wa Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono nikiwa na matumaini kwamba miradi hii itakapokamilika; Mradi wa Maji wa Ruvu Juu umekamilika kwa 97%, nina imani maeneo ya Bagamoyo, Kibaha, Mlandizi, Kisarawe na Mkuranga yanaenda kupatiwa maji kutokana na kukamilika kwa miradi hii ambayo nimeitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mwelekeo wa Mpango huu wa 2016/2017 kwa sababu, suala la elimu; na naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako kwa kuanza mpango wa utoaji wa elimu bure. Natambua wapo baadhi ya Wapigakura wangu wa Mkoa wa Pwani walikuwa wanashindwa kulipa ada ya mitihani ya Baraza la Mitihani; walikuwa wanashindwa kulipa ada ya Sh. 20,000/= mpaka Sh. 70,000/= kwa Shule za Sekondari; walikuwa wanashindwa kugharamia baadhi ya gharama ambazo Serikali imezibeba kupitia *capitation*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema mwanzo wa safari ni moja. Tumeanza vizuri. Naipongeza Serikali, lakini natambua Serikali ipo sasa, inaangalia changamoto zilizojitokeza baada ya kuanza awamu hii ya elimu bure. Naiomba Serikali iangalie sana kwenye baadhi ya maeneo, hasa suala zima la uandaaji wa mitihani, suala zima la gharama, umeme, mlinzi katika shule zetu; nina imani mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika suala hili la elimu, natambua Serikali ya Awamu ya Nne kupitia Bunge hili, tulipitisha Sheria ya Kuanzisha Tume ya Walimu. Naiomba Serikali ya Awamu ya Tano iharakishe uandaaji wa Kanuni ili hii Tume iweze kuwatendea haki Walimu, mishahara yao, kupanda kwa madaraja, lakini pia Serikali iendeele na mpango wa kuzipa Halmashauri zetu kila mwaka milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu na ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

Vile vile Serikali ikiangalie sana Kitengo cha Ukaguzi wa Elimu. Kitengo hiki mara nyingi hakitengewi fedha na tunakitegemea sana katika kukagua ubora wa elimu. Kwa hiyo, hayo yakifanyika, ninaamini utoaji wa elimu bure utaenda sambamba na elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pia umejielekeza kwenye afya vijijini. Kama ambavyo Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilivyoahidi, kila Mkoa kuwa na Hospitali ya Rufaa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati, naomba Serikali itakapokuja na Mpango ujieleze kinagaubaga, awamu hii itaongeza zahanati ngapi katika vijiji vyetu? Itaongeza Vituo vya Afya vingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali hii ijielekeze zaidi kwa watoa huduma kwenye Zahanati hizo na Vituo vya Afya. Yapo maeneo katika Mkoa wetu wa Pwani, hasa maeneo kwenye Jimbo la Kibiti, Kiongoroni, Kiechuu, Maparoni; maeneo haya ni maeneo pekee ambayo yanahitaji uangalizi maalum, kwani zipo Zahanati mpaka sasa hazina watoa huduma, hazina Madaktari wala nyumba. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie maeneo yale maalum hasa yale yanayozungukwa na maji, ikiwemo Wilaya ya Rufiji, hususan Jimbo la Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Sera za Serikali za kubana matumizi na katika Sera za Mapato. Hapa najielekeza kwenye utaratibu wa *retention*. Naipongeza Serikali kwa kuamua ku-*retain* fedha zake na Sheria ya Fedha (*Public Finance Act*) ya mwaka 2001, ilisema kinagaubaga, fedha zote zitaingia kwenye Mfuko Mkuu (*Consolidated Fund*).

Kwa hiyo, hapa nampongeza Dkt. Mpango kwa kuja na hili suala kwamba yapo mashirika ya *EWURA*, *TICRA*, walikuwa na pesa nyingi zaidi. Yapo mashirika, hata hizi tunazosema zinasimamia mbuga zetu, lakini tulijionea Taasisi ya Ngorongoro, *TANAPA*; kuna wakati fedha zilitumika kwa kulingana, siyo na bajeti, lakini matakwa ya viongozi wa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini fedha hizi zikikusanywa kwenye Mfuko Mkuu, lakini naiomba Serikali ijielekeze kuuondoa urasimu. Hazina mjipange kupunguza urasimu na kuzileta pesa hizi kwa mashirika haya kwa wakati uliokusudiwa. Ila ombi langu, Halmashauri zetu tuendeleo kukusanya kwa sababu tunayo Mabaraza ya Madiwani yatasimamia, tutafuata Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Halmashauri, tukusanye na tuweze kufanya maendeleo ambayo yanakusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, najielekeza kwenye suala la kilimo. Tulikuwa na utaratibu wa Kilimo Kwanza, lakini pia tulikuwa na utaratibu wa *SAGCOT*; vile vile kipindi cha *BRN* kuna baadhi ya maeneo yalichaguliwa kuongeza uzalishaji wa sukari, mpunga na mahindi. Nina imani kabisa, kupitia Mpango huu, naomba kipaumbele pia kiwekwe kwenye kilimo na mipango iliyowekwa hii, *BRN*, bado ina nafasi ya kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo ambayo yalitengwa, kwa mfano Wilaya ya Bagamoyo lilitengwa eneo, watu wapo *ECHO Energy*, wanataka kufanya kazi kwa haraka, tuzalishe sukari nyingi tupunguze pesa tunazozitumia kwa ajili ya uagizaji wa sukari zifanye shughuli ambazo ni za kutoa huduma ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika ujenzi wa viwanda; Wilaya ya Kisarawe tumetenga eneo la viwanda. Tunalo, tunategemea miundombinu ya maji na miundombinu ya umeme ili eneo lile wadau mbalimbali wanaojitokeza waweze kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nina imani sana na Serikali. Serikali inaweza! Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ina uthubutu. Serikali hii, amani ipo. Waliokuwa na nia ya kuvuruga amani ni waliokwenda kwenye Vituo vya *Television* na kujitangazia ushindi wamepata kura milioni kumi; hawana fomu za matokeo na walikuwa na Mawakala nchi nzima, wanajitangazia kura wakiwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliokuwa *site*, tuna uhakika, kura tulizihesabu vituoni, tunajua Wagombea Urais walipata kura ngapi, hakukuwa na utata. Matokeo yaliyotangazwa, Rais Dkt. John Pombe Magufuli alishinda, hatukuwaona mlete ushahidi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani Serikali haijachoka, itafanya kazi. Hata hivi karibuni Serikali kupitia utaratibu wa utumbuaji wa majibu, napongeza ilivyotumbua jipu la Hati Fungani. Vipo Vyama vinajidai vinapinga ufasidi, lakini hatukuwaona kwenye majukwaa wakisema kupinga ufasidi. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alijipambanua, alitoa ahadi kwamba yeye atapambana na ufasidi. Wengine hatukuwasikieni! Mlisemea wapi? Leo mkija ndani ya Bunge, mnasema ninyi ndiyo mnapambana na ufasidi, lakini naomba mtoe boriti zilizopo kwenye macho yenu kisha mtazame Vyama vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, napongeza na Bunge hili, wananchi wa Tanzania msibabaishwe na miongozo na kanuni, zimejaa Kanuni nyingi; lakini ukiangalia hata Taarifa yao hiyo waliyoandaa, Mpango huu umeandaliwa kwenye karatasi mbili tu. Zote hizi wameandaa maoni ya Mpango wa Miaka Mitano ambao haujadiliwi sasa! Maoni ya Mpango huu ni kurasa mbili tu. Kuonekana, mmesituka! Hongereni Watanzania. Ahsanteni sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii na kwa sababu nasema kwa mara ya kwanza, nawashukuru sana wananchi wangu wa Songea Mjini kwa ushindi mkubwa walionipatia. Ninachotaka kuwahakikishia ni kwamba, nimekuja kama Mwakilishi wao na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikupata bahati ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini labda nianze na hilo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa 20, pamoja na hotuba nzuri sana aliyotoa, lakini ukurasa wa 20 alikuwa amezungumzia kero kwa wananchi, hasa wafanyabiashara ndogo ndogo kuhusiana na ushuru wanaotoa. Naungana na Mheshimiwa Rais na kwa kweli naomba wenzetu wafanye utaratibu wa kuhakikisha ushuru huu unafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue, kwa sababu ninachokumbuka, ni miaka ya nyuma hivi karibuni walifuta ushuru wa kero kwa wananchi wote kwa maana ya kwamba ushuru uliokuwa unakusanywa kwa njia ya kero ulifutwa na Serikali ilikuwa inatoa ruzuku kwenye Halmashauri za Wilaya ili kufidia ushuru huo wa kero. Sasa sielewi ule ushuru wa kero umeishia wapi. Kwa nini Halmashauri zetu zimeingia tena kuwa-charge wafanyabiashara ndogo ndogo wa mchicha, vitumbua, Mama Ntilie ambapo sasa imekuwa ni kero kubwa mno! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja hapa, inachekesha kweli! Ukiangalia leseni za biashara zinazotoa Sh. 70,000/= kwa mwaka, ukalinganisha na ushuru wanaotoa akinamama Ntilie, unakuta Mama Ntilie

anagharamia gharama kubwa zaidi kuliko mtu anayelipa ushuru wa Sh. 70,000/=. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu za haraka haraka, ni kwamba anayelipa leseni ya Sh. 70,000/= maana yake ukigawanya kwa miezi 12 na ukagawanya kwa siku 30 maana yake mfanyabiashara huyu wa duka au wa mgahawa analipa kwa siku Sh. 194/=. Wakati huyu Mama Ntilie anayelipa Sh. 400/= kama ushuru, ukifanya hesabu za siku maana yake unamkuta analipa ushuru kwa mwaka 144,000/= akimzidi mfanyabiashara wa kawaida wa duka au mgahawa.

Kwa hiyo, ni kitu kinachoshangaza sana. Ni vizuri tukiangalie vizuri; na kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Rais, nadhani umefika wakati sasa tuwafutie ushuru huu ili wananchi wafanye biashara zao vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango, kwanza nami naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi nzuri aliyoifanya. Mpango huu umezungumzia sana mahusiano ya kibiashara, ya kiuchumi kati ya Tanzania na nchi jirani, lakini katika Mpango ule umezungumzia sana mipaka ya Kenya, mipaka ya Uganda na mipaka ya nchi nyingine. Haujazungumzia kabisa mpaka wa Kusini mwa Tanzania, Mkoa wa Ruvuma ukihusika na hasa kwa nchi ya Msumbiji na nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mpango huu utambue kuwapo kwa barabara inayounganisha Tanzania na Msumbiji, kupitia Songea Mjini kwenye eneo la Likuyufusi kwenda kwenye eneo la Mkenda, Kaskazini ya Msumbiji. Barabara hii haijaingizwa na wala haijazungumzwa. Ni vizuri iingizwe na izungumzwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile upanuzi wa uwanja wa ndege wa Songea Mjini ambao ungeweza kusaidia sana suala la wafanyabiashara na wananchi kutoka nchi jirani wanaopenda kutembelea Tanzania, hasa kutoka Msumbiji na Malawi, kuweza kutumia ndege zitakazotoka Songea kwenda Dar es Salaam kufanya shughuli mbalimbali za kibiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vilevile kwa kazi nzuri ya Serikali inayofanywa hasa ya kutengeneza barabara ya kutoka Mtwara kwenda Mbambabay. Barabara hii bado kuna maeneo mawili haijakamilika na wala haijashughulikiwa. Ukitoka Namtumbo kwenda Tunduru kuna Makandarasi wanashughulikia, lakini kati ya Luhira na Ruhuiko, Mjini Songea, wananchi wamewekewa 'X,' wamefanyiwa tathmini, lakini mpaka sasa hawajalipwa fidia zao na kwa hiyo, wanaishi katika maisha ya kutokuwa na uhakika watahama lini. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye utaratibu wa haraka ili watu wanaostahili kulipwa fidia katika eneo hilo waweze kulipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bado kuna kipande kimoja hakijajengwa kati ya Mbinga na Mbambabay. Naomba Serikali ione namna ya kufanya katika hiyo sehemu ili kuhakikisha inatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna mwenzetu mmoja amezungumza habari ya reli; nashukuru kwa mpango kabambe wa Serikali wa kujenga reli ya kati kwa kiwango cha *Standard gauge*, lakini vilevile kwa mpango kabambe ambao upo katika Kitabu chetu cha Mwelekeo wa Uchumi kuhusu barabara ya Mtwara – Mbambabay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi, Serikali ione namna ya kufanya utaratibu wa kuhakikisha reli hii inajengwa ili kuweza kuimarisha uchumi katika Mikoa ya Kusini, hasa kutokea kule Mbambabay. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine. Kwa muda mrefu sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Songea kwa ujumla tumekuwa tukiahidiwa kupatiwa umeme wa *Grid* ya Taifa kutoka Makambako kuja Songea, lakini sasa kila mwaka linazungumzwa hili suala, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye utaratibu na itupe uhakika hili suala la umeme kati ya Makambako na Songea litakamilika lini na kwa hiyo, lini utanza utekelezaji wa suala hilo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, naomba nizungumzie juu ya suala la EPZA. Katika Taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, amezungumzia EPZA katika maeneo mengi sana, lakini Jimboni kwangu Songea kuna wananchi katika maeneo ya Mwenge Mshindo, Luhila Kati, Kilagano, Ruawasi na Ruhuiko, hawa watu wamechukuliwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa ni zaidi ya 2,200 na wamechukuliwa ekari zaidi ya 5,000 kwa ajili ya kuweka EPZA, lakini nasikitika kwamba mpaka sasa watu waliolipwa ni wachache sana, hata kiwango cha fedha walicholipwa ni mwaka 2008. Wamelipa 2015, kiwango kile hakilingani na hali halisi ya sasa na vilevile wanatakiwa kuhama kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inasababisha kero kwa wananchi wangu na vilevile kuhakikisha kuendeleza umaskini, kwa sababu hawawezi kujiendeleza kiuchumi, hawawezi kujenga nyumba, lakini hawana mahali pa kwenda palipoandaliwa na Serikali na pesa waliyopata haiwawezeshi kuweza kwenda kuweka makazi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kutumia nafasi hii naiomba sana Serikali, hebu imalize tatizo hili la wananchi hao niliowataja katika eneo la Mwenge Mshindo ili tuweze kupata maendeleo, wananchi waweze kujiendeleza wakiwa na uhakika wanakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii niseme, kwa jinsi taarifa ilivyoandaliwa na kama tutazingatia haya ambayo tumeyaomba Waheshimiwa Wabunge, basi nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo.

Awali ya yote, napenda sana kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kalenga kwa nafasi ambayo wamenipa kuweza kuliwakilisha Jimbo langu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine tena, mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa Miaka mitano tunaenda kuchangia kwa kipindi cha mwaka mmoja ujao, ningependa kuchangia mambo kadhaa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kujikita kwenye masuala mazima ya ujenzi wa reli. Suala la Reli ya Kati ni suala la muhimu na kwa namna yeyote ile, uchumi wetu wa viwanda ambao tunaenda kuufanya katika kipindi hiki, lazima utegemee mawasiliano ya reli na biashara zake kwa ujumla.

Kwa hiyo, ni lazima tuangalie ni namna gani reli hii tunaweza tukaijenga na Serikali iseme kinagaubaga kwamba ni maeneo gani ambapo reli hii itaenda kujengwa ili tutakapokuja katika Mpango unaofuata tuweze kujua kiuhalisia kwamba Serikali ilifanya nini na imefanya wapi. Tunajua reli ya kati inapita katika mikoa gani, lakini tunaomba katika yale maeneo ya michepuko, basi tujue wazi Serikali inaongea maeneo gani katika uwakilishaji wa reli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa sana kuzungumza ni kwamba katika masuala haya, hasa katika viwanda tunavyovizungumzia, masuala ya viwanda yanaendana moja kwa moja na masuala ya umeme na upatikanaji wa elimu bora. Hatuwezi tukazungumzia masuala ya upatikanaji wa viwanda kama elimu yetu ni duni.

Vile vile hatuwezi tukazungumzia masuala ya viwanda kama masuala mazima ya nishati ya umeme bado haijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda sana kuanza kuwashukuru na kuishukuru Serikali na Mheshimiwa Mhongo kwa kazi nzuri wanayoifanya, wametuonesha njia, hata kule vijijini umeme sasa hivi unawaka. Mheshimiwa Mhongo nakushukuru sana, katika vijiji vyangu 84, leo hii tunazungumza vijiji kama 50 hivi ambavyo vimeshapata umeme. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wao! *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Kwa hiyo, nakushukuru na naomba Mheshimiwa Muhongo na Wizara yako tuweze kufanya namna, tuweze kufika katika Jimbo langu, wananchi bado wanahitaji umeme. Ninaamini Mheshimiwa Muhongo na Serikali kwa ujumla na Wizara tutafanya kila namna tuweze kuhakikisha kwamba vijiji vilivyobaki vinapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa upatikanaji wa umeme katika vijiji hivi ndiyo itatoa dira nzuri ya namna gani tunavyoweza kusonga mbele katika masuala haya ya ukuaji wa viwanda. Tunavyoongelea masuala ya viwanda, ni muhimu sana kujua kwamba ikiwa kama gesi ambayo tayari tumeshaivumbua huko Mtwara tutaitumia vizuri na itakwenda kuwakilishwa au kwenda kutumika ipasavyo katika maeneo yetu, ina maana kwamba upatikanaji wa viwanda utakuwa ni mwepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika kupatikanaji wa viwanda, ni lazima tujue Serikali ina malengo gani au inalenga viwanda vya namna gani? Ni viwanda vya namna gani ambavyo Serikali inakwenda kuvijenga? Siyo tuamke asubuhi na kusema tunaenda kujenga kila aina ya Kiwanda, hatutaweza. Nchi yetu bado ni changa, tunahitaji tuweze kupata mchanganuo ni namna gani au Serikali imejipanga vipi katika ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashauri kwamba katika upande wa kilimo, kuna maeneo mbalimbali hasa ukiangalia maeneo ya nyanda za juu Kusini, tunalima sana mahindi na maharage, lakini bado hatuna viwanda ambavyo vinaweza kusaidia kuchakata haya mambo na kuhakikisha kwamba tunapata mazao na masoko bora katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tukitaka kuangalia, Mkoa wa Iringa kipindi cha nyuma kulikuwa na Shirika la NMC; Shirika hili limekufa na hatujui litafufuka lini. Nina imani kubwa sana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi; na naamini kabisa Serikali ya Mheshimiwa Magufuli itakwenda kufufua viwanda hivi na kile kiwanda cha NMC ambacho kipo pale Iringa kitaenda kufufuliwa tuweze kupata nafaka kwa sababu kilikuwa kinainua uchumi katika Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuangalia katika maeneo mengine ya namna gani tunaweza tukakuza uchumi wa nchi yetu; nchi yetu bado ina matatizo makubwa sana katika upatikanaji wa mapato, nami lazima niongelee suala hili kwa sababu Bunge la Kumi lililopita, nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya Bajeti. Tulijaribu kugusa maeneo mbalimbali kuona kama tunaweza tukafanikiwa vipi katika maeneo ambayo tunaweza tukapata vyanzo mbalimbali vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo Serikali bado inasuasua. Kuna maeneo ya uvuvi wa Bahari Kuu. Uvuvi wa bahari kuu ni uvuvi ambao Tanzania bado tupo nyuma na nchi za kigeni, wageni wanaendelea kuhakikisha kwamba wanaifilisi nchi yetu katika uvuvi wa bahari kuu. Lazima tuamke tuweze kuona kwamba uvuvi wa bahari kuu tunaufanyia kazi na Serikali inaingiza nguvu zake za kutosha ili kuhakikisha kwamba mapato yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania leo hii tuna *loss* ya zaidi ya Shilingi trioni moja kwa kutojiingiza kwenye uvuvi wa bahari kuu. Kuna wageni *(foreigners)* wengi ambao wanaenda kule kuhakikisha kwamba wanapata samaki, lakini vilevile tukiangalia soko la samaki katika bei ya dunia, liko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uvuvi wa samaki wanaoitwa Tuna, ambao leo hii samaki hao kwa kilo moja inanza Dola 10 mpaka Dola 50, lakini bado nchi yetu ya Tanzania hatujajikita huko kuhakikisha kwamba tunapata mapato ya kutosha. Leo hii bado tunaendelea kuwadidimiza wafanyabiashara ndogo ndogo ambao bado mitaji yao ni midogo. Ni lazima tuangalie maeneo makubwa kama haya ili kuhakikisha kwamba tunapata uchumi ambao ni endelevu na uchumi wetu binafsi, tukaachana na uchumi ule wa kuendelea kukopa nje wakati tunavyo vyanzo vyetu wenyewe katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningalie pia suala la utalii; nyanda za juu kusini tumeachwa sana. Najua kabisa kuna mambo mengi yanaendelea Kaskazini, nchi yetu ni moja lakini lazima Serikali iweze kuangalia maeneo ambayo tunaweza kupata vyanzo vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa tuna Mbunga ya Ruaha. Mkoa wa Iringa bado tunaendelea katika utaratibu wa kukuza viwanja vyetu vya ndege. Mheshimiwa Rais alivyokuja alituambia watu wa Iringa kwamba atahakikisha *Airport* yetu ya Mkoa wa Iringa inafufuliwa na inaendelea kuleta watalii katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga yetu ya Ruaha ambayo inapita kwa Mheshimiwa Lukuvi, inapita kwenye Jimbo langu, bado mapato hatupati, jambo ambalo ni la ajabu na kusikitisha. *(Makofi)*

Vile vile upande wa kusini niliongea juzi, nikasema kuna Mbuga la *Selous* ambayo bado nayo tukiamua kuitumia vizuri kwa miundombinu yetu tuliyonayo tunaweza kupata fedha nyingi za kigeni na kuhakikisha kwamba tunasonga mbele kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuisihi Serikali, kuhakikisha kwamba tunafanya kila njia kuweza kuangalia nyanda za juu kusini na maliasili zake kuhakikisha kwamba tunasonga mbele na tunapata hizi fedha ambazo Tanzania bado haijazipata ili kuhakikisha uchumi wetu unasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo kama sitazungumzia masuala ya maji. Jimbo langu la Kalenga lina matatizo makubwa sana ya maji.

Nimeongea na Mheshimiwa Waziri, tukakubaliana kwamba tuongee kuhusu masuala ya maji na naendelea kukuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji. Naomba miradi mitano ya maji ambayo haijakamilika katika Jimbo langu, ikamilike, tuokoe akina mama! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji bado ni kubwa! Wakandarasi hawajalipwa! Naomba fedha ambazo wanadai watu hawa ziweze kulipwa mapema ili bajeti inayokuja tusiweze tena kufika hapa, tukaanza kubishana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana fedha zifike Halmashauri, Wakandarasi walipwe, waendeleo kufanya kazi, miradi ikamilike, wananchi wapate faida na waendeleo kuwa na matumaini na Chama chetu na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuendelea lakini, napenda sana kurudia kwamba suala hili la maji ni la muhimu. Tuhakikishe kwamba Wizara ya Maji inawezeshwa, inapata fedha na inafika vijijini kuhakikisha kwamba maji yanaweza kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa, ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunijalia tena kwa mara nyingine kuwepo katika Bunge hili. Pia nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Musoma kwa kuweza kunipa ridhaa hii kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nijielekeze moja kwa moja katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2016/2017. Kazi yetu ni kuishauri Serikali. Wakati najaribu kupitia Mpango huu kwenye ule ukurasa wa 24, umesema wazi kwamba malengo mahususi ni kuimarisha kasi ya ukuaji na kuongeza uchumi. Hii ni pamoja na uchumi huo uweze kuwanufaisha wananchi waliyo wengi, pamoja na kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango. Kusema kweli amepanga mipango yake vizuri. Ukisoma kwenye huu ukurasa wa 24 mpaka 26 na kuendelea mbele, mipango iliyopangwa ni mizuri sana. Wenzetu wamekuwa wakitubeza kwamba sisi ni wazuri kwa kupanga mipango, lakini tuna tatizo la utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia Mpango na kusoma ukurasa wa 37, kwamba mojawapo ya mikakati ya kutekeleza mipango hii ni pamoja na kuwa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa maana ya *Public, Private Partnership*. Mashaka yangu yawezekana pamoja na mipango yetu mizuri, lakini bado tukakwama kwa sababu ya ukwasi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka tu kushauri au kuchangia katika maeneo manne, nilitaka kuchangia katika eneo la viwanda, kilimo, uvuvi pamoja na mifugo kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuendeleza viwanda, maana Mpango huu mlisema umebainisha namna ambavyo hivi viwanda vinavyotakiwa kwa maana ya vile viwanda vitakavyosaidia kuajiri watu wengi zaidi. Kwa upande wa viwanda, kama tunahitaji kuona Matokeo Makubwa ya Sasa, nashauri tujielekeze kwenye vitu vitatu; kwanza, tuendeleo kupanua hivi Vyuo vyetu vya VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Musoma kipo Chuo cha VETA kimoja ambacho kinachukua wanafunzi kila mwaka wasiozidi 200, sasa ukiangalia wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba pamoja na Kidato cha Nne wale ambao hawapati nafasi ya kuendelea Kidato cha Tano, maana yake tuna wanafunzi wasiopungua 6,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Chuo cha VETA kinachukua wanafunzi wasiozidi 200 tafsiri yake ni kwamba watoto zaidi ya 5,000 wanakaa Mtaani na hawana kazi ya kufanya. Kwa hiyo, nadhani tukiongeze wigo wa

Vyuo vya VETA pamoja na Vyuo vya Ufundi kuchukua wanafunzi wengi, matokeo yake tutapata wanafunzi wengi wenye elimu ya kawaida ya ujasiriamali, elimu ya kawaida ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka hapo kama tumepanga kujikita kwenye viwanda, ningeshauri tufufue lile shirika letu la viwanda vidogo (*SIDO*)..

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba leo tukipata Mkurugenzi Mtendaji mzuri wa *SIDO*, mfano kama alivyo yule Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Nyumba, akaangalia namna gani mafunzo mengi yanaweza kutolewa kwa vijana wengi zaidi; yale mafunzo yatawasaidia kuwajenga vijana wetu, wapate elimu ya ujasiriamali, tena kwa gharama nafuu. Maana kama wote mmetembea; Waheshimiwa Wabunge nadhani ninyi ni mashahidi, mafunzo mengi ya watu wanayojifunza Kule *SIDO*, kitu kikubwa kwanza wanajifunza usindikaji. Kama ni usindikaji wa alizeti, watajifunza; kama ni wa unga watajifunza, lakini ni pamoja na ufundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani watakapoenda pale watajifunza usindikaji pamoja na mambo ya *packaging*. Kwa kufanya hivyo sasa itawapa nafasi ya kuwa na bidhaa ambazo sisi wenyewe tutazitumia na hata nchi zote zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda nchi kama Kenya kuna hawa wanaoitwa Juakali. Juakali Kenya ina nafasi kubwa sana na inawasaidia watu wengi sana. Kwa hiyo, ukiangalia hili Shirika letu la *SIDO* kama tukilifufua na likapata mwendeshaji mzuri, ni dhahiri kwamba tutakuwa na vijana wengi ambao watakuwa na ujuzi wa kuweza kujiajiri. Kwa utaratibu huo sasa, hata hizi taasisi zetu za fedha ni rahisi kuwapa fedha kwa kuwakopesha kwa sababu tayari wanao ujuzi utakaowasaidia katika kusukuma maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine basi, hebu tuendeleo kuimarisha hizo Ofisi zetu za Ubalozi. Maana Ofisi zetu za Ubalozi ni kwamba tukiwa na wale ma-*business attache* wataweza kujua kwamba bidhaa gani zinazotakiwa huko ili waweze kutusaidia watu wetu hawa waweze kuuza huko.

Eneo lingine ni eneo la kilimo, mfano pale Mara, tunalo eneo kama lile shamba la Bugwema ambalo ni heka 20,000, mashamba kama haya yako mengi katika nchi hii. Leo ukitangaza tenda ya nani yuko tayari kufanya *irrigation* katika eneo hilo, labda katika kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Serikali inawalipa fedha za kufanya *irrigation*, matokeo yake ni kwamba lile bonde lenyewe linaweza kuzalisha mazao mengi kama mpunga, alizeti ambayo itasaidia sana watu wetu, siyo wa Musoma peke yake wala si wa Mara, lakini maeneo kama haya yako mengi

ambapo Serikali nadhani kwamba ikijikita katika utaratibu huo itaweze kusaidia watu wetu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapozungumza kwenye suala la mifugo, nini kifanyike? Tunahitaji tutenge maeneo madogo, maana Mpango huu umesema tunahitaji tufungue Vituo vya Uhamilishaji.

Ni kweli kwamba tatizo kubwa tulilionalo, ng'ombe wetu; sisi ni wa tatu katika Afrika, lakini ng'ombe wetu thamani yao ni ndogo. Tunachohitaji, ni lazima tufanye *crossbreed* ili tuzalishe mifugo ambayo itakuwa na tija.

Kama hivyo ndiyo basi, sasa ni lazima tuwe na vituo kama vile ambavyo vitazalisha ng'ombe wanaokuwa haraka ndani ya kipindi cha miaka miwili unaweza kuuza ng'ombe kwa Shilingi milioni moja, mpaka Shilingi milioni mbili kuliko hawa wetu unawachunga miaka mitano mpaka minane lakini unauza kwa Sh. 500,000/= ambazo hazina tija. Kwa hiyo, tunadhani hilo nalo katika mipango yetu linaweza likatusaidia katika kuhakikisha kwamba tunaendelea. nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kwa mara ya kwanza ili niweze kutoa mchango wangu katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehemu ambaye ameniwezesha kuwepo katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Kumi na Moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi hii pia kwa sababu nimesimama kwa mara ya kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara ambao wameniamini na kunipa nafasi hii; kwani hii ni mara ya nne nagombea; na wananchi wa Ngara wamekuwa na imani, Jimbo la Ngara limeshinda kwa kishindo; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepata kura nyingi, Mbunge wa CCM amepata kura nyingi tofauti ya kura 18,000 dhidi ya Mpinzani wa CHADEMA, lakini pia Madiwani wote wa Kata 22 ni wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuonyeshe ni jinsi gani ambavyo wananchi wa Jimbo la Ngara lakini na Watanzania kwa ujumla walivyo na imani na Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. Nachukua nafasi hii pia kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais. Sikupata nafasi ya kuchangia, lakini ni hotuba ambayo ilijaa weledi ambayo ilileta matumaini mapya kwa Watanzania.

Nachukua nafasi hii pia Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa Mpango huu ambao mmeuleta mbele yetu ambao pia unaleta matumaini. Ndugu zangu mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nje ya Bunge hili nilikuwa nikiangalia yaliyokuwa yakiendelea, wakati mwingine nilikuwa nachelea kujua kwamba ni nini, hususan upande mwingine. Ndungu zangu, ninajua kwamba maendeleo ni mchakato. Miaka 54 inayotajwa kwamba ni miaka 54 ya Uhuru ni muda mrefu, naamini ukilinganisha na yaliyofanyika ni mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanasahau kwamba tayari wanayo zaidi ya miaka 29 tangu mwaka 1992, lakini mpaka leo huwezi ukapima. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika kuchangia mpango huu. Vipo vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika Mpango huu ikiwa ni pamoja na kipaumbele cha kilimo, kipaumbele katika Sekta ya Madini. Naomba niwarejeshe katika Mpango huu hususan katika ukurasa ule wa 34. Naanza kuchangia upande wa Utawala Bora. Nina uhakika kwamba huu nao ni msingi katika kutekeleza Mpango huu na msingi ambao unaweza ukatupeleka katika mafanikio katika Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua zimekuwepo jitihada kubwa na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais alijaribu kuangalia akaona kwamba upande huu ni lazima tuushughulikie, ndiyo maana ameanza kuboresha sekta hii upande wa TAKUKURU kama chombo ambacho kinaweza kikasimamia na kuhakikisha kwamba pia utawala bora unafanyika, Mahakama na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze dhahiri kwamba pale ambapo Serikali itaweza kwenda sawasawa na kusimamia Mipango hii kwa umakini kwa kuzingatia Utawala Bora nina uhakika kwamba tunaweza kufanikiwa. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais kwa kutambua kwamba ipo mianya ambayo inasababisha tusiweze kupata mapato vizuri, lakini kwa lengo la kutaka kuimarisha utawala bora kwa maana ya kuziba mianya ya rushwa, kwa makusudi na kwa dhamira ya dhati akasema kwamba lazima sasa aanzishe Mahakama ya Mafisadi ya kushughulikia mafisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkakati mahususi ambao utakapoenda kutekelezwa tuna uhakika kwamba Tanzania mpya itaonekana na Mpango huu utaweza kutekelezwa kwa umakini. Kwa sababu kwa kuziba mianya ya rushwa maana yake ni kwamba pia makusanyo ya Serikali yataweza kuongezeka. Makusanyo yatakapoongezeka, maana yake ni kwamba mipango hii itaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaaminishe Watanzania na ninyi mtakubaliana na mimi kwamba kazi ya kiongozi ni kuonyesha njia na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli tayari ameonyesha njia kwamba

anayo dhamira ya dhati ya kuonyesha kwamba makusanyo yanapatikana, anayo dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba mipango hii inatekelezeka. Tunaongelea siku 100 za utendaji kazi wake, lakini matokeo tumeyaona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongeze Baraza la Mawaziri ambalo ameliunda, kwa sababu kwa kipindi hiki kifupi cha miezi miwili, mitatu tumeona matokeo ya kazi wanayoifanya Mawaziri hawa. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuwapongeza kwa sababu hii inaonyesha mwelekeo tunakokwenda kwamba itaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijelekeze katika suala zima la madini. Tunajua kwamba eneo hili ni eneo ambalo ni nyeti na ambalo tuna uhakika na kuamini kwamba likisimamiwa vizuri linaweza likaendelea kuboresha na kuinua uchumi wa Tanzania.

Katika jimbo langu la Ngara yako madini adimu, madini ya Nickel, madini ambayo yanaifanya Tanzania iingie kwenye ramani ya dunia kuwa na *deposit* kubwa ya Nickel duniani kama siyo ya kwanza itakuwa ni ya pili. Ndiyo maana naunga mkono ujenzi wa reli ya kati pamoja na reli inayotoka Dar es Salaam kuja Isaka, kwenda Mwanza, Tabora, Kigoma, lakini pia mchepuko wa kutoka Isaka kuja Ngara ili kusudi mradi huu uweze kutekelezeka na *nickel* hii iweze kusafirishwa kwa ajili ya kupelekwa sokoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tunategemea kwamba ni mkubwa lakini ambao wananchi wa Ngara kwa muda mrefu wamekuwa wakiuangalia kama tumaini lao kwa ajili ya kusababisha ajira. Tangu mwaka 1973/1974 *exploration* ilianza. Tulitegemea miaka ya 2010/2012 kwamba mradi huu ungeanza lakini mpaka sasa hivi haujaanza. Kulikuwepo na *excuse* ya kwamba hakuna umeme. Nampongaza Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Profesa Muhongo, na timu yake akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wamejitahidi kuhakikisha kwamba sasa umeme unasambazwa katika Wilaya ya Ngara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na Meneja wa Kanda, TANESCO mchana huu akahiadi kwamba tayari Ngara inaunganishwa kwenye *grid* ya Taifa na bahati nzuri kwa Mpango ambao unanza Januari mwaka huu, Ngara imepewa kipaumbele kwenye kuunganishwa kwenye *grid* ya Taifa. Bado pia tuna mradi mkubwa wa umeme katika maporomoko ya Rusumo, mradi ambao unashirikisha nchi tatu; Rwanda, Tanzania na Burundi. Kwa hiyo, naamini kwamba Ngara itaweza kupata umeme wa kutosha na ni eneo ambalo linaweza likawekezwa. Naomba mgodi huu wa Kabanga *Nickel* uangaliwe na uweze kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye suala la afya. Tuna hospitali moja tu ya Wilaya ambayo inahudumia zaidi ya watu takriban 400,000 lakini kipo Kituo cha Afya ambacho tangu mwaka 2006 Halmashauri yangu ya Wilaya ya Ngara iliweza kuomba kupandishwa kuwa hospitali na Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, mwaka 2008 alitangaza kiwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeandika barua mara kadhaa kwa ajili ya kuomba usajili wa kituo hiki kiweze kuwa hospitali; ni hospitali inayotegemewa kwa sababu ina vigezo vyote vya kuitwa Hospitali na barua ya mwisho ilikuwa ni ya mwaka 2013. Nimebahatika kukutana na Naibu Waziri wa Afya na amekubali kulishughulikia hili, naomba liweze kushughulikiwa haraka iwezekanavyo ili kuweza kunusuru afya za wana-Ngara ili Hospitali hii ya Nyamiaga iweze kutambulika kama hospitali na iweze kupata mgao ili iingizwe kwenye bajeti kwa ajili ya kuhudumia wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni pamoja na Kituo cha Murusagamba ambacho Mheshimiwa Rais alishatangaza rasmi kwamba sasa kianze kupanuliwa kwa ajili ya kuwa hospitali kulingana na jiografia ya Jimbo la Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze pia katika suala la maliasili. Tunajua kwamba Halmashauri zina vyanzo vyao vya mapato. Kwa mujibu wa Sheria ya Maliasili, Jimbo la Ngara lina hifadhi mbili; Hifadhi ya Burigi na Hifadhi ya Kimisi. Hifadhi ya Burigi imeingizwa kwenye gazette la Serikali tangu mwaka 1974; Kimisi imeingizwa kwenye gazette la Serikali mwaka 2005. Kwa mujibu wa sheria hiyo kuna tozo ya asilimia 25 ambayo inatakiwa ingie kwenye Halmashauri kama *own source*, lakini kwa miaka yote hiyo kwa hifadhi zote hizi mbili hakuna hata senti tano ambayo imeingia kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri husika kwamba tozo hii ya asilimia 25 ianze sasa kuingia kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, lakini pia hata *arrears* kwa miaka yote hiyo ambayo haikuweza kutolewa kama tozo kwa ajili ya kuimarisha Halmashauri ya Wilaya ya Ngara iweze kutolewa kwa ajili ya kuongeza pato la Wilaya ya Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nangana na waliotangulia, kwamba lazima *retention* hii iweze kukusanywa kwa ajili ya kuweka kwenye mfuko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gashaza, ahsante.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu na Chama changu makini CHADEMA kwa kunipa nafasi hii. Pia napenda kuwapa pole wananchi wa Mtwara Mjini kwa kadhia ya mvua waliyoipata siku ya jana, lakini hii yote imesababishwa na miundombinu mibovu iliyowekwa na Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia mpango huu nitajikita katika mambo mbalimbali. Mtwara imewekwa katika eneo la uwekezaji kwa maana ya viwanda, lakini tatizo kubwa la Mtwara ni maji ya kutosha kuhudumia viwanda. Mtwara Mjini kuna mradi unaotakiwa utoke Mto Ruvuma kuja Mtwara Mjini kuleta maji. Huu mradi umepitia process zote, kilichobaki ni kuwekeana saini kati ya Serikali ya China kupitia *Exim Bank* ya China na Wizara ya Fedha ya Tanzania, lakini huu mradi ulitakiwa uanze tangu mwezi wa Saba mwaka 2015 lakini mpaka leo haujaanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unayehusika, tunaomba mlifuatilie jambo hili ili tuweze kupata maji ya uhakika yatakayotosheleza kwa ajili ya kuhudumia hivyo viwanda vyetu.

Hatuwezi kuhudumia viwanda mfano, Dangote maji anayoyahitaji na maji yanayopatikana sasa hivi, akipewa yeye, maana yake sisi wananchi wa Mtwara Mjini hatuwezi kupata maji ya kutosha. Lakini suala la maji Mtwara Mjini, Serikali hailipi Idara ya Maji. Kinachotokea ni nini? Watu wa Idara ya Maji wameambiwa wajitegemee, wanajitegemea vipi wakati Serikali pale Manispaa ya Mtwara Mjini inadaiwa Shilingi milioni 581? Pesa zinakwenda, mpaka Mkuu wa Mkoa nyumbani wake anadaiwa Shilingi milioni moja na ushee. Kwa hiyo, tunachokisema, Serikali wapeni pesa Idara ya Maji waweze kujendesha ili hata hivyo viwanda vinavyokuja viweze kufanya kazi. Maji ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitaongelea elimu. Nasikitika sana, kila yanapotokea matokeo yawe ya Darasa la Saba, yawe ya *Form Two*, yawe ya *Form Four* na kwingine kote Mtwara lazima iingie kwenye kumi za mwisho. Hii ni aibu na ni fedheha kwetu, hatupendi. Nataka niwaambie, shule tatu katika mtihani wa *Form Two* zilizofanya vibaya, matokeo yaliyotoka juzi juzi zimetokea Mtwara. Mbili kati ya hizo, zimetoka Tandahimba ambako kuna shida kubwa ya maji; na watoto wanaohangaika wanafeli ni watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Mtwara ya Viwanda wakati elimu yetu iko chini. Ndugu zangu tusifanye mambo yale yale kila siku, tusifanye kazi kwa mazoea. Mimi ni Mwalimu wa Walimu, naelewa vizuri. Nimekuwa nikifanya kazi na wanafunzi katika Shule. Mwanafunzi hawezi kusoma kwa kumtolea ada ya Sh. 20,000/= mwanafunzi ili aweze kusoma vizuri, anahitaji

apate vitabu, anahitaji akae pazuri, anahitaji ashibe, anahitaji apate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wa kike wa Mtwara, mnawalalamikia wanaolewa mapema, amefika *Form Two* maji yalikuwa yamhangaisha, amefeli, kinachofuata ni nini?

**MBUNGE FULANI:** Kuolewa!

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Kwa hiyo, Serikali tunaomba muweke kipaumbele kwenye upatikanaji wa maji. Huu mradi wa Mto Ruvuma utahudumia vijiji 26; miongoni mwao vipo Mtwara Vijijini na huko Mtwara Vijijini kuna shule ya mwisho imetokea huko kama sijakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la elimu, mimi natambua kila Wizara ina Kitengo cha Sheria; na Wizara ya Elimu bila shaka itakuwa na Kitengo cha Sheria. Sasa kama Sheria za Elimu zimepitwa na wakati, zinaruhusu matamko ya Mawaziri yanayorudisha elimu yetu nyuma, Kitengo cha Sheria Wizarani wakae wachambue wasiwape Mawaziri mamlaka yanayodidimiza elimu yetu.

Mama yangu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, hapa katika kuzungumza, wanazungumzia Shule za Sekondari na Shule za Msingi. Nataka nikukumbushe kwamba kuna Vyuo vya Ualimu, ndiyo huko nilikotokea mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu yenye matatizo katika tasnia ya Ualimu ni pamoja na Vyuo vya Ualimu. Watu wa Vyuo vya Ualimu naomba ukawasikilize. Sasa hivi wameingiziwa, kuna *NACTE*, kuna Wizara, kuna *TSD*, hawaelewi, wanayumbayumba. Nenda ukawasikilize, ujue matatizo yao, wanashindwa kufanya kazi. Nimetoka huko, mpaka nachaguliwa kuwa Mbunge, nilikuwa nafundisha Chuo cha Ualimu Mtwara kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea barabara. Sijui watu Mtwara tufanye nini ili mtusikie kuhusu barabara ya kutoka Mtwara Mjini, inapita Nanyamba, inapita Tandahimba, Newala Mjini mpaka Masasi. Tufanye nini ili mtusikie? Tunaomba mtujengee barabara. Korosho zinatokea huko kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Bandari yetu ya Mtwara kwanini hamtaki *kui-upgrade*? Kwa saabu ukisoma huu Mpango, asilimia kumi tu ndiyo inaonekana Bandari ya Mtwara na hizo nyingine, lakini asilimia kubwa inatumiwa Bandari ya Dar es Salaam, wakati sisi tuna eneo kubwa. Kwa kuja kuwekeza kule na *kui-upgrade* hii bandari tunaamini vijana wenzangu kama

mimi watapata ajira za kutosha na kuondokana na umaskini ambao unawatala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho maana naona muda umeisha, nataka kusema, Chama cha Mapinduzi kilitengeneza majipu kwa miaka 55, sasa wameanza kuyatumbua hatujui watatumia miaka mingapi! Kwa hiyo, ninachosema, wala msiwaaminishe wananchi kwamba mnafanya kazi kubwa, hayo majipu mliyatengeneza wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba suala la maji lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nauliza jambo moja, naomba ufafanuzi mtakapokuja kujumuisha. Suala la umeme; mimi najua mafuta yanakotoka bei inakuwa ndogo kuliko kwingine. Sisi Mtwara tunanunua mafuta bei kubwa. Kwanini umeme wote tunalipa sawa wakati unazalishwa kule kwetu? Tunalipa sawa na sehemu nyingine! Pia hilo naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii. Kwanza naitumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, lakini nawashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Ukerewe kwa kuniamini na kunituma niwawakilishe kwenye chombo hiki muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mchango wangu utajikita kwenye maeneo kadhaa. Nikianza na eneo la Afya; Mpango ulioletwa katika Bunge ni Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya wananchi kwenye nchi yetu na kaulimbiu ni kutengeneza Tanzania ya Viwanda, lakini hatuwezi kutengeneza Tanzania ya Viwanda kama tutakuwa na jamii yenye afya dhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Afya kwa mfano nikiongelea kwenye eneo langu la Ukerewe; Ukerewe ni kisiwa. Kwa ujumla tuna visiwa zaidi ya 30; visiwa kama 38 hivi, lakini huduma za afya kwenye eneo la Ukerewe ni mbovu sana, kiasi kwamba ikitokea dharura kwa mfano, tuna hospitali ya Wilaya pale, ina matatizo makubwa, wahudumu wachache na tukizingatia mazingira ya jiografia ile, watumishi wengi wanapangiwa kwenye kisiwa kile hawaendi.

Kwa hiyo, naomba katika mipango yenu mliangalie jambo hili na hasa watu wa Utumishi kwamba watumishi wanaopangwa kwenye maeneo ya visiwa kama Ukerewe mhakikishe kwamba wanafika kwa ajili ya kuwahudumia

kwa sababu Ukerewe ni eneo muhimu kama yalivyo maeneo mengine katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu zaidi, ukizingatia kwamba ni kisiwa, tuna usafiri wa meli pale. Kutoka Ukerewe kuja Mwanza, tunatumia zaidi ya masaa matatu, ni masaa matatu kama na nusu hivi. Kwa hiyo, ikitokea dharura, mtu akipata tatizo la dharura la kiafya, kuletwa Mwanza ni tatizo kubwa sana. Wakati fulani tulileta mapendekezo ikaletwa *ambulance boat*, cha ajabu ambacho tulitegemea kwamba itakuwa ni *speed boat*, badala ya kutumia chini ya masaa matatu, boti natumia masaa manane kwa ajili ya kumsaidia mgonjwa.

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Wapi na wapi? Kwa hiyo, pendekezo langu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Ukerewe, hebu tusaidieni *ambulance boat* ili kusaidia huduma za kiafya kwa wananchi wa Ukerewe waweze kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuimarisha uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile bado katika mgao wa watumishi kama nilivyosema ni jambo muhimu sana, watu wa utumishi hakikisheni kwamba kwenye maeneo yaliyoko pembezoni kama Ukerewe, basi watumishi wakipelekwa wanafika kwenye maeneo yale wanawasaidia wananchi wa maeneo yale waweze kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni suala la miundombinu. Tuna barabara inayotuunganisha na maeneo mengine kama Bunda. Tuna barabara ya Bunda, Kisorya, Nansio mpaka Ilangala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu uliowasilishwa nimeona tu eneo la Kisorya, Bunda. Sijaona mwendelezo wa kwenda Nansio, Ilangala, kitu ambacho ni muhimu sana kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Ukerewe. Kwa sababu tunapoongelea habari ya Tanzania ya Viwanda tunahitaji tujenge uchumi wa wananchi na hatuwezi kujenga uchumi wa wananchi hawa kama miundombinu ina matatizo na mojawapo katika miundombinu hiyo ni eneo la barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara hii wakati itakapokuja na Mpango, ioneshe ni mpango gani uliopo juu ya ujenzi wa barabara hii ya Bunda - Kisorya - Nansio -Ilangala. Barabara hii ijengwe kwa lami ili kuimarisha uchumi wa wananchi wa Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni eneo la uvuvi. Uvuvi ndicho chanzo kikubwa cha uchumi wa wananchi wa Kanda ya Ziwa na *specifically* eneo la Ukerewe kama Wilaya. Tunazungukwa na Visiwa na ajira kubwa kwa wananchi wa Ukerewe, ni Sekta ya Uvuvi, lakini uvuvi huu kama chanzo kikubwa cha mzunguko wa pesa na kuimarisha uchumi wa wananchi wa Ukerewe, inakabiliwa na changamoto nyingi sana kubwa; ambapo Mheshimiwa Waziri katika Mpango wako, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na masuala haya ya uvuvi, mwangalie namna gani mnaweza mkawasaidia wavuvi wa Ukerewe ili angalau waweze kuimarisha mazingira yao ya kiuchumi na kujenga uchumi wa Kitaifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Ukerewe wanapata shida kubwa sana, kimsingi katika eneo lote la Ziwa Victoria; wanafanya shughuli zao hawana uhakika na usalama wa maisha yao; wanafanya shughuli zao huku wanavamiwa, wananyang'anywa rasilimali zao kwenye Ziwa Victoria; wengine wanajeruhiwa, wanapoteza maisha yao. Ni lazima Tanzania kama nchi, tufike mahali tuone umuhimu wa jambo hili, tuhakikishe usalama wa watu hawa ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi wakiwa wana uhakika na usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, shughuli zao za uvuvi vile vile watu hawa wanapofanya shughuli zao, uvuvi unakuwa na tozo nyingi mno ambazo zinafanya hata kile wanachokipata, kisiwasaidie sana kuimarisha uchumi wao. Mvuvi mmoja anakuwa na tozo takriban 12, 13, leseni za uvuvi; mtu analipa leseni katika Wilaya moja, akienda Wilaya nyingine anatozwa tena leseni, kitu ambacho kinawaathiri sana kiuchumi. Ni lazima katika Mpango yenu mtakapokuja na Mpango wa jumla, mwangalie namna gani mnaweza mkasaidia watu hawa ili waweze kuwa imara kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Ukerewe kama visiwa, ni eneo ambalo ni *very strategic* tunaweza tukalitumia kwa ajili ya kuimarisha utalii. Maeneo mengine kwenye nchi nyingine wametumia visiwa kwa ajili ya kuimarisha pato la kiutalii kwenye nchi zao. Tunaweza tukaitumia Ukerewe. Kwa mfano, kuna eneo moja la Ukara kuna jiwe linacheza, ambalo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, mnaweza kuona ni namna gani tunaweza tukatumia vyanzo kama hivi kuvutia Watalii, ikasaidia kuongeza pato la nchi yetu. Kwa hiyo, naombeni mlichukue na muweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna changamoto kwenye eneo la usafiri. Kama nilivyosema, sisi tunaishi katika Visiwa, lakini tuna meli moja ya Serikali ambayo ni chakavu. Tulikuwa na meli ya MV Butiama, miaka mitano sasa haifanyi kazi. Wananchi wanasafiri kwa shida kweli kweli na wala hatuoni kama kuna utaratibu wowote au mpango wowote wa kutengeneza meli ile na kuwasaidia Wananchi wa Ukerewe.

Kwa hiyo, napenda kusikia wakati mtakapokuja na Mpango wenu, tujue kwamba ni mpango gani mlionao juu ya kuimarisha hali ya usafiri kwa wananchi wa Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea kwa sababu naona muda siyo rafiki, ni juu ya suala la umuhimu wa Halmashauri katika ujenzi wa uchumi ya nchi yetu. Halmashauri hizi kama tutazitumia na hasa kwa kuimarisha watu walioko katika Halmashauri, ni bahati mbaya sana kwamba katika nchi hii, kwa sababu tunaziita *Local Government*, tunahisi kwamba hata watu waliopo kule, basi ni *local* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzitumie Halmashauri hizi kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu. Halmashauri hizi haziwezi kuwa imara kama hatutaimarisha Viongozi wa Serikali za Mitaa. Kwa sababu tunaongea habari ya kujenga uchumi, lakini tunapojenga viwanda, tunaimarisha mazingira, kuna watu watahitaji kusimamia shughuli kule chini. Kuna Wenyeviti wa Viijiji, Wenyeviti wa Vitongoji, tuwaimarishe ili waweze kusaidia kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kunichagua na kunituma niwe mwakilishi wao katika nyumba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana aliyewasilisha Mapendekezo ya Mpango ambao tunaujadili hivi sasa. Mapendekezo ya Mpango huu tumeletewa ili tuweze kuyaboresha, nami naomba niboresha katika maeneo kadhaa kwa sababu ya muda, ili tuweze kuboresha zaidi Mpango huu kwa masilahi ya watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, naomba sana, tunapokuwa tunaangalia namna ya kukuza uchumi wa nchi, ni lazima tuangalie zaidi upatikanaji wa ajira kwa vijana. Nchi hii ina vijana wengi sana, asilimia zaidi ya 40 ni vijana ambao wanaweza kuajiriwa au ni nguvu kazi ya nchi hii. Hawa wasipowekwa maalum kwenye Mpango, namna gani watapatiwa ajira na tukafanya *projection* ni wangapi watapata ajira kwa Mpango huu, tutakuwa tunachelewesha kukua kwa uchumi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ya kuweza kuwapatia vijana hawa, mathalan wa Bukombe ili uweze kuwapatia ajira, ni lazima uwatengee maeneo ya kuchimba dhahabu. Bukombe ndilo eneo pekee katika Mkoa wa

Geita ambapo maeneo mengi yana dhahabu nyingi, lakini vijana wa Bukombe hawajapatiwa maeneo ya kuchimba dhahabu. Vijana hawa hawawezi kuelewa Serikali kama hawajapatiwa maeneo ya kuweza kufaidi rasilimali za nchi ambazo Mungu amewapatia na wamezaliwa wamezikuta hapo. Wakati umefika Mheshimiwa Waziri tuje na Mpango wa kuangalia namna gani vijana wanapatiwa maeneo ya kuchimba dhahabu katika Mpango wetu huu tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la umeme. Watu wengi hapa wamezungumza, wamepongeza uwepo wa umeme wa REA. Sisi tuna REA I na REA II, mpaka sasa, lakini Wilaya ya Bukombe haijawahi kupata hata awamu moja ya umeme wa REA.

Nakuomba sana Mheshimiwa Profesa Muhongo na Naibu Waziri wako, nafahamu ninyi ni watu wasikivu, mtusaidie Bukombe na sisi tupate umeme wa REA. Haina maana nimesimama hapa kama Mbunge, wenzangu wanashangilia umeme na wewe Mheshimiwa Profesa Muhongo ulisema, sitaenda REA III mpaka viporo vya REA I na REA II viishe, wakati mimi hata REA I na REA II sijawahi kuiona! Mheshimiwa Profesa Muhongo nakusihhi sana, Bukombe uitazame kwa jicho la huruma. Tunahitaji umeme kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Uyovu kuna Kituo cha Afya, kinafanya huduma kubwa ya kuhudumia watu, kinahudumia Wilaya ya Bukombe, kinahudumia Wilaya ya Chato, kinahudumia Wilaya ya Biharamulo, lakini hakuna umeme pale. Madaktari wangu pale wanafanya *operation* kwa tochi. Jana nimepigwiwa simu, wanazalisha mama mmoja wanatumia tochi. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana utusaidie umeme kwa ajili ya watu wa Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba niipongeze sana Serikali kwa kuja na Mpango wa elimu bure kwa Watanzania. Mpango huu kwa maoni yangu naona kama ukichelewa. Kuanzia sasa watoto kuanzia darasa la kwanza mpaka la kumi na mbili watapata elimu bure. Ninafahamu wako watu wengine ambao wanaweza wakapuuza Mpango huu kwa kuona kwamba ni siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikisheni, tulipoanza na Mpango wa kujenga Shule za Kata, watu walitokea hapa wakapuuza namna ile ile, lakini leo ninavyosimama hapa na kuongea mbele yako, Shule za Kata ndiyo zimetusaidia kupata Wataamu wengi wa nchi hii. Nitakupa mfano kwenye Wilaya yetu ya Bukombe, Shule ya pili kwa kufanya vizuri Kidato cha Sita ni Shule ya Kata ya Lunzewe Sekondari, ambayo watu wakati tunaanza walianza kupuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, tusukume na namwomba sana Mheshimiwa Simbachawene, endelea kutuelimisha Watanzania. Tunavyoanza siyo rahisi! Siyo rahisi tunavyoanza tukaenda na mafanikio ya moja kwa moja. Tutapata *setbacks* hapa na hapa, lakini kadri tunavyoendelea ndivyo tutakavyokuwa tuna-*improve* ili twende mbele zaidi kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Mawaziri, naomba sana, sasa tumeshafanya vya kutosha; tumejenga madarasa, sijawahi kuona Mpango wa kuwasaidia Walimu, kuwa-*motivate* Walimu kufanya kazi vizuri. Walimu wa Tanzania wanafanya kazi katika mazingira magumu. Walimu wa Tanzania bado wanalipwa kwa viwango ambavyo havikidhi maisha yao kwa siku 30. Walimu wa Tanzania bado wana wajiri wengi na wanawajibika kwa watu wengi wakati wao ni watu wale wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba na tumelia kwa muda mrefu Walimu wapatiwe Tume ya Utumishi wa Walimu. Wamepatiwa, sasa ninaomba Serikali iharakishe mfumo wa kurekebisha Kanuni hizo zinazotengenezwa ili Tume ya Utumishi wa Walimu ianze kufanya kazi tuwahudumie Walimu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mfumo wa Elimu ndugu zangu umegawanyika katika sehemu tatu, sehemu ya kwanza ni Mtaala, sehemu ya pili ni udhibiti wa ubora na sehemu ya tatu ni *Examiner* au Mtahini yule anayeangalia matokeo ya kile walichojifunza Wanafunzi. Upande wa mtaala ambako Mwalimu ndiko yupo, hakuna nguvu kubwa iliyowekwa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia madarasa, ndiyo! Tunaangalia madawati, amina! Tunaangalia chaki, sawa! Lakini lazima tumwangelie Mwalimu ambaye ndiye mhusika Mkuu na msimamizi mkuu wa Mtaala wa Elimu katika nchi hii. Walimu hawa wanapokuwa wanalalamika na kulia, msitarajie tutapata matokeo ya uhakika. Tunaweza tukawalazimisha wakae darasani, watafanya kazi lakini nataka niwaambieni, *motivation* ya Walimu wa nchi hii bado iko chini. Iko kazi tunapaswa kufanya, tuje na Mpango Waziri wa Fedha, mpango maalum wa kutengeneza *frame work* ya *motivation* ya Walimu. Nchi nyingine zimeshafanya jambo hilo na zimefanikiwa sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili tuliangalie kwa jicho la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pale Bukombe kuna zao maarufu sana. Asali bora nchi hii inatoka Bukombe. Asali inayovunwa Bukombe na watu wamejiunga kwenye vikundi, wanafanya kazi kama yatima. Wako kwenye Vikundi watu 6,000, wanavuna asali zaidi ya lita milioni moja kwa mwaka, lakini hakuna hata Kiwanda kimoja cha kusindika asali. Nakuomba Mheshimiwa

Waziri wa Viwanda na Biashara na tulishazungumza, tuangalie namna ya kupata Kiwanda cha Kusindika Asali ya watu wa Bukombe ili asali yao ipate bei kubwa, ipate soko la uhakika, tubadilishe maisha yao kwa kuwapatia fursa ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, vile vile Wilaya ya Bukombe tuna mifugo mingi, lakini mifugo hiyo haichangii kwenye pato la Taifa. Nchi hii ina mifugo milioni 25, lakini ukiangalia takwimu kwa hali ya uchumi, kwa taarifa ya hali ya uchumi ya Juni, 2015, utaona nchi hii pamoja na kuwa na mifugo milioni 25, tumeuza nje ya nchi mifugo 2,139 na tumepata Shilingi bilioni 34 peke yake. Tuna mbuzi milioni 15, lakini tumeuza mbuzi 264; tumepata Shilingi bilioni 1.7.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, utakapokuja kujumuisha, uje na Mpango wa kutusaidia wafugaji hasa wa Kanda ya Ziwa, wafugaji wa Tanzania, tupate malisho, tumechoka kukimbizana na Wahifadhi wa Wanyamapori, ma-game kupigana kila siku na kuanza kuhangaishana kutozana vifedha vidogo vidogo hivi, wakati tuna uwezo wa kuchangia kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, nimekuwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Ramo, mtu msikivu sana. Alikuwa Jimboni kwangu, akazungumza na wafugaji pamoja na Waziri wa Mifugo, walituambia mambo mengi ya kufanya, lakini cha ajabu, baada ya kauli zao kutoka, siku mbili, tatu, kauli ile ikabadilika kabisa. Wale wafugaji sasa hivi huko ninavyoongea wanatimuliwa kama wakimbizi kwenye nchi yao. Naomba Serikali tuangalie namna ya kuwasaidia watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tatizo la maji, Wilaya ya Bukombe bado tuko nyuma sana. Watu wanaweza kusema kwenye makaratasi asilimia 30 ya watu wanapata maji, hapana. Wanaopata maji Bukombe ni chini ya asilimia 30 na *actually* ni chini ya asilimia kumi. Miradi iliyopo mingi imeshasimama. Mradi wa Msasa haufanyi kazi, Mradi wa Kilimahewa haufanyi kazi ipasavyo, pale Ruhuyobu tuna miradi miwili; mradi mmoja peke yake ndiyo unaofanya kazi, mradi mwingine umesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni kazi ambayo tunahitaji tuione. Nami namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji, unapokuwa na kale kampango ka kupeleka maji Tabora, Nzega, Bukombe pale ni karibu, ukipitia Mbogwe, tunapata maji ya Ziwa Victoria, biashara hii inaisha. Nitakapokuwa nikisimama hapa, Mheshimiwa Waziri wa Maji, nitakuwa nazungumza mambo mengine, siyo maji. Saa imefika, naomba mtusaidie wananchi wa Bukombe tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, najua muda wangu umekwisha. *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii. Kwa kuwa ni mara ya kwanza kabisa kuweza kuchangia katika Bunge hili la Kumi na Moja, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kuendelea kuniamini tena wakanipa ridhaa katika awamu hii. Napenda kuwahakikishia kwamba nitaendelea kufanya kazi kwa nguvu zote ili kuweza kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kupongeza huu Mpango wa mwaka 2016/2017. Ninachopenda zaidi ni kuisitiza suala la reli ya kati. Nazungumzia suala la reli kwa sababu ni injini ya uchumi. Bila ya kuwa na reli, uchumi wetu hauwezi kukua kwa sababu hatuwezi kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwa njia ya barabara, kiasi kwamba mizigo mingi inasababisha barabara zetu ambazo tumezitengeneza kwa fedha nyingi kuharibika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa kwamba hii reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora, Mwanza, kutoka Tabora kuelekea Kigoma; kutoka Isaka kuelekea Keza na nyingine zote, naomba Serikali ituletee Mpango Mkakati, namna itakavyoweza kufanya ili kuweza, kutengeneza reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maji. Naomba katika Mpango huu, Serikali iwekeze Mpango Mkakati wa uhakika, kwa suala la maji, kwa sababu maji ni tatizo kubwa sana hasa vijijini kwa wananchi wa Tanzania. Katika Jimbo la Busanda, pengine ni asilimia kumi tu ya wananchi wanaopata maji safi na salama. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuomba Serikali inapoleta mpango mkakati, ihakikishe suala la maji, linakuwa ni la kipaumbele kikubwa sana kwa sababu maji ni uhai. Hatuwezi kuwa na mapinduzi ya viwanda bila kuwa na maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi katika Mkoa wetu wa Geita tumebahatika kuzungukwa na maji ya Ziwa Victoria. Hebu Serikali basi ifikie hatua, iangalie uwezekano tuweze kupata maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria. Tayari katika Mji wa Geita, tumevuta maji kutoka Ziwa Victoria, kwa hiyo, basi Serikali iangalie uwezekano hata sisi vijijini tuweze kupata maji ya uhakika hasa maeneo ya Busanda na Sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile upande wa afya, napenda kuishauri Serikali iangalie katika Mpango wake wa mwaka 2016/2017, katika Mikoa mipya hatuna Hospitali za Rufaa. Katika Mkoa wa Geita, hatuna Hospitali ya Rufaa. Katika takwimu inaonesha kwamba vifo vya akina mama wajawazito, takwimu

bado iko juu sana. Sasa ili tuweze kupunguza vifo vya akina mama wajawazito, ni vizuri Serikali iweke mkakati mkubwa wa kuwekeza katika upande wa afya hasa kwa kujenga Hospitali za Rufaa katika Mikoa ambayo hatuna Hospitali za Rufaa kama Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia tuangalie katika Kata zetu, tuwe na hospitali, Vituo vya Afya, lakini pia katika Wilaya tuwe na Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, naomba Serikali kweli iwekeze katika upande wa Afya, kwa sababu haiwezekani tukafikia uchumi wa kati bila kuwa na afya kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba sasa katika Mpango Mkakati, nahitaji kuona kabisa kwa dhahiri kwamba Hospitali ya Rufaa ya Geita ipo kwenye Mpango, lakini vile vile Mpango wa Vituo vya Afya katika Kata zetu na Zahanati katika Vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa upande wa elimu, nami naendelea kushukuru sana kwa huu mpango wa elimu bure. Baada ya kutangaza kwamba elimu ni bure, imeonekana hata watoto ambao wanapelekwa shule kuandikishwa Darasa la Kwanza, wameongezeka kwa kiasi kikubwa. Hili linaonesha jinsi ambavyo kumbe wazazi wengi walikuwa hawapeleki watoto wao shule kwa sababu wanaona kwamba ni gharama kuandikisha, ni gharama kulipa ile ada. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo na juhudi ambazo imezifanya.

Naomba tu sasa Serikali iendeleo kuongeza zaidi namna ya kuwezesha hii elimu bure, ili iweze kwenda kwa utaratibu sahihi ili watoto wetu waweze kunufaika zaidi katika elimu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili sasa, ili tuweze kufikia katika uchumi wa kati, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni amesisitiza sana suala la viwanda kwamba Tanzania yetu itakuwa ni Tanzania ya viwanda, nami hili suala nalipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwe na viwanda vya kimkakati kila Kanda. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa, tuna mazao yetu, tuna dhahabu, tuna mifugo, tuna uvuvi; kwa hiyo, Serikali iangalie viwanda gani ambavyo itaweza kuwekeza ili wananchi wetu kulingana na mazao tuliyonayo tuweze kunufaika zaidi na vijana waliyo wengi waweze kupata ajira katika viwanda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie viwanda vya kimkakati katika Kanda ya Ziwa Viwanda vya Samaki; tunahitaji tuwekeze katika Viwanda vya Samaki, Viwanda vya Nyama na vile vile Viwanda vya Dhahabu, yaani kuongeza thamani ya dhahabu. Mkoa wa Geita tumebahatika dhahabu kwa wingi. Naomba pia Serikali katika mwaka huu wa fedha, tuangalie uwezekano

wa kutoa maeneo ya kutosha kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kwa sababu ndiko ambako vijana wengi wamejajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa sababu hii imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, lakini vile vile Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, naomba kweli mwaka huu Serikali iangalie uwezekano wa kutoa maeneo ya kutosha kwa ajili ya kuwapatia wachimbaji wadogo ili vijana wengi waweze kupata ajira katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naiomba sana Serikali kwamba tunaupokea huu Mpango lakini iweke mkakati mzuri na itakapouleta vizuri tuone katika Mpango huu iguse hayo maeneo ambayo pengine hayajaweza kujioneshwa kwa dhahiri ndani ya Mpango ili basi tunapopitisha tuweze kuona kabisa kwamba Tanzania tunapiga hatua katika uchumi, kutoka uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati kama ambavyo mategemeo na matarajio yetu yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa upande wa elimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja, Serikali iendeleo kutekeleza hayo. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo machache hapa na tangazo mojawapo, kuna Mbunge amepoteza kadi yake ya NMB, anaitwa Mheshimiwa Peter Ambrose Paciens, ama kama kuna mtu anamfahamu mwenye hii kadi, anaweza akawasiliana na Ofisi ili aweze kuichukua.

Matangazo mengine, Waheshimiwa Wabunge mnajulishwa kuwa siku ya Alhamis yaani kesho tarehe 4 Februari, 2016 hakutakuwa na kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kwa sababu hatakuwepo Bungeni wakati huo kwa sababu ya majukumu muhimu. *(Makofi)*

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa wataalam wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) watakuwepo hapa Bungeni ili kutoa huduma ya kupiga picha kwa ajili ya vitambulisho vya uraia kwa

Waheshimiwa Wabunge ambao hawana vitambulisho hivi. Kwa hiyo, kama una kitambulisho, huna haja ya kushiriki.

Zoezi hilo litaanza tarehe 4 Februari, 2016 mpaka tarehe 5 Februari, 2016 kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni katika Ukumbi wa Msekwa, Chumba Na. 5. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote ambao hawana vitambulisho vya Uraia wanaombwa wafike kwenye ukumbi huo ili kupewa hiyo huduma.

Matangazo mengine; ninalo tangazo hapa la Mwenyekiti, aliyekuwa ametoa maagizo jana kwamba uthibitisho uwasilishwe na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim wa yale madai aliyokuwa anayatoa. Sasa Mheshimiwa Spika ameagiza kwamba agizo hili la uthibitisho litimizwe Ijumaa. Ijumaa, uthibitisho huo uwasilishwe ofisini kwa Mheshimiwa Spika tarehe 5 Februari, 2016.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pia mtakumbuka leo asubuhi Mwenyekiti alikuwa ameombwa Miongozo miwili; Mwongozo wa kwanza ulikuwa unatoka kwa Mheshimiwa Waitara na Mwongozo wa pili ulikuwa umeombwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Waitara, leo Jumatano nimepewa majibu ya Kiti. Wale ambao hawakuwepo kwa ajili tu ya kuweka kumbukumbu, leo jumatano tarehe 3 Februari, 2016 mara baada tu ya kipindi cha maswali, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) na kuomba Mwongozo kwamba wakati wa majibu ya nyongeza, Swali Na, 82 lililoulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Jimbo la Konde, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisimama na kupewa ruhusa na Mwenyekiti ambapo alimtaka Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutokujibu swali hilo la nyongeza linalohusu wananchi kuruhusiwa kuchukua sheria mkononi.

Mwanasheria Mkuu alisema suala hilo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika muongozo wake Mheshimiwa Waitara alitaka kujua kama kitendo cha Mwanasheria Mkuu kumzuia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kujibu swali hilo hakivunji Kanuni za Bunge na hivyo aliomba swali lake lijibiwe kikamilifu. Mwongozo wa Kiti; Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 39(13) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 inampa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kusimama na kujibu swali lolote lililoelekezwa kwa Waziri yeyote.

Hivyo basi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa na haki ya kusimama na kujibu swali la Mbunge badala ya Naibu Waziri aliyekuwa anajibu

swali hilo. Huo ndiyo Mwongozo uliotolewa kwa maombi aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara. (Makofi)

Mwongozo mwingine uliokuwa umeombwa, uliombwa na Mheshimiwa Tundu Lissu kuhusu majibu ya swali la nyongeza ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu takwimu za namna ambavyo (Waheshimiwa Wabunge, naangalia *Hansard*) misamaha ya kodi ilienda juu ya malengo wakati thamani na msingi wa mapato ya kodi vilipungua. Aidha, wafaidikaji wakubwa wa vivutio na misamaha ya kodi ni kundi dogo la wawekezaji wakati walioingia hasara ni wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Tundu Lissu alitaka Mwongozo wa Mwenyekiti kwa maana ya kwamba afuate lipi? Maana Waziri wa Fedha alikuwa ameonesha thamani, yaani *exemption* kwamba imeshuka lakini wakati anasema, taarifa inaonesha zimepanda. Sasa Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa akiangalia ukurasa wa 11. Waheshimiwa Wabunge, hivi vitabu tulipewa, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa akiangalia *Comprehensive Review Report for Tanzania Five Years Delevelopment Plan 2011/2012, 2015/2016*.

Katika ukurasa wa 11 nitasoma kama sehemu ya huo Mwongozo inasema hivi: *"The value of tax exemption in Tanzania from 2010/2011, 2014/2015 rose from Tanzanian Shillings 6.6 billion in the year 2009/2010 to 1.7 billion in the following year 2011/2012 and decreased to 1.5 billion in the following year 2012/2013. The decrease was the result of the government effort to reduce the tax exemptions as per policy. In 2010/2011 tax exemptions were 18.8% of domestic revenue and increased to 24.5% in 2011/2012 but dropped to 19.1% of domestic revenue in 2012/2013 and then dropped more to 18% in 2013/2014 and 16% in 2014/2015.*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa Kiti ni kwamba maelezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa amesoma tu sehemu ya hiyo sentensi ya hii *paragraph*. Ukiisoma *paragraph* nzima inaonekana ni kweli zile *tax exemptions* zimeshuka kufikia 16% mwaka 2014/2015, tofauti na hapo mwanzo ambapo mwaka 2010/2011 ilifika 18% na 2012 ilifika 24.5%. (Makofi)

Kwa hiyo, ukiisoma hii *paragraph* yote na hizi taarifa wote Waheshimiwa Wabunge tunazo, inaonesha kweli imeshuka imefika 16%. Kwa hiyo, Mwongozo wa Kiti ni kwamba, cha kufuata ni kwamba maelezo kamili ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa sahihi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho asubuhi, saa 3.00 tarehe 4 Februari, 2016.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 4 Februari, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*

## **Kikao cha Nane – Tarehe 4 Februari, 2016**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na Kikao chetu cha Nane katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge la Kumi na Moja. Orodha ya Shughuli zetu za leo mnayo. Katibu!

Haya mmejipangaje, nianze na Mheshimiwa Nchemba, Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu kuhusu hoja iliyotolea kuhusu mnada wa Magena pamoja na jibu lililolenga mnada wa Kilumi. Wizara imepokea malalamiko ya Wabunge mbalimbali wanaotokea Mikoa ya pembezoni ambako kuna minada ya mipakani na changamoto za uendeshaji wa minada iliyoko mipakani. Nakumbuka kwa mara ya kwanza tulipokea kutoka kwa Mheshimiwa Albert Obama wa Manyovu na tumepokea ya upande wa Ukanda wa Kaskazini, na sisi kama Wizara, mimi pamoja na Naibu wangu tumejipanga kutembelea minada yote hiyo ya mipakani ili kuweza kujionea changamoto hizo na hatua za uendeshaji ambazo hazijafanya minada hiyo iendeshwe kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naliomba Bunge lako Tukufu pamoja na meza yako, iridhie jambo hili tukalifanyie *site* kulekule ili kuweza kupata uhalisia na njia muafaka ya kuweza kutekeleza jambo hili ili Watanzania waweze kunufaika.

Sisi kama Wizara tuna manufaa makubwa na uwepo wa minada kwa sababu inatengeneza soko la wafugaji wetu, licha ya fedha za ushuru ambazo zinazoweza kupatikana katika Halmashauri, lakini nawahakikishia eneo la kuuzia mifugo kwa wafugaji wetu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na aliyeomba mwongozo, nitafika Mwenyewe, mimi Mara ni kwetu kwa babu zangu, nitafika mwenyewe nitajionea na wao Wabunge nitawaarifu watakuwepo pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama itakuwepo ili tuweze kupata jawabu la pamoja lakini tutawanyika na Naibu wangu kwenda na maeneo mengine ya minada ipatayo zaidi ya kumi ambayo ipo mpakani ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Nashukuru kwa Mheshimiwa Mbunge kuleta suala la matatizo yaliyowakumba wanafunzi wetu katika Mji wa Bangalore huko India. Taarifa hizi tumezipokea tangu jana kwamba huko India mwanafunzi wa Sudan alimongoa na pikipiki mwanamke wa Kihindi, baada ya tukio hilo kulikuwa na fujo na vurumai katika mitaa ya Bangalore ambayo ilikuwa inawalenga wanafunzi wa Kiafrika wakiwemo

Waafrika kutoka Tanzania. Vurumai hiyo hasa iliwigusa wanafunzi wa Tanzania wanne, mmoja akiwa ni msichana ambaye alidhalilishwa na vijana wa Kihindi katika mitaa ya Bangalore na wengine watatu waliumia na kupelekwa hospitali. Hatua zilizochukuliwa na Ubalizi wetu pale New Delhi, India ni zifuatazo:-

Hatua ya kwanza, ilikuwa kupeleka dokezo la kidiplomasia kwenye Serikali ya India kuonyesha gadhabu zetu kwa hilo lililotokea kwa wanafunzi wetu wa Kitanzania. *(Makofi)*

Hatua ya pili, ilikuwa kulitaka Jeshi la Polisi la India kupeleka ulinzi mahsusi katika meneo yote ambayo wanafunzi wanaishi ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Tanzania. *(Makofi)*

Hatua ya tatu, ilikuwa kuchukua hatua za Kipolisi ili uchunguzi madhubuti ufanyike kwa lile lililotokea la kuwadhalilisha wanafunzi na kuwapiga na wengine kupelekwa hospitali. Hilo nalo linatokea, Askari wamepelekwa, uchunguzi unafanyika. Hata hivyo, kuna sura nyingine ambayo imetokea asubuhi hii. Kati ya wale wanafunzi waliopelekwa hospitali, tumepata taarifa ambazo siyo rasmi lazima zithibitishwe, kwamba mmoja wa wale wanafunzi amefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunataka kuthibitisha kama hilo kweli limetokea na sasa hivi tunawasiliana na Ubalizi wetu ulioko New Delhi na suala hili liko katika mitandao na vyombo vya habari na sisi kama Serikali tunalifuatilia kwa karibu sana na Serikali ya India, hasa hii sura ya pili kwamba inawezekana mwanafunzi mmoja amefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa. Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa anapewa nani?

**MBUNGE FULANI:** Aliyemaliza kuongea.

**MWENYEKITI:** Haya, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana kwa nafasi hii. Nimekaa India Mji wa Bangalore kwa muda wa miaka minne wakati nasoma Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme taarifa hizi za wanafunzi hawa kuvamiwa na kupigwa nilizipata na hili la aliyefariki nimelipata pia. Nitoe taarifa tu kwanza, aliyefariki siyo miongoni mwa waliopigwa. Aliyefariki amefariki kwa

ajali alikuwa anaendesha pikipiki akaparamiwa na Mhindi jana jana katika eneo la Lulu *market* mitaa ya Kothnur mjini Bangalore, kwa hiyo, siyo miongoni mwa wale waliopigwa lakini na yeye mazingira yake ni ya kutatanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, ifike kipindi kama Serikali itoe tamko rasmi la kuonesha kuchukizwa na unyanyasaji na ubaguzi ambao wananchi wa Kitanzania wanatendewa walioko nje. Watu hawa sisi kwetu hapa tunaishi nao vizuri, tunawapenda sana kama ndugu zetu, lakini wengi wetu ambao wanakaa kule, watoto wetu, wadogo zetu wananyanyaswa sana na kubaguliwa sana. Kwa hiyo, Serikali itoe tamko iseme kwamba inakerwa na kitendo hiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo siyo taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme ni kwa sababu ya jazba na uchungu mkubwa ambao nimepata kwa sababu nimekuwa miongoni mwa wahanga wa masuala haya. Ahsante sana naomba niishie hapo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Serikali mnaipokea taarifa hiyo ya sehemu ya kwanza?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA:** Itabidi tukamilishe taarifa za matukio haya yote mawili, hilo la kunyanyaswa na kupigwa na hilo lingine la huyo aliyefariki. Ubalozi wetu unashughulikia hilo. Lakini ni sahihi kabisa kwamba ni taratibu za kidiplomasia mambo haya yakitokea Serikali lazima itoe tamko lakini tamko ambalo linakuwa lina ushahidi wa kutosha. Hilo halina mjadala. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Sasa nimekataa, naomba uketi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Taarifa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Unanipa mimi taarifa ama Serikali?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kama alivyofanya Mheshimiwa. Mheshimiwa Mwenyekiti.....

**MWENYEKITI:** Ngoja basi, keti kwanza. Mheshimiwa Sugu, kwa kuwa Serikali imekubali kulichukua suala hili wakalifanyie kazi, kama wewe una taarifa ya ziada nashauri tu Serikali ipo, Waziri wa Mambo ya Nje yuko hapa mpatie tu

ili tuweze kwenda vizuri. Suala hili ni zito, naomba tu tulichukue kwa utaratibu huo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Basi Balozi, kwa nini Serikali isim-*summon* Balozi wa India, kwa sababu ukisham-*summon* Balozi ndiyo ile Serikali itajua tuko *serious* kiasi gani, imwite Balozi atoe maelezo kwa Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, sasa tusianze kuingilia kwenye maeneo ya kazi. Serikali kupitia Wizara hii ya Mambo ya Nje wanajua utaratibu wa Kidiplomasia wa namna ya kuwasiliana na Wizara husika. Siwezi kukubali kwamba liwe ni agizo kutoka Bungeni kwamba, haiwezekani siyo kazi yetu sisi. Tumeshafikisha ujumbe huo, Tunaenda mbele. Kwa maeneo yale mawili.

Suala la Mheshimiwa Zitto limeshughulikiwa na suala la Mheshimiwa Heche limeshughulikiwa. Kwa haya mawili niwasomee kwanza Kanuni yenyewe inavyosomeka.

“Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema hapa tumesha-*define*. Nimetoa *ruling* siku hiyo, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge. Lilitokea mapema atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au la kwa mujibu wa Kanuni hizi.”

Kuhusu suala la Mheshimiwa Cecil Mwambe nilisema hata mimi, kiti hakifurahishwi na mpangilio wa kubadilisha badilisha. Hii hamisha hamisha vyama husika, Kambi Rasmi ya Upinzani, Kambi ya Chama Tawala. Wao wana utaratibu wa kujua *rearrangement* ya nani aanze, lakini ndani ya mpangilio ule ule. Wakifanya hivyo wala hakuna tatizo. Lakini ile ya kupangua kabisa ambayo sipendi kuamini kwamba inafanywa na Viongozi wa Kambi kwa maelekezo ya Makatibu wa Kambi hizi mbili.

Natoa mwongozo wangu kwa hilo kwamba jambo hilo haliruhusiwi. Kwa hiyo, tuzingatie utaratibu huo lakini *re-arrangement* ndani ya vyama, nani atangulie ndani ya mtiririko huo, hiyo ni kawaida kabisa, inafanyika hiyo. Ambao hawajaomba, haiwezekani wawemo kwenye orodha. Orodha hiyo inasimamiwa na Katibu wa Bunge, haiwezekani kama wewe hoja iliyo mbele ya Bunge ilipowekwa kwenye *order paper* hukuwasilisha ndiyo itakuwa utoe maelezo ya kutosha kwa nini uwaruke wenzako.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia, kama ulichangia kwenye hotuba ya Rais kama Kanuni inavyosema ni lazima tuwape nafasi wengine ambao hawakupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Rais. Ndio tunakwenda kwa utaratibu huo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, suala la Mheshimiwa Kikwembe kwa sababu Serikali ipo nimesema makusudi kwa sababu ni la Kiserikali zaidi. Mawasiliano yamekatika kati ya Katavi, Tabora na Mikoa ya jirani, sasa yawezekana Waziri wa barabara ukaweza kulitolea ufafanuzi, lakini liko nje ya Kanuni zangu. Inaruhusiwa au hairuhusiwi mawasiliano kukatika, haikukatikia ndani ya Bunge. Lakini Serikali kwa sababu tunahudumia wananchi wetu, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua Serikali inafanya nini katika kuhakikisha mawasiliano kati ya Katavi na Mikoa jirani yanapatikana. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa kipindi hiki cha mvua kali zinazoendelea kumekuwa na ukatikaji wa mawasiliano kutoka sehemu moja kwenda nyingine na pia sasa hivi ni kweli kuna tatizo la mawasiliano baina ya Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Katavi, lakini fimu yetu ya wataalam ya *TANROADS*, iko pale masaa 24 kuhakikisha kwamba tunarejesha mawasiliano hayo kwa haraka. Tunategemea kama mvua hazitakuwa nyingi leo kuanzia kesho magari madogo madogo yataanza kupita kwenye daraja hilo na baadaye tutaendelea kuimarisha daraja hilo ili magari makubwa yaweze kupita haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

#### **TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, haya, tutumie vizuri muda wetu sasa.

**MBUNGE FULANI:** Naomba kutoa taarifa kwa Serikali kwamba hilo daraja limekatika kabisa na hakuna gari linalopita. Sasa kwa nini tusiombe Jeshi la Wananchi ambalo huwa lina madaraja ya dharura lipeleke daraja moja pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali imesikia. Katika yale matangazo, baada ya kutoa ule mwelekeo wa shughuli za Kamati, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, yale mazao niliyoyataja ya biashara pamekuwa na *consensus* kwa Wabunge wa maeneo yote yanayolima mazao hayo kwamba kikao hicho badala ya kuwa saa saba, kifanyike jioni tunapoahirisha Bunge. Eneo ni pale pale ukumbi wa Msekwa. Nadhani hilo limekaa vizuri.

Baada ya hayo, Katibu.

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na shughuli yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Jitu Soni akifuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib na mwingine ni Mheshimiwa Devotha Mathew Minja. Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Babati kwa kunirudisha kwa awamu ya pili kuwa mwakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiongozwa na Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa mwendo na kasi na matumaini mapya ambayo wameonyesha kwa Watanzania wote. Vile vile nishukuru uongozi mzima uliochaguliwa ikiwa pamoja na wewe Mwenyekiti, Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzako na Mawaziri wote waliochaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Mpango, Waziri wetu wa Fedha kwa kuja na mpango mzuri, mpango ambao unaonyesha na umeangalia sekta zote. Mpango huu ukitekelezwa vizuri nina uhakika kabisa kwamba yale malengo ambayo tunayo ya kufikia miaka mitano ijayo na huu wa mwaka mmoja ya kufikia kuwa nchi ya kipato cha kati, tutafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Mpango huu inabidi Serikali ijipange vizuri sana, kwanza kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana kwa kutekeleza yale yote ambayo yamepangwa na ambayo yako kwenye Mpango. Pia Watumishi wengi ambao wako Serikalini kubadilika fikra zao, yaani *mindset change*. Tusipobadilika hayo yote yataendelea kubaki kama yalivyokuwa huko nyuma, mipango inakuwa mizuri lakini haitekelezeki.

Muhimu kuliko yote pia ni kuhakikisha kwamba suala lile la nidhamu kwenye matumizi ya fedha iheshimiwe hasa zile fedha ambazo ni *ring-fenced*. Yale yakiheshimiwa nina uhakika kabisa zile fedha ambazo zimepangwa kwenda kutekeleza miradi mbalimbali itakuwa inaenda. Kwa mfano, miradi ya REA na ule mpango wa maji. Yale pia tutaomba wakati wa majumuisho, basi tupatiwe taarifa rasmi ili tuweze kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu lingine ni kuhakikisha kuwa suala zima la PPP linafanyiwa kazi kwa undani kabisa. Serikali ikubali, hasa wale Watumishi wa Umma wajue kabisa kwamba Serikali haiwezi kutekeleza haya mambo yote yaliyoko kwenye Mpango. Sehemu kubwa hasa huko tunakoelekea kwenye viwanda, viwanda vidogo, vya kati, viwanda vikubwa na hata mambo

mbalimbali ya miundombinu ya huduma, wakishirikiana na sekta binafsi, yaani PPP, tutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ni muhimu Serikali ijipange katika uratibu baina ya Wizara moja na nyingine, ile *coordination* iwe ya hali ya juu. Kila Wizara isiwe na mpango wake, kila Wizara ifanye kazi, Wizara zote zishirikiane ili mpango kama ni wa kutekelezwa basi *coordination* iwe ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kabisa kwamba safari hii, sekta kubwa imelengwa ni sekta ya kilimo. Kilimo kwa mapana yake. Kilimo, mifugo, uvuvi yote hayo yapo kwenye mpango huu. Muhimu naomba tujipange. Kulikuwa na ile ambapo Tanzania ilikubaliana kwenye *Maputo Declaration* kwamba asilimia 10 ya bajeti nzima. Kwa hiyo, bajeti ambayo tunategemea kwamba itapangwa safari hii 10% yake itaenda kwenye sekta hiyo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia asilimia moja (1) ya bajeti nzima pia itaenda kwenye sekta ya utafiti kwa sababu bila utafiti hatuwezi kuendelea. Tukiangalia vituo vyetu vya utafiti vina hali mbaya sana, tukiangalia watafiti wetu wana hali mbaya. Sasa tukiwatengea bajeti, mengi tunaweza kuyafanya humu humu nchini kutokana na mazingira yetu na kutokana na hali yetu tunaweza kwenda tunapotarajia kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu ni suala la kwenye bajeti itakayopangwa hiyo ya asilimia 10 kwenye kilimo, suala zima lile la fedha ya kununua mazao, lisiwe kwamba ni moja katika asilimia inayoongezwa pale. Leo unaambiwa bajeti ya kilimo ni kubwa sana lakini utakuta zaidi ya nusu ya ile fedha inakwenda kununua chakula ya hifadhi. Sasa ile siyo maendeleo ya kilimo ile ni pesa tu imewekwa kwa ajili ya kununulia mazao, hiyo iwe kwenye kitengo tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine muhimu ni nidhamu ya matumizi na matumizi mabaya ya fedha. Ni muhimu sasa tujikite huko. Kila mwaka tunasikia na Wabunge wote hapa wamechangia, reli ya kati, unakuta barabara, kila mwaka fedha ya maafa inatumika kwa mabilioni. Kila mwaka sehemu hiyo hiyo. Ni vizuri sasa wale ambao wanaosimamia hayo maeneo kwa nini wanasubiri tu kwamba haya maafa yatokee kila mwaka wapate hizo fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu naona kwamba, labda ni mradi wa namna ya kula hizo fedha, lakini muhimu ilitakiwa kwamba kama haya mafuriko yametokea sehemu fulani, tukaangalia chanzo chake ni nini, kama ni maji yanatokea sehemu fulani tuweke mabwawa huko juu, maji yasije yakaharibu huku chini ili yale maeneo ya huko juu maji yakivunwa yatumike kwenye umwagiliaji, maji ya kunywa, maji ya mifugo na hii fedha badala ya kwenda kila mwaka kwenye maafa itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka kuna mikoa ambayo tunapeleka chakula cha msaada ni mabilioni ya shilingi, lakini hayo mabilioni ya chakula yanayopelekwa kule kwenye mikoa hiyo, ingepelekwa miundombinu wa umwagiliaji, kuvuna maji na umwagiliaji. Baada ya mwaka mmoja mikoa ile ingezalisha chakula kingi, kuliko hii mikoa ambayo tunapeleka chakula huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la matumizi ya fedha Serikali ijikite, tuangalie maeneo yote yale ambapo tunaweza kubana matumizi. Tuweze kubana lakini kabla ya hiyo bajeti pia natarajia kabisa kwamba sheria ya manunuzi tutakuwa tumeifanyia kazi. Hata tungekusanya mabilioni ya shilingi asilimia yote inakwenda kutumika vibaya kwa sababu sheria mbovu, sheria kandamizi, sheria hiyo ya manunuzi. Nashukuru kwamba, miaka minne nilipigia kelele hiyo sheria, sasa italetwa na naamini Wabunge wote tutashirikiana kwa kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningeendelea kushauri, ni kwamba tumeambiwa safari hii katika ile Sheria ya Bajeti, Maafisa Masuuli wa sasa watakuwa wanapanga bajeti kutoka kila Mkoa, kila Idara. Ni vizuri basi ushirikishwaji wa wadau wote katika kila mkoa, katika kila Taasisi, uanze mapema ili maoni ya watu wote namna ya kwenda, namna ya kufanya ufanyiwe kazi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunaposema tunaanza kuwekeza kwenye sekta nzima hii ya kilimo, ili tuweze kuwa na viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa ni vema tujikite maeneo ambayo tayari yanazalisha. Kwa mfano, sukari kuna maeneo ambayo tunazalisha miwa, kwa mfano kule Babati, lakini utakuta kwenye mpango mpya huu wa kuanzisha viwanda vipya, Wilaya ile haipo. Tunataka kuzalisha labda mafuta ya mawese, utakuta Wilaya husika haijahusishwa, kwa hiyo, vizuri yale maeneo husika yafanyiwe kazi na yawe kwenye mpango kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye suala la namna ya kukusanya mapato zaidi ili Serikali iwe na wigo mpana wa kukusanya kodi. Suala la kutumia mashine za EFD'S tunashukuru na tunasema kila Mtanzania ambaye anafanya biashara atumie mashine ya EFD. La muhimu tulipendekeza kwamba, badala ya kuwa *centralized*, kwamba kampuni chache ndiyo ziruhusiwe kuleta hizo mashine na kusambaza, kila Mtanzania ambaye ana nia ya kuwa na mashine hizo na kufanya biashara hiyo, kwa mfano hapa Dodoma, unaweza kuwa mtu anataka mtaa fulani kama zile za *cable* aweze kuwa na bishara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke viwango vya zile mashine zinavyotakiwa kutumika ili *service* ya ile mashine pia ziweze kupatikana katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi Serikali iangalie namna ya kupunguza kodi na tozo mbalimbali, ili viwanda vya ndani viweze kukua. Leo niwape mfano, kwenye sekta ya mbegu tunaagiza asilimia 75 ya mbegu toka nje ya nchi. Ni kutokana na huko nyuma, ilikuwa asilimia 70 inazalishwa ndani 30 inatoka nje.

Baada ya Serikali kuweka kodi na tozo mbalimbali, kwa wingi tayari sekta hiyo imekufa kabisa leo tunaagiza mbegu kutoka nje, ambayo haina kodi kabisa. Madawa ya mifugo kutoka nje, hayana kodi lakini ukizalisha ndani ya nchi ina kodi. Kwa hiyo, mfumo mzima wa utozaji wa kodi, uangaliwe ili sekta binafsi na sekta zote ziweze kukua ndani ya nchi. Viwanda hivi, kama tusiporekebisha, mfumo mzima na tozo mbalimbali haitakua, na watu hawatawekeza katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maeneo mengine tuangalie mbinu mbadala, tushirikishe watu, kwa mfano, kwenye Sekta ya Uvuvi, tulishapendekeza huko nyuma. Tunaweza kutumia nishati mbadala kama gridi ya Taifa haifiki, katika maeneo ya Pwani, katika maziwa mbalimbali, mahali kuna uvuvi tupeleke nishati mbadala, solar na hii ya upepo, ili wakulima wetu, wafugaji wetu, wavuvi kule wawekewe ghala/friji ndogo ndogo za kuhifadhi mazao yao ili badala ya kuuza samaki kwa vikapu, waweze kuhifadhi hawa samaki, waweze kuwauza kwenye soko ili waweze kupata bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo madini mengi, sasa Serikali ijikite kwa mfano, tuna madini ya *gemstones* vito vya thamani ya chini. Tuna kituo pale Arusha cha Kanda ya Kaskazini, ambapo Serikali ingewekeza fedha za kutosha....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji )*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Hamad!

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Hayupo, ndiyo maana nikaomba nafasi hiyo nichukue mimi. Hayupo Dodoma.

**MWENYEKITI:** Hayupo Dodoma. Umejipangia wewe mwenyewe, haya.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikujipangia, nimekuletea ombi la ruksa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Tukitazama utekelezaji wa mpango wetu kwa muda wa miaka mitano iliyopita na hata mwaka mmoja uliopita, hatupati picha yenye kutia moyo. Ingawa umetokelezwa lakini kuna upungufu mwingi, ambapo kwa mfano kwenye umeme hatukuweza kufikia kiwango ambacho tulikuwa tumejiwekea cha zaidi ya megawati 4000. Kwenye barabara hatukuweza kufanikiwa ni chini ya asilimia 50, kwenye reli kilometa 174 au 75 zilizoweza kukarabatiwa. Pia kwenye *irrigation* ambapo jana kuna mtu mmoja alitoa taarifa, nilikuwa sijui kama tuna *potentiality* ya 20 *million* lakini kitu ambacho kimefanywa katika *target* ya milioni moja, tumefikia *only 23%*, pia Deni la Taifa limeongezeka katika miaka hii kutoka tisa mpaka 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kama Wabunge na kama Serikali tunatakiwa tujiulize wanatupa moyo gani au wanatupa *hope* gani ya kuweza kutekelezwa kwa mpango huu unaokuja, wakati Mpango ambao umemalizika ulikuwa *very much under-performed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwamba Serikali wame-*mention* baadhi ya changamoto katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na wamekuja na *solution* katika ukurasa wa 14, katika baadhi ya changamoto zile imezungumziwa pia sekta binafsi kwamba ni *solution* mojawapo ambayo inaweza ikasaidia ikiwa suala zima la *funding* litafanywa kwa uhakika yaani ugharamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niiombe Serikali kwamba, wakati wakija na Mpango kamili hapo baadaye, waje na andiko ambalo litaelezea hii sekta binafsi itachangia vipi katika Mpango huo ili kuhakikisha kwamba *funding* inapatikana ya kutosha ndani lakini pia kutoka nje, baada ya kuwa na andiko ambalo litaonesha namna gani sekta binafsi itaweza kuchangia katika Mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ningependa pamoja na vile vipaumbele pale vilivyowekwa ambavyo ni vinne, ningependa suala la utawala bora lingewekwa kama mtambuka, kwa sababu tunalo tatizo kubwa la utawala bora ambalo huko mbele tatalizungumzia zaidi lakini katika hatua hii nataka niseme kwamba, sasa hivi Tanzania inadaiwa kuwa kuna suala kubwa la rushwa, inaidaiwa kwamba kuna tatizo la utekelezaji hata wa maagizo kutoka Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, lakini pia kuna madai mbalimbali ya wananchi kunyanyaswa katika sehemu mbalimbali. Kwa hivyo, ili Mpango uwe endelevu na unaoweza kuwa wa uhakika, ningependa katika vipaumbele hivi pia suala la utawala bora lingewekwa katika umuhimu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimevutiwa na Mpango wa Serikali wa kuweka katika yale mambo ya vipaumbele, kuweka miradi ya *flagship*, miradi ambayo hiyo itakuwa ni miradi kielelezi. Hili ni wazo zuri na ningefurahi kama katika wazo hilo katika mradi mmojawapo ambao unaweza kuwekwa au katika miradi ambayo itafikiriwa suala la Zanzibar liwe *incoperative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni Mtanzania lakini nampigia kura Rais wa Tanzania, lakini pia kuna Wazanzibar ambao wanatumikia Serikali, sioni sababu gani Serikali ya Muungano haina *specific project* Zanzibar zaidi ya zile za kukagua kodi tu au za *immigration* ambapo kuna jengo kubwa. Hata hivyo, ningependa nione Serikali, inachangia kwa kuwa na mradi maalum (*specific*) ambao ni wa kutoka Zanzibar, ili Wazanzibar waone kwamba Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo katika miradi ambayo ni ya *flagship*, ningependa tuweke mradi, eneo letu ni dogo la ardhi, miradi ambayo inaweza ikaweka; nilisema juzi mama Waziri ulikuwepo, nilikwambia suala *silicon veiling* tunahimiza katika eneo lile la miradi wezeshi, habari ya TEHAMA. Ni vizuri, tukili-consider suala la *silicon veiling*, Tanzania ina urafiki mzuri na *Bill Gates*, tungeweza kutumia ushawishi wetu wa kuleta mradi kama huu wa *silicon veiling* ambao hauhitaji eneo kubwa sana lakini inaweza ikazalisha eneo kubwa. Mpaka sasa katika eneo letu lote la kanda hii hakuna mahali ambapo pana *silicon veiling*. Kwa hivyo, kwa wazo hilo ningependa tulitumie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ningependa kuona kuwa tunatumia bahari yetu. Tuna masafa ya bahari ya kilomita 1,400 kutoka pembe mpaka pembe ya chini. Nchi kama *Seychelles* nchi ndogo kabisa ambayo ina watu laki moja. Ambayo ina eneo inaingia ndani ya Tanzania zaidi ya mara 2000 wao ndiyo wanaongoza duniani kwa uvuvi, wa pili kwa uvuvi wa samaki aina ya Tuna, sisi tuna bahari hapo hatujaweza kuitumia vya kutosha. Kwa hivyo hili, ningependa lifanyiwe mkazo kwa sababu tuna uwezo mkubwa sana wa kuvuna kutoka baharini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho ningependa tukitumie kama alama ya Tanzania ni *excellence in education*. Tunaweza tukajipanga vizuri, tukaweza ku-*specialize* katika maeneo maalum, zamani nakumbuka niliwahi kusikia, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam masuala ya maji Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilikuwa kina-save *almost* kanda yote hii hapa. Mtu yeyote akitaka kuja kusoma maji anakuja Tanzania. hata katika *East Africa* zamani ilikuwa kuna mgawanyiko, ukitaka kwenda kusoma kurusha ndege unakwenda Soruti, ukitaka kufanya kitu gani unakwenda sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ningependa hili tuli-*concentrate*, nchi kama ya *Cyprus* nimekwenda *Northern Cyprus*, uchumi wake mkubwa

unategemea *education* wamejenga vyuo wame-*specialize* katika maeneo maalum wamejitangaza dunia nzima, wamejitangaza katika kanda mbalimbali, kwa hivyo wao wanavuna sana kutokana na suala zima la *education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka kuzungumzia, nilisema pale nitarudia kwenye suala la utawala bora. Nataka nirudie hili la Zanzibar, kwanza nafadhaishwa sana kuona Mawaziri wetu hapa Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri wa Ulinzi wanakataa, wanakana kama hakuna suala la mazombi na masoksi Zanzibar, inaniumiza moyo sana. Labda kwa sababu ndugu yake, labda kwa sababu jamaa yake, au kwa nafasi yake yeye hajawahi kukutana na mazombi wakamduru au wakamfanyia vitu vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya yakitokea tunakwenda katika Uchaguzi wa Zanzibar ,tunaambiwa kama unarudiwa, lakini ningependa Serikali itazame upya, itazame *implication* za kurudia uchaguzi huo, *socially implication*, 2001 siyo mbali, watu 4000 walikimbia nchi hii wakaenda Somalia. Tutazame *economic implication*, ikiharibika Zanzibar hakuna uchumi Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana alikuwa anazungumza mwenzangu mmoja anasema baada ya uchaguzi hapa hatuji hapa kujadili mpango, tutakuja hapa kujadili namna ya kujitoa kiuchumi. Kukiharibika Zanzibar, mtalii haji Ngorongoro, kwa sababu mtalii anaji-*program* kuja Ngorongoro kisha anakuja Zanzibar. Kuna *security implication*, ikiharibika hali ya Zanzibar hapatakuwa salama katika Tanzania, kuna *stability implication*, hali ya Zanzibar ikiharibika pia hapatakuwa *stable* hapa. Mnapotupeleka sasa hivi kama watu hawapati nafasi yao, uhuru wao, kupitia kwenye Katiba watatafuta kwa njia nyingine. Hizo njia nyingine ndiyo ambazo tunataka kuziepuka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ni *negative public relation*, hivi Tanzania inajijengea sifa gani kwa dunia. Tanzania imekuwa mfano wa dunia, kwamba ni nchi ambayo inaheshimu demokrasia, ni nchi ambayo inaheshimu haki za binadamu, inaheshimu uchaguzi. Kwa nini tunalazimisha kwa Zanzibar, tulazimisha uchaguzi ambao hauna hata mantiki moja. Unarejea uchaguzi ili iwe nini, Tume ile ile, kwa maana ya marefa wale wale, ma-*linesmen* wale wale waliokufungisha mabao manne halafu unarudia uchaguzi ule ule, mnarudia uchaguzi ili iwe nini, tupate suluhu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna haja ya Serikali kukaa kwa maana ya uchumi, kwa maana ya *stability*, kwa maana ya *security implication*, tukae chini tutazame suala la Zanzibar. Kama mnataka kumwokoa Dr. Shein awe Rais lazima utafute njia nyingine. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mara ya kwanza kuongea katika Bunge hili la Kumi na Moja, nilikuwa Mbunge wa Viti

Maalum kwa miaka mitano. Kwa kutambua kwamba wanawake tunaweza bila kuwezesha, nikaenda kugombea Jimbo la Mlimba, na wananchi wa Mlimba bila kujali itikadi zao walinipa kura za kutosha na sasa ni Mbunge wa Jimbo jipya la Mlimba ndani ya Wilaya Kilombero Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, nawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Mlimba Mabibi na Mabwana na Wachungaji na Mashekhe waliokuwa wananiombea bila kujali itikadi yangu, bila kujali dini yangu, na jinsia yangu, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mara ya kwanza nachangia nikiwa Mbunge wa Jimbo kwenye haya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Naomba nijikite kwenye mambo kadhaa, ambayo nikijikita nayo, nikizungumza hapa nitakuwa nawasemea na wananchi wa Jimbo la Mlimba na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango kwa sasa umekuja kama mapendekezo na natarajia haya ninayoongea hapa na Wabunge wengine wanayoyaongea, basi katika mpango kamili unaokuja basi kutakuwa na vionjo ambavyo sisi kama Wabunge tumetoa mapendekezo yetu na mpango wakauchukua ili kwenda kupatikana kwenye hiyo bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Utawala Bora; Hivi ninavyokuambia Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero haijaapisha Madiwani wake, hivi ninavyokuambia Halmashauri zingine zote zimeshaanza kukaa na kuangalia bajeti ili waingize kwenye Bajeti Kuu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero haijawahi kufanya kikao chochote, Madiwani hawajaapishwa, uchaguzi haujafanyika, eti kwa sababu tu kwa kazi tuliyofanya ndani ya Wilaya Kilombero CHADEMA, UKAWA tumepata Madiwani wengi na Wabunge wote tumebeba, sasa ni kigugumizi Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inashindwa kupitia Waziri wa TAMISEMI anashindwa kuruhusu wananchi wa Kilombero wapate Wawakilishi wao. Ni kilio, ni kizungumkuti, hapa hamna utawala bora bali kuna wizi, utapeli, uliokithiri kipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo maendeleo ya Wilaya ya Kilombero yatarudi chini, Wilaya ya Kilombero yenye Majimbo mawili, Jimbo la Mlimba na Jimbo la Kilombero, leo Mbunge Peter Lijualikali, Mbunge wa Kilombero, Waziri wa TAMISEMI ameandika barua, eti asiwe mpigakura ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, *shame!* Hiyo haikubaliki. Sasa, katika utawala bora nataka mtuambie, Wilaya ya Kilombero mnatuweka wapi, tuko Tanzania au tuko nje ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti inayokuja ya Wilaya ya Kilombero itaidhinishwa na nani ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero? Naomba majibu ya Serikali maana hapa hamna utawala bora. Hili ni jambo kubwa sana kama ulikuwa hulijui ni aibu kwa Taifa hili, ni aibu Serikali kujisifu kwamba ina

utawala bora lakini kuna ukandamizaji uliopitiliza, wanatutolea Wabunge wa Viti Maalum kutoka Dodoma eti waende wakaape Kilombero, wanaijua wao Kilombero? Matatizo ya Kilombero tunayajua sisi hawezi kujua mtu mwingine. Kilombero hatuna barabara, Kilombero kuna migogoro ya ardhi, Kilombero hakuna maji, Kilombero pamoja tunazalisha umeme kwenye vituo viwili, Kihansi na Kidatu, lakini vijiji vingi havina umeme. Mnatutaka nini wananchi wa Kilombero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo halikubaliki, katika utawala bora naishia hapa ingawaje kuna mambo mengi, kwa sababu katika utawala bora na haki za binadamu, tulitakiwa tuwe na kituo cha Polisi Kilombero, lakini hakuna Kituo cha Polisi Wilaya ya Kilombero tangu uhuru. Wilaya ya Kilombero Askari wamejibana kwenye kituo cha Maliasili, hivi wakati wa mafuriko Askari wanaogelea kama bata pale, kwenye mpango nataka tujue ni namna gani Wilaya ya Kilombero, tutapata kituo cha Polisi, cha uhakika kilichojengwa na Serikali hii ili wananchi wapate huduma zao na haki zao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mlimba ni kubwa lenye Kata 16, hakuna kituo cha Polisi, Askari wamejibana kwenye kituo kidogo kwenye ofisi za TAZARA. Mnatutaka nini wananchi sisi, mnatutaka ubaya kwa sababu gani, tumewakosea nini, lakini ukiachilia hiyo, pale pale hakuna Mahakama ya Mwanzo. Leo mahabusu wakipatikana ndani ya Jimbo la Mlimba wanawekwa Idete, haki za binadamu zinavunjwa hata miaka miwili, kwa sababu hawana usafiri wa kuwapeleka Mahakamani, hawana Mahakama ya Mwanzo, huu utawala bora na haki za binadamu ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango u-reflect ni namna gani mtatuboreshea katika utawala bora ndani ya Wilaya ya Kilombero na Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi oevu, utawala bora uko wapi? Leo ninavyoongea kuna kesi Namba 161 ya mwaka 2012, wananchi, wakulima na wafugaji wameipeleka Serikali Mahakamani, hasa Wizara ya Maliasili na Mahakama Kuu ikatoa order kwamba wale wananchi wasibughudhiwe kwenye lile eneo la oevu kwa sababu, walivyoweka mipaka kule hawakuwashirikisha wadau na Wizara ilikubali inakwenda kurekebisha mipaka, tangu mwaka 2012 mpaka leo! Leo wananchi wanashindwa kulima kule! Hii njaa itaingia mwaka huu! Watu wanapigwa, wafugaji wanachukuliwa pesa zao! Hawapewi risiti, nimelalamika, nimekwenda kwa Waziri Mkuu, nimekwenda kwa Waziri wa Maliasili, Mkurugenzi wa Wanyamapori, hivi ninyi mnatutaka nini sisi? Kwa nini mnatuonea namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wasukuma wako kule wafugaji na makabila yote ukienda ndani ya Wilaya ya Kilombero Jimbo la Mlimba wapo kule, kuna uchakataji, utafutaji wa gesi, wananchi hawajui! Wanakuja tu na magari yao

wanaondoka kwa nini msitoe taarifa kwa wananchi kwamba mnakwenda kuchakata kule kutafuta gesi na mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Mpango utuambie ni namna gani tunaboresha masuala mbalimbali ndani ya Wilaya ya Kilombero, hususan Jimbo la Mlimba. Najua kuna mradi mkubwa wa upimaji ardhi, kama nilivyoongea na Mheshimiwa Lukuvi, lakini mradi huo pamoja unavyokuja sawa, Wilaya ya Kilombero na Ulanga, lakini hivi sasa wakulima wameshindwa kulima! Mnataka mwaka huu tukale wapi? Mnataka mtuletee chakula cha msaada sisi Mlimba, hatukubali! Aisee muda hautoshi! Mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, balaa! Mnasema eti katika Mpango, Mheshimiwa Mpango naomba unisikie, mnasema tu reli ya kati, mmeisahau TAZARA? TAZARA mnaiboreshaje? TAZARA mnaifanyaje? Wafanyakazi hawalipwi! Reli shida! TAZARA mliijenga kwa gharama kubwa wakati wa Nyerere, leo mnaiua kwa sababu gani? Nataka Mpango u-reflect ni namna gani mtaboresha barabara, reli ya TAZARA, Mpango uzungumzie barabara ya kutoka Ifakara mpaka Mlimba, Mlimba mpaka Madeke-Njombe mtaiboreshaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghala la chakula liko Jimbo la Mlimba. SAGCOT, kuna kilimo kikubwa cha mpunga pale KPL (*Kilombero Planting Limited*), malori yanapita pale yanye tani 30 kila siku yamebeba mchele, barabara hamna! Leo kwenye Mpango hakuna hata ile barabara hamuizungumzii! Naomba mzungumzie hiyo barabara.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. SUSAN A. L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajakuruhusu! Majji! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee?

**MWENYEKITI:** Keti kwanza! Taarifa!

### TAARIFA

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akiendelea kuchangia muda mfupi kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), lakini kwa kutumia Kanuni ya 66, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akitoa ufafanuzi wa jambo, alitamka kuwa Mbunge ambaye ni Waziri...

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiyo naongoza shughuli, nitamwongoza tu, mwacheni tu asemel! Ni Taarifa na ukisimama kwa Taarifa tunajua.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametamka hapa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ambaye ni Mbunge katika Bunge hili na mbele ya maelezo yake ametamka neno ambalo kwa lugha rahisi ni tusi. Wakati akitoa maelezo yake kuhusiana na Halmashauri kuwa Mheshimiwa Waziri alipoandika barua ile ya kukana Mbunge kuwa siyo Mjumbe ambaye ataingia katika Halmashauri na akasema ni “Shame!”.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa...! Labda jamani, tutumie taratibu za kawaida kwa sababu, ninapoongea mimi...!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muacheni amalizie!

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Taarifa yako!

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumpa Taarifa Mheshimiwa Mbunge afute kauli ambazo ni za lugha ya matusi katika Bunge hili na ajielekeze kwenye hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. MBUNGE FULANI:** Kaa chini! Kaa chini!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, Taarifa hiyo unaikubali au vipi?

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa siikubali.

**MWENYEKITI:** Haya, malizia dakika yako moja!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimpe tafsiri kwamba, *shame*, maana yake aibuuu! Kwa Taifaaa! Hiyo ndiyo habari ya sasa. Halafu wewe tuna wasiwasi na uraia wako!

Mheshimiwa Mwenyekiti, linda dakika zangu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ulikuwa na dakika moja tu.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mpango uzungumzie kuhusu barabara ya kutoka Ifakara – Mlimba, Mlimba mpaka Madege, Njombe, hili ni eneo ambalo lina uzalishaji mkubwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mpango uzungumzie masuala ya elimu; leo ninavyozungumza kuna shule moja ya Tanganyika mwaka uliopita hakufaulu hata mwanafunzi mmoja wa darasa la nne! Elimu kule siyo nzuri sana, nitawapa takwimu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji; pamoja na kuwa Wilaya ya Kilombero na Jimbo la Mlimba lina mito 38, ilikuwa mpaka 49 lakini maji hakuna! Naomba Wizara ya Maji ifanye mkakati, sisi hatuhitaji visima, mkaboreshe ile mito, ili tupate maji. Kama inatoa umeme kwa nini maji ya kunywa safi na salama tusipate?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwape vyanzo vya mapato, kimoja tu! Naomba mfanye *pilot area* Dar-es-Salaam kuna umeme, hebu hamasisheni mtu ukienda dukani leo mtu anakuhamasisha, nikupe risiti ya TRA au nikupe ya mkono? Hii hapa ina kodi, hii hapa haina kodi! Hivi ni nani Mtanzania leo atakubali yenye kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wekeni mfano mzuri kwa *pilot area* ambayo ina umeme kwamba, wale wote Watanzania na mtu yeyote atakayenunua kwa risiti ya umeme ile ya TRA, baada ya muda fulani, mwaka mmoja, mnampigia hesabu amelipa kodi kiasi gani halafu mnamrudishia kitu kidogo! Mtaona kama watu hawatadai hizo risiti madukani; hicho kitakuwa chanzo kikubwa cha kukusanya kodi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Awali ya yote niwashukuru akinamama wa Mkoa wangu wa Morogoro kwa kunipa fursa ya kuwa mwakilishi wao. Hali kadhalika nikishukuru Chama changu kwa kuniona kwamba nafaa kuwakilisha katika Bunge hili, bila kuwasahau wapambanaji wenzangu wa ITV. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia vizuri sana Mpango ulioletwa mbele yetu. Yako mambo mengi sana, lakini hakika mambo haya nilikuwa nikijiuliza tu, mikakati na mipango mingi kiasi hiki tunaifanya kwa ajili ya watu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikapata jibu ni kwa ajili ya wananchi na maendeleo ya Taifa lao, lakini hivi tunavyojadili mambo haya muhimu ambayo

yanakwenda kulenga kuleta maendeleo ya wananchi, tukiwa tumejifungia, lakini wananchi hawajui ni kitu gani kinachoendelea, kwa kuzuwia chombo cha umma kutangaza matangazo haya moja kwa moja, naona kama hatuwatendei haki wananchi. Hali kadhalika naona kama tutakwama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mataifa mbalimbali yaliyoendelea ni yale ambayo yametumia vizuri vyombo vya Habari. Mfano Malaysia, ukienda ukimuuliza hata dereva *tax*, *National Goal* ni ipi na ni njia gani ya ku-*achive National Goal*? Watakueleza kwa sababu wako *informed* na wanatumia vyema vyombo vya habari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunakuja na Mpango hapa tunasema ni kwa ajili ya wananchi na maendeleo ya Taifa, lakini wananchi hawa hawana fursa ya kupata na kuelewa tunajadili nini! Tumezungumza mambo mbalimbali ambayo ni ya vyanzo vipya vya mapato, tumezungumza habari ya mambo ya *retention*, lakini mambo hayo hamuoni kama wananchi wangepata fursa ya kufuatilia moja kwa moja kujua na sisi tunafanya nini, ingeweza kutusaidia pengine mipango hii ikaweza kutekelezeka kwa uzuri na kwa haraka zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata taarifa hapa kwamba, TBC Chombo cha Umma ambacho kilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma kwa umma; TBC inasema ni gharama kuendesha matangazo haya ya moja kwa moja! Hata hivyo, tumekwenda mbali zaidi kuangalia mchakato, ukiaangalia *Air Time* kwa TBC kwa kipindi cha saa moja gharama yao ni 7,080,000/=, lakini tukiangalia saa ambazo tumekuwa tukizitumia hapa kuanzia masaa sita mpaka saba kuendesha Bunge *live*. Pia tumejaribu ku-*calculate* kwa vipindi vinne vya Bunge kwa maana ya vipindi vitatu vifupi na kipindi kimoja cha Bunge la Bajeti ambacho ni kirefu, tukapata ni sawa na saa 290 za kurusha *Air Time* na ukizidisha unapata 2.2 *billion* na siyo 4.2 kama tulivyoelezwa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tunakumbuka Serikali, kamera tunazoziona huku zilifungwa na *Star TV* enzi hizo, lakini hivi sasa ikatokea mambo mengine mengine hapo wakasema siyo vema ni lazima taarifa hizi zirushwe na vyombo vya umma. TBC ikajengewa uwezo kwa kupewa bilioni 4.6 inunue vyombo vya kisasa na kutumia kamera hizi ambazo zimefungwa na *Star TV*, lakini matokeo yake hiyo 4.6 haijafanya chochote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii TBC wanakuja na crew ya watu 20 kurusha *live* hapa, kitu ambacho kinaongeza gharama. Hamuoni sasa ni wakati wa kuruhusu hivi vyombo binafsi vifanye kazi vizuri, kuhakikisha vinasaidia kusukuma mipango hii kama TBC imeshindwa? Hamuoni kama sasa ni wakati wa Serikali kupunguza hivi vikwazo kwa vyombo hivi binafsi na kupewa hizi

ruzuku ambazo TBC inashindwa kufanya kazi? Ruzuku zielekezwe kwa vyombo binafsi vifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niende kwenye mipango mbalimbali niliyoiona kwenye kitabu hiki; nimeona habari ya reli, miundombinu, barabara, lakini sijaona mahali popote ambapo tumezungumza jinsi ya kusaidia wananchi ambao wameathirika kutokana na miundombinu hii. Nikizungumzia Kilosa hivi sasa kuna wananchi wanaishi kwenye mahema kwa zaidi ya miaka mitano, wameathirika kwa sababu reli ya kati ilikatika katika eneo la Godegode, tuta la Kidete lilivunjika ambalo nimeona mpango mnalitengeneza, lakini kuvunjika kwa tuta lile ambalo lilisababisha mafuriko kwa wananchi hamjaweka mpango wa kuwapa hata viwanja wananchi leo hii, tangu 2010 wanaishi kwenye mahema, wakiwemo wananchi wa Kidete, wananchi wa Mateteni na wananchi wa Magole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni wakati umefika wakati tunaandaa mipango hii tuwafikirie na wananchi hawa ambao waliathirika kutokana na kuharibika kwa miundombinu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mna mpango wa kufanya Tanzania kuwa ni Tanzania ya Viwanda. Tunavyozungumza hivi Morogoro viwanda vilikuwa vingi, leo hii viwanda mbalimbali vimekufa, lakini hamjatueleza kwamba, viwanda hivi vitafufuliwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda mbalimbali ikiwemo kiwanda cha *Canvas*, kiwanda cha *UNAT* cha matunda ambacho akina mama walikuwa wanatumia kwa ajili ya matunda yao! Leo hii akinamama ndiyo wanaotembea na mabeseni kichwani, haikuwa kazi yao! Kiwanda cha *Asante Moproko*, Kiwanda cha *Ceramic*, Kiwanda cha *Tanarries*, ambavyo vyote hivi vilikuwa vinatoa ajira kwa kiasi kikubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye suala la maji; limezungumzwa kila mahali, lakini Mkoa wa Morogoro ni Mkoa ambao una mito mingi sana, lakini Mkoa wa Morogoro ndiyo unaoongoza kwa kukosa maji. Nikianza katika Manispaa ya Morogoro pekee, ambayo kwa sasa inategemea Bwawa la Mindu ambalo limejengwa mwaka 1984 wakati huo idadi ikiwa ndogo sana; leo hii Serikali imekuja na mkakati mpya wa kujenga Bwawa la Kidete, hatukatai! Imekuja na mpango mpya wa kujenga mabwawa mengine ya Vidunda, hatukatai! Lakini kweli mipango hii ni kwa manufaa ya Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii inatumia mito ya Morogoro ambayo maji yatakwenda sehemu nyingine, sisi wana-Morogoro wenye mito yetu tunabaki bila maji! Nenda katika Manispaa nimesikia majibu ya Naibu Waziri leo asubuhi, Kihonda, Area Five, Kilakala, kote huko hakuna maji japo

anasema kwamba, mpango wa MCC ulisaidia, lakini tunavyozungumza hivi sasa huo mpango wa MCC wananchi hivi sasa ni kuandamana kila wakati wakienda MORUWASA kudai maji! Kwa nini sasa kwa mito hii mingi wasifikirie kujenga bwawa jipya kwa kutumia hii mito yetu iliyopo, ili kuhakikisha kwamba wanamaliza tatizo hili la maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye masuala ya migogoro ya wakulima na wafugaji, nazungumza hili kwa masikitiko makubwa. Hivi karibuni kupitia vyombo vya habari tumesikia jinsi mauaji ya mifugo na wananchi yakiendelea katika Wilaya ya Kilosa na Mvomero.

Hivi karibuni nimetembelea vijiji vya Kunke kule Mvomero, wananchi wa vijiji sita wamechangishwa shilingi mia tano kila mmoja eti kwa ajili ya kufanya *operation* ya kuwaondoa wafugaji. Kazi ya kufanya *operation* ya kuwalipa Polisi ni kazi ya wananchi? Wananchi kila mmoja alitozwa shilingi mia tano ili wawaondoe wafugaji, zoezi ambalo linapaswa kusimamiwa na Serikali kupitia Wizara husika, lakini leo hii wananchi wanaambiwa kama ninyi hamtaki migogoro hii basi wachangie ili wafugaji waondolewe. Hii ni kuendelea kuongeza uhasama katika makundi haya mawili kwa kuwa yote yanafanya shughuli halalli ambazo zinachangia pato kwa Serikali.

Tukirudi kwenye suala la Mpango wa NFRA wa kuuza mazao, hivi sasa Serikali imeanzisha soko la Kibaigwa ambalo linatoa huduma kuwezesha wakulima wa Morogoro, Dodoma na Manyara kufanya biashara ya mazao, lakini hivi sasa wakulima wa Morogoro hawapeleki mazao yao pale kwa sababu ushuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. DEVOTHA MATHEW:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenifanya nisimame hapa kwa siku ya leo, pili nawashukuru wananchi hasa wanawake wa Mkoa wa Morogoro walioniwezesha kurudi tena hapa Bungeni. Nampongeza Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Mawaziri wake. Nampongeza pia Waziri wa Fedha kwa mpango mzuri aliouleta mbele yetu, jambo muhimu naomba utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuhusu daraja la Kilombero, nawapa pole wananchi wa Kilombero na Ulanga kwa tatizo hili lililowapata. Kutokana na tatizo hili naomba kwenye mpango wetu huu unaoendelea tuweze kulipatia kipaumbele daraja la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vipaumbele naanza na viwanda; Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa Viwanda, lakini kusema ukweli viwanda vingi vimekufa, imebaki sana Kiwanda cha Tumbaku. Kiwanda cha Tumbaku ni cha watu binafsi, lakini kinafanya kazi nzuri na kimeajiri sana wanawake, kwa hiyo, naomba kiangaliwe vizuri kwa matatizo ambayo yatakuwepo. Kiwanda cha Nguo na chenyewe kinafanya vizuri, kina matatizo madogo madogo kwa sababu mara nyingi huwa kinatumia kuni, kwa hiyo uandaliwe mpango uangaliwe kusudi waweze kutumia nishati bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vya Morogoro vimekufa, kwa hiyo naomba wale watu ambao wamechukua hivi viwanda waweze kuvifufua kama hawatavifufua wapewe *notice* ya kuvirudisha kusudi viweze kufanya kazi. Viwanda hivi tumesema kuwa kwenye mpango viweze kutumia malighafi ambazo zinapatikana hapa nchini na hasa viwanda vya kilimo, uvuvi pamoja na mifugo. Mambo haya yatapendeza kwa sababu yataweza kuinua kipato cha Mtanzania na kitaweza kutoa ajira hasa kwa akinamama pamoja na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, Mkoa wa Morogoro na hasa Manispaa, bado tuna matatizo ya maji. Miradi ipo ya *Millennia* lakini tatizo la maji bado liko hapa hapo, naomba MORUWASA pamoja na Serikali, Serikali yangu naipenda Mkoa wa Morogoro na hasa Manispaa, waweze kuwapatia maji kama nilivyosema kuwa Manispaa inakua na watu wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro una mito mingi kama ninavyosema, lakini Wilaya nyingi zote, Mji mdogo wa Gairo, Mji mdogo wa Mikumi, Morogoro Vijijini na kwingine kote bado wananchi hawapati maji salama. Wanaoteseka sana ni wanawake, badala ya wanawake hawa ambao ni wazalishaji kutumia huu muda wote kuzalisha, hasa wale ambao ni wakulima wanatumia muda mwingi kutafuta maji. Kwa hiyo, nashauri kwenye mpango huu tuangalie suala la maji na sio Morogoro peke yake ni Tanzania nzima, wanawake wanateseka kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira, hapa nasema sana ajira kwa upande wa vijana. Kulikuwepo na Mfuko wa Vijana, naomba kujua unaendeleaje kusudi vijana wanaohitimu kwenye Vyuo vyetu waweze kupata ajira na kutumia vizuri huo Mfuko wa Vijana. Kwa upande wa Morogoro tuna vyuo Vikuu vingi, ambavyo vijana wanahitimu, kwa hiyo naomba huu Mfuko uweze kuwekwa

wazi pamoja na sekta zote ambazo zinaweza kutoa mikopo kusudi vijana waweze kuelewa, waweze kujajiri na kuanzisha Kampuni zao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa misitu; nchi yetu ya Tanzania hasa na Mkoa wa Morogoro misitu imekwisha, wanakata miti wanatengeneza mkaa. Naomba kujua nishati mbadala, wananchi waweze kuelewa kuwa watumie nini hasa? Kuna mpango huu wa kata mti panda mti, lakini nafikiri licha ya hivyo haujatiliwa maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera hii ya agizo la kupanga miti milioni 1,500,000 kwa kila Halmashauri. Ningeomba mkakati uwepo wazi wa kuangalia ni miti mingapi ambayo inaendelea kukua baada ya kupanda, tusiwe tunasema takwimu tu badala ya kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapato; ili nchi yetu iweze kuendelea naomba sana isimamie mapato ya ndani na mapato ya nje ili kusudi tuweze kupata fedha za kutosha kuendeleza nchi yetu. Kwa upande uanzishaji wa Mji wa kilimo (*The Agricultural Center*) ambayo itakuwa Mkulazi kwa upande Morogoro, naomba mpango huu uangaliwe wananchi hawa wa Morogoro Kusini watafaidikaje na huu mradi wa *Agricultural Centre City* ambao utakuwa Mkulazi, hasa kwa upande wa Wanawake na Vijana ili kusudi waweze kufaidika kwenye huu Mji wa Kilimo ambao utakuwa pale Mkulazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa reli ya kati; kama ni reli ya kati ya ujenzi naomba kweli iwe reli ya kati. Tunavyoelewa reli ya kati inaanzia Dar es Salaam, Tabora mpaka Mwanza, halafu Tabora mpaka Kigoma na michepuko mingine. Kwa hiyo, reli ya kati iangaliwe kujengwa kwa *gauge* ambayo imesemwa ili kusudi wananchi waweze kufaidika pamoja na mizigo iweze kupitiwa kwenye reli siyo kwenye barabara, kwa sababu ikipita kwenye barabara hii mizigo mikubwa inaharibu barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Morogoro, pia tunatumia reli ya TAZARA, naomba iangaliwe kwa sababu kutoka Dar es Salaam kuja Kisaki, mpaka Ifakara, Mlimba, Tanganyika Masagati tunatumia reli hii na Mkoa wa Morogoro ni mkoa wa kilimo, reli hii ya TAZARA inafaa kwa kusafirisha mazao yetu yaweze kuinua Mkoa wetu wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa nishati; kama unavyojua Morogoro kweli ina vyanzo viwili vya nishati ambavyo ni Kihansi pamoja na Kidatu, lakini mpaka sasa hivi vijiji vingi vya Mkoa wa Morogoro havina umeme. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo amejitahidi lakini bado hatujapata umeme wa kutosha, kwa hiyo naomba tuweze kuliangalia Mkoa wa morogoro tuweze kupewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi; kwa upande wa kupima ardhi pamoja na umilikishaji, pamoja na kutoa hatimiliki. Mheshimiwa Waziri Lukuvi amejitahidi na ameanza vizuri, naomba aendeleo kwa sababu upimaji wa ardhi unasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija upande wa Morogoro kwa upande wa wafugaji na wakulima, kwa kweli tuna tatizo kwenye Wilaya zetu za Morogoro hususani Mvemero, pamoja na Kilosa, Morogoro Vijijini na Kilombero wote kwa pamoja, kwa hiyo, naomba tuweze kuiangalia hiyo kusudi tuweze kupima ardhi yote na kuwamilikisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo; nikija kwenye upande wa kilimo, Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa kilimo na wanawake ndiyo wakulima kweli, asilimia 70 ya chakula inayotolewa nchini kwetu inazalishwa na wanawake, kwa hiyo, naomba upande wa pembejeo, kwa upande wa Serikali naomba huu mfumo unaotumiwa wa kutoa ruzuku uweze kuangaliwa kusudi uanzishwe mfumo mwingine kama itawezekana wa kuweka pembejeo mwaka mzima lakini kwa kuweka bei elekezi ambayo kila mkulima aweze kuipata kwa wakati wake anaotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maafisa Ugani; tuna Vyuo vingi vya *LITA*, vya *LITI*, Chuo Kikuu cha Kilimo *SUA*, wanatoa Maafisa Ugani, ninashauri hawa Maafisa Ugani waweze kuajiriwa mara moja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mara ya pili nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ndanda baada ya kuamua kuondokana na boya wa Chama cha Mapinduzi walisema nije kuwawakilisha hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nichangie katika huu mpango, kwanza kabisa kwa kumpa pole Mheshimiwa Magufuli kwa sababu amepokea Serikali iliyorithi matatizo mengi sana katika mfumo wetu wa uongozi, lakini hata hivyo namwamini kwa sababu naamini ataweza kutatua mgogoro wa *UDA*, lakini pia hapa ndani tunategemea kusikia mgogoro wa *Home Shopping Center* umetatuliwa, lakini pia tutasikia *issue* ya makontena nayo imekamilika na waliohusika katika hujuma hizo wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja katika hoja, lakini pia nikiwapa pole familia mbili za ma-suppliers ambao wamefariki katika eneo langu, kuna mmoja anaitwa Muwa Gereji na mwingine Ndelemule, hawa watu walikuwa wanaidai Serikali kwa ajili ya kutoa huduma katika Chuo cha Wauguzi cha Masasi mpaka wamefariki Serikali haijaweza kuwalipa fedha zao na kilichowaua ni presha baada ya kuambiwa mali zao zinazwa walizokuwa wamewekea bondi wakati huo. Tunaomba sasa Mpango huu uoneshe wazi mpango wa waziwazi kabisa wa kutaka kusaidia kuwalipa Suppliers pamoja na Wakandarasi wengine katika maeneo mbalimbali tusije tukawaletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara tunaomba kama ingewezekana basi ungeingizwa ikawa ni ajabu nane katika yale maajabu ya dunia. Kwa sababu Mtwara ndiko ambako sisi kwa kipindi kirefu wakati huo nilikuwa naona hapa akina Mzee Nandonde na wengine wakiwakilisha Mkoa ya Mtwara mengi walikuwa wanayasema lakini yalikuwa hayatekelezwi. Siku za hivi karibuni pamegundulika gesi kule pamoja na vitu vingine, Serikali iliyopita ikaamua kuondoa gesi iletena kwa gharama kubwa sana na kuipeleka kwenda kuzalishia umeme maeneo ya Kinyereze megawati 150 bila kuangalia kwamba tunategemea lini kurudisha gharama za uzalishaji ule ili wananchi waweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mkoa wa Mtwara ndiyo Mkoa pekee ambao una chanzo kikubwa cha uzalishaji wa umeme lakini maeneo mengi ya Mkoa ule hakuna hata umeme. Hata yale maeneo ambayo yamepitwa na umeme kwa nguzo juu ya maeneo yale, kwa mfano ukienda Kijiji cha Chipite, ukipita Kijiji cha Mumbulu, ukipita Kijiji cha Liputu na Majani, lakini pia ukienda katika Kijiji cha Rahaleo pamoja na Liloya, maeneo haya nguzo zinapita juu ya vichwa vya watu. Watu wale waliambiwa wakate mikoroshu yao, watu wale waliambiwa wakate miembe katika maeneo yale wakiamini kwamba siku moja watapata umeme lakini hata hivyo watu wale hawana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Waziri wa Nishati na Madini, asipoviingiza vijiji hivi katika Mpango wa kupatia umeme nitakuwa wa kwanza kushika fungu ili bajeti yake isipite katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme wazi, kule kwetu kuna utaratibu wa kitu kinaitwa stakabadhi ghalani. Ule utaratibu siyo mzuri sana kwa mwanzo, lakini kwa sababu upo na upo pale kisheria ninawashauri watu wa Mtwara tuendelee kuutumia, isipokuwa tunataka marekebisho makubwa sana katika utaratibu ule. Wanakijiji wa Kijiji cha Ujamaa Nagoo, walipotelewa Koroshu zao tani 103 mwaka jana, lakini sheria ya stakabadhi ghalani inasema wazi na nitaomba nii-qoute hapa, kwenye *section 18 sub-section (d)*, lakini pia ukienda kwenye *section 22 sub-section 3* inamtaka mmliki wa ghala, utakapotokea

upotevu wa mali yeyote ya mtu aliyetunza katika ghala lake ndani ya siku kumi aweze kulipa na kufidia vile vitu vilivyopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo sasa hivi lina mwaka mmoja, waliyosababisha ule upotevu wanajulikana, akiwemo Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho ambaye tunamwambia kabisa Waziri wa Kilimo kwamba atakapokuja kwetu Mwenyekiti huyo akiendelea kumuacha hatutampa ushirikiano kwa sababu siyo mtu anayetaka kutusaidia kuliendeleza zao la korosho, isipokuwa amekwenda pale kwa ajili ya hujuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikueleze wazi, Masasi ndiko ambako kulikuwa kuna viwanda vikubwa vya korosho, viwanda vile sasa hivi vimegeuzwa kuwa maghala ya kutunzia choroko na mbaazi, havifanyi kazi iliyokusudiwa ya awali. Tunasema hatutaki, mtakapokuwa mnapanga mpango wenu, mkiamua kifikiria viwanda katika maeneo yetu basi tungependa sana muanzie katika viwanda vile ambavyo sisi tulivizoea, msituletee viwanda vya ajabu, halafu mkaja kutujazia watu kutoka maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kwanza tushughulike na korosho yetu kwa kuanzia, baadaye mtutafutie viwanda vingine vitakavyokuwa na tija, lakini tunafahamu ujenzi wa viwanda vipya ni wa muda mrefu tena wenye gharama kubwa, kwa hiyo kwanza mturudishie vile viwanda vyetu vya asili ambavyo ni Viwanda vya Korosho katika eneo letu visitumike kama maghala kama ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikuambie, Msimamizi Mkuu wa Bodi ya leseni za maghala, amekua akihusika kwa kiasi kikubwa kwa kupokea rushwa lakini pia kuto kutenda haki kwenye utoaji wa leseni za maghala. Namtaka pia Waziri wa Kilimo atakapokuja hapa na mpango wake naye atueleze anataka kufanya nini katika eneo hili, kwa sababu sasa hivi kupata leseni za maghala kule kwetu ni sawa na mbingu na dunia kitu ambacho tunasema hatutataka kiendeleo na tusingependa iendeleo kufanyika hivi, utuondolee yule Mkurugenzi katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nirudi katika eneo lingine katika huu utaratibu wa korosho kuna mchango kule unaitwa *export levy*, madhumuni ya awali kabisa ya *export levy* ni kwa ajili ya kuwagharamia wakulima kuweza kupata pembejeo lakini pamoja na mafunzo. Hizi fedha zinaishia Dar es Salaam ambako hakuna mikorosho, sisi kule tunaoishi na mikorosho fedha hizi hatuzioni. Hata hivyo pembejeo zile hazifiki kwa wakati, tunashauri sasa *export levy* ikishakusanywa ile fedha ipelekwe katika kila Halmashauri na Halmashauri zile zitaamua zenyewe kwa sababu Halmashari zote zinazolima korosho zinatofautiana katika misimu ya ulimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asituletee sisi pembejeo Masasi akatufananisha sisi na watu wa Mkuranga kwa sababu misimu yetu inakuwa tofauti katika maeneo haya. Kwa hiyo, nishauri kabisa *export levy* iende moja kwa moja kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kupanga mikakati na wakulima wake waweze kununua pembejeo kwa wakati ziweze kuwafikia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia pia kitabu cha Mpango, Mpango mzuri sana mmeweka humu ndani, lakini niseme, nina maslahi katika eneo hili. Tuje kwenye suala la usafiri na usafirishaji. Imeguswa hapa katika eneo moja kuhusu reli ya kati, niwapongeze sana Wabunge wanaotoka katika reli ya kati na naiomba Serikali ihakikishe inatekeleza hili kwa sababu reli ya kati ni sehemu kubwa sana ya uchumi wetu sisi wote Tanzania hakuna asiyetambua hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niunganishe, mwaka huu naona hapa tuna bahati tumechajiwa kuhusu reli pia ya Mtwara kwenda Mbambabay imetajwa humu kwenye huu mpango. Tusipiona katika utekelezaji nitakuwa wa kwanza kushika kifungu ili kwanza hili litekelezwe kwa ajili ya maslahi ya watu wa Mtwara na watu wa Kusini kwa ujumla ndipo tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningetaka kuwaangaliza jambo moja, unapokuja Mtwara, unaposema unakwenda kwenye barabara ya uchumi, ile barabara ni ndefu sana inaanzia Mtwara Mjini inakwenda mpaka Newala lakini pia inatokea mpaka Masasi. Inaendelea Mpaka Nachingwea, Liwale, Ruangwa anakotokea Waziri Mkuu ambako leo nimepata taarifa kwa sababu na mimi ndugu zangu wanaishi kule kwamba ukitaka kwenda kijijini kwa Waziri Mkuu hakupitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuseme na yeye anahitaji kupata barabara, ile barabara inakuja kutokea Nanganga, nimeona pale kuna daraja limetajwa na Nanganga Two, ningependa siku moja na Waziri tufuatane tukaangalie vizuri huu mpango tuone kama kweli unatekelezeka hasa maeneo ya Kata za Lukuledi na Kata nyingine hapa katikati watu wengi walichorewa nyumba zao X, sasa waliniagiza nije kuuliza lakini pia kutoa taarifa kwa Waziri wa Ujenzi na Miundombinu kwamba X zile kama hamna matumizi nazo basi tunaomba tukazifute, tutatafuta wenyewe rangi ya kufutia kwa sababu zinawapa watu presha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi waliyo na X katika maeneo ya Dar es Salaam wamekuwa wakivunjiwa nyumba zao. Kule kwetu sisi kuna X, hatuambiwi kama barabara ya Masasi kwenda Nachingwea - Liwale, kwenda Ruangwa mpaka Nanganga itajengwa lini? Haya maneno ya upembuzi yakinifu ninaomba mtakapokuwa mnataja miradi yote inayohusika katika eneo

langu lisitumike kwa sababu nitakuja niondoe kifungu, nataka mnipe tarehe mahsusitutaanza siku fulani, tutamaliza siku fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu nimesikia hili neno toka nikiwa mdogo na maeneo mengi yaliyokuwa yanatumika eneo hili vile vitu pale havitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya pekee niseme kule kwetu tuna madhila mengi sana, ukija kwenye masuala ya kiafya sasa hivi kuna mgogoro mkubwa sana unaendelea katika Hospitali ya Wilaya ya Masasi, ningemtaka Waziri tukutane halafu baada ya hapo nimwelekeze nini pale kinaendelea kwa sababu wakubwa waliopo pale hawataki kuambiwa ukweli na watu walioko chini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Daktari mmoja pale anafanyiwa figisu, anataka kufukuzwa na hii inashirikisha Mkurugenzi wa Wilaya pamoja na Daktari Mfawidhi wa pale, amekuwa akiwanyanyasa wafanyakazi wale kimapenzi, kwa hiyo, naomba Waziri nikuletee taarifa hii rasmi na nitaomba nikae na wewe ili tuliweke hili sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri wa Ardhi sasa hivi Wilaya ya Masasi imeanza kuwa na migogoro mikubwa ya ardhi kuhusu upimaji na mambo mengine, Mheshimiwa Lukuvi hili tutaliongea na bahati nzuri uliniambia ulishawahi kuishi maeneo yale sasa umetaka kuanza kutugombanisha kwa ajili ya udongo wetu hasa zaidi katika Kijiji cha Mtandi na hivi ninavyokwambia hapa ninaomba tafadhali tukae nikufahamishe zaidi nayafahamu matatizo ya lile eneo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa niseme kwamba, Tanzania ni nchi kubwa sana tena ni nchi pana, kwa hiyo tunatamani patakapokuwa panafanyika mikakati na mipango ya maendeleo basi mipango hii ingekuwa inagawanywa kwa mtambuka ili kila eneo angalau kidogo watu waguswe nalo, lakini siyo maeneo mengine yanasahaulika moja kwa moja yatakuja kutuletea shida katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba katika maeneo haya kuna shida kubwa sana ya maji, lakini cha kushangaza kuna bomba kubwa la maji linaloelekea katika Wilaya ya Nachingwea likitokea Ndanda kupitia pale Mwinji. Sasa niseme wazi tunaomba utueleze na mpango wako uje utuambie wananchi wanaokaa juu ya bomba lile kuna mpango gani wa kuwapatia maji katika maeneo yao, kama hili halitafanyika nitawahamasisha tutoboe na tuanze kunywa pale katika eneo letu. Hata hivyo, siungi mkono pale nitakapapatiwa maelezo mazuri kuhusu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (Makofi)

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chalinze kwa kunirudisha tena, lakini kipekee kabisa niendeleo sana kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo kuhakikisha kwamba Wilaya ya Bagamoyo inaendelea kuwa chini ya mikono sahihi ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Taarifa tu niwape wenzangu wa upande wa pili, kwamba Bagamoyo Wilaya nzima iko ndani ya Chama cha Mapinduzi, hatujapoteza Kata wala Jimbo CCM oyee! (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Oyeee!.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo hayawezi kuwa maendeleo bila ya kuwa na maji safi na salama. Katika Jimbo langu la Chalinze kwa kipindi kirefu tumekuwa tunashughulika na mradi wa maji tumejitahidi kuhakikisha kwamba mradi ule sasa umefika katika awamu ya pili awamu ambayo imekamilika, lakini tunapoelekea katika awamu ya tatu nimeona kwamba ndani ya Mpango wa Maendeleo kitabu kizuri kabisa kilichowekwa na Dkt. Mpango kinaonesha kwamba wametenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha mradi wa maji wa Chalinze unafanyika. Ninachowaomba Mheshimiwa Waziri wa Maji atakapofika hapa atuambie juu ya jinsi gani amejipanga kwa kuhakikisha kwamba fedha za mradi ule zinafika haraka ili ujenzi wa awamu ya tatu upate kuanza mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia tunatambua maendeleo hayawezi kuwa maendeleo bila kuwa na viwanda lakini viwanda hivyo lazima vitegemee kilimo ikiwa ni kama sehemu ya kupatikana kwa malighafi hizo. Wamesema hapa wenzangu wanaotokea Tabora kwamba leo hii Tabora ndiyo wakulima wazuri wa tumbaku, lakini kiwanda kinachotegemewa kiko Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri muda umefika wa Serikali yetu kuwekeza nguvu zaidi katika kuhakikisha kwamba viwanda vinajengwa karibu na malighafi hizo ili hii taabu ya kupatikana malighafi ambayo zinasafirishwa muda mrefu isiwepo tena. Hata hivyo, siyo hilo tu ili kuhakikisha kwamba malighafi zinafika vizuri viwandani miundombinu ya barabara zetu na reli ni muhimu sana ikawekwa vizuri. (Makofi)

Niungane na wenzangu wanaozungumzia umuhimu wa kujenga reli ya Kati lakini pamoja na hilo pia reli inayokwenda Tanga ambayo inapita katika mashamba ya mkonge, lakini reli pia ya TAZARA inayopita katika maeneo

makubwa yenye kilimo katika Nyanda za Juu Kusini nazo ni muhimu sana zikawekewa umuhimu katika kipindi hiki cha bajeti hii inayofuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo katika ukurasa wa 31 imezungumziwa kuhusu jambo zima la elimu na afya. Ni kweli Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba inaweka mambo mazuri katika upande wa afya hasa za wananchi wetu wa hali ya chini sana. Niwapongeze sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu na rafiki yangu Dkt. Hamis Kigwangalla kwa kazi kubwa ambayo wamekwishaanza kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango yao mizuri ya kuhakikisha kwamba afya zinaendelea kuimarika katika maeneo ya vijiji vyetu na kata zetu, lakini uko umuhimu wa pekee wa kutambua pia kwamba ziko shughuli ambayo zimekwishaanza kufanyika, mimi nazungumzia zaidi katika Jimbo la Chalinze ambapo karibu vijiji vyote vina zahanafi, lakini pia Kata Nane kati ya 15 zilizopo katika Jimbo la Chalinze zina vituo vya afya.

Sasa ninachoomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa kueleza ni vema akatuambia mpango gani walionao kuhakikisha kwamba vituo vyetu vya afya hivi ambavyo tumevianzishwa vinaendelea kuwa bora zaidi hasa kile cha kiwango ambacho tumenunua vifaa vyote lakini mkakati wa kukamilisha ile pale tunasubiri sana kauli toka kwao kama Wizara husika kwa maana nyingine tunazungumzia lugha ya kuja kukagua kwa hatua za mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo tunatambua umuhimu wa elimu ikiwa ni moja ya vitu ambavyo ni muhimu sana vikaangaliwa. Katika maeneo yetu sisi tunayotoka majengo yetu mengi miundombinu yake ni chakavu sana, ikumbukwe kwamba Bagamoyo ni moja ya Wilaya kongwe kabisa Tanzania ambapo shule zimeanza kujengwa siku nyingi na majengo yake yamekuwa chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokuja kuleta bajeti zetu za Halmashauri hasa katika eneo la elimu katika kuimarisha miundombinu yetu, tunaomba sana Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu mpate kuliangalia hili kwa jicho la karibu zaidi ili tuweze kupata fedha za kuweza kuimarisha elimu hii na vijana wetu wapate kuishi katika mazingira mazuri. Bila kufanya hivyo tunaweza kujikuta tunaibukia katika matatizo ya kwenda kuzika vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa taarifa tu na nitoe pole sana kwa ndugu zangu wanaoishi katika Kata ya Kibindu au Kijiji cha Kibindu shule yetu imeanguka kule yote na vijana wetu zaidi ya 1,100 wako nje mpaka sasa hivi tunapongea. Pia kwa kipekee kabisa niwapongeze wananchi wa Kibindu kwa hatua zao kubwa walizoanza za kuhakikisha kwamba wanajenga madarasa na mimi Mbunge wao nitakaporudi ahadi yangu ya kupeleka mifuko

1,500 iko pale pale ili kuhakikisha kwamba shule ile tunaijenga na wananchi wangu waanze kusoma hasa vijana wetu ambao ndiyo tunategemea kesho waje kuturithi mikoba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nizungumzie jambo zima la uchumi, wananchi wa Jimbo la Chalinze wengi wao ni wakulima na wako baadhi yao ni wafugaji. Tunapozungumzia ufugaji tunategemea sana uwepo wa machinjio yetu pale Ruvu yakamilike mapema sana. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alipata nafasi ya kuja pale, tulimsimulia juu ya ufisadi mkubwa unaofanyika pale lakini pia tukamwambia juu ya mambo ambayo yanaendelea na sisi pale wananchi wa Jimbo la Chalinze ni wakarimu kabisa hasa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka hifadhi ile au *ranch* yetu ya NARCO pale Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie juu ya hatua gani wamefikia baada ya mkutano mzuri tuliufanya pamoja na yeye na wananchi wa Kijiji cha Vigwaza, wananchi wa Kijiji cha Mkenge na wananchi wa vijiji vingine ambao vilio vyao kupitia Mbunge wao nilivisema siku hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo natambua pia upo umuhimu wa kumulikwa na umeme, nishati hii ni muhimu sana, wakati wa enzi za Mheshimiwa Waziri Profesa alifanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba umeme unapelekwa katika vijiji vya Jimbo la Chalinze. Mimi binafsi yangu kwa niaba ya wananchi wa Chalinze nimshukuru, lakini pamoja na hilo mahitaji ya kujengwa na kuwekwa transfoma kubwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi wa Kata ya Mbwele, Kata ya Kimange, Kata ya Miono, Kata ya Msata na Kata nyinginezo zenye mahitaji kama haya hasa Kiwangwa ni mambo ambayo ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anapokuja hapa Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya nishati atuambie juu ya mikakati ambayo wamejipanga nayo kuhakikisha kwamba wanamalizia ile kazi ambayo walikwisha ianza katika eneo la Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua pamoja na hayo pia iko kazi nzuri ambayo tulianza katika awamu iliyopita ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo. Nataka niliseme hili kwa sababu kumekuwa na kauli za sintofahamu zinazotoka kwa upande wa Serikali ambazo zimekuwa zinaripotiwa katika magazeti. Unaweza kuwa shuhuda katika gazeti moja miezi kama miwili iliyopita iliripoti kwamba ujenzi wa bandari ile hautokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nilipata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri akanihakikishia kwamba ujenzi wa

bandari ile upo na nifurahi kwamba nimeiona katika kitabu cha maendeleo. Hata hivyo, wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze na Wilaya ya Bagamoyo hawana raha na wakati mwingine hata wakituangalia sisi viongozi wao wanakuwa wanapata mashaka juu ya kauli zetu hasa kwa kuamini kwamba tunakitetea Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa naye awahakikishie wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo kwamba bandari ya Bagamoyo itajengwa kwa sababu bandari hii ni bandari muhimu na ni bandari ambayo imewekwa pale kimkakati. *(Makofi)*

Serikali ya Tanzania imekwisha fanya kazi yake ya kutathmini na kuwalipa fidia wananchi wa maeneo ya Pande-Mlingotini na Kata ya Zinga. Sasa iliyobakia ni kazi ya wawekezaji wa China na Oman kuja kuweka hela kwa ajili ya kuanzisha uchimbaji na ujenzi wa bandari hiyo. Nitahitaji sana kusikia kauli ya Serikali ili wananchi wetu wa Wilaya ya Bagamoyo wapate amani ya mioyo yao wakiamini kwamba maendeleo makubwa na mazuri yanakuja katika eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo nimalize kabisa kwa kuendelea tena kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chalinze, maana sisi kwetu Chalinze ni kazi tu na kwetu sisi tunafanya kazi kwa ushirikiano, wananchi wanafanya kazi na sisi tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Ahsanteni sana.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge kuna kazi moja ninataka niifanye lakini kwa sababu ya muda nitumie madaraka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) kuongeza muda usiozidi dakika 30, najua hatutafika huko lakini lazima tuzingatie Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwasomee uamuzi wa Spika kuhusu suala la Mheshimiwa Jesca Kishoa linalomhusu pia Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

Tarehe 1 Februari, 2016 wakati Mheshimiwa Jesca Kishoa, akichangia hoja yake Bungeni wakati Bunge limekaa kama Kamati ya Mipango kujadili mapendekezo ya Mpango wa Taifa, unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali katika mwaka

wa fedha 2016/2017, pamoja na mambo mengine alielezea kuhusu mjadala uliokuwepo Bungeni siku zilizopita kuhusu hasara ya shilingi bilioni 238 ambazo Taifa lilikuwa limepata kwa kununua mabehewa feki.

Mbunge huyo alijenga hoja hiyo akirejea ripoti ya PPRA ambayo alidai ililetwa kwenye Kamati ambayo yeye ni Mjumbe. Aidha, aliendelea kudai kuwa licha ya mabehewa hayo kuwa feki hata kampuni ambayo ilipewa tenda kuhusiana na ununuzi huo haikukaguliwa, yaani haikufanyiwa *due diligence*.

Kufuatia hasara hiyo Mheshimiwa Jesca Kishoa alielekeza moja kwa moja shutuma zake kwa aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi wakati huo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa maneno yake mwenyewe alisema nanukuu:

“Taifa limeingia hasara ya bilioni 238 kwa sababu ya mtu tu kuwa mzembe kuwajibika, halafu leo jipu linahamishwa mkono wa kushoto linapelekwa mkono... Magufuli alitumbue na jipu limo humu ndani, tunaye Mheshimiwa Mwakyembe lete ripoti hapa kuhusiana na masuala ya mabehewa, mlikataa kuileta hapa kwa nini mnaificha, kama ni safi. Mheshimiwa Mwakyembe umeaminiwa na Serikali ya Magufuli, lete ripoti hapa tusijisahaulishe haya mambo tunayakumbuka tuliona hata tukiwa nje.” Mwisho wa kunukuu.

Kutokana na shutuma hizo mara tu baada ya Mheshimiwa Daniel Nsazungwanko Mbunge, kumaliza mchango wake, Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe alisimama kuhusu utaratibu chini ya kifungu cha 63(3) ambayo inasomeka:

“Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka kuhusu utaratibu na baada ya kuruhusiwa na Spika kudai kwamba Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uwongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni”. Mwisho wa kunukuu.

Baada ya kuruhusiwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria aliithibitishia Kamati ya Mipango kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliponunua mabehewa 204, haijawahi kutumia zaidi ya shilingi bilioni 60 na alimtaka Mheshimiwa Jesca Kishoa aithibitishie Kamati ya Mipango yaani Bunge, kuhusu madai aliyoyatoa kwa maneno yake alisema:

“Mimi ninaomba athibitishie hizo shilingi bilioni 238 na nitashukuru sana akileta hapa hiyo mimi nitajijuzulu hata Ubunge”. Mwisho wa kunukuu.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alimtaka athibitisha na alete ushahidi wake, hapo ndipo malumbano yaliendelea kati ya Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, huku Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Vijana na Walemavu Mheshimiwa Jenista Mhagama wakiingilia kati baada ya kuruhusiwa na Mwenyekiti kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi sahihi ya Kanuni ya 63(3) na 63(4), baada ya kuwasikiliza wote hao Mwenyekiti alirejea uamuzi wake aliutoa awali na kusema nanukuu:

“Kiti kimeshatoa maelekezo naomba tusibishane, mimi nimesema kulingana na Kiti nimetoa maelekezo na nafuata Kanuni. Nimesema Mheshimiwa Jesca *within three days* naomba uwe umetoa ushahidi.” Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maelezo mafupi ya jinsi mtiririko mzima wa jambo hili ulivyokuwa. Mpaka sasa hivi ninavyoongea hakuna ushahidi wowote uliopokelewa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Kishoa kuthibitisha kauli yake aliyotoa siku ya tarehe 1 Februari 2016 kuhusu gharama zilizotumika kufanya manunuzi ya mabehewa hayo.

Kanuni ya 63(6) inaelekeza kwamba endapo Mbunge anatakiwa kuthibitisha ukweli juu ya jambo lolote atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo. Aidha, kanuni ya 63(8) inaelekeza kuwa na ninanukuu:

“Endapo hadi kufika mwisho wa muda aliopewa Mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na kama atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake, basi Spika atamuadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi vitano”. Mwisho wa kunukuu.

Hivyo basi, kwa maelezo haya, namtaka Mheshimiwa Jesca Kishoa afute kauli yake aliyotoa alipokuwa akichangia siku ya tarehe 1 Februari, 2016. Mheshimiwa Jesca!

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme tu kwamba sitafuta kauli niliyoisema kwa sababu Mheshimiwa Mwakyembe mwenyewe hajathibitisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushihi uketi. Mheshimiwa kwa kuwa, Kanuni hii inanitaka kumsimamisha Mheshimiwa Mbunge kwa siku zisizozidi tano na kwa kuwa tumebakiwa na siku mbili tu kabla ya kumaliza Mkutano wa Pili wa Bunge hivyo basi, namsimamisha Mheshimiwa Jesca Kishoa kutohudhuria vikao viwili

vya Bunge vilivyosalia kuanzia sasa hivi, naomba utoke nje, nakutaka utoke nje.  
(Makofi)

*(Hapa Mheshimiwa Jesca D. Kishoa alitoka nje ya  
Ukumbi wa Bunge)*

**WABUNGE FULANI:** Muongo huyo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

### **KAMATI YA MIPANGO**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli yetu. Orodha ni ndefu bado, lakini tutaendelea kutenda haki tu kulingana na matakwa ya Kanuni. Tunaanza na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, atafuatwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae. Mheshimiwa Marwa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama katika Bunge hili Tukufu siku ya leo. Kwa umuhimu zaidi nawashukuru sana wapiga kura wangu, wanawake wa Mkoa wa Mara, walionipigia kura nyingi sana za kishindo hadi leo hii kuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru kwa upekee mama yangu mzazi na baba yangu, pamoja na Mashirika ya Kikristo yaliyonifanyia maombi, pamoja na Mashekhe na wanamaombi wote na watu wote wa Mkoa wa Mara waliokuwa wanafurahia leo hii niwe Mbunge. Nawashukuru sana, nawachidi sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kunukuu kidogo Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sababu sikupata nafasi ya kuongea siku ile. Kwa ruhusa yako naomba ninukuu. Hotuba ya Mheshimiwa Rais iliwakumbusha watumishi wengi wa umma ambao wengi walijisahau wajibu wao, hivyo aliwakumbusha

watumishi wengi kuwajibika kwa umma kwa taaluma na weledi kwa kuzingatia usawa bila upendeleo kwa watu wote, bila kujali itikadi ya vyama na dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, nampongeza Mheshimiwa Rais Magufuli kwa hotuba yake ambayo imehimiza kuzingatia kanuni na maadili ya utumishi wa umma (*integrity*). Hivyo basi, kwa hotuba hiyo nzuri ya Mheshimiwa Rais tunatarajia kwamba kila mtumishi mahali pake pa kazi atimize wajibu wake ipasavyo na kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza ndoto na matarajio ya Watanzania walio wengi hasa wa kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza moja kwa moja kwa kuongelea au kuchangia kwa suala la ujasiriamali. Wajasiriamali au ujasiriamali ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe kwa macho ya ziada, kwa maana katika Mpango wa Taifa au Mpango wa Maendeleo, wajasiriamali ndio wanatoa mchango mkubwa sana kwa Taifa hili; na haswa naanzia na akina mama wa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wa Mkoa wa Mara ambao wanafanya biashara ndogo ndogo, ikiwemo wafanyabishara wa dagaa, ikiwemo wale wanaouza mboga mboga na wengine wa masokoni wananyanyasika sana kutokana na kutozwa ushuru usiokuwa na sababu. Kwa hiyo, naomba tuangalie sana hawa wajasiriamali kwa macho ya huruma, kwa maana na wao wanatoa mchango mkubwa sana katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niende kwenye suala la maji. Suala la maji limekuwa ni ni kilio cha kudumu katika Taifa hili la Tanzania. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangazie sana macho yake na itoe kipaumbele katika suala la maji, kwa maana suala la maji limesababisha matatizo na majanga makubwa hasa kwa wanawake wetu wa Mkoa wa Mara, kwa kuvuruga au kuachanishwa kwa ndoa zao kutokana na umbali mrefu wanakwenda kutafuta maji. Vilevile limekuwa likiwasababishia ulemavu wa migongo, limekuwa pia likiwaletea shida sana katika uzazi. Kwa hiyo, kwa namna ya kipekee sana liangaliwe suala la maji na hasa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia naungana na Waheshimiwa walioongea jana, Mheshimiwa Zitto Kabwe pamoja na Mheshimiwa Lugola, kuhusiana na suala la reli. Ni kweli katika mazingira ya kawaida, utaratibu ambao unatakiwa katika kuunganishwa kwa reli ili nchi ya jirani au ndugu zetu wa jirani wapate unafuu, ni kitu ambacho siyo kizuri sana, kwa sababu kwanza itatupotezea sisi Pato la Taifa na wao kwa ujanja wao, wanachotaka kukifanya ni kwamba wataunganisha kule juu kwa juu nchi nyingine ili malipo haya yasije Tanzania. Kwa hiyo, hilo suala liangaliwe au lipewe kipaumbele, liwe kama lilivyoongelewa na Mheshimiwa Zitto au Mheshimiwa Lugola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie sana suala la polisi kuhusiana na makazi au vituo vya kazi. Vituo vya kazi na masuala ya makazi ya polisi wetu imekuwa ni shida sana. Hivyo, Serikali ingechukua taratibu za ziada ili iingie mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa ili kuwajengea nyumba za kudumu hata baadaye watakapomaliza kuzilipa ziwe za kwao hata pale wanapokuwa hawapo kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu wa upinzani, tumtie moyo Rais wetu Mheshimiwa Magufuli. Ameanza vizuri. Siyo kila kitu tunaongea maneno machafu, maneno ya kashfa, maneno ya dharau, kiasi kwamba hata wewe ukiombwa kitu huwezi ukakubali kama mtu ameongea maneno ya dharau. Hata Mwenyezi Mungu anatoa pale unapomsifia; ndiyo maana unasema; “Baba yetu uliye Mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimie, utakalo lifanyike duniani kama mbinguni,” ukimaliza unampiga kibao Mungu, halafu ndiyo unamwomba, “utupe riziki yetu ya kila siku.” Siyo ninyi kila siku mnatoa matusi tu. Kesho msipofanyiwa maendeleo mnalalamika.

Ndugu zangu Wapinzani nawaomba sana; mmefanyiwa mambo mengi sana kwenye Majimbo yenu kuliko hata sisi wa CCM. Mfano ni Arusha au Mkoa wa Kilimanjaro, uko wazi kabisa, mmefanyiwa mambo mengi mazuri, hata barabara mlizonazo ni kama barabara za Kimataifa, mikoani kwetu, hatuna. Mnatakiwa muwe na Shukurani, lakini pia mnatakiwa mkubali kwamba aliyeshinda, kashinda, ninyi mmeshindwa. *(Makofi)*

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii. Kwa kuwa siku ya leo ni siku yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuipata nafasi hii ya kuwawakilisha akina mama wanawake wa Mkoa wa Rukwa. Mwenyezi Mungu, nakushukuru sana.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote, napenda kuwakumbusha kuhusu hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Magufuli. Kwa kweli hotuba ile ilikuwa ni hotuba ambayo imesheheni kila upande wa Tanzania hii na kila Jimbo la Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba niwakumbushe ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi kwamba, daima mtoto huwa anapiga madongo ya kila aina kwenye mti wenye matunda au mti wenye neema kwao. Mtoto hawezi kutupa madongo yoyote kwenye mti ambao hauna kitu. Kwa hiyo, haya madongo tunayoyapata kutoka upande wa pili, ni ashirio tosha kwamba mti wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake imefanya kazi. Hivyo sasa tunahitajika tukaze buti ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, katika hotuba ya Rais iliweza kugusa kila eneo ambalo kwa namna moja au nyingine limegusia hatua ambazo zinahitajika kufikiwa kwa wananchi wetu wa Tanzania. Sasa basi, kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameshabainisha nini ambacho anachotakiwa kufanya kwa wananchi wa Tanzania ili waweze kupata uchumi wa kati; kwa hiyo, hatuna budi kumuunga mkono na kuifanya kazi hii ili iwe na maendeleo kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Ndugu zangu, leo tuna shughuli ya kuzungumzia juu ya Mpango wetu wa kazi ambayo tunahitajika kuifanya ndani ya mwaka 2016/2017. Mpango huu ni mzuri, ni Mpango ambao umeainisha nini ambacho Chama cha Mapinduzi imesema itafanya ndani ya miaka yake mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, Mpango huu umeona tatizo ni nini? Mbona maendeleo yetu hayakamiliki? Imebainika kwamba tatizo ni mapato. Sasa Serikali imeelekeza kukusanya mapato na hatimaye kuyarejesha mapato hayo kwa wananchi kwa maendeleo yao. Hilo ni jambo zuri na tunaomba tuliunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulizungumzia suala la afya. Tuliamua ndani ya Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015 kuweka zahanati katika vijiji vyote na kazi hiyo wananchi wameweza kuunga mkono na kujenga hizo zahanati. Tatizo, zahanati hizi haziko katika ramani inayofahamika, kila kijiji wamejaribu kutengeneza zahanati kufuatana na nguvu ya mapato waliyokuwanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake tumepata tatizo kubwa katika zahanati hizi kwa sababu eneo la kujifungulia limewekwa karibu na eneo la OPD, limewekwa karibu na eneo ambalo watu wa kawaida wanasubiri madaktari, ndipo palipo na chumba cha kuweka akina mama waende kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri wa Wizara inayohusika, kazi ile ya kujifungua akina mama wana kazi pevu na bora iwe usiku kuliko ikiwa mchana. Mifano tunayo, zahanati ya Kisumba, kwa kweli ile ramani siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba katika Mpango wetu uainishe dhahiri nini watafanya katika suala zima la kuhakikisha wanatembelea ama wanaweka mpango mkakati wa kuhakikisha ramani zilizotengenezwa hivi sasa ziboreshwe ili akina mama tupate eneo la kuifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, zahanati nyingi hazina vitanda vya kuzalia, hakuna vyumba vya kupumzikia, kwa maana ya kwamba hakuna

vitanda vya kupumzikia. Tunaomba tupate vitanda hivyo. Siyo hilo tu ndani ya afya, zahanati zetu nyingi hazina umeme. Pamoja na kwamba kuna umeme wa REA, lakini bado hawajaunganisha kwenye zahanati zetu. *Solar* zilizopo zimeharibika na hakuna mtu tena wa kutengeneza zile *solar*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuunganishwe na umeme wa REA, katika zahanati zetu zote. Siyo hilo tu, maji hakuna kwenye zahanati zetu. Tunaomba Mpango Mkakati wa kuhakikisha kwamba zahanati zetu zinapata huduma ili akina mama waweze kujihifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu suala la elimu. Tumeamua kuboresha elimu yetu na iwe elimu bora, lakini kuna maeneo ambayo tumeanza kuweka utaratibu wa watoto wetu waweze kujifunza teknolojia ya kisasa, kwa maana ya kwamba wamepeleka *computers* katika shule zetu za sekondari. Naomba mipango iwekwe ya kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza, mfano Sekondari, darasa lina watoto 40, lakini kuna mikondo miwili; na mikondo hiyo miwili ni watoto 80, zinapelekwa *computer* 10 ambazo hazitoshelezi. Naomba tuliangalie hilo katika utaratibu. Mifano tunayo, pale Sumbawanga kuna shule za sekondari za Kizito na Mazu wana *computer* 10 na watoto wako 80, watafanya nini wakati wa mitihani yao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni barabara. Maendeleo ya huduma za jamii katika Mikoa ya pembezoni tumekuwa nyuma. Mimi nasikitishwa sana ninaposikia wenzetu wenye barabara, wanaongezewa barabara za juu, wanaongezewa barabara ziwe sita, wapite barabara watu sita. Kwa kweli mimi nasikitishwa sana kwa suala hilo. Maadamu tumeamua kwanza tuunganishe Wilaya, tuunganishe Mikoa, zoezi hili ndugu zangu bado halijakamilika. Sasa kama halijakamilika, huyu aliyekamilika kuongezwa na katika Wilaya zake zimeunganika, Mikoa ya jirani ameunganika; nchi za jirani ameunganika; kwa nini aongezewe tena mradi wa barabara? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuelekeze Mkoa wa Rukwa. Hatujaungana na Katavi, hatujaungana na Kigoma wala na Tabora. Nawaomba ndugu zangu, huo Mpango uje ukionyesha mikakati, tunajitengeneza vipi kuhusu hizi barabara kuweza kuunganika? Vilevile Mkoa wa Rukwa, tumeungana na nchi ya Zambia barabara haijakamilika, nchi ya Zaire bado barabara haijakamilika. Tunaomba sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, tuna mradi mkubwa sana pale Mkoa wa Rukwa karibia shilingi bilioni 30, lakini mradi ule bado haujakamilika, bado pale mjini watu wanahangaika na maji; bado vijijini vya jirani

vinahangaika na maji, tuanomba Mpango unaokuja, huo mwezi wa tatu, uwe umekamilika ili na sisi tuweze kupata maji katika Mkoa wetu wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi, tunaomba wataalam wa upimaji wa vijiji, hawapo wa kutosheleza na hata vifaa vyake havipo vya kutosheleza. Tunaomba tuhesabu ili tuweze kukamilisha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Sasa namwita Mheshimiwa Matiko, akifuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Awali ya yote, nachukua fursa hii ya kipekee kabisa kuwashukuru wananchi wa Tarime Mjini, kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe kuweza kuchagua mwanamke tena kutokea Chama cha Upinzani. Wameudhihirishia ulimwengu kwamba wamechagua mtu ambaye atawasemea na kuwatumikia na siyo jinsia. *(Makofi)*

Vilevile nawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mara kwa kuonesha kwamba wana imani kubwa na UKAWA; na CHADEMA wote mtakumbuka kwamba Bunge lililopita alikuwepo Mbunge mmoja tu wa kuchaguliwa, lakini sasa hivi tupo Wabunge wanne kutoka Mkoa wa Mara licha ya dhuluma nyingi nyingi, lakini nafikiri CCM mmeisoma namba kidogo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuchangia na nianze na utawala bora. Kwenye utawala bora, wakati wa uchaguzi yalijitokeza mambo mengi sana. Cha kusikitisha, hata Mheshimiwa Rais Magufuli alisema uchaguzi umeisha na mambo yameisha; lakini mpaka leo wale ambao wanaonekana walikuwa washabiki wa vyama vya upinzani, wameendelea kunyanyasika, wanakamatwa na wanabambikiwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea hili nikizungumzia Jimbo langu la Tarime Mjini. Kuna wananchi wamebambikiwa kesi, wengine wamepewa *murder case* ya binadamu ambaye anaishi na ameenda akasema kabisa huyu

mtu sijawahi kukosana naye na wala sijafa na nipo hai. Huyu anaitwa Charles Kitela Chacha na amepewa mashitaka ya *murder* mwenye PI No. 37/2015. Utawala bora uko wapi? Mtu ambaye wanasema ni Marehemu ameuawa anaitwa Wambura Ryoba Gucha, yupo hai wa Kijiji cha Turugeti, Tarime. Tunaomba muwe na utawala bora ili haki itendeke; na kama tutaenda kwenye demokrasia na uchaguzi muweze kupata haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Chama tawala kinasikitisha. Mnapoona wapinzani wameshinda, mnawawajibisha watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninavyoongea, Tarime, Watendaji wanawajibishwa, walimu wanasumbuliwa, RPC amehamishwa, OCD amekuwa *demoted* kisa Mheshimiwa John Heche kashinda Tarime, Mheshimiwa Esther Matiko ameshinda Tarime; Halmashauri ya Mji wa Tarime upo CHADEMA; Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, upo CHADEMA. Utawala bora upo wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata watu wakisimama hapa wakaongea yanayotokea upande wa pili, nami nikipata muda baadaye nitazungumzia, mnabaki mnaona kwamba wanaongea ndivyo sivyo mjichunguze, mwitendee haki Tanzania. Tunataka amani, tusiimbe amani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine sasa nichangie kuhusu uchumi na viwanda. Tumekuwa tukishauri; Bunge lililopita nilikuwa Waziri Kivuli wa Mipango na kwa bahati nzuri sana ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mpango alikuwa akituletea. Atakuwa ni shuhuda na amekidhihirisha hiki ambacho naenda kuongea kwamba mnapanga vitu bila uhalisia. Hiki kitu ambacho tunasema uchumi na viwanda hakiwezi kufanikiwa kama tunapanga vitu bila uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Tunajua kabisa ili tuweze kuwa na uchumi na viwanda ni lazima tuwe na barabara ili hata wale wazalishaji, wakulima waweze kusafirisha mazao yao na kufikisha kwenye viwanda. Lazima tuwe na reli imara, lazima tuwe na umeme, maji na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara ukiangalia ukurasa wa 27 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mnatuambia kipengele cha pili ujenzi mpya wa barabara zenye urefu wa kilometa 5,427 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilometa 1,055 kwa kiwango cha lami. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mnaweza mkajenga kilometa 5,427 iwapo kwa miaka mitano mmetujengea kilometa 2,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhalisia gani? Ndani ya mwaka mtajenga Kilometa 5,400! *Let's be realistic!* Ndiyo maana leo tutapoteza nguvu nyingi kuwashauri hapa; tutapoteza fedha nyingi za Watanzania, mnachokiandika hakioneshi uhalisia. Kwa hiyo, naomba kabisa, tuwe tunaonesha uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmeainisha reli nyingi, nyingi! Mimi natokea Kanda ya Ziwa na ningependa kabisa reli ya kati iweze kukamilika ili tuweze kupunguza ajali. Siyo tu kukuza huu uchumi wa viwanda ambao mnasema; jana walisema hapa miundombinu ya barabara haichangii vifo, lakini kiuhalisia tunapoteza nguvu kazi ambazo tumezisomesha, wengine ni ndugu zetu ambao ni wajasiriamali wa kawaida, wanakufa barabarani kwa sababu ya barabara mbovu. Malori yanapita hapo hapo, ajali nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imarisheni reli ili tusafirishe kwa reli. Kwanza tunakuza uchumi lakini hatutapoteza Watanzania. Ninachokiona mmeainisha hapa, tutarudi hapa mwezi wa sita mwakani, mtaanza kusema hatukupata fedha na asilimia nyingi za maendeleo zilikuwa zinatoka kwa wahisani; na sijui sekta binafsi; tutaanza kuimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bora mwandike mtajenga kilometa 300 za lami tutawaelewa, kuliko kutuandikia 5,400 halafu tunakuja hapa mwakani hamjafanya chochote. Tunapenda sana Watanzania tuwe na hiyo mnayosema uchumi wa viwanda; tunapenda kuona Watanzania wengi wakiwa kwenye uchumi wa kati na siyo wachache wapo juu, wachache ni masikini wa kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na uchumi wa viwanda nimeshataja. Kuhusu kilimo chetu; zaidi ya 70% Watanzania tunajishughulisha na kilimo, lakini kilimo ambacho hakina tija. Ie kauli mbiu ya kilimo kwanza tumeimba, tumeicheza hakuna mafanikio. Mkisoma ripoti zenu zenyewe kuhusu kilimo inaainisha dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni shida ingawa mmesema Mpango ulioisha umekamilisha kwa 68% vijijini na 95% mjini. Ndiyo maana nasema tuwe wakweli. Leo kule Tarime Mjini ukiyaona maji utafikiri ni ubuyu, tuje na uhalisia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni kwa wastaafu. Mwaka 2015 tulipitisha tukasema walipwe shilingi 100,000/=, lakini kuna watumishi tena Mapolisi ambao mnawatumia sana, wanalipwa shilingi 20,000/= mpaka leo. Sasa mlipokaa hapo mjiulize, hawa Watanzania wanaishi vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni Mheshimiwa Magufuli alisema na hata kwenye *Star TV* mlikuwa mnarusha sana; ushuru wa kero kwa

maana mboga mboga, matunda, mama ntilie na wengine wote mnaenda kuondoa. Leo Watanzania hawa wananyanyasika; na alisema pia mgambo watatafuta kazi nyingine. Mimi nasema mnisikilize na mwondoe wale mgambo kwenye Jimbo la Tarime Mjini. Watanzania wote, wamama, wababa, vijana wanaojitafutia wamachinga, mlisema ushuru mdogo mdogo mtaondoa. Tubuni vyanzo mbadala tusiwakamue hawa ambao wana kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure, mimi naomba msemi mmepunguza makali ya elimu, lakini siyo elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mchache, nimalizie kwa Zanzibar; ingawa watu walisimama hapa wakasema sisi wa Bara tusizungumzie ya Zanzibar. Kiukweli tujichunguze, kiuhalisia, tena nianze na Mheshimiwa King siku ile alisema kwamba maiti walipiga kura. Kama maiti walipiga kura, ajiulize na yeye huyo maiti alipiga kura tano. Yeye kama Mbunge wa Jamhuri amefuata nini hapa na yeye alipigiwa kura na maiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni sawa na kumwambia muislamu, umepika kitimoto, umechanganya na kuku, unamwambia achukue kuku, aache kitimoto, wakati ile supu yote imechanganyikana. Mmechambua kuku ambao ni wale Wabunge wa Jamhuri na Rais, mmeacha wale Wawakilishi kwamba ndio kitimoto. Jichunguzeni! Kama ni maiti alipiga kura, amepiga kote. Tutendee haki Watanzania wa Zanzibar, tusiingize nchi kwenye machafuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi. Mmeainisha mtapima ardhi, tunaomba mfanye hivyo. Ardhi imepimwa kwa 10% tu, kule Tarime Mjini tunahitaji mpime ardhi ili tupate thamani tuweze kukopa na kujishughulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Mheshimiwa Magufuli kwenye kampeni alisema atatoa shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji na Mtaa. Sijaona mmeainisha; naomba mwainishe, wananchi wa Tarime mimi nina Mitaa 81, ili tuanze kuzipata hizo shilingi milioni 50 kuanzia mwaka huu wa fedha, tuweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii japo kwa ghafla.

**MWENYEKITI:** Niichukue hiyo nafasi nimpe mwingine?

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Aah okay, aah usimpe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini kabla ya kuchangia Mpango kuna jambo naomba niliweke sawa, japo nilitamani sana Mwanasheria Mkuu angekuwepo tukaenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya (1) naomba niisome, inasema: "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano." Kwa hiyo, sisi hapa kama Wazanzibari tumo ndani ya Tanzania na ni Watanzania. Hakuna Mzanzibari kwa mujibu wa Katiba kwa sababu Tanzania ni dola moja tu, wala Zanzibar siyo dora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaposema Wazanzibari wakatatue matatizo yao, huo ni ubaguzi ambao umekatazwa na Katiba. Haiwezekani tatizo linatokea Arusha, mkasema kwamba tatizo hilo ni la Waarusha tu, haliwahusu watu wa maeneo mengine; linawahusu Tanzania nzima. Kwa hiyo, hili naomba niliweke sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili watu wanasema kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haihusiki kabisa na masuala ya Zanzibar, lakini naomba niisome Katiba ya Zanzibar... nani kaikimbiza tena! Aah! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niisome. Ukisoma Katiba ya Zanzibar Ibara ya 119... imechukuliwa bwana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 119(14) inasema kwamba; "Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itashirikiana na Tume ya Taifa katika kuendeleza shughuli zao za uchaguzi."

Sasa ikiwa Tume ya Uchaguzi ya Taifa ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano inashirikiana na Tume ya Zanzibar, kwa hiyo, hata uchaguzi uliofutwa, Tume ya Taifa imeshiriki katika kufuta uchaguzi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja cha busara sana; tumetoka mbali sana na Taifa hili, tuna maingiliano ya muda mrefu; tuna maingiliano toka karne ya 16 na nyuma huko, tumeishi kwa udugu sana, tumeishi kwa mapenzi, tumeishi kwa furaha wala hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo mengi yanayojitokeza madogo madogo, lakini yamekuwa yanapatiwa ufumbuzi na mambo yanakwenda. Leo isifike wakati Mpango huu ukawa hautekelezeki kwa sababu ya mtu mmoja tu peke yake. Nikimtaja mtu anayeitwa Jecha Salum Jecha, msem *laanatullah*, kwa Kiswahili "laana za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi mbalimbali ambao wanaitakia mema nchi hii, naomba nimtaje kwa heshima kubwa Komredi Salim Ahmed Salim, alisema kwamba lazima tatizo la Zanzibar lipatiwe ufumbuzi, lakini pia Mheshimiwa Bernard Membe aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje katika Serikali ya Awamu ya Nne, kwa ufasaha kabisa alisema tatizo hili lazima tulipatie ufumbuzi. Vilevile Jaji Warioba, watu hawa ni watu wenye heshima kubwa katika nchi hii, ni watu ambao tunawaheshimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo lisichukuliwe kama ni tatizo dogo tu. Niwaambie kitu kimoja; tunapanga mipango hapa, hata Kenya na Burundi wana mipango wanapanga, inakuwa sasa? Mara Garissa limelipuka! Mara hapa, mara pale, kwasababu mnaonea watu waliokuwa hawana silaha. Watu waliokuwa hawana silaha, wanatafuta namna.

Kwa mfano, Waziri Mkuu aliyepita alikaa pale wakati Mheshimiwa Mama Asha Bakari, Marehemu, Mungu amrehemu, alipokuwa akisema nchi hii haipatikani kwa vikaratasi. Sasa ukisema nchi hii haipatikani kwa vikaratasi, maana yake ni kwamba, huo ni ugaidi, tutafute utaratibu mwingine. Hata Mheshimiwa Lukuvi naye aligusagusa sana kwenye swali hili, mtu mbaya sana yule! Tuendeleo lakini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwa busara kabisa, viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakae pamoja tuone namna gani wanalishughulikia tatizo la Zanzibar na uchaguzi usifanyike. Uchaguzi kwanza ukae pembeni, usifanyike tuone ni namna gani Serikali hii inatatua tatizo letu hili, kwa sababu mkiacha uchaguzi ule ukifanyika, na sisi tumetangaza rasmi kuwa hatushiriki kwenye uchaguzi ule; ninyi mnaona ni busara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnaona ni busara, endeleeni na uchaguzi, lakini niwaonye kitu kimoja, Serikali mnanisikia vizuri sana, mpo hapo. Haya makundi yote yaliyojitokeza kama *Islamic State, Al-shabab, Boko Haram* yalitokana na kudhulumiwa haki zao. Haya hayakuwa bure! Hayakujitengeneza tu, yalijitengeneza baada ya kudhulumiwa. Sasa msije mkatuharibia nchi yetu kwa kumlinda mtu mmoja tu. Serikali ya Muungano mmewabeba sana Serikali ya Zanzibar! Mmewabeba mwaka 2000... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali!

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Naam!

**MWENYEKITI:** Huo mfano ulioutumia, chimbuko la hayo makundi uliyoyataja wewe, una ushahidi kwamba misingi yake ndiyo hiyo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Unaweza ukatuthibitishia hapa?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Mimi nakusihi sana, ufute tu hiyo kauli yako, tusifike mbali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kauli yangu, haina shida. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa, Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa! Keti tu Mheshimiwa Ngwali, muda wako umekwisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu 104(1), msemaji aliyepita alizumza kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Tanzania Bara na Visiwani inashirikiana; naomba nimsomee Ibara ya 104 (1) inasemaje kuhusu Uchaguzi wa Zanzibar? Inasema: "Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atachaguliwa na wananchi katika Tanzania Zanzibar kwa mujibu ya masharti ya Katiba ya Zanzibar; na kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inayohusu uchaguzi kwa ujumla au uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui Tanzania Bara hapa inaingiaje kwa mujibu wa aliyetangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijamaliza!

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa, unanipa mimi tena!

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Ile iliyotolewa.

**MWENYEKITI:** Aah, sitaki malumbano yenu ya taarifa ambazo hazina tija.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Haya bwana!

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Na mimi kwa kuwa ni mara ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, namshukuru Mwenyezi Mungu, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kupitia Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kunitiua kuwa mgombea wa chama hiki katika Jimbo la Manyoni Magharibi pia nawashukuru wananchi wakazi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa kuniamini na kunipa nafsi hii na leo nasimama mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza tu moja kwa moja kwa sababu muda huu siyo rafiki sana, nianze na suala zima la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya ya Mpango yameonesha maeneo ambayo wataelekeza katika jamii yetu kusaidia maji. Jimbo langu ni miongoni mwa Majimbo machache sana ambayo maji hayapatikani kwa asilimia ya kutosha; ni chini ya asilimia 10.

Naomba sasa kwa Waziri husika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi walimpa kura nyingi, zaidi ya asilimia 80 na alipokuja pale aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi na Mji wa Itigi kwamba atasaidia maji katika kipindi kifupi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Waziri mhusika alione hili ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeze sana Serikali kwa mpango wa elimu bure. Mpango huu una tija na wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi wamenituma niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanya mpango huu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo langu wana tatizo kubwa sana la afya. Tuna Kata 13 lakini Kata zenye vituo vya afya ni mbili. Tunategemea sana Wamisionari; na bila Wamisionari, wananchi wa Jimbo langu wasingekuwa wanaongezeka kwa kiasi hiki ambacho wanaongezeka kwa sababu hata watoto wangukuwa wanakufa mapema. Jiografia yake ni ngumu, lakini vituo vya afya hakuna, zahanati zipo chache; kwa kushirikiana na TASAF zilijengwa lakini hazina matabibu. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri yuko hapa, alifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi pia ya Mheshimiwa Rais. Tunategemea sana hospitali ya Wamisionari ya Mtakatifu Gaspar. Hospitali ile ina gharama kubwa sana. Wakati alipokuja katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka wa 2015 aliwaahidi wananchi wa Jimbo langu kwamba atalipa mishahara yote ya watumishi wa hospitali ile, atatoa ruzuku kwa ajili ya vifaa

tiba na ataleta Madaktari Bingwa. Pia atafanya mgao kutoka MSD ili tu kusaidia wananchi wa Jimbo lile ambao hawana hospitali mbadala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya iko mbali; naomba sana ahadi ya Mheshimiwa Rais itekelezwe, tena katika kipindi kifupi. Wananchi tuna taabu na tunakufa kwa sababu ya gharama ni juu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunganisha mikoa kwa barabara za lami; Mkoa wa Singida umeunganishwa na mikoa mingine; lakini Mkoa wa Singida kuunganisha na Mkoa wa Mbeya, ni kitu ambacho kinashangaza. Mimi kama kiongozi ambaye nimetokana na wananchi wale, leo hii nimepokea message nyingi kwamba barabara baina ya Itigi na Rungwa, imekatika, hakuna barabara. Kikosi kazi kiko pale lakini hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii jana amenipa barua kwamba wanatafuta fedha katika barabara hii ya Mkiwa – Rungwa hadi Makongorosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe kwamba barabara hii amekuwa akiisemea toka Mbunge wa wakati ule Mheshimiwa Iwvata. Mheshimiwa Lwanji katoka hapa miaka kumi, bado ni ahadi zile zile. Naomba sasa mtekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyowaambia wananchi wa Itigi na Jimbo la Manyoni Magharibi kwamba katika utawala wake, atajenga barabara ile kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuwa una-wind-up hapa atuambie ni lini barabara ya kutoka Mkiwa – Itigi – Rungwa itajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Wabunge walioongelea kuhusu reli ya kati, nami Jimbo langu reli inapita pale na wananchi wangu wananufaika sana na reli inapopita pale. Sisi tunatumia usafiri ule wa reli kwa ajili ya kwenda maeneo jirani, lakini pia hata kwenda Kigoma. Mji wa Itigi ni mji ambao tumechanganyika, kwa hiyo, tunatumia sana reli kwa maslahi ya jamii yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kilimo, tufike mahali sasa tuondokane na kilimo hiki cha mvua. Wakati mwingine mvua zinakuja kidogo wakati mwingine zinazidi. Maeneo ya Itigi ni mazuri, tukiweka miundombinu tu ya *Irrigation Schemes* yoyote, *deepwell* ikifanyika pale, maji yatapatikana ya kutosha na tunaweza tukaanzisha *irrigation scheme*, tukaondokana na utaratibu huu wa kutegemea mvua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mpango wa matreka ambao ulikuwepo katika awamu iliyokwisha. Wananchi wa Jimbo langu hakuna hata

mmoja aliyefaidika na manufaa ya Serikali yao; na wao ni waaminifu na ni watiifu, hawajawahi kufikiria kuchagua chama kingine zaidi ya CCM. Hivi tunavyozungumza Halmashauri ya Itigi ni mpya, lakini Madiwani wote ni wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi walione hili kuwasaidia wananchi. hawa ambao ni waaminifu! Waswahili wanasema, chanda chema huvikwa pete. Sasa tunavikaje pete ambacho siyo chanda chema? Tuwaone hawa wananchi ambao ni waaminifu kwa Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo; kuna changamoto kubwa sana kwa bei ya mitamba katika mashamba ya Serikali. Bei ya mitamba ni kubwa kuliko bei ya ng'ombe ambaye unamuza mnadani. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alifuatilie hili ili mitamba ishuke bei, watoe ruzuku ili wananchi tununue, lakini pia madume ya kuhamilisha mifugo ili tutoke katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Hii ya kwanza eh!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye hoja hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Mashimba Ndaki, natoka Maswa Magharibi. Nachukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema zake na uwezo wake ambao umeniwezesha kufika kwenye Bunge lango Tukufu. Pia nachukue nafasi hii kuwashukuru wananchi na wapigakura wangu wa Jimbo la Maswa Magharibi kwa kunipa kura nyingi ambazo hazikuwa na maswali; na hata wapinzani wetu walinyoosha mikono. *(Makofi)*

Nawashukuruni sana wapigakura wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama nilivyokuwa nikiahidi na kama nilivyokuwa nikisema, niko hapa kuwawakilisha, kuwatumikieni na tutafanya kazi pamoja, tumeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Rais Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo ameshaanza kazi baada ya kulihutubia Bunge hili. Tunamtia moyo kwamba sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuko pamoja naye, tutasaidiana naye ili ndoto ambayo anayo kwa ajili ya Watanzania iweze kukamilika. Tunajua anayo ndoto kubwa na inaeleweka mpaka inatisha upande ule wa pili. Tutakusaidia Mheshimiwa Rais kama Wabunge ambao tumeaminiwa na wananchi kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri ambao wameshateuliwa na kuanza kazi zao. Kazi yenu ni njema, endeleeni, msikatishwe tamaa na maneno ya wachache wetu ambao wao siku zote ni kukatisha tamaa tu. Kazi yenu ni njema, tuko pamoja. Mahali ambapo mtahitaji msada wetu, kuweni na uhakika mtaupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwa namna ambavyo mmeanza kwa kasi wengi hawapendi; na hasa hii slogan ya hapa kazi tu, wengine wanajaribu kuipotisha na kusema yasiyokuwepo kwenye hiyo slogan, hata hivyo, endeleeni! Hata ninyi mliofunga mageti, mimi nawapongeza. Wenzetu wanasema eti mngeanza kwa kujengea watu uwezo. Unamjengea mtu uwezo wa namna ya kuja kazini kwa muda uliopangwa! Unataka kumjengea mtu uwezo kwamba atoke saa ngapi kazini anapofika! Hii itakuwa nchi ya namna gani? Endeleeni, chapeni kazi, tuko pamoja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango. Mapendekezo yake ni mazuri na yana kitu ukisoma unaona kabisa kwamba nchi yetu sasa inaelekea wapi. Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa mapendekezo haya na Mpango huu ambao umeuleta mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tofauti sana ukisoma na maoni ya wenzetu. Nimesoma sana ndani yake, huwezi kusema utapata kitu hapa cha ushauri. Sijui kama Mheshimiwa Waziri amesoma na kwamba labda kapata chochote, kwa sababu imejaa malalamiko, manung'uniko, hakuna ushauri wowote ndani yake, ina maneno tupu, wala hakuna takwimu. Sasa sijui kama upinzani wako serious kama wanakuja na vitu vya namna hii Bungeni na wanataka kweli kuongoza nchi hii na kuifikisha mahali pazuri. Wapinzani ninyi ni watu wazuri sana, lakini kuweni serious...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu naomba uketi chini Mheshimiwa Ndaki!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) kuhusu taarifa; kwa sababu msemaji anayezungumza sasa amezungumza

na ametuambia ameisoma vizuri sana Hotuba ya Upinzani na amegundua hotuba hiyo ina upungufu mwingi sana; sasa naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge; je, yuko tayari sasa kueleza upungufu huo kila mahali atakapokwenda katika Jimbo lake na mahali popote ili wananchi waweze kuelewa upungufu huo? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Sasa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Aaah, ngojeni niwafundishe matumizi ya Kanuni. Twendeni tu, nitawa-*guide* vizuri tu na Kanuni. *(Kelele)*

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana mnaniona nilianza kwa Mheshimiwa Ngwali na Mheshimiwa Mbunge wangu wa Tabora Mjini, nikamwambia unafahamu tunafika mahali tunaanza kupata kama aina fulani ya mhemko ambao unatutoa nje ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa sisi kama wanasiasa tunapenda ile ya kuoneshana kidogo, kujibishana. Kuna wakati unaweza ukaitumia hiyo vizuri, lakini tukiiruhusu hii, ndiyo inayotuingiza katika haya ya kuanza kunyanyuliana Kanuni. Mimi nisingependa tuwe tunafika huko.

Mheshimiwa Mbunge wa Maswa Magharibi, kwa heshima zote, kama uliisoma hiyo hotuba ya Waheshimiwa wa Kambi ya Upinzani, Wabunge na Watanzania wamekusikia, sasa tujielekeze tu kwenye hoja iliyo mbele yetu ili tukae vizuri. Sasa umebaki na dakika moja tu. Itumie vizuri, tumalize, twende mbele. *(Makofi)*

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa imefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa nichangie tu kwa haraka haraka katika mapendekezo haya ambayo yako mbele yetu. Kuhusiana na suala la viwanda, naunga mkono kwamba sasa tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda. Nakubaliana kabisa na hayo yaliyoandikwa lakini nataka tu kuweka angalizo kwamba bado tunavyo viwanda kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo ya Mpango sijaona mazingira mazuri yanayojengwa kwa ajili ya viwanda ambavyo tayari vipo na vinajikongoja au vinapata shida kwa sababu ya changamoto mbalimbali.

Kwa hiyo, nilikuwa nasihi kwamba wakati tunatengeneza na kuimarisha Mpango huu kuelezwe bayana kwenye Mpango ni kwa namna gani mazingira yataboreshwa ili viwanda vilivyopo na ha ta hivyo vitakavyokuja viweze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama mahali hapa kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwa kunipa kura nyingi sana za kishindo mimi pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Kwa kipindi cha pili Halmashauri yetu iko ndani ya mikono ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa Mpango wake mzuri ambao ameuweka hapa mezani. Pia napenda niseme jambo moja ambalo lilizungumzwa jana, upande wa upinzani walisema Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwenye kampeni zake alipiga *push-up*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba zile zilikuwa ni mbinu, lakini hata ninyi kuna mizunguko mlikuwa mkiifanya, ile zungusha pamoja na *helicopter* nyingi kwenye Jimbo langu mara nne, lakini hamkufua dafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kujielekeza kwa kuipongeza hotuba hii nzuri. Na mimi pia naungana na wenzangu kuhusu ujenzi wa reli. Ujenzi wa reli utaongeza mapato makubwa sana katika nchi yetu, lakini pia sisi wananchi tunaishi pembezoni mwa nchi ni kwamba vifaa mbalimbali vitashuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano, *cement* kwa Kanda ya Ziwa ni shilingi 18,000/=, shilingi 20,000/= mpaka shilingi 22,000/=; wakati Iringa Mheshimiwa aliyekuja kuwekeza nchini kwetu, Mheshimiwa Dangote, amesema kwamba *cement* itashuka bei mpaka shilingi 8,000/=. Kwa kupitisha kwa njia ya barabara, tutaendelea kuipata ile *cement* wananchi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla kwa bei kubwa. Lakini pindi reli ile itaanza kufanya kazi,

naamini kabisa kwamba *cement* na mazao mbalimbali kwa kuja Dar es Salaam na mali mbalimbali kutoka na kwenda Kanda ya Ziwa, zitashuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ni mzuri, lakini kuna jambo moja naomba nishauri, kuna bwana mmoja na jeshi kubwa sana, hakuingizwa kwenye Mpango huu, naye anaitwa mzee watoto wa mitaani. Mpango huu haukuwekwa. Kwa nini? Kwa sababu jeshi hilo kila mwaka linaongezeka. Serikali ina mpango gani kupunguza watoto wa mitaani? Mtaa hauzai! Serikali ina mpango gani kuhusiana na suala hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale, mimi nimekuwa Mbunge wao takriban huu ni mwaka wa sita, nimekuwa nikipigania tatizo kubwa la maji. Mkondo wa Ziwa Victoria unaanzia kwenye Jimbo la Nyang'hwale, lakini cha ajabu wananchi wa Nyanghwale hawana maji.

Mwaka 2013, Waziri Maghembe nilikataa kupitisha bajeti yake; bahati nzuri Serikali kupitia Benki ya Dunia tuliweza kupewa mradi huo wenye thamani ya fedha shilingi bilioni 15.7. Cha ajabu, mpaka leo hii pesa ambayo imetoka ni shilingi bilioni 1.8. Bajeti ya mwaka 2015/2016 tuliongezewa shilingi milioni 752 lakini fedha hiyo haijatoka. Sasa hivi Wakandarasi wamesimama, hawaendelei na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwa mwaka wangu wa sita waje wamejipanga vizuri Wizara ya Maji. Sitakubaliana! Sisi wananchi wa Nyang'hwale tuna mkosi gani? Naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni Serikali sikivu.

Ndugu zangu, naomba nizungumzie suala la elimu bure. Naishukuru Serikali, imeanza kutekeleza; lakini kuna jambo moja sikuliona ndani ya Mpango kuhusu elimu. Kuna familia nyingine, kaya moja unaikuta inajaza darasa; lakini kuna kaya moja ina watoto wawili. Je, ndani ya Mpango huu, kaya moja ina watoto inajaza darasa moja, kaya mbili zinajaza madarasa mawili.

Ndugu zangu, tujaribuni kuliangalia; ndani ya Mpango tuwekeeni utaratibu mzuri. Yule ambaye ana watoto kuanzia 10, 20, au 30, awekewe naye Mpango mzuri. Nusu ichangie Serikali na nusu achangie. Hili suala ni la msingi sana. Kuna wengine wana wanawake kumi, wengine watano na wengine wamejaliwa kuzaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alifanya ziara kwenye jimbo langu. Alikuwa akaahidi Kituo cha Afya Kalumwa, kukipandisha kuwa Hospitali ya Wilayana tayari imeshapandishwa, lakini ukifika pale, hali ni mbaya! Kuna wodi ya akina baba ina vitanda nane. Wagonjwa wa aina zote wanalazwa mle. Naiomba bajeti hii inayokuja, Wizara ya Afya mje

mmejipanga vizuri kwa ajili ya kuboresha hospitali yetu ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu, kwa kweli miundombinu ya Wilaya ya Nyang'hwale, kuna barabara moja ambayo imeahidiwa kuanzia mwaka 2010 alipokuja Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, alituhidi kutujengea barabara kutoka Busisi kupita Busorwa, kupita Karumwa, Nyang'hwale kupita Msala kwenda Kahama. Leo miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alikuja tena mwaka 2011 wakiwa katika msafara huo, Mheshimiwa Waziri Maghembe alikuwa yumo, Mheshimiwa Majaliwa alikuwa yumo, Mheshimiwa Rais wetu huyu wa sasa hivi wa Awamu ya Tano alikuwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Jakaya Kikwete, walisimama na wakalizungumzia suala la barabara tutajengewa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye Mpango huu, barabara hii haimo. Naomba sasa hii awamu ya hapa kazi tu, atutekelezee. Anaelewa vizuri hiyo barabara, alituhidi akiwa Waziri na leo ni Rais wa nchi. Ninaomba ahadi ya Rais, iwekeni humo barabara hiyo kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo. Wananchi wa Nyang'hwale tuna mabonde mazuri sana, tuna mito mingi, maji yale yanaporomoka yanakwenda Ziwani. Naomba tuweke mpango mzuri wa kuyatega yale maji yaweze kuwasaidia wakulima wetu. Tuweze kupata maji kwa mifugo na matumizi ya binadamu, pia tuweke mpango mzuri wa kilimo cha umwagiliaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tunataka tunyanyue viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa: Je, *material* hayo yatapatikana vipi? Sisi wananchi wa Nyang'hwale ni wakulima wa mpunga, tunategemea mvua za masika, lakini kama tutatengenezewa mabwawa mazuri, kwa umwagiliaji tutalima mara mbili au tatu na tutakuwa watu wazuri sana wa kuweza kuongeza kipato chetu kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kukichagua Chama cha Mapinduzi. Na mimi kama mwakilishi wao nawaahidi nitawafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia Mpango huu kwenye suala zima la miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali ni kuhakikisha mikoa yote inaunganishwa na barabara zote zinajengwa kwa kiwango cha lami. Bahati mbaya sana mikoa ya pembezoni imeachwa bila kuunganishwa ukiwemo mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora ni Mikoa ambayo ilisahaulika kimaendeleo. Katika Mpango huu ambao Serikali imeuleta, tunaomba rasilimali za nchi hii zigawanywe kwa uwiano ulio sawa. Inafanya wananchi wa maeneo mengine katika nchi yetu wanaonekana kama watumwa wakiwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie kwa makini zaidi, tusielekeze kila siku Mikoa ya Kanda ya Kaskazini ndiko ambako wanaelekeza Serikali kupeleka huduma za kijamii. Tunahitaji maeneo ambayo yalisahaulika nayo yaangaliwe na kuwekwa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iharakishe kujenga miundombinu ya barabara. Barabara ya Sumbawanga kuja Mpanda ikamilike, barabara ya kwenda Kigoma kutoka Mpanda ikamilishwe na barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora ikamilishwe. Vilevile bado barabara zile za Mkoa wa Tabora kwenda Kigoma nazo zikamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza leo hii, Mkoa wa Katavi umekaa kisiwani. Barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora haipitiki. Nasikitika tu kwamba hata leo Serikali ilipokuwa inatoa kauli, uwezekano wa kupita barabara ile ya kutoka Sikonge kuja Wilaya ya Mlele, haupo. Bahati mbaya Serikali imesahau maeneo hayo. Naomba miundombinu iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye suala la miundombinu ni ujenzi wa reli. Reli tunayoihitaji Watanzania ni reli ya kutoka Dar es Salaam kuja Tabora; reli ya kutoka Tabora kwenda Mwanza; reli ya kutoka Tabora kwenda Kigoma. Vilevile tawi la reli la kutoka Uvinza kwenda Msongati na tunahitaji reli ya kutoka Tabora kwenda Kaliua - Mpanda – Karema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu za msingi ambazo tunaomba Serikali iangalie. Nchi ya Congo inajenga reli kutoka Lubumbashi kuja Kalemie kwa lengo la kutaka kuunganisha reli inayotoka Karema kwenda Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Wakongo wameona kuna umuhimu bidhaa zao zipitie kwenye nchi yetu, sisi ambao tuna umuhimu wa kutumia Bandari ya Karema na kuifanya Bandari ya Dar es Salaam ipokee mzigo mkubwa, ni kwanini tuwe na vikwazo vya kusuasua tusijenge reli hii na kutoa maamuzi? Naomba Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la kilimo. Watanzania walio wengi wanafanya kazi na wengi wanajishughulisha na shughuli za kilimo. Naiomba Serikali, ni lazima ifike mahali iangalie umuhimu wa kuboresha kilimo. Ili kilimo kiweze kuwa na maboresho, kwanza iangalie gharama za pembejeo. Pembejeo nyingi zinazoletwa kwa ajili ya shughuli za kilimo ni za bei ya ghali. Tena inafikia mahali Jimboni kwangu, bei za pembejeo zenye ruzuku ya Serikali ni za ghali kuliko bei za soko.

Sasa inafanya kilimo hiki kisiweze kwenda. Naomba iangalie umuhimu wa kuboresha shughuli za masoko ili tuweze kusaidia mazao ya kibiashara. Ni lazima Serikali ifike mahali iwe na kitengo maalum cha kutafuta masoko ili kuyasaidia mazao ambayo yanalimwa na Watanzania walio wengi.

Jimboni kwangu kunalimwa zao la tumbaku. Tumbaku sasa hivi ni zao ambalo kwa wananchi ni kama utumwa, kwa sababu masoko yake ni ya shida. Naiomba Serikali iangalie umuhimu sasa wa kujenga kiwanda ambacho kitasindika mazao ya zao hili la tumbaku sambamba na mazao ya korosho, kahawa na mengineyo yale ya kibiashara ambayo yatakuza uchumi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nilikuwa napenda kuishauri Serikali iwekeze kwenye shughuli nzima ya uvuvi na ufugaji. Ili wavuvi waweze kuwa na mazao mazuri yenye tija, ni lazima Serikali iangalie masoko na kuwapa huduma wavuvi ambao wanavua kwenye eneo la Ziwa Tanganyika ambako kunahitaji miundombinu ya umeme ili wananchi wanaofanya shughuli kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika waweze kunufaika na kuona umuhimu wa kuwekeza kwenye suala zima la uvuvi. Tunahitaji Serikali ijenge viwanda vidogo vidogo vitakavyowasadia wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali iangalie suala zima la huduma ya maji. Ili Watanzania waweze kufanya shughuli za kiuchumi vizuri, ni vyema Serikali ikasaidia kuwekeza miundombinu ya maji kwenye maeneo mengi, hasa vijijini. Naiomba Serikali, kwenye Jimbo langu tuna miradi ya maji ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikamilishe haraka; na ipeleke kwenye maeneo mapya ambayo tuna Watanzania walio wengi ambao wapo kule maeneo ya Mishamo, hawana huduma ya maji. Tuna Kijiji cha Kamjela, Kijiji cha Kusi, Ipwaga, Ilangu na maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mapya yanahitaji yapate huduma ya maji. Naomba Serikali iangalie maeneo yale kwani huko nyuma yalikuwa yanahudumiwa na UN, kwa sasa yapo mikononi mwa Serikali. Naomba Serikali pia iangalie eneo la migogoro ya ardhi. Tunayo maeneo

mengi katika Jimbo la Mpanda Vijijini ambalo limezungukwa na mapori, ifike mahali Serikali imalize migogoro ya ardhi, hasa ile ya WMA kwenye vijiji vya Kabage, Sibwesa, Nkungwi, Kasekese na Kaseganyama. Lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Mpango uliopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nami nikaweza kusimama katika Bunge hili Tukufu kuchangia hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana wapigakura wangu, vijana wa Kigoma; nakishukuru Chama changu kupitia Jumuiya yake ya Umoja wa Vijana na Jumuiya ya Umoja wa Wanawake kwa kunipa ridhaa mpaka leo hii nikaweza kuwa mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya hasa katika kupunguza matumizi ya Serikali. Sisi kama vijana tunasema tutamuunga mkono, tutakuwa bega kwa bega na yeye kuhakikisha tunatetea maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa pongeza za dhati kwa Mawaziri wakiongozwa na Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa katika Baraza la Mawaziri kuunda Serikali ya Awamu ya Tano. Sisi kama vijana, tuna imani kwamba mambo makubwa yatafanyika katika Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Mpango huu lakini pia nawapongeza Wabunge kwa michango yao ya kuboresha Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, kwa mujibu wa takwimu za idadi ya watu Tanzania, uwiano unaonyesha kwamba kundi la vijana linachukua asilimia kubwa zaidi. Kwa hiyo, mimi kama mwakilishi kwa vijana ningependa kujikita na kujielekeza kuzungumzia masuala ya vijana na hasa kuishauri Serikali yangu kwamba ili kuleta maendeleo katika Taifa hili, kundi hili maalum ni lazima tujue na Serikali ijue inalifanyia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza na imeweka msisitizo, kuhakikisha kwamba changamoto kubwa sana ya vijana ambayo ni ukosefu wa ajira inapata utatuzi. Katika kuleta utatuzi wa changamoto hii ya ajira inashindikana kusema kwamba hatuzungumzii ni jinsi gani sekta ya elimu inaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ni sekta ambayo Serikali imejitahidi kufanya mambo makubwa sana na tunawapongeza kwa kazi hiyo. Hata katika Mpango wetu katika ukurasa wa 28 wamezungumzia na wameelezea ni jinsi gani Serikali imejipanga kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuishauri Serikali katika mikopo ya wanafunzi waliodahiliwa kusoma katika Vyuo mbali mbali waweze kupatiwa mikopo yao kwa wakati. Kumekuwa na changamoto kubwa sana ya vijana hawa kukosa mikopo yao kwa wakati. Ukosefu wa mikopo yao kwa wakati unachangia hata kubadilisha mienendo yao na unaathiri hata matokeo yao ya kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli Serikali imefanya mambo makubwa katika sekta ya elimu na ninapenda kutoa pongezi za dhati na hasa katika maamuzi yake ya kubadili mfumo wa kupanga ufaulu wa wanafunzi kutoka katika ule mfumo uliokuwa wa GPA na sasa hivi wameweka mfumo wa *division*. Mfumo huu wa *division* sisi kama vijana tunaupongeza kwa sababu tunaelewa zaidi na hata wazazi wanaelewa zaidi na wanaweza kupima ufaulu wa vijana wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu pia napenda kuishauri Serikali kuboresha mitaala ya elimu. Kwa sababu tunasema kwamba tunataka kuwasaidia vijana ambao wanapata changamoto kubwa sana ya ajira, kwa hiyo, mitaala yetu ya elimu lazima ioneshe ni kwa jinsi gani inamwandaa huyu kijana kuweza kujijiri yeye mwenyewe, hasa tukiangalia na tukijua kwamba hamna ajira za kutosha kwenye Serikali na hata taasisi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji kuwa na mitaala ambayo itaweka msisitizo katika taaluma lakini mitaala hiyo iweke msisitizo katika stadi za kazi. Kwa kuzungumzia stadi za kazi, hapa nitazungumzia vile vyuo vya kati ambavyo vinatoa mafunzo kama ya ufundi, vyuo kama *Dar es Salaam Institute of Technology* na *VETA*. Vyuo hivi viweze kuongezewa uwezo ili vidahili vijana wengi zaidi ambao watapata mafunzo ambayo yatawawezesha kujijiri wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya michezo na sanaa ni sekta ambayo inatoa ajira kubwa sana kwa vijana; sio tu vijana lakini kwa Taifa duniani kote. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali yangu iweke msisitizo na kuwezesha

michezo na sanaa kuwekwa katika mitaala yetu ya elimu ili kuibua na kuendeleza vipaji ambavyo vijana wetu wanakua navyo. Ina maana vipaji hivi na sanaa hizi zikifundishwa kwa vijana wetu wanaweza kupata fursa ya kujiajiri wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa hili wako akina Diamond wengi wa kutosha; wako akina Mbwana Samatta wa kutosha; lakini ni kuboresha tu mitaala yetu ili katika mitaala ile ya elimu zipangwe ratiba za kufundisha vijana, michezo, lakini pia kuwa na mafunzo ya sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ajira kwa vijana, nitakuwa sijatenda haki kama nisipozungumzia miundombinu wezeshi.

Napenda kuunga mkono michango ya Waheshimiwa waliotangulia waliosisitiza kwamba Serikali itengeneze mpango wa kujenga reli ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ya Dar es Salaam haiwezi kukamilika pasipo reli ya kati; Bandari ya Kigoma haiwezi kukamilika pasipo reli ya kati. Kimsingi, reli ya kati itapanua sekta nyingi za uchumi na itanufaisha siyo tu Mikoa ya jirani, lakini itaongeza uchumi wa nchi kwa sababu itafungua milango ya biashara na nchi jirani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi ya kuchangia...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami nipate kuchangia Mpango wa Taifa wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi kwa kunipa kauli na pumzi ya bure ninayopumua kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara yangu ya kwanza kusimama kuchangia. Nakishukuru sana chama changu na viongozi wangu wa Kitaifa kwa

kunirejesha tena huku ndani kwa awamu ya pili. Mwenyezi Mungu awabariki sana na awape umri katika maisha yao na utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu nitajikita sana kwenye masuala ya ulinzi na usalama. Tunapeleka vijana kwenye makambi ya Jeshi, kwa mfano JKT, vijana wanaenda kupata mafunzo mbalimbali ya kijeshi, lakini imekuwa katika kundi hili wanachukuliwa vijana wachache sana na vijana wengine wanakuwa hawana ajira. Sasa naomba huu Mpango uelekezwe kwenye Wizara ya Ulinzi na Usalama waangalie ni namna gani ya kuboresha na kuwajengea vijana wote kwenye makambi ya JKT kuhakikisha kunapatikana viwanda vya ujasiriamali kwa ajili ya hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia haya makambi, pia kuna baadhi ya makambi mengine ambayo yamepakana na bahari, mengine yamepakana na maziwa. Pia hawa vijana wanaohitimu mnaweza mkawajengea na mkawapa angalau uvuvi wa bahari, wakaenda zao kujiajiri wenyewe. Sasa mnavyowarudisha vijana hawa mitaani, vijana hawa wamekuwa wanakuja mitaani hawana kazi, ndio hawa mnakuja tena kuwarubuni kwa mambo mengine na ndio wanaokuwa majambazi sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajikuta mnawatumia kwenye vikundi ambavyo havieleweki! Mnawatumia sana kwenye mambo ya siasa! Sasa nawasihi ndugu zangu Chama Tawala, mhakikishe mbegu mnayoipanda, ndiyo mtakayoivuna.

Leo hii mmesahau vikosi vya ulinzi na usalama mnawawezesha kipindi cha uchaguzi. Mkishawawezesha, basi, lakini leo hii vikosi hivi wengi hawana sehemu za kukaa, wanakaa uraiani. Angalieni ni namna gani Mpango huu kuhakikisha vikosi vya ulinzi na usalama vinapata makazi bora ya kuishi na vinaboreshewa mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia yanayoendelea sasa hivi huko Zanzibar, kila kiongozi atakumbukwa kwa matendo yake. Kiongozi na uongozi ni dhamana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Leo hii sisi kama watu waliotokea Zanzibar tutamkumbuka sana Rais Amani kwa mambo yake aliyoyafanya mazuri kutuunganisha na tukaja tukapiga kura ya umoja wa Kitaifa na tukasikilizana na tukazikana na tukawa tunafahamiana. *(Makofi)*

Leo hamtaki kusikia la mwadhini wala mchota maji kanisani, mnakwenda tu. Tukumbuke amani tuliyokuwa nayo ni tunu ya Taifa, lakini amani hii tunaichezea, ni kama vile shilingi ikishadondoka chooni, kwenda kuiondoshwa shilingi ile unapata taabu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmeona kimya; ukimya wa Wazanzibari, lakini siyo ukimya. Siasa ya Zanzibar uliza waliopita Zanzibar. Tulikuwa Wabunge wengi sana ndani ya Bunge hili waliotokea Zanzibar, wengi hawakuweza kurejea. Hawakuweza kurejea! Wabunge walioweza kurejea kama akina Mheshimiwa Masauni watajua ni kwa nini hawakurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamwona Dkt. Mwinyi anakuwa mtulivu na mwenye hekima na busara, tunapomwambia fuatilia jambo fulani, anafuatilia. Ndiyo maana mnamkuta kila siku anarudi kwenye kiti chake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wasizibe masikio yao, wayazibue. Naomba viongozi wote wa Jamhuri ya Muungano, Rais Kikwete alianza sana mambo mazuri ndani ya Zanzibar, lakini sijui ni shetani gani aliyekuja akaingia katikati akatupa mkono Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuhakikishe kunakuwa na Serikali ya umoja wa Kitaifa ambayo ina maridhiano bila kupigana, bila bughudha. Miaka mitano siyo mingi, mtarudia tena uchaguzi na wananchi wa Zanzibar watataka kumpa wanayemtarajia. Niondoke hapo, hilo somo litakuwa limeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kanda zote za Pwani, tuseme mpaka kule kwetu; ukishika Zanzibar na Pemba, bado kuna umaskini, kuna watu ambao hawawezi kujenga nyumba za kisasa. Tuangalie kama mji wa Bagamoyo ni mji wa kitalii, lakini Mji wa Bagamoyo mpaka sasa hivi umesahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani kuendeleza mji wa Bagamoyo ili uweze kuwa ni mji wa Kimataifa kwa utalii na kuhakikisha majengo yote ya Bagamoyo yanaboreshwa? Magofu yote yale ya utalii na yale ya zamani yaboreshwe ili kutangaza mji wa Bagamoyo upate kuwa mji wa kitalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, hata Hospitali ya Bagamoyo, bado hospitali ile mashuka hayakidhi haja; wagonjwa ni wengi na jengo lile ni chakavu. Kwa hiyo, naomba muupe Mji wa Bagamoyo kipaumbele kutokana na kwamba ni mji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe ni namna gani tunatangaza Mji wa Bagamoyo, kwa sababu ukitoka Bagamoyo kuna majumba ya Mji Mkongwe ambayo na Bagamoyo yapo; ni majumba ambayo yanakuwa ni kivutio sana kwa utalii. Majumba haya sasa mengine yamekuwa chakavu na mengine hata katika kujengwa ramani zile zinabomolewa, zinajengwa ramani nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimamie Mji wa Bagamoyo utangazwe katika sekta ya kitalii na majumba ya makumbusho pia yajengwe na vitu vya kale vyote vienziwe ili tupate watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba hii ni awamu yangu ya pili kuwa ndani ya Bunge hili na ninawashukuru sana wananchi wa Arusha, kwa sasa nina Madiwani 34 na Chama cha Mapinduzi kina Diwani mmoja. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niwashangae wenzangu wapinzani wanapowalaumu sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sijui wanategemea nini? Mimi sijawahi kutegemea kitu bora kutoka huko upande huo.

Kwa hiyo, ninavyoona wanatarajia kitu bora kutoka upande huo, nawashangaa. Tutakaa tutaongea ili badala ya kuwalaumu sana, waanze kuwaombea, kwa sababu lawama ikizidi inakuwa laana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea maendeleo ya nchi ni lazima uongelee *stability* ya nchi. Suala la Zanzibar mnafanya nalo mzaha. Aliongea Mheshimiwa Mbunge mmoja kutoka Chama cha CUF na akasema kwamba demokrasia inapokandamizwa na watu wanaposhuhudia uonevu, wakaona hawawezi kujitetea, ugaidi na ujasusi utazaliwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uliomba na mlimpiga miongozo mingi sana, lakini maneno haya alisema Mandela wakati anakwenda jela. Alisema mtu mnyonge anapozalilishwa na kuteswa, hafundishwi uoga, anafundishwa njia ya kutafuta utetezi. Makundi mengi ya ugaidi duniani ukisoma historia, mwende mkasome, yametokana na ukandamizaji uliofanywa na Serikali zilizoko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafanya mzaha na Zanzibar, mtashinda uchaguzi, mtafanya uchaguzi bila uwepo wa vyama vingine, mtapeleka polisi kutoka Bara, mnaweza mkaazima polisi na Kongo, lakini mtakuwa mmeshinda uchaguzi na mtakuwa mmeharibu *the next generation* ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayetakiwa kuongoza Zanzibar aliyeshinda uchaguzi siyo Msudani, ni Mtanzania na ameshafanya kazi kubwa katika Taifa

hili na ni Makamu Kwanza wa Rais wa Taifa hili, hamtaki kumpa nchi kwa sababu mna bunduki, mna majeshi na mnaweza mkawazuia watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliambiwa miaka ya nyuma iliyopita huko na nilisema hapa Bungeni; unaweza ukazini kwa siri, lakini huwezi kuugua UKIMWI kwa siri. Hiki mnachokifanya Zanzibar kitaleta madhara Tanzania Bara huku. Uchaguzi ulikuwa halali na Rais akapatikana. Mnafikiri kumnyang'anya Maalim Seif ushindi wake ni kutunza Muungano, mnachokifanya sasa, ndio mnabomoa Muungano. Hakuna Jeshi lenye nguvu ya kuzuia umma uliochukia kwenye nafsi. Watu wataanza kutafuta mabomu, kutengeneza mabomu, wataanza kufikiria kujilipua. Taifa hili litakuwa mahali pabaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyoongea, Wazungu ambao ni wafadhili wakubwa wa Taifa hili, watalii ambao wanaingia katika Taifa hili, wakizuia watalii kuingia Zanzibar, Arusha itaathirika, Serengeti itaathirika, mtaua uchumi wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zanzibar ni suala la msingi sana na tunapojadili Mpango wa Taifa, *stability* ya Taifa hili ni muhimu kuliko Mpango wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa juzi mmezima matangazo ya *TBC1* na mna mkakati wa kuzima matangazo mengine; mtafanikiwa, mko wengi sana! Mtafanikiwa kila dhambi, lakini mshahara wa dhambi ni mauti. Kila dhambi mnayoipanga mtafanikiwa, lakini mshahara wake ni mauti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi; tunapotengeza Sheria ndani ya Bunge, tunapo-*set precedent* za nchi yetu ndani ya Bunge, leo nyie ni Mawaziri, watoto wenu hawatakuwa Mawaziri. Leo ninyi mna ndugu ma-*JGP*, watoto wenu hawatakuwa ma-*JGP*. Mheshimiwa Mama Mary Nagu alikuwa ni Waziri leo anauliza maswali ya nyongeza. Mtoto wake huko mtaani atakuwa wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapotaka kutengeneza Taifa lenye misingi bora, ni vyema ninyi Wabunge mliopo leo, mkajua nchi hii ina kesho, ambapo hamtakuwa na *influence*. Shangazi zenu hawana *influence* mlizonazo, wengine hapa mliotokea kwenye matembe, mkaenda *university* mmekuwa Wabunge. Tunapokaa Bungeni kuongelea Taifa hili, tunaongelea ndugu zetu, jamaa zetu ambao hawana *influence* tuliyonayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnazuia matangazo *live!* Wananchi wanapoona hawatetewi, watatafuta utetezi! Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania linapokuwa *live...* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godbles Lema, umejenga hoja yako, sasa twende kwenye Mpango usaidie nchi. *(Kicheko)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Huu ndiyo Mpango. Tulia! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuongoea mpango bila kuongea *stability* ya nchi. Tulia Mzee, tulia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezima matangazo hapa ya *TBC1*, leo wananchi nje hawajui kinachoendelea humu ndani. Ninyi mnafikiri tukiwasema sana nyie, mnafikiri chama chetu ama vyama vya upinzani vinajenga umaarufu, lakini kimsingi kabisa, vyama vingi vimeleta amani katika Taifa hili, kwa sababu ni *alternative* ya *peace*. Wananchi wanapoonza tunasuguana ndani ya Bunge, wanakuwa na uhakika wa kesho, wanajua wana watetezi na Serikali ya *tender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmeondoa matangazo, mnafikiri mko salama? Mmeondoa maangazo tukisema tuisike, mnaweza mkafanya kila kitu. Yesu alisema, watu hawa wasipopiga kelele, mawe haya yataimba. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yes! *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunakoelekea watu hawataongea tena, hiki mnachokifanya hamtakifanya tena! Wakishindwa kuandamana, zitaanza *assassination*; wakishindwa kuandamana, nyumba zitaanza kuchomwa moto. Haki itatafutwa kwa gharama yoyote ile! *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yes!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri sana, mkikaa humu ndani, nawe ukikaa hapo juu, unajiona kama ni mdogo wake Mungu, mnakandamiza demokrasia, mnaleta polisi humu ndani, mnadhaliisha watu wanaodai haki! Ipo siku itafika! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Acha kuchochea wewe.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa ni *alternative* ya amani. Wanachama wenu wakichukia, wanakuja kwetu. Siku wakichukia wakaona huku hakuna msaada, wataenda porini. Vijana wenu wakichukia... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Vilevile nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, nitoe pongezi kwa Mawaziri wake kwa kazi nzuri sasa wanayoifanya na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Ilala kwa kunirudisha tena kwenye Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ujangili likiendelea litapunguza mapato kwenye Taifa letu. Mimi nilikuwa naomba kutoa ushauri *and I stand to be corrected.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa majangili ambao wako katika mbunga hizi, wanajichanganya na wawindaji halali, hivi Serikali ikipiga marufuku uwindaji kwa kipindi cha miezi mitatu, hakuna mtu yoyote kuingia na silaha kwenye mbuga hizi; na vyombo vya ulinzi vikafanya *operation* maalumu ya kusaka majangili hawa; nafikiri inaweza ikasaidia kupunguza tatizo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, pembe za nduvu ambazo ziko kwenye bohari, wazifanyie *audit* na wazifanyie *DNA*. Iko hatari kuwa takwimu za pembe za nduvu ziko sahihi, lakini ndovu zile ambazo ziko kwenye magodauni haya zisiwe sahihi. Inawezekana pembe nyingine wala hazitolewi kwenye mbuga, zinatolewa kwenye ma-godown haya ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa taarifa yake na Mapendekezo ya Mpango wake. Ametoa taarifa Bungeni kwamba gharama za kujenga reli ya kati itafika kama bilioni saba, fedha za Kimarekani, takribani kama shilingi trilioni 15. Fedha hizi ni nyingi sana na tusijitie hofu kwa gharama kubwa kama hii ili reli hii isijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zambia wamejenga reli yao kilometa 2,200 na madaraja 48, kwa *one billion US Dollars*. Sisemi *train* ya Zambia ipo sawasawa na ya kwetu, lakini naomba *design cost* zipatikane ili tujue gharama sahihi ya reli hii ili iweze kujengwa, iweze ku-*support* bandari yetu na bandari nyingine ili uchumi wa Taifa yetu uweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye Mpango, kuna Mpango wa kununua ndege. Kununua ndege na kujenga hii reli, Serikali haiwezi. Serikali ijikite

kwenye mipango ya huduma za afya, elimu na kilimo. Miradi mikubwa kama hii iachiwe sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ipo tayari kufanya. Sioni kwa nini Serikali miaka yote haitaki kushirikisha sekta binafsi ikajipunguzia gharama za kutumia fedha za umma kujenga reli hii au kununua ndege hizi na badala yake ikatumia kwenye mipango mingine. Sekta binafsi ikifanya shughuli hizi, itapunguza hata tatizo la watu kula rushwa kwa fedha hizi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege hizi ambazo Serikali inataka kununua; ushauri wa kwa Serikali, wasafishe vitabu vya ATC ili wakaribishe sekta binafsi iendeshe na ilete ndege nchini mwetu. Watanzania wanataka usafiri. Ukienda Marekani, hakuna Shirika la Ndege la Serikali. Sioni sababu kwa nini Serikali ijiingize kwenye miradi mikubwa na baadaye ikaingia kwenye hasara sababu ya kutokuwa na watendaji waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuleta elimu bure Tanzania. Sasa hivi wazazi wengi sana wanapeleka watoto wao kusoma na kujiandikisha. Zipo changamoto, mwanzo ni mgumu. Fedha haziwezi kwenda kwenye shule zote kwa muda mfupi sana ambao umewekwa, lakini changamoto hizi tukiipa muda Serikali, itatafuta njia ya kuhakikisha agizo hili la Rais linatekelezwa kwa ufanisi na Watanzania wakapata *win-win situation* wao na Serikali yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo *issue* ya Watanzania kushindwa kuwa na viwanja kutokana na Serikali kutokuwa na mipango madhubuti ya *ku-ring fence* viwanja maalum vya watu wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Malaysia, Serikali imeweka sheria kabisa ya kuweka viwanja na madhumuni yake ni kusaidia watu wao wa kipato cha chini. Viwanja hivi vinawekewa sheria kwamba yeyote mwenye kipato cha kati, haruhusiwi kuingia kwenye viwanja hivyo. Serikali ikijenga nyumba katika viwanja hivyo, watu wenye kipato cha kawaida hawaruhusiwi kuingia au kumiliki nyumba hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano, maana yake watu kama sisi Wabunge ambao wana uwezo wa kukopa na kujenga, hawataruhusiwa kuchukua viwanja kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo inasababisha watu kujenga kwenye mabonde. Hakuna mtu anayetaka watu wake wajenge kwenye mabonde wapate matatizo ya mafuriko, inasikitisha sana, lakini hawana njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kuna mradi wa *World Bank* kwenye maeneo haya ya mabonde ambayo watu wanaishi. Ninachokiomba, taarifa ambazo ziko kwenye mitandao, *World Bank* wanataka kufanya huu mradi lakini wameweka *component* ya fidia. Kama hizi fedha zimefika, fidia hii ilipwe tunusuru maisha ya hawa watu. Tusiingie tu na mazoezi makubwa ya kuvunja bila kutazama na mustakabali wa wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitetei wananchi wakae katika maji, wala msinieleme vibaya; wanataka wao waendeleo kukaa katika mabonde maeneo ambayo ni hatarishi; lakini taarifa za wao kupewa viwanja Mabwepande, siyo kweli. Nalizungumza hili na ninazo takwimu. Wananchi wa Mchikichini ambao walikumbwa na mafuriko mwaka 2011 walikuwa 4,200; viwanja *allocation* ilitoka kwa wananchi 80 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna taarifa kwamba Mawaziri hawa wanapewa na Mamlaka ya Mkoa kuambiwa kuna watu wanakimbia Mabwebande au wameuza Mabwepande, siyo kweli! Kama kuna mtu ameua kiwanja chake Mwabwepande watuletee taarifa na majina ya watu waliouza na waliokimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie, kuna watu wako tayari kuliboresha bonde hili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa mchango wako. Tunaendelea. Mheshimiwa *Engineer* Nditiye.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado dakika tano!

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwa jina naitwa *Engineer* Nditiye, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunitewa kugombea nafasi hii. Vilevile nawashukuru wananchi wa Jimbo la Muhambwe kwa kuniamini na kuona sasa maneno maneno Bungeni hayatakiwi, inatakiwa Kazi tu! Nawaahidi kwa moyo wa dharti kabisa kwamba *Engineer* Nditiye, nimekuja kufanya kazi wala siwezi kuwa na maneno maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ndugu yangu Mheshimiwa Mpango. Kwanza namsifu sana kwa hotuba yake nzuri sana na mipango yake mizuri sana. Vile vile nashukuru hotuba ya Mheshimiwa Rais, ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango mipango yake mingi ime-base kwenye hotuba ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la elimu; ili tuingize nchi yetu katika uchumi wa viwanda, tunahitaji tuboreshe sana suala letu la elimu. Ni lazima tujikite sana katika kuhakikisha kuanzia shule za msingi, wanafunzi wanapenda masomo kama hesabu na sayansi ili hata hivyo viwanda vitakapoanzishwa tuweze kupata watu sahihi, kwa ajili ya kuviongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimkubushe Waziri wangu wa Nishati, Profesa Muhongo kwamba ili ku-achieve mipango yetu, tunahitaji tupate umeme kwa sababu, Serikali yetu ilitushauri kwamba kila Kata iwe na sekondari, na wananchi waliitikia huo mwito, kila Kata ina sekondari.

Vilevile Serikali yetu ilituambia kwamba kila sekondari ya Kata sasa iwe na maabara. Nikuhakikishie kwamba katika Jimbo langu la Muhambwe, karibu sekondari zote za Kata zimekwisha jenga maabara na tumekwishafikia asilimia 80, tunasubiri tu hatua ndogo ndogo ili maabara zianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyoko ni kwamba, katika Jimbo langu lenye Kata 19, ni Kata tatu tu ambazo zina umeme; na maabara yoyote ile sidhani kama inaweza kuendeshwa kama hakuna umeme. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Muhongo pamoja na kazi nzuri unayoifanya, nakuomba sana ufikirie hilo Jimbo la Muhambwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la reli. Sidhani kama kuna Mbunge yeyote ambaye atasimama hapa aache kuizungumzia reli ya kati, kwa sababu inahudumia mikoa zaidi ya 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile reli ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Hilo liko wazi, tunaomba sana, kwenye mipango yako utueleze *in detail*. Siyo kueleza juu juu tu kwamba kilometa ngapi zitakarabatiwa; tunataka utueleze za wapi na wapi na kivipi? Tunataka reli yote ikarabatiwe kwa sababu umuhimu wa reli hiyo hauna maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ni Mbunge wa kutoka Mkoa wa Kigoma siwezi kumaliza bila kuzungumzia barabara ya kutoka Nyakanazi mpaka Kigoma, nimeiona hapa kwenye ukurasa wa 11 imewekwa, naomba sana na tutakuwa makini kweli kuhakikisha hiyo barabara ambayo kwetu sisi ni ya muhimu kutuunganisha na Mikoa mingine inapewa kipaumbele na ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu ya maji. Kama nilivyozungumza hapo awali, Wilaya yangu ya Kibondo ina Kata 19, lakini Kibondo Mjini kwenyewe hatuna maji ya uhakika wala hayako salama haya yanayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Maji ihakikishe inatafuta chanzo kingine, kwa sababu chanzo kilichokuwepo kimeshavamiwa na shughuli za kibinadamu na hakifai tena; hakitoa maji; na kama Wilaya unaweza ukakaa hata siku nne bila kuwa na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Waziri wa Maji katika mipango yetu hii ahakikishe kwamba wananchi wanapata maji safi na salama ili waweze kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la maliasili. Katika Jimbo langu nina Kata zaidi ya sita ambazo zinapakana na Hifadhi ya Moyowose, Kata za Busunzu, Busagara, Lusohoko, Kitahana, Kata ya Mulungu na vijiji vyake. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukiomba Serikali irekebishe mpaka ili wananchi wapate sehemu ya Kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Vijiji hivi ni vya muda mrefu na wakati huo wananchi hawakuwa wengi, sasa wameshaongezeka na wanahitaji sehemu zaidi ya kulima.

Kwa hiyo, nashukuru sana kwa waraka uliopitishwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kuorodhesha vijiji vyote ambavyo vinapakana na mpaka ili waweze kuongezewa sehemu ya kulima. Nashukuru sana, nami nitashirikiana na wewe kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa haraka haraka. Kwenye kampeni za Mheshimiwa Rais, alipopita Jimboni kwangu pale, aliahidi kuhusu suala la pensheni kwa wazee wote, awe mtumishi, mkulima au mfugaji na wavuvi aliahidi pensheni kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hilo suala litekelezwe na liwekwe kwenye mpango imara ambao utatekelezeka ikiwezekana kuanzia mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, michezo. Nimefurahi sana kwamba hivi karibuni tumetoa *product* moja Tanzania ambayo imesikika moja kwa moja. Huyu anaitwa Mbwana Samatta. Tukumbuke kwamba michezo ni chanzo kizuri sana cha mapato kwa nchi. Angalia nchi kama Brazil, asilimia

kadhaa ya uchumi wake wanategemea sana wanamichezo ambao wanaenda kucheza nchi za nje, wanaleta uchumi nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe sasa tunaanza kuwekeza hasa kwenye Mikoa ile ambayo ni vyanzo vya sanaa na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia Mkoa wa Kigoma, Tanga kidogo na Morogoro kwenye *football* huwezi ku-doubt. Vilevile kwenye sanaa ya muziki, hata maigizo; Mkoa wa Kigoma una mchango mkubwa sana.

Naomba sana Serikali ijikite sana katika kuwekeza katika Mkoa wetu kuhusu suala la michezo na sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami nitoe mawazo yangu kwenye Mpango ulioko mbele yetu, hoja iliyoko mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema ya kusimama kwenye Bunge hili. Nawashukuru wapigakura wa Jimbo la Vunjo walionichagua kwa zaidi ya asilimia 72 ya kura zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango uliopo mbele yetu unatakiwa ujibu yafuatayo:-

(1) Unakuzaje uchumi wa Taifa letu?

(2) Unasaidiaje vijana wetu kupata ajira?

(3) Ujasiriamali wa Taifa hili utaongezeka kwa kiasi gani?

(4) Sekta mbalimbali katika Taifa letu na hasa sekta binafsi Mpango huu utaishirikisha kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hilo kwa sababu Taifa letu hapa tulipofikia sasa Serikali ya Awamu ya Tano siyo kwamba imeanza sifuri. Serikali zilikuwepo za tangu Awamu ya Kwanza mpaka sasa, lakini Taifa letu limekosa itikadi. Leo hii hatuna itikadi ya Taifa ya kutuonesha kwamba itikadi yetu ni nini na malengo yapo namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano nieleweke vizuri, wakati wa Mwalimu Nyerere tulikuwa na itikadi ya ujamaa, lengo likiwa ni kujitegemea na mifumo yetu yote, sekta zetu zote zilikuwa zinatekeleza itikadi ya ujamaa, lengo likiwa ni kujitegemea, lakini leo hii ukiangalia Mpango huu una-address au unatoa mwelekeo gani wa kuonyesha itikadi ya Taifa letu ni ipi kama ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme itikadi ya Awamu ya Tatu ilikuwa ni uwazi na ukweli, ndiyo itikadi au ya Awamu ya Nne labda maisha bora kwa kila Mtanzania au ya Awamu ya Tano useme hapa kazi tu je, hiyo ndiyo itikadi. Tunatakiwa tuwe na itikadi ya Taifa, vyama vishindane kwenye msingi ile ambayo tumekubaliana ya Kitaifa. Kwa mfano, kwenye sekta ya elimu, siyo kwenye sekta ya elimu Waziri aliyekuwepo ndiyo aamue namna ya kuindesha sekta hiyo, tuwe tumekubaliana Kitaifa, sekta ya elimu inaongozwa hivi kwa miaka kumi au ishirini ijayo. Kwa hiyo, yeyote atakayeingia pale ataongoza kwa misingi ambayo imewekwa. Lakini hebu tuangalie muda tunaoupoteza kwenye kugombana, akiingia huyu anabadilisha, akiingia huyu anabadilisha na ni kuvuruga tu Taifa la Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwe na maono ya miaka ishirini au thelathini ijayo, lakini siyo kwamba tunakosa mifumo na hasa ile mifumo inayolinda utu wa mwanadamu, inayokuza utu wa mwanadamu, mifumo hiyo ni ya elimu, mifumo hiyo ni ya kiutamaduni, mifumo hiyo ni yetu sisi kama Taifa ambayo inakuza zaidi utu wa mwanadamu, thamani ya utu wa mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma *Netherlands* miaka ya 2007/2008, Bishop Acronson anakwambia maendeleo ya *Netherlands* yamepatikana kwa kasi kwa miaka 64 kwa sababu ya maelewano ya Kitaifa na kutambua utu wa mwanadamu upo namna gani, kutambua uhai wa mwanadamu upo namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hapa Watanzania sisi sote ni watoto wa mama Tanzania, lakini kama sisi sote ni watoto wa mama Tanzania kwa nini tunabaguana? Kwa nini tunajenga misingi ya kulipasua pasua Taifa la Tanzania? Kwa nini tunajenga misingi leo hii Tanzania ni moja, anasema huyu wa Kusini, huyu wa Kaskazini, huyu wa Mashariki huyu wa Magharibi, ni kwamba tumekosa mifumo inayojali utu kwamba huyu Mtanzania ana haki kama Mtanzania mwingine, kama ni mifumo ya utawala bora, mifumo ya utawala wa kidemokrasia inalinda haki za wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesomea mambo ya majanga, yapo majanga ya aina kuu tatu na zaidi ya asilimia 95 ya majanga yote yanasababishwa na binadamu. Kuna *known knowns risk, known unknowns risk*

*and unknown unknowns risk* ambazo ni *acts of God*, lakini hizi *known known risk* tunazisababisha sisi binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majanga kusipokuwa na utulivu kwenye Taifa, kwa mfano, mwaka 2013 Taifa lilikuwa limekwishaanza kupasuka misingi ya udini, waislamu na wakristo, Taifa litaongozwaje, kuuawa kwa viongozi wa dini, Taifa litaongozwaje, mipango itatekelezwa, lakini tulipokaa watu ambao ni chini ya 100 Taifa lilitulia, Mheshimiwa Lukuvi alikuwepo kwenye mazungumzo yale tuliyojifungia watu chini ya 100 Taifa likatulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tukiwa na meza ya maridhiano, uundwaji wa dola siku zote duniani ni meza ya maridhiano, sisi sote ni Watanzania tuheshimiane na tukubaliane. Yanayotokea Zanzibar tusione kwamba ni mambo madogo, la hasha, ni mambo makubwa sana, yanayotokea Zanzibar leo hii tujue kwamba Tanzania tunaihitaji dunia kuliko dunia inavyoihitaji Tanzania. Narudia, Tanzania inaihitaji dunia kuliko dunia inavyoihitaji Tanzania. Leo hii Tanzania hatuwezi tukawa ni kisiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mipango tunayopanga hapa ni lazima tu-address suala la utawala bora na kwa kuwa tumekubaliana kwenye mfumo huu na Tanzania sisi siyo kisiwa je, duniani, *let us think globally but act locally*. Kama hatuwezi tuka-address kwamba dunia hii ambayo imeshakuwa leo hii ni kijiji, akili zetu zinajishusha kwamba dunia imekuwa ni kijiji kwa kasi ya maendeleo ya kasi ya sayansi lakini leo hii tunarudi hapa kuanza kuulizana wewe wa Kaskazini, wewe wa Kusini, wewe wa Mashariki, wewe wa Magharibi, wewe Mzanzibari, wewe Mbara tunaliua Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokubali kwamba umoja wa Taifa la Tanzania ndiyo utakaoweza kulea kizazi hiki na vizazi vijavyo, tutakuwa tunajimaliza wenyewe. Sisi Wabunge majukumu yetu ya kwanza kwa Taifa tunalileaje Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo rasilimali nyingi tu za Taifa hili, nendeni kwenye ripoti ya kutekeleza Mpango huu na hili nitoe nasaha kwa Mawaziri, kuna baadhi ya Mawaziri wanasema tu sijui ili waonekane kwenye runinga, wanasema ohh, tunaweza tukajitegemea kwa rasilimali zetu sisi wenyewe, mtapata wapi fedha Serikali ya kujenga reli ya kati kwa *standard gauge* kwa rasilimali zetu sisi wenyewe humu ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kabisa kujenga reli ya kati na matawi yake yote kwa kuwa ndiyo langu kuu la uchumi wa Taifa la Tanzania. Tuimarisha Bandari ya Dar es Salaam, tuunganishe na mitandao ya reli, Taifa hili uchumi wake utakwenda kwa kasi kubwa sana. Tusianze kugombana na Kagame na Uhuru Kenyatta wametuamsha, tuwachukulie *positively* katika

kujenga Taifa letu. Tusianze kulalamika lalamika tu hapa ohh, Kagame anatuzidi kete, Kenyatta, kwanza hata lugha hizo ni kwamba umeshindwa kufikiria. Nimeshawahi kusema kuna nguzo kuu sita za umaskini wa fikra ambazo ni ya kwanza, majungu; ya pili fitna; ya tatu umbea; ya nne kusema uongo; ya tano kujenga chuki na ya sita uvivu wa kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let us think big positively* Taifa letu hili tutalipeleka mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Vunjo tunategemea sana sekta ya utalii, Tanzania ni ya pili kwa vivutio vya utalii duniani lakini Tanzania inashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133 kwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwanza kabisa naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mungu wa mbinguni kwa ajili yangu na wengine wote tuliojaliwa kuingia mwaka 2016 na kuletwa humu na wananchi wetu. Zaidi sana nielekeze pia shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi ambacho kimenipatia fursa hii ya kuwawakilisha wanawake wa Manyara. Vilevile niwapongeze wanawake wa Manyara kwa kunipatia nafasi hii ili nije niwawakilishe katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba nielekeze michango yangu moja kwa moja nikianza na elimu. Naomba ku-*declare interest* ya kwamba mimi ni mwekezaji wa ndani katika masuala ya elimu, kwa maana ya shule za binafsi. Nipende kuanza kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambaye ameweza kusikiliza kilio cha Watanzania cha kuondoa GPA na kurudisha mfumo wa *division*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuwa kinafanyika ni sawa na kusalisha mtu mchafu gauni la *gold*. Kwa hiyo, niseme tu Mheshimiwa Profesa Ndalichako na timu yako hongereni sana maana mmedhamiria kuboresha elimu ya nchi yetu Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hakuna nchi ambayo imewahi kuendelea duniani pasipo kuwekeza kwenye elimu, hata maneno matakatifu yanasema; "Mkamate sana elimu usimwache akaenda zake maana yeye ndio uzima wako." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu, kulingana na Mpango uliopo mbele yetu wa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imeazimia kuwekeza sana kwenye elimu kwa kuanza kutoa elimu bure, basi nafikiri ni wakati muafaka kuangalia changamoto zinazokabili tasnia ya elimu nchini. Kwa hiyo kwanza kabisa, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona ya kwamba, potelea mbali vyovyote inavyoitwa ya kwamba ni kupunguza makali kwenye elimu ama ni elimu bure, lakini iwavyo vyovyote ili mradi mtoto wa Kitanzania sasa anakwenda kupata elimu bila vikwazo vya aina yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwaambie tu ndugu zangu Wapinzani, msibeze kila kitu kinachofanywa na Serikali hii, Serikali inajitahidi sana ninyi si Mungu ama malaika ambapo mngepata nafasi hii kwamba mngeweza kuchange dunia *in a day*. Kila kitu kinakwenda taratibu, hatua kwa hatua, changamoto zilizopo kwenye elimu bure zinafanyiwa kazi na zinakwenda kwisha. Kwa hiyo, tambueni juhudi za Serikali kwenye hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye mchango wangu wa elimu. Naomba sasa pia Serikali ijitahidi sana kufanya kazi na sekta binafsi maana kuna wadau wengi sana wamewekeza kwenye elimu na ifike mahali watu hawa waonekane kama siyo *competitors* isipokuwa ni *partners* wanaoweza kusaidia kusomesha watoto wa Kitanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wawekezaji wa ndani katika suala la elimu wanakabiliwa na kodi zisizopungua 13, ndiyo maana inaonekana watu hawa wanatoa elimu kwa gharama ya juu sana mpaka mambo ya ada elekezi yanaingia humu. Shule za binafsi zinalipa *property tax, income tax, service development levy, city levy, land rent*, mabango ya shule yale yaliyo kwenye TANROADS tunalipa kwa dola. Sasa sijui mambo ya dola yanakujaje tena na halafu inaitwa TANROADS halafu tunalipa kwa dola, sasa si tuite tu USROADS. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kodi ya *corporate tax, working permits* kwa walimu ambao siyo Watanzania. Mwalimu mmoja mpaka uweze kumpata anatomia sio chini ya shilingi milioni saba ndipo aweze kupata *working permits* na *residence permit*. Wakati huo huo tuna upungufu wa walimu wasiopungua laki tisa, tulionao ni laki mbili thelathini na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna upungufu wa Walimu wa sayansi na hisabati wasiopungua elfu ishirini, Wizara ama nchi ina uwezo wa kutengeneza Walimu wasiozidi elfu mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, tunachukua *note less than ten years* kutengeneza Walimu tunaowahitaji wa sayansi. Hii imekuwa pia changamoto kubwa kwa ajili ya maabara ambazo tumezijenga majuzi kati,

tuna maabara kila mahali sasa, lakini changamoto kubwa imebaki kwa Walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali sasa kama inawezekana Serikali ione umuhimu wa kupunguza gharama za kuwapata Walimu kutoka nchi jirani kwa gharama ndogo *residence permit* na *working permit* ili waweze kusaidia katika shule zetu.

**MHE. WAITARA M. MWIKABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo suala la afya. Naomba katika suala la afya kwa sababu Serikali pia imeamua kuwekeza sasa kwenye afya ya wananchi wake. Nizungumzie kidogo hospitali ya Hydrom, hospitali ya Hydrom ipo katika Mkoa wa Manyara lakini inasave Mikoa ya Singida na Mikoa ya Arusha kwa maana ya wenyeji wa Karatu na maeneo mengine hata ya Meatu. Kwa hiyo, ifike mahali sasa Serikali isaidiane kabisa kama ilivyoahidi kwenye mfumo huu wa PPP kusaidia hospitali ya Hydrom kuendelea kutoa huduma njema na toshelevu kwa wananchi wake wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena kidogo suala la utalii, utalii wetu umekuwa na changamoto nyingi za kuandamwa na kodi nyingi, mfano wa TALA Licence ni dola 2000 kwa mwaka bila kujali anayelipa ni mzawa ama mageni. Nashauri Serikali ifike mahali wazawa wapewe *first priority* na kwa gharama rahisi kidogo ili wanapowekeza kwenye suala la utalii, basi vijana wengi wakapate ajira kupitia utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari mengi yamekuwa *grounded*, utalii umekuwa *threatend* na masuala haya ya *Al-Shabab* na hata *Ebola*. Wazungu kule nje hawajui umbali wa mahali *Ebola* ilipo na *Al-Shabab* ulipo, kwa hiyo, utalii umeshuka. Mimi naishi Arusha, kwa hiyo, niseme tu utalii umeshuka na imefika mahali hayo magari ya watalii sasa yamekaa tu yanafanya kazi za kubeba abiria wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto, nimesafiri mwenyewe Disemba mwaka uliopita, nimepita geti la Naabi pale wageni wanapoteza masaa yasiyopungua mawili mpaka matatu wakati wa kujiandikisha kuingia hifadhini. Sioni kwa nini hili liendeleo wakati tupo kwenye dunia sasa ya sayansi na teknolojia. Muda mwingi mno unapotea foleni na *jam* inakuwa kubwa pale getini. Namwomba sana Mheshimiwa Jumanne Maghembe aweze kuangalia hilo ni kiikwazo. Mtu anayekwenda *day trip* kuingia pale chini *crater* na kurudi anapoteza masaa yasiyopungua matatu. Kwa hiyo, naomba hili nalo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia katika Mpango huu. Niseme kwamba Serikali haijajipanga, kwa sababu kwa muda mrefu tunakuwa na Mipango lakini haitekelezwi na inachosikitisha ni kwamba Waziri Mpango kama jina lake lilivyo, ndiye aliyekuwa anatuletea Mipango ya siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme, kwa kweli tatizo kubwa Tanzania inajulikana dunia nzima kwa mipango mizuri sana lakini haitekelezeki. Tulikuwa na mipango mpaka inachukuliwa na nchi nyingine inakwenda kutekelezeka lakini kwa kwetu ni tatizo. Vilevile tatizo kubwa ambalo naliona ni kwamba, hii Mipango haipimiki, haina viashiria ni jinsi gani inapimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwa mifano, ukiangalia kwenye suala la kilimo ni kwa kiasi gani wameweza kuoanisha Chuo cha Sokoine ambacho kinatoa wahitimu wa masomo mbalimbali ya kilimo na ni jinsi gani wamewahusisha na wakulima. Leo hii tukiulizwa takwimu za wakulima hapa Tanzania hatuzijui, wakulima wakubwa ni wangapi hatujui. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya Serikali kuchimba zaidi na kuona ni jinsi gani wanapata data za kuweza kutusaidia mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mipango mingine inachekesha. Tunajua Tanzania ni nchi ambayo *geographical location* yake yenyewe ni uchumi wa kutosha, bandari ya Dar es Salaam ingeweza ku-serve nchi zaidi ya sita ambazo ni *land locked*, lakini kwa jinsi gani tunatumia bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, leo tuna mpango wa kujenga Bandari ya Bagamoyo. Sasa unajiuliza hii ni mipango ya namna gani! Ukijenga Bandari ya Bagamoyo maana yake lazima ujenge na reli, kwa sababu huwezi kutoa mizigo bandarini kwa maroli, tunahitaji kuboresha bandari tulizonazo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuboreshe Bandari ya Dar es Salaam, tuboreshe Bandari ya Mtwara na tuboreshe Bandari ya Tanga. Tukishaboresha hivi *then* kama tutapata pesa nyingi, ndiyo sasa tuanze mradi wa Bagamoyo. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Serikali ni lazima iweke vipaumbele vyake vizuri, kile kidogo tulichonacho tuhakikishe tunakitengeneza vizuri ili kuweza kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la elimu na nazungumza kama Mwalimu na mdau namba moja wa elimu. Kumekuwa na pongezi nyingi sana hapa ndani za elimu bure, lakini ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015 na ya mwaka 2015 – 2020, katika suala la elimu anasema sasa tutafanya elimu iwe bora, ubora wa elimu. Hapo hapo unazungumzia ubora wa elimu, lakini unaongeza wanafunzi kibao, mwalimu hawezi kufundisha, darasa lililokuwa na watoto 70, leo lina watoto 200, hakuna nafasi ya mwalimu kupita kuona watoto wanasoma kitu gani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema na siku zote nasema kwamba, suala la elimu bure ilikuwa ni kwenye Ilani ya CHADEMA. Tunashukuru mmechukua, lakini tatizo mme-copy na ku-paste, bila ya kutuuliza hivi ninyi mlikuwa mtekelezeje? Kwa hiyo, hili ndilo tatizo. Hivyo, nawaombeni sana mje CHADEMA au UKAWA muulize ilikuwaje, mlikuwa mmepangaje! Msirukie rukie mambo tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania Education Authority (TEA)*, hili ni Shirika la Elimu ambalo kimsingi lingesaidia sana kuboresha elimu. Tulisema, pamoja na kwamba, tuna sheria ya kuunda hiyo taasisi ilikuwa itolewe 2% ya Bajeti ya Serikali ipewe hii Taasisi ili iweze kusaidia, lakini mpaka leo jambo hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la Mpango. Mimi kama mwanamke niseme mpango huu Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ni mwanamke, Waziri simuoni. Huu Mpango haujagusia kabisa masuala ya kijinsia kwa upana wake. Hakuna kitu chochote kimegusa jinsia, wakati tunajua Tanzania na dunia kwa ujumla, wanawake ni wengi kuliko wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuitake Wizara ya Fedha na Mpango kuhakikisha kwamba masuala ya kijinsia yanaonishwa katika huu Mpango. Jana alizungumza, sitaki kwenda kwa kina lakini niseme watoto wa kike wanashindwa kwenda shule. Kama kweli tunataka kuboresha elimu Mheshimiwa Waziri wa Elimu huko naye ni mwanamke anajua, watoto wa kike wanaanza wakiwa sawa au zaidi kwa idadi na watoto wa kiume wanapoanza darasa la kwanza, lakini unapofika sekondari watoto wa kike zaidi ya nusu hawapo shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na sababu kwamba tumeshindwa kuwasitiri watoto hawa kwa kuwapatia *towel* zao kila mwezi bure. Kwa sababu wenzetu Wakenya wanafanya hivyo. Kwa hiyo, nadhani hili ni suala la msingi sana kama kweli tunataka huo usawa hawa watoto wamalize darasa la saba, wafaulu wafike sekondari na huko wafaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la afya. Takwimu zinaonesha kuwa kila mwaka wanawake zaidi ya 8,500 wanafariki, hii ni sawa na mwanamke mmoja anafariki kila saa. Kwa hiyo naomba sana, suala la afya ni la msingi na ndiyo sababu narudia pale pale kwenye suala langu la asubuhi, kama kweli hii nchi ina kipaumbele na inapenda wananchi wake, Serikali isingethubutu kuleta magari 777 kwa ajili ya uchaguzi, yale magari ya washawasha ambayo nimezungumza asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari moja ni dola 250,000 mpaka 400,000 wakati mashine za CT-Scan na MRI bei yake ni hiyo hiyo na Hospitali ya Taifa kama Muhimbili haina, achilia mbali hospitali za mikoa. Sasa ni kwa nini hizo fedha hata kama ni mkopo zisingetumika kuleta CT-Scan katika hospitali zote za rufaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo nasema mipango yetu ndiyo hiyo mibovu namna hiyo. Saa nyingine unajjuliza hivi hawa watu wanafikiria kwa kutumia kitu gani! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iende ijipange vizuri, ituletee mipango yenye tija, mipango ambayo itahakikisha kwamba kweli inaleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la utawala bora na niombe niungane na wenzangu wote waliozungumzia suala la Zanzibar. Uchaguzi wa marudio wa Zanzibar, utakwenda kutumia shilingi bilioni tisa kama ambavyo tumeambiwa, sijui zinatoka Zanzibar, sijui zinatoka huku, *whatever the case*, kama kweli tunaka kuboresha elimu, watoto wetu wanakaa chini, dawati moja ni shilingi 100,000/=, ina maana tungeweza kununua madawati... *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo nimeipata kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwa kura nyingi sana ambazo wamenipa na kunipa Halmashauri yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nimpongeze sana Mheshimiwa Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, lakini na Baraza lake lote ambalo leo hii linachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mimi pamoja na Watanzania wengi tunayo imani kubwa sana pamoja na kasi ambayo mmeanza nayo. Chapeni kazi, longolongo, umbea, majungu, achaneni nayo, fungeni masikio angalieni

mbele, pigeni kazi. Mwanafalsafa mmoja aliwahi kusema kwamba; “you cannot carry fundamental changes without certain amount of madness.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo niseme tu, nimepata nafasi ya kusikiliza michango mingi sana pande zote mbili katika kuboresha kitu hiki. Nimewasikiliza Wapinzani, lakini nimeguswa sana sana aliposimama kuchangia Mheshimiwa Lema. Mheshimiwa Lema ameongea vitu vingi sana hapa ambavyo kimsingi vimenigusa, lakini kwa sauti yake ya upole ya kutafuta huruma ya wananchi, imedhihirisha kwamba, yale Maandiko Matakatifu yanayosema kwamba angalieni watakuja mbwa mwitu wakiwa wamevaa ngozi ya kondoo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, Mheshimiwa Lema amesema sana kuhusu demokrasia. Anadai kwamba Chama cha Mapinduzi kinakandamiza sana demokrasia katika nchi hii, lakini tukumbuke chama chake, mgombea wao Urais mazingira ambayo walimpata, kahamia kwenye chama chake, kesho yake akapewa kugombea Urais, hiyo ndio demokrasia! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Chama chao ni yule yule na wakati wa uchaguzi wale wote waliotangaza ndiyo wagombea Uenyekiti walifukuzwa kwanza na uchaguzi ukafanyika je, hiyo ndio demokrasia?

Pia kuhusu Viti Maalum, hakuna chama ambacho kimelalamikiwa katika nchi hii kama Chama cha CHADEMA katika mchakato wa kupata Wabunge wa Viti Maalum hiyo ndiyo demokrasia? Mnataka demokrasia tufuate maslahi ya CHADEMA, hiyo ndiyo demokrasia ambayo mnataka tuje kwenu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niendeleo kusema tu, wakati Lema anasema alimwambia Mwenyekiti atulie na ninyi nawaambia tulieni mnyolewe. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Tulieni.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lema amezungumza kuhusu ugaidi hapa. Naomba nisema ugaidi ni *inborn issue* ni *issue* ambayo mtu anazaliwa nayo na sifa zake ni uhalifu na kila mtu anafahamu historia ya Lema hapa. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Anasema kwamba, anasema, tulia unyolewe tulia, tulia unyolewe vizuri, tulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa Wabunge walianza kuongea bila mpangilio wakitaka kupewa nafasi ya kutoa Taarifa)*

**MBUNGE FULANI:** Hawa wajinga hawa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa, tafadhali.

**MWENYEKITI:** Tuvumiliane, tuvumiliane tu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Lema anasema kwamba, amani ya nchi hii ikichafuka...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio wakitaka kupewa nafasi ya kutoa Taarifa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Ahsanteni.

Tunaendelea, nisingependa haya malumbano ambayo hayana tija, tunaendelea na hoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba Taarifa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea *please!*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wamesema watu hawa kama nchi hii itakuwa na vurugu basi mapato au uchumi wa nchi hii utashuka, lakini kila mtu anafahamu kwamba Arusha ni Mji ambao ulisifika kwa kuwa na amani sana, Arusha ni Mji ambao ulisifika kwa kuwa na uchumi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hapa Mjumbe yule aliyesimama amesema uchumi wa Arusha umeshuka. Leo hii kila Mtanzania anajua kwamba Mheshimiwa Mbunge aliyeko sasa hivi wa Arusha Mjini amekuwa ni chanzo cha kuchafua amani ya Mji wa Arusha na amesababisha uchumi wa Arusha kuporoka kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanataka twende kwao tukajifunze nini hawa! Tulieni mnyolewe vizuri. Lakini naomba niseme, ndugu zangu lazima tuwe makini sana na niwasihi, Wapinzani ni marafiki zangu sana wengi. Lazima tuwe wakweli na tulitangulize Taifa letu mbele.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Tunapoomba kuchangia, tuchangie katika namna ya kujenga, siyo katika namna ya kubomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Mpango huu, mpango huu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio wakitaka kupewa nafasi ya kutoa taarifa)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu.

**MWENYEKITI:** Tunatunza dakika zako. Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Taarifa. Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 68(8) na najielekeza kwenye kanuni ya 64. Kwa ruhusa yako naomba nisome inasema: "Bila kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge. Nitaenda pale kifungu (g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine lakini vilevile lugha ya matusi na mambo ya uongo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba nitoe taarifa kwamba, kama mzungumzaji ambaye anaendelea kuchangia anaweza akathibitisha kwamba, Mheshimiwa Lema ndiye anavunja amani Arusha, alijulishe Bunge hili na Watanzania wajue na dunia ijue, vinginevyo afute maneno yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nikupe Taarifa hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nikisimama wote mnaketi.

Waheshimiwa Wabunge, nafahamu baadhi yetu bado tunajifunza kanuni hizi. Ukisimama kwa mujibu wa kanuni ya 68 ya Taarifa. Unampa Taarifa Mbunge ambaye anaongea wakati huo. Kiti kikishakubali wewe unaketi halafu Mbunge huyo ndiyo anatoa Taarifa. Nitakuuliza kama unaikubali au unaikataa, ni hiari ya moyo.

Lakini ukiomba Mwongozo, Mwongozo kama nilivyosema asubuhi ni kweli kwa sababu wengi hatufahamu Kanuni ndiyo maana tunapenda sana tupitie kwenye kuomba Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu unaweza ukaomba kuhusu utaratibu, nikakuuliza ni kanuni ipi uka-*fumble* na nikakwambia *you are out of order* na inakuwa haipendezi kwa kiongozi kumwambia hivyo na ndio maana inapendeza kama mtakuwa mnakuja kuomba Mwongozo wa Spika. Mwongozo wa Spika unaomba tu pale ambapo hakuna Mbunge ambaye anaongea na ndio tutakuwa tunakwenda vizuri.

Unaweza ukatumia Mwongozo wa Spika, kupata suala ambalo ungetaka kulijua kwa utaratibu. Nadhani tukienda hivyo tutakwenda vizuri. Nimeeleweka?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Dakika zangu zimebaki ngapi!

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa baada ya kuzungumza hayo, niende kuzungumza yale ya wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini, dose imeshaingia hiyo.

Suala la kwanza, kwanza niungane na mchangiaji Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa alichozungumza hapa, alizungumza kwamba, Kigoma ni miongoni mwa mikoa ambayo imeachwa nyuma sana. Pamoja na Mpango mzuri ule, naomba niseme kwamba kwanza kwa suala la miundombinu, iko barabara ya kutoka Nyakanazi mpaka Kidahwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma wote wanafahamu kwamba hapo ndipo uchumi wa Kigoma umefungwa. Naomba sana Serikali ya Awamu ya Tano, niseme tu kwamba bajeti ijayo kama haitakuwa na barabara hii nitatoa shilingi kwenye bajeti hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kuhusu reli ya kati kwa *standard gauge*. Reli ya kati ni mhimili wa uchumi wa nchi nzima ya Tanzania, lakini waathirika wakubwa sana ni sisi watu wa kanda ya magharibi. Naomba niseme tu, niungane na wachangiaji wote, tuhakikishe reli hii ya kati inajengwa kwa *standard gauge*. Narudia maneno yale yale, kama kwenye bajeti tutakapokutana hapa kuja kujadili maendeleo haya, reli hii kama hamjatuletea kwa kinagaubaga tutaijengaje kwa kweli nitatoa shilingi. (*Makofi*)

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine...

**MWENYEKTI:** Ahsante sana.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee kidogo.

**MWENYEKTI:** Tunaendelea.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu jioni ya leo. Vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu, muweza wa yote aliyeniwezesha kusimama kuweza kuzungumza jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana sana wananchi wa Tanzania kwa kujua mchele ni upi na pumba ni zipi na kuchagua Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa kishindo kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa upande wa Wabunge 73% na kwa upande wa Madiwani 74% na kwa upande wa Viti Maalum 80%, kwa kweli wananchi Mwenyezi Mungu awajalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kusema hapa, tunawaahidi kwamba imani huzaa imani, tutaendelea kuwatumikia kwa moyo wetu wote na hata pale ambako Chama cha Mapinduzi hakikupata kura tutawahudumia bila ubaguzi likiwemo Jimbo la Arusha na Majimbo mengine ambako CCM haikushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana, mpendwa wetu Rais wetu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi alivyoanza kutekeleza kazi. Ameanza vizuri, anafanya kazi nzuri na kama kura zingepigwa leo ushindi wa CCM ungekuwa ni 69.999%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, napenda sasa kujielekeza kwa mambo machache ambayo nimeyapanga kuyatilia mkazo katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yangu ya kwanza ni kwamba, Waziri wa Fedha na timu yake yote wameandaa vizuri Mwelekeo wa Mpango wa mwaka

2016/2017. Ni Mpango unaoeleweka, wenye matumaini na ambao umelenga kuwakomboa Watanzania katika suala zima la kuwakomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa sababu endapo Mpango huu utapangwa na ukatekelezwa, nina imani yale ambayo tumeyaandika kwenye Ilani ya CCM yataweza kufikiwa. Naomba sasa nitoe ushauri kwa mambo machache yafuatayo na nitaanza suala zima la ukusanyaji wa kodi. Ili mpango utakaotengenezwa usiendelee kubaki kwenye makaratasi, nilikuwa naishauri Serikali yetu hii ya CCM ijielekeze katika kuhakikisha inakusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza kazi nzuri ambayo imeanza kufanywa ya kukusanya mapato, lakini bado kuna baadhi ya mapato yanaishia mifukoni mwa watu, pia bado kuna mashine za kukusanyia mapato ni feki na bado kuna taasisi ambazo zinatumia vitabu ambavyo havieleweki katika mfumo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niishauri Serikali ili Mpango wa Maendeleo uweze kutekelezwa katika mwaka 2016/2017, lazima pia tuweke mkakati namna ambavyo Serikali itakusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nishauri Serikali yetu na Mawaziri wetu kwamba, katika kutekeleza Mpango huu, hauwezi kutekelezeka kama hawajadhibiti upotevu wa mapato na matumizi yasiyokuwa ya lazima. Naiomba sana Serikali yetu, ijielekeze katika kuhakikisha Mpango unaokuja 2016/2017 unalenga kwenda kuwakomboa Watanzania na hasa wanawake. Naomba Mpango unaokuja 2016, tujielekeze katika kuhakikisha suala zima la maji na hasa vijijini linapatiwa ufumbuzi ili wanawake wetu wanaotembea umbali mrefu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, mwaka jana tulipanga mpango mzuri, lakini kwa bahati mbaya sana, hivi ninavyozungumza, sekta ya maji imepata asilimia nane tu ya bajeti. Sasa kama tutatengeneza mpango mzuri kama utakavyokuja na kama fedha hazikutafutwa na zikatengwa, Mpango wetu utabaki kwenye makaratasi na matokeo yake lengo ambalo limekusudiwa halitafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika kuhakikisha Mpango unatekelezwa ni lazima tujielekeze sasa kuweka vipaumbele katika sekta ambazo zitaongeza mapato na napongeza mpango wa Serikali wa kuhakikisha tunafufua viwanda, tunaanzisha viwanda vipya na kukaribisha wawekezaji waje kuwekeza, lakini hapa naomba nitoe ushauri.

Naomba niishauri Serikali kwamba isijitoe katika suala zima la uwekezaji wa viwanda na naomba Serikali isitegemee wawekezaji kutoka nje peke yao. Ni lazima Serikali ijipange kuhakikisha tunawawezesha Watanzania wa kati, wafanyabishara wadogo na wafanyabiashara wakubwa ili wawe na uwezo wa kujenga viwanda hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo viwanda peke yake, ni pamoja na kilimo na hasa Mwenyekiti hapa ninaposisitiza, uchumi wetu hauwezi kukua kama kilimo chetu bado ni cha kutegemea mvua. Nahimiza twende na kilimo cha umwagiliaji na tuongeze wigo, badala ya kutegemea mikoa ya Nyanda za Kaskazini ndiyo zilishe nchi nzima, hebu tuangalie na Kanda ya Ziwa iliyozungukwa na mito na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie mikoa ya Kanda ya Kati ambayo bahati mbaya ni mikoa kame, kuna Mkoa wa Tabora, Singida, Dodoma ambapo sasa hivi mvua zinanyesha mpaka tunakosa pa kupita, lakini Mkoa wa Dodoma kila siku wanalia njaa na tunategemea Mkoa wa Ruvuma na Rukwa. Naiomba Serikali iipe sekta ya kilimo fursa ya pekee na katika bajeti inayokuja tuipe nafasi inayostahili, tuipe fedha ya kutosha ili sekta ya kilimo iweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ili tuweze kufikia malengo tunayokusudia, ni lazima tujielekeze katika suala la uvuvi na tujielekeze katika kuvua katika kina cha bahari kuu. Tujenge Bandari na hasa hiyo ya Bagamoyo na Bandari zingine. Kama hatutaweza kwenda kuvua kwenye kina cha maji marefu, tukaifanya sekta ya uvuvi kama ni sekta ya uzalishaji ya kiuchumi, Mpango wetu utabaki kuwa kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia, hebu watumie ushauri aliotoa Mwenyekiti Chenge na timu yake wakati ule wa bajeti, Waziri wa Fedha, achukue ushauri ule, ni ushauri mzuri sana, kuna mambo mengi sana yapo mle, hebu angalieni vyanzo vipya ili uchumi wa nchi yetu uweze kukua na tuweze kupiga hatua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali yetu, pamoja na mipango mizuri iliyowekwa hapa, lakini tujielekeze katika kuwawezesha wanawake kiuchumi. Nimefurahishwa na Mpango uliopo wa kupeleka milioni 50 katika kila kijiji na mtaa, naomba katika mpango unaokuja, lazima tuweke mfumo, hizi milioni 50 zitafikaje katika kila kijiji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni lini Serikali kwanza, itamteua Kamishna wa Dawa za Kulevya ili kuleta ufanisi wa kazi katika Tume, maana ni muda mrefu tangu aliyekuwa Kamishna muda wake kwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa nini Serikali mmeamua kupeleka fedha za *methadon (MDH)*, badala ya kupitia kwenye Tume ya Dawa za Kulevya kama ilivyokuwa zamani? Serikali haioni kuwa fedha hizo zitakuwa hazifiki kwa wakati kwenye vituo husika vinavyotoa huduma hiyo ya *methadon* kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya?

Tatu, kumekuwa na mkakati wa kuvuruga utaratibu mzima wa kuwarudisha vijana walioathirika na dawa za kulevya kurudi kwenye hali yao ya kawaida, ambapo wauzaji na wasambazaji wa dawa za kulevya huenda kwenye vituo vinavyotoa huduma ya *methadon* kwa kuwashawishi vijana kuanza kutumia tena dawa za kulevya. Kitendo hicho kinarudisha nyuma jitihada za kupambana na dawa za kulevya. Je, Serikali mna mkakati gani wa kuhakikisha mkakati huo unakwama?

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Mpango ulio mbele yetu. Namshukuru Mungu kwa neema na rehema zake kwangu na kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Ileje kwa kunipa ridhaa ya kuwa Mbunge wao, nawaahidi kuwa sitawaangusha na nitawatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake na Maofisa wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwongozo mzuri na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na wa mwaka mmoja. Mpango uliowasilishwa ni mzuri, lakini nianze kwa kumtaka Mheshimiwa Waziri atueleze wananchi wa Ileje kuwa wao atawawezesha vipi kuingia katika uchumi wa nchi? Mpango wa Maendeleo unaotarajiwa umeweka vipaumbele muhimu vilivyomo ukurasa wa 23 hadi 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na viwanda; wazo la viwanda ni jema hasa ukizingatia kuwa kwa muda mrefu bidhaa zetu nyingi zimekuwa zikiuzwa ghali na kwa hivyo kuwapatia fedha kidogo sana wazalishaji. Bidhaa nyingi zimekuwa zikipotea kabla na baada ya kuvuna na hii pia husababisha upotevu

wa fedha za uzalishaji, hii pia imesababisha wazalishaji kupunguza nguvu ya uzalishaji kwa sababu ya kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kupanga maendeleo haya ya viwanda ni lazima mambo ya msingi yatakayowezesha ujenzi na uendeshwaji wa viwanda hivyo yapewe kipaumbele hususan miundombinu ya barabara zinazopitika kwa mwaka mzima, miundombinu ya umeme wa uhakika unaopatikana mwaka mzima, upatikanaji wa maji na upatikanaji wa malighafi za kutosha. Hali ilivyo sasa hata viwanda vilivyopo vina changamoto nyingi za miundombinu tajwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuzungumzia viwanda bila kuainisha mpango wa kuboresha kilimo, ufugaji, uvuvi na uchimbaji wa madini ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo makubwa ya uzalishaji wa kilimo ndiyo kwa kiasi kikubwa ambayo yana miundombinu mibovu sana. Nitoe mfano wa Wilaya ya Ileje, ambao tangu tupate Uhuru na tangu Jimbo lile lianzishwe miaka 40 iliyopita halijawahi kupata barabara ya lami hata moja ilihali Wilaya nyingine zote zinazoizunguka Ileje wana barabara za lami. Sasa kwa hali hii Ileje itawezaje kuvutia wawekezaji wa kilimo cha biashara, uvuvi na ufugaji ambao utaleta ujenzi wa viwanda? Naiomba Serikali iwekeze katika miundombinu ya barabara Ileje ili na sisi Wanaileje tujenge viwanda kuanzia vidogo, vya kati na vikubwa. Suala la miundombinu Ileje ni nyeti na ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna umeme, barabara, masoko, kituo cha forodha, uhamiaji wakati kuna biashara kubwa sana ya mpakani na Malawi na ni njia ambayo ingekuza biashara kubwa sana na nchi jirani ya Malawi. Ileje ni Wilaya ambayo ingepata fursa sawa na Wilaya nyingine ingepiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Ileje inahitaji ni kupimiwa ardhi ili wawekezaji waje kuwekeza. Ileje inahitaji kujengewa masoko na kituo cha mpakani kwa ajili ya kuendeleza vizuri biashara na nchi jirani za Malawi na Zambia. Ileje inahitaji taasisi za ufundi, majengo ya utawala na biashara ili Ileje isibakie kama kijiji kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazingatia kuboresha miundombinu yote na kuboresha kilimo, ufugaji na uvuvi, basi tuzingatie suala la kuwa wazalishaji wakubwa katika sekta hizi ni wanawake. Mpango huu uzingatie na ujielekeze katika masuala ya jinsia na makundi maalum. Tanzania ilishajiingiza katika mfumo wa *gender budgeting*, basi vipaumbele vyote vioneshe jinsi mipango hii inavyozingatia masuala ya kijinsia katika mikakati, katika bajeti zake ili wanawake, vijana, walemavu na wazee wawe sehemu ya Mpango huu wa

Maendeleo. Nashauri Mpango huu uweke wazi mgawanyo huu ili makundi yote muhimu yashiriki kikamilifu katika maendeleo haya yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango unapaswa kuendeleza yale yote yaliyoanzishwa na Serikali kwenye kuleta usawa wa jinsia. MKUKUTA II, hasa ile *cluster* ya pili, *Big Result Now* ilizingatia usawa wa kijinsia. Je, hivi viko wapi sasa katika Mpango huu? Serikali ilikuwa imeshakuwa na mwongozo wa bajeti inayozingatia jinsia kwa Serikali za Mitaa, Serikali Kuu, Vitengo na hata *BRN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chambuzi nyingi zilishafanywa kwenye sekta nne na kulikuwa na tamko la Serikali juu ya kila sekta kuainisha jinsi ambavyo imezingatia masuala ya kijinsia, takwimu zilitakiwa kunyumbulisha masuala ya kijinsia na *labour force survey* iliyofanywa ilionesha masuala ya kijinsia. Tathmini ya matumizi ya fedha za umma ilishafikiwa chini ya *PER* kama nyenzo ya kuhakikisha utekelezaji wa Mpango huu. Malengo ya milenia yalikuwisha na sasa tuko kwenye *SDGs* ambavyo ni lazima ioneshe ni jinsi gani hayo yote yatashughulikiwa katika Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa takwimu kwenye maeneo yote muhimu kijinsia urekebishwe. Msingi wa usawa wa kijinsia ni muhimu kuhakikisha kundi kubwa la wanawake, vijana, walemavu, wazee na wanaoishi na *VVU* kuwa katika Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za kuingiza masuala ya jinsia kwenye Mpango; kwenye utangulizi Serikali ingefanya marejeo kwenye Mpango wa Maendeleo kuhusu masuala ya kijinsia na miongozo tuliyojiwekea katika kuingiza jinsia katika mipango ya maendeleo.

Lengo la tano, kuwe na utambuzi zaidi wa umuhimu wa usawa wa kijinsia. *BRN* imeainisha kipengele cha jinsia na ufuatiliaji na kutathmini mpango mzima, Mpango unyumbulishe viashiria vyote kutumia hali ya uchumi jinsia, walemavu na wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumziwa idadi, ni muhimu tukazingatia kutamka kuwa mfumo una taswira hasi kwa wanawake. Idadi ya Kaya zinazoongozwa na wanawake zinaongezeka, bado hatujasimama katika nafasi nzuri sana katika masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda; je, Serikali imezingatia vipi suala la ujuzi kwa maana ya:-

- (i) Elimu - usawa na jinsia, ufundi, vyo viko, ajira rasmi;
- (ii) Kilimo - kina sura ya mwanamke ambaye hana umiliki wa ardhi wala nyenzo za kisasa za kilimo, ufugaji, mitaji na kadhalika.

Viashiria vya umaskini vina sura ya wanawake vijijini. Je, hili limezingatiwa vipi kwenye Mpango huu?

- (iii) Ajira - 1.4; wanawake wasiokuwa na ajira; je, Mpango unalishughulikia vipi? *BRN* - sura iko kimya kuhusu masuala ya jinsia katika *BRN*, asilimia tano tu ya wanawake wanamiliki ardhi wakati asilimia 44 wanafanya kazi za uzalishaji;
- (iv) Mikopo - wanawake wengi sana hawana fursa, mfumo wa fedha ni mfumo dume;
- (v) Huduma za jamii; na
- (vi) Ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya mama na mtoto, utapiamlo, kukosa haki zao za msingi, kukosa kujiamini na mila na desturi, ugandamizi na sheria. Kuwe na lengo mahsusi la kuzingatia masuala ya kijinsia ili kuzingatia juhudi zilizofanywa na Serikali kujielekeza katika mikakati, viashiria na rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya Tatu; mikakati yote haijanyumbulisha mtazamo wa kijinsia, kwa hiyo, lazima mikakati ioneshe jinsi wanawake, vijana, walemavu watakatavyofikia malengo haya kwa kuwapa vipaumbele kwenye Mpango na kwenye bajeti tajwa. Kwenye kujenga uwezo, nini mkakati wa kuwajengea uwezo watendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *follow up issues* katika Wilaya ya Ileje; kwanza ni ujenzi. Barabara kuu tano zinazounganisha Ileje na Kyela inayotokea Kusumulu - Kyela kupitia Kata ya Ikinga na Malangali hadi Ileje Mjini. Barabara inayounganisha Wilaya ya Rungwe na Ileje inayotokea Mji wa KK Rungwe na Ileje, barabara inayotokea Mji wa KK na kuingia Ileje kupitia Kata za Luswisi, Lubanda, Sange na Kafule. Barabara ya kuunganisha Wilaya ya Momba na Ileje, inaanzia Mpemba na kupitia Kata ya Mbebe, Chitete, hadi Itumba. Barabara inayounganisha Wilaya ya Mbeya Vijijini na Ileje kupitia Mbalizi, kupitia Vitongoji vya Mbeya Vijijini hadi Itale, Ibaba na Kafule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia skimu za umwagiliaji; zilizopo Ileje ni Jikombe iliyopo Chitete na Ikombe iliyopo Itumba yenye banio, lakini mifereji haijachimbwa. Jikombe ilichimbwa lakini mifereji haijasajiliwa, hivyo mfereji umekuwa ukijifulia fulia. Skimu ya Sasenge imebakiza mita 2000 kumaliza usafishaji wa mfereji mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji; Mradi wa Ilanga, Mlale-Chitete inasemekana mingine inasubiri makabidhiano ingawa Malangali na Luswisi inahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa REA; vijiji vilivyopata umeme ni 35 ambavyo umeme umewashwa ni vinne tu. Ileje ina Vijiji saba. Vijiji ambavyo havipo katika orodha ya kuwekewa umeme ni 25. Je, lini Vijiji vilivyopo kwenye orodha vitakamilishiwa na ambavyo havimo kwenye orodha vitajumuishwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi; Ileje imekuwa kwa muda mrefu ikikabiliwa na tatizo la watumishi katika sekta mbalimbali ikiwemo Maaafisa Tathmini (*Valuers, Surveyors* na Afisa Ardhi). Hii imeathiri kwa kiwango kikubwa upimaji ardhi na kutoa hati miliki kwa wananchi na wawekezaji wa viwanda, biashara na kilimo cha biashara. Hii inawanyima fursa nzuri za maendeleo wana Ileje na Taifa kwa ujumla. Lini Serikali itatupatia Wilaya ya Ileje Maaafisa hawa muhimu ili kuharakisha upatikanaji wa hati hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, Ileje inalima kwa wingi nafaka zote unazoweza kuzifikiria, mazao ya mbegu za mafuta, matunda, mboga, pareto, kahawa, miti ya asali na pia ina fursa ya kulima cocoa, vanilla na mazao ya misitu. Kuna fursa ya ufugaji wa mifugo aina zote na nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje inapakana na nchi jirani ya Malawi na Zambia, zaidi ya yote kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi kuna kituo cha mpakani ambacho ni kichekesho! Askari wetu pamoja na Maaafisa wa Uhamiaji wanakaa katika banda la ovyo, hakuna ofisi rasmi na isingekuwa mahusiano yetu mazuri na Malawi hawa wangeshindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Uhamiaji iko katikati ya mji kwenye nyumba ya kupanga. Nafurahi kusikia kuwa, uhamiaji wana mpango wa kuja kujenga Chuo cha Uhamiaji Ileje na vilevile Kituo cha Forodha kinaenda kujengwa ili kihudumie mpaka na kuhakikisha biashara ya mpakani inafanywa kwa ufanisi zaidi kwa manufaa ya Taifa na wananchi wa Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za jamii kama afya, elimu, maji na mazingira pia zizingatiwe. Kuhusu suala la Watumishi wa Umma; kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Idara ya Ardhi, Elimu, Afya na Mazingira. Hii imeathiri sana utendaji na ufanisi na kuzorotesha zaidi maendeleo ya Ileje. Watumishi wengi hawapendi kufanya kazi Ileje na hawaripoti kabisa na hata wakiripoti huondoka na kuacha pengo.

Kuhusu huduma za fedha, ni chache sana, Benki iko ya NMB na Tawi moja tu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma za kifedha katika wilaya nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ni dhahiri kuwa, kwa hali hii Wilaya ya Ileje itachukua miaka mingi sana kufikia uchumi wa kati kama hatua kubwa na za haraka hazitachukuliwa katika:-

(i) Ujenzi wa miundombinu.

(ii) Upatikanaji wa umeme.

(iii) Upatikanaji wa maji.

(iv) Ujenzi wa shule, vyuo na taasisi za kiufundi kama uhamiaji, mamlaka ya kodi, taasisi za kifedha, taasisi za kuhudumia wanawake, vijana, wazee, walemavu na wanaoishi na VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusikia kutoka kwa Waziri, ni nini mkakati wake wa kutuhakikishia Wanaileje kuwa na sisi tutafikia katika uchumi wa kati. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa tunahamia upande wa Serikali, Mawaziri na wenyewe wanachangia, lakini kwa dakika tano tano. Waseme yale ya msingi ili kumuandalia njia Mtoa Hoja. Tutakwenda dakika tano tano, lakini ili tuweze kuendesha shughuli zetu vizuri, tutaona mwishoni pale kama kutakuwa na haja ya kuongeza nusu saa ambayo iko ndani ya mamlaka ya kiti. Tuanze, Mheshimiwa Lukuvi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya dakika tano. Kama tulivyokuwa tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, Wabunge wengi wamerudia maneno mengi ambayo yalisemwa wakati ule. Nataka kurudia kuwaahidi kwamba katika kutayarisha Mpango huu, sekta ya ardhi ni msingi na muhimu sana katika maandalizi ya kujenga uchumi kama ilivyoandaliwa. Hivyo, nataka kuwaahidi kwamba yale yote waliyozungumza tutashirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha mikakati mbalimbali ya kuboresha ardhi ili iweze kutumika vizuri katika uchumi tutaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na michango hii, nataka niseme moja, jana Mheshimiwa Mbunge mmoja Anatropia Theonest, kwanza nataka nimwombe radhi Mheshimiwa uncle wangu Tundu Lissu amejitahidi lakini naona niliseme kwa sababu tunamaliza. Jana alinihusisha kwa jina kwamba mwaka 2011 nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa hiyo nilihusika sana katika kupora viwanja vya Mabwepande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi hata waandishi wa habari wamerekodi kama ilivyo hata kutafakari kidogo, mimi 2011 nilikuwa kwenye kiti

hiki hapa, nilikuwa *Chief Whip*. Sasa mdogo wangu wa Segerea, ungechanganya kidogo tu ungejua kwamba unayoyasema hata kama umeambiwa ungetumia na akili yako, ungejua, lakini sikutaka kuingia kwenye huo mjadala kwa sababu nilimwomba *Chief Whip* wa Upinzani ashughulikie nafikri imeshindikana, lakini nimekuandikia Mheshimiwa Mwenyekiti barua nafikiri kama ana ushahidi atakuletea ili tuendelee na safari hii kwenye Kamati ya Maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nataka kusema, Mpango wa Serikali, mpango unaosimamiwa na Wizara yangu ni kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinapimwa ili kila mwananchi aweze kumiliki. Ni kwa kumiliki ardhi kila mtu ndipo tutaongeza na mapato ya Taifa na ndiyo maana *speed* ya umilikishaji sasa tunaitilia umuhimu na hata sasa nimeagiza, *speed* ya utoaji hata *tittle* ambayo ilikuwa ni miezi sita sasa tumeanza kutoa hati kwa mwezi mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la migogoro, hatuwezi kuujenga uchumi kama hatuna utulivu. Wananchi wanagombana kati ya hifadhi, vijiji na watu binafsi. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishieni taarifa zenu tumeshazipata. Hili halihitaji Mpango kuandikwa, sisi tukitoka Bunge hili tunaanza. Taarifa zenu zilizokuja na Mheshimiwa Maghembe na TAMISEMI tutaanza kushughulikia ili kuhakikisha kwamba watu tunawapa raha, waweze kusimamia shughuli zao za maendeleo ya kiuchumi kwa kupunguza migogoro iliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia upimaji kama nilivyosema, mwezi huu tutaanza Wilaya ya Kilombero na Ulanga kama Wilaya za mfano za upimaji wa kila eneo. Upimaji huu hautanyang'anya ardhi ya mtu, lakini tutahalalisha ardhi yake na tumpe karatasi zitakazomwezesha kutambulika Kiserikali kwamba ni mmiliki halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hizo wilaya, tutaona mfano huo na gharama zake ili twende kufanya nchi nzima. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia tu Waheshimiwa Wabunge, sekta ya ardhi tutasimamia mawazo yenu, haya yaliyopo kwenye mpango na yale ambayo ni ya utekelezaji wa muda mfupi maana yake haya ya mpango yanaweza kuwa yameandikwa machache, lakini tuliyoyasikia ni mengi, tutasimamia ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Ardhi inakuwa kwa manufaa Watanzania wenyewe wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tu kwamba, wakati mwingine kumekuwa na dhoruba za kutupiana maneno, upande wa rafiki zangu hawa, wakati mwingine wanatumia maneno makali sana kwa Mawaziri, wanasahau kwamba Mawaziri hawa ni Wabunge kama ninyi. Hata hivyo, haipiti dakika moja, wana-cross kwa Mawaziri hao hao wanataka kuteta. Sasa mfikirie jamani, binadamu hawa wote tunafanana, haiwezekani huyo Waziri umwite

tapeli, mjinga halafu una-cross hapa akusikilize kama vile hukusema kitu. (Makofi)

Ningependa tujenge hoja kama Mbatia, kama Zitto Kabwe, hoja nzito lakini hazina kashfa wala matusi kwa mtu mmoja mmoja, kwa sababu Mawaziri hawa siyo vyuma, ni binadamu. Kwa hiyo, naomba tu, wote hapa ni marafiki na Serikali haitawabagua, itawatumikia wote, lakini tukiwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kuzungumza machache mbele ya hoja hii iliyoko mbele yetu. Pili, nasema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mjadala huu ulipoanza, Wabunge wote hasa Wabunge wa Kanda ya Ziwa walikuwa wanasimama mbele yetu na kila mmoja kwa hisia tofauti, kwa ukali na kwa uchungu sana wanazungumzia kuhusu reli ya kati. (Makofi)

Mimi Mwenyewe kama Waziri imenigusa sana na inaniuma sana jinsi gani ambavyo tunasimamia mpango wa ujenzi wa reli ya kati. Serikali vilevile inaliona kwamba hili ni jambo muhimu na tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tutajenga reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa reli ya kati unaotarajiwa kujengwa kwa kiwango cha *standard gauge* utakuwa na kilometa 2,560. Mtandao huu utajumuisha reli kati ya Dar es Salaam - Tabora - Isaka, reli kati ya Tabora - Kigoma kilometa 411; reli kati ya Uvinza - Msongati, kilometa 200; reli kati ya Isaka - Mwanza, kilometa 249; reli kati ya Kaliua - Mpanda - Kalema, kilometa 360; na reli kati ya Isaka - Keiza, kilometa 381; pia itakwenda reli kati ya Keiza - Rusumo na mwisho tumalizia kuunganisha na wenzetu wa Kigali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli kati ya Tabora - Kigoma, kilometa 411, zilifanyiwa *feasibility study* mwaka 2015 mwezi Februari na sasa hivi zimekamilika. Reli kati ya Kaliua - Mpanda vilevile zimefanyiwa *feasibility study* katika kipindi hicho. Reli kati ya Isaka - Mwanza, kilometa 249 zilifanyiwa *feasibility study* na kampuni ya Denmark na kazi ilikamilika mwezi Mei mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli kati ya Mpanda - Kalema na Uvinza - Msongati inafanyiwa *feasibility study* na kampuni ya *HP-Gulf* ya Ujerumani. Kazi hiyo ilianza mwezi Machi, 2015 na ikamalizika mwezi Desemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali iko katika mpango wa kutafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati katika kiwango cha *standard gauge* ambapo reli hiyo kama nilivyosema itaunganisha matawi niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na maoni kwamba tutumie Mfuko wa Reli kwa ajili ya kujenga reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Kwa taarifa tu, Mfuko wa Reli kwa mwaka tunapata shilingi bilioni 50. Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, kwa kilometa 2,561 itaigharimu takribani dola za Kimarekani bilioni 7.5, sawa na shilingi trilioni 15. Hii inaweza kupungua ama inaongezeka, itategemea kama tutaamua tutajenga tuta jipya, pesa itakuja hii na tukiamua kuchanganya reli baina ya *meter gage* na *standard gauge* inaweza kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kutumia Mfuko huu wa Reli, itachukua muda mrefu si chini ya miaka 300 kwa shilingi bilioni 50 ndiyo tuweze kupata trilioni 15. Kwa hivyo, Serikali sasa inaweka kipaumbele chake cha kwanza katika kujenga reli ya kati kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu mwingine utakaoweza kutumika ni utaratibu wa ushirikiano baina ya nchi na nchi yaani *Bilateral agreement* ili kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Serikali imeona mradi huu ni muhimu na tutasimamia kwa nguvu zetu zote ili tuhakikishe kwamba reli hiyo ambayo ina manufaa makubwa sana kwa nchi yetu hasa upande wa Congo kule na upande wa Burundi iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napenda kumpongeza sana Dkt. Mpango, Naibu wake na Makatibu Wakuu na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ya kuandaa Mpango na kuuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumefarijika na kama Serikali tumeweka hifadhi ya mazingira kama vipaumbele muhimu katika mipango ya maendeleo ya nchi. Wakati wa bajeti Serikali italeti mipango ya kina ya kueleza tafsiri yake hasa ni nini na nini kitafanyika katika kuhakikisha kwamba hifadhi ya mazingira inazingatiwa katika mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba nimefadhaika kidogo kwa michango iliyotoka hapa Bungeni kwa Wabunge walio wengi. Sisi Wabunge bila kujali Majimbo yetu, shida za watu wetu zinafanana bila kujali Jimbo ni la Upinzani au ni la CCM. Unapoikejeli Serikali, unapomkejeli Rais, unapowakejeli Mawaziri, angalau acha fursa ya uwezekano wa kuomba ushirikiano, kufanya kazi na Serikali hiyo hiyo, Rais na Mawaziri hao hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndiyo wenye Serikali, ndiyo tunapanga bajeti, ndiyo tunatekeleza maendeleo. Acha fursa ya ubinadamu wa kuweza kufanya kazi kwa pamoja. Mimi naelewa kwamba Upinzani kazi yao kulaumu, lakini ipo fursa ya kutoa Mpango mbadala. Hivi ninyi kwa kazi anayoifanya Mheshimiwa Magufuli leo, kipi mngefanya tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bunge lililopita walikuwa wanatulaumu kuna uzembe, kuna ubadhirifu, kuna ufisadi; Mheshimiwa Magufuli anatibu uzembe, ubadhirifu, ufisadi bado mnatulaumu. *What would you have done differently*, leo kama mngekuwa na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tishio hapa, watu wanazungumza amani itavurugika. Maarifa yaliyounda nchi yetu, maarifa yaliyounda Muungano wetu, maarifa yaliyolinda amani yetu mpaka leo ni makubwa kuliko ukomo wa kufikiri wa baadhi ya watu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu utadumu, amani yetu itadumu, nchi yetu itakuwa moja, hizi kauli za kutisha kwamba nchi italipuka, kutakuwa na mvurugano, tusiwatishie wananchi dola ipo na busara ya viongozi ambao walishiriki kwenye kuiunda nchi hii ipo. Wapo ndani ya Chama cha Mapinduzi, wapo ndani ya Serikali, nchi yetu itaendelea kuwa ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa suala la Zanzibar, naelewa haja ya kuonesha hisia ndani ya Bunge hili, lakini ufumbuzi haupo ndani ya Bunge hili. Ufumbuzi wa suala la Zanzibar haupo kwenye Ofisi za Mabalazi wa kigeni, ufumbuzi wa suala la Zanzibar haupo barabarani na mitaani. Ufumbuzi upo ndani ya Katiba na ndani ya Sheria za Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba tupo kama Serikali, tupo imara, tutafanya kazi yetu bila uoga, bila wasiwasi na Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri, anaungwa mkono na Watanzania wote na wenzetu msione aibu kumuunga mkono. Siyo dhambi kama mtu anafanya kazi nzuri, kama Serikali inafanya kazi nzuri, kama Mawaziri wanafanya kazi nzuri, siyo dhambi kuwaunga mkono kwa sababu nchi yetu ni moja, kazi yetu ya kuleta maendeleo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niseme tu kwamba mimi na timu yangu ya wataalam pamoja na Naibu wangu, tumepokea maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge waliyoyatoa kuhusu Wizara yetu ambayo wangependelea yaonekane kwenye Mpango na tutakaa na wenzetu wapokee Mpango wetu kama Wizara waweze kushirikisha kwenye Mpango mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba pia tutatumia mawazo ambayo tumeendelea kukusanya kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na leo hii tunakutana na Wabunge karibu wa sekta zote, nadhani Bunge litahamia pale Msekwa. Lengo letu tunapotoka hapa, tunavyokwenda sasa kukamilisha jambo zima la Mpango tuwe na mawazo kwa upana yanayotokana na uwakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tu kusema kama mnataka mali mtaipata shambani na leo hii niende kwa kusema kwamba tunavyotawanyika hapa katika maeneo ambayo yanahusu sekta yangu, wale ambao wanatusaidia walioko mikoani na wenyewe watusaidie na nitazungukia katika maeneo hayo kuweza kuona utekelezaji wake.

Jambo la kwanza, tunajua utaratibu wa mgawanyo bora wa ardhi unaanzia ngazi ya kijiji, unakwenda mpaka ngazi za mikoa na baadaye unaenda ngazi ya Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara yake ambako kuna timu ya mpango bora wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekeze ofisi zetu za Wakuu wa Mikoa wachukue hatua ya kuzungukia kila eneo, wapange maeneo ambayo wanayabainisha kwa ajili ya ardhi ya mifugo na kwa ajili ya ardhi ya kilimo na nitapita kuzungukia maeneo hayo ili tukishayatenga tuweze kuwa na maeneo ambayo yanajulikana matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti mpaka sasa nchi yetu ina hekta zaidi ya milioni 60 ambazo zinafaa kwa mifugo, lakini eneo ambalo linahusika kwamba hili limepimwa na linalindwa kwa ajili ya mifugo ni 2% tu. Kwa hiyo, tunahitaji maeneo haya yapimwe na yabainishwe matumizi yake na kama shida ni gharama tutaweka hata *beacon* za asili. Nakumbuka vijijini tulikuwa tunapanda hata minyaa, inajulikana kwamba huu ni mpaka. Tutaweka hivyo ili wakulima na wafugaji wasiendeleo kuuana katika nchi ambayo ina wingi wa ardhi ambayo inaweza ikapangiwa matumizi na ikapata matumizi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme, mwenzangu wa Wizara ya Viwanda, kama tutakuwa tumeweka vizuri kwenye upande wa mifugo, pakajulikana wapi pana mifugo kiasi gani, itakuwa rahisi yeye kushawishi mtu aweke kiwanda cha maziwa, kiwanda cha nyama au kiwanda cha ngozi. Hili linawezekana kwa

sababu katika mazingira ya kawaida, Wizara inawaza kutumia wafugaji wetu hawa hawa kuwa chanzo cha kwanza cha watu wa kufikiriwa kuwa wawekezaji kwenye mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye ameweza kufuga kwa shida akapata mifugo 2,000, nina uhakika akitengewa eneo na likawa na miundombinu na huduma za ugani, ni mmoja anayeweza kuwa mwekezaji mkubwa, lakini wakati ule ule wafugaji wetu wakawa wamehama kutoka katika ufugaji wa kuzungukazunguka na kwenda kwenye ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo nilishasema kwamba, tumekusanya mawazo ambayo tutayatumia katika kuondoa zile ambazo ni kero, ambazo Mheshimiwa Rais alishawaahidi Watanzania kwamba atazifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo yamekuwa yakiwasumbua wananchi ni upande wa masoko. Tutaimarisha kuanzia upande wa ubora katika uzalishaji ili kuweza kujihakikishia ubora wa masoko na niwahakikishie kwamba, katika mazao mengi yanayopatikana hapa Tanzania soko lake bado kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, zamani tulikuwa tunajua mahindi ni zao la chakula au mchele ni zao la chakula, lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hivi tunavyoongea, zaidi ya watu bilioni 7.3 wanaoishi hapa duniani, nusu yao wanategemea mchele kama chakula na 40% wanategemea kula ngano kama chakula na zaidi ya bilioni moja wanategemea mahindi kama chakula. Kwa maana hiyo, hilo soko ku-saturate bado sana. Tuna mahali pa kuuzia mchele wetu, licha ya sisi wenyewe kwanza bado tunahitaji kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jambo moja kwenye mazao. Kumekuwepo na unyonyaji mkubwa ukifanywa kwa wananchi wangu, wa upande wa sheria atasema anayehusika na sheria hizo na usimamizi wake, wa upande wa Viwanda pamoja na upande wa TAMISEMI. Wanunuzi wanapokwenda kununua wananunua kwa hivi.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili... ili wananchi wauze kwa vipimo vinavyojulikana. Zimeshakwisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, muda umekwisha.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mpango na naunga mkono hoja iliyoko mezani kwetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa, lakini kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuleta hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri. Katika hatua hii napenda kusema kuwa tumepokea maoni yenu na ushauri wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, masuala makubwa ambayo yamejitokeza katika michango na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni suala la miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ni suala linalohusu ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa kwa mikoa ile mitano mipya, lakini pia na hospitali za kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwepo na suala la rasilimali watu na hili linahusika kwa kiasi fulani na uhaba wa madaktari, wahudumu, wauguzi na wafanyakazi wengine katika sekta ya afya. Lilikuwepo pia suala la upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na kwa upande wa sekta ya maendeleo jamii, jinsia na watoto, masuala makubwa matatu ambayo yamejitokeza katika mjadala huu ni suala la kuwawezesha wanawake kiuchumi. Pia suala la elimu kwa watoto wa kike na suala la *mainstream gender* katika mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nataka kuwathibitisha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba katika suala la miundombinu ya huduma ya afya, tutajenga zahanati katika kila kijiji kama tulivyoahidi, tutaonesha katika bajeti yetu, ni zahanati ngapi tutajenga katika mwaka wa fedha 2016/2017; tutaonyesha ni vituo vya afya vingapi vitajengwa na Hospitali za Wilaya ngapi zitajengwa. Tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba 2020 tunaporudi kuomba kura, Watanzania watatupa kura kwa sababu ya ahadi ya kuboresha miundombinu ya vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rasilimali watu juzi niliongea. Tunao uhaba wa wafanyakazi *especially* madaktari katika vituo vyetu vya afya kuanzia ngazi zote, uhaba ni karibu 52%. Kwa hiyo, bajeti inayokuja ya mwaka 2016/2017, tutajikita katika kuajiri watumishi wapya wa sekta ya afya, Mmadaktari, wauguzi na wakunga lakini pia tutaweka kipaumbele katika ile Mikoa tisa kama nilivyosema ambayo ina uhaba mkubwa ikiwemo Katavi, Geita, Simiyu, Tabora na Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tutalipa kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunatoa motisha kwa Madaktari kukubali kufanya kazi vijijini. Kwa hiyo, tutahakikisha tunajenga nyumba za madaktari, lakini pia tunataka sasa hivi daktari yeyote ambaye anataka kuongeza ujuzi kwa kutumia fedha za Serikali tutampa mkataba, ata-sign mkataba kwamba atakaporudi atakwenda kufanya kazi Katavi kwa miaka mitatu kabla hajaamua kuondoka katika Serikali, hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie suala la vifo vya akinamama wajawazito. Mimi ni mwanamke na nimepewa jukumu hili, nakubali ni changamoto kuona wanawake karibu 7,900 wanafariki kila mwaka kwa sababu tu wanatimiza haki yao ya uzazi. Kila saa moja tulilokaa hapa mwanamke mmoja wa Tanzania anafariki kwa sababu tu anatimiza haki yake ya msingi ya kuzaa. Nimedhamiria, tumedhamiria Wizarani hili suala tutalipa kipaumbele kuhakikisha vituo vya afya vyote vinakuwa na vifaa vya kufanyia upasuaji mdogo, maana wanawake wengi wanakufa kwa sababu wanakosa upasuaji, lakini suala la damu salama, suala pia la kuhakikisha kuna ambulance ili wanawake waweze kukimbizwa pale ambapo watapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala moja ambalo kwa kweli Mheshimiwa Edward Mwalongo amelizungumzia, vikwazo vya mtoto wa kike katika kupata elimu. Kwa mamlaka niliyopewa namtangaza Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini kuwa shujaa, *champion* wa haki ya mtoto wa kike kupata elimu kwa mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutampa tuzo rasmi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Kwa mara ya kwanza katika Bunge hili, mwanaume anasimama, anatetea haki ya zana za kujistiri kwa mtoto wa kike. Hili jambo tumelisema, lakini limesemwa na mwanaume kwa kweli tumepata nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Elimu mwanamke, Mheshimiwa Waziri anayehusika na Utumishi ni mwanamke, Mheshimiwa Jenista na mimi, tutalipigania kuhakikisha watoto wa kike wanapata taulo ili waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie hoja iliyoko mbele yetu.

Kwanza nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mapendekezo mazuri katika sekta ya

elimu. Vilevile nipende kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameleta michango mizuri kwenye elimu na kwa sababu ya muda sitaweza kugusia maeneo yote mliyoyazungumzia, lakini niseme tu kwamba michango yenu ni mizuri, tunashukuru sana na tutaizingatia tunapokuwa tunafanya mapitio na kutengeneza ule Mpango wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuzungumzia masuala machache na ningependa nianze na suala la elimu bila malipo kwa sababu limezungumziwa kwa nyanja tofauti, katika sura ya pongezi na katika sura ya kutoa changamoto na yote tumeyapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuwika wazi jambo moja kwamba, suala la elimu bila malipo linaongozwa na Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015. Waraka huu umebainisha wazi majukumu ya Serikali, majukumu ya wazazi na wadau wengine wote. Kwa hiyo, kuna wengine wanakuja na dhana kuwa Serikali inafanya utapeli, kwamba imewaahidi wananchi kwamba itakuwa ni elimu bure lakini inachangisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhana potofu ambayo ningependa Watanzania waifahamu kwamba waraka umebainisha wazi kabisa, kuna majukumu ya mzazi ambayo bado mzazi atawajibika kumnunulia mtoto wake *uniform*, mzazi atawajibika kugharamia matibabu ya mtoto wake na kumnunulia vifaa vinavyotakiwa kwenda navyo shuleni. Serikali inatoa *capitation grant* kwa ajili ya wanafunzi, Serikali imeondoa ile ada ambayo mwanafunzi alikuwa analipa ambayo ni shilingi 20,000/= kwa mwanafunzi wa kutwa na shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Vilevile Serikali imeondoa gharama za mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa kwa nini baadhi ya watu wanabeza, wakati nikiwa Baraza la Mitihani tulivyokuwa tunatangaza matokeo, wanafunzi wa Tanzania wengi kwa maelfu walikuwa wanazuliwa matokeo yao ya mitihani kwa sababu ya kushindwa kulipa ada, leo hii Serikali imewaondolea, badala ya kushukuru, tunaibeza. Kwa hiyo, naomba tu niseme kwamba majukumu yameaninishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuliweka wazi, Serikali haijakataza wananchi kuchangia katika maendeleo ya elimu. Imeweka wazi kabisa kwamba bado jamiii ina wajibu wa kutoa ushirikiano katika shughuli za kuleta maendeleo katika maeneo yao. Bado imeeleza wazi kwamba jamii ina wajibu wa kuendelea kujitolea nguvu kazi na mali ili kuleta maendeleo katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mbunge ambaye amechangia asubuhi, akasema kwamba kuna matatizo katika Jimbo lake na kwamba

anatoa mifuko 1,500, Waheshimiwa Wabunge wengine wote ruksa fedha zenu za Mifuko ya Majimbo msije mkaacha kuchangia katika sekta ya elimu eti kwamba Serikali imekataza, hakuna hicho kitu. Nimeona nitoe huo ufafanuzi kwa sababu naona labda hii dhana inaweza ikapotoshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kwa kifupi pia suala la ubora wa elimu ambalo limezungumziwa. Naomba niwahakikishie Watanzania kwamba Wizara yangu imejipanga na tuna nia thabiti kabisa ya kuhakikisha ubora wa elimu katika nyanja zote, kuanzia elimu ya awali mpaka elimu ya juu. Tutafanya hivyo kwa kuhakikisha kwanza kwenye elimu ya msingi mpaka sekondari tunafanya ufuatiliaji wa karibu, Wakaguzi wetu tayari wameshaelekezwa kufanya ufuatiliaji kwa kuangalia kile kinachofundishwa darasani, kwa sababu maarifa na stadi zinapatikana ndani ya darasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mamlaka zetu ambazo zina wajibu wa kudhibiti elimu ya kati na elimu ya juu, tutahakikisha kwamba zinafanya kazi zao kwa weledi na vigezo vyao wanavyovitumia katika kuangalia kwamba chuo kinafaa, chuo kina sifa, ni lazima viwe ni vigezo ambavyo kweli vitatutolea wahitimu ambao wana ubora ambao tunauhitaji katika kuipeleka nchi yetu katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia pia kidogo kuhusu elimu kwa watu wenye ulemavu. Nashukuru sana kwa michango iliyotolewa na niseme tu kwamba ni suala ambalo mimi kama mama, kama Waziri mwenye dhamana ya elimu linanigusa sana. Niseme kwamba Watanzania wenye ulemavu ni asilimia ndogo ukilinganisha na Watanzania ambao hawana mahitaji maalum. Hivyo basi Wizara yangu itahakikisha kwamba wana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Nashukuru sana Mwenyekiti naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri ambapo kila Mbunge aliposimama amezungumzia angalau tatizo alilonalo kwenye eneo lake kuhusu upatikanaji wa maji. Kumekuwa na mabishano kuhusu asilimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba tutaendelea kuyapeleka maji, kwa maana kwamba kutokana na ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumesema vijijini tutapeleka kwa 85% ifikapo mwaka 2020 na mijini tutapeleka kwa 95%. Tunafanya hivi kwa kufuata programu ya maji ambayo

tulianza nayo mwaka 2007. Kuna miradi ambayo tulianza kuitekeleza, kwanza tutakamilisha miradi ambayo haijakamilika, halafu tutaingia awamu ya pili ambayo tumeanza sasa hivi, kuweza kuainisha ni miradi ipi na maeneo yapi tunakwenda kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge watakaporudi kwenye Majimbo yao, kwenye Halmashauri zao wakaangalie vipaumbele ambavyo wangetaka tuanze navyo. Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni ameelekeza maeneo 65 nchi nzima ndiyo kipaumbele na sisi katika kufanya kazi tutafuata hilo. Sasa ninyi Waheshimiwa Wabunge mtusaidie ni wapi ungetaka tuanze napo, kwa maana kwamba tuweze kufikisha hizi asilimia tunazosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa, mwaka 2025, lengo la Serikali ni kwamba tutapeleka maji kwa kiwango cha 100% vijijini na mijini. Changamoto tunayoipata katika maeneo ya mijini sasa ukishaongeza upatikanaji wa maji unaongeza pia maji taka. Sasa tunataka katika hii *phase* ya pili, tuingie katika namna ya kuweza kuongeza jinsi tutakavyoondoa maji taka katika miji yetu ili pia tuweze kuondoa changamoto za maradhi kama kipindupindu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hilo tutaliweka kwenye Mpango ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametoa mwelekeo na sasa kila sekta tutakwenda kuangalia ni miradi ipi kulingana na *ceiling* ya bajeti. Pia nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tulishaweka Mfuko wa Maji toka mwaka jana na Mfuko wa Maji huu kutokana na tozo ya mafuta ambayo tuna uhakika, zile shilingi 50 kwa kila lita tutapata kama shilingi bilioni 90 mpaka ikifika Juni. Fedha hizi zitasaidia kulipa wakandarasi ambao sehemu kubwa wamesimama na fedha hiyo imeanza kutoka na tayari tumeanza kupeleka kwenye Halmashauri.

Naomba sana Wakurugenzi wetu fedha zile ambazo tunapeleka *specifically* kwa mradi, walipe miradi ile ambayo tumeamua kuimaliza kwanza. Miradi mingi ipo kwenye 90% na 95%. Tukiweza kuwalipa tuna uhakika wananchi wetu wataanza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana fedha hizi zisiende kufanya kazi nyingine, tutakuwa wakali na tutachukua hatua kwa Mkurugenzi ambaye ataamua kuzitumia fedha hizi anavyotaka yeye. Fedha hizo ni moto, kwa hiyo, tumepeleka tuhakikishe kabisa wanakwenda kulipa Wakandarasi wamalize miradi ili wananchi wetu waanze kupata maji. (*Makofi*)

Kwa upande wa Da es Salaam naomba niseme tu kwamba ikifika mwezi Machi, tutakuwa tumepata maji yanayotosha mahitaji, kwa maana ya kiujumla

wake ya wananchi. Kazi kubwa ambayo tutakuwa tunakwenda kufanya sasa ni ule usambazaji. Kule Kimbiji na Mpera tumeshachimba visima tayari saba kati ya visima 12 kwa ajili ya maeneo mengine ya Kigamboni, Mkuranga ili tuweze kukamilisha na kuhakikisha wananchi wa maeneo yale wanapata maji. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tutachukua haya mawazo yenu yote na tutayaweka kwenye Mpango ili tuhakikishe kwamba tunakwenda kutekeleza kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wengi ambao wanaishi kandokando ya Ziwa Victoria nimetoa ahadi na Rais ameahidi kwamba tutachukua maji ya Ziwa Victoria kuweza kusambaza katika miji yote mikuu ya mikoa inayozunguka Ziwa Victoria pamoja na Makao Makuu ya Wilaya. Hii miradi tumeshaanza, mingine kwa kutumia wafadhili mbalimbali, lakini mengine tutakwenda kufanya kwa kutumia fedha zetu za ndani. Sasa tutakapofika kwenye bajeti, basi Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono ili tuweze kutekeleza miradi kama ilivyokuwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Nashukuru kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Huu ni Mpango mzuri. Waheshimiwa Wabunge mawazo yenu tumeyapata na tutayafanyia kazi na mengine tunayafanyia kazi tayari. Cha maana cha kujua ni kwamba maana ya uchumi ambao unafanyiwa mapinduzi makubwa huwa mara nyingi haukubaliki kiurahisi, ndio historia ya mapinduzi ya kiuchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mafuta na gesi, nataka niwaeleze Watanzania ukweli, wengine wamesema hakuna wataalam siyo kweli na wala hatuhitaji kumleta kama alivyosema mwingine mzungu mmoja aje kutufundisha, haiwezekani hiyo. Kwa sababu huku kuna wataalam kweli kweli. *TPDC* penyewe kuna *Ph.D* nne, kuna *Masters* 62, kuna shahada za kwanza zaidi ya 200. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kina *degree programmes* zaidi ya tano, *UDOM* wapo tano, lengo ni kwamba kwa miaka michache inayokuja Tanzania ndiyo itakuwa na wataalam wengi wa madini na mafuta nchini hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunasomesha watu, mwaka huu Norway tumemaliza *scholarship* ya watu 40 na wengine 40 tutaziomba tena. Kwa hiyo, maana ya mageuzi haya tunayoyaongelea ndugu zangu Wabunge yataendana na uchumi wa gesi, ndiyo roho ya mapinduzi ya uchumi wetu na niwahakikishie tuko kwenye njia nzuri. Wanaosema hawaoni faida, umeme

utatoka huko, viwanda vya mbolea tutajenga, majumbani tutatumia na gesi tutaisindika.

Mheshimwa Mwenyekiti, niongelee kingine ambacho ni injini ya mageuzi yote haya, ni mambo ya umeme. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ni kwamba, umeme wa uhakika na umeme wa bei ndogo lazima utapatikana kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwa mahesabu, sio kwa hisia, sio kwa matusi, sio kwa kumkejeli mtu. Ni lazima tutoke kwenye *power per capita*, yaani mtu mmoja mmoja, mwenye umeme wa *units* 108 kwenda *units* 3000. Ndio kazi ambayo Wizara ya Nishati inaifanya. Hiyo inaendana na ukuaji wa uchumi, utoke sasa hivi asilimia saba mpaka asilimia 10 kwa mwaka ili ifikapo mwaka 2025, tukiwa nchi ambayo ni ya kipato cha kati, yenye Pato la Taifa GDP ya bilioni 240, tunahitaji umeme wa uhakika na Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla ndiyo kazi inayoifanya hiyo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kingine ambacho ni cha kufahamu, tumeongelea sana fedha za wafadhili, Watanzania wote naomba tuelewane, fedha za wafadhili ni tofauti na fedha za uwekezaji. Mimi huku Wizara ya Nishati na Madini, hata wakiniipatia fedha zote za wafadhili, ni fedha kidogo. Fedha za wafadhili, wasiojua siyo zaidi ya dola milioni 500 kwa mwaka, dola za Marekani hazivuki milioni 500. Halafu upatikanaji wake, kwa ndani ya miaka 10 hesabu zimepigwa ni wachache wamevuka asilimia 50 ya ahadi walizozitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kinyerezi I*, megawati 150, uwekezaji ni dola milioni 183. *Kinyerezi II* ambayo tutaweka jiwe la msingi mwezi huu, inahitaji dola za Marekani, milioni 344. Hizo ni zaidi ya fedha za wafadhili. Kwa hiyo, tunachokitafuta sisi, ni fedha za uwekezaji, kwa hiyo, Watanzania msiwe na wasiwasi, fedha za wawekezaji zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamesema *Exim Bank* ya China imekataa, siyo kweli. *President* Jinping alivyokuwa Afrika ya Kusini ametoa dola bilioni 60, kwa uhusiano wa China na Afrika. Tanzania ni kati ya nchi tatu ambazo zitafaidika. Nawaambia Wizara yangu yenyewe, mimi nataka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango. Mapendekezo ya Mpango ni mazuri na kama mnavyojua, lugha ya mjini ni

kujenga uchumi wa viwanda ili kufanya mageuzi ya uchumi yatakayoleta maendeleo ya watu na hiyo inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya upungufu wa muda, ningependa nijibu baadhi ya maswali yaliyojitokeza na nianze na shemeji yangu, kusudi wajomba zangu kule wasijisikie vibaya, baba yao anajua takwimu na mjomba wao anajua takwimu. Kwa nini tunakwenda kwenye viwanda? Tutatengeneza ajira. Ilani ya CCM Ibara ya 32 mpaka 33, inasema asilimia 40 ya nguvu kazi itokane na viwanda, inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini, tunakwenda kwenye viwanda? Tunalenga kwamba asilimia 15 ya GDP basi itokane na viwanda, inawezekana. Kwa nini tunakwenda kwenye viwanda, tunazo rasilimali asilia tulizopewa na Mwenyezi Mungu, sasa ni wakati wa kuzichakata, hizi rasilimali hizo zipitie kwenye viwanda ili pato, tutakalopata liweze kwenda kwenye maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunakwenda kwenye viwanda? Tunakwenda kwenye viwanda kwa sababu kwa kuchakata viwanda vya Mzee Mwigulu tutaweza kuwashirikisha wananchi walio wengi na wananchi walio wengi wakishiriki ule umaskini utaweza kuondoka. Kwa nini tunakwenda kwenye viwanda? Viwanda tulivyonyavyo sasa vimeonyesha utendaji mzuri, *export* ya bidhaa za viwandani zimeongezeka kwa takwimu sahihi. Sasa tunataka kuongeza zaidi, twende kwenye soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza juzi nchi ya India, pamoja na matatizo ya jana, wametufungulia milango kwamba bidhaa itengenezwayo Tanzania na ipelekwe kule. Sasa tunalenga viwanda gani? Tunalenga viwanda vya chuma Mchuchuma na Liganga zichakatwe ziende kule. Engaruka soda *ash* ichakatwe, mazao ya kilimo na mifugo yachakatwe. Hizo ni shughuli ambazo zitashirikisha watu wengi, lakini *edible oil*, alizeti, mawese ya Kigoma yachakatwe tuweze kutosheleza soko la ndani. Tanzania tunaagiza tani 350,000 za mafuta ya kula. Napenda mimi nikiwa katika nafasi hii tusiagize mafuta, ila sisi tuuze nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali lingine, nani atafanya hivi? Kama alivyosema Profesa Muhongo ni mimi na wewe Mbunge, ni sekta binafsi. Sekta binafsi ndiyo injini, sekta binafsi ndiyo itasukuma hii. Kwa hiyo, sekta binafsi ndiyo ambayo itatuongoza katika kutekeleza suala hili. Sekta binafsi, nini jukumu la Serikali, Serikali itatengeneza mazingira safi, kusudi wawekezaji tuwaondolee vikwazo. Njoo kesho iishe, ardhi inapimwa pale, unakuja una mgogoro, mahakamani, mambo yanawekwa sawa. Unakuja saa tatu unasajili saa saba, hiyo iko chini yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kufanya, nini uzoefu wa dunia? Uzoefu wa dunia unaonyesha kwamba asilimia kubwa ya shughuli za ujasiriamali zinamilikiwa na SME, viwanda vidogo na vya kati. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mjiandae, nilikuwa nagawa nguzo mwaka jana, sasa nitakuwa nagawa viwanda vidogo. Kwa hiyo, tafuteni viwanda vidogo, asilimia 99 ya shughuli za kiuchumi duniani ni viwanda vidogo. Lakini GDP angalia mfano wa Brazil, South Korea, India, *coated industry* ndiyo inazalisha bidhaa zilizo nyingi. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, angalieni kwenye Manispaa zote na Miji muangalie, *guest house* yenye vyumba kumi, ni kiwanda kidogo. Mtaji wa milioni 50, milioni 100 unanunua kiwanda kidogo. Juzi, nimenunua Kiwanda Bangkok Thailand, kitazalisha chakula cha samaki, ambacho kwa mwaka kitazalisha samaki wenye thamani ya bilioni 60, juzi wamekizindua Muleba, mimi nakwenda kukihamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rweikiza wa Bukoba Vijijini, amenunua mtambo wa kuchakata nyanya, kwa shilingi milioni 140. Ni Mbunge gani anaweza kukosa kwenda benki akaaminiwa, kwa milioni 140, akawahamasisha wananchi, wakazalisha nyanya, akazichakata. Wale wanaochakata wanaweza kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, tutakutana kwenye Mpango na naunga mkono Mpango. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mapendekezo haya. Niupongeze uongozi mzima wa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote. Mpango huo au mapendekezo haya yaliyowasilishwa kwetu kwa kweli ni mazuri, kwa vigezo vyote, lakini zaidi, ukiangalia katika masuala matatu.

Mapendekezo haya ya Mpango, yamejengwa katika mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Kwanza. Pili, mapendekezo haya yamezingatia Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, inayotekelezeka, iliyo bora, lakini vilevile ni ilani ambayo inapimika, lakini tatu, ukiangalia umezingatia, mabadiliko yaliyopo katika Serikali ya Awamu ya Tano, katika utendaji wake kazi na kupitia dhana nzima ya hapa kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na masuala ya Utawala Bora, katika Mpango huu, utaona kabisa suala zima la utawala bora limewekwa kama kipaumbele muhimu sana. Ukiangalia ili tuweze kupata mafanikio yoyote, ili tuweze kufanikiwa katika

uchumi huu wa viwanda, ni lazima tuweze kuwa na mafanikio makubwa katika utawala bora.

Kwa upande wetu tutahakikisha kwamba, tunaimarisha taasisi zetu mbalimbali zinazotekeleza masuala ya utawala bora ikiwemo TAKUKURU, ikiwemo Sekretarieti ya Maadili, lakini vilevile kwa upande wa Mahakama na taasisi nyingine za utoaji haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao walisema hakuna utaratibu wa kuandaa viongozi. Niseme tu kwamba katika Serikali utaratibu huo upo na hivi sasa wameandaliwa viongozi wengi, wamepatiwa mafunzo na wengi wao wapo katika kanzidata ambapo itkapojitokeza tuna mahitaji, basi wanaweza kuchukuliwa na kuweza kupewa nafasi mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza. Tunayo *assessment center methodology*, ambayo kimsingi imeweka watumishi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo tu kurudia na kusisitiza kwa watumishi wenzangu wa umma. Tuombe sana sana, waweze kuzingatia nidhamu ya hali ya juu. Waweze kuwa wabunifu, waweze kuzingatia maadili, kwa sababu bila ya kuwa na watumishi wa umma wenye sifa na wenye kutekeleza majukumu yao kwa kujituma na kuwa na uwajibikaji, Mpango huu utakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali, tutaendelea kufuatilia na kuchukua hatua, dhidi ya mtumishi yoyote wa umma ambaye atakiuka utumishi wake. Vilevile kama mnavyofahamu, kupitia utumishi wa umma, viongozi mbalimbali wamesaini, wamekula kiapo, kupitia ahadi ya uadilifu. Niwaombe tu watumishi hawa wa umma waendeleo kuishi, kupitia viapo vile walivyokula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tumeyapokea yote mengi mazuri, ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyapendekeza hapa na tutayatekeleza. Pia niseme kwamba, kupitia TAKUKURU tutaendelea kuijengea uwezo. Ukiangalia hivi sasa, wanazo ofisi 52 tu nchi nzima, majengo 52. Ukiangalia katika kila Wilaya mahitaji ni zaidi ya watumishi sita mpaka saba ili uweze kuwa na ufanisi. Hivi sasa wapo watumishi watatu tu na kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, tutahakikisha tunawapa idadi kubwa ya watumishi wasiopungua 400 katika mwaka ujao wa fedha, ili basi kila Wilaya iweze kuwa na ufanisi katika suala zima la ufuatiliaji kwa watu wanaokiuka masuala mbalimbali ya uadilifu, lakini vilevile wanaochukua rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa inaathiri masuala ya haki za binadamu, rushwa inaongeza tofauti kubwa iliyopo kati ya walionacho na wasionacho, rushwa kwa kiasi kikubwa, imekuwa ikiathiri sana utoaji wa huduma. Kama ambavyo nilisisitiza wakati ule nikiwa nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, tutaendelea kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo na kuhakikisha

kwamba fedha zile zinazotengwa, basi zinakuwa na ufanisi na zitatumika kama zilivyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uongozi, tutaendelea kutoa programu mbalimbali za mafunzo, lakini vilevile kwa upande wa sekta ya umma tunaamini, ni lazima tuhakikishe tunaboresha huduma tunazozitoa. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba watumishi wa umma wanaendelea kuongezeka, kwa kadri ya mahitaji na kadri uchumi utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunafahamu kwamba watumishi hawa hawawezi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, bila ya kuangalia maslahi mbalimbali ya watumishi wa umma. Niwatoe hofu, watumishi wa umma wenzangu, tutayaangalia kwa kina na wataweza kupata maslahi ambayo wanastahili baada ya kuwa tumefanya tathimini ya kazi, itakapokamilika baada ya miezi 15. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Nianze nami kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake kwa kazi nzuri sana. Kwenye hotuba ya Waziri na makabrasha naona hapa, wameongelea kuhusu maboresho yanayofanyika Bandari ya Itungi, lakini kwa kifupi sana, nataka nieleze tu, kuyapanua kwa sababu nilikuwa huko hivi majuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yanayotokea Bandari ya Itungi, ni mapinduzi makubwa, katika historia ya miundombinu nchini. Kwa sababu kwa mara ya kwanza toka Uhuru, Tanzania inajiondoa kwenye utegemezi kwa nchi ndogo ya Malawi katika kukarabati vyombo vyake vya majini. Sasa hivi kutokana na chelezo ambayo imefungwa pale, Tanzania tunaweza sasa katika Ziwa Nyasa kujenga vyombo vyetu sisi wenyewe, kuviunda vipya na kukarabati vyombo vipya. Sasa hivi zinajengwa bajezi mbili pamoja kuanzia mwezi wa sita tunajenga meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *initiative* ya TPA na baada ya pale wanahamia *Lake Tanganyika* na *Lake Victoria*. Kwa hiyo, wananchi wanaona hayo na tuendelea tu na juhudi hizo. Nimefurahi vilevile kusikia, kwenye hotuba ya Waziri kuhusu ujenzi wa hivi vituo, Kituo cha Utoaji Huduma Pamoja, hivi vinavyoitwa *One Stop Border Posts*, tumejenga nyingi kwa Rwanda, Burundi, tunayo Uganda, kwa mpaka wetu na Kenya tunazo tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunajenga Zambia, sasa ipo ya Malawi na Tanzania. Kwa kweli, ni taarifa nzuri sana kwa wafanyabiashara wa Malawi na

Tanzania na vile vile fursa ya kufanya biashara kubwa kwa wananchi wa Wilaya Kyela na Kasumulu upande wa Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dogo tu kuhusu masuala ya Katiba. Wiki hii tumekuwa tukijenga msingi wa kutekeleza masharti ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ambayo inasema; "Bunge hili, litajadili na kuidhinisha Mpango wa muda mrefu au muda mfupi wa Taifa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi walidhani Serikali inakuja na Mpango, ilionekana hapa katika majadiliano ya mwanzo pale. Inakuja na Mpango, hapana hapana, hili ni zoezi shirikishi la Kikatiba, linataka sisi tuchangie. Nataka nisisitize tu hapa kwamba, dhana ya zoezi hili kuwa shirikishi, linatokana na masharti ya Ibara ya 8 ya Katiba hii, inayosema kwamba; "Wananchi wa Tanzania ndiyo msingi wa mamlaka yote. Pili, lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi. Tatu, Serikali inawajibika kwa wananchi. Nne, wananchi washirikishwe au watahiriki katika shughuli za Serikali."

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze maneno yangu, kupitia wawakilishi wao ambao ni Wabunge. Sasa Ibara ya 63(3)(c) inatutaka sisi wawakilishi wa wananchi, sasa tuchangie tuweze ku-reflect haya, kwamba Serikali katika mipango yake, inajali ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbie tu neno moja dogo la haraka haraka lingine, maana muda wenyewe ndiyo huo. Kumekuwa pia na kejeli katika kuiangalia hii kaulimbiu ya hapa kazi tu, inaonekana kama ni kauli ngeni, kauli ya kipropaganda tu, lakini nataka kusisitiza hapa kwamba hii ni kaulimbiu ya Kikatiba, tena Katiba yenu wenyewe hii hapa, niliyoishika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 25(1) inasema: "Kazi pekee ndio huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndiyo chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu na kila mtu anao wajibu wa kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na ya uzalishaji mali."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Ibara ya 9(e), Katiba inasema; "Serikali itahakikisha kwamba kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, anafanya kazi na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali, inayompatia mtu riziki yake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea tena ibara ya 22 inatupa *confidence*, inasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe shukrani na pongezi za dhati sana kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango. Tunamshukuru sana na tunampongeza kwa kweli kwa Mpango mzuri, Mpango utakaotuvusha nchi yetu katika kutupeleka kwenye Taifa na hali ile tunayoitaka, Taifa la kipato cha kati. Mheshimiwa Waziri wa Mipango tunakushukuru na tunakupongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema mambo machache sana. Nafurahi kuona kwamba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango sasa ametuletea dira inayotupeleka kujibu hoja kubwa sana ya ajira kwa vijana wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo yote Mheshimiwa Rais wetu wakati akiwa kwenye kampeni za uchaguzi, hoja iliyotawala kwa vijana wa Tanzania ni namna gani wanaweza kutengenezewa mazingira ya kupata ajira kwa utaratibu wa aina tofauti na kwa misingi ya ajira za aina tofauti.

Kwa hiyo, Mpango huu ukiutazama na hasa mtazamo huu wa kulifanya Taifa letu sasa liende kuwa Taifa la viwanda na viwanda vile vikiwa katika *level* mbalimbali, naomba niwahakikishie vijana wa Tanzania tatizo la ajira sasa litakwenda kutatuliwa kwa kiasi cha kutosha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanahitaji sasa watambuliwe. Mchango wao kwenye maendeleo ya Taifa hili ueleweke wazi, lakini wanahitaji kuwezeshwa, kutengenezewa miundombinu ambayo itawasaidia kushiriki katika uchumi wao wa Taifa. Mpango huu unatuelekeza huko na Mpango huu unatuambia kama tunakwenda kufungua viwanda kazi yetu sisi sasa, kama Wizara ya Kazi, ni kuhakikisha tunaanza kuwa na programu maalum, moja; ya kuwafanya vijana waweze kupata mitaji na mifumo itakayowafanya waweze kupata fedha za kujiingiza katika Mpango huo wa Maendeleo.

La pili, ni lazima sasa kupitia Wizara hii tujipange kuona vijana hawa sasa wanapata ujuzi, zile *skills* zinazohitajika ili waweze kujiajiri na kuajirika katika kujenga uchumi huu na kukamata uchumi wa nchi yao. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge muunge mkono mapendekezo haya ya Mpango ili tatizo la ajira katika nchi yetu ya Tanzania tuweze kulitatua kwa kiasi cha kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme; Mpango huu pia, unakwenda kujibu hoja nyingi sana za muda mrefu za kundi maalum kabisa la wenye

ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania. Mpango huu sasa pia, utakwenda kutafsiri sheria na mikakati mbalimbali ambayo itakwenda kuwaruhusu watu wenye makundi ya ulemavu katika hatua mbalimbali na wao washirikishwe katika mipango ya maendeleo. Waweze kushiriki katika uchumi, waweze kushiriki katika uzalishaji, waweze kushiriki katika shughuli zote ambazo zitajitokeza kwa kuzingatia Mpango tulionao.

Kwa hiyo, naomba niwaambie Watanzania, Mpango ulioletwa na Serikali unakwenda kujibu matatizo mengi katika nchi yetu ya Tanzania na kama tulivyoona tutakapokuja kuunganisha Mpango huu sasa na bajeti, utajibu mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ambao wamesoma, vijana ambao wako kwenye elimu za kati, vijana ambao wako vijijini, unaona kabisa Mpango huu sasa tutakwenda kujipanganao na hayo matatizo yote ya makundi hayo yatakwenda kupatiwa majibu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kuyashughulikia yale mnayotambia ili tuweze kupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa hapa mambo mbalimbali, kero za dawa za kulevya; naomba niwaombe Watanzania wote tushirikiane kwa pamoja. Kama tunazungumzia maendeleo ya uchumi, tusipopambana na dawa za kulevya vijana hawa tutashindwa kuwashirikisha katika kujenga uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Sheria na mikakati yote itakayoletwa na Serikali tuiunge mkono, ili ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba Serikali iende mbele. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini zaidi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuendelea kuishi na kuweza kuchangia katika Bunge hili Tukufu.

Kwanza kabisa niseme naunga mkono hoja, nawashukuru Wizara ya Fedha kwa kuja na Mapendekezo haya ya Mpango. Pia nawashukuru Wabunge wote kwa kuhudhuria na kushiriki kikao hiki, lakini pia na kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuzungumza hoja chache zile ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema. Moja, nimalizie pale alipoishia Mheshimiwa Mwakyembe kwamba haya ni mapendekezo katika

kipindi hiki hatuhitaji Sheria; ile Kanuni ya 94 ipo wazi kabisa, lakini baadaye Mpango ukisoma sasa Kifungu cha 20 cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 na Kifungu cha 26 cha Sheria ya Bajeti, Mpango huu utakapoletwa mahususi wenyewe ndiyo msingi wa kutengenezea Bajeti. Halafu baadae Bajeti inapokuja kutengenezwa ndiyo inatengenezewa Sheria ya *Appropriation Act*, Sheria ya...

Kwa hiyo, nafikiri niiweke hii wazi kwa baadhi ya Wabunge ambao walikuwa wamefikiri kwamba Serikali imekosea kutokuja hata na Sheria.

**MWENYEKITI:** Samahani sana, nilipitiwa kidogo, muda unakwisha. Kwa hiyo, natumia mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 25(5), niongeze muda usiozidi nusu saa tumalize shughuli zilizo mbele yetu. Endelea AG!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niliona nilitolee ufafanuzi hili kwa sababu baadhi ya Wabunge walikuwa wanajjuliza kwa sababu hawaoni hata Muswada wa Sheria! Nimeona niliweke wazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo naomba kuliongelea ni suala la Zanzibar. Suala hili ni suala nyeti kwa mustakabali wa Taifa. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua uwepo wa Serikali mbili na hizi Serikali uwepo wake ni Katiba; kuna Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya (4) ya Katiba hiyo siyo tu inaweka mgawanyo wa madaraka katika mihimili mitatu ya dola, lakini pia, inaweka mgawanyo wa madaraka kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na imeelezwa vizuri na kuna mambo ya Muungano na ambayo siyo ya Muungano. Kwa hiyo, Katiba ya Zanzibar sio ya Muungano, ila Katiba ya Jamhuri ni ya Muungano na Katiba ile ya Zanzibar ndiyo inazaa Tume ya Uchaguzi ambayo inasimamia uchaguzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kile ambacho baadhi ya Wabunge wamekisema hapa, ni kama kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano iingilie mamlaka ya Zanzibar! Tafsiri yake ni kwamba kama unataka kuleta hoja ya kujengwa Serikali moja, lakini kwa mujibu wa Katiba ni Serikali mbili. Sasa tukienda kwa namna hiyo tutakuwa tunavunja siyo tu Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini pia Katiba ya Zanzibar. Serikali haiwezi ikakifanya hicho na kuwepo kwa Serikali yoyote ni Katiba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya kusema kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano iingilie kule, Rais Magufuli aingilie, ana mamlaka tu yeye kuingilia mambo ya ulinzi na usalama ndiyo ya Muungano na mpaka sasa kule

Zanzibar kuna amani, Rais anafanya kazi yake vizuri, utengamano ni mkubwa kabisa na usalama upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo nishauri Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapochangia suala la Zanzibar lazima tuheshimu mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tuchangie kwa namna ambayo si ya kuhamasisha uvunjifu wa amani, uhaini au kuvunja umoja na mshikamano! Ikitokea uvunjifu wa amani hapa hakuna yeyote atakayefaidi, wala hatafaidi siasa wala kitu gani! Niliona nilishauri hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena nikushukuru na niwashukuru Wabunge wote. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi!

Nina matangazo mawili hivi; lile tangazo la asubuhi la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, walisema saa saba, lakini baadaye tukaona kwa sababu ya shughuli ya Vikao vya Kamati, Wabunge wanaotoka kwenye maeneo yanayolima pamba, tumbaku, kahawa, korosho, chai, miwa, katani, ufuta, mifugo, wafugaji pia na wavuvi, tulikuwa tukutane Ukumbi wa Msekwa; anatoa taarifa hiyo Mheshimiwa Waziri tukutane sasa hivi *briefly* kwa sababu gani? Kwa upande wa Wabunge wa CCM nina tangazo kwamba, saa mbili kamili usiku kuna Kikao cha Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi katika Ukumbi wa Chama cha Mapinduzi, *White House* pale na wote mnatakiwa muwe pale.

Kwa hiyo, wale Wabunge tunaotoka kwenye maeneo yanayolima hayo mazao ya kibiashara, tukutane tukubaliane! Nadhani itakuwa *very tight* kwa leo, tutaelewana, lakini tufike pale.

Baada ya kusema hayo sina lingine, niwashukuruni tu Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo tumefanya tangu Jumatatu, kutendea haki Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo unaoletwa na Serikali. Serikali naamini imepata maboresho katika maeneo mengi na watajumuisha na ya wadau wengine, sekta binafsi, NGOs, ili kuweza kuboresha Mpango huu.

Kwa hiyo, wanapokuja mwezi wa Tatu, *Inshallah*, watakuwa na kitu ambacho kina sura nzuri, hatimaye kwenye Bunge hili la mwezi wa Juni, Serikali inapowasilisha Bajeti yake tutakuwa tumepata Mpango kamili wa mwaka 2016/2017 na pia na Mpango ule wa miaka mitano utakaotokana na huu ambao tunatoa mapendekezo sasa hivi.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 5 Februari, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*

## **Kikao cha Tisa – Tarehe 5 Februari, 2016**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### **D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri majadiliano kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa lakini pia Mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017, hotuba ambayo niliwasilisha tarehe 1 Februari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini lakini pia aliyekuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge 121 wamechangia kwa kuzungumza na 30 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kunipatia dakika zake kumi ili niweze kuzitumia kutoa majumuisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao ulisisitizwa sana. Kwa kuwa tulichowasilisha ni Mapendekezo ya Mpango na Waheshimiwa Mawaziri wenye dhamana ya kusimamia sekta mbalimbali walipata nafasi ya kutoa maelezo yao basi nitakuwa na machache sana juu ya sekta moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla tumepokea ushauri mzuri ambao naomba kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutautumia kuandaa Rasimu ya Mpango wenyewe lakini pia kuandaa mapendekezo ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Taarifa zote mbili zitawasilishwa kwa Wabunge tarehe 11 Machi, 2016, ambayo itakuwa ni siku ya kazi, siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze mambo makubwa ambayo yalisisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge wameshauri tuweke nguvu kubwa katika ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vya sasa na vyanzo vipya ili kuongeza bajeti ya maendeleo na kuhakikisha fedha inatolewa kama ilivyo pangwa.

La pili ilisisitizwa kwamba ni lazima sasa tuongeze uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, tatu, ujenzi wa reli ya kati na matawi yake yote nchini kwa kiwango cha *standard gauge* na nne, Serikali ipeleke fedha zaidi kutekeleza programu na miradi ya maji mijini na vijijini kwa matumizi ya binadamu, mifugo, viwanda na umwagiliaji lakini ikiwa ni pamoja na dhamira ya Serikali ya kupunguza adha kubwa kwa akina mama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tumepokea ni kwamba ni lazima katika Mpango ujao tuendeleze jitihada za kujenga na kuimarisha miundombinu ya bandari, reli, barabara, viwanja vya ndege na kuboresha huduma husika ikiwa ni pamoja na usafiri katika maziwa makuu na bahari kwa kununua meli mpya na kukarabati zilizopo. Pia tumeshauriwa kwamba Mpango ujao usisitize kutenga na kupima ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao na ufugaji ili kuepuka migogoro na kulipa fidia ya ardhi kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ilisisitizwa kwamba tuwekeze zaidi katika kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu ili kiweze kutupatia chakula cha kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje lakini pia kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi za viwandani na masoko ya Kikanda na Kimataifa. Tulipokea ushauri pia kwamba Shirika letu la Ndege (ATCL) lifanyiwe mageuzi makubwa yaani *restructuring* na kununua ndege mpya kwa kuhusisha taasisi zinazohusika na utalii ili kuwa na *National Airline* endelevu na yenye ufanisi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilisisitizwa pia kwamba ujenzi wa viwanda uanze kwa kufufua viwanda vilivyopo na vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini hususan viwanda ambavyo vitatumia ngozi lakini pia viwanda vya nyama, maziwa, matunda, asali, mbao, pamba, korosho, mafuta ya mbegu, uchakataji wa samaki na kuongeza thamani ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine tuliupokea na ulisemwa sana ni kwamba viwanda vidogo vipewe msukumo pamoja na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani mkali kutoka nje. Lakini pia elimu inayotolewa iwiane na mahitaji ya viwanda hususani rasilimali watu yenye uwezo na ujuzi na ilisisitizwa sana elimu ya ufundi na ufundi stadi. Jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walisitiza ni kwamba sera ya elimu msingi bila malipo iende sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya elimu, hususani ujenzi wa madarasa, vifaa vya maabara, upatikanaji wa madawati na kuhakikisha kwamba walimu wa sayansi wanakuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea ushauri kwamba katika Mpango ujao ni muhimu kuongeza kasi ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini. Pia kupiga vita rushwa, urasimu, kuboresha miundombinu na kuharakisha maamuzi. Yalisemwa mengi, naomba niseme moja la mwisho ambalo lilisisitizwa sana nalo ni kwamba Mpango wa Maendeleo 2016/2017 ujielekeze katika miradi inayogusa maisha ya watu na hasa makundi ya watu maskini na wale wenye mahitaji maalum. Baadhi ya maeneo yaliyosisitizwa ni barabara za vijijini, nyumba za walimu, zahanati na vituo vya afya lakini pia programu ya kuwawezesha wachimbaji wadogo na maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza baadhi ya maeneo makubwa ambayo yalisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge, naomba uniruhusu nianze kufafanua baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza na naomba nianze na zile zinazohusu uchumi jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja moja ilikuwa kwamba kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi kwa takribani asilimia 7 haigusi maisha ya wananchi wengi hasa wanaoishi vijijini. Ni kweli kuwa uchumi wa Taifa umekua kwa kasi kubwa. Kwa zaidi ya muongo mmoja na nusu sasa uchumi wa Taifa letu, kwa maana ya *real GDP growth* umefika wastani wa asilimia saba kwa mwaka. Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa katika Bara la Afrika. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010 - 2014, uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha umaskini kikipimwa kwa mahitaji ya msingi (*basic needs poverty*), kimepungua kwa takribani asilimia 6.2 kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 mpaka asilimia 28.2 mwaka 2012. Hili lilitokana kwanza na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi lakini pia juhudi za Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu hususan maji, afya, elimu na ujenzi wa miundombinu. Umaskini ukipimwa kwa kutumia kigezo cha chakula (*food poverty*) nao ulipungua kutoka asilimia 11.8 mwaka 2007 hadi asilimia 9.7 mwaka 2012. Hata hivyo, ni ukweli pia ulio bayana kwamba kiwango cha umaskini bado ni kikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama pia vigezo vya umaskini ambavyo siyo wa kipato, takwimu zilizopo zinaonesha ulipungua. Hili linadhihirishwa na Watanzania ambao sasa wana kaya ambapo nyumba zao zimejengwa kwa kutumia saruji na mabati, kaya zinatumia umeme, kaya zinamiliki nyumba zao, wananchi wana simu za mkononi, redio luinga, baiskeli, pikipiki lakini pia kumiliki ardhi na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nieleze changamoto mbili kubwa ambazo zinasababisha kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi tuliyonayo isijidhihirishe katika kasi kubwa zaidi ya kupunguza umaskini.

Changamoto ya kwanza ni kwamba sekta zinazokua haraka ambazo ni ujenzi, mawasiliano, huduma za fedha na bima, haziajiri watu wengi. Sekta ya kilimo ambayo ndiyo mwajiri wa Watanzania walio wengi imekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.6 kwa mwaka. Sababu zake ni nyingi ikiwemo tija ndogo, teknolojia ya kale lakini pia matatizo ya mitaji, kutegemea mvua, shida za masoko na hata tozo na kodi za kero mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, ni kasi ya ongezeko la idadi ya watu ambayo ni kubwa bado takribani asilimia 2.7 kwa mwaka. Ukuaji halisi wa uchumi wa Taifa kwa ujumla, ukizingatia kasi ya ongezeko la idadi ya watu, maana yake ni kwamba uchumi wa Taifa unakua kwa asilimia nne tu ambayo inapatikana kwa kuchukua wastani wa ukuaji kwa uchumi asilimia 6.7 ukatoa kasi ya ongezeko la idadi ya watu ambayo ni asilimia 2.7. Mbaya zaidi kwa kuwa wastani wa ukuaji katika sekta ya kilimo ni takribani asilimia 3.6 tu maana yake ni kwamba kama unazingatia ukuaji wa idadi ya watu, sekta ya kilimo kiuhalisia inakua kwa asilimia 0.9 peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi ndiyo sababu za msingi kwa nini kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi haijaonekana sana kwa maana ya kupungua kwa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi kubwa ya ukuaji wa idadi ya watu inapeleka familia nyingi hasa vijijini kuwa na idadi kubwa ya wategemezi na kushindwa kuweka akiba ya kutosha kwa ajili ya kumudu mahitaji yao ya maisha lakini pia huduma za jamii na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake nini? Ili tuweze kuhakikisha kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi inagusa wananchi wengi, moja, inabidi kuongeza kasi zaidi ya ukuaji wa uchumi. Hakuna nchi popote ulimwenguni ambapo umaskini umepungua bila kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi wake. Kwa Tanzania tunakadiria kwamba siyo asilimia saba tena, tunatakiwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa uende hata kufika asilimia 10 na zaidi. Hili litawezekana kama tutajielekeza kuongeza tija katika kilimo, kwa maana ya kutumia mbegu bora, mbolea, upatikanaji wa mikopo, kujikita katika kilimo cha umwagiliaji lakini pia ujenzi wa maghala na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata mazao na kulenga kukuza kilimo cha mazao yenye thamani kubwa na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alishawishi kwamba kati ya mazao yenye thamani kubwa ni pamoja na mirungi na bangi.

Nafikiri yako mazao mengi ambayo yana thamani kubwa na hayana madhara kama haya yanayopendekezwa. Ningesauri tujielelekeze huko zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili ni kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Hapa kikubwa ni kuweka mikakati ya kusaidia kuhakikisha kwamba wasichana wengi na hususan kutoka familia maskini, wanaendelea na masomo ya sekondari na elimu ya juu. Mkakati wa kutoa elimu bure ni muhimu sana kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu kwa ajili ya kupunguza kasi ya ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa tatu, ni kupanua fursa za ajira katika shughuli na huduma zenye mahusiano ya karibu na zile sekta nilizozitaja ambazo uchumi wake unakua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba matumizi ya dola kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini ni vyema yakadhishiwa. Utafiti ambao Benki Kuu imefanya unaonesha kuwa ni asilimia 3.2 tu ya wafanyabiashara wote ndiyo wanaoweka bei kwa dola na ni asilimia 0.1 tu ya wafanyabiashara ndiyo wanaodai kulipwa kwa dola peke yake. Utafiti huo unabainisha kwamba ukiacha mahoteli ambayo wameruhusiwa, kubadilisha fedha za kigeni, maeneo sugu ambayo bei zinatajwa kwa dola ni pamoja na nyumba za kupanga na baadhi ya taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya dola sambamba na shilingi tunatambua kwamba yanaweza kuchochea utoroshwaji wa fedha za kigeni lakini pia mitaji kwa maana ya *capital flight* kwenda katika mabanki nje ya nchi. Kwa kawaida wanakuwa wanakimbia usumbufu katika kupata fedha za kigeni. Pia kama unadhifiti dola kupita kiasi mara nyingi inasababisha dola iuzwe kwa bei kubwa zaidi mitaani yaani kwenye *black market*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatambua shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini yaani ndiyo *legal tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tamko la Serikali la Agosti, 2007, liliagiza kuwa bei zote nchini zitangazwe katika shilingi. Maana yake ni kwamba shilingi ya Tanzania haipaswi kukataliwa na mtu yeyote kwa malipo halali hapa nchini na mtu hapaswi kulazimishwa kufanya malipo yoyote kwa dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kikubwa kwa kuzingatia kwamba idadi ya wafanyabiashara ambao wanadai dola, kama nilivyoieleza hapo awali ni ndogo na kwa kuzingatia faida ambazo wananchi wenzetu wanaofanya biashara wanapata kwa kuwa na akiba zao za dola wenyewe ambayo inawarahisishia kufanyabiashara, lililo kubwa ni kusimamia sheria lakini pia Benki

Kuu kuendelea kusimamia *Bureau de Change* na kuzitaka zitumie *Electronic Fiscal Devices* ili tuweze kupata taarifa sahihi za miamala yao na kodi stahiki iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni kwamba Serikali ina mkakati gani kudhibiti kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola. Ni kweli thamani ya shilingi imeshuka kwa kasi katika kipindi cha karibuni, kwa mfano, mwezi Januari, 2015, dola moja ya Kimarekani ilikuwa inabadilishwa kwa shilingi za Kitanzania 1,782.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Disemba, 2015, dola hiyo moja ya Kimarekani ilikuwa inabadilishwa kwa shilingi 2,148.5. Kushuka huku kwa thamani kuna sababu nyingi, mojawapo ni kuimarika kwa dola dhidi ya sarafu nyingine duniani wala siyo kwa shilingi peke yake. Hii imetokana na uchumi wa Marekani kuwa mzuri na kuwavutia wawekezaji wengi kukimbilia kuwekeza zaidi katika dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli pia kwamba katika miezi ya karibuni tumeona bei ya dhahabu katika soko la dunia ikiporomoka sana pia baadhi ya mazao ambayo tunauza katika masoko ya nje hasa pamba nayo pia yaliteremka. Hii maana yake mahitaji yetu ya kuweza kununua bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi yalikuwa hayawezi kukidhiwa na mauzo yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine mwaka 2015 ulikuwa na changamoto mbalimbali ambapo tulishuhudia misaada ya kibajeti ambayo inaingia kwetu katika fedha za kigeni ilichelewa kutufikia na mingine haikuja kabisa. Vilevile palikuwepo na ongezeko la mahitaji ya dola kwa ajili ya malipo ya gawio nje ya nchi kwa baadhi ya makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafanya nini? Hatua za kuimarisha thamani ya shilingi ni pamoja na kuongeza mauzo yetu nje ya nchi na hili ni lazima tulifanye kwa kutafuta bidhaa ambazo zina soko kubwa, zina thamani zaidi katika masoko ya nje lakini pia lazima tupanue wigo wa bidhaa ambazo tunauza nje ya nchi yaani *export diversification*. Tunahitaji kudhibiti biashara ya fedha za kigeni ambazo haziambatani na shughuli za kiuchumi kwa maana ya *currency swaps*. Vilevile tunahitaji kupunguza ujazi wa fedha katika uchumi ili kudhibiti miamala ambayo inafanyika katika soko la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ilikuwa kwamba Serikali haikutenga asilimia 35 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Miaka Mitano. Hili siyo kweli hata kidogo na wengine walidai kwamba Serikali wakati mwingine haijawahi kutenga hata senti moja kutekeleza miradi ya maendeleo.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kutenga bajeti ya maendeleo kwa wastani wa asilimia 35. Kuanzia mwaka 2011/2012, Serikali iliweza kutenga fedha kama ifuatavyo: Shilingi trilioni 3.8 mwaka 2011/2012, shilingi trilioni 4.5 mwaka 2012/2013 na shilingi trilioni 4.6 mwaka 2014/2015 na mwaka huu unaoendelea zilitengwa shilingi trilioni 5.9 na mwaka ujao kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja yangu tunatarajia kwamba bajeti ya maendeleo itafikia shilingi trilioni 6.02.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kuwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ilitenga fedha za maendeleo kwa wastani wa asilimia 27 kwa hiyo, miaka yote mitano ikilinganishwa na lengo la asilimia 35.

Kwa hiyo, ukiliangalia tu hivi, unaweza ukasema kwamba hatukufikia asilimia 35. Hii siyo kweli kwa sababu kwa jinsi mfumo wa bajeti ulivyo, yapo matumizi ambayo yanahesabiwa kwamba yako kwenye matumizi ya kawaida lakini kiuhalisia ni matumizi ya maendeleo. Mathalani fedha kwa ajili ya elimu na afya, hizi tunawekeza kwa ajili ya kesho lakini tunapoandika vitabu vya bajeti zinahesabika kuwa upande wa *recurrent* lakini hizi kwa kweli tunawekeza ni fedha za maendeleo. Hata zile za kulipia deni la Taifa, nazo zinahesabika ni *recurrent* lakini kwa kweli tumekopa kwa ajili ya maendeleo na hivyo hizi ni fedha ambazo kiuhalisia ni kwa ajili ya *development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukijumlisha matumizi yote haya pamoja na yale ya asilimia 27 niliyosema, wastani wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka inafika asilimia 48 ya bajeti ya Serikali kwa kipindi hicho cha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Pia ni vizuri nikiri kwamba kutokana na matumizi ya lazima, kwa mfano, kugharamia Bunge la Katiba, Uchaguzi Mkuu, kununua chakula cha hifadhi sambamba na ukusanyaji wa mapato kutofikia malengo na wahisani kupunguza misaada yao ya kibajeti, kuna kipindi haikuwezekana kutoa fedha zote za maendeleo kama ilivyokuwa imepangwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie kwenye baadhi ya hoja ambazo zinahusu mwongozo wa bajeti. Hoja moja kubwa iliyojitokeza ilikuwa kwamba uamuzi wa kufuta utaratibu wa kubakiza mapato (*retention*) usitekelezwe kwa kuwa ni kinyume cha Sera ya Ugatuzaji Madaraka *D by D* na kwamba itaathiri shughuli mbalimbali kama uhifadhi wa mbuga za wanyama, huduma katika viwanja vyetu vya ndege na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba Sheria ya Bajeti, Na.11 ya 2015, kifungu cha 58(a)-(c) kinaelekeza

kwamba mapato yote ya Serikali yakusanywe na kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na Bunge hili ndilo lililopitisha sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *retention* ulianza zamani kidogo katika miaka ya 1996/1997 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato na kuziruhusu taasisi zinazokusanya maduhuli kubakiza sehemu ya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ukusanyaji. Pia ilikuwa ni kuipunguzia Serikali mzigo wa kupata fedha zaidi kutoka kwa taasisi hizo kwa ajili ya matumizi ya taasisi nyingine ambazo hazipo kwenye huo utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unahusisha baadhi tu ya Wizara na Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Nishati na Madini; Maliasili na Utalii; Mambo ya Nje; Ushirikiano wa Kimataifa; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Jeshi la Polisi; Idara ya Zima Moto; Jeshi la Magereza; Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano; Maji na Umwagiliaji; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Waziri Mkuu; Uhamiaji; Mfuko wa Mahakama; Ofisi ya Mkaguzi na Mdhifiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto. Nirudie kuisitiza kwamba Serikali inakusudia kusitisha utaratibu huu kuanzia mwaka ujao wa fedha kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya sababu ni kuwa taasisi zinazohusika zimeacha jukumu lao la msingi na kuegemea zaidi kwenye mapato. Pia ni dhahiri kuwa wakati taasisi ambazo zipo kwenye mfumo wa *retention* zinapata fedha nyingi bila kujali uhaba wa fedha ambao unakabili Wizara, Idara na Taasisi ambazo hazipo kwenye mfumo huu. Vilevile tumeshuhudia kwamba taasisi nyingi sasa nazo zinadai ziingie kwenye utaratibu huo. Siyo hivyo tu, pamoja na kubakiza sehemu ya mapato wanayokusanya bado tunashuhudiwa kwamba wanaendelea kulipwa mishahara kwa asilimia 100 kutoka kwenye Mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize kwamba utaratibu huu sasa tunaufuta kuanzia mwaka ujao wa fedha lakini uamuzi huu hautahusu mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika maeneo yao na wala haitagusa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kwa sababu hili halikueleweka ilivyo. Wakati nasoma hotuba yangu nilieleza bayana kwamba uamuzi huu hautahusu mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na ni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa, Na.9 ya 1982 lakini pia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii haitaguswa na utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano ilijitokeza hoja kwamba tufute utaratibu huu, lakini kuna ukiritimba Wizara ya Fedha katika utaoaji wa mapato. Kati ya Februari na Juni, 2016, tutakaa na wadau wote wanaohusika na *retention* ili tukubaliane utaratibu mpya wa kutoa fedha hizo. Tukishafanya makubaliano, tutatoa Waraka ambao utaelekeza utaratibu mpya. Tunaamini kabisa uamuzi huu utasaidia sana katika ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi, lakini pia utatusaidia katika kutunza hesabu na kutoa taarifa kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyokuwa moto ni uamuzi wa Serikali wa kuondoa fedha za taasisi zote za umma kutoka kwenye benki za biashara kwenda Benki Kuu. Hoja ilikuwa kwamba utaratibu huu utakuwa na madhara ya kiuchumi. Kwa kipindi kirefu mashirika ya umma yamekuwa yakitunza fedha zao katika mabenki ya biashara na kufanya matumizi kupitia benki hizo. Hata hivyo, kutokana na utaratibu huo, kumekuwa na ugumu wa kupata taarifa za mapato na matumizi ya mashirika hayo kwa wakati na kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa Serikali kufuatilia usahihi wa matumizi ya mashirika ya umma ili kujihakikishia kuwa wanaelekeza fedha hizo katika vipaumbele, umekuwa finyu sana. Hiyo ilisababisha baadhi ya mashirika kutochangia ipasavyo katika mapato ya Serikali. Vilevile baadhi ya taasisi zimekuwa zikiweka fedha katika akaunti za mabenki ya biashara kwa muda mrefu bila kuzitumia wala kuziwekeza na badala yake fedha hizo zimekuwa zikiwekezwa na mabenki husika ikiwa ni pamoja na kununulia hati fungani na dhamana za Serikali kwa riba kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ni kuwa fedha ambazo sasa tunatoa maelekezo kwamba zifunguliwe akaunti Benki Kuu bado zitabaki kuwa ni fedha za mashirika husika. Mashirika hayo yataendelea kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya fedha hizo ikiwa ni pamoja na kuziwekeza kulingana na vipaumbele na miongozo ya Serikali. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa tunapata taarifa sahihi za makusanyo yote yanayokusanywa na taasisi ya umma kama nilivyosema; kuhakikisha kwamba mashirika ya umma yanachangia ipasavyo kwenye mapato yasiyo ya kodi lakini pia kuhakikisha kuwa hakuna fedha zinakaa kwenye akaunti za mashirika bila mipango ya matumizi yake. Hatua hiyo pia itatuwezesha kupunguza utegemezi wa baadhi ya mabenki kwa fedha za mashirika na hivyo kufanya yajielekeze zaidi kufanya biashara na wananchi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize tu kwamba akaunti zitakazofunguliwa Benki Kuu zitatumika kukusanya mapato yote ya mashirika ya umma kama *holding account* wakati akaunti za matumizi (*operational accounts*) zitaendelea kuwa katika mabenki ya biashara ili kuyawezesha mashirika

kufanya miamala yake. Mwaka 2014/2015, hii ilikuwa ni moja ya ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba Serikali iondoe fedha za mashirika ambazo hazizalishi kutoka katika mabanki ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasiwasi kwamba hatua hiyo italeti madhara ya kiuchumi, tarehe 22 Januari, mashirika yote yalikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 435 kwenye akaunti za hundi (*current account*). Baada ya uamuzi huo, hadi kufikia tarehe 22 Januari, kiasi cha shilingi bilioni 238 kwa mashirika 15 kulishahamishiwa Benki Kuu na hakukuwa na athari zozote za kibanki zilizojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine muhimu sana ilihusu kujenga reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Nilishalieleza mwanzo na jana Waziri mwenye dhamana ya sekta hii alilitolea maelezo. Naomba nitoe maelezo upande wa ugharamiaji wa ujenzi wa reli hiyo. Kwanza, utafiti ambao umekwishafanyika, umebaini kuwa ili mradi huu uweze kuwa *commercially viable*, itahitajika reli yote na matawi yake kwenda nchi jirani yajumuishwe. Kwa hiyo, matawi ya kwenda Burundi - Rwanda - Congo kutokea Burundi na Rwanda, ili mradi huu uwe *viable commercially*, inahitajika haya matawi yawe yamejumuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama Tanzania itaamua vinginevyo, kama nilivyosikia baadhi ya Wabunge wakisema kwamba sisi tuhangaike tu na reli yetu ya kati humu ndani...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo, naomba umalize, una dakika tano za kuhitimisha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama tutaamua vinginevyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutakuwa tumekosa fursa kubwa kwa kuwa mzigo wa kusafirisha kwenye reli yetu ya kati kutoka ndani na matawi yake hautatoshwa kuweza kurudisha gharama ya kujenga reli hiyo. Pia nchi yetu itakosa fursa ya kunufaika na maendeleo mengine ambayo yapo katika nchi jirani na hasa soko na mizigo kutoka kwenye nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) na *World Economic Forum* ambao wamekuwa mstari wa mbele kugharamia *feasibility studies* na kutafuta *financing* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, kwa hakika wataona ugumu sana kuendelea na *initiative* hii ambayo inaungwa mkono na *African Union* lakini pia *Southern Africa Infrastructural Development Initiative* ikiwa pamoja na *Development Bank of Southern Africa* ambayo inaratibu ufuatiliaji wa fedha za kujenga reli hii ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kujenga reli ya kati inakadiriwa kuwa kati ya dola bilioni 7,000 mpaka bilioni 9.5 kama itajengwa kwenye tuta jipya. Kama itajengwa kwenye tuta lililopo itagharimu nusu ya fedha hizo. Kwa uchumi wetu ambapo tuna GDP ya dola bilioni 53 au shilingi trilioni 100 na zaidi, uchumi wetu bado ni mdogo kuweza kubeba mzigo huu. Mfuko wa Reli ni mdogo sana, kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 50 na kama tukiamua kwamba tunaweza kujenga reli yetu ya kati kwa hela hizo tu, itatuchukua takribani miaka 320 kujenga reli hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Ndiyo namba zilivyo. Hata kama tungeweza kutumia mapato yetu yote ya kodi kwa mwaka ambazo ni takribani dola trilioni 12 itatulazimu kujinyima kabisa fedha zote hizo kwa mwaka 1.3 ili ziweze kufikia hizo trilioni 16 au dola bilioni 8. Hata tukiamua kwamba tunaijenga kwa miaka minne maana yake itabidi kila mwaka tutenge shilingi trilioni 4 kwa ajili ya kujenga reli hiyo. Kwa namba hizi, nataka kuonyesha tu jinsi ilivyo kazi ngumu kujenga reli yetu ya kati kwa kutumia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha, napenda kurejea kwa kulisitiza masuala muhimu ambayo yamebeba uzito wa pekee kwa Taifa letu kama yalivyoelekezwa kwenye mwongozo. Kwa kifupi, Maafisa Masuuli waandae bajeti ya mwaka ujao kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Na.11 ya 2015; ni lazima kuimarisha ukusanyaji wa mapato; ni lazima kusimamia matumizi ya Serikali na kuondokana na matumizi yasiyo na tija na ni lazima kulipa na kudhibiti ongezeko la madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha maandalizi na utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Nirudie tena kuziomba Wizara na Idara za Serikali wazingatie yale ambayo yameelekezwa kwenye hotuba niliyoitoa na wazingatie Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hatua zinazoongozwa na Wizara yangu za kuhakikisha kuwa tunaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, ya kodi na yasiyo ya kodi na kuelekeza matumizi kwenye maeneo yenye tija kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kama Waziri alivyosema anawashukuru sana kwa michango yenu, nichukue fursa hii kuiagiza Serikali ifanyie kazi maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala na mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge yatumike kuandaa Bajeti na Mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mpango huu utaletwa Juni, 2016 wakati wa kuwasilisha Mpango na Bajeti.